سواحيلي

# TAFSIRI YA SEHEMU YA KUMI YA MWISHO YA QUR'ANI TUKUFU

Ikifuatiwa na:

## SHERIA MUHIMU KWA MUISLAMU

ISBN : 978-603-90233-4-0

www.tafseer.info

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu, na rehema na amani zimfikie Bwana wetu, Mtume wetu Muhammad, Kipenzi chetu na Mtume wa Mwenyezi Mungu

**Baada ya hayo, jua ndugu yangu Mwislamu, Mwenyezi Mungu akurehemu, kwamba inatupasa kujifunza masuala manne:**

**❶LA KWANZA: Ni Elimu**. Nayo ni elimu ya 1) Kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu, 2) Kumjua Mtume wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. 3) Kuijua dini ya Kiislamu, kwa sababu ilivyo ni kwamba haifai kumwabudu Mwenyezi Mungu bila ya elimu. Na anayefanya hivyo, basi mwisho wake ni upotofu, na kwa hakika atakuwa amejifananisha na Wakristo katika hilo

**❷LA PILI: Kutekeleza.** Anayejua na asitekeleze, atakuwa amejifananisha na Wayahudi, kwa sababu wao walijua na hawakutekeleza. Miongoni mwa mbinu za shetani ni kwamba anafanya elimu ichukiwe akimlaghai mwanadamu kuwa, kwa sababu ya kutojua kwake, basi wakati huo atasamehewa mbele ya Mwenyezi Mungu. Hakujua kwamba aliyepata uwezekano wa kusoma na asifanye hivyo, basi imepatikana hoja juu yake. Hii ni mbinu ya watu wa (Mtume) Nuhu kama alivyo waeleza mwenyezi mungu katika qur-ani : ﴿كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَن مُّنكَرٍ فَعَلُوهُ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ﴾ "***Waliweka vidole vyao katika masikio yao na kujifinika nguo zao***. **Sura Nuuh 71, aya 7.** Walifanya hivyo ili isije ikasimama hoja dhidi yao.

**❸LA TATU: Kuihubiri** {kuilingania}elimu hiyo. Kwa sababu, wanazuoni na wahubiri{walinganiaji} ndio warithi wa Mitume. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewalaani Wana Wa Israili kwa sababu : ﴿جَعَلُوا أَصَابِعَهُمْ فِي آذَانِهِمْ وَاسْتَغْشَوْا ثِيَابَهُمْ﴾ " ***Walikuwa hawakatazani maovu waliyoyafanya. Kwa yakini, ni vibaya sana hivyo walivyokuwa wakifanya***. **Sura Al-maaida 5, .aya 79.**

Elimu na kuhubiri ni Faradhi ya Kutoshana. Iwapo wataitekeleza Faradhi hiyo watu ambao wanatosha, hakuna yeyote atakayepata dhambi. Iwapo watu wote wataacha kuitekeleza, basi watapata dhambi wote.

**❹LA NNE : Ni kuwa na uvumilivu** juu ya maudhi katika kujifunza elimu hiyo, kuitekeleza na kuihubiri.

Kwa kuchangia katika kufuta ujinga na kurahisisha upatikanaji wa elimu ya wajibu, tumekusanya katika kitabu hiki kifupi taaluma chache sana za kisheria ambazo zinatosheleza wajibu pamoja na Juzuu (sehemu) tatu za mwisho za Qur'an na tafsiri yake, kwa kuwa zinakaririka sana kusomwa, na "**Lisilowezekana lote, haliachwi lote**".

Katika yote hayo, tumejihimu sana kufupisha. Pia tumezingatia yale yaliyo sahihi kunukuliwa kutoka kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Hatudai kuwa tumefikia kufanya yaliyo kamili, kwani hilo linamhusu Mwenyezi Mungu pekee. Hizi ni juhudi za mwenye uwezo mdogo. Juhudi zikiwa ni sahihi, zinatokana na Mwenyezi Mungu na kama zikiwa na makosa basi zinatokana na nafsi zetu na shetani, na Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawahusiki nazo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe rehma kila atakayetupa zawadi ya aibu zetu kwa ukosoaji wenye lengo jema, wenye kujenga.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu pia amlipe malipo mema zaidi kila aliyeshiriki katika kukiandaa kitabu hiki, kukichapisha na kukisambaza, na pia aukubali mchango wao huo na awazidishie thawabu na malipo.

Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi. Tunaomba rehema na amani zimfikie Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad, Jamaa na Swahaba wake wote.


| KITABU HIKI | CHAPA YA 3 | Wanachuoni na wasomi kadhaa katika ulimwengu wa Kiislamu wamekiridhia kitabu hiki |
|---|---|---|
| Kinatolewa bure Na haifai kuuzwa | Imeongezwa na kusanifiwa Mfungo Mosi 1432H | Kwa taarifa zaidi au kusaidia au kushiriki au kuomba kitabu: **Tovuti: www.tafseer.info Barua pepe: swa@tafseer.info** |

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| 1. FADHILA ZA QUR'ANI | 2 |
| 2. TAFSIRI YA SEHEMU YA KUMI YA MWISHO YA QUR'ANI | 4 |
| 3. MASWALI MUHIMU KATIKA MAISHA YA MWISLAMU | 108 |
| 4. NI YAPI MAJINA MAZURI YA MWENYEZI MUNGU? | 110 |
| 5. MATENDO YA NYOYO | 129 |
| 6. MAHOJIANO TULIVU | 139 |
| 7. KUKIRI KUWA HAKUNA ANAYE STAHIKI KUABUDIWA ISIPOKUWA MWENYEZI MUNGU TU | 156 |
| 8. KUKIRI KUWA MUHAMMAD NI MTUME (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) WA MWENYEZI MUNGU | 158 |
| 9. TWAHARA | 160 |
| 10. SHERIA ZA MWANAWAKE | 165 |
| 11. MWANAMKE KATIKA UISLAMU | 167 |
| 12. SALA | 172 |
| 13. ZAKA | 180 |
| 14. KUFUNGA SAUMU | 183 |
| 15. HIJA NA UMRA | 186 |
| 16. Huu ni muhtasari wa matendo ya Hija kwa mpangilio: | 190 |
| 17. FAIDA MBALI MBALI | 191 |
| 18. RUQ-YA KISHERIA | 197 |
| 19. DUA | 204 |
| 20. DUA MUHIMU AMBAZO INATAKIWA KUZIHIFADHI NA KUOMBA KWAZO | 206 |
| 21. BIASHARA YENYE FAIDA | 210 |
| 22. NYIRADI ZA KILA SIKU, ASUBUHI NA JIONI | 212 |
| 23. KAULI NA VITENDO AMBAVYO NDANI YAKE KUNA MALIPO MAKUBWA | 214 |
| 24. MAMBO YALIYOKATAZWA | 221 |
| 25. SAFARI YA MILELE | 225 |
| 26. NAMNA YA KUTAWADHA | |
| 27. NAMNA YA KUSALI | |
| 28. ELIMU INAHITAJI UTEKELEZAJI | |

# FADHILA ZA QUR'ANI

Qur'ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu, na ubora wake, ukilinganisha na maneno mengine, ni kama ubora wa Mwenyezi Mungu juu ya viumbe wake. Kuisoma Qur'ani ni jambo bora sana ambalo ulimi umelitamka.

**MIONGONI MWA FADHILA ZA KUJIFUNZA QUR'NI NA KUIFUNDISHA NI:**

**MALIPO YA KUIFUNDISHA** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "Mbora wenu zaidi ni yule aliyejifunza Qur'ani na akaifundisha". **Bukhari.**

**MALIPO YAKUISOMA** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "Mwenye kusoma herufi katika kitabu cha Mwenyezi Mungu atapata zuri (moja) kwa herufi hiyo (moja aliyoisoma), na zuri (moja) ni kwa mazuri kumi mfano wake ". **Tirmidhiy.**

**FADHILA ZA KUJIFUNZA QUR'ANI, KUIHIFADHI NA KUISOMA KWA UHODARI** Amesema Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: *"Mfano wa ambaye anaisoma Qur'ani na ilhali ni mwenye kuihifadhi, atakuwa pamoja na Malaika, Watukufu, Wema. Na mfano wa ambaye anaisoma Qur'ani na ilhali yeye anaipatiliza na huku ikiwa ngumu kwake, basi atapata malipo mawili"*. **Bukhari, Muslim.**

Na Amesema Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: *"Ataambiwa msomaji wa Qur'ani kwamba: Soma na panda (daraja) na soma kama ulivyokuwa ukisoma duniani, kwani daraja yako ni pale mwisho wa aya utakayoisoma"*. **Tirmidhiy.**

**MALIPO YA MTU AMBAYE MTOTO WAKE AMEJIFUNZA QUR'ANI** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Yeyote aliyesoma Qur'ani na akajifunza na akaitekeleza, wazazi wake watavalishwa taji la nuru Siku ya Kiyama. Mwangaza wake ni mfano wa mwangaza wa jua. Na wazazi wake watavalishwa suti mbili, na kwa sababu hiyo, watauliza: Ni kwa sababu ya jambo gani tumevishwa haya? Watajibiwa: Ni kwa sababu ya mtoto wenu kujifinza Qur'ani"*. **Al-haakim.**

**QUR'ANI KUMUOMBEA MSOMAJI WAKE HUKO AKHERA** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Someni Qur'ani, kwani itakuja Siku ya Qiyama ikiwa ni muombezi wa wasomaji wake"*. **Muslim.**

Aidha Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Saumu na Qur'ani zitamuombea mja Siku ya Kiyama"*. **Ahmad, Al-haakim.**

**MALIPO YA KUJUMUIKA KWA AJILI YA KUSOMA QUR'ANI NA KUIDURUSU** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Hawakukusanyika watu katika nyumba miongoni mwa nyumba za Mwenyezi Mungu Mtukufu wakikisoma kitabu chake na kukidurusu*

*baina yao isipokuwa tu unawashukia utulivu na inawaenea rehma na Malaika huwazunguka na Mwenyezi Mungu huwataja pamoja na viumbe walioko kwake*".

**Abudaud**

## BAADHI YA KANUNI ZA USOMAJI:

**TARATIBU ZA USOMAJI** Ibn-kathiir ametaja taratibu nyingi. Miongoni mwake ni hizi: Mtu kutoshika Qur'ani na kutoisoma isipokuwa tu anapokuwa twahara, kupiga mswaki kabla ya kuisoma Qur'ani, mtu kuvaa nguo zake nzuri sana, kuelekea Qibla, kusitisha kusoma mtu anapokwenda myayo, kutokatisha kusoma kwa kuzungumza isipokuwa tu kwa dharura, kuwa makini, kusitisha kusoma katika aya za ahadi (za rehma) ili msomaji aombe (rehma) na kusitisha kusoma katika aya za makamio (ya adhabu) ili msomaji aombe kinga, kutouweka msahafu ukiwa umetandazwa chini na kutoweka kitu chochote juu yake, baadhi ya wasomaji kutosoma kwa sauti ya juu mbele ya baadhi ya wasomaji wengine (ili wasiwe kero) katika kusoma na kutosoma masokoni na katika sehemu za zogo.

**NAMNA YA KUSOMA**

*Kusoma Qur'ani na nyiradi katika sala hakutambuliki mpaka tu mtu atamke kwa kiasi ajisikilizishe yeye mwenyewe bila ya kumtatiza mwengine.

*Inatakiwa mtu awe mtulivu katika kusoma kwake. Anas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, aliulizwa kuhusu usomaji wa Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akasema: *"(Mtume)* (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) *Alikuwa anavuta sana anaposoma **"Bismil-laahir-rahmaanir-rahiim"**Anavuta **"Bismillaah"**. Anavuta **"Arrahmaan "** Anavuta **"Arrahiim "***. **Bukhariy**.

---

**KUSOMA KWA KUHIFADHI** Ikiwa msomaji wa Qurani anapata mazingatio, tafakuri na umakini zaidi akisoma kutokana na kuhifadhi kwake, basi **kusoma kwa kuhifadhi ni bora zaidi** kuliko kuangalia msahafu. Ikiwa kusoma kwa kuhifadhi na kuangalia msahafu kuko sawa, **basi kusoma kwa kuangalia msahafu ni bora zaidi**.

- **USIA:** Ndugu yangu, fanya bidii ya kuutumia wakati wako katika kuisoma Qur'ani. Jiwekee kiwango cha kila siku na usikiache vyovyote iwavyo. Kichache kinachodumu ni bora zaidi kuliko kingi kisichodumu. Ikiwa utaghafilika au utalala, basi kilipe kesho. Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Aliyelala akapitwa na hizbu (uradi) yake au sehemu ya hizbu yake akaisoma katika wakati uliopo baina ya sala ya Alfajiri na sala ya Adhuhuri, ataandikiwa kama ameisoma usiku*". **Muslim**.
- Usiwe miongoni mwa walioiacha Qur'ani au kuisahau kwa namna yoyote; kama kuacha kuisoma au kuacha kuizingatia au kuacha kuitekeleza au kuacha kuifanya tiba.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾
الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٢﴾ الرَّحْمَٰنِ
الرَّحِيمِ ﴿٣﴾ مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٤﴾ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ
نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾ اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿٦﴾
صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ
عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٧﴾

# SUURATUL-FAATIHA

Sura hii imeitwa Faatihatulkitaab (Mwanzo wa Kitabu) kwa kuwa Qur'ani imeanzwa kwayo, kwani Faatiha ndio kitu cha kwanza mwandishi anachokiandika katika Msahafu, na ni kitu cha kwanza msomaji anachosoma katika kitabu kitukufu. Sura hiyo sio Qur'ani ya mwanzo kuteremka. Imesemwa kuwa Sura hiyo imeteremka Makka, na pia yasemekana kuwa imeteremk12a Madina. Sura hii inaitwa Faatihatulkitaab, na pia yaitwa Ummul-kitaab(Msingi wa kitabu), Assab-ulmathaaniy (Aya saba zinazorudiwa rudiwa kusomwa), Suuratul-hamd (Sura ya shukurani), Suuratus-swalaa (Sura ya sala) na Al-waaqiya (Kinga). Zimekuja Hadithi nyingi katika kuelezea ubora wake. Miongoni mwa Hadithi hizo ni kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kwamba: ***"Alhamdu lillaahi rabbil-aalamiin ndio As-sab-ulmathaaniy (Aya saba zinazorudiwa rudiwa kusomwa) na Qur'ani Tukufu ambayo nimepewa"***. Bukhariy, Ahmad.

(1) **KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.** Bismillahi sio aya mwanzo wa sura zote za Qur'ni, lakini ni aya inayotenganisha kati ya kila sura mbili. Inapendekezwa kuisoma isipokuwa tu katika sura Attawbah (9); inakuwa makuruhu. **ALLAH** Ni jina maalum ambalo hajaitwapo kwa jina hilo asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Asili yake in Ilaah (Mungu). Kabla ya kusarufiwa, kilikuwa kikiitwa kwa jina hilo kila kinachoabudiwa, kwa haki au kwa batili. Baadae, ikaghilibu kuitwa yule aabudiwae kwa haki tu. Arrahmaan Arrahiim = MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU Haya ni majina mawili yaliyochukuliwa kutoka katika nomino asilia ya **Arrahma** (rehema). **Rahmaan** ina maana pana zaidi kuliko **Rahiim**. **Rahmaan** ni sifa ambayo haikutumika kwa mwengine isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu tu.

(2) **SIFA NJEMA ANAZISTAHIKI MWENYEZI MUNGU, BWANA WA WALIMWENGU.** Sifa njema (**Al-Hamd**) ni kusifu kwa ulimi juu ya jambo zuri lililofanywa kwa hiyari. Sifa (**Al-hamd**) zinakuwa kwa ulimi tu. Ama shukurani (**Ash-shukr**) zinakuwa kwa ulimi, moyo na viungo (vitendo). Shukurani hazitolewi ila kwa sababu ya neema iliyotendwa. Ama sifa (Al-hamdu) zinatolewa kwa ajili ya ukamilifu wa mwenye kusifiwa, hata kama hakuna neema (aliyotendewa anayesifu). Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye tu anayestahiki sifa na shukurani. **BWANA WA WALIMWENGU. Bwana (Rabb)** ni jina miongoni mwa majina ya Allah Mtukufu. Mwengine yeyote hapewi jina hilo ila tu linapokuwa limeegemezwa kwenye jambo husika, kama unavyoweza kusema: Mtu huyu ni Bwana wa nyumba hii. Bwana ni Mmiliki, Mtengenezaji mambo, Mpangaji mambo na Mwabudiwa. Walimwengu ni wingi wa neno mlimwengu, ambalo maana yake ni kila kitu kilichopo na ambacho sio Allah Mtukufu. Tafsiri ya mlimwengu ni kiumbe chenye akili, na ambacho ni aina nne: Wanadamu, Majini, Malaika na Mashetani.

(3) **MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU**. Ilipokuwa katika kujisifu kwake Mwenyezi Mungu kwa sifa ya Bwana (**Rabb)** kuna maana ya kuogofya, ameikutanisha sifa hiyo na sifa za **MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU**, kwa kuwa sifa hizi zinakusanya matumaini, ili Mwenyezi Mungu katika sifa zake, kwa pamoja, awe ana sifa ya kuogopwa na kutumainiwa, ili hilo liweze kumsaidia zaidi mja katika kumtii Allah.

(4) **MMILIKI WA SIKU YA MALIPO** kwa matendo yake na dhati yake yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu. Siku ya malipo ni siku ambayo Mwenyezi Mungu atawalipa waja wake. Imepokewa kutoka kwa Qataada akisema kuwa "Siku ya Malipo ni siku ambayo Mwenyezi Mungu atawalipa waja kwa mujibu wa matendo yao".

(5) **WEWE TU TUNAKUABUDU NA WEWE TU TUNAKUOMBA MSAADA.** Tunakukusudia wewe tu kwa ibada na tunakukusudia wewe tu kwa kukuomba msaada. Hatumwabudu mwengine na wala hatumuombi msaada mwengine badala yako. **Ibada** ni unyenyekevu na utiifu wa kiwango cha juu. **Katika sheria**, Ibada, kwa pamoja, inajumuisha hofu, upendo na unyenyekevu uliokamilika. Imetangulizwa Ibada kabla ya msaada (Wewe tu tunakuabudu_na wewe tu tunakuomba msaada), kwa sababu, Ibada ndio nyenzo ya kuufikia

msaada. Katika kufasiri neno la Mwenyezi Mungu ***"Wewe tu tunakuabudu na wewe tu tunakuomba msaada",*** imepokewa kwa Ibn-abbas akisema kuwa: "Wewe tu, ewe Mola wetu, tunakupwekesha na kukuogopa, na si mwenginewe, na wewe tu tunakuomba msaada katika kukutii na katika mambo yetu yote".

(6) **TUONGOZE NJIA NYOOFU**. Muongozo ni aina mbili: **1) Muongozo wa kuwezeshwa.** Huu unamhusu Allah Mtukufu, na miongoni mwake ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "Kwa yakini, wewe huwezi kumuongoza umpendaye na lakini Mwenyezi Mungu anamuongoza amtakaye". **Sura Al-qasas (28), aya 56.** **2)** Aina ya pili ni muongozo wa kuelekeza na kufahamisha. Huu ni muongozo wa Mitume na wafuasi wao ambao ni wanazuoni na wahubiri. Miongoni mwa muongozo huu ni kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: "Na, kwa yakini kabisa, wewe unaongoza kwenye njia iliyo nyooka". Sura Ash-shuuraa (42), aya 52. Aya hii inaonesha aina zote mbili za muongozo, kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye anayewezesha kufanya kheri naye pia ndiye aliyewaagiza Mitume watuelekeze kwenye kheri. Njia iliyo nyooka katika lugha ni njia isiyokuwa na kona kona. Makusudio hapa ni njia ya Uislamu.

(7) **NJIA YA AMBAO UMEWANEEMESHA.** Hao ni wale waliotajwa katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "Na wenye kumtii Allah na Mtume, basi hao wako pamoja na watu ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha, na ambao ni Mitume na masadiki (waumini walio sadiki dini ya Mwenyezi Mungu) na mashahidi (waliouawa katika kuitetea/kuiendeleza dini ya Mwenyezi Mungu), na watu wema. Na ni vizuri (mtu) kuwafanya hao (kuwa) marafiki (zake)". Sura An-nisaa (4), aya 69.

**WASIOGHADHIBIKIWA.** Walioghadhibikiwa ni Wayahudi, kwa sababu wao waliijua haki na wakaiacha, wakaipa kisogo kwa kujua na, kwa hiyo, wakastahili kupata ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Imam Ahmad na Ibn-maaja wamenukulu kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akisema kuwa: ***"Hawakuoneeni kijicho (hawakuhusuduni) Wayahudi juu ya jambo kama wanavvyokuoneeni kijicho juu ya salaam (kusalimiana kwenu) na Aamiin (katika sala na katika dua).*** Waliopotea ni Wakristo, kwa sababu waliipa kisogo haki kwa ujinga na, kwa hiyo, wakawa katika upotofu wa wazi juu ya suala la (Mtume) Issa, Mwenyezi Mungu amfikishie amani. Maana ya Amiin ni: Ewe Mola wetu, tukubalie.

ترتيبها ٥٨ — سُورَةُ المُجَادَلَةِ — آياتها ٢٢

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ
وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ١ الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ
مِنكُم مِّن نِّسَائِهِم مَّا هُنَّ أُمَّهَاتِهِمْ ۖ إِنْ أُمَّهَاتُهُمْ إِلَّا اللَّائِي
وَلَدْنَهُمْ ۚ وَإِنَّهُمْ لَيَقُولُونَ مُنكَرًا مِّنَ الْقَوْلِ وَزُورًا ۚ وَإِنَّ
اللَّهَ لَعَفُوٌّ غَفُورٌ ٢ وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِن نِّسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ
لِمَا قَالُوا فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن قَبْلِ أَن يَتَمَاسَّا ۚ ذَٰلِكُمْ تُوعَظُونَ
بِهِ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ٣ فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ
مُتَتَابِعَيْنِ مِن قَبْلِ أَن يَتَمَاسَّا ۖ فَمَن لَّمْ يَسْتَطِعْ فَإِطْعَامُ سِتِّينَ
مِسْكِينًا ۚ ذَٰلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۗ
وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ٤ إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ كُبِتُوا
كَمَا كُبِتَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ وَقَدْ أَنزَلْنَا آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۚ وَلِلْكَافِرِينَ
عَذَابٌ مُّهِينٌ ٥ يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُهُم بِمَا
عَمِلُوا ۚ أَحْصَاهُ اللَّهُ وَنَسُوهُ ۚ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ٦

## SURATUL-MUJAADALAH(58)

(1) **MWENYEZI MUNGU AMEKWISHA SIKIA KAULI YA MWANAMKE AMBAYE ANAJADILIANA NAWE KUHUSU MUMEWE** Yaani: Anakurudishia maneno katika shani yake (jambo lake). **NA ANAMSHITAKIA MWENYEZI MUNGU** Imepokewa kutoka kwa Aisha akisema: Ametukuka ambaye usikivu wake umekienea kila kitu. Mimi nasikia maneno ya Khaula Binti Thaalabah, na baadhi yake yananfichika kwangu, na yeye anamshtaki mumewe kwa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) na akisema:Ewe Mtume wa Allah: (Mume wangu) amekula ujana wangu na nilimtandazia tumbo langu hadi umri wangu ulipokuwa mkubwa na uzazi wangu ukakatika, amenifanyia Dhihari. Ewe Mola wangu, nakushtakia kwako. Aisha akasema:Basi hakuondoka (yule mwanamke) hadi aliposhuka Jibril na aya hizi: **MWENYEZI MUNGU AMEKWISHA SIKIA KAULI YA MWANAMKE AMBAYE ANAJADILIANA NAWE KUHUSU MUMEWE** Mume huyo ni Uwesu bin As-Swaamit, mmoja katika Answaar. **NA MWENYEZI MUNGU ANAYASIKIA**

**MAJADILIANO YENU.** Yaani: Mwenyezu Mungu anasikia maneno mnayojibizana.

(2) **WALE WANAOWAFANYIA DHIHARI WAKE ZAO KATIKA NYINYI.** Maana ya Dhihari ni mtu kumwambia mkewe: 'Wewe kwangu ni kama mgongo wa mama yangu'. Na wala hakuna upinzani katika maana hii ya Dhihari.

(3) **HAO SIO MAMA ZAO.** Yaani: Wake zao sio mama zao, hivyo basi huo ni uongo wao. Katika hili, kuna kuwafedhehesha na kuwaliza wanaofanya Dhihari **HAWAKUWA MAMA ZAO ILA TU WALE WALIOWAZAA** Yaani: Hawakuwa mama zao ila tu wale kinamama waliowazaa wao. **NA HAKIKA, WAO WANASEMA MANENO YA KUCHUSHA NA UZUSHI.** Yaani: Kwa hakika, wenye kufanya Dhihari, kwa kauli yao hii, wanasema maneno ya uovu, yaani ni maneno machafu yanayokanushwa na sheria, na ambayo ni mtu kumfananisha mkewe anayejamiiana naye (kumfananisha) na mama yake. Katika hili, kuna udhalilishaji mkubwa wa mama yake. Uzushi ni uongo. **NA KWA YAKINI, MWENYEZI MUNGU NI MWINGI WA KUSAMEHE, MSAMEHEVU SANA.** Yaani: Mwingi wa kusameha na kughufiria, kwa kule kuwawekea kafara kuwa mwokozi wa kuwanasua kutoka katika uovu huu.

(4) **NA WALE WANAOWAFANYIA DHIHARI WAKE ZAO KISHA WAKARUDI KATIKA YALE WALIYOYASEMA.** Wakarudi katika ile hali waliyokuwa nayo ya kutaka kujamiiana **BASI NI KUMKOMBOA MTUMWA.** Yaani: Ni wajibu kwao, kwa sababu ya yale waliyoyasema, kumkomboa mtumwa wa kike au wa kiume mwenye kumilikiwa. Imesemwa kuwa kurudi ni kumzuia mke baada ya Dhihari pamoja na kuwa na uwezo wa kumpa Talaka. **KABLA HAWAJAGUSANA.** Muradi wa kugusana hapa ni kujamiiana. Kwa hiyo, haifai kwa mwenye kufanya Dhihari kumjamii mkewe mpaka atoe kafara. **HAYO KWENU** Hukumu iliyotajwa **MNAONYWA KWAYO.** Yaani: Mnaamrishwa au mnakemewa kwa hayo ili muache kufanya Dhihari.

(5) **NA ASIYEPATA (MTUMWA WA KUMKOMBOA), BASI NI KUFUNGA MIEZI MIWILI MFULULIZO KABLA YA KUGUSANA.** Yaani: Asiyepata mtumwa katika miliki yake, na asiwe na thamani yake, au hakupata mtumwa wa kumnunua, basi ni juu yake kufunga miezi miwili yenye kufuatana; hafungui ndani yake. Kama akifungua, basi ataanza upya, ikiwa kafungua huko ni bila ya udhuru. Lau kama atajamiiana naye usiku au mchana kwa makusudi, ataanza upya kufunga. **NA ASIYEWEZA** Yaani:Asiyeweza kufunga miezi miwili mfululizo, **BASI NI KUWAPA CHAKULA MASIKINI SITINI.** Kila masikini apewe nusu pishi ya ngano au tende au mchele au mfano wake. Inafaa kuwapa chakula kilichopikwa wakala hadi wakashiba, au awape kitakachowashibisha. **HAYO NI KWA AJILI MPATE KUMUAMINI MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE** Yaani: Tumehukumu hilo ili mkubali kuwa Allah ameliamrisha na ameliwekea sheria, na ili msimame kwenye mipaka ya sheria wala msiivuke, na msirudie Dhihari ambayo ni kauli chafu na ni uzushi. **NA HIZO** Sheria zilizotajwa **NI MIPAKA YA MWENYEZI MUNGU** Kwa hiyo, msivuke mipaka yake aliyokuwekeeni, kwa kuwa yeye amekubainishieni kuwa Dhihari ni maasi, na kuwa kafara iliyotajwa inawajibisha msamaha na maghufira. **NA MAKAFIRI** Ambao hawasimami kwenye mipaka ya Allah **WATAPATA ADHABU IUMIZAYO.** Nayo ni adhabu ya Jahanamu.

(6) **HAKIKA, WANAOMPINGA MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE.** Upinzani ni kufanyiana ugumu, uadui na ukinzani. **WATADHALILISHWA KAMA WALIVYO DHALILISHWA WALIOKUWEPO KABLA YAO.** Yaani: Watadhalilishwa na kufedheheshwa.

(7) **SIKU MWENYEZI MUNFU ATAKAPOWAFUFUA WOTE.** Yaani: Wakiwa wamejumuika katika hali moja. Hatabaki yeyote asiyefufuliwa. **NA AWAAMBIA YALE WALIYOYATENDA.** Vitendo vibaya walivyovitenda duniani, ili kukamilisha hoja dhidi yao. **MWENYEZI MUNGU AMEYADHIBITI.** Allah ameyadhibiti yote (waliyoyatenda) na hakikumpita chochote katika hayo. **NA WAMEYASAHAU.** Wao hawakuyahifadhi, na kwa hiyo, watayakuta yako mbele yao, yakiwa yameandikwa katika madaftari yao. **NA MWENYEZI MUNGU NI MWENYE KUSHUHUDIA KILA KITU.** Ni Mwenye kujua na Mwenye kuona.

(8) **HIVI HUONI KWAMBA MWENYEZI MUNGU ANAVIJUA VILIVYOMO NDANI YA MBINGU NA VILIVYOMO NDANI YA ARDHI?** Yaani: Ujuzi wake umevizunguka vilivyomo ndani ya mbingu na ardhi, kwa namna ambayo hakifichikani kwake kitu chochote katika vilivyomo humo. **HAUPATIKANI MNON'GONO WOWOTE WA WATU WATATU.** Hakupatikani kunong'ona kwa watu watatu **ISIPOKUWA TU YEYE NI WA NNE WAO.** Anashirikiana nao katika kuujua mnong'ono huo. **WALA WA WATU WATANO ISIPOKUWA TU YEYE NI WA SITA WAO** Kwa sababu Yeye Mtukufu yuko pamoja na idadi zote; chache au nyingi, anajua siri na dhahiri, wala hakifichikani kwake cha kujificha. **WALA CHACHE ZAIDI YA HIYO WALA NYINGI**

أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ ۖ مَا يَكُونُ
مِن نَّجْوَىٰ ثَلَٰثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ
وَلَآ أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَآ أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا۟ ۖ ثُمَّ يُنَبِّئُهُم
بِمَا عَمِلُوا۟ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧﴾ أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلَّذِينَ
نُهُوا۟ عَنِ ٱلنَّجْوَىٰ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا نُهُوا۟ عَنْهُ وَيَتَنَٰجَوْنَ بِٱلْإِثْمِ
وَٱلْعُدْوَٰنِ وَمَعْصِيَتِ ٱلرَّسُولِ وَإِذَا جَآءُوكَ حَيَّوْكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ
بِهِ ٱللَّهُ وَيَقُولُونَ فِىٓ أَنفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا ٱللَّهُ بِمَا نَقُولُ ۚ حَسْبُهُمْ
جَهَنَّمُ يَصْلَوْنَهَا ۖ فَبِئْسَ ٱلْمَصِيرُ ﴿٨﴾ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا
تَنَٰجَيْتُمْ فَلَا تَتَنَٰجَوْا۟ بِٱلْإِثْمِ وَٱلْعُدْوَٰنِ وَمَعْصِيَتِ ٱلرَّسُولِ وَتَنَٰجَوْا۟
بِٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ٱلَّذِىٓ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٩﴾ إِنَّمَا ٱلنَّجْوَىٰ
مِنَ ٱلشَّيْطَٰنِ لِيَحْزُنَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَلَيْسَ بِضَآرِّهِمْ شَيْـًٔا
إِلَّا بِإِذْنِ ٱللَّهِ ۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١٠﴾ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ
ءَامَنُوٓا۟ إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوا۟ فِى ٱلْمَجَٰلِسِ فَٱفْسَحُوا۟ يَفْسَحِ
ٱللَّهُ لَكُمْ ۖ وَإِذَا قِيلَ ٱنشُزُوا۟ فَٱنشُزُوا۟ يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ دَرَجَٰتٍ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١١﴾

**ZAIDI.** Yaani: Na haipatikani idadi chache zaidi kuliko iliyotajwa, kama moja na mbili, wala nyingi zaidi ya hizo, kama sita na saba **ILA TU YEYE YU PAMOJA NAO.** Anayajua wanayonong'onezana, na hakijifichi kwake chochote katika hayo. **POPOTE PALE WALIPO** Mahali popote katika maeneo. **KISHA ATAWAAMBIA.** Yaani: Atawapa habari ya **WALIYOKUWA WAKIFANYA, SIKU YA KIYAMA.** Yaani: Ili wajue kuwa minong'ono yao haikuwa imejificha kwake, na ili kule kuwajulisha kwake wale waliokuwa wakinong'onezana maovu kuwe ni kuwafedhehesha, kuwaibisha na kuwalazimisha kukubali hoja.

(9) **HIVI HUWAONI WALE WALIOKATAZWA KUNON'GONEZANA KISHA WAKAYARUDIA YALE WALIYOKATAZWA?** Wayahudi walikuwa akipita kwao mtu katika waumini wananong'onezana baina yao, hadi muumini anadhania vibaya. Kwa hiyo, Allah akawakataza na hawakukatazika. Kwa sababu hiyo, ilishuka aya hii. **NA WANANON'GONEZANA DHAMBI.** Kwa kuwasengenya na kuwaudhi waumini na mfano wa hayo, kama kudhulumu na kusema uongo. **NA UADUI** wananong'onezana yale ambayo yana uadui kwa waumini. **NA KUMUASI MTUME** Kumpinga. **NA WAKIKUJIA, WANAKUAMKIA KWA MAAMKIZI ASIYOKUAMKIA KWAYO MWENYEZI MUNGU.** Wanaokusudia kwa aya hiyo ni Wayahudi. Walikuwa wanamjia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na kusema: "Assaamu Alayka". Kwa kusema hivyo, wanakusudia maamkizi kwa dhahiri na ilhali wao kwa undani wanakusudia kifo. Kwa hiyo, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) anasema: "Alaykum". **NA WANASEMA KATIKA NAFSI ZAO:** Yaani: Baina ya wao kwa wao kwamba: **MBONA MWENYEZI MUNGU HATUADHIBU KWA TUYASEMAYO?** Yaani: Wanasema: "Lau kama Muhammad angekuwa Mtume, basi Allah angetuadhibu kwa kauli zetu za kumdharau". Imesemwa pia kwamba maana ni hii: "Lau kama Muhammad angekuwa ni Mtume, angejibiwa dhidi yetu, pale yeye anaposema: "Alaykum", na yangetufika mauti wakati huo. **JAHANAMU ITAWATOSHA.** Kuwaadhibu. Yaani: Adhabu yake itawatosha na mauti ya hivi sasa. **WATAIINGIA, NA MAREJEO MABAYA KABISA NI HAYO.** Nayo ni Jahanamu.

(10) **ENYI MLIOAMINI, MNAPONON'GONEZANA MSINON'GONEZANE DHAMBI NA UADUI NA KUMUASI MTUME.** Kama Wayahudi na wanafiki wafanyavyo hivyo. **NA NON'GONEZANENI WEMA NA UCHAMUNGU.** Yaani: Non'gonezaneni utiifu na kuacha dhambi. **NA MCHENI MWENYEZI MUNGU AMBAYE KWAKE TU MTAKUSANYWA.** Kwa hiyo, atakulipeni kwa mujibu wa matendo yenu.

(11) **KWA HAKIKA, HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA MINON'GONO** Yaani: Kunon'gona dhambi, uadui na kumuasi Mtume **INATOKANA NA SHETANI** Sio kutoka kwa mwengine. Yaani: Ni kutokana na upambaji na ushawishi kwake. **ILI WAHUZUNIKE WALE WALIOAMINI** Yaani: Kwa ajili ya kuwatia katika huzuni, kutokana na shaka inayowapata kuwa ni katika vitimbi wanavyofanyiwa. **NA SI MWENYE KUWADHURU CHOCHOTE.** Yaani: Na shetani mwenyewe au minon'gono anayoipamba haiwezi kuwapa waumini madhara yoyote **ILA TU KWA IDHINI YA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Kwa matakwa yake. **NA KWA MWENYEZI MUNGU TU WATEGEMEE WAUMINI.** Yaani: Waegemeze mambo yao kwake, na kumtegemea katika mambo yao yote. Wajikinge kwa Allah kutokana na shetani, wala wasijali minong'ono anayoipamba shetani. Bukhari na Muslim na wapokezi wengine

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا نَـٰجَيْتُمُ ٱلرَّسُولَ فَقَدِّمُواْ بَيْنَ يَدَىْ نَجْوَىٰكُمْ
صَدَقَةً ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَأَطْهَرُ ۚ فَإِن لَّمْ تَجِدُواْ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ
﴿١٢﴾ ءَأَشْفَقْتُمْ أَن تُقَدِّمُواْ بَيْنَ يَدَىْ نَجْوَىٰكُمْ صَدَقَـٰتٍ ۚ فَإِذْ لَمْ تَفْعَلُواْ
وَتَابَ ٱللَّهُ عَلَيْكُمْ فَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَطِيعُواْ ٱللَّهَ
وَرَسُولَهُۥ ۚ وَٱللَّهُ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٣﴾ ۞ أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلَّذِينَ تَوَلَّوْاْ قَوْمًا
غَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِم مَّا هُم مِّنكُمْ وَلَا مِنْهُمْ وَيَحْلِفُونَ عَلَى ٱلْكَذِبِ
وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٤﴾ أَعَدَّ ٱللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا ۖ إِنَّهُمْ سَآءَ مَا كَانُواْ
يَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾ ٱتَّخَذُوٓاْ أَيْمَـٰنَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّواْ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ فَلَهُمْ
عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿١٦﴾ لَّن تُغْنِىَ عَنْهُمْ أَمْوَٰلُهُمْ وَلَآ أَوْلَـٰدُهُم مِّنَ ٱللَّهِ
شَيْـًٔا ۚ أُوْلَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَـٰلِدُونَ ﴿١٧﴾ يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ
ٱللَّهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُۥ كَمَا يَحْلِفُونَ لَكُمْ ۖ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَىْءٍ ۚ أَلَآ
إِنَّهُمْ هُمُ ٱلْكَـٰذِبُونَ ﴿١٨﴾ ٱسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ ٱلشَّيْطَـٰنُ فَأَنسَىٰهُمْ ذِكْرَ
ٱللَّهِ ۚ أُوْلَـٰٓئِكَ حِزْبُ ٱلشَّيْطَـٰنِ ۚ أَلَآ إِنَّ حِزْبَ ٱلشَّيْطَـٰنِ هُمُ ٱلْخَـٰسِرُونَ
﴿١٩﴾ إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحَآدُّونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ أُوْلَـٰٓئِكَ فِى ٱلْأَذَلِّينَ ﴿٢٠﴾
كَتَبَ ٱللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا۠ وَرُسُلِىٓ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ قَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾

wamenukuu kutoka kwa Ibn Masoud akiesema kuwa: *"Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba: Mnapokuwa watatu, wasinong'one wawili bila ya watatu (kujua), kwa sababu hilo litamhuzunisha".*

(12) **ENYI MLIOAMINI, MNAPOAMBIWA: TOENI NAFASI KATIKA MABARAZA** Allah amewaamrisha Waumini kufanyiana adabu nzuri wao kwa wao kwa kutoa nafasi katika vikao na kuacha kubanana katika kukaa humo. Qatadah na Mujahid wamesema kuwa: "Watu walikuwa wanashindana katika kikao cha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). Kwa hiyo, wakaamriwa baadhi yao kuwapatia nafasi wengine. **BASI TOENI NAFASI, MWENYEZI (NAYE) ATAKUPENI NAFASI** Yaani: Panueni nafasi, na Allah atakukunjulieni nafasi katika pepo. Aya hiyo inaenea katika kila kikao ambacho Waislamu wanakusanyika, kwa ajili ya kutafuta kheri na thawabu, sawa iwe ni kikao cha vita au kumkumbuka Allah au hotuba ya Ijumaa. Kila mmoja ana haki zaidi ya mahali pake ambapo ametangulia (amepawahi), isipokuwa tu anatakiwa kumpanulia nafasi ndugu yake. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema kuwa: *"Mtu asimsimamishe mtu (mwengine) katika majlisi yake kisha akakaa yeye, na lakini toeni nafasi na panueni".* **NA MKIAMBIWA: ONDOKENI, BASI ONDOKENI.** Yaani: Pindi baadhi ya waliokaa katika kikao wakiombwa kuinuka kutoka katika sehemu zao ili wakae hapo watu wenye fadhila (ubora) katika dini, na wanazuoni wanaomjua Allah, basi wainuke. **MWENYEZI MUNGU ATAWANYANYUA DARAJA NYINGI WALE WALIOAMINI MIONGONI MWENU NA WALE WALIOPEWA ELIMU.** Yaani: Atawanyanyua wale waliopewa elimu miongoni mwenu daraja za juu katika heshima duniani na thawabu Akhera. Basi mwenye kukusanya imani na elimu, Allah atamnyanyua kwa imani yake daraja nyingi, kisha atamnyanyua kwa elimu yake daraja (nyingine) nyingi. Na ni katika jumla ya unyanyuliwaji huo kuheshimiwa kwake katika vikao. **NA MWENYEZI MUNGU NI MTAMBUZI WA MNAYOYATENDA.**

(13) **ENYI MLIOAMINI, MNAPONON'GONEZANA NA MTUME TOENI SADAKA KABLA YA KUNON'GONA KWENU** Yaani: Mnapotaka kuzungumza kwa siri na Mtume katika jambo lolote miongoni mwa mambo yenu, basi kabla ya kuzungumza naye tangulizeni kutoa sadaka. Mwenyezi Mungu aliiteremsha aya hii, na hivyo, watu waovu wakakoma kumnon'goneza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwakuwa wao hawakutanguliza kutoa sadaka kabla ya mazungumzo yao. Pia jambo hili lilikuwa zito kwa watu wa imani, na walijizuia kunong'ona na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa sababu ya udhaifu wa wengi wao wa kutoweza kutoa sadaka. Halafu Mwenyezi Mungu akawafanyia tahfifu ya jambo hilo kwa aya inayofuata. **JAMBO HILO** Kutoa sadaka kabla ya kunong'ona na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) **NI BORA ZAIDI KWENU NA NI UTAKASO ZAIDI** Kwa kuwa katika kufanya hivyo kuna kumtii Allah. **NA IKIWA HAMKUPATA, BASI MWENYEZI MUNGU NI MWINGI WA MSAMAHA, MWINGI WA REHEMA** Yaani: Yeyote miongoni mwao ambaye hakupata hiyo sadaka, hana kosa katika kunong'ona na Mtume bila ya kutoa sadaka.

(14) **HIVI MNACHELEA KUTANGULIZA KUTOA SADAKA KABLA YA KUNONG'ONA KWENU?** Yaani: Hivi mmeogopa ufukara na umasikini kwa kufanya hilo? Muqaatil amesema kuwa: *"Hilo lilikuwa katika siku kumi kisha likafutwa".* **KWA KUWA HAMKUTEKELEZA** jambo mliloamriwa la kutoa sadaka kabla ya kunon'gona, kwa sababu ya kuwa zito kwenu **NA MWENYEZI MUNGU AKAKUSAMEHENI** Kwa kuwa amekupeni ruhusa ya kuacha **BASI SIMAMISHENI SALA NA TOENI ZAKA.**

Maana yake: Ukikutokozeeni uzito wa kutoa sadaka kabla ya kunon'gona, basi kuweni imara katika kusimamisha sala, kutoa zaka na kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. **NA MWENYEZI MUNGU NI MWENYE HABARI ZA MNAYOYATENDA** Basi yeye ndiye atakaye kulipeni.

(15) **HIVI HUWAONI WALE AMBAO WAMEFANYA URAFIKI NA WATU** Yaani: Wamewafanya marafiki wa ndani, nao ni wanafiki waliofanya urafiki na Wayahudi **AMBAO MWENYEZI MUNGU AMEWAKASIRIKIA?** Waliokasirikiwa ni Wayahudi. **WAO SI KATIKA NYINYI WALA SI KATIKA WAO** Kama Allah alivyowaelezea kuwa**: "*Wanayumbayumba kati ya hilo; sio kwa hawa na wala sio kwa hawa (huku hawako na huko hawako*)."** Sura ,aya Inawezekana pia kuwa hao ni Wayahudi; kwa maana kwamba Mwenyezi Mungu anawaambia waumini kwamba: Wayahudi sio miongoni mwenu wala sio miongoni mwa wanafiki, sasa kwa nini wanafiki wasiwafanye Wayahudi marafiki zao? **NA WANA'APA UONGO** Yaani: Wana'apa kuwa wao ni Waislamu, au wanaapa kuwa wao hawakuhamisha habari kupeleka kwa Wayahudi. Yaani: Wanajua kuwa wanayoapia ni batili na ni uongo usiokuwa na ukweli wowote.

(16) **MWENYEZI MUNGU AMEWAANDALIA ADHABU KALI** Kwa sababu ya urafiki huu na kuapia batili. **KWA YAKINI, WALIYOKUWA WAKITENDA NI MAOVU SANA** Ni katika vitendo vibaya.

(17) **WAMEFANYA VIAPO VYAO NI NGAO** Nao ni ule uongo waliokuwa wakiapia kwamba wao ni miongoni mwa Waislamu, kwa lengo la kujilinda wasiuawe kwa sababu ya ukafiri. Kwa hiyo, wakafanya viapo hivi ni kinga na ngao ya kulinda damu zao. Kwa hiyo, ndimi zao zimeamini, kwa kuogopa kuuawa na nyoyo zao hazikuamini.**NA HIVYO WAKAWA KIKWAZO DHIDI YA NJIA YA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Wamezuia watu wasiufuate Uislamu kwa sababu ya hujuma wanazofanya, kufifisha mambo Waislamu na kudhoofisha nguvu yao. **BASI HAO WATAPATA ADHABU INAYONYONGESHA.** Yaani: Adhabu itakayowadhalilisha na kuwafedhehesha.

(18) **SIKU MWENYEZI MUNGU ATAKAPOWAFUFUA NA WAKAMUAPIA KAMA WANAVYOKUAPIENI NYINYI.** Yaani: Wata'apa uongo kwa Allah Siku ya Kiama, kama wanavyokuapieni nyie duniani. Watasema:*"Wallahi Mola wetu, hatukufanya hivyo"*. Na hii ni kutokana na ukubwa wa uovu wao, kwakuwa ukweli Siku ya Kiama utafunuka, na mambo yatakuwa yanajulikana kwa kuonekana. **NA WANADHANI KUWA WAMEPATA KITU** Yaani: Watadhani huko Akhera kuwa wao, kwa hivyo viapo vyao vya uongo, wana jambo la kuwapatia manufaa, au kuwaondolea madhara, kama walivyokuwa wakidhania hivyo duniani.

(19) **SHETANI AMEWATAWALA** Yaani: Amewashinda, amewakalia juu na kuwazingira. **HIVYO, AKAWASAHAULISHA KUNKUMBUKA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Wakaacha maamrisho yake na wakaacha kumtii. **HAO NI KUNDI LA SHETANI** Yaani: Ni jeshi lake, wafuasi wake na kundi lake **EE! KWA YAKINI, KUNDI LA AHETANI NDIO LENYE HASARA** Kwa kuwa wao wameuza pepo kwa moto, uongofu kwa upotevu, wamemuongopea Allah na Mtume wake (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*). Watapata hasara duniani na Akhera.

(20) **HAKIKA, WALE WANAOMPINGA MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE** Maana ya kumpinga Allah na Mtume wake imetangulia kuelezwa mwanzoni mwa sura hii. **HAO WATAKUWA KATIKA WATU DHALILI SANA** Watakuwa jumla ya yale mataifa aliowadhalilisha Allah, duniani na akhera.

(21) **MWENYEZI MUNGU AMEANDIKA KUWA: KWA YAKINI KABISA, NITASHINDA; MIMI NA MITUME WANGU** Amekata shauri katika elimu yake ya azali kuwa: Mimi na Mitume wangu tutashinda, kwa hoja na uwezo. **KWA YAKINI, MWENYEZI MUNGU NI MWENYE NGUVU, MWENYE KUSHINDA** Ni Mwenye nguvu katika kuwanusuru mawalii (wapenzi) wake, Mwenye kuwashinda adui zake. Hakuna yeyote amshindaye.

(22) **HUWAKUTI WATU WANAOMWAMINI MWENYEZI MUNGU NA SIKU YA MWISHO WANAPENDANA NA WALE WANAOPINGANA NA MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE** Wanawapenda na kuwa na uswahiba wa ndani na wale wanaomfanyia uadui na kumpinga Allah na Mtume wake. **NA HATA KAMA WALIKUWA BABA ZAO AU WATOTO WAO AU NDUGU ZAO AU JAMAA ZAO.** Yaani: Japokuwa wanaopingana na Allah na Mtume wake ni baba wa hao wanaopenda, kwa sababu imani inakemea kulikataza hilo. Kulichunga hilo ni jambo linalotakiwa kuwa na nguvu zaidi kuliko kuchunga ubaba, utoto, udugu na ujamaa. **HAO** Yaani: Wale ambao hawawapendi wanaopingana na Allah na Mtume wake **(ALLAH) AMEANDIKA IMANI KATIKA NYOYO ZAO** Ameiimarisha. Imesemwa pia: Ameijaalia. Pia imesemwa:

لَّا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ يُوَآدُّونَ مَنْ
حَآدَّ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَوْ كَانُوٓا۟ ءَابَآءَهُمْ أَوْ أَبْنَآءَهُمْ
أَوْ إِخْوَٰنَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ كَتَبَ فِى قُلُوبِهِمُ
ٱلْإِيمَٰنَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ ۖ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِى
مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَا ۚ رَضِىَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟
عَنْهُ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ حِزْبُ ٱللَّهِ ۚ أَلَآ إِنَّ حِزْبَ ٱللَّهِ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿٢٢﴾

ترتيبها ٥٩ — سُورَةُ ٱلْحَشْرِ — آياتها ٢٤

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ ۖ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ
﴿١﴾ هُوَ ٱلَّذِىٓ أَخْرَجَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِنْ أَهْلِ ٱلْكِتَٰبِ مِن دِيَٰرِهِمْ
لِأَوَّلِ ٱلْحَشْرِ ۚ مَا ظَنَنتُمْ أَن يَخْرُجُوا۟ ۖ وَظَنُّوٓا۟ أَنَّهُم مَّانِعَتُهُمْ
حُصُونُهُم مِّنَ ٱللَّهِ فَأَتَىٰهُمُ ٱللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا۟ ۖ وَقَذَفَ
فِى قُلُوبِهِمُ ٱلرُّعْبَ ۚ يُخْرِبُونَ بُيُوتَهُم بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِى ٱلْمُؤْمِنِينَ
فَٱعْتَبِرُوا۟ يَٰٓأُو۟لِى ٱلْأَبْصَٰرِ ﴿٢﴾ وَلَوْلَآ أَن كَتَبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِمُ
ٱلْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ فِى ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَهُمْ فِى ٱلْـَٔاخِرَةِ عَذَابُ ٱلنَّارِ ﴿٣﴾

Ameikusanya. **NA AMEWAPA NGUVU KWA ROHO KUTOKA KWAKE** Amewatia nguvu kwa msaada utokao kwake, wa kuwashinda maadui zao duniani. Msaada wake kwao ameuita kuwa ni roho, kwa sababu mambo yao yanakuwa hai kwa msaada huo. **NA ATAWAINGIZA KATIKA BUSTANI AMBAZO INAPITA MITO KATI YAKE, WAKIDUMU HUMO MILELE** milele. **MWENYEZI MUNGU AMEWAWIA RADHI** Yaani: Amekubali matendo yao na kuwamiminia rehema zake za za sasa (duniani) na za baadae (Akhera). **NA (WAO) WAMEMUIA RADHI** Yaani: Wameyafurahia yale Allah aliyowapa sasa (hapa duniani) na (atakayowapa) baadae (Akhera). **HAO NDIO KUNDI LA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Jeshi lake ambalo linatekeleza amri zake, wanapigana na adui zake na wanawanusuru mawalii (wapenzi) wake. **EE! KWA YAKINI, KUNDI LA MWENYEZI MUNGU NDIO WENYE KUFAULU** Ndio wenye kufuzu kwa kupata wema wa duniani na Akhera. Ibni Abuhatim, Tabarani na Hakim wamesimulia kwamba: *"Mzazi wa Abuobaidah Ibni Jarrah alikuwa anamshambulia Abuobaidah siku ya (vita vya) Badri, na Abuobaidah akawa anamkwepa. Lakini mzazi wake alipozidi kumshambulia, Abuobaidah naye alimshambulia baba yake na kumuua. Kwa sababu hiyo, ilishuka aya hii".*

# SURATUL-HASHRI (59)

*(Imeteremka Madina)*

2 **YEYE NDIYE ALIYEWATOA WALE WATU WA KITABU WALIOKUFURU KUTOKA KATIKA MIJI YAO KWA MJUMUIKO WA KWANZA** Hao ni Baninadhiir, kundi la Wayahudi katika kizazi cha Huruna. Walifika Madina katika wakati wa misukosuko ya Waisraili. Kwa hiyo, walimfanyia vitimbi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) baada ya kuwa wamewekeana naye mkataba (wa amani), na hivyo, wakawa wako pamoja na makafiri dhidi yake. Hapo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliwazingira hadi waliporidhia kuondoka. Kalbiy amesema kuwa: *"Walikuwa ni Watu wa Kitabu wa kwanza kufukuzwa katika kisiwa cha Arabuni (Arabian Peninsula). Halafu wa mwisho wao kufukuzwa ni wakati wa Umar (Binkhattab). Kwa hiyo, kufurushwa kwao (wakati wa Mtume) kulikuwa ni mjumuiko wa kwanza kuondoka Madina, na mkusanyiko wa mwisho ni pale Umar alipowatimua".* Imesemwa pia kwamba: Mjumuiko wa mwisho ni pale watu wote watakapokusanywa kuelekea katika ardhi ya Mjumuiko. **HAMKUDHANI KUWA WATATOKA** Yaani: Hamkudhani enyi Waislamu kwamba Baninadhiir wangetoka katika miji yao, kutokana na nguvu yao na uimara wao. Walikuwa na ngome madhubuti, majumba na mashamba makubwa ya mitende, idadi kubwa ya watu na silaha. **NA (WAO) WALIDHANI KUWA NGOME ZAO ZITAWALINDA (WASIADHIBIWE) NA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Baninadhiir walidhani kuwa ngome zao zitawakinga na adhabu za Allah. **MWENYEZI MUNGU AKAWAFIKIA KWA NAMNA AMBAYO HAWAKUITAZAMIA** Yaani: Mambo ya Mwenyezi Mungu yaliwafikia kwa namna ambayo haikuingia akilini mwao kwamba yangewafikia kwa namna hiyo. Namna yenyewe ni kwamba Allah Mtukufu alimuamrisha Mtume wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kupigana nao na kuwafukuza. Hawakudhania kuwa hali ingefikia hatua hiyo. Walikuwa wakijiona kuwa wao ni watukufu sana na wenye nguvu sana. **NA AKATIA WOGA KATIKA NYOYO ZAO** Woga ni hofu ya hali ya juu. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema kuwa: *"Nimenusuriwa kwa woga umbali wa mwezi mzima".* **(WAKAWA) WANAZIBOMOA NYUMBA**

**ZO KWA MIKONO YAO NA MIKONO YA WAUMINI.** Hali hiyo ni kwamba walipokuwa na uhakika wa kufukuzwa, waliwaonea gere Waislamu kuwa watakaa katika nyumba zao, na hivyo, wakaamua kuzivunja kwa ndani, na huku Waislamu nao wakawa wanazivunja kwa nje. Azzuhriy na Urwa bin Zubeir wanasema kuwa: *"Mtume* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *alipofanya nao makubaliano ya kuwa wachukue vitu ambavyo vinaweza kubebwa na ngamia, waliona kuwa ni vizuri wachukue mbao na nguzo. Kwa hiyo, wakabomoa nyumba zao na kuchukua vitu hivyo kwa kutumia ngamia wao, na Waislamu wakabomoa sehemu zilizobaki".* **BASI ZINGATIENI ENYI WENYE MACHO!** Yaani: Jueni kwamba Allah anafanya hivyo kwa yule ambaye amekengeuka ahadi na kupingana na Mwenyezi Mungu.

(3) **NA LAU KAMA MWENYEZI MUNGU ASINGELIWAANDIKIA KUONDOLEWA, ANGELIWAADHIBU DUNIANI** Yaani: Lau kama Allah asingewaandikia kuondolewa katika miji yao kwa njia hiyo na kulihukumu hilo kwao, angewaadhibu kwa kuuawa na kutekwa duniani, kama alivyofanya kwa Baniquraidhah.

(4) **HIYO NI KWA SABABU, WAO WALIPINGANA NA MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE** Yaani: Kwa sababu ya uadui wao kwa Allah na Mtume wake na kuvunja kwao ahadi, wamestahili kuadhibiwa.

(5) **MTENDE WOWOTE MLIOUKATA AU MLIOUACHA UMESIMAMA JUU YA MASHINA YAKE, BASI NI KWA IDHINI YA MWENYEZI MUNGU.** Baadhi ya Waislamu katika vita vya Baninadhiir walikuwa wanakata mitende ya makafiri kwa ajili ya kuwaudhi. Baninadhiir, ambao ni Watu wa Kitabu, wakasema: *"Ewe Muhammad, si unadai kuwa wewe ni Mtume unayetaka kufanya wema? Sasa je, ni katika wema kukata mitende na kuchoma miti? Je, umepata katika uliyoteremshiwa kuhalalisha ufisadi (uharibifu) katika ardhi?".* Hilo likawa zito kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na Waislamu wakapata huzuni katika nafsi zao. Kwa sababu hiyo, ikashuka aya hii: **NA ILI AWAFEDHEHESHE WAOVU**. Yaani: Ili awadhalilishe waliotoka kwenye utii, nao ni Wayahudi na kuwaudhi kwa kuikata mitende na kuiacha. Wao walikuwa wakiwaona Waislamu wakifanya watakavyo katika mali zao, wanazidi kupata maudhi na kufedheheka.

(6) **NA KILE ALICHOKILETA MWENYEZI MUNGU KWA MTUME WAKE KUTOKA KWAO, HAMKUKIENDEA MBIO KWA FARASI WALA NGAMIA**. Yaani: Zile mali za Baninadhiir alizozirudisha Allah kwa Mtume wake

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُّوا۟ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ ۖ وَمَن يُشَآقِّ ٱللَّهَ فَإِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ
ٱلْعِقَابِ ﴿٤﴾ مَا قَطَعْتُم مِّن لِّينَةٍ أَوْ تَرَكْتُمُوهَا قَآئِمَةً
عَلَىٰٓ أُصُولِهَا فَبِإِذْنِ ٱللَّهِ وَلِيُخْزِىَ ٱلْفَٰسِقِينَ ﴿٥﴾ وَمَآ أَفَآءَ ٱللَّهُ
عَلَىٰ رَسُولِهِۦ مِنْهُمْ فَمَآ أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلَا رِكَابٍ
وَلَٰكِنَّ ٱللَّهَ يُسَلِّطُ رُسُلَهُۥ عَلَىٰ مَن يَشَآءُ ۚ وَٱللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ
قَدِيرٌ ﴿٦﴾ مَّآ أَفَآءَ ٱللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ مِنْ أَهْلِ ٱلْقُرَىٰ فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ
وَلِذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ كَىْ لَا يَكُونَ
دُولَةًۢ بَيْنَ ٱلْأَغْنِيَآءِ مِنكُمْ ۚ وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا
نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٧﴾
لِلْفُقَرَآءِ ٱلْمُهَٰجِرِينَ ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِمْ وَأَمْوَٰلِهِمْ
يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ ٱللَّهِ وَرِضْوَٰنًا وَيَنصُرُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ
هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ ﴿٨﴾ وَٱلَّذِينَ تَبَوَّءُو ٱلدَّارَ وَٱلْإِيمَٰنَ مِن قَبْلِهِمْ
يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِى صُدُورِهِمْ حَاجَةً
مِّمَّآ أُوتُوا۟ وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ
وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِۦ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾

(Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) hamkupanda farasi wala ngamia ili kuzipata, na wala hamkuzipatia usumbufu wowote, wala hamkuzipigania vita vyovyote, kwani zilikuwa maili mbili kutoka Madina. Kwa hiyo, Allah akafanya mali za Baninadhiir ni za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) pekee kwa sababu hii, kwa kuwa yeye alizikomboa kwa suluhu na kuchukua mali hizo, na hakuzigawa kwa waliozikusanya.

(7) **KILE ALICHOKILETA MWENYEZI MUNGU KWA MTUME WAKE KUTOKA KWA WATU WA VIJIJINI** Huu ni ufafanuzi wa maeneo ya mgawo wa fay-I (ngawira) baada ya ule ufafanuzi wa awali kwamba ngawira ni za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) tu. Na hiyo ndio sheria ya kila kitongoji atakachokikomboa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na suluhu bila ya vita, hadi Siku ya Kiama, na ikiwa Waislamu hawakuzipatia tabu ngawira hizo kwa kutumia farasi wala kipando. **BASI NI KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU** Anahukumu ndani yake kwa atakavyo. **NA KWA AJILI YA MTUME** Inakuwa ni miliki yake, kisha itumike katika maslahi ya Waislamu. **NA NDUGU** Hao ni Banihashim na Banimutwalib. Yaani: Wapewe fukara katika wao, kwa sababu wamekatazwa kuchukua sadaka, na hivyo, wamewekewa haki

katika ngawira. **NA YATIMA** Watoto waliofiwa na baba zao kabla ya kufikia balehe. **NA MASIKINI** Fukara. **NA MSAFIRI** Mgeni ambaye matumizi yake yamekwisha. **ILI KISIWE KIKIZUNGUKA BAINA YA MATAJIRI TU MIONGONI MWENU** Matajiri wakawazidi masikini wakawa wanapeana wao kwa wao. **NA ANACHOKUPENI MTUME KICHUKUENI, NA ANACHOKUKATAZENI JIEPUSHENI NACHO.** Yaani: Mali ya ngawira aliyokupeni ichukueni, na aliyokukatazeni kuchukua iacheni na msiichukue. **WAPEWE FUKARA WAHAMIAJI, WALIOTOLEWA KATIKA MIJI YAO** Makkah. Waliwalazimisha kutoka humo wakatoka, na kwa hiyo wakawekewa haki katika ngawira ili iwakimu. **WAKITAFUTA FADHILA NA RADHI KUTOKA KWA MWENYEZI MUNGU.** Kwa riziki duniani na radhi Akhera. **NA WAKIMNUSURU MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE** Kwa kupigana Jihadi na makafiri. **HAO TU NDIO WAKWELI.** Yaani: Wenye kubobea katika ukweli.

(9) **NA WALE WALIOFANYA MAKAZI YA MJI NA IMANI KABLA YAO** Hao ni Ansari (Watetezi wa Mtume) walioishi Madina kabla ya Wahamiaji (Muhajirina), na wakamwamini Allah na Mtume wake. **WANAWAPENDA WALE WALIOHAMIA KWAO.** Waliwafanyia mambo mazuri Muhajirina na kuwashirikisha katika mali zao na makazi yao. **NA HAWAONI SHIDA YOYOTE KATIKA VIFUA VYAO** Kwa kuona husuda au chuki au kukerwa. **KUTOKANA NA VILE VITU WALIVYO PEWA (WAHAMIAJI).** Yaani: Kutokana na waliyopewa Muhajirina. Bali nafsi zao zilikuwa radhi kwa hilo, na Muhajirina wakawa wanakaa katika nyumba za Ansari. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alipopata ghanima ya mali za Baninadhir aliwaita Ansari na kuwashukuru kwa wema waliowafanyia Muhajirina; wa kuwaweka kwenye makazi yao na kuwashirikisha katika mali zao. Kisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akasema: "*Mkipenda, nitagawa ile ngawira aliyonipa Allah kutoka kwa Baninadhiir baina yenu na baina ya Muhajirina, na Muhajirina waendelee na hali yao hiyo hiyo ya kuishi katika makazi yenu na kushirikiana katika mali zenu. Na mkipenda, nitawapa wao hiyo ngawira na watoke katika nyumba zenu*". Wakaridhia mgao huo wa kupewa Muhajirina na nafsi zao zikawa radhi. **BALI WANAWAPENDELEA KULIKO NAFSI ZAO** Wanawatanguliza Muhajirina kuliko nafsi zao katika maslahi ya kidunia **NA JAPOKUWA WAO WANA UHITAJI** Yaani: Shida na ufukara. **NA WENYE KUEPUSHWA UCHOYO WA NAFSI ZAO, BASI HAO NDIO WENYE KUFANIKIWA** Yaani: Ambaye Allah amemkinga na tamaa ya nafsi yake na ubahili wake, na kwa hiyo, akatekeleza yaliyowajibishwa na sheria, katika mali, ikiwa ni pamoja na Zaka au haki, basi huyo atakuwa amefuzu na kufaulu. Na hatafuzu ambaye ameyafanyia ubahili hayo, na nafsi yake ikayafanyia uchoyo.

(10) **NA WALIO KUJA BAADA YAO** Nao ni wale wenye kuwafuata wao kwa uzuri hadi Siku ya Kiama. **WANASEMA: EWE MOLA WETU, TUSAMEHE SISI NA NDUGU ZETU WALIOTUTANGULIA KWA IMANI** Ambao wanawapenda Muhajirina na Ansari waliotangulia, na wanawaombea msamaha. **WALA USIFANYE NDANI YA NYOYO ZETU MFUNDO (HUSDA) KWA WALIOAMINI** Yaani: Udanganyifu, bughudha na husuda. Kwa hiyo, wanaingia katika hali hiyo Swahaba kuingia kwa mwanzo, kwa kuwa wao ni Waumini watukufu zaidi, na kwakuwa mtiririko wa aya hizi unawazungumzia wao. Basi atakayepata chuki moyoni mwake ya kuwachukia wao, kama vile Shia, basi huyo amepatwa na mguso wa shetani na limemuangukia fungu kubwa la kumuasi Allah kwa kuwafanyia uadui Mawalii wake na watu bora zaidi wa umma wa Mtume wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), na hana haki yoyote katika ngawira. Ni hivyo hivyo aliyewatukana au kuwaudhi au kuwadharau.

(11) **HIVI HUWAONI WALE WALIOFANYA UNAFIKI** Hao ni Abdallah bin Ubayya bin Saluul na wafuasi wake. Walituma ujumbe kwa Baninadhir kwamba: *Kuweni imara na kazaneni. Sisi hatutakuacheni mshambuliwe. Na kama mkipigwa tutapigana pamoja nanyi, na mkitolewa* **TUTATOKA PAMOJA NANYI.** Yaani: Tutatoka majumbani mwetu ili tuwe pamoja nanyi. **NA HATUTAMTII** Yaani: Katika suala lenu na kwa ajili yenu **YEYOTE** Miongoni mwa wanaotaka kutukataza kutoka pamoja nanyi **ABADANI** Hata kama muda ukirefuka. **NA MKIPIGWA VITA, LAZIMA TUTAKUSAIDIENI** Dhidi ya adui wenu. Kisha Allah (Subhaanahu wa Taala) akakanusha madai yao na kusema: **NA MWENYEZI MUNGU ANASHUHUDIA KUWA, KWA YAKINI KABISA, WAO NI WAONGO** Katika yale waliyo waahidi, ikiwa ni pamoja na kutoka pamoja nao na kuwasaidia.

(12) **KWA YAKINI KABISA, IKIWA WATATOLEWA HAWATATOKA PAMOJA NAO, NA WAKIPIGWA HAWATAWASAIDIA.** Na hali ilikuwa hivyo. Wanafiki hawakutoka pamoja na Wayahudi waliofukuzwa na ambao ni Baninadhiir na waliokuwa pamoja nao. Pia wanafiki hawakuwasaidia Wayahudi waliopigwa na ambao ni Baniquraidha na watu wa Khaybar. **NA KAMA WATAWASAIDIA BASI WATARUDI NYUMA** Huku wakiwa

wameshindwa **KISHA HAWATANUSURIWA** Wanafiki hawatakuwa wenye kunusuriwa baada ya hapo, bali Allah atawadhalilisha na wala unafiki wao hautawanufaisha.

(13) **KWA HAKIKA KABISA, NYINYI NI TISHIO ZAIDI KATIKA VIFUA VYAO KULIKO MWENYEZI MUNGU** Yaani: Nyinyi, enyi mjumuiko wa Waislamu, mnatisha na kuogopwa sana vifuani mwa wanafiki au vifuani mwa Wayahudi kuliko wanavyomuogopa Allah. **HAYO NI KWA KUWA WAO NI WATU WASIOFAHAMU.** Na lau kama wangekuwa na ufahamu wangejua kuwa Allah (Subhaanahu wa Taala.) ndiye aliyekusalitisheni dhidi yao, na kwa hiyo basi yeye ndiye mwenye haki zaidi ya kuogopwa kuliko nyinyi.

(14) **HAWATAPIGANA NANYI KWA PAMOJA** Yaani: Wakiwa wamejumuika pamoja ili kukupigeni **ISIPO KUWA TU KATIKA VIJIJI VILIVYO IMARISHWA KWA ULINZI** Yaani: Katika vichochoro na nyumba **AU NYUMA YA KUTA** Yaani: Nyumba ya kuta ambazo wanajificha, kwa sababu ya uoga wao na hofu yao. **VITA VYA WAO KWA WAO NI VIKALI** Yaani: Baadhi yao ni wakorofi na wababe dhidi ya wengine. **UTAWADHANIA KUWA WAKO PAMOJA, NA ILHALI NYOYO ZAO NI MBALI MBALI** Yaani: Mkusanyiko wao ni mkusanyiko wa nje tu, kwa sababu ya kutafautiana nyoyo zao kwa ndani, mawazo yao yakiwa tofauti na mielekeo yao tofauti. **HAYO NI KWA KUWA WAO NI WATU WASIO NA AKILI.** Na lau kama wangekuwa na akili, wangeijua haki na kuifuata, na kwa hiyo wangekuwa pamoja wala wasingetofautiana.

(15) **NI KAMA MFANO WA WALE WALIOKUWEPO KABLA YAO** Ambao ni makafiri wa Kishirikina. **HIVI KARIBUNI** Yaani: Katika zama za karibu **WALIONJA UOVU WA MAMBO YAO** Yaani: Ubaya wa matokeo ya ukafiri wao katika dunia kwa kuuawa kwao siku ya vita vya Badri. Na hilo lilitokea kabla ya vita vya Baninadhiir kwa miezi sita.

(16) **NI KAMA MFANO WA SHETANI ALIPOMWAMBIA MWANADAMU: KUFURU** Yaani: Mfano wao katika kufedheheshana kwao na kutonusuriana ni kama mfano wa shetani kwa mwanadamu. Alimshawishi kukufuru, akampambia ukafiri na kumtwisha nao. **ALIPOKUFURU, AKAMWAMBIA: MIMI SIKO PAMOJA NAWE** Yaani: Mwanadamu alipokufuru kwa kumfuata shetani na kukubali kupamba kwake ukafiri, shetani alimwambia: *"Mimi najitenga nawe* **HAKIKA, MIMI NAMUOGOPA MWENYEZI MUNGU, MOLA WA WALIMWENGU".**

وَالَّذِينَ جَاءُو مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا
وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا
غِلًّا لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿١٠﴾ أَلَمْ تَرَ إِلَى
الَّذِينَ نَافَقُوا يَقُولُونَ لِإِخْوَانِهِمُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ
الْكِتَابِ لَئِنْ أُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ مَعَكُمْ وَلَا نُطِيعُ فِيكُمْ
أَحَدًا أَبَدًا وَإِنْ قُوتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ
﴿١١﴾ لَئِنْ أُخْرِجُوا لَا يَخْرُجُونَ مَعَهُمْ وَلَئِنْ قُوتِلُوا لَا يَنْصُرُونَهُمْ
وَلَئِنْ نَصَرُوهُمْ لَيُوَلُّنَّ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ ﴿١٢﴾
لَأَنْتُمْ أَشَدُّ رَهْبَةً فِي صُدُورِهِمْ مِنَ اللَّهِ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ
لَا يَفْقَهُونَ ﴿١٣﴾ لَا يُقَاتِلُونَكُمْ جَمِيعًا إِلَّا فِي قُرًى
مُحَصَّنَةٍ أَوْ مِنْ وَرَاءِ جُدُرٍ بَأْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيدٌ تَحْسَبُهُمْ
جَمِيعًا وَقُلُوبُهُمْ شَتَّىٰ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٤﴾
كَمَثَلِ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَرِيبًا ذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ
أَلِيمٌ ﴿١٥﴾ كَمَثَلِ الشَّيْطَانِ إِذْ قَالَ لِلْإِنْسَانِ اكْفُرْ فَلَمَّا كَفَرَ
قَالَ إِنِّي بَرِيءٌ مِنْكَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦﴾

Hii ni miongoni mwa kauli ya shetani katika njia ya kumkana mwanadamu.

(18) **ENYI MLIO AMINI, MCHENI MWENYEZI MUNGU** Yaani: Ogopeni adhabu yake kwa kufanya aliyokuamrisheni na kuacha aliyokukatazeni. **NA KILA NAFSI IANGALIE: IMEFANYA NINI KWA AJILI YA KESHO?** Yaani: Iangalie: Imefanya amali gani kwa ajili ya Siku ya Kiama?

(19) **NA MSIWE KAMA WALE WALIOMSAHAU MWENYEZI MUNGU** Yaani: Wameacha amri zake na hawakujali kumtii. **NA YEYE AKAWASAHAULISHA NAFSI ZAO** Amewafanya wazisahau nafsi zao kwa sababu ya kumsahau kwao Allah, na kutojishughulisha na matendo yatakayowaokoa na adhabu. Pia imesemwa kuwa maana nyingine ni kuwa: Walimsahau Mwenyezi Mungu wakati wa raha, Naye akawasahaulisha nafsi zao wakati wa shida. **HAO NDIO WAOVU** Yaani: wametoka katika kumtii Mwenyezi Mungu.

(20) **WATU WA PEPONI NDIO TU WENYE KUFUZU** Yaani: Ndio wenye kupata kila watakalo, wenye kuokoka na kila walichukialo.

(21) **LAU KAMA TUNGEITEREMSHA HII QUR'ANI JUU YA MLIMA, BASI BILA YA**

فَكَانَ عَٰقِبَتَهُمَآ أَنَّهُمَا فِي ٱلنَّارِ خَٰلِدَيۡنِ فِيهَاۚ وَذَٰلِكَ جَزَٰٓؤُاْ
ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿١٧﴾ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَلۡتَنظُرۡ
نَفۡسٞ مَّا قَدَّمَتۡ لِغَدٖۖ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرُۢ بِمَا تَعۡمَلُونَ
﴿١٨﴾ وَلَا تَكُونُواْ كَٱلَّذِينَ نَسُواْ ٱللَّهَ فَأَنسَىٰهُمۡ أَنفُسَهُمۡۚ أُوْلَٰٓئِكَ
هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ ﴿١٩﴾ لَا يَسۡتَوِيٓ أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِ وَأَصۡحَٰبُ
ٱلۡجَنَّةِۚ أَصۡحَٰبُ ٱلۡجَنَّةِ هُمُ ٱلۡفَآئِزُونَ ﴿٢٠﴾ لَوۡ أَنزَلۡنَا هَٰذَا
ٱلۡقُرۡءَانَ عَلَىٰ جَبَلٖ لَّرَأَيۡتَهُۥ خَٰشِعٗا مُّتَصَدِّعٗا مِّنۡ خَشۡيَةِ
ٱللَّهِۚ وَتِلۡكَ ٱلۡأَمۡثَٰلُ نَضۡرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمۡ يَتَفَكَّرُونَ
﴿٢١﴾ هُوَ ٱللَّهُ ٱلَّذِي لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَۖ عَٰلِمُ ٱلۡغَيۡبِ وَٱلشَّهَٰدَةِۖ
هُوَ ٱلرَّحۡمَٰنُ ٱلرَّحِيمُ ﴿٢٢﴾ هُوَ ٱللَّهُ ٱلَّذِي لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ
ٱلۡمَلِكُ ٱلۡقُدُّوسُ ٱلسَّلَٰمُ ٱلۡمُؤۡمِنُ ٱلۡمُهَيۡمِنُ ٱلۡعَزِيزُ
ٱلۡجَبَّارُ ٱلۡمُتَكَبِّرُۚ سُبۡحَٰنَ ٱللَّهِ عَمَّا يُشۡرِكُونَ
﴿٢٣﴾ هُوَ ٱللَّهُ ٱلۡخَٰلِقُ ٱلۡبَارِئُ ٱلۡمُصَوِّرُۖ لَهُ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰۚ
يُسَبِّحُ لَهُۥ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۖ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ﴿٢٤﴾

ترتيبها ٦٠ — سُورَةُ المُمۡتَحَنَةِ — آياتها ١٣

**SHAKA UNGELIUONA UKINYENYEKEA, UKIPASUKAPASUKA KWA KUMUOGOPA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Qur'ani jinsi ilivyo, utukufu wake, ufasaha wake, kukusanya kwake mawaidha ambayo nyoyo zinalainika kwa mawaidha hayo, imefikia kiwango kwamba lau kama ingeshushwa juu ya mlima katika milima mikubwa, ungeuona mlima huo, pamoja na kuwa kwenye kiwango cha juu cha ugumu na umadhubuti na ukubwa wa umbo, ungeuona ukipasukupasuka kutokana na kumuogopa Allah, kujihadhari na adhabu zake na kuchelea kutotekeleza wajibu wa kuheshimu maneno ya Allah. **NA HIYO MIFANO TUNAWAPIGIA WATU ILI WAFIKIRI** Wafikiri katika yanayowapasa kuyafikiri, ili waonyeke kwa mawaidha, na wakatazike kwa makemeo.

(22) **MWENYE KUJUA YALIYOFICHIKANA NA YANAYO ONEKANA** Yaani: Yeye ni mjuzi wa yalisiyokuwepo kwenye hisia. Ama yaliyo dhahiri, hayo yanaonekana kwa macho.

(23) **YEYE NDIYE MWENYEZI MUNGU AMBAYE HAPANA APASAYE KUABUDIWA ISIPOKUWA YEYE TU** Amerudiarudia kwa ajili ya msisitizo na kuthibitisha. **MFALME, MTAKATIFU** Yaani: Aliyetakasika na kila aibu, Mwenye kutakaswa na kila kasoro. Imesemwa pia kuwa maana yake ni: Ambaye viumbe wamesalimika na kudhulumiwa naye. **MWENYE AMANI** Yaani: Ambaye amewapa waja wake amani ya kusalimika na dhuluma. Pia imesemwa kuwa: Yey ni mwenye kusadikisha Mitume wake kwa kuonyesha miujiza. **MWENYE KUTAWALIA** Yaani: Mwenye kushuhudia waja wake kwa matendo yao, Mwenye kuwachunga. **MWENYE NGUVU** Mshindi asiyeshindwa **JABARI** Ujabari wa Allah ni ukubwa na utukufu wake. Aidha imesemwa kuwa: Jabari ni Yule ambaye mashambulizi yake hayazuiliki. **MWENYE KIBURI** Yaani: Ambaye ametakabari dhidi ya kila kasoro na akatukuka dhidi ya kila lisilofanana na yeye. Kiburi katika sifa za Allah ni sifa nzuri, na katika sifa za viumbe ni sifa mbaya.

(24) **YEYE NDIYE MWENYEZI MUNGU, MUUMBAJI** Yaani: Mwenye kukadiria mambo kwa muktadha wa matakwa yake, na utashi wake. **MTENGENEZAJI** Yaani: Mwanzilishi na mbunifu wa vitu, Mwenye kuviunda. **MTIA SURA** Yaani: Mwenye kuweka sura na kuziunda katika maumbo mbali mbali. **VINAMTAKASA YEYE VILIVYOMO KATIKA MBINGU NA ARDHI** Yaani: Kila kilichomo ndani ya mbingu na ardhi kinazungumzia utukufu wa Allah kwa ulimi wa hali kilivyo au kwa maneno.

## SURATUL-MUMTAH'INAH (60)

*(Imeteremka Madina)*

(1) **ENYI MLIO AMINI, MSIWAFANYE MAADUI WANGU NA MAADUI WENU MARAFIKI.** Aya hii imeshuka kwa Hatib bin Abibalta-a wakati alipowaandikia washirikina wa Kiqureishi barua akiwapa habari ya ujio wa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) kwao, katika vita vya Ukombozi wa Makka, mwaka wa nane wa Hijiria. Aya hii inafundisha kukataza kufanya urafiki wa ndani na makafiri kwa njia yoyote ile. **MNAWAPELEKEA (TAARIFA) KWA SABABU YA MAPENZI** Yaani: Mnwafikishia habari za Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*), kwa sababu ya mapenzi yaliopo baina yenu na wao. **NA ILHALI WAO WAMEKWISHA IKATAA HAKI ILIYO KUJIENI** Yaani: Wamemkufuru Allah, Mtume, Qur-ani na mwongozo wa Mungu. **WANAMFUKUZA MTUME NA NYINYI** Yaani: Wamemfukuza yeye na nyinyi kuondoka Makkah, kwa sababu ya kuikataa kwao haki iliyokujieni. Sasa vipi mnapendana nao? **KWA SABABU MNAMUAMINI MWENYEZI MUNGU MOLA WENU.** Yaani: Wanakufukuzeni kwa sababu ya kumuamini kwenu

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمۡ أَوۡلِيَآءَ تُلۡقُونَ
إِلَيۡهِم بِٱلۡمَوَدَّةِ وَقَدۡ كَفَرُواْ بِمَا جَآءَكُم مِّنَ ٱلۡحَقِّ يُخۡرِجُونَ ٱلرَّسُولَ
وَإِيَّاكُمۡ أَن تُؤۡمِنُواْ بِٱللَّهِ رَبِّكُمۡ إِن كُنتُمۡ خَرَجۡتُمۡ جِهَٰدٗا فِي سَبِيلِي
وَٱبۡتِغَآءَ مَرۡضَاتِيۚ تُسِرُّونَ إِلَيۡهِم بِٱلۡمَوَدَّةِ وَأَنَا۠ أَعۡلَمُ بِمَآ أَخۡفَيۡتُمۡ
وَمَآ أَعۡلَنتُمۡۚ وَمَن يَفۡعَلۡهُ مِنكُمۡ فَقَدۡ ضَلَّ سَوَآءَ ٱلسَّبِيلِ ١ إِن
يَثۡقَفُوكُمۡ يَكُونُواْ لَكُمۡ أَعۡدَآءٗ وَيَبۡسُطُوٓاْ إِلَيۡكُمۡ أَيۡدِيَهُمۡ وَأَلۡسِنَتَهُم
بِٱلسُّوٓءِ وَوَدُّواْ لَوۡ تَكۡفُرُونَ ٢ لَن تَنفَعَكُمۡ أَرۡحَامُكُمۡ وَلَآ أَوۡلَٰدُكُمۡۚ
يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ يَفۡصِلُ بَيۡنَكُمۡۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ بَصِيرٞ ٣ قَدۡ
كَانَتۡ لَكُمۡ أُسۡوَةٌ حَسَنَةٞ فِيٓ إِبۡرَٰهِيمَ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ إِذۡ قَالُواْ لِقَوۡمِهِمۡ
إِنَّا بُرَءَٰٓؤُاْ مِنكُمۡ وَمِمَّا تَعۡبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ كَفَرۡنَا بِكُمۡ وَبَدَا بَيۡنَنَا
وَبَيۡنَكُمُ ٱلۡعَدَٰوَةُ وَٱلۡبَغۡضَآءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤۡمِنُواْ بِٱللَّهِ وَحۡدَهُۥٓ إِلَّا
قَوۡلَ إِبۡرَٰهِيمَ لِأَبِيهِ لَأَسۡتَغۡفِرَنَّ لَكَ وَمَآ أَمۡلِكُ لَكَ مِنَ ٱللَّهِ مِن شَيۡءٖۖ
رَّبَّنَا عَلَيۡكَ تَوَكَّلۡنَا وَإِلَيۡكَ أَنَبۡنَا وَإِلَيۡكَ ٱلۡمَصِيرُ ٤ رَبَّنَا لَا تَجۡعَلۡنَا
فِتۡنَةٗ لِّلَّذِينَ كَفَرُواْ وَٱغۡفِرۡ لَنَا رَبَّنَآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ٥

Allah, au kwa sababu ya kuchukia tu kwamba nyinyi ni waumini. **IKIWA NYINYI MLITOKA KWA AJILI YA JIHADI KATIKA NJIA YANGU NA KUTAFUTA RADHI ZANGU** Yaani: Ikiwa mko hivyo, basi msiwafanye maadui wangu na maadui wenu marafiki wa undani. **MNAWAFIKISHIA TAARIFA ZA SIRI KWA SABABU YA MAPENZI** Yaani: Mnawapa habari za siri kwa sababu ya mapenzi. **NA MIMI NAYAJUA SANA MLIYOYAFICHA NA MLIYOYAFANYA DHAHIRI** Najua, kwa kila mmoja, mliyoyafanya; ya kuwapelekea habari. **NA YEYOTE MWENYE KUFANYA HAYO KATIKA NYINYI, BASI AMEIPOTEA NJIA YA SAWA.** Ameikosa njia ya haki na ya usawa, na ameipotea njia iliyokusudiwa.

2 **WAKIKUWEZENI WANAKUWA MAADUI ZENU** Kwa hakika, wao wakikutana nanyi na kukushtukizeni watakudhihirishieni uadui uliomo nyoyoni mwao. **NA WANAKUKUNJULIENI MIKONO YAO NA NDIMI ZAO KWA UOVU** Yaani: Wanakunyosheeni mikono yao kwa kukupigeni na mfano wake, na kukufungulieni midomo yao kwa matusi na mfano wake. **NA WANGEPENDA MUWE MAKAFIRI** Wametamani kuritadi kwenu na kurejea kwenu kwenye ukafiri.

3 **HAWATAKUFAENI JAMAA ZENU, WALA WATOTO WENU** Watoto wenu na ndugu zenu hawatakunufaisheni Siku ya Kiama hata mpendane na makafiri kwa ajili yao, kama ilivyotokea kutoka kisa cha Haatib. Bali ambacho kitakunufaisheni ni yale aliyokuamrisheni Allah ya kuwafanya makafiri maadui, kupigana nao Jihadi na kuacha kupendana nao. **SIKU YA KIYAMA (MWENYEZI MUNGU) ATAPAMBANUA BAINA YENU** Watu waliomtii atawaingiza peponi, na watu waliomuasi atawaingiza motoni.

4 **KWA YAKINI KABISA, NYINYI MNAO MFANO MZURI** Yaani: Mfano maridhawa wa kuiga. **KWA IBRAHIM NA WALE WALIOKUWA PAMOJA NAYE** Anasema: Hivi humuigi Ibrahimu ewe Haatib, na hivyo, ukajitenga na watu wako kama Ibrahimu alivyojitenga na baba yake na watu wake? **WALIPOWAAMBIA WATU WAO KUWA: "HAKIKA, SISI TUMEJITENGA NANYI"** Yaani: Tumejitenga nanyi, kwa hiyo, sisi sio katika nyinyi na nyie sio katika sisi, kwa sababu ya kumkufuru kwenu Allah. **"NA (TUMEJITENGA NA) VILE MNAVYOVIABUDU BADALA YA MWENYEZI MUNGU"**. Navyo ni masanamu. **"TUMEKUKATAENI"** Yaani: Tumeikataa dini yenu au vitendo vyenu. **"HAKIKA, UMEKWISHA DHIHIRI UADUI NA CHUKI BAINA YETU NA NYINYI MILELE"**. Yaani: Huu ndio msimamo wetu kwenu madamu mko kwenye ukafiri wenu. **"MPAKA MTAKAPO MUAMINI MWENYEZI MUNGU PEKE YAKE"** Na mkaacha shirki mliyo nayo. Mtakapofanya hivyo, uadui utabadilika na kuwa urafiki, na chuki itabadilika na kuwa upendo. **ISIPOKUWA KAULI YA IBRAHIMU YA KUMWAMBIA BABA YAKE KWAMBA: "KWA YAKINI KABISA, NITAKUOMBEA MSAMAHA"** Yaani: Mnao mfano mzuri wa kuiga katika maneno yote ya Ibrahimu, isipokuwa tu ile kauli yake ya kumwambia baba yake. Kwa hiyo, msimuige mkawaombea msamaha washirikina, kwa sababu hiyo ilikuwa ni ahadi aliyomuahidi. *"Lakini ilipo mbainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye"*. Sura Attauba (9), aya 117. **"NA SIMILIKI CHOCHOTE KWA AJILI YAKO MBELE YA MWENYEZI MUNGU"** Yaani: Siwezi kukukinga chochote na adhabu ya Allah.

5 **EWE MOLA WETU, USITUFANYE MTIHANI KWA WALIO KUFURU.** Mujahid amesema kuwa maana ni kwamba: *"Usituadhibu kwa mikono yao, wala kwa adhabu yoyote toka kwako, wasije wakasema: Lau hawa wangekuwa katika haki, yasingewakuta haya"*.

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِيهِمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ
وَمَن يَتَوَلَّ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٦﴾ ۞ عَسَى اللَّهُ أَن يَجْعَلَ
بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ الَّذِينَ عَادَيْتُم مِّنْهُم مَّوَدَّةً ۚ وَاللَّهُ قَدِيرٌ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ
﴿٧﴾ لَّا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم
مِّن دِيَارِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ
﴿٨﴾ إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُم
مِّن دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَن تَوَلَّوْهُمْ ۚ وَمَن يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَٰئِكَ
هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٩﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا جَاءَكُمُ الْمُؤْمِنَاتُ
مُهَاجِرَاتٍ فَامْتَحِنُوهُنَّ ۖ اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِهِنَّ ۖ فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ
فَلَا تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى الْكُفَّارِ ۖ لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ ۖ وَآتُوهُم
مَّا أَنفَقُوا ۚ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ أَن تَنكِحُوهُنَّ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۚ
وَلَا تُمْسِكُوا بِعِصَمِ الْكَوَافِرِ وَاسْأَلُوا مَا أَنفَقْتُمْ وَلْيَسْأَلُوا مَا أَنفَقُوا ۚ
ذَٰلِكُمْ حُكْمُ اللَّهِ ۖ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ ۚ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾ وَإِن فَاتَكُمْ
شَيْءٌ مِّنْ أَزْوَاجِكُمْ إِلَى الْكُفَّارِ فَعَاقَبْتُمْ فَآتُوا الَّذِينَ ذَهَبَتْ
أَزْوَاجُهُم مِّثْلَ مَا أَنفَقُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي أَنتُم بِهِ مُؤْمِنُونَ ﴿١١﴾

(6) **KWA YAKINI KABISA, UMEPATIKANA MFANO MZURI KWENU KATIKA (MSIMAMO) WAO.** Yaani: Mmepata mfano mzuri wa kuiga Ibrahimu na wale waliokuwa pamoja naye. **KWA ANAYEMTARAJI MWENYEZI MUNGU NA SIKU YA MWISHO.** Yaani: Mfano huu mzuri wa kuiga unapatikana kwa yule anaye tamani kupata kheri kutoka kwa Allah duniani na Akhera. **NA MWENYE KUGEUKA** Anayepinga hayo **BASI HAKIKA, MWNYEZI MUNGU NI MWENYE KUJITOSHA TU.** Hawategemei viumbe wake. **MSIFIWA** Na wapenzi wake.

(7) **HUENDA MWENYEZI MUNGU AKATIA MAPENZI BAINA YENU NA BAINA YA WALE AMBAO MIONGONI MWAO MMEFANYIANA NAO UADUI** Baina yenu na baina ya Washirikina wa Makkah. Hilo linawezekana kwa wao kusilimu na wakawa katika watu wa dini yenu. Na kweli, walisilimu watu miongoni mwao baada ya Makka kukuombolewa, na Uislamu wao ulikuwa mzuri. Ulipatikana upendo baina yao na baina ya wale waliowatangulia katika Uislamu. Walipigana Jihadi, na wakafanya matendo yaliyo waweka karibu na Allah. Mtume(*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) alimuoa Ummuhabiba mtoto wa Abisufiani, na kupendana kwa Mtume na Abisufiani hakukupatikana isipokuwa tu baada ya kusilimu kwake siku ya ukombozi (wa makka), na Abusufiani kuacha kumfanyia uadui Mtume wa Mwenyezi Mungu (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*). Imenukuliwa kwa Abuhuraira akiesema kuwa: *"Aliyepigana mwanzo na watu walioritadi juu ya kusimamisha dini ya Allah ni Abusufiani bin Harb, na kwa ajili yake ilishuka aya hii: Huenda Mwenyezi Mungu akatia mapenzi baina yenu na baina ya wale ambao miongoni mwao mmefanyiana nao uadui".* **NA MWENYEZI MUNGU NI MUWEZA** Mwenye uwezo wa kiwango cha juu, Mwenye kuweza kubadilisha nyoyo za wapinzani ili awaingize katika msamaha wake na rehema zake.

(8) **MWENYEZI MUNGU HAKUKATAZENI KUHUSU WALE AMBAO HAWAKUKUPIGENI VITA KWA SABABU YA DINI, WALA HAWAKUKUFUKUZENI KATIKA MIJI YENU** Yaani: Hakukatazeni kwa hawa **KUWAFANYIA WEMA** Kuwafanyia yale ambayo ni ya wema, kama kuunga udugu, kumsaidia jirani na kukirimu wageni. **NA KUWAFANYIA UADILIFU**. Fanyeni uadilifu baina yenu na baina yao kwa kuwatekelezea haki zao, kama kuwatimizia ahadi, kurejesha amana na kulipa thamani ya vitu mnavyonunua kwao, ikiwa kamili bila ya kupungua. **HAKIKA, MWENYEZI MUNGU ANAWAPENDA WAFANYAO UADILIFU** Maana ni kwamba: Allah hakatazi kuwatendea wema watu wa ahadi ikiwa ni pamoja na makafiri ambao wameingia mikataba na Waislamu ya kuacha vita na kuacha kuwasaidia makafiri dhidi yao. Pia hakatazi kuamiliana nao (kuwa na mahusiano nao) kwa uadilifu.

(9) **HAKIKA, HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA MWENYEZI MUNGU ANAKUKATAZENI KUFANYA URAFIKI (NA KUSAIDIANA) NA WALE WALIO KUPIGENI VITA KWA SABABU YA DINI, NA WAKAKUFUKUZENI KATIKA MIJI YENU.** Hao ni vigogo wa Kikuraishi na mfano wao, miongoni mwa wale wenye kuwapiga vita Waislamu. **NA WAKASAIDIA KATIKA KUFUKUZWA KWENU** Yaani: Wakawasaidia wale wanaokupigeni vita na na wanao kufukuzeni, nao ni watu wa Makkah walio baki na wenye kuwaunga mkono katika mikataba yao. **NA WANAO WAFANYA HAO MARAFIKI, BASI HAO NDIO MADHAALIMU.** Kwa kuwa wao wamewapenda watu wanaostahiki kufanyiwa uadui, kwa sababu ya kuwa kwao adui wa Allah, Mtume wake na kitabu chake.

(10) **ENYI MLIO AMINI, WAKIKUJIENI**

**WANAWAKE WAUMINI WAKIWA WAHAMIAJI** Wakiwa wameondoka kwa makafiri. Suala hilo ni kwamba, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alitiliana saini mkataba wa maridhiano na Makuraishi Siku ya Hudaibiya kwa kukubaliana kumrudisha kwa makafiri mtu ambaye amekwenda kwa Waislamu akiwa amesilimu. Basi wanawake walipohama kwenda kwa Mtume, Allah alikataa kuwarudisha kwa makafiri. Aliamrisha wahojiwe. **BASI WAFANYIENI MTIHANI** Yaani: Wahojini ili mjue kiwango cha utashi wao wa kutaka kuingia katika Uislamu. Walikuwa wakiapishwa kwa jina la Allah kuwa: Hawakuondoka kwa sababu ya kuchukizwa na waume (zeo), wala kupenda kuhama kutoka mji kwenda mji mwingine, wala kutafuta (maslahi ya) dunia; bali ni kwa ajili ya kumpenda Allah na Mtume wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). Basi mwanamke alipokubali kuyachukulia kiapo mambo hayo, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alimrudishia mumewe mahari yake na gharama alizomgharamia, na hakumrejesha kwake. **MWENYEZI MUNGU NDIYE MWENYE KUJUA ZAIDI IMANI YAO.** Kwa kubainisha kuwa hakuna ajuae uhakika wa hali yao isipokuwa Allah (Subhaanahu wa Taala) tu. Mwenyezi hakukukalifisheni hilo, bali amekukalifisheni kuwahoji mpaka yakubainikieni yale yanao onesha ukweli wa madai yao katika kuupenda Uislamu**.** **MKIWAJUA KUWA NI WAUMINI** Kwa dhahiri yake, baada ya mahojiano ambayo mmeamriwa **BASI MSIWARUDISHE KWA MAKAFIRI** Msiwarudishe kwa waume zao makafiri. **WANAWAKE HAO SIO HALALI KWAO, NA WAO SIO HAWAWI HALALI KWA WANAWAKE HAO.** Kwa hiyo, mwanamke Muislamu si halali kwa kafiri. Na kusilimu kwa mwanamke kunawajibisha kumtenganisha na mumewe, sio kule kuhama kwake tu. **NA WAPENI HAO (WANAUME) KILE WALICHO TOA.** Wapeni waume wa hawa wanawake ambao wamehama na kuingia katika Uislamu mfano wa mahari walizotoa. Shaafii amesema kuwa: *"Na atakapomtaka asiyekuwa mumewe, miongoni mwa jamaa za mumewe atazuiwa bila ya mbadala wowote".* **WALA HAPANA MAKOSA KWENU KUWAOA** Yaani: Baada ya eda, kwa kuwa wao wamekwisha kuwa watu wa dini yenu. **ENDAPO MTAWAPA MALIPO YAO** Yaani: Mahari zao. Na hilo ni baada ya eda zao kwisha. **NA MSIWAWEKE WANAWAKE MAKAFIRI KATIKA HIFADHI YA NDOA ZENU.** Maana ni kwamba: Ambaye ana mke kafiri, huyo sio mkewe, kwa sababu ya kukatika kwa hifadhi yake ya ndoa kwa kutofautiana dini. Makafiri walikuwa wanawaozesha Waislamu, na Waislamu wanaoa wanawake makafiri. Kisha hilo likafutwa kwa aya hii. Hukumu hii inawahusu wanawake makafiri washirikina wasiokuwa Ahlulkitab (Wayahidi na Wakristo). **NA TAKENI MLICHO KITOA** Yaani: Daini mahari za wake zenu watakaporitadi**.** **NA WAO WATAKE WALICHO KITOA.** Wafasiri wamesema kuwa: *"Ilikuwa mwanamke wa Kiislamu akiritadi na kwenda kwa makafiri walio na mikataba ya amani na Waislamu, makafiri walikuwa wanaambiwa: Leteni mahari yake. Na mwanamke kutoka kwa makafiri akija kwa Waislamu na kusilimu, Waislamu huambiwa: Rejesheni mahari yake kwa mumewe kafiri".* **HAYO KWENU** Yaani: Kurudisha kwa mahari kwa pande zote mbili **NDIO HUKUMU YA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Ndio hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa makafiri baada ya mkataba wa maridhiano wa Hudaibiya, tofauti makafiri ambao hawana mkataba. Hukumu hii pia imefutwa. Kurtubi amesema kuwa: *"Jmabo hili lilikuwa linahusu zama hizo katika tukio hilo tu, yaani: suala linalo husiana na kurudisha mahari, sio kutenganisha baina ya wanandoa wawili anaposilimu mmoja wao".*

(11) **NA AKIKUTOROKENI YEYOTE KATIKA WAKE ZENU KWENDA KWA MAKAFIRI** Mwanamke wa Kiislamu atakaporitaji na kurudi kwenye nyumba ya ukafiri hata kama makafiri hao ni Ahlulkitab **NA MKATESA (MKASHINDA)** Yaani: Mkashinda ngawira na zikawa zenu **BASI WAPENI WALIO KIMBIWA NA WAKE ZAO MFANO WA KILE WALICHO TOA.** Wameamriwa kuwapa kutoka kwenye ngawira wale ambao wake zao wameondoka mfano wa mahari zao, kama makafiri hawakurudisha mahari zao. **NA MCHENI MWENYEZI MUNGU AMBAYE NYINYI MNAMUAMINI** Yaani: Jihadharini msije mkajiingiza katika jambo miongoni mwa mambo yenye kuwajibisha adhabu juu yenu.

(12) **EWE MTUME, WATAKAPO KUJIA WANAWAKE WAUMINI WAKILA KIAPO CHA UTII** Yaani: Wakikukusudia kula kiapo cha utii kwako juu ya Uislamu **KWAMBA HAWATAKISHIRIKISHA NA MWENYEZI MUNGU KITU CHOCHOTE** Vyoyote kiwavyo. Hii ilikuwa siku ya ukombozi wa Makkah. Wanawake wa watu wa Makkah walikwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wakitaka kula kiapo cha kumkubali na kumtii. Allah akamuamuru achukue ahadi yao kuwa hawatamfanyia Shirki Allah. **NA HAWATAWAUA WATOTO WAO** Tendo hilo la kuua watoto kwa kuwafukia wakiwa hai ni jambo walilokuwa wakilifanya

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ إِذَا جَآءَكَ ٱلۡمُؤۡمِنَٰتُ يُبَايِعۡنَكَ عَلَىٰٓ أَن لَّا يُشۡرِكۡنَ
بِٱللَّهِ شَيۡـٔٗا وَلَا يَسۡرِقۡنَ وَلَا يَزۡنِينَ وَلَا يَقۡتُلۡنَ أَوۡلَٰدَهُنَّ وَلَا يَأۡتِينَ
بِبُهۡتَٰنٖ يَفۡتَرِينَهُۥ بَيۡنَ أَيۡدِيهِنَّ وَأَرۡجُلِهِنَّ وَلَا يَعۡصِينَكَ
فِي مَعۡرُوفٖ فَبَايِعۡهُنَّ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لَهُنَّ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ
﴿١٢﴾ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَوَلَّوۡاْ قَوۡمًا غَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِمۡ
قَدۡ يَئِسُواْ مِنَ ٱلۡأٓخِرَةِ كَمَا يَئِسَ ٱلۡكُفَّارُ مِنۡ أَصۡحَٰبِ ٱلۡقُبُورِ ﴿١٣﴾

ترتيبها ٦١ — سُورَةُ الصَّفِّ — آياتها ١٤

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلۡأَرۡضِۖ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ
﴿١﴾ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفۡعَلُونَ ﴿٢﴾
كَبُرَ مَقۡتًا عِندَ ٱللَّهِ أَن تَقُولُواْ مَا لَا تَفۡعَلُونَ ﴿٣﴾ إِنَّ
ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلَّذِينَ يُقَٰتِلُونَ فِي سَبِيلِهِۦ صَفّٗا كَأَنَّهُم
بُنۡيَٰنٞ مَّرۡصُوصٞ ﴿٤﴾ وَإِذۡ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوۡمِهِۦ يَٰقَوۡمِ لِمَ
تُؤۡذُونَنِي وَقَد تَّعۡلَمُونَ أَنِّي رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيۡكُمۡۖ فَلَمَّا
زَاغُوٓاْ أَزَاغَ ٱللَّهُ قُلُوبَهُمۡۚ وَٱللَّهُ لَا يَهۡدِي ٱلۡقَوۡمَ ٱلۡفَٰسِقِينَ ﴿٥﴾

makafiri wa wakati wa ujinga. **NA HAWATALETA UZUSHI WANAO UZUA BAINA YA MIKONO YAO NA MIGUU YAO** Yaani: Hawatawaunganisha na waume zao watoto wasiokuwa wao. Alfarraa amesema kuwa: *"Mwanamke alikuwa anaokota mtoto na kumwambia mumewe: Huyu ni mtoto wangu niliyezaa nawe".* Ibniabbaas amesema kuwa: *"Ilikuwa mwanamke anazaa mtoto wa kike na anabadilisha mahali pake kwa mtoto wa kiume".* **NA HAWATAKUASI KATIKA JAMBO JEMA.** Yaani: Hawatafanya uasi wa kila jambo ambalo ni utii kwa Allah, kama kukataza kuomboleza kwa kupiga kelele, kuchanachana nguo (kwa ajili ya msiba), kunyonyoa nywele, kurarua nyuso na kuomba balaa. **BASI KUBALIANA NAO KATIKA KIAPO HICHO CHA UTII, NA WAOMBEE MSAMAHA KWA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Muombe Mwenyezi Mungu awasamehe baada ya wao kula kiapo chao cha kukutii wewe.

(13) **ENYI MLIO AMINI, MSIWAFANYE MARAFIKI WATU AMBAO MWENYEZI MUNGU AMEWAKASIRIKIA.** Hao ni makundi yote ya makafiri. Pia imesemwa kuwa hao: Ni Wayahudi tu. **WAMEKWISHA KATA TAMAA YA AKHERA**. Yaani: Wao hawaiamini kabisa Akhera, kwa sababu ya ukafiri wao. **KAMA MAKAFIRI WALIVYO WAKATIA TAMAA WATU WA MAKABURINI.** Kama wanavyo kata tamaa ya kufufuliwa kwa maiti wao, kwa sababu ya itikadi yao kwamba hakuna kufufuliwa.

# SURAT ASS'AF (61)

*(Imeteremka Madina)*

(2) **ENYI MLIO AMINI, KWA NINI MNASEMA MSIYO YATENDA?** Imenukuliwa kwa Ibniabbas akisema kuwa: *"Kulikuwa na watu katika Waislamu kabla ya kufaradhishwa kwa Jihadi wakisema kwamba: Tulitamani lau Allah angetufahamisha amali (ibada) anayoipenda zaidi ili tuifanye. Basi alipowambia kuwa amali anayoipenda zaidi ni Jihadi, baadhi ya watu katika Waumini walilichukia jambo hilo. Kwa sababu hiyo, ilishuka aya hii"*.

(3) **IMECHUKIZA VIKUBWA MNO KWA MWENYEZI MUNGU KUWA MNASEMA MSIYO YATENDA.** Yaani: Mwenyezi Mungu Mtukufu anachukia hayo kuchukia kukubwa. Pia imesemwa kuwa aya hii imeshuka kuwazungumzia watu waliokuwa wakija kwa Mtume na mmoja wao akawa anasema kwamba: *"Nimepigana kwa upanga wangu, na nimepiga hivi na vile"*, na ilhali kwa hakika hawakufanya hayo.

(4) wenyezi Mungu anawabainishia Waumini kuwa, kupigana katika njia ya Allah ni jambo la juu zaidi katika mambo anayoyapenda Allah kwa waja wake. Imekuja katika Hadithi kwamba: *"Kichwa cha jambo ni Uislamu na nguzo yake ni swala na kilele chake ni kupigana Jihadi kwa ajili ya Allah"*. **WAKIWA SAFU MOJA.** Yaani: Wenyewe wakiwa wamejipanga safu. **KAMA KWAMBA WAO NI JENGO LILIO KAMATANA.** Lililoshikamana kwa pamoja mpaka likawa kama kitu kimoja. Na hili linatokana na ukakamavu wao na nguvu zao kwa ajili ya amri za Allah; hawana kusuasua katika hilo, wala adui hawezi kupenya kwao.

(5) **NA (KUMBUKA) WAKATI MUSA ALIPOWAAMBIA WATU WAKE.** Mwenyezi Mungu Mtukufu alipotaja kuwa anawapenda wale wanaopigana kwa ajili yake, amebainisha kuwa Mussa na Issa waliamrisha Tawhidi, walipigana kwa ajili yake na adhabu ikawa halali kuwashukia waliowapinga. Yote haya yametajwa ili kuitahadharisha kaumu ya Muhammad wasije wakamfanyia Mtume wao kama kaumu ya Musa na Isa walivyowafanyia Mitume yao. **ENYI WATU WANGU, KWA NINI MNANIUDHI?** Kwa kuzipinga zile sheria ninazo kuamrisheni na

وَإِذۡ قَالَ عِيسَى ٱبۡنُ مَرۡيَمَ يَٰبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ إِنِّي رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيۡكُم مُّصَدِّقٗا
لِّمَا بَيۡنَ يَدَيَّ مِنَ ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَمُبَشِّرَۢا بِرَسُولٖ يَأۡتِي مِنۢ بَعۡدِي ٱسۡمُهُۥٓ أَحۡمَدُۖ فَلَمَّا
جَآءَهُم بِٱلۡبَيِّنَٰتِ قَالُواْ هَٰذَا سِحۡرٞ مُّبِينٞ ٦ وَمَنۡ أَظۡلَمُ مِمَّنِ ٱفۡتَرَىٰ
عَلَى ٱللَّهِ ٱلۡكَذِبَ وَهُوَ يُدۡعَىٰٓ إِلَى ٱلۡإِسۡلَٰمِۚ وَٱللَّهُ لَا يَهۡدِي ٱلۡقَوۡمَ ٱلظَّٰلِمِينَ
٧ يُرِيدُونَ لِيُطۡفِـُٔواْ نُورَ ٱللَّهِ بِأَفۡوَٰهِهِمۡ وَٱللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِۦ وَلَوۡ كَرِهَ
ٱلۡكَٰفِرُونَ ٨ هُوَ ٱلَّذِيٓ أَرۡسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلۡهُدَىٰ وَدِينِ ٱلۡحَقِّ لِيُظۡهِرَهُۥ
عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِۦ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡمُشۡرِكُونَ ٩ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ هَلۡ أَدُلُّكُمۡ
عَلَىٰ تِجَٰرَةٖ تُنجِيكُم مِّنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ ١٠ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَتُجَٰهِدُونَ
فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ بِأَمۡوَٰلِكُمۡ وَأَنفُسِكُمۡۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ١١
يَغۡفِرۡ لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡ وَيُدۡخِلۡكُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ وَمَسَٰكِنَ
طَيِّبَةٗ فِي جَنَّٰتِ عَدۡنٖۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ ١٢ وَأُخۡرَىٰ تُحِبُّونَهَاۖ نَصۡرٞ
مِّنَ ٱللَّهِ وَفَتۡحٞ قَرِيبٞۗ وَبَشِّرِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ١٣ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُونُوٓاْ
أَنصَارَ ٱللَّهِ كَمَا قَالَ عِيسَى ٱبۡنُ مَرۡيَمَ لِلۡحَوَارِيِّـۧنَ مَنۡ أَنصَارِيٓ إِلَى ٱللَّهِۖ
قَالَ ٱلۡحَوَارِيُّونَ نَحۡنُ أَنصَارُ ٱللَّهِۖ فَـَٔامَنَت طَّآئِفَةٞ مِّنۢ بَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ
وَكَفَرَت طَّآئِفَةٞۖ فَأَيَّدۡنَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ عَلَىٰ عَدُوِّهِمۡ فَأَصۡبَحُواْ ظَٰهِرِينَ ١٤

ambazo Mwenyezi Mungu amezifaradhisha kwenu? Au maana ni kwamba: Kwa nini mnaniudhi kwa kunitukana na kunivunjia heshima? **NA ILHALI MNAJUA KWA YAKINI KUWA MIMI NI MTUME WA MWENYEZI MUNGU NILIYE TUMWA KWENU?** Maana yake ni kwamba: Ni vipi mnaniudhi, pamoja na kujua kwenu kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na ilhali Mtume huwa anaheshimiwa? Hakuna shaka yoyote iliyobaki kwenu katika ujumbe niliotumwa, kwa sababu ya miujiza mliyoiona na inayolazimisha kwenu kuukubali utume wangu, na kukuelimisheni kuujua kwa yakini. **WALIPO POTOKA, MWENYEZI MUNGU ALIZIACHA NYOYO ZAO ZIPOTOKE** Yaani: Walipoacha kufuata haki kwa kumuudhi Nabii wao, Mwenyezi Mungu alizipindisha nyoyo zao zikaacha kufuata haki, ikiwa ni malipo kwa yale waliyoyafanya.

(6) **NA (KUMBUKA) WAKATI ISSA BIN MARIAMU ALIPOSEMA: ENYI WANA WA ISRAILI, HAKIKA MIMI NI MTUME WA MWENYEZI MUNGU KWENU, NIKIWA MTHIBITISHAJI WA TORATI ILIYOKUWA KABLA YANGU.** Yaani: Mimi ni Mtume niliyetumwa kwenu kuleta Injili. Sikukuleteeni kitu kinachopingana na Torati, bali Torati imekusanya ubashiri kwangu. Sasa vipi mnanikimbia na kunipinga? **NA NIKIWA MBASHIRI WA KUJA KWA MTUME ATAKAYE KUJA BAADA YANGU, JINA LAKE NI AHMAD.** Na kama niko hivyo, hakuna sababu ya kunipinga. Ahmad ni jina la Mtume wetu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), na tafsiri yake kimsingi ni: Mtu ambaye anasifiwa sana kwa sababu ya mambo ya kheri aliyonayo kuliko asifiwavyo mwengine yeyote. **ALIPOWALETEA HOJA ZILIZO WAZI, WALISEMA: HUU NI UCHAWI ULIO DHAHIRI.** Yaani: Issa alipowaletea miujiza walisema: Haya alioyotuletea ni uchawi ulio dhahiri. Na imesemwa kuwa kilichokusudiwa ni Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). Yaani: Pindi alipowaletea hayo, walisema kuwa: Huyu ni mchawi.

(7) **NA NI NANI DHALIMU ZAIDI KULIKO YULE ALIYE MZUSHIA MWENYEZI MUNGU UONGO, NA ILHALI YEYE ANAITWA KWENYE UISLAMU?** Uislamu ambao ndio dini iliyo bora na tukufu zaidi. Hii ni kwa sababu, ambaye yuko hivyo ni haki yake kutomzushia mwengine uongo, sasa iweje auzushe uongo huo kwa Mola wake? **NA MWENYEZI MUNGU HAWAONGOZI WATU DHALIMU.** Ni wale waliotajwa ni miongoni mwa jumla yao.

(8) **WANATAKA KUIZIMA NURU YA MWENYEZI MUNGU KWA VINYWA VYAO.** Yaani: Hali yao katika kujaribu kwao kuubana Uislamu na kuzuia mwongozo wake kwa maneno yao ya uongo, ni kama hali ya mtu anayetaka kuzima mwangaza mkubwa kwa mpulizo wa mdomo wake. **NA MWENYEZI MUNGU ATAKAMILISHA NURU YAKE** Kwa kudhihirisha dini ya Uislamu sehemu zote na kuinyanyua iwe juu ya dini nyingine.

(9) **YEYE NDIYE ALIYEMTUMA MTUME WAKE KWA MWONGOZO NA DINI YA HAKI, ILI AIFANYE IWE JUU YA DINI ZOTE** Ili aifanye iwe juu, yenye kuzishindi dini zote, ikizikalia juu na kuzishinda. **NA JAPOKUWA WASHIRIKINA WATACHUKIA.** Bila shaka hilo litakuwa bila pingamizi lolote lile.

(10) **ENYI MLIO AMINI, HIVI NIKUONESHENI BIASHARA ITAKAYO KUOKOENI NA ADHABU ILIYO CHUNGU?** Ameiweka amali katika daraja ya biashara, kwa kuwa wao watapata faida katika amali, kama wanavyopata faida katika biashara. Na hilo litapatikana kwa kuingia kwao peponi, na kuokoka kwao na moto. Biashara hii ndio aliyoibainisha katika aya mbili zifuatazo, kwa kuwa maana yake ni kwamba, Jihadi na imani

thamani yake kwa Allah ni pepo. Na hiyo ni biashara yenye faida.

12 allah **ATAKUSAMEHENI DHAMBI ZENU.** Kwanza ametaja bidhaa ambayo wataifanyia biashara, na hapa anataja thamani ambayo amewaahidi. Yaani: Mkiamini, mtasamehewa. **NA (ATAKUWEKENI KATIKA) MAKAZI MAZURI KATIKA BUSTANI ZA MILELE.** Yaani: Mtakaa katika ukaazi wa kudumu, usiokatika kwa mauti wala kwa kutoka humo. **HUKO NDIKO KUFUZU KUKUBWA.** Yaani: Hayo yaliyotajwa; ya kupata msamaha na kuingizwa peponi ni kufuzu ambako hakuna kufuzu kwingine baada yake, na ni mafanikio ambayo hakuna mafanikio yanayo fanana nayo.

13 **MKIPENDACHO.** Yaani: Na mtapata jambo jingine litakalokufurahisheni. **NI NUSURA ITOKAYO KWA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Hicho mkipendacho ni nusura kutoka kwa Allah ya kukunusurini nyinyi. **NA UKOMBOZI ULIO KARIBU.** Atakaouleta kwenu. Yaani: Nusura ya kuwashinda Wakuraishi na ukombozi wa mji wa Makkah. Ataa amesema kuwa: *" (Allah) Anakusudia ukombozi wa Fursi (Persia) na Roma".* **NA WAPE HABARI NJEMA WAUMINI.** Maana ni kwamba: Ewe Muhammad, wape Waislamu habari njema ya kupata ushindi na ukombozi duniani, na kupata pepo Akhera.

14 **ENYI MLIO AMINI, KUWENI WASAIDIZI WA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Dumuni juu ya zile harakati mlizonazo za kuinusuru dini. **KAMA ALIVYO SEMA ISSA MWANA WA MARIAMU KUWAAMBIA HAWARIYINA: NI NANI WASAIDIZI WANGU KWA MWENYEZI MUNGU?** Inusuruni dini ya Allah kama nusura ya Hawariyina wakati Issa alipowaambia ***Ni nani wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu?*** wao wakasema: **SISI NI WASAIDIZI WA MWENYEZI MUNGU.** Na maana ni kwamba: Ni nani miongoni mwenu atakaye beba jukumu la kuninusuru na kunisaidia katika mambo yanayokurubisha kwa Allah? Hawariyina ni wafuasi wa Masia, wafuasi wake waaminifu na watu wa mwanzo kabisa waliomuamini, na walikuwa watu kumi na mbili. **BASI KUNDI KATIKA WANA WA ISRAILI LILIAMINI** Lilimuamini Issa. **NA LIKAKUFURU** (kumkufuru Issa) **KUNDI JINGINE. HIVYO, TUKAWAPA NGUVU WALE WALIOAMINI YA KUWASHINDA ADUI WAO.** Yaani: Tukawapa nguvu wale walio katika haki miongoni mwao dhidi ya wale walioko katika batili. **WAKAWA WENYE KUSHINDA.** Wako juu, washindi. Imenukuliwa kwa Katada katika kuielezea kauli ya allah *"Enyi mlio amini, kuweni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu"* akisema kuwa: *"Hilo lilipatikana kwa shukurani za Allah. Walimwendea Mtume watu sabini, na kula kiapo cha kumtii pale Aqaba, na walimhami Mtume na kumsaidia mpaka Mwenyezi Mungu akaipa ushindi dini yake".* Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwamba: *Niteulieni watu kumi na wawili miongoni mwenu wawe wawakilishi wa watu wao, kama Hawariyina walivyomhami Issa mwana wa Mariamu. Kisha aliwaambia wale wateuliwa kuwa: Nyie ni wawakilishi wa watu wenu kama usaidizi wa Hawariyina kwa Issa mwana wa Mariamu, na mimi ni mwakilishi wa watu wangu. Wakasema: Ndio".*

# SURATUL-JUMUA' (62)

***(Imeteremka Madina)***

1 **MFALME, MTAKATIFU.** Mtakatifu ni yule aliyetakasika na kila kasoro.

2 **YEYE NDIYE ALIYEMPELEKA MTUME MIONGONI MWAO KWA WATU WASIOJUA KUSOMA.** Makusudio ya wasiojua kusoma ni Waarabu; wanaojua kuandika na wale wasiojua kuandika miongoni mwao, kwa sababu wao hawakuwa watu wa kitabu. Asiyejua kusoma ni mtu ambaye hajui kuandika wala kusoma kilichoandikwa. Waarabu wengi walikuwa hivyo. **AWASOMEE AYA ZAKE** Yaani: Awasomee Qur-ani, pamoja na kuwa yeye ni ngumbaru; hajui kusoma wala kuandika, na hakujifunza kwa yeyote. **NA AWATAKASHE** Yaani: Awatakashe kutokana na uchafu wa ukafiri, madhambi na tabia mbaya. Na imesemwa pia kuwa: Awafanye wawe na nyoyo safi kwa Imani. **NA AWAFUNDISHE KITABU NA HEKIMA** Kitabu ni Qur-ani, na Hekima ni Sunna. Na imesemwa pia kuwa, Kitabu ni kuandika kwa kalamu, na Hekima ni Elimu ya kuijua dini. Amesema haya Malik bin Anas. **NA JAPOKUWA KABLA YA HAYA WALIKUWA KATIKA UPOTOFU ULIO DHAHIRI** Yaani: Japo walikuwa katika shirki na kuiacha haki.

3 **NA WENGINE MIONGONI MWAO BADO HAWAJAUNGANA NAO** Yaani: Hawajakutana nao katika wakati huo, na watakutana nao baadae. Yaani: (Mjumbe ametumwa ili) Awatakashe (wao) na awatakashe wengine miongoni mwao, nao ni wale Waislamu Waarabu na wasiokuwa Waarabu waliokuja baada ya Swahaba hadi siku ya Kiama. Bukhari akinukuu kutoka kwa Abuhuraira amesema kuwa: *"Tulikuwa tumekaa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wakati iliposhuka sura Al-Jumuah. Akaisoma, na alipofika: Na wengine miongoni mwao bado hawajaungana nao, mtu mmoja alimuuliza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kuwa: Ni kina nani hawa ambao hawajakutana na sisi? Mtume aliweka mkono wake kwa Salman Farsiy*

*na kusema: Nina apa kwa (Mwenyezi Mungu) Ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba, lau kama imani ingekuwa kwenye (nyota ya) Thureya, wangeipata watu miongoni mwa hawa"*. **NA YEYE NDIYE MWENYE NGUVU, MWENYE HEKIMA**. Yaani: Mwingi wa nguvu na hekima.

(5) **MFANO WA WALE WALIOBEBESHWA TORATI.** Mfano huu Mwenyezi Mungu Mtukufu ameupigia Wayahudi ambao wameacha kuitekeleza Torati. Yaani: Waliamrishwa kuisimamia na kuyafanyia kazi yaliyomo **KISHA WASIIBEBE.** Yaani: Hawakutekeleza kwa mujibu wake, wala hawakuyatii yale waliyoamriwa humo. **NI MFANO WA PUNDA ANAYEBEBA VITABU VIKUBWA.** Punda hajui kama: Ni kitabu kilichopo mgongoni mwake au ni uchafu? **NI MFANO MBAYA MNO WA WATU WALIOKADHIBISHA AYA ZA MWENYEZI MUNGU**. Yaani: Huyu punda aliyefananishiwa na ambaye kwa haki kabisa anafanana na Wayahudi ni mfano mbaya sana wanaofananishwa wenye kukadhibisha (mafundisho ya Allah). Yaani: Enyi Waislamu, msiwe kama wao. Allah ametanguliza haya ili kuwapa hadhari wale waliomuacha Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) akiwa amesimama juu ya mimbari (jukwaa) akihutubia, wakaenda kwenye biashara. Anafana na hawa kila ambaye anaipuuza hotuba (ya Ijumaa) ilhali anaisikia, kama ilivyo katika Hadithi. Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) amesema kuwa: *"Mwenye kuzungumza siku ya Ijumaa na ilhali imamu anahutubia, basi mfano wake ni kama mfano wa punda akiwa amebeba vitabu. Na ambaye anamwambia mwenzake: 'Nyamaza', hana Ijumaa"*.

(6) **SEMA: ENYI MLIO WAYAHUDI, IKIWA MNADAI KUWA NYINYI NI WAPENZI WA MWENYEZI MUNGU KINYUME NA WATU WENGINE** Muradi wa Wayahudi ni wale walioubeba Uyahudi. Na hiyo ni kwa sababu Wayahudi walidai kuwa: *wao wako juu ya watu wengine kwa ubora, wao ni wapenzi hasa wa Allah na sio watu wengine na kwamba wao ni watoto wa Allah na vipenzi vyake.* Kwa hiyo, pale walipodai madai haya batili, Mwenyezi Mungu Mtukufu akamuamrisha Mtume wake (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) awaambie kwamba: **BASI TAMANINI KUFA** ili muende kwenye utukufu uliopo katika madai yenu **IKIWA NYINYI NI WAKWELI** Katika madai haya, kwa sababu ***aliyejua kuwa yeye ni katika watu wa peponi, atapenda kuachana na nyumba hii (dunia).***

(7) **NA HAWATAMANI HUKO KUFA ASILANI, KWA SABABU YA YALE AMBAYO MIKONO YAO IMEYATENDA.** Kwa sababu ya yale waliyoyafanya, ikiwa ni pamoja na ukafiri, maasi, upotoshaji na ubadilishaji.

ترتيبها ٦٢ — سُورَةُ الجُمُعَةِ — آياتها ١١

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ
يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلۡأَرۡضِ ٱلۡمَلِكِ ٱلۡقُدُّوسِ ٱلۡعَزِيزِ
ٱلۡحَكِيمِ ١ هُوَ ٱلَّذِي بَعَثَ فِي ٱلۡأُمِّيِّـۧنَ رَسُولٗا مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ
عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمۡ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ وَإِن كَانُواْ
مِن قَبۡلُ لَفِي ضَلَٰلٖ مُّبِينٖ ٢ وَءَاخَرِينَ مِنۡهُمۡ لَمَّا يَلۡحَقُواْ بِهِمۡۚ
وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ٣ ذَٰلِكَ فَضۡلُ ٱللَّهِ يُؤۡتِيهِ مَن يَشَآءُۚ وَٱللَّهُ
ذُو ٱلۡفَضۡلِ ٱلۡعَظِيمِ ٤ مَثَلُ ٱلَّذِينَ حُمِّلُواْ ٱلتَّوۡرَىٰةَ ثُمَّ لَمۡ
يَحۡمِلُوهَا كَمَثَلِ ٱلۡحِمَارِ يَحۡمِلُ أَسۡفَارَۢاۚ بِئۡسَ مَثَلُ ٱلۡقَوۡمِ
ٱلَّذِينَ كَذَّبُواْ بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِۚ وَٱللَّهُ لَا يَهۡدِي ٱلۡقَوۡمَ ٱلظَّٰلِمِينَ ٥
قُلۡ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ هَادُوٓاْ إِن زَعَمۡتُمۡ أَنَّكُمۡ أَوۡلِيَآءُ لِلَّهِ مِن
دُونِ ٱلنَّاسِ فَتَمَنَّوُاْ ٱلۡمَوۡتَ إِن كُنتُمۡ صَٰدِقِينَ ٦ وَلَا يَتَمَنَّوۡنَهُۥٓ
أَبَدَۢا بِمَا قَدَّمَتۡ أَيۡدِيهِمۡۚ وَٱللَّهُ عَلِيمُۢ بِٱلظَّٰلِمِينَ ٧ قُلۡ إِنَّ
ٱلۡمَوۡتَ ٱلَّذِي تَفِرُّونَ مِنۡهُ فَإِنَّهُۥ مُلَٰقِيكُمۡۖ ثُمَّ تُرَدُّونَ
إِلَىٰ عَٰلِمِ ٱلۡغَيۡبِ وَٱلشَّهَٰدَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمۡ تَعۡمَلُونَ ٨

(8) **SEMA: HAYO MAUTI MNAYO YAKIMBIA, BILA YA SHAKA YATAKUKUTENI.** Yaani: Yatakujieni kutokea upande ambao nyie mnaukimbilia, na yatakabiliana nanyi uso kwa uso. **KISHA MTARUDISHWA KWA MWENYE KUYAJUA YALIYO FICHIKANA NA YANAYO ONEKANA** Na hilo ni siku ya Kiama. **HIVYO, ATAKUAMBIENI YALE MLIYOKUWA MKIYATENDA.** Matendo maovu mliyokuwa mkiyatenda, na atakulipeni kwa mujibu wake.

(9) **ENYI MLIO AMINI, UTAKAPO TOLEWA WITO KWA AJILI YA SALA.** Muradi wake ni Adhana, pale Imamu atakapokaa kwenye minbari (jukwaa) siku ya Ijumaa, kwa sababu wakati wa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) hakukuwa na wito mwingine usiokuwa huo. Ama Adhana ya kwanza ya (sala ya) Ijumaa aliiongeza Uthman, (Mwenyezi Mungu amuwiye radhi), na Swahaba wakiwepo, pale mji wa Madina ulipopanuka. **NENDENI UPESI KWENYE KUMTAJA MWENYEZI MUNGU**. Yaani: Fanyeni bidii ya kwenda kwenye kumtaja Allah, na utajo huo ni hotuba na sala ya Ijumaa katika misikiti ya Ijumaa. Jishughulisheni na sababu zake, ikiwa ni

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَوٰةِ مِن يَوۡمِ ٱلۡجُمُعَةِ
فَٱسۡعَوۡاْ إِلَىٰ ذِكۡرِ ٱللَّهِ وَذَرُواْ ٱلۡبَيۡعَۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُمۡ
تَعۡلَمُونَ ٩ فَإِذَا قُضِيَتِ ٱلصَّلَوٰةُ فَٱنتَشِرُواْ فِي ٱلۡأَرۡضِ
وَٱبۡتَغُواْ مِن فَضۡلِ ٱللَّهِ وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ كَثِيرٗا لَّعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ
١٠ وَإِذَا رَأَوۡاْ تِجَٰرَةً أَوۡ لَهۡوًا ٱنفَضُّوٓاْ إِلَيۡهَا وَتَرَكُوكَ قَآئِمٗاۚ قُلۡ
مَا عِندَ ٱللَّهِ خَيۡرٞ مِّنَ ٱللَّهۡوِ وَمِنَ ٱلتِّجَٰرَةِۚ وَٱللَّهُ خَيۡرُ ٱلرَّٰزِقِينَ ١١

ترتيبها ٦٣ — سُورَةُ المُنَافِقُونَ — آياتها ١١

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا جَآءَكَ ٱلۡمُنَٰفِقُونَ قَالُواْ نَشۡهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ
إِنَّكَ لَرَسُولُهُۥ وَٱللَّهُ يَشۡهَدُ إِنَّ ٱلۡمُنَٰفِقِينَ لَكَٰذِبُونَ ١
ٱتَّخَذُوٓاْ أَيۡمَٰنَهُمۡ جُنَّةٗ فَصَدُّواْ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِۚ إِنَّهُمۡ سَآءَ مَا كَانُواْ
يَعۡمَلُونَ ٢ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمۡ ءَامَنُواْ ثُمَّ كَفَرُواْ فَطُبِعَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمۡ
فَهُمۡ لَا يَفۡقَهُونَ ٣ ۞ وَإِذَا رَأَيۡتَهُمۡ تُعۡجِبُكَ أَجۡسَامُهُمۡۖ
وَإِن يَقُولُواْ تَسۡمَعۡ لِقَوۡلِهِمۡۖ كَأَنَّهُمۡ خُشُبٞ مُّسَنَّدَةٞۖ يَحۡسَبُونَ كُلَّ
صَيۡحَةٍ عَلَيۡهِمۡۚ هُمُ ٱلۡعَدُوُّ فَٱحۡذَرۡهُمۡۚ قَٰتَلَهُمُ ٱللَّهُۖ أَنَّىٰ يُؤۡفَكُونَ ٤

pamoja na kuoga, kutawadha na kuelekea msikitini. **NA ACHENI BIASHARA** Yaani: Acheni kufanya biashara. Na zinaunganishwa na biashara shughuli nyingine zilizobaki. Kwa hiyo, atakapoadhini muadhini siku ya Ijumaa, basi si halali kuuza na kununua (kufanya biashara). **HAYO** ya kuharakisha kwenda kwenye kumtaja Allah na kuacha biashara **NI JAMBO BORA ZAIDI KWENU.** Ni bora zaidi kuliko kufanya biashara na kuacha kuharakisha, kwa vile ndani ya kutekeleza amri kuna ujira na malipo.

(10) **NA IKISHATEKELEZWA SALA** Yaani: Mkishaitekeleza sala na mkaimaliza, **TAWANYIKENI KATIKA ARDHI** Kwa ajili ya biashara, na kufanya mambo ya maisha yenu mnayoyahitaji. **NA TAFUTENI KATIKA FADHILA ZA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Tafuteni katika riziki yake ambayo anawafadhili waja wake, ikiwa ni pamoja na faida katika miamala na machumo (kazi). **NA MKUMBUKENI SANA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Katika kuuza na kununua kwenu, msisahau kumtaja sana Allah kwa kumshukuru kwa kheri za duniani na akhera alizokuongozeni kuzifanya. Pia mtajeni kwa kwa kutumia nyiradi zinazokufanyeni muwe karibu naye, kama Tahmiid (Alhamdu Lillah), Tasbihi (Subhanallah), Takbira (Allahu Akbar) na Istighfaar (Astaghfirullah) na mfano wake. **ILI MPATE KUFANIKIWA.** Yaani: Ili mfuzu kwa kupata kheri za nyumba mbili; dunia na Akhera.

(11) **NA WANAPOIONA BIASHARA AU PUMBAO WANAYAKIMBILIA HAYO.** Sababu ya kushuka kwa aya hizi ni kwamba, uliwatokea watu wa Madina ufukara na shida. Ukaja msafara kutoka Shamu, na Mtume akiwa anahutubia siku ya Ijumaa. Watu wakatimka na kuukimbilia msafara huo, mpaka ikawa hawakubaki msikitini isipokuwa watu kumi na wawili tu. Katika upokezi mwengine imenukuliwa kwamba na wanawake saba walibaki pamoja na hao watu kumi na wawili. **NA WAKAKUACHA UKIWA UMESIMAMA.** Yaani: Ukiwa umesimama katika minbari. **SEMA: YALIYOKO KWA MWENYEZI MUNGU** Malipo makubwa ambayo ni pepo **NI BORA KULIKO PUMBAO NA BIASHARA** Mambo ambayo mliyakimbilia na mkaacha kubaki msikitini na kusikiliza hotuba ya Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) kwa sababu ya mambo hayo. **NA MWENYEZI MUNGU NI MBORA WA WATOA RIZIKI.**

## SURATUL-MUNAAFIQUN (63)

*(Imeteremka Madina)*

(1) **WANAPO KUJIA WANAAFIKI** Yaani: Wanafiki wakija kwako na kuhudhuria kikao chako **HUSEMA: TUNAKIRI KUWA, KWA YAKINI KABISA WEWE NI MTUME WA MWENYEZI MUNGU.** Wamesisitiza kukiri kwao kwa kutangaza kuwa kukiri huko kunatoka ndani ya nyoyo zao, na kwamba wao wana nia safi (Ikhlas) katika itikadi yao. Maana ya: Tunakiri ni: Tunajua. **NA MWENYEZI MUNGU ANAJUA KUWA, KWA YAKINI KABISA WEWE NI MTUME WAKE**. Huu ni uthibitisho kutoka kwa Allah wa yale madhumuni ya maneno yao ya kukubali kwamba Muhammad (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) ni Mjumbe, na ili ukadhibisho ujao usije ukafahamika kuwa unarudi kwenye hilo. **NA MWENYEZI MUNGU ANASHUHUDIA YA KUWA, KWA YAKINI WANAFIKI NI WAONGO** Yaani: Ni waongo katika kudai kuwa kumkubali kwao Mtume kwamba ni Mjumbe kunatoka ndani ya nyoyo, na kunatokana na itikadi safi, na wala sio matamshi ya maneno yao ya mdomoni. Na huko kushuhudia kwao Utume ni haki.

(2) **WAMEVIFANYA VIAPO VYAO NI KINGA.** Yaani: Wamefanya kiapo chao ambacho wanakiapa kwenu ni kinga ya kujikinga na

nyinyi, na ni hifadhi wanayo jihami kwayo wasiuawe au kutekwa. **KWA HIVYO, WAKAZUIA NJIA YA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Wakawazuia watu wasiamini, wasipigane Jihadi na wasitende matendo ya utii, kwa sababu ya yale wanayoyafanya ya kuutia shaka na kuutia ila Utume. **HAKIKA, NI MABAYA KABISA WALIYO KUWA WAKIYAFANYA.** Nayo ni unafiki na kuzuia.

(3) **HAYO NI KWA SABABU YA KUWA WAO WALIAMINI.** Yaani: Waliamini kwa unafiki **KISHA WAKAKUFURU** Kwa ndani. Na imesemwa kuwa: Aya hii imeshuka kwa watu walioamini kisha wakakufuru. **KWA HIVYO UMEPIGWA MUHURI JUU YA NYOYO ZAO.** Zimepigwa muhuru wwa hitimisho kwa sababu ya kukufuru kwao, na kwa hiyo, hazitaingiwa na imani baada ya hapo. **KWA HIVYO, WAO HAWAFAHAMU.** Hawayafahamu mambo yenye ustawi wao na uongofu wao.

(4) **NA UKIWAONA, MIILI YAO INAKUPENDEZA.** Yaani: Utapendezwa na maumbo yao na hadhi zao. Maumbo na hadhi hizo zinampendeza anayewaona, mvuto na unyororo ulio nazo. **NA WAKISEMA, UTASIKILIZA MANENO YAO.** Utadhani kuwa maneno yao ni kweli na haki, kwa sababu ya ufasaha wao na uhodari wao wa lugha. Abdallah bin Ubayyi bin Saluul alikuwa fasaha, mwenye mwili mkubwa na mzuri. **KAMA KWAMBA WAO NI MAGOGO YALIYO EGEMEZWA.** Katika kukaa kwao katika vikao vyao vya Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), wamefananishwa na mbao zilizosimamishwa ukutani, ambazo hazifahamu wala hazijui kitu, kwa kuwa hawana ufahamu wenye manufaa, na elimu ambayo mwenye nayo ananufaika nayo. **WANADHANI KILA UKELELE UNAOPIGWA NI KWA AJILI YAO.** Imesemwa kuwa: Wanafiki walikuwa kwenye hofu ya kushuka aya itakayofunua siri zao na kuhalalisha damu zao na mali zao. **HAO NDIO MAADUI; KWA HIYO, TAHADHARI NAO.** Wasije kumakinika na kupata fursa ya kuona chochote au kujua siri zako, kwa sababu wao ni wapelelezi wa adui zako makafiri. **MWENYEZI MUNGU AWAANGAMIZIE MBALI!** Yaani: Mwenyezi Mungu awalaani. Au hilo ni funzo kwa waumini waseme hivyo. **VIPI WANAPOTOKA?** Vipi wanakengeuka na kuiacha haki na kuelemea kwa makafiri?

(5) **NA WANAPOAMBIWA: NJOONI ILI MTUME WA MWENYEZI MUNGU AKUOMBEENI MAGHFIRA, HUVIGEUZA VICHWA VYAO.** Yaani: Wanavitingisha vichwa vyao kwa kulidhihaki hilo, na kutotaka kuombewa maghfira. **NA UNAWAONA WANAGEUKA** Wanampuuza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) **NA ILHALI WAMEJAA KIBURI** Kuhusu kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na kumuomba awaombee msamaha. Wanajiona kuwa wao ni wakubwa zaidi wasioweza kufanya hilo, na wanaona kuwa ni kujidunisha kama wangefanya.

(6) **NI SAWA KWAO; UMEWAOMBEA MAGHFIRA AU HUKUWAOMBEA MAGHFIRA.** Hilo halitowasaidia, kwa sababu ya kung'ang'ania kwao unafiki na kudumu kwao kwenye ukafiri. **MWENYEZI MUNGU HATAWAGHUFIRIA.** Yaani: Mwenyezi Mungu hatawasamehe madamu wanaendelea kuwa katika unafiki. **HAKIKA, MWENYEZI MUNGU HAWAONGOZI WAOVU.** Yaani: Wakamilifu katika kutoka katika utii, na kuzama katika kumuasi Allah. Katika hili, wanafiki wanaingia mwanzo kabisa.

(7) **HAO NDIO WANAOSEMA: MSITOE MALI KWA WALE WALIOKO KWA MTUME WA MWENYEZI MUNGU MPAKA WAONDOKE!** Yaani: Mpaka waachane naye. Kwa hilo, wanawakusudia wale Muhajirina mafukara. **NA MWENYEZI MUNGU TU NDIYE MWENYE HAZINA ZA MBINGUNI NA ARDHINI**. Yaani: Yeye ndiye Mtoaji riziki kwa hawa Muhajirina. **LAKINI WANAFIKI HAWAFAHAMU.** Hawafahamu kuwa hazina za riziki zipo mkononi mwa Allah, kwa hiyo, wakadhani kuwa Allah hatawakunjulia (riziki) waumini.

(8) **WANASEMA: TUKIREJEA MADINA, BILA YA SHAKA MWENYE UTUKUFU ZAIDI ATAMFUKUZA HUMO ALIYE MNYONGE ZAIDI.** Msemaji ni Abdallah bin Ubayyi bin Saluul, kiongozi wa wanafiki. Kwa 'Mtukufu zaidi', alimaanisha yeye mwenyewe na waliopo pamoja naye. Na kwa 'Dhalili zaidi', alimkusudia Mtume wa Mwenyezi Mungu na waliopo pamoja naye. Na muradi wake wa 'Kurejea' ni kurejea kwao kutoka kwenye vita hivyo. Imepokewa kutoka kwa Zaid bin Arqam akisema kuwa: *"Nilikuwa pamoja na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) katika vita. Abdallah bin Ubayyi akasema: 'Kama tukirejea Madina, bila shaka watukufu zaidi watawafukuza humo madhalili zaid'. Akasema: Nikamuendea Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) nikamwambia. Basi Abdallah bin Ubayyi akaapa kuwa hakukuwa na kitu kama hicho. Zaid akasema: Watu wangu wakanilaumu na kusema: Ulikuwa unataka nini kwenye hili? Zaid akasema: Basi nikaondoka na kwenda kulala nikiwa mnyonge, mwenye huzuni. Akasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu akaniita na kusema: "Hakika,*

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْاْ يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ ٱللَّهِ لَوَّوْاْ رُءُوسَهُمْ
وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّونَ وَهُم مُّسْتَكْبِرُونَ ٥ سَوَآءٌ عَلَيْهِمْ
أَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ أَمْ لَمْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ لَن يَغْفِرَ ٱللَّهُ لَهُمْ إِنَّ
ٱللَّهَ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلْفَٰسِقِينَ ٦ هُمُ ٱلَّذِينَ يَقُولُونَ
لَا تُنفِقُواْ عَلَىٰ مَنْ عِندَ رَسُولِ ٱللَّهِ حَتَّىٰ يَنفَضُّواْ وَلِلَّهِ
خَزَآئِنُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَلَٰكِنَّ ٱلْمُنَٰفِقِينَ لَا يَفْقَهُونَ
٧ يَقُولُونَ لَئِن رَّجَعْنَآ إِلَى ٱلْمَدِينَةِ لَيُخْرِجَنَّ ٱلْأَعَزُّ
مِنْهَا ٱلْأَذَلَّ وَلِلَّهِ ٱلْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِۦ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَٰكِنَّ
ٱلْمُنَٰفِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ٨ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تُلْهِكُمْ
أَمْوَٰلُكُمْ وَلَآ أَوْلَٰدُكُمْ عَن ذِكْرِ ٱللَّهِ وَمَن يَفْعَلْ
ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْخَٰسِرُونَ ٩ وَأَنفِقُواْ مِن مَّا رَزَقْنَٰكُم
مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِىَ أَحَدَكُمُ ٱلْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَآ أَخَّرْتَنِىٓ
إِلَىٰٓ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ١٠ وَلَن
يُؤَخِّرَ ٱللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَآءَ أَجَلُهَا وَٱللَّهُ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ١١

ترتيبها ٦٤ — سُورَةُ التَّغَابُنِ — آياتها ١٨

*Allah ameteremsha udhuru wako na amekusadikisha, na akateremsha aya hii".*

(9) **ENYI MLIO AMINI, YASIKUSAHAULISHENI MALI YENU WALA WATOTO WENU KUMKUMBUKA MWENYEZI MUNGU.** Allah anawatahadharisha waumini tabia za wanafiki ambao mali zao na watoto wao wamewapumbaza wakapuuza kumkumbuka Allah; faradhi za Uislamu. Imesemwa pia kuwa kinachokusudiwa (kwa kumkumbuka Allah) ni kusoma Qur-ani. **NA WENYE KUFANYA HAYO** Yaani: Wenye kubweteka na dunia wakapuuza dini **HAO NDIO WENYE HASARA.** Yaani: Hao ndio wakamilfu katika kupata hasara.

(10) **NA TOENI KATIKA TULIVYO KUPENI.** Yaani: Toeni katika njia ya kheri baadhi ya tuliyokuruzukuni. Na imesemwa kinachokusudiwa ni Zaka ya faradhi. **KABLA HAYAJAMFIKIA MMOJA WENU MAUTI.** Kwa kumfika sababu zake, au kwa kuona kuhudhuria alama zake. **AKASEMA: EWE MOLA WANGU, NATAMANI UNIAHIRISHE NIPATE MUDA KIDOGO!** Yaani: Naomba unipe muda na uahirishe mauti yangu hadi muda mwingine mfupi. **NIPATE KUTOA SADAKA.** Yaani: Ili mali yangu niitoe sadaka. **NA NIWE MIONGONI MWA WATU WEMA!**

(11) **NA MWENYEZI MUNGU HATOAHIRISHA NAFSI YOYOTE UNAPOFIKA MUDA WAKE.** Yaani: Unapokuja muda wake na unapokwisha umri wake. **NA MWENYEZI MUNGU ANAZO HABARI ZA MNAYO YATENDA.** Hakijifichi chochote kwake katika hayo. Yeye atakulipeni kwa mujibu wa matendo yenu.

## SURATUT-TAGHAABUN (64)

*(Imeteremka Madina)*

(2) **YEYE NDIYE ALIYE KUUMBENI. MIONGONI MWENU YUPO AMBAYE NI KAFIRI, NA MINGONI MWENU YUPO AMBAYE NI MUUMINI.** Allah (Subhaanahu wa Taala) amemuumba kafiri, na ukafiri wake ni matendo yake na ni chumo lake. Na amemuumba muumini, na imani yake ni matendo yake na ni chumo lake. Kafiri anakufuru na anachagua ukafiri. Muumini naye anaamini na anachagua imani. Na yote hayo ni kwa idhini ya Allah. Allah amesema kuwa: *"Na hamtaki ila tu akitaka Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu".* Sura Attakwiir (81), aya 29.

(3) **NA AKAKUPENI SURA, NA AKAZIFANYA NZURI SURA ZENU.** Yaani: Yeye Allah (s.w) amekuumbeni katika sura kamilifu sana na umbo zuri sana. Ubora wa binadamu katika uzuri wa sura na uzuri wa kimo haujifichi, na kwamba huo ni ushahidi wa wazi kwa watu wenye akili juu ya uwezo wa Muumba, hekima zake na ukufu wake. Kadhalika sura ya kisaikolojia ya mwanadamu na uwezo wake mkubwa wa kiakili ni dalili nyingine kubwa zaidi ya hiyo, kama Allah alivyosema kuwa: *"Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini. Na pia katika nafsi zenu. Je, hamuoni?".*Sura Adh-dhaariyaat (51), aya 20-21.

(5) **JE, HAIKUKUJIENI HABARI YA AMBAO WALIKUFURU KABLA YENU?** Hao ni makafiri wa mataifa yaliyopita, kama watu wa Nuhu, Aad na Thamuud. Allah Mtukufu anesema kuwa: Ni hakika, imekujieni habari yao katika Qur-ani na jinsi Mitume wao walivyowalingania watu wao kwenye kumpwekesha Allah, kumuabudu na kuacha vile vitu walivyovifanya miungu badala Mwenyezi Mungu, na jinsi mambo ya makafiri yalivyoishia kwenye maangamivu, na mambo ya Mitume na waumini yalivyoishia kwenye uokovu. **WAKAONJA UGUMU WA MAMBO YAO** Wakaonja uzito na shida; mateso ya dunia yaliyo wakumba. **NA WATAPATA ADHABU ILIYO CHUNGU.** Nayo ni adhabu ya moto.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ
يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۖ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ۖ
وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ فَمِنكُمْ كَافِرٌ
وَمِنكُم مُّؤْمِنٌ ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢﴾ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ
وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ ۖ وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ﴿٣﴾
يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُسِرُّونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ۚ وَاللَّهُ
عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٤﴾ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَبْلُ
فَذَاقُوا وَبَالَ أَمْرِهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥﴾ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُ كَانَت تَّأْتِيهِمْ
رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَقَالُوا أَبَشَرٌ يَهْدُونَنَا فَكَفَرُوا وَتَوَلَّوا ۚ وَّاسْتَغْنَى
اللَّهُ ۚ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٦﴾ زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي
لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾ فَآمِنُوا بِاللَّهِ
وَرَسُولِهِ وَالنُّورِ الَّذِي أَنزَلْنَا ۚ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٨﴾ يَوْمَ
يَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ ۖ ذَٰلِكَ يَوْمُ التَّغَابُنِ ۗ وَمَن يُؤْمِن بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ
صَالِحًا يُكَفِّرْ عَنْهُ سَيِّئَاتِهِ وَيُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا
الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٩﴾

(6) **HAYO** ya kupata mateso katika nyumba mbili (mateso ya duniani na adhabu ya Akhera) **NI KWA SABABU MITUME WAO WALIKUWA WAKIWAPA HOJA ZILIZO WAZI** Ni kwa sababu kwamba Mitume waliotumwa kwao walikuwa wanawaletea miujiza ya wazi **WAKASEMA: HIVI, BINADAMU NDIO ATUONGOZE?** Yaani: Kila watu miongoni mwao walimwambia maneno haya Mtume wao wakipinga Mtume kuwa ni katika jinsi ya wanadamu, na walilistaajabu jambo hilo. **HIVYO, WAKAKUFURU, NA WAKAGEUKA UPANDE.** Yaani: Waliwakataa Mitume na waliyakataa yale waliyokuja nayo, waliwapuuza na hawakuyatia maanani yale waliyokuja nayo. **NA MWENYEZI MUNGU AKAJITOSHA.** Akawa hana haja ya imani yao na ibada zao. **NA MWENYEZI MUNGU NI MKWASI, NI MSIFIWA** Yaani: Si mhitaji wa walimwengu wala ibada zao wanazomfanyia, ni mwenye kuhimidiwa (kusifiwa) na viumbe wake wote, kwa lugha ya maneno au hali halisi.

(7) **SEMA: KWANINI ISIWE? NINA APA KWA MOLA WANGU KWAMBA, KWA YAKINI KABISA MTAFUFULIWA.** Allah Mtukufu amemuamuru Mtume wake awape habari kuwa Allah atawafufua baada ya kufa, na kuwaapia jambo hilo. Yaani: Nina apa kuwa mtatolewa kwenye makaburi yenu. **NA KISHA HAPANA SHAKA KUWA MTAAMBIWA MLIYO YATENDA.** Yaani: Mtapewa habari ya hayo, kwa ajili ya kuwasimamishia hoja, kisha mtalipwa kwayo. **NA HILO** la kufufuliwa na kulipwa **KWA MWENYEZI MUNGU NI JAMBO JEPESI.**

(8) **NA NURU TULIYO ITEREMSHA.** Nayo ni Qur-ani, kwakuwa ni nuru inayoongoza dhidi ya kiza cha upotevu.

(9) **SIKU ATAKAYO KUKUSANYENI KWA AJILI YA SIKU YA MKUSANYIKO.** Yaani: Kwa ajili ya Siku ya Kiama. Hiyo ni siku ambayo watu wa mahali pa kukusanyiwa watakusanywa kwa ajili ya malipo. Ndani ya siku hiyo, patakusanywa baina ya kila mtendaji na vitendo vyake, na baina ya kila Nabii na umma wake, baina ya kila aliyedhulumiwa na aliyedhulumu, na baina ya watu wa mwanzo na watu wa mwisho. **HIYO NI SIKU YA KUPUNJANA.** Katika siku hiyo, watu wa mahali pa kukusanywa watapunjana wenyewe kwa wenyewe. Siku hiyo, watu wa haki watawapunja watu wa batili. Na wala hakuna kupunjwa kukubwa zaidi kuliko watu wa peponi watakavyowapunja watu wa motoni; kana kwamba watu wa motoni wamebadilisha kheri kwa shari, kizuri kwa kibaya na neema kwa adhabu. Watu wa peponi wako tofauti na hivyo. Kwa hiyo, aliyepunjwa kweli ni yule aliyepunjwa jamaa na makazi yake peponi. **NA YEYOTE ANAYE MUAMINI MWENYEZI MUNGU NA AKATENDA MEMA, ATAMFUTIA MAOVU YAKE.** Yaani: Ambaye imepatikana kwake imani pamoja na matendo mema, basi anastahiki kufutiwa makosa yake.

(11) **HAUFIKI MSIBA WOWOTE ILA KWA IDHINI YA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Kwa hukumu yake na kudura yake. Imesemwa kuwa: Na sababu ya kuteremsha kwa aya hiyo ni kwamba: Makafiri waliesema kuwa: *"Ikiwa yale walionayo Waislamu ni haki, bila shaka Mwenyezi Mungu angewalinda wasipate misiba matatizo katika dunia"*. **NA MWENYE KUMUAMINI MWENYEZI MUNGU, HUUONGOA MOYO WAKE.** Yaani: Ambaye anaamini na anajua kuwa hayampati ila tu yale aliyopangiwa na Allah, basi atauongoza moyo wake wakati wa msiba. Kwa hiyo, atajua kuwa msiba huo unatokana na Allah, na kwamba yaliyompata yasingemkosa, na yaliyomkosa yasingempata. Anaikubali hukumu ya Allah, na kuyarejesha mambo yote kwake. Akipatwa na

mitihani anavumilia, na akipewa neema anashukuru. **NA MWENYEZI MUNGU NI MJUZI WA KILA KITU.** Yaani: Mwingi wa elimu, hakifichiki kwake chochote katika hayo.

(12) **NA MTIINI MWENYEZI MUNGU, NA MTIINI MTUME.** Yaani: Jishughulisheni na kumtii Allah na kumtii Mtume wake. **MKIGEUKA,** Yaani: Mkipinga kutii basi madhambi yenu ni juu ya nafsi zenu, na Mtume hana tatizo lolote. **BASI HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA LILILO WAJIBU JUU YA MTUME WETU NI KUFIKISHA (UJUMBE) KULIKO WAZI.** Hana wajibu zaidi ya hilo, na amelifanya.

(14) **MAADUI ZENU.** Yaani: Wanakushughulisheni msifanye kheri. Sababu ya kushuka (aya hii) ni kuwa, kuna watu kutoka Makkah walisilimu na wakataka kuhama (kwenda Madina). Basi wake zao na watoto wao hawakuwaacha (wahame). Mujahidi amesema kuwa: "*Wallahi, hawakuwafanyia uadui duniani, lakini mapenzi yao yaliwachukua kwenye kuwafanyia haramu, na waliwapa*". **BASI TAHADHARINI NAO.** Yaani: Chukueni hadhari na wake na watoto, ili mapenzi yenu kwao na huruma yenu kwao isiathiri katika kumtii Allah, na wala kheri mnayopenda waipate isikuchukueni kwenye kuchuma riziki kwa kumuasi Allah. **NA MKISAMEHE, NA MKAPUUZA, NA MKAGHUFIRIA** Yaani: Mkisamehe makosa yao waliyoyafanya, na mkaacha kulaumu na mkazisitiri **BASI HAKIKA, MWENYEZI MUNGU NI MWINGI WA MAGHFIRA, MWENYE KUREHEMU** Ni mwenye kuwasamehe na kuarehemu nyinyi na wao. Imesemwa kuwa: Mtu mmoja ambaye alikuwa amedhibitiwa na mke na watoto wake asihame (kwenda Madina), akiwaona watu wamemtangulia kwenye hilo na wanajua dini, basi hutaka kuwaadhibu wake zake na watoto wake.

(15) **HAKIKA HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA MALI ZENU NA WATOTO WENU NI MTIHANI.** Yaani: Ni balaa, majaribio na msukusuko. Wanakupelekeni kwenye kuchuma haramu, na kuzuia haki ya Allah. **NA KWA MWENYEZI MUNGU UPO UJIRA MKUBWA.** Ujira kwa aliyeupa kipumbele utii kwa Allah, na akaacha kumuasi kwa sababu ya kupenda mali yake na watoto wake.

(16) **BASI MCHENI MWENYEZI MUNGU KADIRI MUWEZAVYO.** Yaani: Kadiri mnavyoweza, na kadiri juhudi zenu zilipoifikia. **NA SIKIENI, NA TIINI.** Yaani: Sikieni na tiini amri za Allah na Mtume wake. **NA TOENI, ITAKUWA KHERI KWA NAFSI ZENU.** Yaani: Toeni katika mali zenu ambazo Allah amekuruzukuni katika njia za kheri. Wala msizifanyie ubahili, na tangulizeni kufanya heri kwa ajili ya nafsi zenu. **NA MWENYE KUEPUSHWA NA UCHOYO WA NAFSI YAKE, BASI HAO NDIO WALIO FANIKIWA** Yaani: Yule ambaye Allah amemkinga na ugonjwa wa ubahili na, kwa hiyo, akatoa katika njia ya Allah na katka milango ya kheri, basi hao ndio waliopata kheri zote, na waliofuzu kupata mahitaji yote.

(17) **MKIMKOPESHA MWENYEZI MUNGU MKOPO MZURI.** Yaani: Mkitumia mali zenu katika njia za kheri kwa nia safi, na ridhaa ya nafsi **ATAKUZIDIDISHIENI MARADUFU.** Atalifanya jambo zuri moja kwa mazuri kumi mfano wake, hadi nyongeza mia saba. **NA ATAKUSAMEHENI.** Yaani: Anakuongezeni msamaha wa dhambi zenu kwenye nyongeza hiyo. **NA MWENYEZI MUNGU NI MWINGI WA SHUKURANI, MPOLE.** Yaani: Humpa thawabu anayemtii kwa kumuongezea nyongeza nyingi, wala hafanyi haraka kumuadhibu mwenye kumuasi.

وَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَكَذَّبُواْ بِـَٔايَٰتِنَآ أُوْلَٰٓئِكَ أَصۡحَٰبُ
ٱلنَّارِ خَٰلِدِينَ فِيهَاۖ وَبِئۡسَ ٱلۡمَصِيرُ ١٠ مَآ أَصَابَ مِن
مُّصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذۡنِ ٱللَّهِۗ وَمَن يُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ يَهۡدِ قَلۡبَهُۥۚ وَٱللَّهُ بِكُلِّ
شَيۡءٍ عَلِيمٞ ١١ وَأَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَۚ فَإِن
تَوَلَّيۡتُمۡ فَإِنَّمَا عَلَىٰ رَسُولِنَا ٱلۡبَلَٰغُ ٱلۡمُبِينُ ١٢ ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ
إِلَّا هُوَۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَلۡيَتَوَكَّلِ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ١٣ يَٰٓأَيُّهَا
ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّ مِنۡ أَزۡوَٰجِكُمۡ وَأَوۡلَٰدِكُمۡ عَدُوّٗا
لَّكُمۡ فَٱحۡذَرُوهُمۡۚ وَإِن تَعۡفُواْ وَتَصۡفَحُواْ وَتَغۡفِرُواْ
فَإِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٌ ١٤ إِنَّمَآ أَمۡوَٰلُكُمۡ وَأَوۡلَٰدُكُمۡ
فِتۡنَةٞۚ وَٱللَّهُ عِندَهُۥٓ أَجۡرٌ عَظِيمٞ ١٥ فَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ مَا ٱسۡتَطَعۡتُمۡ
وَٱسۡمَعُواْ وَأَطِيعُواْ وَأَنفِقُواْ خَيۡرٗا لِّأَنفُسِكُمۡۗ وَمَن
يُوقَ شُحَّ نَفۡسِهِۦ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ١٦ إِن تُقۡرِضُواْ
ٱللَّهَ قَرۡضًا حَسَنٗا يُضَٰعِفۡهُ لَكُمۡ وَيَغۡفِرۡ لَكُمۡۚ وَٱللَّهُ شَكُورٌ
حَلِيمٌ ١٧ عَٰلِمُ ٱلۡغَيۡبِ وَٱلشَّهَٰدَةِ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ١٨

## سُورَةُ الطَّلَاقِ

ترتيبها ٦٥ — آياتها ١٢

# 65. SURATUT-T'ALAAQ

*(Imeteremka Madina)*

1 **EWE NABII, MTAKAPO WAPA TALAKA WANAWAKE.** Kwanza amemwita Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa ajili ya kumtukuza. Kisha amemsemesha yeye pamoja na umma wake. Maana ni kwamba: Mnapotaka kuwapa talaka wanawake na mkaazimia kulifanya hilo **BASI WAPENI TALAKA KWA EDA ZAO.** Yaani: Wakielekea eda zao, au kabla ya eda zao. Muradi ni kuwataliki katika tohara ambayo haijatokea ndani yake kujamiiana. Kisha wanaachwa hadi eda yao iishe. Kwa hiyo, wakiwapa Talaka kwa namna hii, basi wanakuwa wamewapa Talaka kwa eda zao. Imenukuliwa kwa Ibni-umar kuwa *"Alimpa Talaka mkewe akiwa na hedhi. Umar akalisema hilo kwa Mtume Mtume wa Mwenyezi* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). *Mtume wa Mwenyezi Mungu* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *Alikasirika kisha akasema: Amrudie, kisha akaye naye hadi atoharike, kisha apate hedhi na atoharike. Basi ikimdhihirikia kuwa anataka kumpa talaka, ampe ilhali akiwa tohara, kabla ya kumgusa. Hiyo ndio eda aliyoiamrisha Allah wanawake kuachwa kwa ajili yake".* **NA IFANYIENI HISABU EDA.** Yaani: Ihifadhini Eda na hifadhini wakati ambao ndani yake imetokea Talaka hadi Eda itimie. Na Eda ni tohara tatu. Maneno haya wanaambiwa waume. **NA MCHENI MWENYEZI MUNGU, MOLA WENU.** Msimuasi katika yale aliyokuamrisheni, wala msiwadhuru (wake zenu). **MSIWATOE KATIKA NYUMBA ZAO.** Yaani: Msiwafukuze katika nyumba ambazo walikuwemo humo wakati wa Talaka, madamu wamo katika Eda. Na amezihusisha nyumba kwao *'Nyumba Zao'*, kwa ajili ya kubainisha ukamilifu wa kustahiki kwao kukaa humo katika muda wa Eda. Na pia amewakataza wake kutoka wenyewe, akasema: **WALA WASITOKE.** Yaani: Wasitoke kwenye nyumba hizo madamu wamo katika Eda, ispokuwa kwa jambo la dharura, lisilo epukika. **ILA TU WAKIFANYA JAMBO LA UCHAFU ULIO WAZI.** Yaani: Msiwafukuze kwenye nyumba zao, isipokuwa tu watakapofanya uchafu wa zinaa. Imesemwa kuwa: Uchafu huo ni uchafu wa lugha, na kutumia lugha chafu hiyo dhidi ya yule ambaye anaishi naye katika nyumba hiyo. **HIYO NDIYO MIPAKA YA MWENYEZI MUNGU.** Maana ni kwamba: Sheria hizi ambazo Mwenyezi Mungu amezibainisha kwa waja wake, ndiyo mipaka yake aliyowawekea. Sio halali kwao kuikiuka na kwenda kwenye mengine. **NA MWENYE KUIKIUKA MIPAKA YA MWENYEZI MUNGU, BASI AMEJIDHULUMU MWENYEWE.** Kwa kujiingiza katika maangamizi. **HUJUI; LABDA MWENYEZI MUNGU BAADA YA HAYO**

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَطَلِّقُوهُنَّ لِعِدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا۟
ٱلْعِدَّةَ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ رَبَّكُمْ ۖ لَا تُخْرِجُوهُنَّ مِنۢ بُيُوتِهِنَّ
وَلَا يَخْرُجْنَ إِلَّآ أَن يَأْتِينَ بِفَٰحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ ۚ وَتِلْكَ حُدُودُ
ٱللَّهِ ۚ وَمَن يَتَعَدَّ حُدُودَ ٱللَّهِ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُۥ ۚ لَا تَدْرِى لَعَلَّ
ٱللَّهَ يُحْدِثُ بَعْدَ ذَٰلِكَ أَمْرًا ﴿١﴾ فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ
بِمَعْرُوفٍ أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا۟ ذَوَىْ عَدْلٍ مِّنكُمْ
وَأَقِيمُوا۟ ٱلشَّهَٰدَةَ لِلَّهِ ۚ ذَٰلِكُمْ يُوعَظُ بِهِۦ مَن كَانَ يُؤْمِنُ
بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ ۚ وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجْعَل لَّهُۥ مَخْرَجًا ﴿٢﴾ وَيَرْزُقْهُ
مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۚ وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُۥٓ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ
بَٰلِغُ أَمْرِهِۦ ۚ قَدْ جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُلِّ شَىْءٍ قَدْرًا ﴿٣﴾ وَٱلَّٰٓـِٔى يَئِسْنَ
مِنَ ٱلْمَحِيضِ مِن نِّسَآئِكُمْ إِنِ ٱرْتَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَٰثَةُ أَشْهُرٍ
وَٱلَّٰٓـِٔى لَمْ يَحِضْنَ ۚ وَأُو۟لَٰتُ ٱلْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَن يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ
وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجْعَل لَّهُۥ مِنْ أَمْرِهِۦ يُسْرًا ﴿٤﴾ ذَٰلِكَ أَمْرُ ٱللَّهِ أَنزَلَهُۥٓ
إِلَيْكُمْ ۚ وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يُكَفِّرْ عَنْهُ سَيِّـَٔاتِهِۦ وَيُعْظِمْ لَهُۥٓ أَجْرًا ﴿٥﴾

**ATALETA JAMBO.** Yaani: Aliyepewa Talaka akibaki kwenye nyumba yake, huenda Allah akaziunganisha nyoyo zao, na wakarudiana.

2 **BASI WANAPO FIKIA MUDA WAO,** Wakikaribia kufikia kuisha kwa muda wa Eda, na kuona mwisho wake **WASHIKENI KWA WEMA** Yaani: Warudieni kwa mafungamano mazuri, na kwa kuwahitaji, bila ya kukusudia kuwafanyia madhara. **AU TENGANENI NAO KWA WEMA.** Yaani: Waacheni mpaka Eda yao iishe, na hivyo wawe huru, pamoja na kuwatimizia haki zao kwenu na kuacha kuwadhuru. Yaani: Nyie hamna jambo jingine wakati wa kwisha kwa Eda yao isipokuwa tu kuishi kwa wema au kutengana kwa wema. Ama kuishi kwa kufanyiana madhara au kuachana kwa maudhi pamoja na kuzuia haki, hilo sio halali kwenu. **NA WASHUHUDISHENI WAWILI WENYE UADILIFU MIONGONI MWENU.** Wekeni mashahidi juu ya Rejea iwapo mtarejea, au Talaka iwapo mtaachana, kwa ajili ya kukata mizozo na kuondoa kiini cha uhasama. **NA SIMAMISHENI USHAHIDI KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU.** Hii ni amri kwa mashahidi kwamba watoe ushahidi wa walichoshuhudia kwa njia ya haki, kwa minajili

ya kujikurubisha kwa Allah. **HAYO KWENU ANAPEWA MAWAIDHA KWAYO YULE ANAYE MUAMINI MWENYEZI MUNGU NA SIKU YA MWISHO.** Amehusishwa Muumini kwa kuwa yeye ndiye anaye nufaika na hayo, kinyume cha mwengine. **NA ANAYE MCHA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Atakayemcha Allah kwa kusimama katika ile mipaka yake aliyo wawewekea waja wake **HUMTENGEZEA PA KUTOKEA.** Kutokana na jambo lililomsibu.

3 **NA HUMRUZUKU KWA NAMNA ASIYO TAZAMIA.** Yaani: Kwa njia isiyopita mawazoni mwake, wala isiyokuwepo hisabuni mwake. Kwa hiyo, atakaye toa Talaka, kisha wakati wa kutengana akaweka mashahidi juu ya kwisha kwa Eda au wakati wa kurejeana, Allah atamfanyia matokeo na faraja. Hakuna vingine isipokuwa kwamba dhiki inakuwa kwa yule anayevunja sheria za Mwenyezi Mungu katika Talaka na Rejea. **NA ANAYE MTEGEMEA MWENYEZI MUNGU, YEYE HUMTOSHA.** Yaani: Na mwenye kumtegemea Allah katika yaliompata, Allah atamtosheleza katika yale yanayomsumbua. **HAKIKA, MWENYEZI MUNGU NI MWENYE KUTIMIZA JAMBO LAKE.** Yaani: Hakimpiti kitu, na halimshindi liombwalo. **MWENYEZI MUNGU KAJAALIA KILA KITU NA KIPIMO CHAKE.** Allah (Subhaanahu ) ameiwekea shida muda inaoishia hapo, na raha pia ameiwekea muda inaoishia hapo. *"Sudiyu amesema kuwa: Hicho ni kipimo cha Hedhi na Eda".*

4 **NA WALE WALIO ZIKATIA TAMAA HEDHI MIONGONI MWA WANAWAKE WENU.** Na hao ni wanawake wazee ambao Hedhi zao zimekatika na wamezikatia tamaa. **IKIWA MNAYO SHAKA** Yaani: Mkiwa na shaka na hamkujua eda zao zikoje **BASI EDA YAO NI MIEZI MITATU, NA AMBAO HAWAPATI HEDHI.** Na ambao hawapati Hedhi kwa udogo wao na kutofikia kwao umri wa kupata Hedhi. Yaani: Eda yao ni miezi mitatu pia. **NA WENYE MIMBA, MUDA WAO NI KUJIFUNGUA MIMBA ZAO.** Yaani: Kwisha kwa Eda zao ni kwa kujifungua. **NA ANAYE MCHA MWENYEZI MUNGU, HUMFANYIA WEPESI KATIKA MAMBO YAKE.** Dhahaki amesema kuwa: *"Mwenye kumcha Allah na akatatoa Talaka kwa kufuata Sunnah (mafundisho ya Mtume), Allah atamfanyia wepesi katika jambo lake katika Rejea".*

5 **NA ATAMPA MALIPO MKUBWA.** Yaani: Atampa malipo mkubwa huko Akhera, nayo ni pepo.

6 **WAPENI MAKAZI PALE MNAPOKAA NYINYI.** Huu ni ubainisho wa makazi wanayopasa kupewa wake waliopewa Talaka. Yaani: Wapeni makazi katika baadhi ya makazi yenu. **KWA KADIRI YA PATO LENU.** Yaani: Kutokana nafasi na uwezo wenu. Ha hili ni kwa mke alieachwa Talaka Rejea. Ama ambaye ameachwa Talaka tatu, huyo hana haki ya makazi wala matumizi. **WALA MSIWALETEE MADHARA MKAWADHIKI** Katika makazi au matumizi. **NA WAKIWA WAJAWAZITO, WAPENI MATUMIZI MPAKA WAJIFUNGUE.** Wala hakuna upinzani baina ya wanazuoni katika kupasa matumizi na makazi kwa mke mjamzito aliyeachwa. **NA WAKIKUNYONYESHEENI** Yaani: Wakiwanyonyesha watoto wenu baada ya hapo **BASI WAPENI UJIRA WAO.** Yaani: Ujira wa kunyonyesha kwao. **NA SHAURIANENI KWA WEMA.** Hili ni agizo kwa waume na wake ambao baina yao kumetokea kutengana kwa Talaka. Yaani: Shaurianeni baina yenu kwa mambo ambayo ni mazuri, yasiyo chukiza. Baadhi yenu wakubali kwa wenziwe yaliyo mema na mazuri kuhusu masuala ya watoto. Na hili ni kama alivyosema Allah Taalaa kuwa: *"Basi kama wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa kuridhiana na kushauriana, basi si vibaya kwao".* **Sura Albaqara (2), aya 233.** **NA MKITILIANA UZITO,** Yaani: Mkitiliana uzito katika ujira wa kunyonyesha; kwa baba kukataa kumpa mama ujira ambao anataka, na mama akakataa kunyonyesha isipokuwa tu kwa ujira anaoutaka **BASI MWANAMKE MWENGINE AMNYONYESHEE.** Yaani: Aajiri mnyonyeshaji mwingine amnyonyeshee mtoto wake.

7 **MWENYE WASAA ATOE KUTOKANA NA WASAA WAKE.** Ndani ya aya hii kuna amri kwa wenye uwezo, kwamba wawakunjulie wanyonyeshaji miongoni mwa wake zao, kwa kadiri ya wasaa wao. **NA AMBAYE RIZIKI YAKE IMEPANGWA KUWA NDOGO** Yaani: Ambaye amebanwa katika riziki akawa fukara **ATOE KUTOKANA NA KILE MWENYEZI MUNGU ALICHOMPA.** Yaani: Atoe kutoka katika ile riziki aliyopewa na Allah, na hana wajibu zaidi ya huo. **MWENYEZI MUNGU HAIKALIFISHI NAFSI ILA TU KILE ALICHO IPA.** Ila tu ile riziki aliyoipa. Fukara hakalafishwi kutoa ambacho hakipo katika uwezo wake, kama matumizi ya tajiri. **MWENYEZI MUNGU ATAJAALIA WEPESI BAADA YA UZITO.** Yaani: Baada ya dhiki na shida, atafanya ukunjufu na utajiri.

8 **NA NI VIJIJI VINGAPI VILIVUNJA AMRI YA MOLA WAKE NA MITUME WAKE?** Yaani: Ni watu wengi wa vitongojini waliasi amri ya Allah na Mitume wake na wakapuuza. **TUKAVIHISABU HISABU**

**NGUMU.** Mwenyezi Mungu akavihisabu kwa matendo yake viliyoyatenda duniani **NA TUKAVIADHIBU ADHABU KALI.** Tuliwaadhibu watu wake adhabu kubwa, mbaya Akhera, na duniani tuliwaadhibu kwa njaa, ukame, kudidimizwa na kubadilishwa maumbile.

(9) **VIKAONJA UBAYA WA MAMBO YAKE** Yaani: Wakaonja mwisho wa adhabu nzito ambayo ndio malipo ya ukafiri wao. **NA MWISHO WA MAMBO YAKE IKAWA HASARA.** Yaani: Maangamizi duniani na adhabu Akhera. Kwa hiyo, wamepata hasara za mali zao, watu wao na nafsi zao.

(10) (11) **MWENYEZI MUNGU AMEWAANDALIA ADHABU KALI.** Nayo ni adhabu ya moto. **BASI MCHENI MWENYEZI MUNGU, ENYI WENYE AKILI**. Yaani: Enyi watu wenye akili kali, nao ni Umma wa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). **AMBAO WAMEAMINI** Ambao wamejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na kumfuata Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). Kwa hiyo, kuweni wakweli katika imani yenu, na wala msiwe kama mataifa yaliyoasi kabla yenu. Wakahesabiwa hesabu nzito, na wakaadhibiwa kwa adhabu ya jinsi hiyo. **HAKIKA MWENYEZI MUNGU AMEKUTEREMSHIENI UKUMBUSHO** Ukumbusho ni Qur'ani Tukufu. Na imesemwa kuwa ukumbusho hapa ni Mtume mwenyewe, na kwa ajili hiyo Allah amesema kuwa: **MTUME.** Yaani: Amekuteremshieni Qur'ani, na amekutumieni Mtume akiwa na hii Qur'ani **ANAYE KUSOMEENI AYA ZA MWENYEZI MUNGU ZINAZO BAINISHA.** Anawabainishia watu hukumu wanazozihitaji. **ILI AWATOE WALIO AMINI NA WAKATENDA MEMA KUTOKA GIZANI KUWAPELEKA KWENYE NURU.** Ili, kwa aya hizi, Allah awatoe ambao wameamini na wakafanya matendo mema kutoka kwenye giza la upotevu na kuwapeleka kwenye nuru ya uongofu, na kutoka kwenye giza la ukafiri kwenda kwenye nuru ya imani.

(12) **MWENYEZI MUNGU AMBAYE AMEUMBA MBINGU SABA, NA KATIKA ARDHI MFANO WAKE**. Yaani: Na ameumba katika ardhi mfano wake, yaani: Ardhi saba. Na katika Hadithi sahihi iliyonukuliwa kwa Mtume kuna msisitizo wa hilo. Hiyo ni kauli ya Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) iliyokuja kueleza kwamba: *"Mwenye kudhulumu shubiri ya ardhi, ataviringishiwa shingoni kutokea ardhi saba"*. **AMRI INASHUKA BAINA YAO.** Yaani: Amri na hukumu zinashuka kutoka katika mbingu saba kwenda kwenye ardhi saba. Kwa hiyo, mvua inashuka (inanyesha) na mimea inaota. Analeta usiku na mchana, kusi na kaskazi.

أَسْكِنُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ سَكَنتُم مِّن وُجْدِكُمْ وَلَا تُضَآرُّوهُنَّ لِتُضَيِّقُوا۟
عَلَيْهِنَّ ۚ وَإِن كُنَّ أُو۟لَٰتِ حَمْلٍ فَأَنفِقُوا۟ عَلَيْهِنَّ حَتَّىٰ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ
فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَـَٔاتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۖ وَأْتَمِرُوا۟ بَيْنَكُم بِمَعْرُوفٍ ۖ وَإِن
تَعَاسَرْتُمْ فَسَتُرْضِعُ لَهُۥٓ أُخْرَىٰ ﴿٦﴾ لِيُنفِقْ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِۦ ۖ
وَمَن قُدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُۥ فَلْيُنفِقْ مِمَّآ ءَاتَىٰهُ ٱللَّهُ ۚ لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفْسًا
إِلَّا مَآ ءَاتَىٰهَا ۚ سَيَجْعَلُ ٱللَّهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ﴿٧﴾ وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ
عَتَتْ عَنْ أَمْرِ رَبِّهَا وَرُسُلِهِۦ فَحَاسَبْنَٰهَا حِسَابًا شَدِيدًا وَعَذَّبْنَٰهَا
عَذَابًا نُّكْرًا ﴿٨﴾ فَذَاقَتْ وَبَالَ أَمْرِهَا وَكَانَ عَٰقِبَةُ أَمْرِهَا خُسْرًا ﴿٩﴾
أَعَدَّ ٱللَّهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا ۖ فَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ يَٰٓأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ۚ
قَدْ أَنزَلَ ٱللَّهُ إِلَيْكُمْ ذِكْرًا ﴿١٠﴾ رَّسُولًا يَتْلُوا۟ عَلَيْكُمْ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ مُبَيِّنَٰتٍ
لِّيُخْرِجَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ مِنَ ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّورِ ۚ
وَمَن يُؤْمِنۢ بِٱللَّهِ وَيَعْمَلْ صَٰلِحًا يُدْخِلْهُ جَنَّٰتٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا
ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۖ قَدْ أَحْسَنَ ٱللَّهُ لَهُۥ رِزْقًا ﴿١١﴾ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَ
سَبْعَ سَمَٰوَٰتٍ وَمِنَ ٱلْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ ٱلْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوٓا۟ أَنَّ
ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ ٱللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَىْءٍ عِلْمًۢا ﴿١٢﴾

## SURATUT-TAHRIIM (66)

(1) **EWE MTUME, KWA NINI UNAHARAMISHA ALICHO KUHALALISHIA MWENYEZI MUNGU?** Imesemwa kuwa, *Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa akinywa asali kwa Bibi Zainabu binti Jahshi. Aisha na Hafsa wakala njama dhidi ya Zainabu kwamba wamwambie Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) pindi atakapokutana nao kuwa: 'Tunasikia harufu mbaya kutoka kwako'. Kwa sababu hiyo, Mtume akajiharamishia asali.* **UNATAFUTA KUWARIDHISHA WAKE ZAKO?** Kwa kujiharamishia katika nafsi yako kitu alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu?

**NA MWENYEZI MUNGU NI MWINGI WA KUSAMEHE, MWENYE KUREHEMU.** Mwingi wa msamaha kwa yale yaliyokutokea. Imesemwa kuwa: *Na hayo yalikuwa ni madhambi katika madhambi madogo, na ndio maana Mola wake amemlaumu kwa hilo.*

(2) **HAKIKA MWENYEZI MUNGU KAKUWEKEENI (SHERIA YA) KUFUNGUA VIAPO VYENU.** Yaani: Amekuwekeeni sheria ya kufungua viapo vyenu kwa kutoa Kafara,

سُورَةُ التَّحْرِيمِ
ترتيبها ٦٦ — آياتها ١٢

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَآ أَحَلَّ ٱللَّهُ لَكَ تَبْتَغِي مَرْضَاتَ أَزْوَٰجِكَ وَٱللَّهُ
غَفُورٌ رَّحِيمٌ ١ قَدْ فَرَضَ ٱللَّهُ لَكُمْ تَحِلَّةَ أَيْمَٰنِكُمْ وَٱللَّهُ مَوْلَىٰكُمْ
وَهُوَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ ٢ وَإِذْ أَسَرَّ ٱلنَّبِيُّ إِلَىٰ بَعْضِ أَزْوَٰجِهِۦ حَدِيثًا
فَلَمَّا نَبَّأَتْ بِهِۦ وَأَظْهَرَهُ ٱللَّهُ عَلَيْهِ عَرَّفَ بَعْضَهُۥ وَأَعْرَضَ عَنۢ بَعْضٍ
فَلَمَّا نَبَّأَهَا بِهِۦ قَالَتْ مَنْ أَنۢبَأَكَ هَٰذَا قَالَ نَبَّأَنِيَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْخَبِيرُ
٣ إِن تَتُوبَآ إِلَى ٱللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا وَإِن تَظَٰهَرَا عَلَيْهِ
فَإِنَّ ٱللَّهَ هُوَ مَوْلَىٰهُ وَجِبْرِيلُ وَصَٰلِحُ ٱلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ
بَعْدَ ذَٰلِكَ ظَهِيرٌ ٤ عَسَىٰ رَبُّهُۥٓ إِن طَلَّقَكُنَّ أَن يُبْدِلَهُۥٓ أَزْوَٰجًا
خَيْرًا مِّنكُنَّ مُسْلِمَٰتٍ مُّؤْمِنَٰتٍ قَٰنِتَٰتٍ تَٰٓئِبَٰتٍ عَٰبِدَٰتٍ سَٰٓئِحَٰتٍ
ثَيِّبَٰتٍ وَأَبْكَارًا ٥ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ قُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ
نَارًا وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَٰٓئِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ
لَّا يَعْصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ٦ يَٰٓأَيُّهَا
ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ لَا تَعْتَذِرُوا۟ ٱلْيَوْمَ إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ٧

kama ilivyokuja katika kauli ya Allah isemayo kuwa: *"…Basi Kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha familia zenu, au kuwapa mavazi, au kumkomboa mtumwa. Asiye pata hayo, basi afunge siku tatu…"*. **Sura Almaaida (5), aya 89**. Haifai kwa yeyote yule kuharamisha kitu alichokihalalisha Mwenyezi Mungu. Akifanya, haifungamani na haimlazimu aliyefanya kutekeleza, kwani kuharamisha na kuhalalisha ni miliki inayorejea kwa Allah Mtukufu tu. Lakini, ikiwa atafanya hivyo, baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa: Kama akijiharamishia katika nafsi yake kwa mfano nguo au chakula au kinywaji au chochote kile alichokiruhusu Allah (Subhaanahu wa Taala) hiyo inasimama nafasi ya kiapo. Akirejea kufanya alichojiharamishia, ni wajibu wake kutoa kafara ya Kiapo. Akitoa kafara wakati huo, Kiapo chake kitakuwa kimefunguka. Hukumu hii ni katika kila kitu hata kwa mke kama atakuwa amejiharimishia. Wanazuoni wengine wamesema kuwa: "Akijiharamishia mke na, kwa kuharamisha huko, akakusudia Talaka, basi Talaka itakuwa imepatikana. Mwenyezi Mungu ndiye ajuae zaidi.

**NA MWENYEZI MUNGU NDIYE MOLA WENU.** Yaani: Ni Mola wenu na ni mwenye kukunusuruni. **NA YEYE NI MWENYE KUJUA** Mwenye kujua yale ambayo yana manufaa yenu na mafanikio yenu. **MWENYE HEKIMA.** Katika matendo yake na kauli zake.

(3) **NA (KUMBUKA) WAKATI NABII ALIPO MWAMBIA MMOJA WA WAKE ZAKE HABARI YA SIRI.** Naye ni Hafsa, kama tulivyoeleza hapo nyuma. Mazungumzo yenyewe yanahusu kuharamisha asali. Alkuleibiy Amesema kuwa: *"Mtume alimwambia Hafsa kuwa: Baba yako na baba yake Aisha watakuwa makhalifa wangu kwa ummah wangu baada yangu"*. **BASI (YULE MKE) ALIPO LITANGAZA HILO** Yaani: Mtume alimueleza yale mazungumzo aliyoyatangaza **AKASEMA: NI NANI ALIYE KUAMBIA HAYA?** Yaani: Ni nani aliyekujulisha hayo? **MTUME AKASEMA: KANIAMBIA MJUZI, MWENYE KHABARI ZOTE.** Yaani: Aliyenipa habari za hayo ni Mwenyezi Mungu ambaye kwake hakijifichi kitu.

(4) **MKITUBU KWA MWENYEZI MUNGU, BASI NYOYO ZENU ZIMEKWISHA ELEKEA HUKO.** Maneno haya anaambiwa Bibi Aisha na Hafsa. Yaani: Kama mkitubu kwa Allah, basi mioyo yenu itaelekea katika kutubia na kuacha kusaidiana dhidi ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). **NA MKISAIDIANA DHIDI YAKE,** Yaani: Mkiungana na kusaidiana katika wivu wenu kwake na kufichua siri yake **BASI HAKIKA MWENYEZI MUNGU NDIYE KIPENZI CHAKE, NA JIBRILI, NA WAUMINI WEMA.** Yaani: Mwenyezi Mungu atasimamia kumnusuru. Pia Jibrili na waumini wema katika waja wake; kama vile Abubakar na Omar. Hatakosa wa kumnusuru. **NA MALAIKA BAADA YA HAYO** Baada ya kunusuriwa na Allah na baada ya nusura ya Jibrili na waumini wema **WATASAIDIA.** Watakuwa wasaidizi wanaomsaidia. Na imesemwa kuwa ushirikiano ulikuwa ni baina ya Aisha na Hafsa katika kumshinikiza Mtume katika suala la matumizi.

(5) **AKIKUPENI TALAKA, ASAA MOLA WAKE AKAMBADILISHIA WAKE (WENGINE), WALIO BORA ZAIDI KULIKO NYINYI.** Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaambiwa wake wa Mtume wake kuwa, kutokana na uwezo wake, lau kama Mtume akiwapa Talaka basi Mwenyezi Mungu atampa wake mbadala walio bora zaidi kuliko wao. Amefanya hivyo, kwa kuwatisha. **WAISLAMU, WAUMINI** Wanaotekeleza majukumu ya Uislamu, wanaomwamini Mwenyezi Mungu, Malaika wake, vitabu vyake na Mitume yake. **WATIIFU**

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ تُوبُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمْ
أَن يُكَفِّرَ عَنكُمْ سَيِّـَٔاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِى
مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ يَوْمَ لَا يُخْزِى ٱللَّهُ ٱلنَّبِىَّ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
مَعَهُۥ ۖ نُورُهُمْ يَسْعَىٰ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَٰنِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَآ
أَتْمِمْ لَنَا نُورَنَا وَٱغْفِرْ لَنَآ ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ٨
يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ جَٰهِدِ ٱلْكُفَّارَ وَٱلْمُنَٰفِقِينَ وَٱغْلُظْ عَلَيْهِمْ ۚ
وَمَأْوَىٰهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ ٱلْمَصِيرُ ٩ ضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلًا
لِّلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ٱمْرَأَتَ نُوحٍ وَٱمْرَأَتَ لُوطٍ ۖ كَانَتَا تَحْتَ
عَبْدَيْنِ مِنْ عِبَادِنَا صَٰلِحَيْنِ فَخَانَتَاهُمَا فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهُمَا
مِنَ ٱللَّهِ شَيْـًٔا وَقِيلَ ٱدْخُلَا ٱلنَّارَ مَعَ ٱلدَّٰخِلِينَ ١٠
وَضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱمْرَأَتَ فِرْعَوْنَ إِذْ
قَالَتْ رَبِّ ٱبْنِ لِى عِندَكَ بَيْتًا فِى ٱلْجَنَّةِ وَنَجِّنِى مِن فِرْعَوْنَ
وَعَمَلِهِۦ وَنَجِّنِى مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ١١ وَمَرْيَمَ ٱبْنَتَ
عِمْرَٰنَ ٱلَّتِىٓ أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهِ مِن رُّوحِنَا
وَصَدَّقَتْ بِكَلِمَٰتِ رَبِّهَا وَكُتُبِهِۦ وَكَانَتْ مِنَ ٱلْقَٰنِتِينَ ١٢

Watiifu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. **WENYE KUTUBU** Yaani: Wanaotubu dhambi. **WAFANYAO IBADA** Wanaomfanyia ibada Mwenyezi Mungu, wanyenyekevu kwake. **WANAOFUNGA (SAUMU) THAYIBU (WALIOWAHI KUOLEWA) NA BIKIRA.** Thayibu ni mwanamke aliyeolewa kisha mumewe akamtaliki au mwanamke aliyefiwa na mumewe. Ama bikira ni mwanamke ambaye hajawahi kuolewa.

(6) **ENYI MLIO AMINI, ZILINDENI NAFSI ZENU** Yaani: Zilindeni nafsi kwa kutenda aliyokuamrisheni Allah, na kuyaacha aliyokukatazeni. **NA FAMILIA ZENU** kwa kuwaamrisha kumtii Allah na kuwakataza wasimuasi. **DHIDI YA MOTO AMBAO KUNI ZAKE NI WATU NA MAWE.** Yaani: Moto mkubwa unaowaka kwa kutumia watu na mawe, kama unavyowaka moto mwingine kwa kutumia kuni. Ibnijariir amesema kuwa: *"Yatupasa tuwafundishe watoto wetu dini na kheri na maadili muhimu"*. **WANAUSIMAMIA MOTO HUO MALAIKA WAKALI, WENYE NGUVU.** Yaani: Motoni kuna Malaika wanaouhudumia, na kusimamia kuwaadhibu watu wa motoni. Ni wakali kwa watu wa motoni, hawana huruma nao wakiwaomba wawahurumie. Kwa hakika, wameumbwa ili kuadhibu tu. **HAWAMUASI MWENYEZI MUNGU KWA ANAYO WAAMRISHA.** Yaani: Hawaendi kinyume na maamrisho yake. **NA WANATENDA WANAYO AMRISHWA.** Yaani: Wanayafanya kwa wakati wake bila ya kuchelewa. Hawacheleweshi jambo na ilhali wana uwezo nalo. Hawashindwi na lolote vyovyote liwavyo.

(7) **ENYI MLIO KUFURU, MSILETE UDHURU LEO.** Yaani: Wataambiwa maneno haya wakati wa kuingizwa motoni, kwa lengo la kuwakatisha tamaa na kukata matumaini yao. **HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA MTALIPWA MLIYOKUWA MKIYATENDA.** Mtalipwa yale matendo yenu ya duniani.

(8) **ENYI MLIO AMINI, TUBUNI KWA MWENYEZI MUNGU TOBA NASAHA.** Toba Nasaha ni toba ya kweli. Na imesemwa kuwa ni Toba halisi. Toba Nasaha ni kujuta ndani ya moyo kwa madhambi yaliyotangulia, kuomba msamaha kwa kutamka, kuacha madhambi kwa vitendo na kuazimia kutoyarudia. **NURU YAO INAKWENDA MBELE YAO NA PANDE ZAO ZA KULIA.** Yaani: Nuru inakuwa pamoja nao wakati wa kutembea kwao katika Sirati.

(9) **EWE NABII, PAMBANA NA MAKAFIRI** Yaani: Pambana na makafiri kwa vita. **NA WANAFIKI** Kwa kuwahukumu kwa kuwa sheria za Allah. Walikuwa wakifanya yanayowajibisha hukumu hizo *(Haddi)*. Na tumia ukakamavu kwa makundi yote mawili (makafiri na wanafiki) ili uweke heshima.

(10) **WAKAWAFANYIA HIANA**. Imesemwa kuwa: Mke wa Nuhu alikuwa akiwaambia watu kuwa mumewe ni mwendawazimu. Na mke wa Luti alikuwa akiwapa habari watu wake kuhusu wageni wake. **HAWAKUWASAIDIA KITU KWA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Nuhu na Luti hawakuwafaa wake zao manufaa ya aina yoyote kwa sababu ya kuwa wao ni wake wa Mitume, wala hawakuweza kuzuia adhabu ya Allah pamoja na utukufu wao kwa Allah. **NA PAKASEMWA: INGIENI MOTONI PAMOJA NA WANAOINGIA.** Ingieni pamoja na wanaoingia humo; ambao ni makafiri na wafanyao maasi.

(11) **NA MWENYEZI MUNGU AMEWAPIGIA MFANO WALIO AMINI WA MKE WE FIRAUNI.** Yaani: Utawala wa ukafiri hautawadhuru kama ambavyo haukumdhuru mke wa Firauni. Alikuwa chini ya kafiri mkubwa zaidi wa makafiri, na kwa sababu ya imani yake akawa katika pepo yenye neema. **WAKATI ALIPOSEMA: EWE MOLA WANGU, NIJENGEE NYUMBA KWAKO PEPONI.**

ترتيبها ٦٧ — سُورَةُ المُلۡكِ — آياتها ٣٠

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

تَبَٰرَكَ ٱلَّذِي بِيَدِهِ ٱلۡمُلۡكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٌ ١ ٱلَّذِي خَلَقَ
ٱلۡمَوۡتَ وَٱلۡحَيَوٰةَ لِيَبۡلُوَكُمۡ أَيُّكُمۡ أَحۡسَنُ عَمَلٗاۚ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡغَفُورُ ٢
ٱلَّذِي خَلَقَ سَبۡعَ سَمَٰوَٰتٖ طِبَاقٗاۖ مَّا تَرَىٰ فِي خَلۡقِ ٱلرَّحۡمَٰنِ مِن
تَفَٰوُتٖۖ فَٱرۡجِعِ ٱلۡبَصَرَ هَلۡ تَرَىٰ مِن فُطُورٖ ٣ ثُمَّ ٱرۡجِعِ ٱلۡبَصَرَ كَرَّتَيۡنِ
يَنقَلِبۡ إِلَيۡكَ ٱلۡبَصَرُ خَاسِئٗا وَهُوَ حَسِيرٞ ٤ وَلَقَدۡ زَيَّنَّا ٱلسَّمَآءَ
ٱلدُّنۡيَا بِمَصَٰبِيحَ وَجَعَلۡنَٰهَا رُجُومٗا لِّلشَّيَٰطِينِۖ وَأَعۡتَدۡنَا لَهُمۡ عَذَابَ
ٱلسَّعِيرِ ٥ وَلِلَّذِينَ كَفَرُواْ بِرَبِّهِمۡ عَذَابُ جَهَنَّمَۖ وَبِئۡسَ ٱلۡمَصِيرُ
٦ إِذَآ أُلۡقُواْ فِيهَا سَمِعُواْ لَهَا شَهِيقٗا وَهِيَ تَفُورُ ٧ تَكَادُ تَمَيَّزُ
مِنَ ٱلۡغَيۡظِۖ كُلَّمَآ أُلۡقِيَ فِيهَا فَوۡجٞ سَأَلَهُمۡ خَزَنَتُهَآ أَلَمۡ يَأۡتِكُمۡ نَذِيرٞ ٨
قَالُواْ بَلَىٰ قَدۡ جَآءَنَا نَذِيرٞ فَكَذَّبۡنَا وَقُلۡنَا مَا نَزَّلَ ٱللَّهُ مِن شَيۡءٍ إِنۡ أَنتُمۡ
إِلَّا فِي ضَلَٰلٖ كَبِيرٖ ٩ وَقَالُواْ لَوۡ كُنَّا نَسۡمَعُ أَوۡ نَعۡقِلُ مَا كُنَّا فِيٓ أَصۡحَٰبِ
ٱلسَّعِيرِ ١٠ فَٱعۡتَرَفُواْ بِذَنۢبِهِمۡ فَسُحۡقٗا لِّأَصۡحَٰبِ ٱلسَّعِيرِ ١١
إِنَّ ٱلَّذِينَ يَخۡشَوۡنَ رَبَّهُم بِٱلۡغَيۡبِ لَهُم مَّغۡفِرَةٞ وَأَجۡرٞ كَبِيرٞ ١٢

Yaani: Nijengee nyumba karibu ya rehema zako katika sehemu yenye daraja la walio karibu nawe. **NA UNIOKOE NA FIRAUNI NA VITENDO VYAKE** Yaani: Niepushe naye na niepushe na vitendo vya uovu anavyo vifanya. **NA UNIOKOE NA WATU MADHALIMU.** Nao ni Waqibti makafiri.

(12) **NA MARIAMU BINTI WA IMRANI** Mwenyezi Mungu alimkusanyia baina ya utukufu wa duniani na Akhera, na akamchagua kuwa ni bora zaidi katika wanawake wa ulimwenguni, pamoja na kuwa alikuwa pamoja na watu wenye kufanya maasi. **ALILINDA UKE WAKE.** Yaani: Aliulinda usifanye mambo machafu. **TUKAPULIZA HUMO KATIKA ROHO YETU.** Hali hiyo ni kwamba Jibrili alipuliza katika shingo ya nguo yake, akashika mimba ya Issa. **AKASADIKISHA MANENO YA MOLA WAKE** Yaani: Akaziamini sheria zake alizowawekea waja wake, na pia aliamini yale maneno ambayo malaika alimwambia; nayo ni kauli ya Jibrili alipomwambia kwamba: *"Hakuna vingine isipokuwa kwamba mimi ni Mjumbe wa Mola wako"*. Pia aliamini maneno aliyoambiwa na malaika ya kubashiriwa kumzaa Issa na kwamba atakuwa Mtume miongoni mwa waliopewa ukaribu (na Allah). **NA VITABU VYAKE.** Navyo ni vitabu vilivyoteremshwa kwa Manabii. **NA ALIKUWA MIONGONI MWA WATIIFU.** Alikuwa miongoni mwa watu watiifu kwa Mola wao. Watu wake walikuwa wema na watiifu.

# SUURATUL MULK (67)

Imeteremka Makka Aya zake ni thalathini (30)

***Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.***

(1) **METUKUKA AMBAYE UKO MKONONI MWAKE UFALME** *"Ametukuka"* Yaani: Zimekuwa nyingi baraka za Mwenyezi Mungu na zimekuwa kubwa. Ufalme ni ufalme wa mbinguni na ardhini, duniani na akhera. **NA YEYE JUU YA KILA KITU NI MUWEZA** Hakimshindi kitu chochote. Yeye katika ufalme wake, anafanya atakavyo, ikiwa ni pamoja na kuneemesha na kuadhibu, kunyanyua (hadhi) na kuteremsha na kutoa na kunyima. Waumini wanalijua Jambo hili hapa duniani na makafiri wanalikana. Ama huko Akhera, hakuna yeyote atakayedai ufalme isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, na hapatakuwa na yeyote atakayekana ufalme wake. Kwa sababu hiyo, Mwenyezi Mungu amesema: "***Mwenye kumiliki Siku ya Malipo***" Suuratulfaatiha (1), aya 4. Pia amesema: "***Siku ambayo wao watadhihiri. Hapatafichika chochote kwao juu ya Mwenyezi Mungu. Ufalme leo ni wa nani? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu kubwa***". Suurat Ghaafir (40), aya 16.

(2) **AMBAYE AMEUMBA MAUTI NA UHAI** Mauti ni kukatika kwa uhusiano wa roho na mwili na kutengana nao. Uhai ni fungamano la roho na mwili na mawasiliano yake na mwili huo. Kwa hivyo, uhai unamaanisha Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu na kumuumbia roho mwanadamu huyo. **ILI AKUJARIBUNI; NI YUPI KATI YENU MZURI ZAIDI WA VITENDO** Yaani: Mwenyezi Mungu ameumba mauti na uhai; kwa maana kuwa amekufanyeni watu wenye akili ili akupeni majukumu kisha akujaribuni na kukulipeni juu ya hayo. Na makusudio ya msingi ya kujaribiwa ni kuonekana dhahiri ukamilifu wa uzuri wa watendao mazuri. **NA YEYE NI MWENYE KUSHINDA** Yaani: Ni mshindi ambaye hashindwi. **MWINGI WA KUSAMEHE** Kwa anayetubu na kurejea.

(3) **AMBAYE AMEUMBA MBIGU SABA KWA TABAKA** Yaani: Baadhi yake juu ya baadhi nyingine. **HUTAONA TOFAUTI YOYOTE KATIKA UUMBAJI WAKE MWINGI WA REHEMA** Hutaona tofauti ya

kupingana, kutofautiana, kupindapinda wala kukinzana. Mbingu hizo ziko sawasawa,zimenyooka zikiwa ni dalili ya Muumbaji wake. **BASI RUDISHA JICHO. JE, UTAONA UFA WOWOTE?** Yaani: Rudia kuelekeza jicho lako mbinguni na tazama kwa makini. Je, pamoja na ukubwa wake na upana wake, utaona humo mpasuko au ufa wowote?

(4) **HALAFU RUDIA KUANGALIA MARA MBILI** Yaani: Mara baada ya nyingine hata kama mara hizo zitakuwa nyingi. Kufanya hivyo, itakuwa jambo kubwa mno katika kusimamisha hoja na linalokata zaidi visingizio. **JICHO LITARUDI KWAKO LIKIWA DHALILI** Litakuwa dhalili, duni lililoshindwa kuona kasoro yoyote katika maumbile ya mbingu. **NA LIKIWA LIMEHEMEWA** Yaani: limenyon'gonyea, limetindikiwa.

(5) **NA KWA YAKINI KABISA, TUMEIPAMBA MBINGU YA KARIBU KWA TAA** Ikawa katika umbo zuri sana, sura kamilifu sana na mandhari ya kupendeza mno. Nyota zimeitwa taa kwa sababu zinatoa mwanga kama taa itoavyo mwanga. **NA TUKAZIFANYA VIPIGIO VYA MASHETANI** Yaani: Tumezifanya taa hizo vipigio ambavyo kwavyo Mashetani hupigwa. Hii ni faida nyingine mbali ya kuwa nyota hizo ni pambo la mbingu ya dunia. Qataada amesema kuwa: “*Mwenyezi Mungu ameumba nyota kwa ajili ya mambo matatu:* **1)** *Pambo la mbingu na* **2)** *Vipigio vya mashetani na* **3)** *Alama zitumikazo kuongoza katika bara na baharini*". **NA TUMEWAANDALIA ADHABU YA MOTO MKALI** Yaani: Na tumewaandalia mashetani huko akhera adhabu ya moto baada ya kuunguzwa duniani kwa vimondo.

(6) **NA WALE WALIOMKUFURU MOLA WAO** Ikiwa ni makafiri wa kibinadamu au makafiri wa makundi yote mawili; makafiri wa kijini na wa kibinadamu. **WATAPATA ADHABU YA JAHANAMU, NA MAREJEO MABAYA NI HAYO** Jahanam ndio marejeo watakayorejea.

(7) **WATAKAPOTUPWA HUMO** Yaani: Watakapotupwa humo kama kuni zinavyotupwa ndani ya moto **WATASIKIA MRINDIMO WAKE** Yaani: Watasikia sauti kama sauti ya punda mwanzo wa mlio wake. **NA ILHALI IKIWA INACHEMKA** Jahanamu itachemka wakiwemo humo kama kichemkavyo chungu.

(8) **INAKARIBIA KUPASUKA KUTOKANA NA HASIRA** Yaani: Jahanamu itakaribia kupasuka na kuachana sehemu moja na nyingine, kwa sababu ya ghadhabu zake juu ya makafiri. **KILA KUNDI LIKITUPWA HUMO** Kundi ni kundi la watu.au la majini **WALINZI WAKE** Ambao ni malaika **WATAWAULIZA** Swali la kusuta na kusimanga: **HIVI HAKUKUJIENI** Duniani **MUONYAJI YEYOTE?** Akikuhofisheni siku hii na kukutahadharisheni nayo?

(9) **WATASEMA: "HAPANA. KWA YAKINI, AMETUJIA MUONYAJI** Ametujia Mjumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mola wetu akatuonya, akatuhofisha na kutupa habari za siku hii. **NASI TUKAKADHIBISHA** Tukamkadhibisha muonyaji huyo **NA TUKASEMA: MWENYEZI MUNGU HAKUTEREMSHA KITU CHOCHOTE** Kupitia ndimi zenu ikiwa ni pamoja na mambo ya Ghaibu (mambo ya itikadi yasiyoonekana), habari za akhera na sheria ambazo zinakusanya ufafanuzi wa mambo anayoyataka Mwenyezi Mungu kwetu. **HAMKUWA NYINYI ISIPOKUWA TU MUMO KATIKA UPOTEVU MKUBWA"** Yaani: Tuliwaambia Mitume hao: Kwa hakika, nyinyi mko mbali na haki na mko mbali na yaliyo sawa sawa.

(10) **NA WAKASEMA: LAU TUNGELIKUWA TUNASIKIA AU TUNATUMIA AKILI, TUSINGELIKUWA KATIKA WATU WA MOTONI** Lau tungelikuwa tunasikia usikiaji wa anayezingatia, au tunatumia akili utumiaji akili wa mtu anayepambanua na kutafakari, tusingelikuwa miongoni mwa watu wa motoni. Bali tungelikuwa tumeyaamini yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na tungemfuata Mtume.

(11) **KWA HIYO, WAMEKIRI DHAMBI YAO** Ambayo kwayo wamestahiki adhabu ya moto. Dhambi hiyo ni kule kukufuru na kukadhibisha Mitume. **BASI NI UANGAMIVU KWA WATU WA MOTONI** Yaani: Wako mbali na Mwenyezi Mungu na rehema zake. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewalazimisha kupata adhabu baada ya kukiri kwao dhambi kwa sababu kwa njia hiyo itasimama hoja juu yao na hapatabakiwa na udhuru wowote.

(12) **KWA HAKIKA. WALE WANAO MUOGOPA MOLA WAO KWA GHAIBU** Yaani: Wanao ogopa adhabu yake na ilhali hawakumuona (kwa macho) na, kwa hiyo, wakamuamini kwa kuiogopa adhabu yake. **WATAPATA MSAMAHA** Mkubwa ambao kwa msamaha huo Mwenyezi Mungu atawasamehe madhambi yao. **NA MALIPO MAKUBWA** Nayo ni pepo.

(13) **NA ZISEMENI KWA SIRI KAULI ZENU AU ZITAMKENI DHAHIRI** Maana ni kwamba: Ikiwa mmeficha maneno yenu au mweyadhihirisha katika jambo la Mjumbe wa

وَأَسِرُّواْ قَوۡلَكُمۡ أَوِ ٱجۡهَرُواْ بِهِۦٓۖ إِنَّهُۥ عَلِيمُۢ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ ١٣ أَلَا
يَعۡلَمُ مَنۡ خَلَقَ وَهُوَ ٱللَّطِيفُ ٱلۡخَبِيرُ ١٤ هُوَ ٱلَّذِي جَعَلَ لَكُمُ
ٱلۡأَرۡضَ ذَلُولٗا فَٱمۡشُواْ فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُواْ مِن رِّزۡقِهِۦۖ وَإِلَيۡهِ ٱلنُّشُورُ
١٥ ءَأَمِنتُم مَّن فِي ٱلسَّمَآءِ أَن يَخۡسِفَ بِكُمُ ٱلۡأَرۡضَ فَإِذَا هِيَ
تَمُورُ ١٦ أَمۡ أَمِنتُم مَّن فِي ٱلسَّمَآءِ أَن يُرۡسِلَ عَلَيۡكُمۡ حَاصِبٗاۖ
فَسَتَعۡلَمُونَ كَيۡفَ نَذِيرِ ١٧ وَلَقَدۡ كَذَّبَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ فَكَيۡفَ
كَانَ نَكِيرِ ١٨ أَوَلَمۡ يَرَوۡاْ إِلَى ٱلطَّيۡرِ فَوۡقَهُمۡ صَٰٓفَّٰتٖ وَيَقۡبِضۡنَۚ مَا
يُمۡسِكُهُنَّ إِلَّا ٱلرَّحۡمَٰنُۚ إِنَّهُۥ بِكُلِّ شَيۡءِۭ بَصِيرٌ ١٩ أَمَّنۡ هَٰذَا ٱلَّذِي
هُوَ جُندٞ لَّكُمۡ يَنصُرُكُم مِّن دُونِ ٱلرَّحۡمَٰنِۚ إِنِ ٱلۡكَٰفِرُونَ إِلَّا فِي غُرُورٍ
٢٠ أَمَّنۡ هَٰذَا ٱلَّذِي يَرۡزُقُكُمۡ إِنۡ أَمۡسَكَ رِزۡقَهُۥۚ بَل لَّجُّواْ فِي عُتُوّٖ
وَنُفُورٍ ٢١ أَفَمَن يَمۡشِي مُكِبًّا عَلَىٰ وَجۡهِهِۦٓ أَهۡدَىٰٓ أَمَّن يَمۡشِي سَوِيًّا
عَلَىٰ صِرَٰطٖ مُّسۡتَقِيمٖ ٢٢ قُلۡ هُوَ ٱلَّذِيٓ أَنشَأَكُمۡ وَجَعَلَ لَكُمُ ٱلسَّمۡعَ
وَٱلۡأَبۡصَٰرَ وَٱلۡأَفۡـِٔدَةَۚ قَلِيلٗا مَّا تَشۡكُرُونَ ٢٣ قُلۡ هُوَ ٱلَّذِي ذَرَأَكُمۡ
فِي ٱلۡأَرۡضِ وَإِلَيۡهِ تُحۡشَرُونَ ٢٤ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَٰذَا ٱلۡوَعۡدُ إِن كُنتُمۡ
صَٰدِقِينَ ٢٥ قُلۡ إِنَّمَا ٱلۡعِلۡمُ عِندَ ٱللَّهِ وَإِنَّمَآ أَنَا۠ نَذِيرٞ مُّبِينٞ ٢٦

Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu anayajua yote hayo. Katika hayo, hakuna chochote cha kujificha kinachofichika kwake. **KWA YAKINI, YEYE NI MJUZI ZAIDI WA YALIYOMO KATIKA NYOYO** Yaliyomo katika nyoyo ni yale yaliyofichwa na nyoyo.

(14) **OH! HIVI ASIJUE YULE ALIYEUMBA?** Hivi asizijue siri na dhamira za nyoyo yule aliyeumba hayo na kuunda? Yeye aliyetukuka ndiye aliyemuumba binadamu kwa mkono wake. Mjuzi zaidi wa kilichotengenezwa ni yule mtengenezaji wake. **NA ILHALI YEYE NI MJUZI, MWELEWA?** Ambaye ujuzi wake unayafikia yaliyomo ndani ya nyoyo, na ni Mwelewa wa mambo ambayo nyoyo zinayaficha na kuyadhamiria. Katika hayo, hapana lolote la kujificha linalofichikana kwake.

(15) **YEYE NDIYE AMBAYE AMEKUUMBIENI NYINYI ARDHI IKIWA DHALILI** Yaani: Amekufanyieni ardhi kuwa sahali, laini, mnatulia juu yake. Hakuifanya ngumu kiasi kwamba msiweze kukaa humo na kutembea juu yake. **BASI TEMBEENI KATIKA PANDE ZAKE** Tembeeni katika njia zake, kingo zake na pembezoni mwake. **NA KULENI KATIKA RIZIKI ZAKE** Yaani: Kuleni katika vile alivyokuruzukuni na kuviumba katika ardhi kwa ajili yenu. Mwenyezi Mungu anajifakharisha kwa wanadamu kwa kule kuwawezesha kuitumia hii ardhi, na kuwapa uwezo wa kujipatia kheri zake. Lakini ni wajibu kwa wanadamu kujua kwamba wao watarejea kwake. Kwa sababu hiyo, ndipo Mwenyezi Mungu akasema: **NA NI KWAKE YEYE TU KUFUFULIWA** Yaani: Kufufuliwa kutoka makaburini mwenu. Ni kwake yeye tu si kwa mwengine.

(16) **HIVI MNADHANI MKO SALAMA NA ALIYEKO MBINGUNI?** Huyo ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. **KUKUDIDIMIZENI ARDHINI?** Akaing'oa mkiwemo juu yake kama alivyofanya kwa Karuni baada ya kuwa ameifanya sahali mkitembea katika pande zake? **TAHAMAKI IKAWA INAYUMBA?** Yaani: Inatetemeka na kutingishika kinyume kabisa na utulivu udhalili iliyokuwa nao?

(17) **AU HIVI MNADHANI MKO SALAMA NA YULE ALIYEKO MBINGUNI KUKUANGUSHIENI MAWE?** Mawe kutoka mbinguni kama alivyowaangushia watu wa Luti na wale watu wa ndovu. Yasemekana kuwa (kitacho shushwa) ni upepo ambao ndani yake mna mawe. **HIVI PUNDE MTAJUA; UKOJE UONYAJI WANGU** Yaani: Mtajua ukoje uonyaji wangu pale mtakopoiona kwa macho adhabu, na kujua huku hakutakusaidieni.

(18) **NA KWA HAKIKA, WALIKADHIBISHA WALE WALIOKUWA KABLA YAO. BASI KULIKUWAJE KUKEMEA KWANGU?** Yaani: Kulikuwaje kuwakemea kwangu kwa adhabu mbaya niliyowapa?

(19) **HIVI HAWAKUWAANGALIA NDEGE JUU YAO WAKIWA WAMEJIPANGA KWA MISTARI** Wamenyoosha mbawa zao katika anga na wanazikunjua wakati wa kuruka kwao. **NA HUZIKUNJA** Yaani: Huzikunja mbawa zao. **HAKUNA AWAZUIAYE** Huko angani wakati wa kuruka, kukunja na kukunjua (mbawa zao) **ISIPOKUWA MWINGI WA REHEMA** Mwenye uwezo juu ya kila kitu. Yaani: Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwazuia wasianguke kwa sababu ya ustadi wa kuumba, wepesi wa miili yao na kuivalisha manyoya na kuyakunjua kwa namna maalum; mambo ambayo Mwenyezi Mungu ameyajaalia katika ndege! Manyoya yakipigwa hewani, ndege huruka na kwenda mbele. Ametakasika Muumba wake! **KWA YAKINI, YEYE NI MJUZI WA KILA KITU** Hakijifichi kitu chochote kwake.

(20) **AU NI LIPI HILI AMBALO NI JESHI LENU LITAKALO KUNUSURUNI BADALA YA MWINGI WA REHEMA?** Maana ni kwamba:

Nyinyi hamna jeshi lolote litakalo kuzuieni msipate adhabu ya Mwenyezi Mungu. Ni dhalili yupi huyu ambaye, katika madai yenu, ni jeshi lenu litakalosimamia kukunusuruni kama Mwenyezi Mungu hatakunusuruni kwa rehema zake na msaada wake? **HAWAKUWA MAKAFIRI ISIPOKUWA KWAMBA WAMO KATIKA KUDANGANYIKA TU** Kudanganyika kukubwa kunakotokana na shetani anaye wadanganya.

(21) **AU NI NANI HUYU AMBAYE ATAKURUZUKUNI IKIWA ATAZUIA RIZIKI ZAKE?** Yaani: Ni nani atakaye kumiminieni riziki, ikiwemo mvua na nyinginezo, ikiwa Mwenyezi Mungu atayazuia hayo na akakunyimeni? **BALI WAMEZAMA KATIKA UASI NA KIBURI** Wamezama kabisa katika kukaidi na kuifanyia kiburi haki. Hawakuzingatia wala kutafakari!

(22) **HIVI AMBAYE ANATEMBEA HUKU AKIINAMIA USONI MWAKE NDIYE MUONGOFU ZAIDI?** Huyo ni kafiri. Anazama katika kumuasi Mwenyezi Mungu duniani. Mwenyezi Mungu atamfufua siku ya Kiyama akiwa ameinamia uso wake. **AU NI YULE ANAYETEMBEA AKIWA SAWASAWA?** Amelingana sawa akiangalia mbele yake? **AKIWA YUKO KATIKA NJIA ILIYONYOOKA?** Yaani: Akiwa katika njia iliyo nyooka, isiyokuwa na kupindapinda wala konakona. Huyo ni Muislamu ambaye amekuwa akiishi duniani katika mfumo wa Mwenyezi Mungu akiwa katika wongofu na utambuzi. Atafufuliwa huko akhera akiwa sawasawa, akiwa katika njia iliyo nyooka na itakayompeleka peponi.

(23) **WAAMBIE: YEYE NDIYE ALIYEKUUMBENI NYINYI MWANZO** Mwenyezi Mungu aliyetakasika amemuamuru Mjumbe wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani,awaambie kwamba Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaumba umbo la kwanza. **NA AKAKUUMBIENI** Akawaumbia wao **MASIKIO** Ili kwayo wasikie. **NA MACHO** Ili kwayo waone. **NA MIOYO** Nayo ni mioyo ambayo kwayo wanatafakari katika viumbe vya Mwenyezi Mungu. **MNASHUKURU KIDOGO MNO** Yaani: Nyinyi hamumshukuru Mola wa neema hizi kwa kumpwekesha yeye, isipokuwa shukrani chache mno.

(24) **WAAMBIE: YEYE NDIYE AMBAYE AMEKUUMBENI KATIKA ARDHI** Amewaumba katika ardhi, akawatawanya humo na kuwasambaza juu ya mgongo wake. **NA KWAKE YEYE TU MTAKUSANYWA** Sio kwa mwengine yeyote.

(25) **NA WANASEMA: ITAKUWA LINI AHADI HII?** Ya kukusanywa, Kiyama, moto na adhabu ambayo mnatutajia. **IKIWA NYINYI NI WAKWELI?** Katika hilo. Basi tuambieni au tubainishieni au tuleteeni.

(26) **WAAMBIE: HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA UJUZI UKO KWA MWENYEZI MUNGU TU** Yaani: Kujua wakati hasa wa kusimama Kiyama kuko kwa Mwenyezi Mungu. Hapana ajuae isipokuwa yeye tu. **NA HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA MIMI NI MUONYAJI TU NINAYEBAINISHA** Ninakuonyeni na kukugopesheni hatima ya ukafiri wenu, na ninakubainishieni yale aliyoniamuru Mwenyezi Mungu kuyabainisha. Kamwe hakuniamuru nikufahamisheni wakati wa kusimama (kutokea) kwa Kiyama.

(27) **WAKATI WATAKAPOIONA IPO KARIBU** Watakapoiona adhabu ipo karibu **ZITAKUWA MBAYA NYUSO ZA WALE WALIOKUFURU** Yaani: Zitakuwa nyeusi, zitajawa na huzuni na kufunikwa na unyonge. **NA PATASEMWA: HAYA NDIO YALE MLIYOKUWA MNAYADAI** Yaani: Haya ndio ambayo mlikuwa mkiyaomba duniani kwa istihzai na kutaka yaje haraka!

(28) **WAAMBIE: HIVI MWAONAJE IWAPO MWENYEZI MUNGU ATANIANGAMIZA MIMI** Kwa kifo au kuuawa kama mnavyonitamania mimi hayo na kungojelea inifike misiba na maafa. **NA WALIOPO PAMOJA NAMI** Miongoni mwa waumini. **AU AKITUREHEMU,** Kwa kuyachelewesha hayo kwa muda. Kama ikikadiriwa kututokea hayo, **BASI NI NANI ATAKAYEWAOKOA MAKAFIRI NA ADHABU IUMIZAYO?** Yaani: Hakuna yeyote wa kuwaokoa na hayo; sawa Mwenyezi Mungu atamuangamiza Mjumbe wake pamoja na wauminiu walioko naye kama makafiri walivyokuwa wanatamani au ataahirisha kuwaangamiza.

(29) **WAAMBIE: YEYE NI MWINGI WA REHEMA. TUMEMWAMINI** Yeye peke yake. Hatumshirikishi na kitu chochote. **NA YEYE TU TUMEMTEGEMEA** Si kwa yeyote mwengine. Kutegemea ni kuyaegemeza mambo yote kwake yeye mwenye kushinda na kutukuka. **BASI PUNDE TU MTAJUA NI NANI HASA YUKO KATIKA UPOTEVU WA DHAHIRI** Kati ya sisi na nyinyi.

(30) **WAAMBIE: JE, MNAONAJE KAMA MAJI YENU YATAKUWA YAMEZAMA** Yaani: Niambieni; ikiwa maji yenu ambayo Mwenyezi Mungu amekuneemesheni katika chemchem, visima na mito yatakuwa yamedidimia chini ya ardhi kwa namna ambayo

فَلَمَّا رَأَوۡهُ زُلۡفَةٗ سِيٓـَٔتۡ وُجُوهُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَقِيلَ هَٰذَا ٱلَّذِي
كُنتُم بِهِۦ تَدَّعُونَ ﴿٢٧﴾ قُلۡ أَرَءَيۡتُمۡ إِنۡ أَهۡلَكَنِيَ ٱللَّهُ وَمَن مَّعِيَ
أَوۡ رَحِمَنَا فَمَن يُجِيرُ ٱلۡكَٰفِرِينَ مِنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ ﴿٢٨﴾ قُلۡ هُوَ
ٱلرَّحۡمَٰنُ ءَامَنَّا بِهِۦ وَعَلَيۡهِ تَوَكَّلۡنَاۖ فَسَتَعۡلَمُونَ مَنۡ هُوَ فِي ضَلَٰلٖ مُّبِينٖ
﴿٢٩﴾ قُلۡ أَرَءَيۡتُمۡ إِنۡ أَصۡبَحَ مَآؤُكُمۡ غَوۡرٗا فَمَن يَأۡتِيكُم بِمَآءٖ مَّعِينِۭ ﴿٣٠﴾

ترتيبها ٦٨ — سُورَةُ القَلَمِ — آياتها ٥٢

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

نٓۚ وَٱلۡقَلَمِ وَمَا يَسۡطُرُونَ ﴿١﴾ مَآ أَنتَ بِنِعۡمَةِ رَبِّكَ بِمَجۡنُونٖ ﴿٢﴾
وَإِنَّ لَكَ لَأَجۡرًا غَيۡرَ مَمۡنُونٖ ﴿٣﴾ وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٖ ﴿٤﴾
فَسَتُبۡصِرُ وَيُبۡصِرُونَ ﴿٥﴾ بِأَييِّكُمُ ٱلۡمَفۡتُونُ ﴿٦﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ
أَعۡلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦ وَهُوَ أَعۡلَمُ بِٱلۡمُهۡتَدِينَ ﴿٧﴾ فَلَا تُطِعِ
ٱلۡمُكَذِّبِينَ ﴿٨﴾ وَدُّواْ لَوۡ تُدۡهِنُ فَيُدۡهِنُونَ ﴿٩﴾ وَلَا تُطِعۡ كُلَّ
حَلَّافٖ مَّهِينٍ ﴿١٠﴾ هَمَّازٖ مَّشَّآءِۭ بِنَمِيمٖ ﴿١١﴾ مَّنَّاعٖ لِّلۡخَيۡرِ مُعۡتَدٍ
أَثِيمٍ ﴿١٢﴾ عُتُلِّۭ بَعۡدَ ذَٰلِكَ زَنِيمٍ ﴿١٣﴾ أَن كَانَ ذَا مَالٖ وَبَنِينَ
﴿١٤﴾ إِذَا تُتۡلَىٰ عَلَيۡهِ ءَايَٰتُنَا قَالَ أَسَٰطِيرُ ٱلۡأَوَّلِينَ ﴿١٥﴾

hayakubaki kabisa humo, au yakawa yamekwenda mahala mbali katika ardhi kiasi kwamba ndoo haziwezi kuyafikia, **BASI NI NANI ATAKAYE KULETEENI MAJI YATIRIRIKAYO?** Yaani: Maji mengi, yapitayo, yasiyokwisha? Yaani: Hakuna yeyote atakayekuleteeni isipokuwa Mwenyezi Mungu tu aliyetukuka, atakayekuleteeni mvua na mito mpaka mkaneemeka kwazo.

## SUURATUL QALAM (68)

Imeteremka Makka Aya zake ni

hamsini na mbili (52)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

(1) **NUUN** Ni moja katika herufi za kuundia maneno, kama vyanzo vingine vilivyopo katika mwanzo wa sura zilizoanzwa kwa herufi hizo. **NA KWA KALAMU** Mwenyezi Mungu ameapa kwa kalamu kwa sababu ubainifu uliopo katika kalamu. Ubainifu unapatikana katika kila kalamu inayotumika katika kuandika. **NA YALE WANAYOYAANDIKA** Yaani: Elimu ambazo watu wanaziandika kwa kalamu.

(2) **WEWE, KWA NEEMA ZA MOLA WAKO, SIO MWENDAWAZIMU** Yaani: Kwa yakini, wewe Muhamad, kwa neema za Mwenyezi Mungu ambazo amekuneemesha na ambazo ni Utume na Uongozi kwa jumla, umeepukana kabisa na uwendawazimu.

(3) **NA KWA YAKINI WEWE UNAYO MALIPO** Yaani: Unazo thawabu kutokana na majukumu mazito ya Utume uliyoyabeba na aina mbali mbali za shida ulizopambana nazo. **YASIYO KATIKA** Yaani: Malipo yasiyokuwa na mwisho au ambayo watu hawatakusimbulia.

(4) **NA KWA YAKINI, WEWE UKO JUU YA TABIA** Maana ni kwamba: Wewe uko katika tabia zile alizokuamuru Mwenyezi Mungu katika Qur'ani. Imethibiti katika Sahihi ikinukuliwa kutoka kwa Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba aliulizwa kuhusu tabia za Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani: akasema:
*"Tabia zake zilikuwa ni Qur'ani".*

(5) **BASI HIVI KARIBU TU UTAONA NA WATAONA** Yaani: Utaona ewe Muhamad, na makafiri nao wataona haki itakapodhihiri na pazia kufunuka. Hiyo ni siku ya Kiyama.

(6) **NI NANI MIONGONI MWENU MWENYE KUTAHINIWA?** Yaani: Ni nani miongozi mwenu aliyepewa mtihani wa (ugonjwa wa) wazimu. Hayo ni majibu ya madai yao kwamba Muhamad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa mwenye kufitiniwa, mpotevu. Kwa sababu hiyo, ndipo Mwenyezi Mungu akasema:

(7) **KWA YAKINI, MOLA WAKO NI MJUZI ZAIDI WA ALIYEIPOTEA NJIA YAKE** Yaani: Mwenyezi Mungu anajua ni nani hasa aliyepotea; ni wewe au ni yule aliyekutuhumu wewe kwa upotevu? Maana ni kwamba wao ndio wapotevu, kwa sababu ya kupinga kwao yale ambayo yana manufaa kwao duniani na akhera na kuchagua kwao yale ambayo ndani yake mna madhara yao duniani na akhera. **NA YEYE NI MJUZI ZAIDI WA WALIO ONGOKA** Anawajua zaidi waliyoongoka kwenye njia yake inayofikisha kwenye furaha ya sasa hivi (duniani) na ya baadae (akhera).

(8) **BASI USIWATII WAKADHIBISHAO** Mwenyezi Mungu amemkataza Mtume wake kuwalainikia Washirkina. Na hao ni wale viongozi wa makafiri wa Makka, kwa sababu wao walikuwa wanamlingania (wanamhubiria) Mtume kwenye dini ya baba zake, ndipo Mwenyezi Mungu akamkataza kuwatii.

(9) **WAMETAMANI LAU UNGELAINIKA, NAO WALAINIKE** Maana ni kwamba: Wametamani lau ungelikuwa laini kwao, na wao

wakawa laini kwako. Imesemwa pia kwamba maana ni kuwa: Wametamani lau ungeliwafuata na kuiacha haki uliyonayo. Wao wanakupaka mafuta; kwa maana ya kuwa wanakuonesha ulaini ili uwe pamoja nao.

(10) **NA USIMTII KILA MUAPAJI SANA** Yaani: Usimtii mwenye kuapa sana kwa batili. **MPUUZI** Ni duni.

(11) **FEDHULI, MTEMBEZAJI SANA FITINA** *"Hammaaz*" Fedhuli" ni mtu anayewataja watu kwa ubaya mbele yao. *"Lammaaz*" Msengenyaji" ni mtu anayewataja watu wakiwa hawapo. *"Mash-shaain-binamiim"* Mtembezaji sana fitina ni mtu anayetembeza uchochezi kati ya watu ili aharibu uhusiano uliopo kati yao.

(12) **MZUIAJI SANA WA KHERI, MWENYE KUVUKA MIPAKA, MWINGI WA MADHAMBI** Yaani: Bahili wa kutoa mali, hana ukarimu, ni mwenye kuvuka mipaka aliyowekewa na Mwenyezi Mungu; iwe ni amri au makatazo, ni mwingi wa kutenda maasi yanayompa wingi wa madhambi.

kwa jeuri na utovu wa adabu: Haya si chochote ila tu ni visa na simulizi ambazo ziliandikwa katika vitabu vya watu wa kale na sio maneno ya Mwenyezi Mungu.

(13) **MWENYE ROHO NGUMU,(NA)JUU YA HAYO (HANA NAFUU HATA CHEMBE) KAMA KITU KILICHOPACHIKWA KISIPACHIKIKE VIZURI.** Yaani**:**Yeye pamoja na kasoro na aibu zake zilizo tajwa pia ni mtoto wa zinaa.

(14) **KWA AJILI YA KUWA NI MWENYE MALI NA WATOTO(NDIO ANAFANYA KIBURI)** Yaani**:**usimtii kwa sababu ya malizake na watoto wake.

(15) **ANAPOSOMEWA AYA ZETU ANASEMA"(HIZI)NI SIMULIZI ZA UONGO ZA WATU WA ZAMANI."**

(16) **PUNDE TUTAMTIA ALAMA JUU YA PUA** Yaani: Hivi punde tu tutamtia alama (kovu) nyeusi juu ya pua. Hiyo ni kwamba uso wake utafanywa uwe mweusi kwa moto kabla ya kuingia motoni na, kwa hiyo, atakuwa na alama juu ya pua yake, na tutampachika kitu ambacho hakimtoki na atajulikana kwa alama hiyo.

(17) **KWA HAKIKA, SISI TUMEWAPA MTIHANI** Yaani: Makafiri wa Makka. Mwenyezi Mungu amewapa mtihani wa njaa na ukame kwa apizo la Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwao. **KAMA TULIVYOWAPA MTIHANI WENYE SHAMBA** Ambao habari zao zinajulikana kwa WaquraishI. Habari hiyo ni kwamba: Katika ardhi ya Yemen kiasi cha umbali wa Farsakhi mbili kutoka Sanaa, palikuwepo na shamba la mtu mmoja aliyekuwa akitekeleza haki ya Mwenyezi Mungu katika shamba hilo. Yule mtu akafa na shamba likawa la watoto wake. Wale watoto wakawanyima watu kheri zake, wakaionea ubahili haki ya Mwenyezi Mungu katika shamba hilo na kusema: "Mali ni kidogo na watoto ni wengi na hutuwezi kufanya kama alivyokuwa akifanya baba yetu". Wakaazimia kuwanyima masikini. Hatima yao ikawa vile alivyohadithia Mwenyezi Mungu katika kitabu chake: **WAKATI WALIPOAPA KWAMBA WATAVUNA SHAMBA HILO WAKATI WA ASUBUHI** Yaani: Waliapa kwamba wao watavuna mazao yake wakati wa asubuhi.

(18) **NA HAWAKUCHOMOA** Yaani: Na hawakusema *Inshaa-Allah* "Akipenda Mwenyezi Mungu". Imesemwa pia kuwa maana ni kwamba hawakuwachomolea masikini katika jumla ya kile kiasi ambacho baba yao alikuwa akikitoa kuwapa masikini hao.

(19) **KWA HIYO, LIKALIZUNGUKA SHAMBA HILO JANGA LINALOZUNGUKA KUTOKA KWA MOLA WAKO NA ILHALI WAO WAMELALA** Yaani: Ulilizingira shamba hilo moto kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ulioliunguza mpaka likawa jeusi.

(20) **HIVYO, LIKAWA KAMA LENYE KUVUNWA** Yaani: Kama shamba ambalo matunda yake yameshavunwa; yaani yamekatwa.

(21) **BASI WAKAITANA WAKATI WA ASUBUHI** Walipofika asubuhi, walisema baadhi yao kuwaambia wengine:

(22) **KWAMBA: WAHINI ASUBUHI KWENDA SHAMBANI KWENU** Tokeni mapema asubui kwenda kwenye matunda na mimea. **IKIWA NYINYI NI WAVUNAJI** Yaani: Ikiwa mnakusudia kuvuna.

(23) **WAKAONDOKA NA ILHALI WANANON'GONEZANA** Yaani: Wakatoka huku wakisemezena kwa siri:

(24) **KWAMBA: KAMWE ASIINGIE SHAMBANI KWENU LEO HII MASIKINI YEYOTE** Baadhi yao wakiwaambia kwa siri baadhi nyingine maneno haya; nayo ni kauli yao: "Asiingie shambani mwenu humu leo hii masikini yeyote akikuombeni mumpe kutoka humo kile alichokuwa baba yenu akimpa".

(25) **WAKATOKA ASUBUHI PEKE YAO** Yaani: Wakatoka peke yao wakiwa wamewaacha watu wao bila ya kuchanganyika nao. **WAKIDHANI KUWA WANA UWEZO** Wakadhani katika nafsi zao kuwa wanao uwezo juu ya shamaba lao.

(26) **WALIPOLIONA, WAKASEMA: HAKIKA, SISI TUMEPOTEA** Yaani: Baadhi yao wakawaambia wengine: Tumepotea njia ya

سَنَسِمُهُۥ عَلَى ٱلْخُرْطُومِ ﴿١٦﴾ إِنَّا بَلَوْنَـٰهُمْ كَمَا بَلَوْنَآ أَصْحَـٰبَ ٱلْجَنَّةِ إِذْ أَقْسَمُوا۟
لَيَصْرِمُنَّهَا مُصْبِحِينَ ﴿١٧﴾ وَلَا يَسْتَثْنُونَ ﴿١٨﴾ فَطَافَ عَلَيْهَا طَآئِفٌ مِّن رَّبِّكَ
وَهُمْ نَآئِمُونَ ﴿١٩﴾ فَأَصْبَحَتْ كَٱلصَّرِيمِ ﴿٢٠﴾ فَتَنَادَوْا۟ مُصْبِحِينَ ﴿٢١﴾ أَنِ
ٱغْدُوا۟ عَلَىٰ حَرْثِكُمْ إِن كُنتُمْ صَـٰرِمِينَ ﴿٢٢﴾ فَٱنطَلَقُوا۟ وَهُمْ يَتَخَـٰفَتُونَ ﴿٢٣﴾
أَن لَّا يَدْخُلَنَّهَا ٱلْيَوْمَ عَلَيْكُم مِّسْكِينٌ ﴿٢٤﴾ وَغَدَوْا۟ عَلَىٰ حَرْدٍ قَـٰدِرِينَ ﴿٢٥﴾ فَلَمَّا
رَأَوْهَا قَالُوٓا۟ إِنَّا لَضَآلُّونَ ﴿٢٦﴾ بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ﴿٢٧﴾ قَالَ أَوْسَطُهُمْ أَلَمْ أَقُل
لَّكُمْ لَوْلَا تُسَبِّحُونَ ﴿٢٨﴾ قَالُوا۟ سُبْحَـٰنَ رَبِّنَآ إِنَّا كُنَّا ظَـٰلِمِينَ ﴿٢٩﴾ فَأَقْبَلَ
بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَلَـٰوَمُونَ ﴿٣٠﴾ قَالُوا۟ يَـٰوَيْلَنَآ إِنَّا كُنَّا طَـٰغِينَ ﴿٣١﴾ عَسَىٰ
رَبُّنَآ أَن يُبْدِلَنَا خَيْرًا مِّنْهَآ إِنَّآ إِلَىٰ رَبِّنَا رَٰغِبُونَ ﴿٣٢﴾ كَذَٰلِكَ ٱلْعَذَابُ ۖ وَلَعَذَابُ
ٱلْـَٔاخِرَةِ أَكْبَرُ ۚ لَوْ كَانُوا۟ يَعْلَمُونَ ﴿٣٣﴾ إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ عِندَ رَبِّهِمْ جَنَّـٰتِ ٱلنَّعِيمِ
﴿٣٤﴾ أَفَنَجْعَلُ ٱلْمُسْلِمِينَ كَٱلْمُجْرِمِينَ ﴿٣٥﴾ مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٣٦﴾ أَمْ
لَكُمْ كِتَـٰبٌ فِيهِ تَدْرُسُونَ ﴿٣٧﴾ إِنَّ لَكُمْ فِيهِ لَمَا تَخَيَّرُونَ ﴿٣٨﴾ أَمْ لَكُمْ أَيْمَـٰنٌ
عَلَيْنَا بَـٰلِغَةٌ إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَـٰمَةِ ۙ إِنَّ لَكُمْ لَمَا تَحْكُمُونَ ﴿٣٩﴾ سَلْهُمْ أَيُّهُم
بِذَٰلِكَ زَعِيمٌ ﴿٤٠﴾ أَمْ لَهُمْ شُرَكَآءُ فَلْيَأْتُوا۟ بِشُرَكَآئِهِمْ إِن كَانُوا۟ صَـٰدِقِينَ ﴿٤١﴾
يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى ٱلسُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٤٢﴾

shamba letu na silo hili. Halafu walipotafakari na kujua kwamba lile ndilo hasa shamba lao, na kwamba Mwenyezi Mungu aliyetakasika amewaadhibu wao kwa kuyaondoa matunda na mimea iliyokuwemo shambani humo, walisema:

(27) **BALI SISI TUMEPOKONYWA** Yaani: Mwenyezi Mungu ametupokonya matunda ya shamba letu kwa sababu ya azma tuliyoifanya ya kuwazuia masikini wasipate kheri za shamba.

(28) **AKASEMA MBORA WAO ZAIDI:** Yaani: Akasema yule mbora wao zaidi na mwenye busara zaidi katika wao kwamba: **JE, SIKUKUAMBIENI KWAMBA MTAKASE?** Yaani: Je, sikukuambieni kwamba kitendo chenu hiki cha kuzuia haki ya masikini ni dhuluma? Kwa nini basi msimtakase Mwenyezi Mungu hivi sasa baada ya kuwa mmebaini kuwa yeye yuko katika kuwavizia madhalimu na mkamuomba msamaha kwa matendo yenu na mkatubu kwake kwa nia hii mliyoiazimia?

(29) **WAKASEMA: UTAKASIFU NI WA MOLA WETU. KWA HAKIKA, SISI TULIKUWA MADHALIMU** Yaani: Mola wetu ametakasika kuwa dhalimu katika yale aliyoyafanya kwenye shamba letu. Kwa hakika, hayo ni kwa sababu ya dhambi yetu tuliyoifanya katika kuwazuia kwetu wale masikini.

(30) **BAADHI YAO WAKAWAELEKEA BAADHI WAKIWA WANALAUMIANA** Yaani: Wanalaumiana wao kwa wao kwa kupeana ushauri mbaya uliopelekea kuwafika yaliyowafika.

(31) **WAKASEMA: EE! OLE WETU. KWA HAKIKA, SISI TULIKUWA WENYE KUPINDUKIA MIPAKA** Yaani: Sisi tulivuka mipaka aliyoiweka Mwenyezi Mungu kwetu ya kutaka kuwatendea hisani masikini na wenye shida mbali mbali, nasi tukaacha kufanya hivyo. Si hivyo tu, bali tuliacha hata kumshukuru Mwenyezi Mungu juu ya neema zake kwetu.

(32) **HUENDA MOLA WETU AKATUBADILISHIA KHERI ZAIDI KULIKO HIYO. KWA HAKIKA, SISI NI WENYE MATARAJIO MEMA KWA MOLA WETU** Yaani: Sisi ni wenye kuomba kheri kwake, ni wenye kutaraji msamaha wake.

(33) **ADHABU NI KAMA HIYO** Yaani: Mfano wa adhabu hiyo tuliyowapa mtihani kwayo, tutawajaribu watu wa Makka kwa adhabu ya duniani. **NA KWA YAKINI, ADHABU YA AKHERA NI KUBWA ZAIDI INGALIKUWA WANAJUA** Yaani: Adhabu ya akhera ni kali sana na ni kubwa sana lau washirikina ingalikuwa wanajua. Lakini hawajui.

(34) **KWA HAKIKA, WENYE UCHAMUNGU WATAKUWA NA BUSTANI ZA NEEMA KWA MOLA WAO** Yaani: Wale wamchao Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza amri zake na kuacha makatazo yake watakuwa katika pepo yenye mabustani mazuri kwa Mola wao.

(35) **HIVI TUWAFANYE WAISLAAMU KAMA WAOVU?** Vigogo wa makafiri wa Kiqureishi walikuwa wakisema kwamba: Ikiwa ni sahihi anayoyadai Muhammad, basi hali yetu na hali ya hao Waislaamu haitakuwa isipokuwa kama hivi ilivyo hapa duniani. Sisi huko akhera tutapata neema za peponi mfano wa watakazopata wao. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu akatoa habari kwamba: Si katika uadilifu kufanya sawa sawa kati ya yule anayejilazimisha kumtii Mwenyezi Mungu na kati ya yule ambaye ni muovu, mbaya asiyejali kumuasi Mwenyezi Mungu.

(36) **MNA NINI NYINYI? VIPI MNAHUKUMU?** Mnahukumu vipi hukumu hii iliyopindapinda, kama kwamba mambo ya kulipa mmeachiwa nyinyi?

(37) **AU NYINYI MNACHO KITABU MNASOMA HUMO?** Yaani: Mnasoma katika kitabu hicho na kukuta humo kwamba: *Mtiifu ni kama muasi?*

(38) **KWAMBA NYINYI MTAPATA HUMO**

**MNACHOKICHAGUA?** Yaani: Je, katika kitabu hicho kuna maandishi kwamba nyinyi huko akhera mtapata yale myatakayo na kuyatamani?

(39) **AU MNAZO AHADI KWETU ZINAZOENDELEA MPAKA SIKU YA KIYAMA KWAMBA NYINYI MTAPATA YALE MNAYOHUKUMU?** Maana ni kuwa: Je, mnayo ahadi kwa Mwenyezi Mungu aliyokuapieni viapo madhubuti kwamba atakuingizeni peponi; viapo thabiti kwenu mpaka siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu hatavunja ahadi hizo hata hukumu yenu siku hiyo akuachieni nyiye?

(40) **WAULIZE: NI NANI KATI YAO MDHAMINI WA HAYO?** Yaani: Ewe Muhammad, waulize hao makafiri ukiwasuta na kuwacharura kuwa: Ni nani kati yao mwenye kuwadhaminia hayo kwamba huko akhera watapata yale watakayoyapata Waislaamu huko?

(41) **AU WANAO WASHIRIKA? BASI WAWALETE WASHIRIKA WAO IKIWA WAO NI WAKWELI** Maana ni kwamba: Je, wanao washirika wa Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa madai yao wenye uwezo wa kuwafanya wao sawa na Waislamu huko akhera?

(42) **SIKU AMBAYO PATAFUNULIWA MUUNDI** Mwenyezi Mungu ataufunua muundi (mguu) wake. Imamu Bukhari na maimamu wengine wamenukuu kutoka kwa Abuu Saidi akisema kuwa: Nimemsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akisema: "*Mola wetu atafunua muundi (mguu) wake. Basi kila muumini wa kiume na muumini wa kike atausujudia. Na atabaki yule ambaye hapa duniani alikuwa akisujudu kwa kujionesha na kutaka kusikika. Atakwenda ili akasujudu lakini mgongo wake utarudi na kuwa tabaka moja*". **NA WATAITWA KUJA KUSUJUDU NA HAWATAWEZA** Viumbe wote watamsujudia Mwenyezi Mungu sijida moja, na watabaki makafiri na wanafiki wakiwa wanataka kusujudu lakini hawataweza, kwa sababu migongo yao itakakamaa na haitalainika kwa ajili ya kusujudu. Hawakuwa wamemwamini Mwenyezi Mungu duniani na hawakumsujudia.

(43) **MACHO YAO YAKIWA NYENYEKEVU** Kunyenyekea ni utiifu, udhalili na kunyon'gonyea. **UNYONGE UKIWAFINIKA** Utawafunika udhalili mkubwa, majuto na kulalama. **NA, KWA HAKIKA, WALIKUWA WANAITWA KWENYE KUSUJUDU** Yaani Duniani. **NA ILHALI WAO WAKO SALAMA** Yaani: Wakiwa hawana ugonjwa, wanao uwezo wa kufanya. Ibrahimu At-taymiy amesema kuwa: "*Walikuwa wakiitwa kwa Adhana na Iqama na wanakataa*".

(44) **BASI NIACHE NA ANAYEKADHIBISHA MAZUNGUMZO HAYA** Niache: Yaani: Usiingilie kati yangu na kati yake. Mambo yake niachie mimi. Moyo wako usishughulik naye. Mimi nitakutosha mambo yake. Makusudio ya "MAZUNGUMZO HAYA" ni Qur'ani. **TUTAWAVUTA KIDOGO KIDOGO KWA NAMNA WASIYOJUA** Yaani: Tutawaadhibu kwa ghafla, na tutawakokota kuwapeleka kwenye adhabu hiyo hatua kwa hatua mpaka tuwatumbukize humo ilhali hawajui kwamba huko ni kuvutwa kidogo kidogo, kwa sababu wao watadhani kuwa huko ni kuneemeshwa, na wala hawafikirii mwisho wake, na yale watakayokutana nayo mwishoni mwake.

(45) **NA NINAWAPA MUDA.** Yaani: Ninawapa muda ili wazidi kufanya dhambi. **KWA HAKIKA, VITIMBI VYANGU NI MADHUBUTI** Yaani: Ni vina nguvu, vikali. Hakitaniponyoka kitu chochote.

(46) **AU UNAWAOMBA MALIPO?** Yaani: Je, unawaomba malipo juu ya hiyo imani ya kumwamini Mwenyezi Mungu unayowahubiria? **KWA HIYO WAO KUTOKANA NA GHARAMA NI WENYE KUELEMEWA?** Anayegharimika ni yule anayechukua gharama ya malipo hayo. Yaani: Inawawia uzito kwao kumudu malipo hayo kwa sababu ya ubahili wao wa kutoa mali. Je, uliwataka ujira ndipo wakaacha kukujibu kwa sababu hii?

(47) **AU WANAYO GHAIBU KWA HIYO WANAANDIKA?** Yaani: Au je, wanayo elimu ya mambo yaliyofichikana (ghaibu) ndipo wao: **a)**Wanaandika yale wayatakayo katika hoja wanazozidai?, na **b)**Wanajadiliana nawe kwa hayo wanayoyaandika kutokana na elimu hiyo?, na **c)**Wanajihukumia wao wenyewe mambo wayatakayo, na kwa hayo wanatosheka na kuacha kukuitikia wewe na kuyatekeleza yale unayoyasema?

(48) **BASI NGOJEA HUKUMU YA MOLA WAKO** Kati yako na kati ya hao wapinzani wa haki, na usijali yanayokusibu kutoka kwao au kutokuamini kwao. **NA USIWE KAMA MTU WA CHEWA** Aliyemezwa na chewa ni Mtume Yunus, Mwenyezi Mungu amfikishie amani. Yaani: Usiwe kama yeye katika kughadhibika na kukereka. **WAKATI ALIPOITA NA ILHALI YEYE NI MWENYE KUZONGWA** Mwenyezi Mungu anampa pole Mtume wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na kumuamuru kuvumilia na asifanye haraka kama alivyofanya haraka yule mwenye kumezwa na chewa. Yametangulia maelezo ya kisa cha Mtume aliyemezwa na chewa katika Suuratil Anbiyaa (21)

خَٰشِعَةً أَبۡصَٰرُهُمۡ تَرۡهَقُهُمۡ ذِلَّةٞۖ وَقَدۡ كَانُواْ يُدۡعَوۡنَ إِلَى ٱلسُّجُودِ وَهُمۡ سَٰلِمُونَ
٤٣ فَذَرۡنِي وَمَن يُكَذِّبُ بِهَٰذَا ٱلۡحَدِيثِۖ سَنَسۡتَدۡرِجُهُم مِّنۡ حَيۡثُ
لَا يَعۡلَمُونَ ٤٤ وَأُمۡلِي لَهُمۡۚ إِنَّ كَيۡدِي مَتِينٌ ٤٥ أَمۡ تَسۡـَٔلُهُمۡ أَجۡرٗا فَهُم
مِّن مَّغۡرَمٖ مُّثۡقَلُونَ ٤٦ أَمۡ عِندَهُمُ ٱلۡغَيۡبُ فَهُمۡ يَكۡتُبُونَ ٤٧ فَٱصۡبِرۡ
لِحُكۡمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُن كَصَاحِبِ ٱلۡحُوتِ إِذۡ نَادَىٰ وَهُوَ مَكۡظُومٞ ٤٨ لَّوۡلَآ
أَن تَدَٰرَكَهُۥ نِعۡمَةٞ مِّن رَّبِّهِۦ لَنُبِذَ بِٱلۡعَرَآءِ وَهُوَ مَذۡمُومٞ ٤٩ فَٱجۡتَبَٰهُ رَبُّهُۥ
فَجَعَلَهُۥ مِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ٥٠ وَإِن يَكَادُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ لَيُزۡلِقُونَكَ بِأَبۡصَٰرِهِمۡ
لَمَّا سَمِعُواْ ٱلذِّكۡرَ وَيَقُولُونَ إِنَّهُۥ لَمَجۡنُونٞ ٥١ وَمَا هُوَ إِلَّا ذِكۡرٞ لِّلۡعَٰلَمِينَ ٥٢

ترتيبها ٦٩ — سُورَةُ الحَاقَّةِ — آياتها ٥٢

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

ٱلۡحَآقَّةُ ١ مَا ٱلۡحَآقَّةُ ٢ وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا ٱلۡحَآقَّةُ ٣ كَذَّبَتۡ ثَمُودُ
وَعَادُۢ بِٱلۡقَارِعَةِ ٤ فَأَمَّا ثَمُودُ فَأُهۡلِكُواْ بِٱلطَّاغِيَةِ ٥ وَأَمَّا
عَادٞ فَأُهۡلِكُواْ بِرِيحٖ صَرۡصَرٍ عَاتِيَةٖ ٦ سَخَّرَهَا عَلَيۡهِمۡ
سَبۡعَ لَيَالٖ وَثَمَٰنِيَةَ أَيَّامٍ حُسُومٗاۖ فَتَرَى ٱلۡقَوۡمَ فِيهَا صَرۡعَىٰ
كَأَنَّهُمۡ أَعۡجَازُ نَخۡلٍ خَاوِيَةٖ ٧ فَهَلۡ تَرَىٰ لَهُم مِّنۢ بَاقِيَةٖ ٨

na suurat Yunus (10) na suuratis Saaffaat (37). Kuita kwake kulikuwa kwa kauli yake iliyosema: "HAPANA MOLA APASAYE KUABUDIWA KWA HAKI ISIPOKUWA WEWE TU. KUTAKASIKA NI KWAKO WEWE. KWA HAKIKA, MIMI NILIKUWA MIONGONI MWA MADHALIMU” Hakuwa mvumilivu katika mahubiri yake kwa watu wake. Na kauli ya Mwenyezi Mungu: " NA ILHALI YEYE NI MWENYE KUZONGWA", yaani: Mwenye kukerwa, mwenye kutaabika. Pia yawezekana kuwa muradi (wa Mwenye kuzongwa) ni: Mwenye kufungiwa ndani ya tumbo la chewa.

(49) **BASI KAMA ISINGELIMUWAHI NEEMA KUTOKA KWA MOLA WAKE** Neema yenyewe ni Mwenyezi Mungu kumuwezesha kutubu na kukubali kutubu kwake. **KWA YAKINI, ANGELITUPWA JANGWANI** Yaani: Angelitemwa kutoka tumboni mwa tumbo la chewa hadi juu ya ardhi isiyokuwa na mimea. **NA ILHALI YEYE NI MWENYE KUSHUTUMIWA** Yaani: Anashutumiwa na kulaumiwa kwa kosa ambalo amelifanya na angefukuzwa katika rehema.

(50) **KWA HIYO, MOLA WAKE AKAMTEUA** Yaani: Alimteua na kumchagua kwa Utume. **NA AKAMFANYA KUWA MIONGONI MWA WATU WEMA** Yaani: Watu waliokamilika katika wema. Imesemwa pia kwamba: Mwenyezi Mungu alimrudishia Utume na kumpa uombezi kwa nafsi yake, watu wake na akampeleka kwa watu laki moja au wanaozidi na wote wakaamini, kama ilivyotangulia kuelezwa.

(51) **NA ILIVYO NI KWAMBA WALE AMBAO WAMEKUFURU WANAKARIBIA KUKUTELEZESHA KWA MACHO YAO** Ibni-Qutaiba amesema kuwa: *"Mwenyezi Mungu hakusudii kwamba wao watakudhuru kwa macho yao, kama mwenye kijicho anavyokidhuru kwa jicho la husuda kile anachokiangalia. Hakuna vingine isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu anakusudia kwamba wao wanakuangalia wewe pale unaposoma Qur'ani uangaliaji mkali kwa uadui na chuki, unaokaribia kukuangusha".* **PALE WALIPOSIKIA UKUMBUSHO** Yaani: Wakati wa kusikia kwao Qur-ani, kwa sababu ya kuchukia kwao chuki kubwa sana. **NA WANASEMA: HAKIKA, YEYE NI MWENDAWAZIMU** Yaani: Wanasema kwa kushangazwa na habari zake na hukmu zake; eti yeye ni mwendawazimu.

(52) **NA HAIKUWA HIYO ISIPOKUWA NI UKUMBUSHO KWA WALIMWENGU** Yaani: Haikuwa hii Qur'ani ambayo anaisoma Muhamad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na ambayo wao hawataki kuiamini ispokuwa kwamba ni ukumbusho tu kwa walimwengu wote. Hivyo, haiwezekani ukumbusho wa walimwengu wote uteremshwe kwa mtu mwendawazimu.

## SUURATUL-HAAQQAH (69)

Imeteremka Makka Aya zake ni hamsimi na mbili (52)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

(1) **TUKIO LA HAKI** Tukio hilo ni Kiyama, kwa sababu mambo ni ya hakika katika tukio hilo. Tukio la haki ni siku ya haki kwa sababu siku hiyo haki zitadhihiri.

(2) **NINI TUKIO LA HAKI?** Maana ni kuwa: Ni kitu gani hicho katika hali yake na sifa zake?

(3) **NA NINI KILICHOKUJULISHA WEWE, NI NINI TUKIO LA HAKI?** Yaani: Ni kitu gani kilichokujulisha wewe, ni nini hicho? Kama kwamba kiko nje kabisa ya eneo la elimu ya viumbe.

(4) **THAMUDI NA ADI WALIKADHIBISHA KIGONGACHO** Yaani: Kigongacho ni Kiyama, na kimeitwa hivyo kwa sababu kitawagonga watu na kuwakwaruza kwa matukio yake ya kutisha.

(5) **AMA THAMUDI, WALIANGAMIZWA**

وَجَآءَ فِرۡعَوۡنُ وَمَن قَبۡلَهُۥ وَٱلۡمُؤۡتَفِكَٰتُ بِٱلۡخَاطِئَةِ ﴿٩﴾ فَعَصَوۡاْ رَسُولَ
رَبِّهِمۡ فَأَخَذَهُمۡ أَخۡذَةٗ رَّابِيَةً ﴿١٠﴾ إِنَّا لَمَّا طَغَا ٱلۡمَآءُ حَمَلۡنَٰكُمۡ فِي ٱلۡجَارِيَةِ
﴿١١﴾ لِنَجۡعَلَهَا لَكُمۡ تَذۡكِرَةٗ وَتَعِيَهَآ أُذُنٞ وَٰعِيَةٞ ﴿١٢﴾ فَإِذَا نُفِخَ فِي ٱلصُّورِ
نَفۡخَةٞ وَٰحِدَةٞ ﴿١٣﴾ وَحُمِلَتِ ٱلۡأَرۡضُ وَٱلۡجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةٗ وَٰحِدَةٗ ﴿١٤﴾
فَيَوۡمَئِذٖ وَقَعَتِ ٱلۡوَاقِعَةُ ﴿١٥﴾ وَٱنشَقَّتِ ٱلسَّمَآءُ فَهِيَ يَوۡمَئِذٖ وَاهِيَةٞ
﴿١٦﴾ وَٱلۡمَلَكُ عَلَىٰٓ أَرۡجَآئِهَاۚ وَيَحۡمِلُ عَرۡشَ رَبِّكَ فَوۡقَهُمۡ يَوۡمَئِذٖ ثَمَٰنِيَةٞ
﴿١٧﴾ يَوۡمَئِذٖ تُعۡرَضُونَ لَا تَخۡفَىٰ مِنكُمۡ خَافِيَةٞ ﴿١٨﴾ فَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ
كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ فَيَقُولُ هَآؤُمُ ٱقۡرَءُواْ كِتَٰبِيَهۡ ﴿١٩﴾ إِنِّي ظَنَنتُ أَنِّي مُلَٰقٍ
حِسَابِيَهۡ ﴿٢٠﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٖ رَّاضِيَةٖ ﴿٢١﴾ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٖ ﴿٢٢﴾
قُطُوفُهَا دَانِيَةٞ ﴿٢٣﴾ كُلُواْ وَٱشۡرَبُواْ هَنِيٓـَٔۢا بِمَآ أَسۡلَفۡتُمۡ فِي ٱلۡأَيَّامِ
ٱلۡخَالِيَةِ ﴿٢٤﴾ وَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ بِشِمَالِهِۦ فَيَقُولُ يَٰلَيۡتَنِي لَمۡ أُوتَ كِتَٰبِيَهۡ
﴿٢٥﴾ وَلَمۡ أَدۡرِ مَا حِسَابِيَهۡ ﴿٢٦﴾ يَٰلَيۡتَهَا كَانَتِ ٱلۡقَاضِيَةَ ﴿٢٧﴾ مَآ أَغۡنَىٰ
عَنِّي مَالِيَهۡۜ ﴿٢٨﴾ هَلَكَ عَنِّي سُلۡطَٰنِيَهۡ ﴿٢٩﴾ خُذُوهُ فَغُلُّوهُ ﴿٣٠﴾ ثُمَّ ٱلۡجَحِيمَ
صَلُّوهُ ﴿٣١﴾ ثُمَّ فِي سِلۡسِلَةٖ ذَرۡعُهَا سَبۡعُونَ ذِرَاعٗا فَٱسۡلُكُوهُ ﴿٣٢﴾ إِنَّهُۥ
كَانَ لَا يُؤۡمِنُ بِٱللَّهِ ٱلۡعَظِيمِ ﴿٣٣﴾ وَلَا يَحُضُّ عَلَىٰ طَعَامِ ٱلۡمِسۡكِينِ ﴿٣٤﴾

**KWA KILICHO PINDUKIA MPAKA** Thamudi ni watu wa Mtume Salehe. Kilichopindukia mpaka ni ukelele ambao umevuka kiwango.

(6) **NA AMA ADI, WAO WALIANGAMIZWA KWA UPEPO ULIO BARIDI, USIOKINGIKA** Adi ni watu wa Mtume Hudi. Upepo ulio baridi ni upepo wenye baridi kali sana. Usiokingika ni upepo mkavu ambao umevuka mpaka kwa ukali wa kuvuma kwake, na kurefuka kwa muda wake na ukali wa baridi yake.

(7) **ALIWAPELEKEA UPEPO HUO USIKU SABA NA MICHANA MINANE** Yaani: Mwenyezi Mungu amewapelekea upepo huo muda wote huu mfululizo, hausimami na hautulii. Ulikuwa ukiwauwa kwa changarawe. **UNAOWAMALIZA** Yaani: Unaowaangamiza na kuwamaliza. **UTAWAONA WATU HUMO** Yaani: Katika siku hizo. Au makusudio ni kuwa: Katika nyumba zao. **WAMEANGUKA** Wameanguka chini wakiwa wamekufa. **KAMA KWAMBA WAO NI MAGOGO YA MITENDE YALIYO WAZI NDANI** Yaani: Magogo ya mitende yaliyoanguka au yaliyooza.

(8) **JE, UNAONA KWAO CHOCHOTE KILICHOBAKI?** Yaani: Je, unaona kundi lililobaki, au nafsi iliyobaki? Yaani: Hakubaki yeyote miongoni mwao.

(9) **NA AKAJA FIR'AUNI NA WALIOKUWA KABLA YAKE** Yaani: Katika mataifa ya makafiri. **NA WALIOFIDIKIZIWA** Hao ni watu wa vijiji vya watu wa Mtume Luti. Maana ni kwamba wakaja waliofidikizwa. **KWA SABABU YA KOSA** Yaani: Kwa sababu ya vitendo vibaya, navyo ni ushirikina na maasi.

(10) **BASI WAKAMUASI MJUMBE WA MOLA WAO** Yaani: Kila uma ulimuasi mjumbe wao aliyetumwa kwao. **AKAWAKAMATA MKAMATO WA ZIADA** Yaani: Mwenyezi Mungu akawakamata (akawatia mikononi kwa kuwaadhibu) mkamato ukubwa uliozidi mikamato ya mataifa mengine.

(11) **KWA HAKIKA, MAJI YALIPOFURIKA** Yaani: Yalipopindukia mpaka wake katika kunyanyuka na kupanda juu. Hiyo ni tufani iliyotokea wakati wa Mtume Nuhu pale watu wake walipoung'an'gania ukafiri na wakamkadhibisha. **SISI TULIKUPAKIZENI NYINYI KATIKA KIENDACHO** Yaani: Tulikupakizeni mkiwa katika migongo ya baba zenu (kabla hamjazaliwa). Na "Kiendacho" ni jahazi la Mtume Nuhu, kwa sababu lilikuwa likitembea katika maji.

(12) **ILI TUKIFANYE UKUMBUSHO KWENU** Enyi uma wa Muhamad. Ukumbusho ni mazingatio na mawaidha mtakayoyatumia kuwa dalili ya kufahamu uwezo mkubwa wa Mwenyezi Mungu, uhodari wake wa kutengeneza na adhabu zake kali. **NA LIKIHIFADHI SIKIO LENYE KUHIFADHI** Yaani: Na ili sikio linalohifadhi mambo linayoyasikia liweze kuhifadhi tukio hilo baada ya kulisikia.

(13) **NA BARAGUMU LITAKAPOPULIZWA MPULIZO MMOJA** Ni mpulizo wa kwanza.

(14) **NA ARDHI NA MILIMA IKAONDOLEWA** Yaani: Ikanyanyuliwa kutoka mahala pake ilipotulia kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. **IKAPONDWA MPONDO MMOJA TU** Yaani: Vikavunjwa mvunjo mmoja usiokuwa na ziada. Pia imesemwa kuwa IKAPONDWA yaani: itatandazwa mtandazo mmoja tu.

(15) **BASI SIKU** litakuwa **HIYO LIMETOKEA LA KUTOKEA** Yaani: Kimesimama Kiyama.

(16) **NA MBINGU ZITAPASUKA. BASI SIKU HIYO, ZITAKUWA DHAIFU** Yaani: Zitapasuka kwa ajili ya kuteremka kwa Malaika waliomo humo. Siku hiyo zitakuwa dhaifu, zilizojiachia.

(17) **NA MALAIKA WAKIWA KANDO YAKE** Yaani: Malaika watakuwepo pembezoni mwake mpaka pale Mola atakapo waamuru ndipo wateremke duniani na kuizunguka na waliomo humo. **NA WANANE WATABEBA**

**ARSHI YA MOLA WAKO SIKU HIYO** Yaani: Malaika wanane wataibeba Arshi juu ya vichwa vyao siku ya Kiyama. Na imesemwa pia kuwa: Ni safu nane za Malaika, hakuna ajuaye idadi yao isipokuwa Mwenyezi Mungu tu.

(18) **SIKU HIYO MTAHUDHURISHWA** Yaani: Waja watahudhurishwa kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuhesabiwa. **HAKITAFICHIKA KWENU CHOCHOTE CHA KUFICHIKA** Hakifichiki kwa Mwenyezi Mungu cha kufichika; vyovyote iwavyo, iwe ni nyinyi wenyewe au kauli zenu au vitendo vyenu.

(19) **BASI AMA YULE ALIYEPEWA KITABU CHAKE KWA MKONO WAKE WA KULIA** Yaani: Amepewa kitabu chake ambacho Malaika wanaotunza wameandika humo matendo yake. **BASI ATASEMA: "CHUKUENI, SOMENI KITABU CHANGU** Yaani: Atayasema hayo kwa furaha na bashasha.

(20) **KWA YAKINI, MIMI NILIKUWA NA YAKINI KWAMBA NITAIKUTA HISABU YANGU** Yaani: Nilijua na kuwa na yakini duniani kwamba mimi nitahisabiwa huko Akhera. Na imesemwa pia kuwa maana ni kwamba: Mimi nilikuwa na yakini kwamba Mwenyezi Mungu ataniadhibu kwa madhambi yangu, kwa hakika amenifadhili kwa msamaha wake na hakunipatiliza.

(21) **BASI HUYO ATAKUWA KATIKA MAISHA MARIDHAWA** Maisha yenye kuridhiwa, sio ya karaha.

(22) **KATIKA PEPO ILIYO JUU** Yaani: Pepo iliopo mahali palipo juu, kwa sababu pepo hiyo iko mbinguni. Au maana ni kwamba pepo hiyo ni yenye hadhi tukufu na cheo cha juu.

(23) **MAKONYO YAKE YAKO KARIBU** Maana ni kwamba matunda yake yako karibu kwa anayeyachuma; iwe amesimama au amekaa au amejilaza.

(24) **"KULENI NA KUNYWENI** Yaani: Wataambiwa humo peponi: Kuleni na kunyweni. **KWA RAHA NA WASAA** Hakuna kinywaji kitakachochafuliwa humo na hakuna chakula kitachosumbua koo au tumbo. **KWA SABABU YA YALE MLIYOTANGULIZA KUYAFANYA KATIKA SIKU ZILIZOPITA"** Yaani: Kwa sababu ya amali njema mlizozifanya duniani.

(25) **NA AMA YULE ALIYEPEWA KITABU CHAKE KWA MKONO WAKE WA KUSHOTO, ATASEMA:** Kwa huzuni na kusikitikia maovu yake atakayoyaona humo. **"EE! LAITI MIMI NISINGEPEWA KITABU CHANGU** Yaani: Nisingepewa kabisa kitabu changu (kuliko kuwa nimepewa kikiwa kimejaa maovu tu)].

(26) **NA NISINGEJUA: NI NINI HISABU YANGU?** Yaani: Laiti pia nisingelijua kabisa: Hisabu yangu ni kitu gani? Atatamani hivyo kwa sababu yote yaliyomo humo yako dhidi yake.

(27) **EE! LAITI YANGEKUWA NI YENYE KUMALIZA** Yaani: Laiti mauti niliyokufa yangekuwa yenye kumaliza, na nisingelifanywa kuwa hai baada yake. Ametamani kudumu kwa mauti na kutofufuliwa kwa sababu ya vitendo vyake viovu alivyoviona na adhabu aliyoiendea.

(28) **HAIKUNIFAA MALI YANGU** Yaani: Mali niliyoichuma haikunikinga chochote na adhabu ya Mwenyezi Mungu.

(29) **HOJA ZANGU ZIMENIPOTEA"** Yaani: Hoja zangu zimenipotea na kunitoweka. Imesemwa pia kwamba: Muradi wa "HOJA = SULTAAN" ni cheo, hadhi na ufalme. Hapo, ndipo Mwanyezi Mungu atakaposema:

(30) **MKAMATENI NA MTIENI MAKONGO** Yaani: Ifungeni mikono yake kwenye shingo kwa makongo. (pingu za minyororo inayofunga shingo, mikono na miguu)

(31) **KISHA MTIENI MOTONI** Yaani: Mtieni motoni ili apate joto lake.

(32) **TENA KATIKA MINYORORO AMBAYO UREFU WAKE NI DHIRAA SABINI MUINGIZENI** Minyororo ni vikuku vilivyopangiliwa. Dhiraa ni urefu wake. Sufiani amesema kuwa: *Imetufikia habari kuwa mnyororo huo utamwingia mtu katika njia yake ya haja kubwa na kutokea mdomoni.*

(33) **KWA HAKIKA, YEYE ALIKUWA HAMUAMINI MWENYEZI MUNGU MTUKUFU**

(34) **NA HAHIMIZI JUU YA KUMPA CHAKULA MASIKINI** Yaani: Hajihimizi yeye mwenyewe kumpa chakula masikini kutoka katika mali yake au hamhimizi mtu mwengine katika kumpa chakula masikini.

(35) **BASI LEO HII HANA RAFIKI YEYOTE HAPA** Yaani: Siku ya Kiyama huko akhera, hatakuwa na atakayemsaidia au kumuombea, kwa sababu hiyo ni siku ambayo ndugu atamkimbia ndugu yake na mpenzi atamkimbia mpenzi wake mbele yake.

(36) **NA HANA CHAKULA ILA TU MAJI YA USAHA** Isipokuwa ni usaha wa watu wa motoni na damu chafu na usaha unaotiririka kutoka katika miili yao kutokana na kuoga kwao.

(37) **HAWALI CHAKULA HICHO ISIPOKUWA TU WENYE MAKOSA** Watu wenye makosa na wenye madhambi.

(38) **BASI NINA APA KWA MNAVYOVIONA**

(39) **NA MSIVYOVIONA** Yaani: Nina apa kwa vile vyote; vinavyo onekana na visivyo onekana.

(40) **KWA HAKIKA, HIYO NI KAULI YA MJUMBE MWENYE HESHIMA** Yaani: Kwa

فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هَاهُنَا حَمِيمٌ ﴿٣٥﴾ وَلَا طَعَامٌ إِلَّا مِنْ غِسْلِينٍ ﴿٣٦﴾ لَا يَأْكُلُهُ
إِلَّا الْخَاطِئُونَ ﴿٣٧﴾ فَلَا أُقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٨﴾ وَمَا لَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٩﴾
إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٤٠﴾ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَا تُؤْمِنُونَ ﴿٤١﴾
وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَا تَذَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾ تَنْزِيلٌ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٣﴾ وَلَوْ
تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤٤﴾ لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا
مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٤٦﴾ فَمَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِنَّهُ لَتَذْكِرَةٌ
لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾ وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنْكُمْ مُكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى
الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾ وَإِنَّهُ لَحَقُّ الْيَقِينِ ﴿٥١﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٥٢﴾

ترتيبها ٧٠ — سُورَةُ الْمَعَارِجِ — آياتها ٤٤

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ﴿١﴾ لِلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُ دَافِعٌ ﴿٢﴾ مِنَ
اللَّهِ ذِي الْمَعَارِجِ ﴿٣﴾ تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي
يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ﴿٤﴾ فَاصْبِرْ صَبْرًا جَمِيلًا ﴿٥﴾
إِنَّهُمْ يَرَوْنَهُ بَعِيدًا ﴿٦﴾ وَنَرَاهُ قَرِيبًا ﴿٧﴾ يَوْمَ تَكُونُ السَّمَاءُ كَالْمُهْلِ
﴿٨﴾ وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ ﴿٩﴾ وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿١٠﴾

yakini, Qur'ani ni kisomo cha Mjumbe mwenye heshima. Na muradi ni Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani au ni kauli ambayo Mjumbe mwenye heshima kubwa anaifikisha, akikusudiwa kuwa ni Jibrili.

(41) **NA SIO KAULI YA MSHAIRI** Kama mnavyodai, kwa sababu hiyo Qur'ani sio miongoni mwa aina za ushairi. **KUAMINI KWENU NI KUCHACHE MNO** Yaani: Mnaamini imani ndogo na mnakubali kukubali kudogo.

(42) **WALA SI KAULI YA KUHANI** Kama mnavyodai, kwani ukuhani ni jambo jingine kabisa. Hakuna uhusiano wowote kati yake na kati ya hii Qur'ani. **KUWAIDHIKA KWENU NI KUDOGO MNO** Yaani: Mnaonyeka kuonyeka kudogo sana.

(43) **NI UTEREMSHO UTOKAO KWA MOLA WA WALIMWENGU WOTE** Maana ni kuwa: Hiyo ni kauli ya Mjumbe mwenye heshima, na pia ni uteremsho utokao kwa Mola wa walimwengu wote kupitia ulimini mwake.

(44) **NA LAU ANGETUZULIA BAADHI YA MANENO** Yaani: Lau Mjumbe huyo ambaye ni Muhammad au Jibrili kwa mujibu wa maelezo yaliyotangulia, angetusingizia; lau angejikalifisha chochote katika hayo, na akayabuni yeye mwenyewe na akayahusisha kwa Mwenyezi Mungu,

(45) **TUNGEMSHIKA KWA MKONO WA KULIA** Yaani: Kwa mkono wake wa kuume.

(46) 46. **KISHA TUNGEMKATA MSHIPA MKUBWA WA MOYO** “Mshipa mkubwa wa moyo "*Alwatiin”* ni mshipa unaopita mgongoni mpaka unaungana na moyo. Hii ni taswira ya kuangamizwa kwake kwa adhabu mbaya sana ambayo watawala wanawafanyia watu wanaowachukia.

(47) **HAKUNA YEYOTE WA KUMKINGA NA ADHABU HIYO MIONGONI MWENU** Yaani: Hapana yeyote kati yenu atakayetukinga tusimpate au atakaye muokoa atuponyoke. Sasa vipi anajikalifisha kumsingizia Mwenyezi Mungu kwa ajili yenu?

(48) **NA KWAMBA HIYO NI UKUMBUSHO KWA WENYE UCHAMUNGU** Yaani: Qur'ani ni ukumbusho kwa wenye uchamungu, kwa sababu wao ndio wanaofaidika nayo.

(49) **NA KWA YAKINI, SISI TUNAJUA KWAMBA MIONGONI MWENU WAMO WAKADHIBISHAJI** Yaani: Baadhi yenu wanaikadhibisha Qur'ani. Sisi tutawalipa kwa hayo.

(50) **NA KWA YAKINI, HIYO ITAKUWA MAJUTO KWA MAKAFIRI** Yaani: Kwa yakini, Qur'ani itakuwa hasara na majuto kwa makafiri siku ya Kiyama.

(51) **NA KWA YAKINI, HIYO NI HAKI YA HAKIKA** Qur'ani ni haki ya hakika kwa kuwa inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Shaka haizunguki kandokando yake haiisogelei.

(52) **BASI LITUKUZE JINA LA MOLA WAKO MTUKUFU** Yaani: Mtakase na yasiyofaa kwake kwa kuleta Tasbihi ambao ni uradi maarufu.

## SUURATUL MAARIJ (70)

Imeteremka Makkah Aya zake ni arobaini na nne( 48)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

(1) **ALIOMBA MWENYE KUOMBA KUIOMBA ADHABU YENYE KUTOKEA** Maombi hapa yamekusanyiwa maana ya kuapiza. Maana ni kwamba: Muombaji amejiombea dua mbaya ya kufikwa na adhabu yenye kutuka. (amejiapiza) Imesemwa kuwa muombaji huyu ni Annadh-ri Ibn Al-haarith wakati aliposema kwamba: "*Ewe Mola wangu, ikiwa haya ayasemayo Muhammad ni haki kutoka kwako, basi nyesheleza juu yetu mawe kutoka mbinguni au tuletee adhabu iumizayo*".

(2) **KWA MAKAFIRI HAINA MWENYE**

يُبَصَّرُونَهُمْ يَوَدُّ الْمُجْرِمُ لَوْ يَفْتَدِي مِنْ عَذَابِ يَوْمِئِذٍ بِبَنِيهِ ﴿١١﴾
وَصَاحِبَتِهِ وَأَخِيهِ ﴿١٢﴾ وَفَصِيلَتِهِ الَّتِي تُؤْوِيهِ ﴿١٣﴾ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ
جَمِيعًا ثُمَّ يُنْجِيهِ ﴿١٤﴾ كَلَّا إِنَّهَا لَظَىٰ ﴿١٥﴾ نَزَّاعَةً لِلشَّوَىٰ ﴿١٦﴾ تَدْعُو
مَنْ أَدْبَرَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٧﴾ وَجَمَعَ فَأَوْعَىٰ ﴿١٨﴾ ۞ إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا
﴿١٩﴾ إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ﴿٢٠﴾ وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٢١﴾ إِلَّا
الْمُصَلِّينَ ﴿٢٢﴾ الَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ﴿٢٣﴾ وَالَّذِينَ فِي
أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَعْلُومٌ ﴿٢٤﴾ لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿٢٥﴾ وَالَّذِينَ يُصَدِّقُونَ
بِيَوْمِ الدِّينِ ﴿٢٦﴾ وَالَّذِينَ هُمْ مِنْ عَذَابِ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ ﴿٢٧﴾ إِنَّ عَذَابَ
رَبِّهِمْ غَيْرُ مَأْمُونٍ ﴿٢٨﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٢٩﴾ إِلَّا عَلَىٰ
أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٣٠﴾ فَمَنِ ابْتَغَىٰ وَرَاءَ
ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٣١﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمَانَاتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ
﴿٣٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ بِشَهَادَاتِهِمْ قَائِمُونَ ﴿٣٣﴾ وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ
﴿٣٤﴾ أُولَٰئِكَ فِي جَنَّاتٍ مُكْرَمُونَ ﴿٣٥﴾ فَمَالِ الَّذِينَ كَفَرُوا قِبَلَكَ مُهْطِعِينَ
﴿٣٦﴾ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٣٧﴾ أَيَطْمَعُ كُلُّ امْرِئٍ مِنْهُمْ
أَنْ يُدْخَلَ جَنَّةَ نَعِيمٍ ﴿٣٨﴾ كَلَّا إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِمَّا يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾

**KUIZUIA** Adhabu hiyo yenye kutuka itawashukia makafiri, hapana yoyote atakayeizuia.

(3) **ITOKAYO KWA MWENYEZI MUNGU MWENYE VIPANDIO** Adhabu inatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye vipandio ambavyo Malaika wanapanda kupitia vipandio hivyo. (ngazi) Imesemwa pia kuwa vipandio ni utukufu.

(4) **MALAIKA NA ROHO WANAPANDA HUMO KWENDA KWAKE** Yaani: Malaika wanapanda kwenda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika ngazi hizo ambazo Mwenyezi Mungu amezifanya kwa ajili yao. Roho ni Jibrili. Imesemwa pia kuwa roho hapa ni Malaika mwingine mkubwa, sio Jibrili. **KATIKA SIKU AMBAYO KIPIMO CHAKE KITAKUWA MIAKA HAMSINI ELFU** makusudio ni siku ya Kiyama. Muda wa kusimama waja kwa ajili ya kuhesabiwa ni kiasi hiki cha miaka. Kisha baada ya hapo, watu wa peponi watatulizana katika pepo, na watu wa motoni watatulizana katika moto. Na imesemwa pia kuwa kiasi cha siku ya Kiyama kwa makafiri ni miaka hamsini elfu, na kwa waumini ni muda ulio kati ya Adhuhuri na Alasiri.

(5) **KWA HIYO, VUMILIA UVUMILIVU MZURI** Yaani: Vumilia ewe Muhammad juu ya upinzani wao kwako na kukufuru kwao yale ambayo umekuja nayo. Vumilia kuvumilia ambako hakuna malalamiko ndani yake na hakuna mashtaka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Hii ndio maana ya uvumilivu mzuri.

(6) **HAKIKA, WAO WANAIONA SIKU HIYO KUWA IKO MBALI** Yaani: Wanaiona siku ya Kiyama ambayo kipimo chake ni miaka hamsini elfu iko mbali na ni jambo lisilowezekana, muhali.

(7) **NA SISI TUNAIONA IKO KARIBU** Yaani: Sisi tunajua kuwa ni yenye kutokea, iko karibu kwa sababu "Kila kijacho, kiko karibu".

(8) **SIKU AMBAYO MBINGU ZITAKUWA KAMA MADINI YALIYOYAYUSHWA** Madini yaliyoyayushwa ni shaba, risasi na fedha iliyoyayushwa. Na imesemwa pia kuwa ni tope za mafuta.

(9) **NA MILIMA ITAKUWA KAMA SUFI ILIYOCHAMBULIWA** Milima itakuwa kama sufi iliyochambuliwa, kwa sababu ikisha pondwapondwa na kurushwa angani itafanana na sufi iliyo chambuliwa wakati inapopeperushwa na upepo.

(10) **NA NDUGU HATAMUULIZA NDUGU** Ndugu hatamuuliza ndugu yake; kuhusu mambo yake katika siku hiyo kutokana uzito wa matukio makubwa yatakayo washukia.

(11) **WATAONESHWA NDUGU ZAO HAO** Kila ndugu atamuona ndugu yake. Hataweza kujificha kwa yeyote. Lakini Hawataulizana wala hawatasemeshana. **MUOVU ATAPENDA** Atatamani kila mwenye dhambi aliyestahiki kuingia motoni kwa dhambi hiyo. **SIKU HIYO KUJIKOMBOA KWA WATOTO WAKE KUTOKANA NA ADHABU YA SIKU HIYO** Siku ya Kiyama ambayo imemshukia.

(12) **NA MKE WAKE NA NDUGU YAKE** Hawa ni watu adhimu na watukufu zaidi kwake. Lau ungekubaliwa ukombozi kwake, angejikomboa kwa kuwatoa hao na asalimike na adhabu iliyomshukia.

(13) **NA UKOO WAKE AMBAO UNAMHAMI** Jamaa zake wa karibu zaidi ambao wanahusiana naye katika uzawa au wakati wa matatizo, na ambao anakimbilia kwao.

(14) **NA WALIO KATIKA ARDHI WOTE, KISHA KUJIKOMBOA HUKO KUMUOKOE** Muovu atatamani kujikomboa kwa wote waliomo katika ardhi, wakiwemo binadamu, majini na viumbe wengine wasiokuwa hao, kisha kujikomboa huko kumuokoe na adhabu ya Jahanamu.

(15) **HAPANA! HAKIKA, HUO NI MBIMBIRIKO** HAPANA! Ni neno la kumkemea mouvu aache matumaini hayo, na kumuwekea wazi kutowezekana kwa ukombozi

alioupenda. HAKIKA, HUO NI MBIMBIRIKO Mbimbiriko *Ladhwaa* ni jina la Jahannamu. Jina hilo limechukuliwa kutokana na mbimbiriko katika moto, ambao ni muwako unaotoa miali na sauti.

(16) **UNABAMBUA NGOZI YA KICHWA** Unabambua nyama na ngozi na kuitenganisha na mfupa mpaka usibakishe kitu katika mfupa huo.

(17) **UNAMWITA MWENYE KUPUUZA NA KUPINGA** Yaani: Jahannamu inamwita mwenye kuikataa haki duniani na akaipuuza

(18) **NA AKAKUSANYA NA AKAHIFADHI** Yaani: Amekusanya mali akaiweka katika hifadhi, na hakutumia chochote katika mali hiyo katika njia za kheri.

(19) **KWA YAKINI, MWANADAMU AMEUMBWA AKIWA MWENYE KULALAMA** Kulalama ni pupa mbaya sana na manun'guniko machafu kabisa.

(20) **IKIMPATA SHARI, NI MWINGI WA KULALAMA SANA**

(21) **NA IKIMPATA KHERI NI MZUIAJI SANA** Yaani: Mwanadamu ukimpata ufukara au shida au ugonjwa au mfano wa hayo, anakuwa mwingi wa kulalama. Na ikimpata kheri kama vile utajiri, rutuba (katika kilimo), wasaa na mfano wa hayo, yeye anakuwa mwingi wa kuzuia na kubania.

(22) **ILA TU WENYE KUSWALI** Ila wenye kudumisha kuswali. Yaani: Wao hawako katika sifa hizo za kulalama, kunun'gunika na kuzuia , na kwamba wao wamo katika sifa za kusifika na vitendo maridhawa, kwa kuwa imani yao na dini ya haki inawakemea kusifika na sifa hizo, na inawaongoza kwenye kusifka na sifa njema.

(23) **AMBAO WAO JUU YA SWALA ZAO NI WENYE KUDUMU** Hawajishughulishi na la kushughulisha wakaiacha sala na wanazitekeleza swala zilizofaradhiwa katika nyakati zake.

(24) **NA AMBAO KATIKA MALI ZAO KUNA HAKI YENYE KUJULIKANA** Muradi wa haki yenye kujulikana ni zaka yenye kufaradhiwa. Imesemwa pia kuwa muradi wake ni kuunga udugu.

(25) **KWA MWENYE KUOMBA NA MWENYE KUNYIMWA** Imetangulia tafsiri ya mwenye kuomba na mwenye kunyimwa katika Sura Al-dhaariyaat.

(26) **NA WALE AMBAO WANAISADIKISHA SIKU YA MALIPO** Hiyo ni siku ya Kiyama. Hawaitilii shaka wala hawaikanushi.

(27) **NA AMBAO WAO WANAIOGOPA ADHABU YA MOLA WAO** Wanaihofu na kuiogopa adhabu hiyo pamoja na kuwa wanayo matendo ya ibada, kwa kuyaona duni matendo yao na kuungama yale yaliyo wajibu kwao kumfanyia Mwenyezi Mungu Mtukufu.

(28) **HAKIKA, ADHABU YA MOLA WAO SI YENYE KUAMINIWA** Yaani: Haitakikani kwa yeyote kujiaminisha nayo, na kwamba haki ya kila mmoja ni kuiogopa.

(29) **NA AMBAO WAO NI WENYE KUZIHIFADHI TUPU ZAO.** Wasizitumie katika njia za maasi.

(30) **ILA KWA WAKE ZAO** wa halali **AU WALE AMBAO IMEWAMILIKI MIKONO YAO YA KULIA** wajakazi. **HAKIKA, WAO SI WENYE KULAUMIWA.** Hawatalaumiwa au kuadhibiwa ikiwa watakidhi hapo matamanio ya nafsi zao.

(31) **BASI MWENYE KUTAKA KINYUME CHA HAYO, HAO NDIO WENYE KUVUKA MIPAKA** yaani watakaokidhi matamanio ya nafsi zao kwa njia nyingine mbali na hizo zilizotajwa basi hao ndio waliopindukia mipaka ya Mwenyezi Mungu na kuingia katika aliyoharamisha.

(32) **NA AMBAO WAO NI WENYE KUCHUNGA AMANA ZAO NA AHADI ZAO** Yaani: Hawapuuziii kitu chochote katika amana ambazo wanaoaminiwa kuzichunga, na hawavunji kitu chochote katika ahadi ambazo wanazifunga juu ya nafsi zao.

(33) **NA AMBAO WAO NI WENYE KUSIMAMISHA USHAHIDI WAO** Yaani: Wanatoa ushahidi kama ulivyo kwa yule ambaye unatakiwa kutolewa ushahidi juu yake; awe ni ndugu au mtu kando, mwenye hadhi au mtu wa kawaida. Hawafichi ushahidi na hawaubadilishi.

(34) **NA AMBAO WAO SWALA ZAO WANAZIHIFADHI** Yaani: Wanahifadhi nyiradi zake, nguzo zake na masharti yake. Hawaachi kitu chochote katika hayo, na lolote la kushughulisha haliwashughulishi wakaiacha sala. Wanaihifadhi swala baada ya kuitekeleza kwa kuacha kutenda mambo ambayo yanaipomosha na kubatilisha malipo yake.

(35) **HAO KATIKA MABUSTANI WATAKIRIMIWA** Watatulizana humo na watakirimiwa kwa namna mbalimbali za takrima.

(36) **WANA NINI WALE AMBAO WAMEKUFURU WANAKUKODOLEA MACHO?** Yaani: Wanafanya haraka kukupinga na kukucheza shere. Na imesemwa pia kuwa wananyoosha shingo zao wakikuangalia sana.

(37) **KULIANI NA KUSHOTONI WAKO MAKUNDI MAKUNDI** Yaani: Kuliani kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na kushotoni kwake kuna makundi yenye kusambaa.

(38) **HIVI KILA MTU KATIKA WAO ANATAMAA YA KUINGIZWA KATIKA PEPO YENYE NEEMA?** Washirikina walikuwa

فَلَآ أُقۡسِمُ بِرَبِّ ٱلۡمَشَٰرِقِ وَٱلۡمَغَٰرِبِ إِنَّا لَقَٰدِرُونَ ﴿٤٠﴾ عَلَىٰٓ أَن نُّبَدِّلَ خَيۡرٗا مِّنۡهُمۡ
وَمَا نَحۡنُ بِمَسۡبُوقِينَ ﴿٤١﴾ فَذَرۡهُمۡ يَخُوضُواْ وَيَلۡعَبُواْ حَتَّىٰ يُلَٰقُواْ يَوۡمَهُمُ ٱلَّذِي
يُوعَدُونَ ﴿٤٢﴾ يَوۡمَ يَخۡرُجُونَ مِنَ ٱلۡأَجۡدَاثِ سِرَاعٗا كَأَنَّهُمۡ إِلَىٰ نُصُبٖ يُوفِضُونَ
﴿٤٣﴾ خَٰشِعَةً أَبۡصَٰرُهُمۡ تَرۡهَقُهُمۡ ذِلَّةٞۚ ذَٰلِكَ ٱلۡيَوۡمُ ٱلَّذِي كَانُواْ يُوعَدُونَ ﴿٤٤﴾

ترتيبها ٧١ — سُورَةُ نُوحٍ — آياتها ٢٨

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِنَّآ أَرۡسَلۡنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوۡمِهِۦٓ أَنۡ أَنذِرۡ قَوۡمَكَ مِن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَهُمۡ
عَذَابٌ أَلِيمٞ ﴿١﴾ قَالَ يَٰقَوۡمِ إِنِّي لَكُمۡ نَذِيرٞ مُّبِينٌ ﴿٢﴾ أَنِ ٱعۡبُدُواْ
ٱللَّهَ وَٱتَّقُوهُ وَأَطِيعُونِ ﴿٣﴾ يَغۡفِرۡ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمۡ وَيُؤَخِّرۡكُمۡ
إِلَىٰٓ أَجَلٖ مُّسَمًّىۚ إِنَّ أَجَلَ ٱللَّهِ إِذَا جَآءَ لَا يُؤَخَّرُۚ لَوۡ كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ
﴿٤﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوۡتُ قَوۡمِي لَيۡلٗا وَنَهَارٗا ﴿٥﴾ فَلَمۡ يَزِدۡهُمۡ دُعَآءِيٓ إِلَّا
فِرَارٗا ﴿٦﴾ وَإِنِّي كُلَّمَا دَعَوۡتُهُمۡ لِتَغۡفِرَ لَهُمۡ جَعَلُوٓاْ أَصَٰبِعَهُمۡ
فِيٓ ءَاذَانِهِمۡ وَٱسۡتَغۡشَوۡاْ ثِيَابَهُمۡ وَأَصَرُّواْ وَٱسۡتَكۡبَرُواْ ٱسۡتِكۡبَارٗا
﴿٧﴾ ثُمَّ إِنِّي دَعَوۡتُهُمۡ جِهَارٗا ﴿٨﴾ ثُمَّ إِنِّيٓ أَعۡلَنتُ لَهُمۡ وَأَسۡرَرۡتُ
لَهُمۡ إِسۡرَارٗا ﴿٩﴾ فَقُلۡتُ ٱسۡتَغۡفِرُواْ رَبَّكُمۡ إِنَّهُۥ كَانَ غَفَّارٗا ﴿١٠﴾

wakisema kuwa: "*Hawa Waislamu wakiingia peponi, kwa hakika sisi tutaingia kabla yao*". Kutokana na maneno hayo, ilishuka aya hii.

(39) **HIVYO SIVYO! KWA YAKINI, SISI TUMEWAUMBA WAO KUTOKANA NA KILE AMBACHO WANAKIJUA** Yaani: Tumewaumba kutokana na uchafu ambao wanaujua. Kwa hiyo, haitakikani kwao kufanya kiburi hiki. Imam Ahmad, Ibn-maja na Ibn-saad wamesimulia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alisoma aya hizi: " *WANA NINI WALE AMBAO WAMEKUFURU WANAKUKODOLEA MACHO? KULIANI NA KUSHOTONI WAKO MAKUNDI MAKUNDI? HIVI ANATAMAA KILA MTU KATIKA WAO YA KUINGIZWA KATIKA PEPO YENYE NEEMA? HIVYO SIVYO! KWA YAKINI, SISI TUMEWAUMBA KUTOKANA NA KILE AMBACHO WANAKIJUA*" Kisha Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alitema mate juu ya kiganja chake na kuweka kidole chake juu yake na akasema: "*Mwenyezi Mungu anasema kuwa: Ewe mwanadamu, vipi utanishinda na ilhali nimekuumba kutokana na mfano wa mate haya? Mpaka nilipokutengeneza sawa sawa na kukunyoosha umekuwa unatembea kati ya shuka mbili na ardhi ikawa tulivu kwako, ukakusanya na umezuia , mpaka roho ilipofikia katika mishipa ya shingo ndio umefika wakati wa kutoa sadaka!"*

(40) **HIVYO BASI, NINAAPA KWA MOLA WA MASHARIKI NA MAGHARIBI, KWA YAKINI SISI NI WENYE KUWEZA** Ninaapia kwa Mola wa mashariki ya kila siku katika siku za mwaka na magharibi yake.

(41) **KUBADILISHA WALIO BORA ZAIDI KULIKO WAO, NA SISI SIO WENYE KUSHINDWA** Yaani: Tunaweza kuwaumba watu bora zaidi kuliko wao na wenye kumtii zaidi Mwenyezi Mungu kuliko wale waliomuasi na tukawaangamiza. *"Na sisi sio wenye kushindwa"*, tukitaka kufanya hivyo. Bali tunafanya lile tunalolitaka. Hakitukwepi kitu chochote, na halitushindi jambo lolote.

(42) **BASI WAACHE WAZAME NA WACHEZE MPAKA WAKUTANE NA SIKU YAO AMBAYO WANAAHIDIWA** Waache wazame katika batili yao, na wacheze katika ulimwengu wao. Wewe shughulika na lile ambalo umeamrishwa, na yasikutie jekejeke kabisa yale waliyonayo. Wajibu wako ni kufikisha ujumbe tu. **MPAKA WAKUTANE NA SIKU YAO AMBAYO WANAAHIDIWA** Hiyo ni siku ya kiyama.

(43) **SIKU AMBAYO WATATOKA KATIKA MAKABURI YAO HUKU WAKIENDA HARAKA, KANA KWAMBA WAO KWENYE MEDE WANAKIMBILIA** Siku watakapotoka makaburini haraka kama kwamba wanashindana kufika haraka kwenye kitu kilicho simamishwa, kama vile bendera.

(44) **YAKIWA DHALILI MACHO YAO HUKU UKIWAFUNIKA UNYONGE. HIYO NDIO SIKU AMBAYO WALIKUWA WAKIAHIDIWA** Macho yao yatakuwa manyonge, hawawezi kuyanyanyua kutokana na adhabu wanayoitazamia. Madhila makubwa sana yatawagubika.

## SUURAT NUUH (71)

Imeteremka Makkah Aya zake

ni ishirini na nane (28)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

(1) **KWA YAKINI, SISI TULIMPELEKA NUHU KWA WATU WAKE TUKAMWAMBIA: WAHOFISHE WATU WAKO KABLA YA KUWAJIA WAO ADHABU IUMIZAYO SANA** Imetangulia huko nyuma kueleza kwamba Nuhu ndiye Mtume wa kwanza ambaye Mwenyezi Mungu amemtuma. Na umetajwa ufafanuzi wa muda wa kukaa kwake kwa watu wake katika Suuratul Ankabuut (29) kuwa ni

miaka alfu moja kupungua hamsini **KWAMBA WAHOFISHE WATU WAKO** Yaani: Tulimwambia: "Wahofishe watu wako" **KABLA HAIJAWAJIA ADHABU IUMIZAYO SANA** Adhabu yenye maumivu makali, nayo ni adhabu ya moto, au adhabu hiyo ni ile gharika iliyowashukia.

(2) **ALISEMA: ENYI WATU WANGU, HAKIKA, MIMI KWENU NI MUONYAJI MWENYE KUWEKA WAZI** Mimi ni mwenye kutahadharisha na ni mwenye kukuhofisheni adhabu ya Mwenyezi Mungu. MWENYE KUWEKA WAZI Ninakuwekeeni wazi yale ambayo ndani yake kuna wokovu wenu.

(3) **KWAMBA: MWABUDUNI MWENYEZI MUNGU NA MCHENI NA MNITII MIMI** Mtekelezeeni haki yake ya kujidhalilisha na kupenda, na tekelezeni yale ambayo amekuamrisheni na msishirikishe naye mwengine. NA MCHENI Yaani: Jiepusheni na yale ambayo yatakuingizeni katika adhabu yake. NA MNITII MIMI Mnitii mimi katika yale ambayo ninakuamrisheni, kwani mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenu.

(4) **ATAKUSAMEHENI KATIKA MADHAMBI YENU** Yaani: Atakusameheni baadhi ya madhambi yenu, nayo ni yale ambayo yametangulia kutendwa kabla ya kumtii Mtume na kuitika wito wake. **NA ATAKUCHELEWESHENI MPAKA MUDA ULIO TAJWA.** Yaani: Na atachelewesha kufa kwenu mpaka muda wa juu kabisa ambao Mwenyezi Mungu ameukadiria kwenu. Muradi ni kwamba ataurefusha umri umma wenu na kuishi kwao duniani madamu watadumu katika kumtii Mwenyezi Mungu. **KWA YAKINI, MUDA WA MWEMWEZI MUNGU PINDI UKIJA HAUCHELEWESHWI** Yaani: Muda aliokukadirieni Mwenyezi Mungu ukija na ilhali nyinyi bado mumo katika ukafiri, hauta ahirishwa. Bali utatotokea bila ya kizuizi. Kwa hiyo, fanyeni haraka kuamini na kutii. **LAU MNGEKUWA MNAJUA** Yaani: Mngejua kwamba muda wa Mwenyezi Mungu pindi ukija hauacheleweshwi.

(5) **ALISEMA: EWE MOLA WANGU, KWA YAKINI MIMI NIMEWALINGANIA WATU WANGU USIKU NA MCHANA** Yaani: Niliwahubiria imani ambayo umeniamrisha niwahubirie. Niliwahubiria mahubiri endelevu; usiku na mchana bila ya kuzembea.

(6) **KULINGANIA KWANGU HAKUKUWAZIDISHIA ILA TU KUKIMBIA** Kulingania kwangu hakukuwazidishia ila kuyakimbia yale ambayo ninawalingania, na kuyakalia mbali.

(7) **NA KWA YAKINI, MIMI KILA NILIPOWALINGANIA ILI UWASAMEHE,** Yaani: Kila nilipowaita kwenye sababu ya kusamehewa, nayo ni kukuamini wewe na kukutii, **WALITIA VIDOLE VYAO MASIKIONI MWAO** ili wasiisikie sauti yangu. **NA WALIJIFUNIKA NGUO ZAO** Walizificha nyuso zao kwa nguo zao hizo ili wasinione na ili wasiyasikie maneno yangu. **NA WALIN'GAN'GANIA** ukafiri. **NA WALITAKABARI** Walifanya kiburi cha kukataa kuikubali haki. **KIBURI KIKUBWA** Kutakabari kukubwa sana.

(8) **KISHA KWA YAKINI, MIMI NILIWALINGANIA KWA UWAZI** Niliwawekea wazi wito, nikiwakabili kwa uwazi kuhusu mahubiri hayo.

(9) **KISHA HAKIKA, MIMI NIMEWADHIHIRISHIA** Yaani: Niliwalingania nikiwawekea wazi wito. **NA NILIWAFANYIA SIRI SANA** Niliwahubiria kwa siri. Mtu alikuwa anamlingania mtu baada ya mtu; anazungumza naye kwa siri kati yake na mtu huyo. Mtume Nuhu aliwalingania watu wake kwa kutumia njia mbali mbali na mbinu tofauti. Imesemwa pia kwamba maana ya "NILIWAFANYIA SIRI" ni "Niliwaendea majumbani mwao nikawalingania humo".

(10) **NIKASEMA: MUOMBENI MSAMAHA MOLA WENU** Yaani: Muombeni msamaha kutokana na madhambi yenu yaliyotangulia, kwa kuitakasa nia. **HAKIKA, YEYE AMEKUWA MWINGI WA KUSAMEHE** Yeye ni mwingi wa kuwasamehe wenye makosa.

(11) **ATAPELEKA MAWINGU KWENU YAKITIRIRISHA MAJI SANA** Yenye kutiririsha sana ni kuchiriza kwa wingi, na huko ni kule kujikamua kwa mvua. Katika aya hii, kuna dalili ya kwamba kuomba msamaha ni miongoni mwa sababu kubwa za kupata mvua na kupata aina mbali mbali za riziki.

(12) **ATAKUSAIDIENI KWA MALI NA WATOTO, NA ATAKUFANYIENI BUSTANI NA ATAKUFANYIENI MITO** Atazifanya nyingi mali zenu na watoto wenu. Kumwamini kwao Mwenyezi Mungu kunawakusanyia wao rutuba na utajiri duniani pamoja na fungu kubwa huko Akhera.

(13) **MNA NINI NYINYI, HAMTARAJI UTUKUFU WA MWENYEZI MUNGU?** Mna nini hamumuogopi Mwenyezi Mungu na kwa hiyo, mkampwekesha na mkamtii?

(14) **NA ILHALI AMEKUUMBENI HATUA BAADA YA HATUA?** Amekuumbeni kupitia hatua mbali mbali; kutoka tone la manii, kisha pande la damu, kisha pande la nyama mpaka maumbile kukamilika, kama ufafanuzi wake ulivyotangulia kuelezwa katika *Suuratul Muuminuun*. Halafu mtakuwa watoto, halafu

يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُم مِّدْرَارًا ﴿١١﴾ وَيُمْدِدْكُم بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ وَيَجْعَل
لَّكُمْ جَنَّاتٍ وَيَجْعَل لَّكُمْ أَنْهَارًا ﴿١٢﴾ مَّا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٣﴾
وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١٤﴾ أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ
طِبَاقًا ﴿١٥﴾ وَجَعَلَ الْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ الشَّمْسَ سِرَاجًا ﴿١٦﴾
وَاللَّهُ أَنبَتَكُم مِّنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا ﴿١٧﴾ ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجُكُمْ
إِخْرَاجًا ﴿١٨﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ بِسَاطًا ﴿١٩﴾ لِّتَسْلُكُوا مِنْهَا
سُبُلًا فِجَاجًا ﴿٢٠﴾ قَالَ نُوحٌ رَّبِّ إِنَّهُمْ عَصَوْنِي وَاتَّبَعُوا مَن لَّمْ يَزِدْهُ
مَالُهُ وَوَلَدُهُ إِلَّا خَسَارًا ﴿٢١﴾ وَمَكَرُوا مَكْرًا كُبَّارًا ﴿٢٢﴾ وَقَالُوا
لَا تَذَرُنَّ آلِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَلَا سُوَاعًا وَلَا يَغُوثَ وَيَعُوقَ
وَنَسْرًا ﴿٢٣﴾ وَقَدْ أَضَلُّوا كَثِيرًا وَلَا تَزِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا ضَلَالًا ﴿٢٤﴾
مِّمَّا خَطِيئَاتِهِمْ أُغْرِقُوا فَأُدْخِلُوا نَارًا فَلَمْ يَجِدُوا لَهُم مِّن دُونِ
اللَّهِ أَنصَارًا ﴿٢٥﴾ وَقَالَ نُوحٌ رَّبِّ لَا تَذَرْ عَلَى الْأَرْضِ مِنَ الْكَافِرِينَ
دَيَّارًا ﴿٢٦﴾ إِنَّكَ إِن تَذَرْهُمْ يُضِلُّوا عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوا إِلَّا فَاجِرًا
كَفَّارًا ﴿٢٧﴾ رَّبِّ اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَن دَخَلَ بَيْتِيَ
مُؤْمِنًا وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَلَا تَزِدِ الظَّالِمِينَ إِلَّا تَبَارًا ﴿٢٨﴾

vijana, halafu wazee. Sasa vipi mnazembea kumtukuza yule ambaye amekuumbeni katika hatua hizi za ajabu?

(15) **HIVI HAMKUONA NAMNA MWENYEZI MUNGU ALIVYOUMBA MBINGU SABA ZIKIWA KATIKA TABAKA?** Zenye kupangana; baadhi yake zikiwa juu ya baadhi nyingine.

(16) **NA AMEUFANYA MWEZI HUMO** Yaani: Katika mbingu hizo, na mwezi huo upo katika mbingu iliyo karibu. **UKIWA UNATOA MWANGAZA** Unauangazia uso wa ardhi, ikiwa hamna joto ndani yake. **NA JUA AMELIFANYA TAA** Amelifanya jua kama taa kwa watu wa ardhini, ili kwa taa hiyo wafikie kwenye kufanya mambo ya maisha wanayoyahitajia. Ndani ya jua mna joto na mwangaza.

(17) **NA MWENYEZI MUNGU AMEKUOTESHENI KUTOKANA NA ARDHI KAMA MMEA** Mwenyezi Mungu anakusudia Adam, kwa kuwa alimuumba kutokana na uso wa ardhi. Kisha akaukuza mche wake katika ardhi kwa ukubwa baada ya udogo na urefu baada ya ufupi. Kwa hakika, Mwenyezi Mungu amewakuza wanadamu kwa sehemu za ardhi wanazokula baada ya kubadilika na kuwa mimea au wanyama.

(18) **KISHA ATAKURUDISHENI HUMO** Yaani: Atakurudisheni ardhini. Mtakufa na, kwa hiyo, viungo vyenu vitaachana mpaka virudi viwe mchanga na kujichanganya na ardhi. **NA ATAKUTOENI TU** Yaani: Atakutoeni katika hiyo ardhi kwa kukufufueni siku ya Kiyama. Atakutoeni mara moja, sio kwa kukuotesheni hatua kwa hatua kama mara ya kwanza.

(19) **NA MWENYEZI MUNGU AMEKUFANYIENI ARDHI KUWA TANDIKO** Yaani: Ameitandika na kuitandaza. Mnageuka geuka juu yake kama mnavyogeuka geuka juu ya mazulia yenu majumbani mwenu.

(20) **ILI MPITE HUMO NJIA PANA** Yaani: Njia zilizo pana. "FAJJ" Ni njia iliyo kati ya milima miwili.

(21) **NUHU ALISEMA: EWE MOLA WANGU, HAKIKA, WAO WAMENIASI** Yaani: Wameendelea kuniasi na hawakuuitika wito wangu. Nuhu amewashitaki watu wake kwa Mwenyezi Mungu, na yeye analijua zaidi hilo. **NA WAMEMFUATA YULE AMBAYE MALI YAKE NA WATOTO WAKE HAWAMZIDISHII ISIPOKUWA HASARA TU** Yaani: Wadogo wamewafuata viongozi wao na wenye utajiri katika wao na ambao wingi wa mali na watoto haukuwaongozea isipokuwa upotevu hapa duniani na adhabu huko akhera.

(22) **NA WALIFANYA VITIMBI VIKUBWA SANA** Yaani: Vitimbi vikubwa sana, ambavyo ni kuwashakiza watu wao wa chini juu ya kumuua Mtume Nuhu.

(23) **NA WALISEMA:** Viongozi kuwaambia wafuasi wakiwashawishi kumuasi Mtume Nuhu: **MSIWAACHE KABISA WAUNGU WENU** Msiache kuwaabudu waungu wenu, na waungu hao ni masanamu na mapicha ambayo walikuwa nayo, kisha Waarabu waliyaabudu baada yao. **NA MSIMWACHE KABISA WADI NA SUWAA NA YAGHUTHi NA YAUKA NA NASRI** Yaani: Msiache kuyaabudu masanamu haya. Muhammad Bin Ka'abi amesema kuwa: "Haya ni majina ya watu wema ambao walikuwepo kati ya Adamu na Nuhu. Baada yao, wakatokea watu waliokuwa wakiwafuata katika kuabudu. Ibilisi akawaambia: Lau mngelitengeza picha zao, jambo hilo lingekuhamasisheni na kukuchangamsheni sana katika kuabudu. Wakafanya hivyo. Kisha wakatokea watu wengine baada yao. Ibilisi akawaambia: *"Watu waliokuwepo kabla yenu, walikuwa wanayaabudu masanamu haya. Kwa hiyo, na nyinyi yaabuduni"* na huo ndio ulikuwa *mwanzo wa kuabudiwa masanamu".*

24 **NA KWA HAKIKA, WAMEWAPOTEZA WATU WENGI** Viongozi na wakubwa wao wamewapotosha watu wengi. Imesemwa pia kwamba muradi ni msanamu. Yamewapotosha watu wengi. **NA USIWAONGEZEE MADHALIMU ISIPOKUWA UPOTEVU TU** Yaani: Usiwaongezee madhalimu ila hasara tu. Imesemwa pia kwamba: Usiwaongezee ila upotevu katika vitimbi vyao.

25 **KUTOKANA NA MAKOSA YAO, WALIGHARIKISHWA** Yaani: Kwa ajili ya makosa yao waliangamizwa kwa Tufani. **NA WAKATIWA MOTONI** Wakatiwa motoni baada ya hapo, nao ni moto wa akhera. Imesemwa pia kuwa moto ni adhabu ya kaburini. **HIVYO, HAWAKUJIPATIA WA KUWANUSURU BADALA YA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Hawakumpata yeyote wa kuwakinga adhabu ya Mwenyezi Mungu.

26 **NA NUHU ALISEMA: EWE MOLA WANGU, USIACHE JUU YA ARDHI MKAZI YEYOTE KATIKA MAKAFIRI** Mtume Nuhu alipokata tamaa ya watu wake kuamini, aliwaapiza (aliwaombea dua mbaya) baada ya kuwa amepewa ufunuo unaosema kwamba: "*Hawataamini katika wao isipokuwa tu wale ambao wamekwisha amini*". Mwenyezi Mungu aliyakubali maombi yake na akawangamiza kwa gharika.

27 **KWA YAKINI, WEWE UKIWAACHA, WATAWAPOTEZA WAJA WAKO** Watawapotosha waikose njia ya haki. **NA HAWATAZAA ILA MUOVU** Yaani: Hawatazaa ila tu mtu muovu kwa kuacha kukutii. **MWINGI WA KUKUFURU** Mwingi wa kuzikufuru neema zako.

28 **EWE MOLA WANGU, NISAMEHE MIMI NA WAZAZI WANGU** Na walikuwa waumini. **NA ATAKAYEINGIA NYUMBANI MWANGU** Nyumba yake ambayo alikuwa akikaa humo. Imesemwa pia kwamba ni jahazi lake. **AKIWA MUUMINI** Anatoka katika maombi haya yule ambaye ataingia katika nyumba yake akiwa hana sifa ya imani, kama vile mke wake na mtoto wake ambaye alisema: "NITAJIHIFADHI KWENYE MLIMA UTAKAONIKINGA NA MAJI". *Suurat Huud (11) aya 43*. **NA WAUMINI WANAUME NA WAUMINI WANAWAKE** Yaani: Nakuomba umsamehe kila mwanaume na mwanamke mwenye kusifika na sifa ya imani. **NA USIWAONGEZEE MADHALIMU ILA TU HASARA** Hilaki, hasara kuporomoka. Maombi yake haya yanamhusu kila dhalimu mpaka siku ya Kiyama.

# SUURATUL JINN (72)

Imeteremka Makka Aya zake
ni ishirini na nane (28)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

1 **SEMA: PAMEFUNULIWA KWANGU** Maana ni kwamba: Sema ewe Muhammad kuwaambia uma wako kuwa Mwenyezi Mungu ameleta ufunuo kwangu kupitia ulimi wa Jibrili **"KWAMBA KUNDI KATIKA MAJINI LILISIKILIZA";** yaani idadi fulani miongoni mwao walisikiliza kusoma kwangu Kur'ani. Sura ambayo Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa anaisoma ni *Suurat Iqra'* "SOMA KWA JINA LA MOLA WAKO AMBAYE AMEUMBA" Sura Al'alaq. Mwenyezi Mungu hakupeleka kwao Mjumbe katika wao, kwani Mitume wote wanatokana na binadamu. **WAKASEMA: KWA YAKINI, SISI TUMEISIKIA QUR'ANI YENYE KUSTAAJABISHA** Walisema kuwaambia watu wao waliporejea kwao kwamba: Tumesikia maneno yenye kusomwa, yenye kustaajabisha katika ufasaha wake. Imesemwa pia: Qur'ani ni yenye kustaajabisha katika mawaidha yake, na imesemwa pia kuwa ni yenye kustaajabisha katika baraka zake.

2 **INAELEKEZA KWENYE UONGOFU** Yaani: Inaongoza kwenye haki, sawa na kumjua Mwenyezi Mungu. **KWA HIYO TUKAIAMINI** Yaani: Tumeamini kwamba Qur'ani inatoka kwa Mwenyezi Mungu. **NA HATUTAMSHRIKISHA YEYOTE NA MOLA WETU** Hatutamshirikisha Mwenyezi Mungu na yeyote katika viumbe vyake. Hatutafanya Mungu mwengine pamoja naye. Majini waliamini kwa kuisikia Qur'ani mara moja, na walielewa kwa akili zao kwamba Qur'ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu, na makafiri wa Kiquraishi na hasa viongozi wao hawakunufaika pamoja na: **1)**Kuisikia Qurani mara nyingi sana, **2)** Mtume anatokana na wao na anaisoma Qur'ani kwa lugha yao. Ni hakika kabisa kuwa Mwenyezi Mungu amewaangusha muangusho wa kudhalilisha sana na amewauwa mauaji mabaya sana. Katika aya hii, kuna mafunzo kwamba jambo kubwa zaidi lililomo katika mahubiri ya Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuepukana na ushirikina na washirikina.

3 **NA KWAMBA HALI ILIVYO NI KUWA UMETUKUKA UTUKUFU WA MOLA WETU** Umetukuka utukufu na ukubwa wa Mola wetu. Imesemwa pia kwamba: Umetukuka uwezo wake. **HAKUFANYA MKE WALA MTOTO** Umetakasika utukufu na ukubwa wa Mola wetu na ameepukana na kufanya mke au mtoto, kama makafiri ambao wanamnasibishia

ترتيبها ٧٢ — سُورَةُ الجِنِّ — آياتها ٢٨

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ ٱسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ ٱلْجِنِّ فَقَالُوٓا۟ إِنَّا سَمِعْنَا قُرْءَانًا
عَجَبًا ﴿١﴾ يَهْدِىٓ إِلَى ٱلرُّشْدِ فَـَٔامَنَّا بِهِۦ ۖ وَلَن نُّشْرِكَ بِرَبِّنَآ أَحَدًا ﴿٢﴾
وَأَنَّهُۥ تَعَٰلَىٰ جَدُّ رَبِّنَا مَا ٱتَّخَذَ صَٰحِبَةً وَلَا وَلَدًا ﴿٣﴾ وَأَنَّهُۥ كَانَ
يَقُولُ سَفِيهُنَا عَلَى ٱللَّهِ شَطَطًا ﴿٤﴾ وَأَنَّا ظَنَنَّآ أَن لَّن تَقُولَ ٱلْإِنسُ
وَٱلْجِنُّ عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا ﴿٥﴾ وَأَنَّهُۥ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ ٱلْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ
مِّنَ ٱلْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا ﴿٦﴾ وَأَنَّهُمْ ظَنُّوا۟ كَمَا ظَنَنتُمْ أَن لَّن يَبْعَثَ
ٱللَّهُ أَحَدًا ﴿٧﴾ وَأَنَّا لَمَسْنَا ٱلسَّمَآءَ فَوَجَدْنَٰهَا مُلِئَتْ حَرَسًا
شَدِيدًا وَشُهُبًا ﴿٨﴾ وَأَنَّا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقَٰعِدَ لِلسَّمْعِ ۖ فَمَن
يَسْتَمِعِ ٱلْـَٔانَ يَجِدْ لَهُۥ شِهَابًا رَّصَدًا ﴿٩﴾ وَأَنَّا لَا نَدْرِىٓ أَشَرٌّ أُرِيدَ
بِمَن فِى ٱلْأَرْضِ أَمْ أَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ﴿١٠﴾ وَأَنَّا مِنَّا ٱلصَّٰلِحُونَ
وَمِنَّا دُونَ ذَٰلِكَ ۖ كُنَّا طَرَآئِقَ قِدَدًا ﴿١١﴾ وَأَنَّا ظَنَنَّآ أَن لَّن نُّعْجِزَ
ٱللَّهَ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَن نُّعْجِزَهُۥ هَرَبًا ﴿١٢﴾ وَأَنَّا لَمَّا سَمِعْنَا ٱلْهُدَىٰٓ
ءَامَنَّا بِهِۦ ۖ فَمَن يُؤْمِنۢ بِرَبِّهِۦ فَلَا يَخَافُ بَخْسًا وَلَا رَهَقًا ﴿١٣﴾

Mwenyezi Mungu mke na mtoto wanavyosema.

(4) **NA KWAMBA HALI ILIVYO NI KUWA: WAPUMBAVU WETU WALIKUWA WAKISEMA JUU YA MWENYEZI MUNGU MANENO YALIYOPINDUKIA MIPAKA** Majini wanakanusha maneno ya washirikina katika wao na wajinga wao kusema urongo juu ya Mwenyezi Mungu kwa kudai kuwa ana mke na mtoto na madai mengine yasiyokuwa hayo. Maneno yaliyopindukia mipaka ni ukafiri wa kiwango cha juu, kuwa kando ya makusudio na kupindukia mipaka.

(5) **NA HAKIKA, SISI TULIDHANI KUWA WATU NA MAJINI HAWATASEMA UONGO JUU YA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Sisi tulidhani kuwa watu na majini walikuwa hawasemi urongo juu ya Mwenyezi Mungu pale waliposema kuwa Mwenyezi Mungu ana mshirika na ana mke na mtoto, na kwa hiyo, sisi tukawaamini katika hilo. Haikupita katika mioyo yetu kuwa kuna yeyote anayejasiri kusema urongo juu ya Mwenyezi Mungu kama walivyofanya wahubiri wa kumshirikisha Mwenyezi Mungu na wahudumu wa Miungu bandia, mpaka tulipoisikia Kur,ani. Hapo, ndipo tukaelewa ubatilifu wa ukweli tuliokuwa tunaudhani kwao.

(6) **NA KWAMBA HALI ILIVYO NI KUWA: WANAUME KATIKA WATU WALIKUWA WANAJIKINGA KWA WANAUME KATIKA MAJINI** Mtu katika Waarabu alipokuwa akifika katika jangwa fulani anasema: "*Naomba hifadhi kwa Bwana wa jangwa hili anikinge dhidi ya shari ya watu wake wajinga"*. Basi hulala katika dhamana yake mpaka asubuhi.

**WAKAWAONGEZEA BALAA** Wanaume katika majini wakawaongezea wanaume wa kibanadamu upumbavu kutoka kwa majini wenyewe juu ya binadamu wenye kutaka hifadhi kwa majini hao. Au maana ni kwamba waliwaongezea balaa, udhaifu na hofu.

(7) **NA KWA YAKINI, WAO WALIDHANI KAMA MLIVYODHANI NYINYI KWAMBA MWENYEZI MUNGU HATAMFUFUA YEYOTE** Maana ni kwamba watu walidhani kama mlivyodhani nyinyi majini kwamba hakuna kufufuliwa na hakuna malipo yoyote.

(8) **NA KWA YAKINI, SISI TULIZIGUSA MBINGU** Yaani: Sisi tulizitafuta habari za mbinguni kama ilivyokuwa kawaida yetu, **TUKAZIKUTA ZIMEJAZWA WALINZI** Zimejazwa walinzi wa Kimalaika wanazilinda dhidi ya kuibia kusikiliza. **WENYE NGUVU** Walinzi wenye nguvu. **NA VIMWENGE** Vimwenge ni moto wa nyota kama ufafanuzi wake ulivyotangulia katika kufasiri kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa "**NA TUKAZIFANYA VIPIGIO VYA MASHETANI**" katika *Suurat Tabaaraka, aya 5.*

(9) **NA KWAMBA KWA YAKINI, SISI TULIKUWA TUKIKAA KATIKA HIZO MBINGU KATIKA MAKAO KWA AJILI YA KUSIKILIZA** Ili wasikie kutoka kwa Malaika habari za mbinguni na wazifikishe kwa wachawi na makuhani. Wakati Mwenyezi Mungu alipomtuma Mtume wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akazilinda mbingu kwa kutumia vimwenge vinavyounguza. **BASI YEYOTE ATAKAYESIKILIZA HIVI SASA, ATAJIPATIA KIMWENGE CHENYE KUVIZIA** Yaani: Kimwenge kinachomvizia ili kimtupe na kumzuia asisikilize.

(10) **NA KWA YAKINI, SISI HATUJUI; NI SHARI IMEKUSUDIWA KWA WALIOMO KATIKA ARDHI** Kwa ulinzi huu wa mbingu **AU MOLA WAO AMEWATAKIA UONGOFU?** Yaani: Au Mola wao amekusudia heri kwao? Ibn-zaid Amesema kuwa: "*Alisema Ibilisi kwamba: Hatujui, Mwenyezi mungu kwa kuzuia huku amekusudia kuteremsha adhabu kwa waliomo katika ardhi au amekusudia*

*kuwapelekea mjumbe?".*

(11) **NA KWA YAKINI, KATIKA SISI WAPO WALIOKUWA WEMA** Yaani: Baadhi ya majini walisema kuwaambia baadhi yao wakati walipowalingania wenzao wamwamini Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: Kabla ya kuisikiliza Qurani, walikuwepo miongoni mwetu waliokuwa wakisifika kwa wema. **NA KATIKA SISI WAPO AMBAO HAWAKO HIVYO** Yaani: Na miongoni mwetu kuna kundi ambalo haliko hivyo. Imesemwa pia kwamba: kwa **WALIOKUWA WEMA** Mwenyezi Mungu amewakusudia waumini, na kwa **AMBAO HAWAKO HIVYO** amewakusudia makafiri. **TULIKUWA NJIA MBALI MBALI** Yaani: Tulikuwa makundi mbali mbali, aina tofauti na mielekeo mbali mbali. Saidi amesema kwamba: *Walikuwa Waislamu, Wayahudi, Wakristo na Majusi* (wanaoabudu moto).

(12) **NA KWA YAKINI, SISI TULIKUWA TUNADHANI KWAMBA HATUTAMSHINDA MWENYEZI MUNGU KATIKA ARDHI** Yaani: Na sisi tulijua kwamba hatuwezi kumtoroka Mwenyezi Mungu akitaka kwetu jambo. **NA HATUTAMSHINDA KWA KUKIMBIA** Yaani: Hatuwezi kumkimbia.

(13) **NA KWA YAKINI, SISI WAKATI TULIPOUSIKIA UONGOFU** Wanakusudia: Qur'ani. **TULIUAMINI.** Tuliiamini kuwa inatoka kwa Mwenyezi Mungu, na hatukuikanusha kama wanadamu makafiri walivyoikanusha. **KWA HIYO, YEYOTE MWENYE KUMWAMINI MOLA WAKE, HAOGOPI KUPUNJWA WALA KUTWIKWA** Kupunjwa ni kupunguziwa na kutwikwa inakusudiwa kufanyiwa uadui na udhalimu.

(14) **NA KWA YAKINI, KATIKA SISI WAPO WAISLAMU, NA KATIKA SISI WAPO WAKENGEUKAJI** Wakengeukaji ni madhalimu jasiri ambao wameikwepa njia ya haki. **BASI WENYE KUSILIMU, HAO WAMEUKUSUDIA UONGOFU** Yaani: Wameikusudia njia ya haki na ya kheri, wametoa juhudi katika kuitafuta mpaka wakawawezeshwa kuifata.

(15) **AMA WAKENGEUKAJI, WAMEKUWA KUNI ZA JAHANAMU** Yaani: Watakuwa kuni za moto utakaowashwa kwa miili yao kama utakavyowashwa kwa miili ya makafiri wanadamu.

(16) **NA KWAMBA LAU WANGENYOOKA JUU YA NJIA** Maana ni kwamaba: Nimeletewa ufunuo kuwa mambo yalivyo ni kwamba lau kama majini au watu au wote kwa pamoja wangesimama sawa sawa juu ya njia ya Uislamu, Tungewanywesha maji **TUNGEWANYWESHA MAJI MENGI** mengi na tungewapa heri nyingi na wasaa.

(17) **ILI TUWAJARIBU KATIKA HILO** Yaani: Ili tuwajaribu na, kwa hiyo, tujue zikoje shukurani zao juu ya neema hizo. **NA YEYOTE MWENYE KUPUUZA UTAJO WA MOLA WAKE, ATAMWINGIZA KATIKA ADHABU NGUMU** Yaani: Na yeyote mwenye kuipuuza Qur'ani au mawaidha, Mwenyezi Mungu atamuingiza katika adhabu kali, ngumu.

(18) **NA KWA YAKINI, MISIKITI NI YA MWENYEZI MUNGU.** Yaani: Na nimeletewa ufunuo kwamba misikiti inahusika na Mwenyezi Mungu. Saidi amesema kwamba: *"Majini walisema: Vipi itawezekana kwenda misikitini na kusali pamoja nawe na ilhali sisi tuko mbali na wewe? Hapo, ndio ikashuka aya hii".* Imesemwa pia kuwa misikiti ni maeneo yote ya ardhi, kwa sababu ardhi yote ni msikiti. **KWA HIYO, MSIMUOMBE YEYOTE PAMOJA NA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Katika mambo ambayo hakuna ayawezaye ila Mwenyezi Mungu tu msimuombe msaada yeyote katika viumbe wake, vyovyote atakavyokuwa, kwani kuomba ni Ibada.

(19) **NA ILIVYO NI KWAMBA MJA WA MWENYEZI MUNGU ALIPOSIMAMA** Naye ni Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. **AKIMUOMBA** Akimuomba Mwenyezi Mungu na kumwabudu. Tukio hilo lilikuwa mahali panapoitwa *Bathnin-nakhla* kama ilivyo tangulia kuelezwa. **WALIKARIBIA KUSONGAMANA KWAKE** Majini walikaribia kuwa juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na wakiwa wamepandana kutokana na kusongamana kwao juu yake kwa kuisikiliza Qura'ni kutoka kwake. Imesemwa pia kwamba makusudio ni kwamba Majini na wanadamu walijumuika juu ya jambo hili la Uislamu ili walizime, na Mwenyezi Mungu akakataa ila tu kuunusuru Uislamu na kuitimiza nuru yake.

(20) **SEMA: HAPANA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA NINAMUOMBA MOLA WANGU** Na ninamuabudu. **NA SIMSHIRIKISHI NAYE YEYOTE** Simshirikishi naye kiumbe wake yeyote. Sababu ya kushuka kwa ya hii ni kwamba makafiri wa Kiquraishi walimwambia Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: Hakika, wewe umekuja na jambo kubwa na watu wote umewafanyia uadui. Kwa hiyo, rejea uliache jambo hili. Sisi tutakulinda.

(21) **SEMA: KWA YAKINI, MIMI SIMILIKI KWENU MADHARA WALA UONGOFU** Yaani: Siwezi kukuondoleeni madhara wala kukueteeni heri katika dunia au dini.

وَأَنَّا مِنَّا الْمُسْلِمُونَ وَمِنَّا الْقَاسِطُونَ ۖ فَمَنْ أَسْلَمَ فَأُولَٰئِكَ
تَحَرَّوْا رَشَدًا ﴿١٤﴾ وَأَمَّا الْقَاسِطُونَ فَكَانُوا لِجَهَنَّمَ حَطَبًا ﴿١٥﴾
وَأَلَّوِ اسْتَقَامُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ لَأَسْقَيْنَاهُم مَّاءً غَدَقًا ﴿١٦﴾ لِّنَفْتِنَهُمْ
فِيهِ ۚ وَمَن يُعْرِضْ عَن ذِكْرِ رَبِّهِ يَسْلُكْهُ عَذَابًا صَعَدًا ﴿١٧﴾ وَأَنَّ
الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾ وَأَنَّهُ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ
يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿١٩﴾ قُلْ إِنَّمَا أَدْعُو رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ
بِهِ أَحَدًا ﴿٢٠﴾ قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَلَا رَشَدًا ﴿٢١﴾ قُلْ إِنِّي
لَن يُجِيرَنِي مِنَ اللَّهِ أَحَدٌ وَلَنْ أَجِدَ مِن دُونِهِ مُلْتَحَدًا ﴿٢٢﴾ إِلَّا بَلَاغًا
مِّنَ اللَّهِ وَرِسَالَاتِهِ ۚ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ
خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ﴿٢٣﴾ حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا مَا يُوعَدُونَ فَسَيَعْلَمُونَ
مَنْ أَضْعَفُ نَاصِرًا وَأَقَلُّ عَدَدًا ﴿٢٤﴾ قُلْ إِنْ أَدْرِي أَقَرِيبٌ
مَّا تُوعَدُونَ أَمْ يَجْعَلُ لَهُ رَبِّي أَمَدًا ﴿٢٥﴾ عَالِمُ الْغَيْبِ فَلَا
يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ فَإِنَّهُ
يَسْلُكُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ رَصَدًا ﴿٢٧﴾ لِّيَعْلَمَ أَن قَدْ أَبْلَغُوا
رِسَالَاتِ رَبِّهِمْ وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿٢٨﴾

(22) **SEMA: KWA YAKINI, MIMI HATANIKINGA YEYOTE NA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Hakuna yeyote atakayenikinga isinipate adhabu ya Mwenyezi Mungu iwapo atanishushia. **NA SITAPATA PASIPOKUWA KWAKE MAKAO SALAMA** Yaani: Na sitapata pasipokuwa kwake mahali pa kukimbilia, mahali pa kutegemea na hifadhi.

(23) **ISIPOKUWA TU KUFIKISHA KUTOKA KWA MWENYEZI MUNGU NA UJUMBE WAKE.** Yaani: Similiki ila tu kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na kuufanyia kazi ujumbe wake. Ninailazimisha nafsi yangu kufanya yale ambayo ninamuamuru mwengine. Nikifanya hivyo, nimeokoka na vinginevyo nimeangamia. **NA YEYOTE ATAKAYE MUASI MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE, HAKIKA HUYO ATAPATA MOTO WA JAHANNAMU AKIISHI HUMO MILELE**

(24) **MPAKA WATAKAPOYAONA YALE WANAYOAHIDIWA, HAPO WATAJUA KUWA: NI NANI MNYONGE ZAIDI WA KUNUSURU?** Watajua ni nani mwenye askari wanyonge zaidi atakaojinusuru kwao.. **NA MWENYE IDADI CHACHE ZAIDI?** Je, mchache wa idadi zaidi ni wao au Waislamu?

(25) **SEMA: KWA YAKINI, MIMI SIJUI; JE, YAKO KARIBU YALE MNAYOAHIDIWA** Sijui ukaribu wa adhabu ambayo Mwenyezi Mungu anakuahidini. **AU MOLA WANGU ATAYAFANYIA MUDA** Yaani: Au Mola wangu ameyawekea ukomo na muda na, kwa hiyo, hakuna ajuaye ni lini siku ya Kiyama ila Mwenyezi Mungu peke yake.

(26) **MJUZI WA GHAIBU. HAMUONESHI YEYOTE GHAIBU YAKE** Hamuoneshi Ghaibu yeyote katika waja. Ghaibu ni yale mambo ambayo yako mbali na waja (hawayaoni kwa macho).

(27) **ILA TU MTUME ALIYEMRIDHIA** Mwenyezi Mungu amewatoa Mitume aliowaridhia. Kwa njia ya ufunuo kwao, amewapa amana ya Ghaibu aliyoiataka. Na Ghaibu hiyo ameifanya kuwa ni muujiza kwao na ushahidi wa kweli juu utume wao, sio mnajimu na mwenye kufanana naye, ikiwa ni pamoja na: wanaopiga ramli, wenye kutazama katika vitanga vya mikono, wenye kuzuia (watu kufanya mambo yao) kwa (sababu ya nuksi na mkosi wa) ndege ambao mtu amewaridhia. Hao ni wenye kumkufuru Mwenyezi Mungu na wenye kumzulia kwa sababu ya dhana zao na urongo wao. **KWANI YEYE HUPELEKA MBELE YAKE NA NYUMA YAKE WALINZI** Mwenyezi Mungu Mtukufu hujaalia mbele ya Mitume na nyuma yake walinzi wa Kimalaika wanaomlinda na mashetani wasiingilie ile Ghaibu anayomuonesha na wanamzunguka wakimkinga dhidi ya mashetani wasiibie na kuyapeleka kwa wachawi

(28) **ILI AJUE KWAMBA WAMEFIKISHA UJUMBE WA MOLA WAO** Yaani: Ili Mwenyezi Mungu ajue kuwa Mitume wake wamefikisha ujumbe wake. Ili alijue hilo kwa kuona kama alivyolijua hilo kwa Ghaibu. **AMEYAZUNGUKA YALE AMBAYO YAKO MBELE YAO NA AMEKIDHIBITI KILA KITU KWA IDADI** na ameyazunguka yaliyo kwa walinzi katika malaika, au yale ambayo yako mbele za Mitume ambao wanaufikisha ujumbe wake, na pia anazijua hali walizonazo.

## SUURATUL MUZZAMMIL (73)

Imeteremka Makka aya zake ni ishirini (20)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

(1) **EWE MWENYE KUJIFUNIKA** Usemeshwaji huu umeelekezwa kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Mwanzo kabisa Jibrili alipokuwa akimletea

Mtume wahyi alikuwa anajifunika kwa kumuogopa. Aliposikia sauti ya Malaika na kumuangalia, ilimshika hofu na hivyo akenda kwa mkewe na kumwambia: *"Nifunikeni, nifunikeni"*. Halafu baada ya hapo, akawa anasemeshwa kwa sifa ya utume na ujumbe na akamzoea Jibrili.

(2) **SIMAMA USIKU ISIPOKUWA SEHEMU CHACHE** Yaani: Simama ili uswali usiku. Swali usiku wote isipokuwa sehemu ndogo ya usiku huo.

(3) **NUSU YAKE AU PUNGUZA KIDOGO KWENYE NUSU HIYO**

(4) **AU ONGEZA JUU YAKE NA ISOME QUR'ANI VILIVYO** Kana kwamba amesema: Simama theluthi mbili za usiku au nusu yake au theluthi yake. Imam Ahmad na Muslim wamenakili kutoka kwa Saad bin Hishaam akisema kuwa: "Nilimwambia Aisha: Nieleze kuhusu kusimama (kuswali) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, usiku, akasema: *Kwani husomi sura hii* "EWE MWENYE KUJIFUNIKA"*? Nikasema: Ninaisoma. Akasema: Mwenyezi Mungu amewajibisha kusimama usiku mwanzoni mwa sura hii. Kwa hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu na Swahaba wake walisimama usiku kwa muda wa mwaka mmoja mpaka miguu yao ikavimba, na Mwenyezi Mungu akawa ameuzuia mbinguni mwisho wa sura hiyo miezi kumi na miwili. Halafu Mwenyezi Mungu akateremsha tahafifu mwisho wa sura hii. Kwa hiyo, kusimama usiku ikawa ni tendo la hiyari baada ya kuwa la lazima"*. **NA ISOME QUR'ANI VILIVYO** Yaani: Isome Kur'ani kwa utulivu, herufi kwa herufi pamoja na mazingatio. Kusoma vilivyo ni kuziweka bayana herufi zote na kuzishibisha haki yake bila ya kujikamua katika kutamka.

(5) **SISI TUTAKUTUPIA KAULI NZITO** Yaani: Tutakuletea wahyi wa Qur'ani. Kur'ani ni neno zito; mambo yake ya wajibu, mipaka yake, mambo yake ya halali na mambo yake ya haramu. Hakuna kinachohimili Qur'ani isipokuwa tu moyo uliotiwa nguvu kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na nafsi iliyopambwa kwa Tauhidi.

(6) **KWA YAKINI, KIZUSHI CHA USIKU** Kisimamo cha usiku kinaitwa (*Naashi'a* = kizushi) ikiwa kusimama huko ni baada ya kulala. Kama utalala mwanzo wa usiku, kisha ukaamka (kwa kufanya ibada) hicho ndio kisimamo cha usiku **NDICHO TU KIKANYAGO KIZITO ZAIDI** Ni kizito zaidi kwa mwenye kusali kuliko sala ya mchana, kwa sababu usiku ni kwa ajili ya kulala.

**NA KAULI NYOOFU ZAIDI** Yaani: Kina maneno muafaka zaidi na kisomo makini zaidi,

سُورَةُ المُزَّمِّلِ — ترتيبها ٧٣ — آياتها ٢٠

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمُزَّمِّلُ ١ قُمِ ٱلَّيۡلَ إِلَّا قَلِيلٗا ٢ نِّصۡفَهُۥٓ أَوِ ٱنقُصۡ مِنۡهُ قَلِيلًا
٣ أَوۡ زِدۡ عَلَيۡهِ وَرَتِّلِ ٱلۡقُرۡءَانَ تَرۡتِيلًا ٤ إِنَّا سَنُلۡقِي عَلَيۡكَ قَوۡلٗا
ثَقِيلًا ٥ إِنَّ نَاشِئَةَ ٱلَّيۡلِ هِيَ أَشَدُّ وَطۡـٔٗا وَأَقۡوَمُ قِيلًا ٦ إِنَّ لَكَ فِي
ٱلنَّهَارِ سَبۡحٗا طَوِيلٗا ٧ وَٱذۡكُرِ ٱسۡمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلۡ إِلَيۡهِ تَبۡتِيلٗا ٨
رَّبُّ ٱلۡمَشۡرِقِ وَٱلۡمَغۡرِبِ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ فَٱتَّخِذۡهُ وَكِيلٗا ٩ وَٱصۡبِرۡ
عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَٱهۡجُرۡهُمۡ هَجۡرٗا جَمِيلٗا ١٠ وَذَرۡنِي وَٱلۡمُكَذِّبِينَ
أُوْلِي ٱلنَّعۡمَةِ وَمَهِّلۡهُمۡ قَلِيلًا ١١ إِنَّ لَدَيۡنَآ أَنكَالٗا وَجَحِيمٗا ١٢
وَطَعَامٗا ذَا غُصَّةٖ وَعَذَابًا أَلِيمٗا ١٣ يَوۡمَ تَرۡجُفُ ٱلۡأَرۡضُ وَٱلۡجِبَالُ
وَكَانَتِ ٱلۡجِبَالُ كَثِيبٗا مَّهِيلًا ١٤ إِنَّآ أَرۡسَلۡنَآ إِلَيۡكُمۡ رَسُولٗا شَٰهِدًا
عَلَيۡكُمۡ كَمَآ أَرۡسَلۡنَآ إِلَىٰ فِرۡعَوۡنَ رَسُولٗا ١٥ فَعَصَىٰ فِرۡعَوۡنُ ٱلرَّسُولَ
فَأَخَذۡنَٰهُ أَخۡذٗا وَبِيلٗا ١٦ فَكَيۡفَ تَتَّقُونَ إِن كَفَرۡتُمۡ يَوۡمٗا يَجۡعَلُ
ٱلۡوِلۡدَٰنَ شِيبًا ١٧ ٱلسَّمَآءُ مُنفَطِرُۢ بِهِۦۚ كَانَ وَعۡدُهُۥ مَفۡعُولًا ١٨
إِنَّ هَٰذِهِۦ تَذۡكِرَةٞۖ فَمَن شَآءَ ٱتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِۦ سَبِيلًا ١٩

kwa ajili ya moyo kuwa hadhiri katika kisomo hicho. Pia kisomo cha kisimamo hicho kinakuwa kimemakinika zaidi kwa vile kipindi hicho sauti zimetulia na ulimwengu umetulia.

(7) **KWA YAKINI, UNAO WASAA MREFU MCHANA** Yaani: Unao wakati wa kutekeleza mahitaji yako; kwenda na kurudi, kwenda na kurudi. Kwa hiyo, usiku: swali.

(8) **NA LITAJE JINA LA MOLA WAKO** Usiku na mchana. Fanya hivyo kwa wingi. **NA JITUPE KWAKE KWELI KWELI** Yaani: Jisalimishe kwa Allah kikweli kweli kwa kushughulika na kumuabudu na kuyaomba yale yaliyoko kwake.

(9) **MOLA WA MASHARIKI NA MAGHARIBI. HAKUNA ANAYESTAHIKI KUABUDIWA ILA YEYE TU. KWA HIYO, MFANYE YEYE MTEGEMEWA** Yaani: Ukishajua kwamba yeye tu ndio muhusika na uungu, basi mfanye mtegemewa; yaani: msimamizi wa mambo yako, na mtegemee katika mambo yako yote.

(10) **NA VUMILIA JUU YA YALE WANAYOSEMA** Yakiwemo: Maudhi, matusi na kejeli. Hayo yasikuhuzunishe. **NA WAHAME UHAMAJI MZURI** Yaani: Usiwafanye lolote na

wala usijishughulishe na kuwarudi. Imesemwa pia kwamba uhamaji mzuri ni uhamaji usiokuwa na masikitiko. Haya yalikuwa kabla ya amri ya vita.

(11) **NA NIACHE MIMI NA WANAOPINGA** Yaani: Niache nao. Usishughulike nao. Mimi nitakutosheleza dhidi yao na nitawaadhibu kwa ajili yako. **WENYE NEEMA** Yaani: Wenye utajiri, nafasi, anasa na starehe duniani. **NA WAPE MUDA KIDOGO** Mpaka hapo muda wao utakapo malizika. Imesemwa pia kwamba: Mpaka hapo itakapo wateremkia adhabu ya duniani.

(12) **KWA YAKINI, KWETU KUNA MAKONGWA** Makongwa ni pingu. Pia imesemwa kuwa makusudio ya makongwa ni aina za adhabu kali. **NA MOTO** Yaani: Moto uliobimbirishwa.

(13) **NA CHAKULA CHENYE KUSAKAMA** Yaani: Hakipiti kirahisi kooni, bali kinakwama; hakishuki wala hakitoki. **NA ADHABU IUMIZAYO** Yaani: Na kuna aina nyingine za adhabu mbali ya hiyo iliyotajwa.

(14) **SIKU ITAKAPOTETEMEKA ARDHI NA MILIMA** Itatikisika na kuwatingisha waliopo juu yake. Kutetemeka ni mtingishiko mkubwa. **NA MILIMA IKAWA KAMA CHUNGU YA MCHANGA ULIOACHIANA** Yaani: Milima itakuwa hivyo. Chungu ya mchanga ni changarawe zilizo rundikana. Na ulioachiana ni mchanga unakanyagika; yaani changarawe laini kutokana na uzito wa tetemeko.

(15) **SISI TUMEKULETEENI MTUME AKIWA SHAHIDI JUU YENU** Atakuwa shahidi juu yenu siku ya Kiyama kwa matendo yenu. Yaani: kama Mkimuasi. **KAMA TULIVYOMPELEKEA FIRAUNI MTUME** Yaani: Musa.

(16) **FIRAUNI AKAMUASI MTUME** Na akamkataa na hakuyaamini yale aliyokuja nayo. **NA, KWA HIYO, TUKAMSHIKA MSHIKO MKALI** Yaani: Mshiko mkali, mzito na mkubwa. Maana yake ni kwamba: Tukamuadhibu Firauni adhabu kali na nzito kwa kumzamisha baharini.

(17) **VIPI MTAJIKINGA** Yaani: Vipi mtazikinga nafsi zenu. **IKIWA MTAKUFURU** Yaani: Ikiwa mtaendelea na ukafiri wenu. **SIKU** Yaani: Adhabu ya siku ambayo. **ITAWAFANYA WATOTO WADOGO WAWE WAZEE?** Kwa ukubwa wa misukosuko yake. Yaani: Watoto wadogo siku hiyo watakuwa wenye nywele nyeupe. Hili ni fumbo la hofu kubwa.

(18) **MBINGU ITACHANIKA KWAYO** Yaani: Itapasuka kwa siku hiyo kwa sababu ya ukubwa wake na ukubwa wa misukosuko yake. Kupasuka kwake ni kwa ajili ya kuteremka kwa Malaika. **AHADI YAKE IMETEKELEZWA** Yaani: Itakuwa. Hakuna pingamizi.

(19) **KWA YAKINI, HAYA** Yaani: Hizi aya zilizotangulia. **NI UKUMBUSHO** Ni mawaidha. **KWA HIYO, YEYOTE ANAYETAKA, ATATENGENEZA NJIA KWENDA KWA MOLA WAKE** Yaani: Atatengeneza njia itakayomfikisha kwenye radhi za Mwenyezi Mungu peponi kwa utiifu ambao aina yake muhimu zaidi ni kumpwekesha Allah (Tauhidi).

(20) **KWA YAKINI, MOLA WAKO ANAJUA KUWA WEWE UNASIMAMA CHINI ZAIDI YA THELUTHI MBILI ZA USIKU NA NUSU YAKE NA THELUTHI YAKE** Maana ni kwamba: Mwenyezi Mungu anajua kuwa Mjumbe wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, wakati mwengine anasimama chini zaidi ya theluthi mbili za usiku, anasimama nusu yake na anasimama theluthi yake. **NA KUNDI KATIKA WALE AMBAO WAKO PAMOJA NAWE** Yaani: Na kundi katika Swahaba wako linasimama kiwango hicho pamoja nawe. **NA MWENYEZI MUNGU ANAKADIRIA USIKU NA MCHANA** Yaani: Aanajua viwango vya usiku na mchana katika uhakika wake. Anajua kiwango ambacho mnasimama usiku. **AMEJUA KUWA HAMTAUDHIBITI** Kwamba hamtaweza kujua viwango vya usiku na mchana katika uhakika. Imesemwa pia kwamba maana ni kwamba: Mwenyezi Mungu amejua kuwa nyinyi hamtaweza kusimama usiku mzima. **KWA HIYO, AKAKUSAMEHENI** Yaani: Akakusameheni na kukupeni ruhusa ya kuacha kusimama usiku, pale mnaposhindwa. Amekutoeni katika zito na kukuwekeni kwenye tahafifu na kutoka katika ugumu kukuwekeni kwenye wepesi. **SOMENI KILE KILICHOKUWA CHEPESI KATIKA QUR'ANI** Yaani: Someni katika swala za usiku [au nje ya swala] kile kilichokuwa chepesi kwenu, bila ya kusubiri wakati. Aya hii imefuta wajibu wa kusimama usiku. Hadithi sahihi zilizotamka wazi kauli ya mtu aliyemuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: *Je, kuna (swala) nyingine zaidi ya (swala) hizo (tano) zinazoniwajibikia*? Mtume akasema: *Hapana, isipokuwa tu kama utafanya kwa hiyari,* Hadithi hizo zinajulisha kuwa hakuna swala nyingine za wajibu. Kwa maelezo haya, umeondoka wajibu wa kusimama usiku kwa umma. **AMEJUA KUWA MIONGONI MWENU WATAKUWEPO WAGONJWA** Kwa hiyo, hawataweza kusimama usiku. **NA WENGINE WANASAFIRI KATIKA DUNIA WAKITAFUTA KATIKA FADHILA ZA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Wanasafiri katika dunia kwa biashara na faida. Wanatafuta katika riziki za Mwenyezi Mungu kile wanachokihitaji

katika maisha yao na, kwa hiyo, hawawezi kusimama usiku. **NA WENGINE WANAPIGANA KATIKA NJIA YA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Mujahidina. Wao hawawezi kusimama usiku. Hapa Mwenyezi Mungu ametaja sababu tatu zilizopelekea kutoa ruhusa na, kwa hiyo, akauondoa wajibu wa kusimama usiku kwa umma wote kwa sababu hizi ambazo zinawatokea baadhi yao. **KWA HIYO, SOMENI KIASI KILICHOKUWA CHEPESI KATIKA HIYO QUR'ANI NA SIMAMISHENI SWALA** Yaani: Sala zilizo faradhishwa. **NA TOENI ZAKA** Yaani: Zaka ya wajibu katika mali. Imesemwa pia kwamba zaka hapa ni matendo yote ya heri. **NA MKOPESHENI MWENYEZI MUNGU MKOPO MZURI** Yaani: Toeni katika njia ya heri mali zenu utoaji mzuri kwa kuipatia familia matumizi, katika jihadi na zaka ya wajibu. **NA HERI YOYOYE MNAYOITANGULIZA KWA AJILI YA NAFSI ZENU** Yaani: Heri yoyoye katika heri ambazo zimetajwa na amabazo hazikutajwa. **MTAIKUTA MBELE YA MWENYEZI MUNGU. HILO LIMEKUWA BORA ZAIDI NA LENYE MALIPO MAKUBWA ZAIDI** Hayo ni bora zaidi kuliko yale mnayoyaahirisha mpaka wakati wa kufa. Au maana ni kwamba: Hayo ni bora zaidi kuliko kile mnachousia kitolewe baada ya kufa. Pia yawezekana kuwa kilicho kusudiwa ni kwamba: Hayo ni bora zaidi kuliko mnachokitoa katika uhai wenu au ni bora zaidi kuliko kinachosalia kikiwa ni mali ya kurithiwa baada ya kufa kwenu. **NA MUOMBENI MSAMAHA MWENYEZI MUNGU** Kwa madhambi yenu, kwani haiwezekani kuwa hamna makosa mnayofanya. **KWA YAKINI, MWENYEZI MUNGU NI MWINGI WA KUSAMEHE, MWENYE REHEMA** Yaani: Mwingi wa msamaha kwa mwenye kumuomba msamaha, mwingi wa rehema kwa mwenye kumuomba rehema.

## SUURATUL MUDDATH-THIR (74)

*Imeteremka Makka aya zake ni hamsini na sita(56)*

Wafasiri wamesema kuwa: Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipoanza kuteremshiwa *wahyi* (ufunuo) alimjia Jibrili, na Mtume wa Mwenyezi Mungu, alimuona Jibrili akiwa juu ya kitanda baina ya mbingu na ardhi kama nuru inayong'ara. Mtume akafazaishwa na kuzimia. Alipozinduka, aliingia kwa (mkewe) Hadija. Akataka maji, akamwagiwa na kusema: Nifunikeni, nifunikeni. Walimfunika kwa shuka.

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

إِنَّ رَبَّكَ يَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدْنَىٰ مِن ثُلُثَيِ ٱلَّيْلِ وَنِصْفَهُۥ وَثُلُثَهُۥ وَطَآئِفَةٌ
مِّنَ ٱلَّذِينَ مَعَكَ ۚ وَٱللَّهُ يُقَدِّرُ ٱلَّيْلَ وَٱلنَّهَارَ ۚ عَلِمَ أَن لَّن تُحْصُوهُ فَتَابَ
عَلَيْكُمْ ۖ فَٱقْرَءُوا۟ مَا تَيَسَّرَ مِنَ ٱلْقُرْءَانِ ۚ عَلِمَ أَن سَيَكُونُ مِنكُم مَّرْضَىٰ ۙ
وَءَاخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِى ٱلْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِن فَضْلِ ٱللَّهِ ۙ وَءَاخَرُونَ
يُقَـٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ۖ فَٱقْرَءُوا۟ مَا تَيَسَّرَ مِنْهُ ۚ وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُوا۟
ٱلزَّكَوٰةَ وَأَقْرِضُوا۟ ٱللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا ۚ وَمَا تُقَدِّمُوا۟ لِأَنفُسِكُم مِّنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ
عِندَ ٱللَّهِ هُوَ خَيْرًا وَأَعْظَمَ أَجْرًا ۚ وَٱسْتَغْفِرُوا۟ ٱللَّهَ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌۢ ﴿٢٠﴾

سُورَةُ المُدَّثِّرِ
ترتيبها ٧٤ — آياتها ٢٠

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾
وَٱلرُّجْزَ فَٱهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمْنُن تَسْتَكْثِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَٱصْبِرْ ﴿٧﴾
فَإِذَا نُقِرَ فِى ٱلنَّاقُورِ ﴿٨﴾ فَذَٰلِكَ يَوْمَئِذٍ يَوْمٌ عَسِيرٌ ﴿٩﴾ عَلَى ٱلْكَـٰفِرِينَ
غَيْرُ يَسِيرٍ ﴿١٠﴾ ذَرْنِى وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا ﴿١١﴾ وَجَعَلْتُ لَهُۥ مَالًا
مَّمْدُودًا ﴿١٢﴾ وَبَنِينَ شُهُودًا ﴿١٣﴾ وَمَهَّدتُّ لَهُۥ تَمْهِيدًا ﴿١٤﴾ ثُمَّ يَطْمَعُ
أَنْ أَزِيدَ ﴿١٥﴾ كَلَّآ ۖ إِنَّهُۥ كَانَ لِـَٔايَـٰتِنَا عَنِيدًا ﴿١٦﴾ سَأُرْهِقُهُۥ صَعُودًا ﴿١٧﴾

(1) **EWE MWENYE KUJIFUNIKA FUNIKA** Ewe ambaye amejifunika nguo zake; amejigubika nguo hizo.

(2) **SIMAMA UHADHARISHE** Yaani: Nyanyuka uwaonye watu wa Makka na wahadharishe adhabu iwapo hawatakuwa Waislamu.

(3) **NA MOLA WAKO MTUKUZE** Yaani: Bwana wako, Mmiliki wako na Mtengenezaji wa mambo yako mtukuze yeye tu kwa kumsifia. Kumtukuza Mola Mtukufu ni kumsifu kwa sifa ya kiburi na utukufu, na kwamba yeye ni mkubwa zaidi kiasi cha kutohitaji kuwa na mshirika.

(4) **NA NGUO ZAKO ZITWAHARISHE** Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuamuru Mtume wake kutwaharisha nguo zake na kuzitunza zisiingiwe na najisi. Qatada amesema kuwa: *"Itwaharishe nafsi yako isitende madhambi"*.

(5) **NA MASANAMU YAHAME** Yaani: Yaache masanamu na, kwa hiyo, usiyaabudie kwakuwa masanamu hayo ni sababu ya adhabu.

(6) **NA USIFANYE KWA KUTAKA ULIPWE WINGI** Yaani: Usimsimbulie Mola wako kwa sababu ya majukumu ya utume unayo yabeba, ukawa kama yule anayeyaona mengi majukumu anayoyabeba kwa sababu ya kumtendea mtu mwengine. Imesemwa pia kuwa

maana ni kwamba: Unapompa mtu kitu, mpe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na usiwasimbulie watu kwa ulichotoa.

(7) **NA KWA AJILI YA MOLA WAKO TU VUMILIA** Yaani: Umebeba jambo kubwa ambalo Waarabu na wasiokuwa Waarabu watakupiga vita juu ya jambo hilo. Ivumilie hali hiyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

(8) **ITAKAPOPULIZWA PARAPANDA** Kinachokusudiwa hapa ni kupulizwa kwa baragumu, kana kwamba imesemwa kuwa: Vumilia maudhi yao, kwa kuwa mbele yao kuna siku kubwa ambayo ndani ya siku hiyo watakutana na matokeo mabaya ya mambo yao.

(9) **HIYO, SIKU HIYO, NI SIKU NZITO**

(10) **KWA MAKAFIRI, SIO NYEPESI**

(11) **NIACHE MIMI NA YULE NILIYEMUUMBA PEKEE** Niache mimi na yule ambaye niliyemuumba akiwa peke yake tumboni mwa mama yake; hana mali, hana mtoto. Au maana ni kwamba: Niache peke yangu mimi pamoja na yeye. Mimi nitakutoshelezea kumuadhibu. Wafasiri wamesema kuwa huyo (anayekusudiwa hapa) ni Waliid binil Mughiira.

(12) **NA NIKAMPA MALI YENYE KUKUNJULIWA** Yaani: Waliid binil Mughiira alikuwa mashuhuri kwa wingi wa mali.

(13) **NA WATOTO WASIOSAFIRI** Yaani: Na nikampa watoto walioko pamoja naye Makka; hawasafiri na hawana haja ya kutawanyika katika kutafuta rizqi, kwa sababu ya wingi wa mali za baba yao. Imesemwa pia kwamba watoto hao walikuwa kumi na tatu, wote wanaume.

(14) **NA NIKAMTAYARISHIA MATAYARISHO** Yaani: Nikampa wasaa katika maisha, umri mrefu na uongozi katika jamii ya Waquraishi.

(15) **KISHA ANATAUMAI NIONGEZEE**

(16) **HAPANA** Simuongezei. **KWA HAKIKA, YEYE ALIKUWA MPINZANI WA AYA ZETU** Anazipinga aya zetu, anayakufuru yale tuliyo yateremsha kwa Mjumbe wetu.

(17) **NITAMBEBESHA NGUMU** Yaani: Nitamkalifisha adhabu ngumu. Kubebesha ni kumtwisha mtu kitu kizito ambacho hakiwezi.

(18) **KWA YAKINI, YEYE AMEFIKIRI NA AMEPANGA** Amefikiri kuhusu Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na amepanga nafsini mwake, yaani: ameyaandaa nafsini mwake yale maneno anayoyasema. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu amemshutumu.

(19) **KWA HIYO, AKALAANIWA** Yaani: Akalaaniwa na kuadhibiwa. **VIPI ALIPANGA?** Yaani: Ni katika hali gani aliyapanga maneno aliyoyapanga?

(20) **KISHA AMELAANIWA. VIPI ALIPANGA?**

(21) **KISHA ALITAFAKARI** Yaani: Alitafakari, ataipinga Qur'ani kwa kitu gani na ataitia kasoro kwa kitu gani?

(22) **KISHA AKAKUNJA USO** Yaani: Alikunja uso wake alipokosa hila ambayo kwayo ataitia kasoro Qur'ani. **NA AKABADILIKA** Ulisinyaa uso wake na kubadilika.

(23) **KISHA AKAPUUZA NA AKALETA KIBURI**

(24) **AKASEMA: HAYAKUWA HAYA ILA TU NI UCHAWI UNAONUKULIWA** Yaani: Amesema: Hii Qur'ani si chochote isipokuwa tu ni uchawi ambao Muhammad anaunukuu kutoka kwa mtu mwengine na huyo mwengine ananukuu kwake.

(25) **HAYAKUWA HAYA ILA TU NI MANENO YA MWANADAMU** Yaani: Amesema kwamba "Qur'ani ni maneno ya mwanadam, na sio maneno ya Mwenyezi Mungu. Yatakuja maelezo kwamba Waliid Binil Mughiira aliyasema haya ili kuwaridhisha watu wake, baada ya kukiri kwake kwamba Qur'ani ina utamu na kwamba juu yake ina uzuri.

(26) **NITAMUINGIZA SAQAR** Yaani: Nitamuingiza katika moto. *Saqar* ni miongoni mwa majina ya moto wa jahannam

(27) **NA NINI KILICHO KUJULISHA WEWE, NI NINI SAQAR?**

(28) **HAIBAKISHI NA HAIACHI**

(29) **YENYE KUWAANGAZIA SANA WATU** Jahannamu itawaangazia watu hadi waione kwa uwazi. Imesemwa pia kwamba "YENYE KUWAANGAZIA SANA WATU" maana yake ni kuwa Jahannamu itazibadilisha nyuso za watu mpaka ziwe nyeusi.

(30) **JUU YAKE KUNA KUMI NA TISA** Huko motoni kuna malaika kumi na tisa. Wao ndio wahudumu wa motoni. Imesemwa pia kwamba kumi na tisa ni aina kumi na tisa za malaika.

(31) Ilipoteremka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa "JUU YAKE KUNA KUMI NA TISA", Abuu jahali alisema: "Hivi Muhammad hana wasaidizi isipokuwa kumi na tisa tu? Hivi kila watu mia moja miongoni mwenu watashindwa kumshika mmoja wa hao malaika kumi na tisa kisha wakatoka motoni? Hapo, ikateremaka aya hii: **NA HATUKUWAFANYA WALINZI WA MOTONI ISIPOKUWA MALAIKA TU** Hivyo basi, ni nani atakayewaweza malaika? Ni nani atakayewashinda, na ilhali malaika wao ndio viumbe madhubuti zaidi wa kusimamia haki ya Mwenyezi Mungu, wanaopandwa na hasira zaidi kwa ajili yake, wenye nguvu sana na wakali sana wa kukamata? **NA HATUKUIFANYA IDADI YAO ISIPOKUWA TU IWE MTIHANI KWA**

إِنَّهُۥ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿١٨﴾ فَقُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿١٩﴾ ثُمَّ قُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ نَظَرَ
﴿٢١﴾ ثُمَّ عَبَسَ وَبَسَرَ ﴿٢٢﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ وَٱسْتَكْبَرَ ﴿٢٣﴾ فَقَالَ إِنْ هَٰذَآ إِلَّا سِحْرٌ
يُؤْثَرُ ﴿٢٤﴾ إِنْ هَٰذَآ إِلَّا قَوْلُ ٱلْبَشَرِ ﴿٢٥﴾ سَأُصْلِيهِ سَقَرَ ﴿٢٦﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ
مَا سَقَرُ ﴿٢٧﴾ لَا تُبْقِى وَلَا تَذَرُ ﴿٢٨﴾ لَوَّاحَةٌ لِّلْبَشَرِ ﴿٢٩﴾ عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ
﴿٣٠﴾ وَمَا جَعَلْنَآ أَصْحَٰبَ ٱلنَّارِ إِلَّا مَلَٰٓئِكَةً ۙ وَمَا جَعَلْنَا عِدَّتَهُمْ إِلَّا فِتْنَةً
لِّلَّذِينَ كَفَرُوا۟ لِيَسْتَيْقِنَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ وَيَزْدَادَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِيمَٰنًا ۙ
وَلَا يَرْتَابَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْمُؤْمِنُونَ ۙ وَلِيَقُولَ ٱلَّذِينَ فِى قُلُوبِهِم مَّرَضٌ
وَٱلْكَٰفِرُونَ مَاذَآ أَرَادَ ٱللَّهُ بِهَٰذَا مَثَلًا ۚ كَذَٰلِكَ يُضِلُّ ٱللَّهُ مَن يَشَآءُ وَيَهْدِى
مَن يَشَآءُ ۚ وَمَا يَعْلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ ۚ وَمَا هِىَ إِلَّا ذِكْرَىٰ لِلْبَشَرِ ﴿٣١﴾ كَلَّا
وَٱلْقَمَرِ ﴿٣٢﴾ وَٱلَّيْلِ إِذْ أَدْبَرَ ﴿٣٣﴾ وَٱلصُّبْحِ إِذَآ أَسْفَرَ ﴿٣٤﴾ إِنَّهَا لَإِحْدَى
ٱلْكُبَرِ ﴿٣٥﴾ نَذِيرًا لِّلْبَشَرِ ﴿٣٦﴾ لِمَن شَآءَ مِنكُمْ أَن يَتَقَدَّمَ أَوْ يَتَأَخَّرَ ﴿٣٧﴾ كُلُّ
نَفْسٍۭ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٣٨﴾ إِلَّآ أَصْحَٰبَ ٱلْيَمِينِ ﴿٣٩﴾ فِى جَنَّٰتٍ يَتَسَآءَلُونَ
﴿٤٠﴾ عَنِ ٱلْمُجْرِمِينَ ﴿٤١﴾ مَا سَلَكَكُمْ فِى سَقَرَ ﴿٤٢﴾ قَالُوا۟ لَمْ نَكُ مِنَ
ٱلْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ وَلَمْ نَكُ نُطْعِمُ ٱلْمِسْكِينَ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا نَخُوضُ مَعَ
ٱلْخَآئِضِينَ ﴿٤٥﴾ وَكُنَّا نُكَذِّبُ بِيَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿٤٦﴾ حَتَّىٰٓ أَتَىٰنَا ٱلْيَقِينُ ﴿٤٧﴾

**WALE WALIOKUFURU** Yaani: Tumeifanya idadi yao iliyotajwa (ya kumi na tisa) kwa ajili ya kuwapoteza na kuwapa mtihani makafiri mpaka wakasema waliyoyasema, ili adhabu yao iongezeke na hasira za Mwenyezi Mungu juu yao pia ziongezeke. **ILI WAPATE YAKINI WALE AMBAO WAMEPEWA KITABU** Wayahudi na Wakristo kwa sababu ya kuyaafiki yaliyoshuka katika Qur'ani kwamba idadi ya wahudumu wa motoni ni kumi na tisa, kwa mujibu wa waliyo nayo katika vitabu vyao. **NA ILI WALIOAMINI WAONGEZEKE IMANI** Kwa kuona waliopewa kitabu wanakubaliana nao. **NA ILI WAUMINI NA WALE WALIOPEWA KITABU WASIWE NA SHAKA** Katika dini, au shaka katika idadi ya wahudumu wa motoni ni kumi na tisa. **NA ILI WASEME WALE AMBAO NYOYONI MWAO MNA UGONJWA** Hao ni wanafiki. Makusudio ya ugonjwa ni kule tu kuwa na shaka. **NA MAKAFIRI:** Miongoni mwa watu wa Makka na wengineo. **NI NINI AMEKUSUDIA MWENYEZI MUNGU KWA MFANO HUU?** Yaani: Mwenyezi Mungu amekusudia kitu kutoka kwa idadi hii inayo shangaza mshangao wa kufananisha? **KAMA HIVYO, MWENYEZI MUNGU ANAMPOTEZA AMTAKAYE NA ANAMUONGOZA AMTAKAYE NA HALIJUI JESHI LA MOLA WAKO ISIPOKUWA YEYE TU** Na wahudumu wa motoni. Na ingawa wahudumu hao ni kumi na tisa lakini wanao wasaidizi na jeshi la malaika ambao hakuna anayewajua isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu tu. **NA HAYO SI CHOCHOTE ILA TU NI UKUMBUSHO KWA WANADAMU** Yaani: Haikuwa *Saqar* na idadi ya wahudumu wake waliotajwa isipokuwa tu ni ukumbusho na mawaidha kwa walimwengu ili wajue uwezo kamilifu wa Mwenyezi Mungu na kwamba yeye hana haja ya wasaidizi na watetezi.

32 **HAPANA! NINAAPA KWA MWEZI** Mwenyezi Mungu ameapa juu ya hayo kwa mwezi na viumbe vingine vilivyotajwa baada ya mwezi.

33 **NA USIKU UNAPO ONDOKA** Usiku unapo tokomea.

34 **NA ASUBUHI INAPO PAMBAZUKA** Yaani: Inapotoa mwanga na kubainika.

35 **KWA YAKINI, HIYO NI MOJAWAPO YA MAKUBWA** Yaani: Kwa yakini kabisa, Saqar ni mojawapo ya majanga na maafa makubwa. Imesemwa pia kwamba neno "HIYO" linaashiria kwenye kumkataa kwao Mtume Muhammad; kwamba kukataa huko ni mojawapo ya madhambi makubwa.

36 **IKITOA TAHADHARI KWA WANADAMU:** Ni moto. Imesemwa pia kuwa ni Qur'ani. Qur'ani inatoa tahadhari kwa wanadamu kwa zile ahadi njema na mbaya zilizomo ndani yake.

37 **KWA ANAYETAKA KUSONGA MBELE MIONGONI MWENU** Kwa kuamini. **AU KURUDI NYUMA** Kwa kupinga.

38 **KILA NAFSI KWA ILICHOCHUMA IMEJIFUNGA** Yaani: Nafsi itahukumiwa kwa mujibu wa matendo yake ambayo imefungika kwayo; ima yataiokoa au yataiangamiza.

39 **ISIPOKUWA WATU WA KULIANI** Hao ni waumini. Wao hawatakuwa wamejifunga kwa madhambi, bali watakombolewa kwa matendo yao mazuri waliyo yatenda.

40 **NDANI YA BUSTANI** Yaani: Wao watakuwa ndani ya bustani. **WANAULIZANA** Wanaulizana wao kwa wao.

41 **KUHUSU WAOVU** Yaani: Wataulizana wao kwa wao kuhusu hali ya watu waovu.

42 **NI NINI KILICHO KUINGIZENI KATIKA SAQAR?** Waumini watawauliza waovu: Ni nini kilichokuingizeni motoni?

43 **WATASEMA: HATUKUWA MIONGONI MWA WENYE KUSWALI**

فَمَا تَنفَعُهُمْ شَفَٰعَةُ ٱلشَّٰفِعِينَ ﴿٤٨﴾ فَمَا لَهُمْ عَنِ ٱلتَّذْكِرَةِ مُعْرِضِينَ
﴿٤٩﴾ كَأَنَّهُمْ حُمُرٌ مُّسْتَنفِرَةٌ ﴿٥٠﴾ فَرَّتْ مِن قَسْوَرَةٍۭ ﴿٥١﴾ بَلْ يُرِيدُ
كُلُّ ٱمْرِيٍٕ مِّنْهُمْ أَن يُؤْتَىٰ صُحُفًا مُّنَشَّرَةً ﴿٥٢﴾ كَلَّا ۖ بَل لَّا يَخَافُونَ
ٱلْءَاخِرَةَ ﴿٥٣﴾ كَلَّآ إِنَّهُۥ تَذْكِرَةٌ ﴿٥٤﴾ فَمَن شَآءَ ذَكَرَهُۥ ﴿٥٥﴾
وَمَا يَذْكُرُونَ إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ ۚ هُوَ أَهْلُ ٱلتَّقْوَىٰ وَأَهْلُ ٱلْمَغْفِرَةِ ﴿٥٦﴾

ترتيبها ٧٥ — سُورَةُ القِيَامَةِ — آياتها ٤٠

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

لَآ أُقْسِمُ بِيَوْمِ ٱلْقِيَٰمَةِ ﴿١﴾ وَلَآ أُقْسِمُ بِٱلنَّفْسِ ٱللَّوَّامَةِ ﴿٢﴾ أَيَحْسَبُ
ٱلْإِنسَٰنُ أَلَّن نَّجْمَعَ عِظَامَهُۥ ﴿٣﴾ بَلَىٰ قَٰدِرِينَ عَلَىٰٓ أَن نُّسَوِّىَ بَنَانَهُۥ ﴿٤﴾ بَلْ
يُرِيدُ ٱلْإِنسَٰنُ لِيَفْجُرَ أَمَامَهُۥ ﴿٥﴾ يَسْـَٔلُ أَيَّانَ يَوْمُ ٱلْقِيَٰمَةِ ﴿٦﴾ فَإِذَا بَرِقَ ٱلْبَصَرُ
﴿٧﴾ وَخَسَفَ ٱلْقَمَرُ ﴿٨﴾ وَجُمِعَ ٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ ﴿٩﴾ يَقُولُ ٱلْإِنسَٰنُ يَوْمَئِذٍ
أَيْنَ ٱلْمَفَرُّ ﴿١٠﴾ كَلَّا لَا وَزَرَ ﴿١١﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ ٱلْمُسْتَقَرُّ ﴿١٢﴾ يُنَبَّؤُا۟ ٱلْإِنسَٰنُ
يَوْمَئِذٍۭ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿١٣﴾ بَلِ ٱلْإِنسَٰنُ عَلَىٰ نَفْسِهِۦ بَصِيرَةٌ ﴿١٤﴾ وَلَوْ أَلْقَىٰ
مَعَاذِيرَهُۥ ﴿١٥﴾ لَا تُحَرِّكْ بِهِۦ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِۦٓ ﴿١٦﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُۥ
وَقُرْءَانَهُۥ ﴿١٧﴾ فَإِذَا قَرَأْنَٰهُ فَٱتَّبِعْ قُرْءَانَهُۥ ﴿١٨﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُۥ ﴿١٩﴾

(44) **NA HATUKUWA TUKIWAPA CHAKULA MASIKINI**

(45) **NA TULIKUWA TUNASHIRIKI UOVU PAMOJA NA WAOVU** Yaani: Tulikuwa tukishirikiana na waovu katika uovu wao. Kila akipotea mpoteaji, basi tunapotea naye. Ibni-zaidi amesema kuwa: *"Tulikuwa tunasema maovu pamoja na wasemao uovu kuhusu suala la Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Uovu huo ni ile kauli yao kwamba Muhammad ni mrongo, kichaa, mchawi na mshairi".*

(46) **NA TULIKUWA TUNAIKADHIBISHA SIKU YA MALIPO** Yaani: Siku ya malipo na hesabu.

(47) **MPAKA YAKINI IKATUJIA** Yakini hiyo ni mauti.

(48) **BASI HAYATAWASAIDIA MAOMBEZI YA WAOMBEAJI** Yaani: Halitawasaidia ombi la Malaika na Mitume, kama ombi hilo litakavyowasaidia watu wema.

(49) **WANA NINI; WANAPUUZA MAWAIDHA?** Yaani: Ni kitu gani kimewapata katika hali ya kuwa wao wanaipuuza Qur'ani ambayo imesheheni ukumbusho na mawaidha makubwa.

(50) **KAMA KWAMBA WAO NI PUNDA WALIOKURUPUSHWA** Yaani: Wamekuwa kama punda wakimbiao kwa kasi.

(51) **WANAOKIMBIA KAS-WARA** Yaani: *Qas-wara* ni walengamishale wanaoirusha. Imesemwa pia kwamba Qas-wara kwa lugha ya Waarabu ni simba.

(52) **BALI KILA MTU MIONGONI MWAO ANATAKA APEWE NYARAKA ZILIZOKUNJULIWA** Wafasiri wamesema kuwa makafiri wa Kiquraishi walimwambia Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: "Ikifika asubuhi, iwe kila mmoja wetu ana kitabu kichwani kwake kilichokunjuliwa na kinachotoka kwa Mwenyezi Mungu kikieleza kuwa wewe ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu".

(53) **HAPANA! BALI HAWAIOGOPI AKHERA** Kwa sababu wao kama wangaliuogopa moto, wasingalipendekeza miujiza.

(54) **HAPANA! KWA YAKINI, HUO NI UKUMBUSHO** Yaani: Qur'ani.

(55) **ATAKAYE, UTAMKUMBUSHA** Yaani: Atakaye kuonyeka kwa Qur'ani, ataonyeka.

(56) **NA HAWATAKUMBUKA ISIPOKUWA TU AKITAKA MWENYEZI MUNGU** Isipokuwa tu Mwenyezi Mungu awatakie kuongoka. **YEYE NDIYE MWENYE HAKI YA KUOGOPWA** Yaani: Yeye ndiye mwenye haki ya wenye kuogopa wamuogope kwa kuacha kumuasi na kujilazimisha kumtii. **NA NDIYE MWENYE HAKI YA KUSAMEHE** Yaani: Na yeye ndiye mwenye haki ya kuwasamehe waumini yale madhambi waliyoyafanya. Pia yeye ni mwenye haki ya kukubali toba ya wafanya maasi wenye kutubu na, hivyo, kuwasamehe madhambi yao.

## SUURATUL QIYAAMAH (75)

Imeteremka Makka aya zake ni arobaini(40)
*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

(1) **NINAAPA KWA SIKU YA KIYAMA** Ninaapa kwa Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu anapoapa kwa Siku ya Kiyama, ni kuonesha utukufu wa siku hiyo na ukubwa wake. Na Mwenyezi Mungu anayo haki ya kuapa kwa kiumbe chake chochote atakacho katika viumbe vyake.

(2) **NA NINAAPA KWA NAFSI YENYE KULAUMU SANA** Ninaapa kwa nafsi inayomlaumu mwenye nafsi hiyo kwa uzembe wake. Hiyo ni nafsi ya muumini. Inalaumu juu ya yaliyopita na inajuta. Inajilaumu kwa maovu; kwa nini iliyafanya? Na inajilaumu kwa heri;

kwa nini haikufanya sana? Muqaatil amesema kwamba: "*Hiyo ni nafsi ya kafiri. Atajilaumu na kujuta huko akhera kwa kuzembea kwake upande wa Mwenyezi Mungu*". [Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mambo mawili yote kwamba yeye ataikusanya mifupa kisha atampa uhai kila mwanadamu ili amuhesabu na amlipe].

3 **HIVI MWANADAM ANADHANI KUWA HATUTAIKUSANYA MIFUPA YAKE?** Baada ya mifupa hiyo kuwa vumbi, tutairejesha iwe umbile jipya. Hiyo ni dhana batili. Sisi tutaikusanya.

4 **KWA NINI TUSIWEZE? TUNAWEZA** Yaani: Kwa nini tusiweze? Tunaweza: **KUVIFANYA SAWA VIDOLE VYAKE** Yaani: Tunaweza kukusanya baadhi yake juu ya baadhi nyingine tukavifanya kipande kimoja kama unyayo wa ngamia. Lakini sisi tumemneemesha mwanadamu kwa hivi vidole vikiwa vidogo vidogo, vizuri, vyenye maungio, kucha, mishipa midogo na mifupa laini. (Imesemwa pia kwamba huu ni uzindushi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba vidole vya kila mtu vinatofautiana na vya watu wengine katika mpangilio wa michoro ya sehemu yake ya kukamatia. Kama Mwenyezi Mungu angalitaka, angalivifanya vinalingana na kufanana).

5 **BALI MWANADAMU ANATAKA AFANYE UOVU MBELE YAKE** Anataka autangulize uovu wake wakati ujao na, kwa hiyo, atangulize kufanya dhambi na acheleweshe kutubu. Anataka afanye maovu maisha yake yote na asikumbuke kufa.

6 **ANAULIZA: NI LINI SIKU YA KIYAMA?** Anauliza: Ni lini siku ya Kiyama? Ni swali la kebehi na kuona kuwa jambo hilo ni la mbali sana!

7 **BASI JICHO LITAKAPO PARAMA,** Litakapo fazaika, kuduwaa na kuhemewa kutokana na kukikodolea macho kifo au kukodolea kufufuliwa.

8 **NA MWEZI IKAFUNIKWA NURU YAKE** Mwanga wake wote ukaondoka na usirudi kama unavyorudi hapa duniani mwezi unapopatwa.

9 **NA LIKAKUSANYWA JUA NA MWEZI** Yaani: Mwanga wa juu wa mwezi utaondoka wote. Jua na mwezi vitakusanywa pamoja na, hivyo, hakutakuwa na kupishana kwa usiku na mchana.

10 **SIKU HIYO MWANADAMU ATASEMA: NI WAPI PA KUKIMBILIA?** Tutamkimbia wapi
Mwenyezi Mungu, hisabu yake na adhabu yake?

11 **HAPANA! HAKUNA PA KUKIMBILIA** Yaani: Hakuna mlima, ngome wala mahali pa kumkimbia Mwenyezi Mungu siku hiyo.

12 **NI KWA MOLA WAKO TU SIKU HIYO SEHEMU YA UTUILIVU** Yaani: Sehemu ya utulivu ni marejeo, ukomo na hatima.

13 **MWANADAMU ATAELEZWA SIKU HIYO KILE ALICHO KITANGULIZA NA ALICHO KICHELEWESHA**

14 **BALI MWANADAMU NI MWENYE KUIJUA SANA NAFSI YAKE** Anajua ukweli wa hali aliyo nayo; imani au ukafiri, utiifu au uasi, uongofu au upotofu. Imesemwa pia kuwa maana ni kwamba: Bali viungo vya mwanadamu vitakuwa shahidi wake.

15 **NA HATA KAMA ATATOA UDHURU** Yaani: Japokuwa atatoa udhuru na kubishana akijitetea. Hayo hayatamsaidia.

16 **USITIKISE ULIMI WAKO KWAYO ILI UIHARAKISHE** Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa anachezesha midomo yake na ulimi wake kwa Qur'ani inapoteremshwa kwake, kabla Jibrili hajamaliza kuusoma *Wahyi.* Mtume alikuwa akifanya hivyo kwa shauku ya kuhifadhi. Kwa sababu hiyo, iliteremka aya hii. Yaani: Usichezeshe chezeshe ulimi wako kwa ajili ya Qur'ani wakati wa kupokea *wahyi* ili uipokee haraka kwa kuhofia kukutoka.

17 **KWA YAKINI, NI JUU YETU KUIKUSANYA NA KUISOMA** Ni juu yetu kuikusanya Qur'ani kifuani mwako ili kiasi chochote cha Qur'ani hiyo kisikuponyoke. **NA KUISOMA** Yaani: Na ni juu yetu kuthibitisha usomaji wake ulimini mwako katika njia iliyo sahihi.

18 **TUKISHA ISOMA,** Yaani: Tukisha kamilisha kukusomea kwa ulimi wa Jibrili, **BASI WEWE FUATISHA KISOMO CHAKE** Msikilize Jibrili na usikilize usomaji wake.

19 **KISHA KWA YAKINI, NI JUU YETU UFAFANUZI WAKE** Yaani: Ni juu yetu tafsiri ya yaliomo katika Qur-ani, ikiwa ni pamoja na mambo ya halali, mambo ya haramu na utatuzi wa mambo yaliyo na utata. Baada ya hapo, Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akawa ananyamaza Jibrili anapomjia. Jibrili akiondoka, Mtume anasoma kama alivyo ahidiwa na Mwenyezi Mungu.

20 **HAPANA! BALI MNAPENDA CHA HARAKA** "Hapana" ni kemeo la kukataza haraka na kushawishi umakini.

21 **NA MNAIACHA AKHERA** Hamfanyi matendo mema kwa ajili yake.

22 **NYUSO FULANI SIKU HIYO NI ZENYE KUNAWIRI** Yaani: Zitakuwa nyororo, nzuri.

23 **NI ZENYE KUMUANGALIA MOLA WAKE** Zinamuangalia Muumba wake na Mmiliki wa mambo yake. Zinaangalia: Hivi

كَلَّا بَلْ تُحِبُّونَ ٱلْعَاجِلَةَ ﴿٢٠﴾ وَتَذَرُونَ ٱلْءَاخِرَةَ ﴿٢١﴾ وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٢٢﴾
إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾ وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍۭ بَاسِرَةٌ ﴿٢٤﴾ تَظُنُّ أَن يُفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ﴿٢٥﴾
كَلَّآ إِذَا بَلَغَتِ ٱلتَّرَاقِىَ ﴿٢٦﴾ وَقِيلَ مَنْ ۜ رَاقٍ ﴿٢٧﴾ وَظَنَّ أَنَّهُ ٱلْفِرَاقُ ﴿٢٨﴾ وَٱلْتَفَّتِ
ٱلسَّاقُ بِٱلسَّاقِ ﴿٢٩﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ ٱلْمَسَاقُ ﴿٣٠﴾ فَلَا صَدَّقَ وَلَا صَلَّىٰ
﴿٣١﴾ وَلَـٰكِن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿٣٢﴾ ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ يَتَمَطَّىٰٓ ﴿٣٣﴾ أَوْلَىٰ لَكَ
فَأَوْلَىٰ ﴿٣٤﴾ ثُمَّ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰٓ ﴿٣٥﴾ أَيَحْسَبُ ٱلْإِنسَـٰنُ أَن يُتْرَكَ سُدًى ﴿٣٦﴾
أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِّن مَّنِىٍّ يُمْنَىٰ ﴿٣٧﴾ ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً فَخَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٣٨﴾ فَجَعَلَ مِنْهُ
ٱلزَّوْجَيْنِ ٱلذَّكَرَ وَٱلْأُنثَىٰٓ ﴿٣٩﴾ أَلَيْسَ ذَٰلِكَ بِقَـٰدِرٍ عَلَىٰٓ أَن يُحْـِۧىَ ٱلْمَوْتَىٰ ﴿٤٠﴾

## سُورَةُ الإِنسَانِ

ترتيبها ٧٦ — آياتها ٣١

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ

هَلْ أَتَىٰ عَلَى ٱلْإِنسَـٰنِ حِينٌ مِّنَ ٱلدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْـًٔا مَّذْكُورًا ﴿١﴾
إِنَّا خَلَقْنَا ٱلْإِنسَـٰنَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَـٰهُ سَمِيعًۢا
بَصِيرًا ﴿٢﴾ إِنَّا هَدَيْنَـٰهُ ٱلسَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾
إِنَّآ أَعْتَدْنَا لِلْكَـٰفِرِينَ سَلَـٰسِلَا۟ وَأَغْلَـٰلًا وَسَعِيرًا ﴿٤﴾ إِنَّ
ٱلْأَبْرَارَ يَشْرَبُونَ مِن كَأْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُورًا ﴿٥﴾

ndivyo zilivyo jumuika Hadithi sahihi kwamba waja watamuona Mola wao Siku ya Kiyama, kama wanavyouona mwezi usiku wa kukamilika kwa mduwara wa mwezi.

(24) **NA NYUSO NYINGINE SIKU HIYO NI ZENYE KUSINYAA** Yaani: Ni zenye kujikunja, ni zenye kusinyaa, ni zenye majonzi.

(25) **ZITADHANI KUFIKWA NA LA KUVUNJA MGONGO** La kuvunja mgongo *"Faaqirah"* ni janga kubwa, kama vile linavunja uti wa mgongo.

(26) **HAPANA! ROHO ITAKAPOFIKA MTULINGA,** Yaani: Nafsi au roho itakapofika katika mtulinga. Mtulinga ni mfupa uliopo kati ya tundu la shingo na bega. Roho kufika kwenye mtulinga, maneno haya hutumika kufumbia hali ya nafsi kukaribia kufa.

(27) **NA PAKAULIZWA: NI NANI TABIBU?** Yaani: Ndugu aliyemtembelea ndugu yake mgonjwa atasema: Ni nani atakayemtibu na kumponya kwa tiba yake? Wamemtafutia matabibu na hawakuweza kumsaidia chochote atoke katika hukumu ya Mwenyezi Mungu.

(28) **NA AKADHANI KWAMBA HUO NDIO UTENGANO** Yaani: Yule ambaye roho yake imefika mtulinga akawa na yakini kuwa huo ndio wakati wa kutengana na dunia, familia mali na watoto,

(29) **NA MUUNDI UKAPACHANA NA MUUNDI,** Yaani: Ugoko wake utakapokutana na ugoko wake mwengine wakati wa kufikwa na mauti. Miguu yake itakuwa imekufa na goko zake zimekauka na haziwezi tena kumbeba wakati alikuwa akitembea sana kwa miguu hiyo. Watu watauandaa mwili wake, na malaika wataiandaa roho yake.

(30) **NI KWA MOLA WAKO TU SIKU HIYO KUCHUNGWA** Yaani: Roho baada ya kutolewa kwenye miili zitachungwa kupelekwa kwa Muumba wako.

(31) **KWA HIYO, HAKUKUBALI NA HAKUSWALI** Yaani: Hakuukubali utume wala Qur'ani na hakuswali kwa ajili ya Mola wake. Kwa hiyo, hakuamini kwa moyo wake wala hakutenda kwa mwili wake.

(32) **NA LAKINI AMEPINGA NA AMEPUUZA** Yaani: Amempinga Mtume na yale aliyokuja nayo, na amepuuza kutii na kuamini.

(33) **KISHA AKENDA KWENYE FAMILIA YAKE HUKU AKIRINGA** Yaani: Akiringa na kujidai katika kutembea kwake kwa kuona fahari kufanya hivyo. Au anakuwa mzito na mvivu wa kumfuata mwenye kuhubiri haki.

(34) **KUANGAMIA NI KWAKO TENA KUANGAMIA,**

(35) **KISHA KUANGAMIA NI KWAKO TENA KUANGAMIA** Yaani: Kitakacho kutawala wewe ni kuangamia. Asili yake ni: Mwenyezi Mungu ameyapa utawala kwako yale mambo unayoyachukia. Yanakurudia mara kwa mara.

(36) **HIVI MWANADAMU ANADHANI KUWA ATAACHWA HIVI HIVI TU?** Yaani: Anadhani ataachwa bure; hataamrishwa na hataakatazwa? Hatahesabiwa na hataadhibiwa?

(37) **HIVI KWANI HAKUWA TONE LA MANII YAMIMINWAYO?** Yaani: Hivi mwanadamu huyo hakuwa tone la *manii* yanayo miminwa katika mfuko wa uzazi?

(38) **KISHA AKAWA PANDE LA DAMU** Yaani: Baada ya kuwa tone la *manii* akawa pande la damu. **AKAUMBA** Yaani: Akakadiria kwa kulifanya pande la damu hilo kuwa pande la nyama lenye maumbile. **AKAWEKA SAWA** Yaani: Akamrekebisha mwanadamu, akakamilisha makuzi yake na akapuliza roho ndani yake.

(39) **AKAUMBA KUTOKANA NAYO** Yaani: Kutokana na manii hayo baada ya kuyapa umbo. **JINSIA MBILI** Yaani: Aina mbili za aina ya mwanadamu. **MWANAMUME NA MWANAMKE**

(40) **HIVI HUYO** Aliyeanzisha umbile hili zuri

na akaliweza. **HAKUWA MWENYE UWEZO WA KUHUISHA WALIOKUFA?** Yaani: Kuirejesha miili kwa kuifufua kama ilivyokuwa duniani? **Kurudisha ni rahisi zaidi kuliko kuanza**. Imepokewa kutoka kwa Abuhuraira, akiseama: Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kwamba: "*Atakayesoma miongoni mwenu* ***laa uqsimu biyaumil-qiyaama*** *mpaka akafika* ***Alaisa dhaalika biqaadirin alaa anyuh-yiyal-mautaa****, aseme:* ***balaa*** *= Hapana! Anaweza".*

## SUURATUL INSAAN (76)

Imeteremka Madina aya zake ni thalathini na moja(31)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

1 **HAKIKA, KIMEMPITIA MWANADAMU** Yaani: Kimewapitia wanadamu kupitia kwa baba yao Adamu, **KIPINDI CHA WAKATI** Imesemekana kuwa kipindi hicho ni miaka arobaini kabla mwanadamu hajapuliziwa roho. Ameumbwa kwa tope, kisha kwa udongo mweusi uliofinyangwa, kisha kwa udongo mkavu utoao sauti (kama utagongwa). Yasemekana pia kwamba muradi wa MWANADAMU hapa ni wanadamu. KIPINDI CHA WAKATI ni kipindi cha ujauzito. **HAKUWA KITU KINACHOTAJWA** Alfarraa-u na Atha'alabi wamesema kuwa: "Maana ni kwamba mwanadamu alikuwa mwili uliotiwa sura, mchanga, tope. Hatajwi na hajulikani. Jina lake halijulikani, wala nini kinachokusudiwa kwake. Kisha akapuliziwa roho akawa mwenye kutajwa". Imesemwa pia kwamba maana ni kuwa: Zilipita nyakati na Adamu hakuwa chochote na wala hajaumbwa na wala hatajwi na kiumbe yeyote.

2 **KWA YAKINI, SISI TUMEMUUMBA MTU KUTOKANA NA TONE LA MAJI YA UZAZI** Muradi wa mtu hapa ni mwanadamu. Tone la maji ya uzazi ni Manii. **MCHANGANYIKO** Mchanganyiko ni vitu vilivyochanganywa. Kilichokusudiwa ni mchanganyiko wa tone la manii ya mwanamume na tone la manii ya mwanamke. Imesemwa Mchanganyiko kwa sababu ni mchanganyiko wa aina na maumbo tofauti anayoumbwa mwanadamu kwayo. **TUMTAHINI** Yaani: Tumemuumba tukikusudia kumtahini kwa kheri, shari na majukumu. **HIVYO, TUKAMFANYA MWENYE KUSIKIA, MWENYE KUONA** Yaani: Tumepandikiza kwake njia za ufahamu ili kuelewa kwake kuwe kukubwa na, kwa hiyo, iwezekane kumpa mtihani.

3 **KWA YAKINI, SISI TUMEMUELEKEZA NJIA; IMA AWE MWENYE KUSHUKURU NA IMA AWE MWENYE KUKUFURU** Yaani: Tumemfafanulia na kumjulisha njia ya uongofu na ya upotovu, kheri na shari. Pia tumemjulisha manufaa yake na madhara yake ambayo anayaelewa kwa maumbile yake na akili yake timamu. Sawa awe ameshukuru au amekufuru.

4 **KWA YAKINI, SISI TUMEWAANDALIA MAKAFIRI MINYORORO NA MAKONGO NA MOTO MKALI** Yaani: Tumewaandalia hayo ili tuwaadhibu kwayo. MAKONGO ni kitu ambacho hutumika kufungia mikono kwenye shingo (pingu). MOTO MKALI ***Sa'iir*** ni nishati inayowaka moto ulio mkali sana.

5 **KWA HAKIKA, WEMA WATANYWEA GLASI** Wema ni watu wa utiifu *ikhlasi* (utakaso) ambao wanatekeleza haki ya Mwenyezi Mungu. Glasi ni chombo ambacho ndani yake mna kinywaji. **AMBAZO MCHANGANYIKO WAKE NI KAFURI** Yaani: Kinywaji chake kimechanganywa na *kafuri* ili harufu na ladha ya mvinyo ikamilike na iwe mzuri.

6 **NI CHEMCHEMI WATAKAYO KUNYWA WAJA WA MWENYEZI MUNGU** Yaani: Watakunywa mvinyo kutoka kwenye chemchem hiyo. Inawezekana pia kuwa maana ni kwamba watakunywa mvinyo wao ukiwa umechanganywa na maji ya chemchemi hiyo. **WATAIPITISHA CHEMCHEMI HIYO UPITISHAJI** Yaani: Wataiwekea njia za kuipitisha kuelekea watakapo na wataitumia watakavyo. Wataipasulia njia kama unavyopasuliwa njia mto na kuupeleka hapa na pale.

7 **WANATEKELEZA NADHIRI** Wanapoweka Nadhiri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu wanatekeleza. Nadhiri katika sheria ni jambo ambalo mtu ameiwajibisha nafsi yake kulifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ikiwa ni pamoja na swala, kufunga au kuchinja au jambo jingine lolote katika mambo ambayo sio wajibu kwake kwa mujibu wa sheria. **NA WANAIOGOPA SIKU AMBAYO SHARI YAKE ITAKUWA IMEENEA** Makusudio ni kwamba wanaiogopa Siku ya Kiyama. Shari ya siku hiyo itaenea mpaka ijaze mbingu na ardhi; mbingu zitapasuka, nyota zitapukutika, ardhi itapondwapondwa na milima kusagwasagwa.

8 **NA WANATOA CHAKULA, PAMOJA NA KUKIPENDA, KUWAPA MASIKINI, YATIMA NA WAFUNGWA** Yaani: Wanawapa chakula aina tatu za watu hawa pamoja na uchache wa chakula walichonacho, kukipenda, na kukitamani. Imesemwa pia kwamba wanatoa chakula juu ya kumpenda Mwenyezi Mungu.

9 **SI VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA TUNAKUPENI CHAKULA KWA AJILI YA MWENYEZI MUNGU TU** Hawatazamii kulipwa wala kusifiwa na watu kwa hilo.

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا عِبَادُ ٱللَّهِ يُفَجِّرُونَهَا تَفْجِيرًا ﴿٦﴾ يُوفُونَ بِٱلنَّذْرِ وَيَخَافُونَ
يَوْمًا كَانَ شَرُّهُۥ مُسْتَطِيرًا ﴿٧﴾ وَيُطْعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسْكِينًا
وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا شُكُورًا
﴿٩﴾ إِنَّا نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿١٠﴾ فَوَقَىٰهُمُ ٱللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ
ٱلْيَوْمِ وَلَقَّىٰهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا ﴿١١﴾ وَجَزَىٰهُم بِمَا صَبَرُوا۟ جَنَّةً وَحَرِيرًا
﴿١٢﴾ مُّتَّكِـِٔينَ فِيهَا عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ ۖ لَا يَرَوْنَ فِيهَا شَمْسًا وَلَا زَمْهَرِيرًا ﴿١٣﴾
وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلَٰلُهَا وَذُلِّلَتْ قُطُوفُهَا تَذْلِيلًا ﴿١٤﴾ وَيُطَافُ عَلَيْهِم بِـَٔانِيَةٍ
مِّن فِضَّةٍ وَأَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيرَا۠ ﴿١٥﴾ قَوَارِيرَا۟ مِن فِضَّةٍ قَدَّرُوهَا تَقْدِيرًا ﴿١٦﴾
وَيُسْقَوْنَ فِيهَا كَأْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَنجَبِيلًا ﴿١٧﴾ عَيْنًا فِيهَا تُسَمَّىٰ سَلْسَبِيلًا
﴿١٨﴾ ۞ وَيَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَٰنٌ مُّخَلَّدُونَ إِذَا رَأَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنثُورًا
﴿١٩﴾ وَإِذَا رَأَيْتَ ثَمَّ رَأَيْتَ نَعِيمًا وَمُلْكًا كَبِيرًا ﴿٢٠﴾ عَٰلِيَهُمْ ثِيَابُ سُندُسٍ
خُضْرٌ وَإِسْتَبْرَقٌ ۖ وَحُلُّوٓا۟ أَسَاوِرَ مِن فِضَّةٍ وَسَقَىٰهُمْ رَبُّهُمْ شَرَابًا
طَهُورًا ﴿٢١﴾ إِنَّ هَٰذَا كَانَ لَكُمْ جَزَآءً وَكَانَ سَعْيُكُم مَّشْكُورًا ﴿٢٢﴾ إِنَّا
نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ ٱلْقُرْءَانَ تَنزِيلًا ﴿٢٣﴾ فَٱصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تُطِعْ
مِنْهُمْ ءَاثِمًا أَوْ كَفُورًا ﴿٢٤﴾ وَٱذْكُرِ ٱسْمَ رَبِّكَ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٢٥﴾

Mwenyezi Mungu alililijua hilo kutoka ndani ya nafsi zao na ndio akawasifu kwalo. **HATUTAKI KUTOKA KWENU KULIPWA WALA SHUKURANI** Yaani: Hatutaki kutoka kwenu malipo kwa tendo hili la kukupatieni chakula, na wala hatutaki kutoka kwenu mtushukuru. Bali hayo tuliyofanya tumeyafanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu.

10 **SISI TUNAOGOPA KWA MOLA WETU SIKU YA KUKUNJANA KWA USO** Nyuso siku hiyo zitakunjana kwa misukosuko yake na uzito wake. **MGUMU SANA** Yenye shida, yenye usumbufu.

11 **MWENYEZI MUMNGU AKAWAKINGA SHARI YA SIKU HIYO** Yaani: Akawakinga shari yake kwa sababu ya kumuogopa yeye na kutoa kwao chakula kwa ajili yake. **NA AKAWAKUTANISHA NA UNAWIRI NA FURAHA** Akawapa kunawiri katika nyuso na furaha rohoni badala ya kukunjana kwa nyuso kuliopo kwa makafiri. Kunawiri ni weupe na kutakata kuliopo katika nyuso zao kutokana na athari ya neema.

12 **NA AKAWALIPA PEPO NA HARIRI KWA UVUMILIVU**

13 **WAKIWA WAMEEGEMEA HUMO JUU YA VITI** Amewalipa pepo huku wakiwa wameegema peponi humo juu ya viti ambavyo juu yake vina vitambaa laini. **HAWATAONA HUMO JUA WALA BARIDI** Hawataona peponi joto la jua wala baridi kali.

14 **NA VIKO KARIBU NAO VIVULI VYAKE** Maana ni kwamba vivuli vya miti ya peponi viko karibu na wao, vimewafunika, ikiwa ni nyongeza juu ya neema zao ingawa huko hakuna jua. **NA VIMERAHISISHWA SANA VIKONYO VYA MATUNDA YAKE** Matunda yake yamerahisishwa kwa wachumaji wake urahisi anaoumudu aliyesimama, aliyekaa kitako na aliyejilaza ubavu. Umbali au mwiba hauwi kikwazo cha kuyachuma.

15 **NA WATAZUNGUSHIWA VYOMBO VYA FEDHA NA GLASI** Yaani: Wanapotaka vinywaji, wahudumu watawazungushia vyombo vya fedha na glasi za fedha.

16 **GLASI ZA FEDHA** Glasi za watu wa peponi ni za fedha. Umekutana kwenye glasi hizo weupe wa fedha na weupe wa kioo. Vioo vilivyopo duniani vinatokana na kokoto. Mwenyezi Mungu amejulisha ubora wa vioo hivyo kuwa vinatokana na fedha. Kwa nje yake, kinaonekana kilichomo ndani yake. **WAMEZIKADIRIA MAKADIRIO** zimekadiriwa zikaja kama walivyotaka katika umbile. Haziongezeki wala hazipungui.

17 **NA WATANYWESHWA HUMO GLASI AMBAZO MCHANGANYIKO WAKE NI TANGAWIZI** Glasi ni chombo ambacho ndani yake mna mvinyo. Yaani: Mvinyo uliochanganywa na Tangawizi.

18 **CHEMCHEMI ILIOMO HUMO INAITWA SALSABIL** Salsabil katika lugha ya Kiarabu ni jina la maji yaliyofikia kilele cha wepesi, yapitayo kwa kasi, yanayopita kwa ulaini kwenye koo zao.

19 **NA WATAWAZUNGUKA VIJANA WENYE KUDUMU.** Vijana wenye kubaki katika hali yao ya ujana, unawiri na ushababi. Hawazeeki, hawabadiliki na wala hawafi. **UKIWAONA UTAWADHANIA LULU ZILIZOSAMBAZWA** Kwa sababu ya uzuri wao uliozidi, un'garaji wa rangi zao na unawiri wa nyuso zao. Mwenyezi Mungu amewafananisha na lulu zilizo sambazwa kwa vile wao ni wepesi sana katika kutoa huduma, tofauti na *Huuril-aini* ambao amewafananisha na lulu iliyomo ndani ya chaza kwa sababu wao hawashughuliki kutoa huduma.

20 **NA KAMA UTAKUONA HUKO** Yaani: Kama utatupia macho yako huko peponi. **UTAONA NEEMA** isiyo elezeka. **NA UFALME**

**MKUBWA** Usiowezekana kukadiriwa.
21 **JUU YAO KUNA NGUO YA SUNDUSI YA KIJANI NA ISTABRAKI** ***Sundusi*** ni hariri nyepesi, na ***Istabraki*** ni hariri nzito. **NA WAMEPAMBWA KWA VIKUKU VYA FEDHA** Katika Suurat Faatir, imesemwa kuwa: **"WATAPAMBWA HUMO KWA VIKUKU VYA DHAHABU".** Suurat Faatir (35), aya 33. Kila mmoja, atavaa kile nafsi yake inachokipenda katika mapambo hayo. **NA MOLA WAO ATAWANYWESHA KINYWAJI SAFI** Abu-qilaaba na Ibrahim Annakha'ii wemesema kuwa: "*Wataletewa chakula. Wakifikia mwisho wake, wataletewa kinywaji safi. Watakunywa na matumbo yao yatajaa kutokana na kinywaji hicho na jasho litachuruzika kutoka kwenye miili yao likinukia vizuri kama harufu ya Miski.*
22 **KWA YAKINI, HAYA YAMEKUWA MALIPO KWENU** Yaani: Wataambiwa: "Hizi aina za neema zilizotajwa ni malipo yenu kwa sababu ya matendo yenu". **NA MATENDO YENU YAMEKUWA YENYE KUSHUKURIWA** Kushukuru kwa Mwenyezi Mungu matendo ya mja wake ni kuyakubali matendo hayo kwa sababu ya utiifu wake.
23 **KWA YAKINI, SISI NDIO TULIOKUTEREMSHIA QUR'ANI KUITEREMSHA KIDOGO KIDOGO** Yaani: Katika kuiteremsha, tumeiteremsha kwa mafungu mafungu na hatukuiteremsha kwa mkupuo mmoja. Pia haikutoka kwako kama makafiri wanavyodai.
24 **KWA HIYO, IVUMILIE HUKUMU YA MOLA WAKO** Na miongoni mwa hukumu zake ni kuchelewesha msaada wake kwako mpaka pale busara zake zilipotaka. **NA USIMTII MIONGONI MWAO MFANYAMADHAMBI AU MPINGAJI SANA** Yaani: Usimtii yeyote miongoni mwao, iwe ni mfanyamakosa au mwenye kupindukia mipaka katika ukafiri. Imesemwa pia kwamba muradi wa kauli yake MFANYAMADHAMBI ni Utba bin Rabia, na MPINGAJI SANA ni Waliid binil Mughiira, kwa sababu wao walimwambia Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: "Acha jambo hili (la mahubiri yako) na sisi tutakuridhisha kwa mali na kukuozesha".
25 **NA LITAJE JINA LA MOLA WAKO ASUBUHI NA JIONI** Swali kwa ajili ya Mola wako mwanzo wa mchana na mwisho wake. Mwanzo wa mchana ni swala ya Asubuhi, na mwisho wake ni swala ya Alasiri.
26 **NA KATIKA USIKU MSUJUDIE NA UMTAKASE KIPINDI KIREFU CHA USIKU**
27 **KWA YAKINI, HAWA WANAPENDA YA HARAKA** Yaani: Makafiri wa Makka na wale wanaoafikiana nao wanaipenda nyumba ya haraka, nayo ni nyumba ya dunia. **NA WANAIACHA NYUMA YAO SIKU NZITO** Hiyo ni siku ya Kiyama. Imeitwa siku nzito kwa sababu ya matatizo na misukosuko iliomo ndani ya siku hiyo. Wao hawajiandai kwa siku hiyo na wala hawaijali!
28 **SISI TUMEWAUMBA WAO NA TUMEVITIA NGUVU VIUNGO VYAO** Yaani: Tumevitia nguvu viungo vyao kwa kuviunganisha baadhi kwa baadhi nyingine kwa mishipa midogo na mikubwa. **NA TUKITAKA TUTABADILISHA MFANO WAO KUBADILISHA** Yaani: Kama tungalitaka tungaliwaangamiza na tukawaleta walio watiifu zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko wao.
29 **KWA HAKIKA, HUU NI UKUMBUSHO** Yaani: Sura hii ni ukumbusho. **BASI ANAYE TAKA, ATATENGENEZA NJIA YA KWENDA KWA MOLA WAKE** Yaani: Kwa kuamini na kutii.
30 **NA HAMTATAKA ILA TU AKITAKA MWENYEZI MUNGU MOLA WA WALIMWENGU** Yaani: Hamtataka kufanya njia ya kwenda kwa Mwenyezi Mungu isipokuwa tu apende Mwenyezi Mungu. Jambo hilo liko kwake na sio kwao. Kheri na shari iko mkononi mwake. Utashi wa mja ni mtupu, hauleti kheri na wala hauondoi shari, isipokuwa tu ikiwa Mwenyezi Mungu ataidhinisha hayo. **KWA YAKINI, MWENYEZI MUNGU NI MJUZI SANA, MWENYE HEKIMA SANA**
31 **ANAMUINGIZA AMTAKAYE KATIKA REHEMA ZAKE** Yaani: Anamuingiza katika rehema zake amtakaye kumuingiza humo, au anamuingiza katika pepo yake yule amtakaye katika waja wake. **NA MADHALIMU AMEWAANDALIA ADHABU IUMIZAYO.**

## SUURATUL MURSALAAT(77)

Imeteremka Makka aya zake ni hamsini
*Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.*

1 **NINAAPA KWA VITUMWAVYO KWA UPOLE** Mwenyezi Mungu Mtukufu anaapa kwa Malaika watumwao kufikisha *wahyi* (ufunuo) wake, amri zake na makatazo yake.
2 **NA VIVUMISHAVYO UPEPO KWA KASI** Hao ni Malaika waliopewa jukumu la kupeleka upepo wakiupeleka kwa kasi. Imesemwa pia kwamba: Hao ni Malaika wanaozipeleka roho za makafiri kwa kasi. Pia imesemwa kwamba VINAVYOTUMWA KWA UPOLE na VIVUMISHAVYO UPEPO ni upepo unaopelekwa kwa sura ya kimbunga kivumacho

وَمِنَ ٱلَّيْلِ فَٱسْجُدْ لَهُۥ وَسَبِّحْهُ لَيْلًا طَوِيلًا ﴿٢٦﴾ إِنَّ
هَٰٓؤُلَآءِ يُحِبُّونَ ٱلْعَاجِلَةَ وَيَذَرُونَ وَرَآءَهُمْ يَوْمًا ثَقِيلًا ﴿٢٧﴾ نَّحْنُ
خَلَقْنَٰهُمْ وَشَدَدْنَآ أَسْرَهُمْ ۖ وَإِذَا شِئْنَا بَدَّلْنَآ أَمْثَٰلَهُمْ تَبْدِيلًا
﴿٢٨﴾ إِنَّ هَٰذِهِۦ تَذْكِرَةٌ ۖ فَمَن شَآءَ ٱتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِۦ سَبِيلًا ﴿٢٩﴾
وَمَا تَشَآءُونَ إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٠﴾
يُدْخِلُ مَن يَشَآءُ فِى رَحْمَتِهِۦ ۚ وَٱلظَّٰلِمِينَ أَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٣١﴾

## سُورَةُ المُرْسَلَات

ترتيبها ٧٧ — آياتها ٥٠

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلْمُرْسَلَٰتِ عُرْفًا ﴿١﴾ فَٱلْعَٰصِفَٰتِ عَصْفًا ﴿٢﴾ وَٱلنَّٰشِرَٰتِ نَشْرًا ﴿٣﴾
فَٱلْفَٰرِقَٰتِ فَرْقًا ﴿٤﴾ فَٱلْمُلْقِيَٰتِ ذِكْرًا ﴿٥﴾ عُذْرًا أَوْ نُذْرًا ﴿٦﴾ إِنَّمَا
تُوعَدُونَ لَوَٰقِعٌ ﴿٧﴾ فَإِذَا ٱلنُّجُومُ طُمِسَتْ ﴿٨﴾ وَإِذَا ٱلسَّمَآءُ فُرِجَتْ
﴿٩﴾ وَإِذَا ٱلْجِبَالُ نُسِفَتْ ﴿١٠﴾ وَإِذَا ٱلرُّسُلُ أُقِّتَتْ ﴿١١﴾ لِأَىِّ يَوْمٍ أُجِّلَتْ
﴿١٢﴾ لِيَوْمِ ٱلْفَصْلِ ﴿١٣﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا يَوْمُ ٱلْفَصْلِ ﴿١٤﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ
لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٥﴾ أَلَمْ نُهْلِكِ ٱلْأَوَّلِينَ ﴿١٦﴾ ثُمَّ نُتْبِعُهُمُ ٱلْءَاخِرِينَ
﴿١٧﴾ كَذَٰلِكَ نَفْعَلُ بِٱلْمُجْرِمِينَ ﴿١٨﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٩﴾

kwa kutekeleza kile ambacho upepo huo umetumwa kukitekeleza, iwe ni neema au nakama (shari). Upepo huo pia ni ule unao sambaza mawingu na kuyatawanya.

(3) **NA VINAVYOSAMBAZA KUSAMBAZA** Hao ni Malaika waliopewa jukumu la kusambaza mawingu ya mvua na kuyatawanya, au wanakunjua mbawa zao angani wakati wa kuteremka na *wahyi*.

(4) **NA VINAVYOTENGANISHA KUTENGANISHA** Yaani: Malaika wanaoteremka na yanayo tenganisha kati ya haki na batili, halali na haramu.

(5) **NA VINAVYORUSHA UKUMBUSHO** Hao ni Malaika. Yaani: Wanapeleka wahyi kwa Mitume. Pia imesemwa kwamba aya tatu za mwanzo ni upepo, na aya ya nne na ya tano ni Malaika.

(6) **KWA KUONDOA UDHURU AU KUHADHARISHA** Maana ni kwamba Malaika wanapeleka wahyi ikiwa ni kwa ajili ya kuondoa hoja ya kuwepo kwa udhuru ambayo Mwenyezi Mungu anaielekeza kwa viumbe wake na pia ni kwa ajili ya hadharisho la adhabu yake. Imesemwa pia kwamba: Ni kwa ajili ya udhuru kwa wenye kufanya haki na hadharisho kwa wafanya maovu.

(7) **KWA YAKINI, MNACHOAHIDIWA KITATOKEA** Yaani: Yale mnayoahidiwa ikiwa ni pamoja na kuja kwa Kiyama na kufufuliwa yatatokea tu, hakuna pingamizi. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akafafanua ni lini yatatokea hayo akasema:

(8) **BASI NYOTA ZITAKAPOZIMWA,** Yaani: Itakapofutwa nuru yake na mwanga wake ukaondoka,

(9) **NA MBINGU ITAKAPOPASULIWA** Yaani: Mbingu ikakapofunguliwa na kupasuliwa.

(10) **NA MILIMA ITAKAPONG'OLEWA** Yaani: Itakapong'olewa kutoka mahali ilipo na kupeperuka angani ikawa vumbi na, hivyo, pale mahali ilipong'olewa pakawa tambarare sawa na ardhi.

(11) **NA MITUME WATAKAPOPANGIWA WAKATI** Wakapangiwa wakati wa hukumu kati yao na kati ya umma.

(12) **KWA SIKU IPI WAMEWEKEWA MUDA?** Yaani: Ni kwa siku kubwa ambayo waja wataishangaa kwa sababu ya uzito wake na mikukusuko yake ya ziada. Mitume wamewekewa muda wa kujumuika kwao. Watafika muda huo ili watoe ushahidi juu ya umma wao.

(13) **KWA SIKU YA KUTENGANISHA** Siku hiyo, patatenganishwa kati ya watu kwa matendo yao. Watatenganishwa; wa peponi kwenda peponi na wa motoni kwenda motoni.

(14) **NA NINI KILICHOKUJULISHA WEWE, NI IPI SIKU YA KUTENGANISHA?** Yaani: Na ni kitu gani kilichokujulisha siku ya kutenganisha? Yaani: Hilo ni jambo kubwa mno lisilokadirika!

(15) **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Yaani: Ole wao ndani ya siku hiyo ya kutisha! Ole wao ni tishio la maangamizi.

(16) **HIVI HATUKUWAANGAMIZA WA MWANZO?** Hao ni makafiri wa mataifa yaliyopita kuanzia Adamu mpaka kabla ya Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Mwenyezi Mungu anakusudia kuwa amewaangamiza kwa adhabu hapa duniani pale walipowapinga Mitume wao.

(17) **KISHA TUTAWAFUATISHIA WA MWISHO** Yaani: Wa mwisho ni makafiri wa Makkah na wale wanaokubaliana nao pale walipompinga Mtume Muhammad Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.

(18) **KAMA HIVYO TUTAFANYA KWA WAOVU** Yaani: Maangamizi kama hayo tutayafanya kwa kila mshrikina, ima duniani au Akhera.

(19) **OLE WAO SIKU HIYO WENYE**

أَلَمْ نَخْلُقكُّم مِّن مَّآءٍ مَّهِينٍ ﴿٢٠﴾ فَجَعَلْنَٰهُ فِى قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿٢١﴾ إِلَىٰ قَدَرٍ
مَّعْلُومٍ ﴿٢٢﴾ فَقَدَرْنَا فَنِعْمَ ٱلْقَٰدِرُونَ ﴿٢٣﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٤﴾
أَلَمْ نَجْعَلِ ٱلْأَرْضَ كِفَاتًا ﴿٢٥﴾ أَحْيَآءً وَأَمْوَٰتًا ﴿٢٦﴾ وَجَعَلْنَا فِيهَا رَوَٰسِىَ
شَٰمِخَٰتٍ وَأَسْقَيْنَٰكُم مَّآءً فُرَاتًا ﴿٢٧﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٨﴾
ٱنطَلِقُوٓا۟ إِلَىٰ مَا كُنتُم بِهِۦ تُكَذِّبُونَ ﴿٢٩﴾ ٱنطَلِقُوٓا۟ إِلَىٰ ظِلٍّ ذِى ثَلَٰثِ
شُعَبٍ ﴿٣٠﴾ لَّا ظَلِيلٍ وَلَا يُغْنِى مِنَ ٱللَّهَبِ ﴿٣١﴾ إِنَّهَا تَرْمِى بِشَرَرٍ
كَٱلْقَصْرِ ﴿٣٢﴾ كَأَنَّهُۥ جِمَٰلَتٌ صُفْرٌ ﴿٣٣﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٤﴾
هَٰذَا يَوْمُ لَا يَنطِقُونَ ﴿٣٥﴾ وَلَا يُؤْذَنُ لَهُمْ فَيَعْتَذِرُونَ ﴿٣٦﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ
لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٧﴾ هَٰذَا يَوْمُ ٱلْفَصْلِ جَمَعْنَٰكُمْ وَٱلْأَوَّلِينَ ﴿٣٨﴾ فَإِن كَانَ
لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيدُونِ ﴿٣٩﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٠﴾ إِنَّ ٱلْمُتَّقِينَ فِى
ظِلَٰلٍ وَعُيُونٍ ﴿٤١﴾ وَفَوَٰكِهَ مِمَّا يَشْتَهُونَ ﴿٤٢﴾ كُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ هَنِيٓـًٔا
بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٤٤﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ
لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٥﴾ كُلُوا۟ وَتَمَتَّعُوا۟ قَلِيلًا إِنَّكُم مُّجْرِمُونَ ﴿٤٦﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ
لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ ٱرْكَعُوا۟ لَا يَرْكَعُونَ ﴿٤٨﴾ وَيْلٌ
يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ فَبِأَىِّ حَدِيثٍۭ بَعْدَهُۥ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٠﴾

**KUPINGA** Yaani: Siku ya maangamizi hayo, Ole wao wenye kupinga vitabu vya Mwenyezi Mungu na Mitume wake.

(20) **HIVI HATUKUKUUMBENI NYINYI KUTOKANA NA MAJI DUNI?** Yaani: Maji dhaifu, duni, nayo ni tone la *manii.*

(21) **TUKAYAWEKA MAHALA TULIVU, MADHUBUTI** Yaani: Mahali penye ulinzi, napo ni mfuko wa uzazi.

(22) **MPAKA MUDA MAALUM** Nao ni muda wa ujauzito (miezi tisa kwa kawaida).

(23) **TUKAKADIRIA NA WAKADIRIAJI WAZURI NI SISI** Yaani: Tukavikadiria viungo vyake na sifa zake, na kila hali miongoni mwa hali zake tukaziweka katika sifa tuliyoitaka. Kwa hiyo, mkadiriaji bora ni Mwenyezi Mungu S.W.

(24) **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Ole wao wenye kupinga uwezo wetu juu ya hayo.

(25) **HIVI HATUKUIFANYA ARDHI NI KIKUSANYAJI?** Kukusanya ni kujumuisha. Maana ni kwamba : Hivi hatukuifanya ardhi imekusanya juu ya mgongo wake viumbe walio hai ndani ya majumba yao, na wafu ndani ya tumbo lake inawakusanya?

(26) **WALIO HAI NA WALIOKUFA** Khalili amesema kuwa: *Kaft (kujumuisha) ni kukigeuza kitu; ndani nje na nje ndani. (Wanadamu wanakuwa wametokana na mchanga wa ardhi. Kisha wataishi juu ya mgongo wake wakiwa hai. Kisha watabadilika humo wakiwa maiti)*

(27) **NA TUKAWEKA HUMO MILIMA MIREFU NA TUKAKUNYWESHENI MAJI MATAMU** Yaani: Maji matamu. Haya yote ni ya ajabu zaidi kuliko kufufua.

(28) **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Ole wao wenye kupinga neema zetu tulizowaneemesha na amabazo hizi ni jumla ya neema hizo.

(29) **NENDENI KWENYE KILE MLICHOKUWA MNAKIPINGA** Nendeni kwenye kile mlichokuwa mnakipinga duniani. Hayo wataambiwa na wahudumu wa Jahanamu. Yaani: Nendeni kwenye ile adhabu mliyokuwa mnaipinga.

(30) **NENDENI KWENYE KIVULI CHENYE MATAWI MATATU** Yaani: Nendeni kwenye kivuli cha moshi wa Jahannamu uliofuka kisha ukagawika makundi matatu. Mtakuwemo humo mpaka imalizike hisabu.

(31) **SI KIVULI CHA KUPOZA WALA HAKIKINGI UKALI WA MIALE YA MOTO** Hamna katika kivuli hicho baridi ya kivuli cha duniani na wala hakitawakinga joto la Jahannamu.

(32) **KWA YAKINI, MOTO HUO UNARUSHA CHECHE KAMA JUMBA** Yaani: Kila cheche miongoni mwa cheche zake unazozirusha ni kama jumba miongoni mwa majumba katika ukubwa wake. Cheche ni moto unaopeperuka ukiwa umeachana. Jumba ni jengo kubwa.

(33) **KAMA KWAMBA CHECHE HIZO NI NGAMIA WA MANJANO** Hao ni ngamia. Alfarraa-u amesema kuwa: "*Ngamia wa manjano ni ngamia weusi. Hawezi kuonekana ngamia mweusi isipokuwa atakuwa amechanganyika na umanjano. Kwa ajili hiyo, Waarabu wamewaita ngamia weusi ngamia wa manjano"*. Imesemwa pia kwamba cheche inapopeperuka na kuanguka na ikawa ingali na rangi ya moto, inakuwa kitu kinachofanana sana na ngamia mweusi.

(34) **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Ole wao wenye kuwapinga Wajumbe wa Mwenyezi Mungu na aya zake.

(35) **HII NI SIKU AMBAYO HAWATATAMKA** Yaani: Hawatazungumza, kwa sababu ya misukosuko watakayoiona ikiwakumba waja katika mahali pa mkusanyiko.

(36) **NA HAWATARUHUSIWA KUTOA UDHURU** Yaani: Mwenyezi Mungu hawapi ruhusa ili wapate kutoa udhuru.

(37) **OLE WAO SIKU HIYO WENYE**

**KUPINGA**
38 **HII NDIO SIKU YA UTENGANO. TUMEKUKUSANYENI NYINYI NA WA MWANZO** Yaani: Wataambiwa: "Hii ndio siku ya utengano ambayo kutatenganishwa kati ya viumbe. Pia haki itatengana na batili. Tumekukusanyeni ninyi makafiri wa Kiquraishi pamoja na makafiri wa mwanzo ambao ni makafiri wa mataifa yaliyopita.
39 **BASI IKIWA MNAVYO VITIMBI,** Yaani: Mkiweza kufanya vitimbi hivi sasa,
**NIFANYIENI** Mwenyezi Mungu anasema: Ikiwa mnao ujanja basi fanyeni dhidi yangu.
40 **OLE WAO SIKU HIYO WENYE UPINGA**
41 **KWA YAKINI, WENYE UCHAMUNGU WATAKUWA KATIKA VIVULI NA CHEMCHEMI** Yaani: Watakuwa katika vivuli vya miti na vivuli vya majumba, sio kama kivuli cha moshi au moto kwa makafiri kama ilivyotangulia kuelezwa.
42 **NA MATUNDA KATIKA YALE WAYAPENDAYO** Katika yale ambayo nafsi zao zinayataka na hamu zao zinayatamani.
43 **KULENI NA KUNYWENI KWA RAHA, KWA SABABU YA YALE MLIYOKUWA MNAYAFANYA** Yaani: Kwa sababu ya matendo mema mliyokuwa mnayafanya duniani.
44 **KWA YAKINI, SISI, KAMA HIVYO, TUNAWALIPA WAFANYAO MAZURI** Yaani: Mfano wa malipo hayo makubwa tunawalipa wafanyao vizuri katika matendo yao.
45 **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Pale watakapokuwa katika dhiki kubwa mno, na waumini wakiwa katika neema ya kudumu.
46 **KULENI NA STAREHENI KIDOGO. KWA YAKINI, NYINYI NI WAOVU** Yaani: Wanaambiwa haya duniani, na waovu washirikina wanaomshirikisha Mwenyezi Mungu.
47 **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Mwenyezi Mungu amerudia rudia maneno haya kwa kutahayariza na kugonga.
48 **NA PINDI WAKIAMBIWA: RUKUUNI, HAWARUKUU** Yaani: Wakiamrishwa kuswali hawaswali. Imesemwa pia kwamba: Wataambiwa hayo huko akhera pale watapotakiwa kusujudu na, lakini, hawataweza.
49 **OLE WAO SIKU HIYO WENYE KUPINGA** Ole wao wenye kupinga amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu na makatazo yake.
50 **BASI NI MAELEZO YAPI BAADA YAKE WATAYAAMINI?** Yaani: Ni maelezo yapi yasiyokuwa Qur'ani watayakubali wasipoikubali Qur'ani?

# SURA ANNABA'I (78)

*Ni ya Makka Aya zake ni arobaini*

1 **KUHUSU NINI WANAULIZANA?** Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipopewa utume na kuwaeleza watu wa Makka upekee wa Mwenyezi Mungu, kufufuliwa baada ya kufa na kuwasomea Qur'ani, walikuwa wakiulizana kati yao wakisema: Hivi huyu Muhammad amepatwa na nini? Na ni kitu gani ameletewa? Mwenyezi Mungu aliiteremsha aya hii. Maana ya aya ni kwamba: Wanaulizana kuhusu nini? Kisha akalijibu Mwenyezi Mungu swali hili kwa neno lake:
2 **NI KUHUSU HABARI KUBWA** Ni habari nzito, nayo ni Qur'ani tukufu, kwa vile inazungumzia upekee wa Mwenyezi Mungu, ukweli wa Mtume (Muhammad) na kutokea kufufuliwa na kukusanywa (baada ya kufa).
3 **(HABARI) AMBAYO WAO NDANI YAKE WANATOFAUTIANA** Wametofautiana katika Qur'ani. Baadhi yao wameifanya kuwa ni uchawi, baadhi yao wameifanya kuwa ni ushairi na baadhi yao wamesema kuwa ni vigano vya watu wa kale.
4 **WAKOME. PUNDE TU WATAJUA** Ni kemeo kwao. Kisha Mwenyezi Mungu amelirudia kemeo hilo akasema:
5 **KISHA WAKOME. PUNDE TU WATAJUA** Huu ni upeo wa juu wa kusisitiza, na ni kemeo kali. Maana ya makemeo haya ni kwamba: Haistahiki watofautiane kuhusu Qur'ani, kwani Qur'an ni kweli na, kwa hiyo, wale wanaoipinga watakujajua hatima ya kupinga kwao.
6 **HIVI HATUKUIFANYA ARDHI KUWA TANDIKO?** Tandiko ni kikanyagio na kilalio kama vile kilalio cha mtoto anachotandikiwa na kulazwa juu yake.
7 **NA MILIMA KUWA VIGINGI?** Yaani: Tumeifanya milima kama vigingi kwa ardhi ili itulie na isitikisike.
8 **NA TUMEKUUMBENI (NYINYI KUWA) PEA** Yaani: Wanaume na wanawake.
9 **NA TUMEUFANYA USINGIZI WENU KUWA PUMZISHO** Yaani: Pumzisho la miili yenu. *Subaat*: ni kuisha kwa harakati za mtu na ilhali roho ikiwa bado ipo mwilini mwake.
10 **NA TUMEUFANYA USIKU KUWA VAZI** Yaani: Tunakuvisheni giza lake na kukufinikeni kwa giza hilo kama vazi linavyokufinikeni.
11 **NA TUMEUFANYA MCHANA KUWA NI WAKATI WA MAISHA** Yaani: Tumeufanya mchana utoe mwanga ili wanadamu wahangaikie mambo yanayohusu maisha yao na riziki anazowakasimia Allah.
12 **NA TUMEJENGA JUU YENU MBINGU SABA MADHUBUTI** Mwenyezi Mungu

anakusudia kuwa ni mbingu saba zenye umbile lenye nguvu na lililojengwa madhubuti.

**13 NA TUMEWEKA TAA YENYE KUWAKA** Kusudio la taa ni jua. Mwenyezi Mungu ameweka ndani yake mwanga na joto. Neno *wahj* (muwako) linakusanya mwanga na joto.

**14 NA TUMETEREMSHA KUTOKA MAWINGUNI MAJI YANAYO TIRIRIKA KWA WINGI** *Al-Mu'uswiraat* ni mawingu yanayojikamua kwa maji wakati bado hazijanyesha mvua. *Thajjaaj* ni maji yanoyomiminika kwa wingi.

**15 ILI TUTOE KWA MAJI HAYO NAFAKA NA MIMEA** Yaani: Ili tutoe (tuoteshe) kwa maji hayo nafaka za chakula kama vile ngano, shairi na mfano wake. Na mimea ni ile wanayokula wanyama kama vile nyasi na mimea mingine.

**16 NA BUSTANI ZENYE KUSONGANA** Bustani zenye kushikana kwa matawi yake mengi.

**17 HAKIKA YA SIKU YA KUTENGANA INA WAKATI** Wakati wa mkusanyiko na muda wa kukusanyika watu wa mwanzo na wa mwisho. Katika muda huo, watu watakuwa wamefika kwenye yale waliyoahidiwa; ikiwa ni thawabu au adhabu. Siku hiyo imeitwa "Siku ya Kutengana" kwa sababu Allah atatenganisha kati ya viumbe wake (kati ya wema na waovu).

**18 SIKU ITAKAPOPULIZWA PARAPANDA MKAJA MKIWA MAKUNDI KWA MAKUNDI** Yaani: Mtakuja mahali pa kukusanywa mkiwa makundi makundi. Parapanda ni pembe ambayo (Malaika) Israafiil ataipuliza.

**19 NA IKAFUNGULIWA MBINGU IKAWA MILANGO** Itafunguliwa mbingu na kuwa na milango mingi ili Malaika wateremke.

**20 NA IKAENDESHWA MILIMA IKAWA MAN'GATI.** Milima itango'lewa kutoka katika sehemu zake na kupeperushwa hewani ikawa vumbi lililosambaa kiasi mtazamaji atadhani kuwa ni man'gati.

**21 HAKIKA YA JAHANNAMU NI KIVIZIO** Jahannamu katika hukumu ya Mwenyezi Mungu ni mahali pa kuvizia. Malaika wa motoni wanawavizia makafiri ili wawape adhabu humo, au (inawezekana kuwa) Jahanamu yenyewe inawanyemelea makafiri waingiao humo kama wawindaji wanavyonyemelea mnyama anayewapitia na anayewajia.

**22 KWA WANAOA MIPAKA NI MAREJEO** Ni marejeo watakayorejea.

**23 WATABAKI HUMO MILELE** Yaani: Makafiri watabaki motoni zama zote. "*Haqab*" ni kipindi kirefu cha muda. Kinapopita kipindi, kinaingia kingine, kisha kingine, kisha hivyo hivyo mpaka milele.

**24 HAWAONJI HUMO BARIDI WALA KINYWAJI** Yaani: Hawataonja ndani ya Jahanamu au ndani ya kipindi hicho baridi itakayowapoza na joto lake wala kinywaji kitachowasaidia kupoza kiu chake.

سُورَةُ النَّبَإِ — ترتيبها ٧٨ — آياتها ٤٠

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

عَمَّ يَتَسَاءَلُونَ ﴿١﴾ عَنِ النَّبَإِ الْعَظِيمِ ﴿٢﴾ الَّذِي هُمْ فِيهِ مُخْتَلِفُونَ ﴿٣﴾
كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ﴿٤﴾ ثُمَّ كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ﴿٥﴾ أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِهَادًا ﴿٦﴾
وَالْجِبَالَ أَوْتَادًا ﴿٧﴾ وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا ﴿٨﴾ وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا
﴿٩﴾ وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٠﴾ وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١١﴾ وَبَنَيْنَا
فَوْقَكُمْ سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٢﴾ وَجَعَلْنَا سِرَاجًا وَهَّاجًا ﴿١٣﴾ وَأَنزَلْنَا
مِنَ الْمُعْصِرَاتِ مَاءً ثَجَّاجًا ﴿١٤﴾ لِّنُخْرِجَ بِهِ حَبًّا وَنَبَاتًا ﴿١٥﴾ وَجَنَّاتٍ
أَلْفَافًا ﴿١٦﴾ إِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ كَانَ مِيقَاتًا ﴿١٧﴾ يَوْمَ يُنفَخُ فِي الصُّورِ
فَتَأْتُونَ أَفْوَاجًا ﴿١٨﴾ وَفُتِحَتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ أَبْوَابًا ﴿١٩﴾ وَسُيِّرَتِ
الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٢٠﴾ إِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿٢١﴾ لِّلطَّاغِينَ
مَآبًا ﴿٢٢﴾ لَّابِثِينَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿٢٣﴾ لَّا يَذُوقُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا
﴿٢٤﴾ إِلَّا حَمِيمًا وَغَسَّاقًا ﴿٢٥﴾ جَزَاءً وِفَاقًا ﴿٢٦﴾ إِنَّهُمْ كَانُوا
لَا يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿٢٧﴾ وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كِذَّابًا ﴿٢٨﴾ وَكُلَّ شَيْءٍ
أَحْصَيْنَاهُ كِتَابًا ﴿٢٩﴾ فَذُوقُوا فَلَن نَّزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٣٠﴾

**25 ISIPOKUWA MAJI YA MOTO NA USAHA** Hayo ni maji yaliyokolea moto. Na huo usaha ni wa watu wa motoni.

**26 IKIWA NI MALIPO MUAFAKA** Adhabu imelingana na kosa. Hakuna kosa kubwa zaidi ya shirki na hakuna adhabu kali zaidi ya moto. Matendo ya makafiri yalikuwa mabaya mno, kwa hiyo, Mwenyezi Mungu akawapa kile kitakachowaumiza zaidi.

**27 HAKIKA YA WAO WALIKUWA HAWATARAJII HISABU** Yaani: Walikuwa hawana tamaa ya kupata thawabu na walikuwa hawaogopi hisabu, kwa vile wao walikuwa hawaamini kufufuliwa.

**28 NA WAMEZIPINGA AYA ZETU KWA NGUVU ZAO ZOTE** Yaani: Wamezipinga aya za Qur'ani upinzani mkubwa kabisa.

**29 NA KILA KITU TUMEKIHIFADHI KWA MAANDISHI** Kila kitu tumekiandika katika *Lauhil-Mahfuudh* (Ubao uliohifadhiwa) ili Malaika wakielewe.Yasemekana pia kwamba

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا ﴿٣١﴾ حَدَآئِقَ وَأَعْنَٰبًا ﴿٣٢﴾ وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا ﴿٣٣﴾ وَكَأْسًا
دِهَاقًا ﴿٣٤﴾ لَّا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِذَّٰبًا ﴿٣٥﴾ جَزَآءً مِّن رَّبِّكَ عَطَآءً
حِسَابًا ﴿٣٦﴾ رَّبِّ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ٱلرَّحْمَٰنِ لَا يَمْلِكُونَ
مِنْهُ خِطَابًا ﴿٣٧﴾ يَوْمَ يَقُومُ ٱلرُّوحُ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ صَفًّا لَّا يَتَكَلَّمُونَ
إِلَّا مَنْ أَذِنَ لَهُ ٱلرَّحْمَٰنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾ ذَٰلِكَ ٱلْيَوْمُ ٱلْحَقُّ فَمَن
شَآءَ ٱتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِۦ مَـَٔابًا ﴿٣٩﴾ إِنَّآ أَنذَرْنَٰكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا يَوْمَ
يَنظُرُ ٱلْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ وَيَقُولُ ٱلْكَافِرُ يَٰلَيْتَنِى كُنتُ تُرَٰبًا ﴿٤٠﴾

## سُورَةُ النَّازِعَاتِ
ترتيبها ٧٩ — آياتها ٤٦

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلنَّٰزِعَٰتِ غَرْقًا ﴿١﴾ وَٱلنَّٰشِطَٰتِ نَشْطًا ﴿٢﴾ وَٱلسَّٰبِحَٰتِ سَبْحًا
﴿٣﴾ فَٱلسَّٰبِقَٰتِ سَبْقًا ﴿٤﴾ فَٱلْمُدَبِّرَٰتِ أَمْرًا ﴿٥﴾ يَوْمَ تَرْجُفُ ٱلرَّاجِفَةُ
﴿٦﴾ تَتْبَعُهَا ٱلرَّادِفَةُ ﴿٧﴾ قُلُوبٌ يَوْمَئِذٍ وَاجِفَةٌ ﴿٨﴾ أَبْصَٰرُهَا
خَٰشِعَةٌ ﴿٩﴾ يَقُولُونَ أَءِنَّا لَمَرْدُودُونَ فِى ٱلْحَافِرَةِ ﴿١٠﴾ أَءِذَا كُنَّا
عِظَٰمًا نَّخِرَةً ﴿١١﴾ قَالُوا۟ تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ﴿١٢﴾ فَإِنَّمَا هِىَ زَجْرَةٌ
وَٰحِدَةٌ ﴿١٣﴾ فَإِذَا هُم بِٱلسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾ هَلْ أَتَىٰكَ حَدِيثُ مُوسَىٰٓ ﴿١٥﴾

alichokikusudia Mwenyezi Mungu hapa ni matendo ya waja ambayo Malaika wanaotunza matendo yao wanayaandika.

(30) **KWA HIYO, ONJENI. KWANI HATUTAKUONGEZEENI ISIPOKUWA ADHABU TU** Wataelezwa haya kwa sababu ya ukafiri wao, matendo yao mabaya na kupinga kwao aya. Yaani: watakuwa katika nyongeza ya adhabu ya Mwenyezi Mungu siku zote.

(31) **HAKIKA,WENYE KUMCHA MWENYEZI MUNGU TU NDIO WENYE MAFANIKIO** Mafanikio *Mafaaz* ni kufanikiwa kukipata kinachohitajika na kusalimika na moto.

(32) **BUSTANI NA MIZABIBU**

(33) **NA WANAWAKE WENYE MATITI YALIYOSIMAMA, WENYE UMRI MMOJA** Yaani: Watapata wanawake wenye matiti yaliyosimama.Yaani: Matiti yao yamesimama vifuani mwao, hayakuanguka; kwa kuwa wao ni wanawali, vigoli na wanaolingana katika umri.

(34) **NA GLASI ZILIZOJAA** Yaani: Glasi zilizojaa pombe.

(35) **HAWATASIKIA HUMO UPUUZI WALA KADHIBISHO** Yaani: Hawatasikia peponi upuuzi. Upuuzi ni maneno yasiyofaa. Na wala hawatakadhibiana wao kwa wao.

(36) **NI MALIPO KUTOKA KWA MOLA WAKO, NI TUZO, NI HISABU** Yaani: Mwenyezi Mungu amewalipa yaliyotajwa kwa sababu ya imani yao na matendo yao mema. Amewapa tuzo kwa kadiri ya wanayopaswa kuyapata kwa mujibu wa ahadi ya Allah. Kwani Allah ameahidi kulipa jema moja kwa kumi, na amewaahidi wengine jema moja kwa nyongeza mia saba, na amewaahidi wengine malipo yasiyo na mwisho wala kiwango.

(37) **MOLA WA MBINGU NA ARDHI NA VILIVYOMO KATI YAKE, MWENYE REHEMA NYINGI. HAWAMILIKI KWAKE KUSEMESHA** Yaani: Hawawezi kuomba ila kile walichoruhusiwa na Allah, na hawamilimki kuwaombea wenye makosa ila kwa ruhusa yake.

(38) **SIKU ATAKAYOSIMAMA ROHO NA MALAIKA KWA MSTARI. HAWATASEMA ISIPOKUWA TU WALE WALIORUHUSIWA NA (MWENYEZI MUNGU) MWINGI WA REHEMA NA WAKISEMA YALIYO SAHIHI** Yaani: Malaika watakuwa wamesimama safu. Roho hapa ni malaika. Yasemekana kuwa ni malaika Jibril, na yasemekana kuwa maana ya roho hapa ni jeshi katika majeshi ya Mwenyezi Mungu na sio malaika. Pia yasemekana kuwa ni roho za wanadamu ambazo zitasimama mstari na malaika nao watasimama mstari. Hayo yatatokea kati ya pulizo mbili kabla roho hazijarejeshwa kwenye miili. Isipokuwa yule aliyeruhusiwa na Mwenyezi Mungu kuwaombea wenye makosa. Au hawatazungumza isipokuwa tu kuhusu haki ya mtu aliyemruhusu Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema mtu huyo akawa ni miongoni mwa watu waliokuwa duniani. (Yaani: Alikuwa akithibitisha upekee wa Mwenyezi Mungu (Tawhiid).

(39) **HIYO NDIYO SIKU YA HAKI. HIVYO, ANAYETAKA ATAJIANDALIA KWA MOLA WAKE MAREJEO** Siku ya kusimama kwao katika sura hiyo ni yenye kutokea hasa. Basi anayetaka atafanya marejeo kwa Mola wake kwa kutenda matendo mema.

(40) **HAKIKA YA SISI TUMEKUHADHARISHENI ADHABU ILIYO KARIBU. SIKU MTU ATAKAPOANGALIA KILICHOTANGULIZWA NA MIKONO YAKE NA KAFIRI ATASEMA: EE, LAITI MIMI NINGELIKUWA MCHANGA** Mwanadamu atayaona aliyoyatenda iwe ni kheri au shari. Kafiri atatamani awe mchanga, kwa sababu ya kuona adhabu mbali mbali alizoandaliwa na Allah.

# SURA ANNAAZIAAT (79)

*Ni ya Makka Aya zake ni arobaini na sita*
Sura hii pia inaitwa *Suratis-saahirah*

(1) **NINA APA KWA WANAON'GOA KWA NGUVU** Mwenyezi Mungu ameapa kwa Malaika ambao wanazitoa roho za waja kwenye miili yao, kama mtu anavyovuta mshale kwenye upinde akaukunjua mpaka mwisho. Wanavuta mvuto wa nguvu kabisa, kwa kuwa wanazitoa roho hizo kutoka ndani ya miili.

(2) **NA WENYE KUVUTA KWA HARAKA** Yaani: Malaika wanaozitoa roho kwenye miili kwa kuzivuta kwa nguvu. ANNASHT: ni kuvuta kwa haraka. Imesemwa kuwa Malaika ni wenye kuzitoa kwa haraka roho za waumini, na ni wenye kuzin'goa kwa nguvu roho za makafiri.

(3) **NA WANAO OGELEA KUOGELEA** Yaani: Malaika wanaoteremka kutoka mbinguni kwa haraka ili kutekeleza amri ya Allah.

(4) **KISHA WAENDAO KASI** Hao ni Malaika waendao kasi ili kuzifikisha haraka roho za waumini peponi.

(5) **KISHA WAPANGAO MAMBO** Upangaji mambo wa Malaika ni kule kuleta (ufunuo wa mafundisho ya) halali na haramu na ufafanuzi wake, na kuwapangia watu wa ardhini katika pepo, mvua na mengine yasiyokuwa hayo. Yasemwa kuwa upangaji wa mambo kwa watu wa duniani uko kwa malaika wanne, nao ni Jibril, Mikail, Izrail na Israfil. Jibril amepewa kazi ya pepo na askari. Mikail amepewa kazi ya mvua na mimea. Izrail amepewa kazi ya kutoa roho na Israfil yeye anawaletea wenzake amri (za Mwenyezi Mungu).

(6) **SIKU LITAKAPOTETEMESHA LA KUTETEMESHA** Tetemesho hilo ni mpulizo wa kwanza ambao kwa mpulizo huo viumbe vyote vitakufa.

(7) **LITAFUATIWA NA LA KULIFUATIA** La kulifuatia ni mpulizo wa pili ambao wakati wake viumbe vitafufuliwa.

(8) **NYOYO SIKU HIYO ZITAJAA HOFU** Nafsi zitajaa hofu na kutetemeka kwa sababu ya misukosuko ya siku ya Qiyama watakayoiona. Kwa sababu hiyo, nyoyo zitakuwa na hofu na mshtuko.

(9) **MACHO YAKE YATAKUWA DHALILI** Utajitokeza machoni mwao udhalili watakapoiona misukosuko ya siku ya Qiyama. Mwenyezi Mungu hapa anakusudia macho ya wale watakaokufa wakiwa hawako katika dini ya Kiislamu.

(10) **WANASEMA: HIVI SISI TUTAREJESHWA KATIKA MASHIMO?** Maneno haya wanayasema wale wapingao kufufuliwa wanapoambiwa kuwa watafufuliwa. Wanasema: Hivi tutarejeshwa katika hali yetu ya mwanzo na tuwe hai baada ya kufa na kuwa katika mashimo ya makaburi?

(11) **HIVI TUTAKAPOKUWA MIFUPA ILIYO CHAKAA (TUTAREJESHWA)?** Yaani: Tutakapokuwa mifupa iliyochakaa tutarejeshwa na kufufuliwa pamoja na kuwa hali hiyo iko mbali mno na uhai?

(12) **WAMESEMA: HAYO KAMA YATAKUWA KWELI, BASI NI MAREJEO YENYE HASARA** Yaani: Ikiwa tutarejeshwa baada ya kufa, tutapata hasara kwa sababu yatatupata hayo ayasemayo Muhammad.

(13) **HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA HUO NI MPULIZO MMOJA TU** Yaani: Msilione hilo haliwezekani, kwani huo ni mpulizo mmoja tu. Huu ni mpulizo wa pili ambao kwa mpulizo huo viumbe watafufuliwa.

(14) **MARA TU WAO WATAKUWA SAAHIRA** Imesemwa kuwa Saahira ni ardhi nyeupe ambayo Mwenyezi Mungu ataileta ili viumbe wahisabiwe juu yake.

(15) **JE, IMEKUFIKIA HABARI YA MUSA?** Yaani: Hakika, yamekujia na kukufikia katika visa vya Fir'auni na Musa mambo ambayo kwayo hujulikana habari zao.

(16) **WAKATI MOLA WAKE ALIPOMWITA KWENYE JANGWA TAKATIFU LA TUWA** Tuwaa ni jangwa twahara na lenye kubarikiwa. Nalo ni jangwa lililopo kwenye mlima Sinai mahali ambapo Allah alizungumza na Musa.

(17) **NENDA KWA FIR'AUNI, YEYE AMEVUKA MIPAKA** Yaani: Firauni amepindukia mipaka katika kufanya maasi, kiburi na kumkufuru Allah.

(18) **KAMWAMBIE: JE, WAPENDA KUTAKASIKA?** Yaani: Ukifika mwambie: Je, wapenda kutakasika na shirki? Musa aliamrishwa azungumze na Firauni kwa upole.

(19) **NA NIKUELEKEZE KWA MOLA WAKO ILI UOGOPE?** Yaani: Nikupe maelekezo ya kumwabudu na kumpwekesha Mola wako ili upate kuogopa adhabu yake? Woga haupatikani ila tu kwa mtu muongofu, aliyeongoka.

(20) **KISHA AKAMUONESHA MUUJIZA MKUBWA** Yasemekana kuwa muujiza huo ni fimbo, na yasemekana kuwa ni mkono wake.

(21) **AKAPINGA NA AKAASI** Firauni alimpinga Musa na yale aliyokuja nayo, na alimuasi Allah na hivyo hakumtii.

(22) **KISHA AKAPUUZA HUKU AKIHANGAIKA** Yaani: Firauni akaondoka na kuipuuza Imani. Akafanya uovu ardhini na kufanya juhudi za kuyapinga mambo aliyokuja nayo Musa.

(23) **KISHA AKAKUSANYA NA AKATOA WITO** Yaani: Firauni alikusanya jeshi lake kwa ajili ya: **1)** Kupigana vita au. **2)** Aliwakusanya wachawi ili kupingana (na Musa) au. **3)** Aliwakusanya watu ili washuhudie kinachotokea.

إِذۡ نَادَىٰهُ رَبُّهُۥ بِٱلۡوَادِ ٱلۡمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٦﴾ ٱذۡهَبۡ إِلَىٰ فِرۡعَوۡنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿١٧﴾
فَقُلۡ هَل لَّكَ إِلَىٰٓ أَن تَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾ وَأَهۡدِيَكَ إِلَىٰ رَبِّكَ فَتَخۡشَىٰ ﴿١٩﴾ فَأَرَىٰهُ
ٱلۡأٓيَةَ ٱلۡكُبۡرَىٰ ﴿٢٠﴾ فَكَذَّبَ وَعَصَىٰ ﴿٢١﴾ ثُمَّ أَدۡبَرَ يَسۡعَىٰ ﴿٢٢﴾ فَحَشَرَ
فَنَادَىٰ ﴿٢٣﴾ فَقَالَ أَنَا۠ رَبُّكُمُ ٱلۡأَعۡلَىٰ ﴿٢٤﴾ فَأَخَذَهُ ٱللَّهُ نَكَالَ ٱلۡأٓخِرَةِ وَٱلۡأُولَىٰٓ
﴿٢٥﴾ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبۡرَةٗ لِّمَن يَخۡشَىٰٓ ﴿٢٦﴾ ءَأَنتُمۡ أَشَدُّ خَلۡقًا أَمِ ٱلسَّمَآءُۚ بَنَىٰهَا
﴿٢٧﴾ رَفَعَ سَمۡكَهَا فَسَوَّىٰهَا ﴿٢٨﴾ وَأَغۡطَشَ لَيۡلَهَا وَأَخۡرَجَ ضُحَىٰهَا ﴿٢٩﴾
وَٱلۡأَرۡضَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ دَحَىٰهَآ ﴿٣٠﴾ أَخۡرَجَ مِنۡهَا مَآءَهَا وَمَرۡعَىٰهَا ﴿٣١﴾
وَٱلۡجِبَالَ أَرۡسَىٰهَا ﴿٣٢﴾ مَتَٰعٗا لَّكُمۡ وَلِأَنۡعَٰمِكُمۡ ﴿٣٣﴾ فَإِذَا جَآءَتِ ٱلطَّآمَّةُ
ٱلۡكُبۡرَىٰ ﴿٣٤﴾ يَوۡمَ يَتَذَكَّرُ ٱلۡإِنسَٰنُ مَا سَعَىٰ ﴿٣٥﴾ وَبُرِّزَتِ ٱلۡجَحِيمُ
لِمَن يَرَىٰ ﴿٣٦﴾ فَأَمَّا مَن طَغَىٰ ﴿٣٧﴾ وَءَاثَرَ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا ﴿٣٨﴾ فَإِنَّ ٱلۡجَحِيمَ
هِيَ ٱلۡمَأۡوَىٰ ﴿٣٩﴾ وَأَمَّا مَنۡ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ وَنَهَى ٱلنَّفۡسَ عَنِ ٱلۡهَوَىٰ
﴿٤٠﴾ فَإِنَّ ٱلۡجَنَّةَ هِيَ ٱلۡمَأۡوَىٰ ﴿٤١﴾ يَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلسَّاعَةِ أَيَّانَ مُرۡسَىٰهَا
﴿٤٢﴾ فِيمَ أَنتَ مِن ذِكۡرَىٰهَآ ﴿٤٣﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ مُنتَهَىٰهَآ ﴿٤٤﴾ إِنَّمَآ أَنتَ مُنذِرُ
مَن يَخۡشَىٰهَا ﴿٤٥﴾ كَأَنَّهُمۡ يَوۡمَ يَرَوۡنَهَا لَمۡ يَلۡبَثُوٓاْ إِلَّا عَشِيَّةً أَوۡ ضُحَىٰهَا ﴿٤٦﴾

ترتيبها ٨٠ — سُورَةُ عَبَسَ — آياتها ٤٢

**(24) KISHA AKASEMA: MIMI NDIYE MUNGU WENU MKUBWA ZAIDI** Alichokusudia hapa mlaaniwa huyu ni kwamba hakuna mungu zaidi yake1.

**(25) BASI MWENYEZI MUNGU AKAMWADHIBU ADHABU YA LA MWISHO NA LA MWANZO** Yaani: Allah akamwadhibu Firauni adhabu ya tamko la mwisho nayo ni adhabu ya moto, na tamko la mwanzo, nayo ni ile adhabu ya duniani kwa kuzama baharini[1]. Mwenyezi Mungu amefanya hivyo ili iwe onyo kwa yule atakayesikia habari za fir'auni.

**(26) HAKIKA, KATIKA HAYO KUNA MAZINGATIO KWA MWENYE KUOGOPA** Yaani: Katika kisa cha firauni na yaliyoelezwa katika kisa hicho, kuna mazingatio makubwa kwa mwenye utashi wa kumuogopa Allah.

**(27) HIVI NYINYI NDIO MLIO NA UMBILE ZITO ZAIDI AU MBINGU ALIZOJENGA?** Yaani: Je, kuumbwa na kufufuliwa kwenu baada ya kufa ndiko kugumu zaidi kwenu na katika makadirio yenu au kuumbwa kwa mbingu ndiko kugumu zaidi? Kwa sababu aliyeweza kuumba mbingu zilizo na umbile hili kubwa na ndani yake mna viumbe na uwezo wa ajabu ulio wazi kwa wenye kuangalia, vipi atashindwa kuirejesha miili aliyoiua baada ya kuwa yeye ndiye aliyeiumba kwa mara ya kwanza?

**(28) AMENYANYUA KIMO CHAKE AKAZIWEKA SAWA** Yaani: Amezifanya mbingu kama jengo lililo nyanyuka juu ya ardhi Ameliweka sawa umbile lake; hazikutofautiana, hazikupinda pinda, hazina dosari wala nyufa.

**(29) NA AKAUTIA GIZA USIKU WAKE NA AKAUFANYA KUWA NA MWANGA MCHANA WAKE** Akaufanya usiku kuwa na giza, na akaufanya mchana wake kuwa unatoa mwanga kwa mwangaza wa jua.

**(30) NA ARDHI BAADA YA HAPO AKAITANDIKA** Yaani : Baada ya kuumba mbingu, akaikunjua ardhi.

**(31) AKATOA HUMO MAJI YAKE NA MALISHO YAKE** Yaani: Akapasua ardhini mito, bahari na chemchem na akaotesha kutokana nayo nyasi zinazolishiwa wanyama.

**(32) NA MILIMA AKAISIMIKA** Na akaifanya milima kama vigingi kwa ardhi ili isiwayumbishe walio juu ya ardhi hiyo.

**(33) KWA AJILI YA RAHA YENU NA WANYAMA WENU**

**(34) BASI LITAKAPOFIKA BALAA KUBWA** Yaani: Litakapokuja Balaa kubwa linaloyazidi mabalaa yote. Balaa hilo ni mpulizo wa pili ambao utawafikisha watu wa peponi peponi na wa motoni motoni.

**(35) SIKU ATAKAPOKUMUBUKA MWANADAMU ALIYOYAFANYA** Mwanadamu atakumbuka aliyoyafanya; yawe ni ya kheri au ya shari, kwa sababu yote aliyoyatenda atayaona yameandikwa kwenye nyaraka za matendo yake.

**(36) NA IKADHIHIRISHWA JAHANAMU KWA MWENYE KUONA** Yaani: Jahanamu itadhihirishwa bayana, haitajificha kwa yeyote. Amesema Muqaatil:"Litaondolewa pazia lake na viumbe wote wataiona". Muumin, kwa kuiona Jahanamu, ataelewa thamani ya neema ya Allah juu yake kwa kumsalimisha na janga hilo. Ama kafiri, ataongezeka huzuni juu ya huzuni aliyonayo, na majuto juu ya majuto aliyonayo.

**(37) BASI AMA YULE ALIYEKIUKA MIPAKA** Yaani: Aliyekiuka mipaka katika ukafiri na maasi.

**(38) NA AKAYATHAMINI MAISHA YA DUNIA**

---

[1] Tamko la kwanza la Firauni aliloadhibiwa kwalo ni pale aliposema kuwa hajui kama kuna Mungu mwengine badala yake (Sura Al-qasas 28, aya 37. Na tamko lake la pili aliloadhibiwa kwalo ni pale aliposema kuwa yeye ndiye Mungu mkubwa zaidi (Sura An-naaziaat 79, aya 24) – Mrejeaji.

Yaani: Akayaweka mbele maisha ya dunia kuliko ya Akhera, hakujiaandaa kwa ajili ya Akhera na hakufanya lolote katika matendo ya Akhera.

39 **BASI HAKIKA, JAHANAMU NDIO MAKAZI** Jahanamu ndio mahali ambapo ataishi na sio pengine.

40 **NA AMA ALIYEOGOPA KUSIMAMA MBELE YA MOLA WAKE NA AKAIKATAZA NAFSI INAVYOTAKA** Yaani: Yule aliyeogopa kusimama kwake mbele ya Mola wake siku ya Qiyama na akaikemea nafsi yake isiende kwenye maasi na haramu ambayo inataka kuyafanya

41 **BASI HAKIKA, PEPO NDIO MAKAZI** Pepo ndio makazi ambayo atakuwa akiishi humo na hatakuwa na makazi mengine yasiokuwa hayo.

42 **WANAKUULIZA KUHUSU QIYAMA: NI LINI KUSOZA KWAKE?** Yaani: Ni lini Qiyama kitafika na kutokea kama inavyosoza mashua?

43 **UKO WAPI WEWE NA KUWATAJIA KWAKE?** Yaani: Huna,ewe Muhammad, lolote la kukieleza Qiyama na kukiulizia kwa maana huna lolote la kukijua na kukielezea. Hakuna vingine isipokuwa kwamba anayekijua Qiyama ni Allah Mtukufu tu.

44 **NI KWA MOLA WAKO TU NDIO UKOMO WAKE** Yaani: Upeo wa kukijua Qiyama upo kwa Allah tu. Ujuzi wake haupatikani kwa mwenginewe. Iwapo ni hivyo, vipi basi wanakuuliza na kukutaka ufafanuzi wa wakati wa kutokea kwake?

45 **HAKUNA VINGINE ISIPOKUWA KWAMBA WEWE NI MHADHARISHAJI TU WA ANEYEKIOGOPA** Yaani: Wewe ni muonyaji wa anayeogopa kuja kwa Qiyama.

46 **SIKU WATAKAPOKIONA, WATAJIONA KAMA VILE HAWAKUISHI ISIPOKUWA JIONI MOJA AU ASUBUHI YAKE** Yaani: Watajiona kuwa hawakuishi duniani isipokuwa kiasi cha mwisho wa mchana au mwanzo wake au kiasi cha asubuhi ambayo ilifuatia jioni hiyo. Madhumuni ni kuonesha kuwa watakapoiona misukosuko ya Qiyama wataona katika nafsi zao kuwa muda walioishi duniani ni mchache.

# SURAT ABASA (80)

*Ni ya Makka Ina aya arobaini na mbili*

1 **AMEKUNJA USO NA AMEPUUZA** Yaani: Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikunja uso wake na kupuuza.

2 **KWA KUWA ALIMJIA KIPOFU** Yaani: Mtume alikunja uso kwa kujiwa na kipofu. Sababu ya kuteremka sura hii ni kwamba watu fulani miongoni mwa waheshimiwa wa Kiquraishi walikuwa kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, naye alikuwa na tamaa ya wao kusilimu. Hivyo, akamjia mtu kipofu naye ni Abdallah Ibn Ummi-Maktuum. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, hakufurahi Ibni Ummi-maktuum kumkatiza katika mazungumzo yake,
kwa hiyo akampuuza, ndipo ikateremka sura hii.

3 **NA NINI KITAKUJULISHA HUENDA AKAJITAKASA** Yaani: Huenda huyu kipofu akajitakasa na madhambi kwa matendo mema atayojifunza kwako.

4 **AU AKAKUMBUKA NA MAWAIDHA HAYO HIVYO YAKAMNUFAISHA** Yaani: Huenda akakumbuka na hivyo, akaonyeka kwa mawaidha utayomfundisha.

5 **AMA ALIYETOSHEKA** Yaani: Ama mtu mwenye mali na utajiri au mtu aliyepuuza imani na elimu uliyonayo.

6 **BASI WEWE UNAMUELEKEA** Yaani: Unamuelekea kwa uso wako na mazungumzo yako ilhali yeye anaonesha kutokukuhitaji wewe na kupuuza uliyokuja nayo.

7 **NA SI JUU YAKO ASIPOTAKASIKA** Yaani: Ni kitu gani kitakulazimu asiposilimu na kuongoka? Hakuna linalokulazimu isipokuwa kufikisha ujumbe tu. Kwa hiyo, usishughulike na mambo ya makafiri ambao mambo yao yako hivi.

8 **NA AMA YULE ALIYEKUJIA HARAKA** Yaani : Amekujia haraka akikutaka umuelekeze kwenye kheri na umuonye kwa mawaidha ya Allah.

9 **NA HUKU YEYE AKIOGOPA** Yaani: Akimuogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

10 **BASI WEWE UNAMPUUZA** Yaani: Unaacha kumshughulikia, unampuuza na kutomjali.

11 **USIFANYE HIVYO. HAKIKA YA HAYO NI MAWAIDHA** Baada ya tukio hili, usifanye tena mfano wa tendo hili la kumpuuza fukara, na kumpatiliza tajiri, pamoja na kuwa tajiri huyo si moingoni mwa wanaotaka kujitakasa. Usiache kumuongoza aliyekujia akiwa ni miongoni mwa watu wanaotaka kujitakasa na kupokea mawaidha. Aya hizi au sura hii ni mawaidha. Stahiki yake ni uonyeke nayo, uyakubali, uyafanyie kazi wewe na umma wako wote.

12 **BASI ANAYETAKA, ATAONYEKA NAYO** Yaani : Atakayeyapenda atajionya kwayo, atayachunga na kufanya mambo kwa mujibu wake.

13 **YAMO NDANI YA NYARAKA TAKATIFU** Yaani: Maonyo hayo yamo katika nyaraka takatifu mbele ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya elimu na hekima zilizomo ndani yake, au ni takatifu kwa sababu zimeteremka kutoka *Allauhilmahfuudh*.

14 **YALIYO WEKWA JUU, YALIYO TWAHARISHWA** Maonyo hayo yana daraja ya

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

عَبَسَ وَتَوَلَّىٰٓ (١) أَن جَآءَهُ ٱلْأَعْمَىٰ (٢) وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّهُۥ يَزَّكَّىٰٓ (٣) أَوْ
يَذَّكَّرُ فَتَنفَعَهُ ٱلذِّكْرَىٰٓ (٤) أَمَّا مَنِ ٱسْتَغْنَىٰ (٥) فَأَنتَ لَهُۥ تَصَدَّىٰ (٦)
وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزَّكَّىٰ (٧) وَأَمَّا مَن جَآءَكَ يَسْعَىٰ (٨) وَهُوَ يَخْشَىٰ (٩) فَأَنتَ
عَنْهُ تَلَهَّىٰ (١٠) كَلَّآ إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ (١١) فَمَن شَآءَ ذَكَرَهُۥ (١٢) فِى صُحُفٍ مُّكَرَّمَةٍ
(١٣) مَّرْفُوعَةٍ مُّطَهَّرَةٍۭ (١٤) بِأَيْدِى سَفَرَةٍ (١٥) كِرَامٍۭ بَرَرَةٍ (١٦) قُتِلَ ٱلْإِنسَٰنُ
مَآ أَكْفَرَهُۥ (١٧) مِنْ أَىِّ شَىْءٍ خَلَقَهُۥ (١٨) مِن نُّطْفَةٍ خَلَقَهُۥ فَقَدَّرَهُۥ (١٩) ثُمَّ
ٱلسَّبِيلَ يَسَّرَهُۥ (٢٠) ثُمَّ أَمَاتَهُۥ فَأَقْبَرَهُۥ (٢١) ثُمَّ إِذَا شَآءَ أَنشَرَهُۥ (٢٢) كَلَّا لَمَّا
يَقْضِ مَآ أَمَرَهُۥ (٢٣) فَلْيَنظُرِ ٱلْإِنسَٰنُ إِلَىٰ طَعَامِهِۦٓ (٢٤) أَنَّا صَبَبْنَا ٱلْمَآءَ صَبًّا
(٢٥) ثُمَّ شَقَقْنَا ٱلْأَرْضَ شَقًّا (٢٦) فَأَنۢبَتْنَا فِيهَا حَبًّا (٢٧) وَعِنَبًا وَقَضْبًا (٢٨)
وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا (٢٩) وَحَدَآئِقَ غُلْبًا (٣٠) وَفَٰكِهَةً وَأَبًّا (٣١) مَّتَٰعًا لَّكُمْ
وَلِأَنْعَٰمِكُمْ (٣٢) فَإِذَا جَآءَتِ ٱلصَّآخَّةُ (٣٣) يَوْمَ يَفِرُّ ٱلْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ (٣٤)
وَأُمِّهِۦ وَأَبِيهِ (٣٥) وَصَٰحِبَتِهِۦ وَبَنِيهِ (٣٦) لِكُلِّ ٱمْرِئٍ مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ
يُغْنِيهِ (٣٧) وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ (٣٨) ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ (٣٩) وَوُجُوهٌ
يَوْمَئِذٍ عَلَيْهَا غَبَرَةٌ (٤٠) تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ (٤١) أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْكَفَرَةُ ٱلْفَجَرَةُ (٤٢)

juu mbele ya Allah, yametakaswa, hawayashiki ila tu wale waliotwaharishwa. Yamehifadhiwa; mashetani na makafiri hawayafikii.

(15) **YALIYO KATIKA MIKONO YA WAJUMBE** Wajumbe hapa ni Malaika wanaowakilisha wahyi (ufunuo) kati ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Neno Wajumbe latokana na neno Ujumbe ambao ni hali ya kwenda kati ya watu.

(16) **WATUKUFU, WEMA** Yaani: Wenye heshima mbele ya mola wao, waliojitenga na maasi, wacha Mungu, watiifu kwa Mola wao, wakweli katika imani yao.

(17) **AMELAANIWA MWANADAMU! UKAFIRI WAKE ULIOJE!** Yaani: Amelaaniwa mwandamu kafiri. Lo, ukafiri wake ni mkubwa!

(18) **AMEMUUMBA KUTOKANA NA NINI?** Yaani: Kwani Mwenyezi Mungu amemuumba huyu kafiri kutokana na nini?

(19) **KUTOKANA NA TONE AMEMUUMBA KISHA AKAMTENGENEZA SAWASAWA** Yaani: Mwenyezi Mungu amemuumba kutokana na maji duni. Ni vipi anakuwa na kiburi kiumbe aliyetoka katika njia ya mkojo mara mbili? Amemuumba sawa na akamuandaa kwa maslahi ya nafsi yake na akamuumbia mikono miwili, miguu miwili, macho mawili, nyenzo na njia nyingine za fahamu.

(20) **KISHA AKAMRAHISISHIA NJIA** Yaani: Amemrahisishia njia ya kupata kheri au shari.

(21) **KISHA AKAMFISHA NA KUMUWEKA KABURINI** Yaani: Amemuwekea kaburi ambalo anahifadhiwa humo kwa heshima yake. Hakumfanya katika jumla ya viumbe vinavyotupwa tu kwenye uso wa ardhi vikaliwa na wanyama wakali na ndege.

(22) **KISHA AKITAKA, ATAMFUFUA** Yaani: Mwenyezi Mungu Mtukufu akitaka kumfufua, atampa uhai baada ya kufa kwake, katika wakati autakao.

(23) **NI KWELI. BADO HAJATEKELEZA AMBAYO AMEMUAMURU** Baadhi hawakuyatekeleza waliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu kwa ukafiri, na wengine kwa uasi. Hakuna waliotekeleza waliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu ila wachache tu.

(24) **HEBU MWANADAMU AANGALIE CHAKULA CHAKE** Yaani: Aangalie namna gani Allah alivyomuumbia chakula chake ambacho amekifanya kuwa ndio sababu ya uhai wake.

(25) **KWAMBA SISI TUMEMIMINA MAJI MMIMINO**

(26) **KISHA TUKAIPASUA ARDHI MPASUO** Yaani: Tukaipasua ardhi kwa mmea unaotoka ardhini humo kwa sababu ya kuteremka mvua, mpasuko mzuri unaolingana na mmea unaotoka hapo kwa udogo, ukubwa, umbile na aina.

(27) **KISHA TUKAOTESHA HUMO NAFAKA** Yaani: Tukaotesha nafaka za chakula. Maana ni kwamba tumeotesha mmea unaoendelea kukua na kuongezeka mpaka unakuwa nafaka.

(28) **NA ZABIBU NA MALISHO** Malisho ni majani mabichi wanayolishwa wanyama.

(29) **NA MIZAITUNI NA MITENDE**

(30) **NA BUSTANI ZILIZOSTAWI** Bustani zilizostawi ni mitende bora iliyo na mashina manene.

(31) **NA MATUNDA NA NYASI** Nyasi ni kila mmea unaooteshwa na ardhi, usioliwa na wanadamu na usiolimwa, ikiwa ni pamoja na majani na aina nyengine za malisho.

(32) **IKIWA NI STAREHE KWENU NA WANYAMA WENU**

(33) **BASI WAKATI LITAKAPOKUJA LA KUZIBA MASIKIO** Yaani: Utakapokuja ukelele wa siku ya Qiyama ambao utaziba masikio na hivyo utayatia uziwi na hayatosikia.

(34)-(36) **SIKU MTU ATAKAPOMKIMBIA NDUGU YAKE NA MAMA YAKE NA BABA YAKE NA MKE WAKE NA WATOTO WAKE** Hawa ni ndugu wa karibu sana na wenye haki zaidi ya kupata mapenzi na huruma. Kwa

hiyo, kuwakimbia hawa hakutokei isipokuwa tu kwa sababu ya msukosuko mkubwa na janga lenye kutisha.

(37) **KILA MTU MIONGONI MWAO SIKU HIYO ATAKUWA NA JAMBO LINALOMTOSHA** Kila mtu atakuwa na jambo litakalomshughulisha ashindwe kuwashughulikia ndugu na kumuweka mbali nao. Atawakimbia ndugu kwa kuhadhari wasimuombe msaada kwa sababu uhusiano uliopo kati yao, na pia wasipate kuziona tabu alizo nazo yeye.

(38) **NYUSO SIKU HIYO NI ZENYE KUN'GARA** Hizo ni nyuso za waumini. Zitatoa nuru na mwanga kwa sababu wao wakati huo watakuwa wameshajua neema na takrima watakazopata.

(39) **NI ZENYE KUCHEKA, ZENYE FURAHA**

(40) **NA NYUSO NYINGINE SIKU HIYO ZITAKUWA NA VUMBI** Yaani: Zitakuwa na vumbi na takataka kwa sababu ya adhabu watakayoiona na ambayo Mwenyezi Mungu amewaandalia.

(41) **ZITAFINIKWA NA WEUSI** Yaani: Zitafunikwa na weusi, kuchujuka, udhalili na matatizo.

(42) **HAO NI MAKAFIRI TU, WAOVU** Yaani: Hao wenye nyuso zenye vumbi ni makafiri na waovu. Waovu ni watenda mambo maovu, waongo.

## SURATUT-TAKWIIR (81)

*Ni ya Makka Ina aya ishirini na tisa*

Amepokea Imam Ahmad na Ttirmidhiy wakimnukuu Swahaba Ibni-omar akisema kuwa: "Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: Mtu ambaye kunamfurahisha kuiangalia Siku ya Qiyama kama anaiona kwa macho, basi asome (sura hizi): Idhash-shamsu kuwwirat (81), na Idhas-samaa unfatwarat (82), na Idhas-samaa unshaq-qat (84)".

(1) **WAKATI JUA LITAKAPOVIRINGWA** Jua litaviringwa kama mpira, lita kunjwakunjwa na kisha kurushwa.

(2) **NA WAKATI NYOTA ZITAKAPO PUKUTIKA** Yaani: Nyota zitakapoanguka, kupukutika na kutawanyika. Yasemekana pia kuwa kupukutika kwa nyota ni kufutwa mwanga wake.

(3) **NA WAKATI MILIMA ITAKAPOENDESHWA** Yaani: Milima itakapong'olewa ardhini na kupeperushwa angani.

(4) **NA WAKATI NGAMIA WENYE MIMBA WATAKAPOACHWA** Ngamia wenye mimba ni wale ambao matumboni mwao kuna watoto. Wamehusishwa ngamia hawa tu kutajwa kwa vile (walikuwa) ni mali ya thamani sana kwa Waarabu. Maana ya kuachwa kwao ni kule

ترتيبها ٨١ — سُورَةُ التَّكۡوِيرِ — آياتها ٢٩

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا ٱلشَّمۡسُ كُوِّرَتۡ ١ وَإِذَا ٱلنُّجُومُ ٱنكَدَرَتۡ ٢ وَإِذَا ٱلۡجِبَالُ
سُيِّرَتۡ ٣ وَإِذَا ٱلۡعِشَارُ عُطِّلَتۡ ٤ وَإِذَا ٱلۡوُحُوشُ حُشِرَتۡ
٥ وَإِذَا ٱلۡبِحَارُ سُجِّرَتۡ ٦ وَإِذَا ٱلنُّفُوسُ زُوِّجَتۡ ٧ وَإِذَا
ٱلۡمَوۡءُۥدَةُ سُئِلَتۡ ٨ بِأَيِّ ذَنۢبٖ قُتِلَتۡ ٩ وَإِذَا ٱلصُّحُفُ نُشِرَتۡ
١٠ وَإِذَا ٱلسَّمَآءُ كُشِطَتۡ ١١ وَإِذَا ٱلۡجَحِيمُ سُعِّرَتۡ ١٢ وَإِذَا ٱلۡجَنَّةُ
أُزۡلِفَتۡ ١٣ عَلِمَتۡ نَفۡسٞ مَّآ أَحۡضَرَتۡ ١٤ فَلَآ أُقۡسِمُ بِٱلۡخُنَّسِ ١٥
ٱلۡجَوَارِ ٱلۡكُنَّسِ ١٦ وَٱلَّيۡلِ إِذَا عَسۡعَسَ ١٧ وَٱلصُّبۡحِ إِذَا تَنَفَّسَ ١٨
إِنَّهُۥ لَقَوۡلُ رَسُولٖ كَرِيمٖ ١٩ ذِي قُوَّةٍ عِندَ ذِي ٱلۡعَرۡشِ مَكِينٖ ٢٠ مُّطَاعٖ
ثَمَّ أَمِينٖ ٢١ وَمَا صَاحِبُكُم بِمَجۡنُونٖ ٢٢ وَلَقَدۡ رَءَاهُ بِٱلۡأُفُقِ ٱلۡمُبِينِ
٢٣ وَمَا هُوَ عَلَى ٱلۡغَيۡبِ بِضَنِينٖ ٢٤ وَمَا هُوَ بِقَوۡلِ شَيۡطَٰنٖ رَّجِيمٖ ٢٥
فَأَيۡنَ تَذۡهَبُونَ ٢٦ إِنۡ هُوَ إِلَّا ذِكۡرٞ لِّلۡعَٰلَمِينَ ٢٧ لِمَن شَآءَ مِنكُمۡ أَن
يَسۡتَقِيمَ ٢٨ وَمَا تَشَآءُونَ إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢٩

ترتيبها ٨٢ — سُورَةُ الانفِطَارِ — آياتها ١٩

kuachwa hivi hivi bila ya mchungaji, kutokana na misukosuko mikubwa ambayo watu wataiona.

(5) **NA WAKATI WANYAMAPORI WATAKAPOKUSANYWA** Wanyamapori ni wale wanyama wa bara wasiofugwa. Maana ya kukusanywa kwao ni kufufuliwa kwao ili walipizane visasi wao kwa wao (kutokana na kudhulumiana kwao duniani). Yasemekana pia kuwa maana ya kukusanywa kwao ni kufa kwao.

(6) **NA WAKATI BAHARI ZITAKAPOWASHWA MOTO** Yaani: Bahari zitawashwa na kuwa moto unaobimbirika.

(7) **NA WAKATI NAFSI ZITAKAPOOZESHWA** Yaani: Nafsi za waumini zitafungishwa ndoa na Mahuril-aini, na nafsi za makafiri zitakutanishwa na mashetani. Amesema Imam Alhasan kuwa: "Kila mtu atakutanishwa na kundi lake: Wayahudi kwa Wayahudi, Wakristo kwa Wakristo, Majusi (Waabudu jua) kwa Majusi, aliyekuwa anaabudu kisichokuwa Allah atakutanishwa nacho, na wanafiki kwa wanafiki na waumini wataunganishwa na waumini wenzao".

(8) (9) **NA WAKATI MSICHANA ALIYEZIKWA AKIWA HAI ATAKAPOULIZWA: NI KWA KOSA**

**GANI ALIULIWA?** Ilikuwa mila ya Waarabu (wa zamani) akizaliwa mtoto wa kike, basi anamzika akiwa hai, kwa kuogopa aibu au umasikini. Atatahayarizwa mtu aliyemuua mtoto wa kike kwa vile binti huyo ameuliwa bila ya kosa lolote alilotenda.

(10) **NA WAKATI NYARAKA ZITAPOKUNJULIWA** Yaani: Nyaraka zilizoandikwa matendo (ya waja) zitafunuliwa kwa ajili ya hisabu.

(11) **NA WAKATI MBINGU ZITAKAPO ONDOLEWA** Yaani: Mbingu zitapasukapasuka na kuondolewa.

(12) **NA WAKATI JAHANAMU ITAKAPOWASHWA MOTO** Jahanamu itawashwa moto mkali sana kwa ajili ya maadui wa Mwenyezi Mungu. Amesema Qatada: "Makosa ya wanadamu na hasira za Allah zitaufanya moto wa Jahanamu uwake vikali sana".

(13) **NA WAKATI PEPO ITAKAPOSOGEZWA KARIBU** Pepo itasogezwa na kuwa karibu na Wachamungu. Yasemekana kuwa mambo haya kumi na mbili, sita kati ya hayo yatatokea hapa duniani, nayo ni kuanzia mwanzo wa sura hii mpaka aya ya (6) Na mambo sita mengine yatatokea Akhera, nayo ni yaliyotajwa kuanzia aya ya (7) hadi ya (13)

(14) **ITAJUA NAFSI ILICHOKILETA** Madhumuni ni kwamba kila nafsi itajua nini imekifanya na kukileta wakati wa kukunjuliwa nyaraka za matendo. Yaani: Kila nafsi itajua ilichofanya, iwe ni kheri au shari.

(15) **NINAZIAPIA NYOTA ZINAZOREJEA** Hizo ni nyota zinazojificha mchana chini ya mwanga wa jua, hazionekani. Nyota hizo ni: *Zohal, Almushtari, Almirrikh, Azzuhra* na *Atwaarid* kama zilivyotajwa na wanazuoni wa tafsiri. Na amesema katika As-swihaah kuwa: NYOTA ZINAZOREJEA ni nyota zote, kwa sababu mchana zinajificha.

(16) **ZINAZOTEMBEA, ZINAZOJIFICHA** Zinatembea katika mihimili yake. Zinajificha nyuma ya upeo wa anga wakati wa kuzama kwake. Neno *Alkunnas* limechukuliwa kutoka kwenye neno *Alkinaas,* yaani: kichaka wanachojificha humo wanyama wakali.

(17) **NA USIKU UNAPOINGIA NA KUTOKA** Waarabu wanasema: *"As-asallailu"* unapoingia usiku. Na *"As-asa llailu"* unapoondoka.

(18) **NA ASUBUHI INAPOPUMUA** Kupumua kwa asubuhi ni kuingia kwake, kwa vile asubuhi inaingia ikiwa na hewa nyororo.

(19) **KWA YAKINI, HILO NI NENO LA MJUMBE MTUKUFU** Mjumbe ni Jibril, kwa sababu yeye ndiye aliyeteremka na Qur'ani kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuileta kwa Mtume wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.

(20) **MWENYE NGUVU, MBELE YA MWENYE ARSHI TUKUFU NI MWENYE HADHI** Yaani: Yeye Jibril ni mwenye cheo cha juu na nafasi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

(21) **MWENYE KUTIIWA HUKO, MWAMINIFU** Mwenye kutiiwa kati ya Malaika, wanawajibika kwake na wanamtii. Ameaminiwa kwa wahyi (ufunuo) na mengineyo.

(22) **NA MWENZENU SI MWENDAWAZIMU** Na Muhammad, enyi watu wa Makkah, hana kichaa. Mwenyezi Mungu amemtaja Mtume Muhammad kwa sifa ya mwenzenu ili kuonesha kuwa wanalijua vilivyo suala lake na kwamba yeye ni mwenye akili timamu zaidi kuliko watu wengine na ni mkamilifu wao zaidi.

(23) **NA KWA YAKINI AMEMUONA KATIKA ANGA LILILO SAFI** Yaani: Muhammad amemuona Jibril upande wa mashariki mwa mawio ya jua akiwa katika sura yake (ya Kimalaika), akiwa na mbawa mia sita. Mujahid amesema: Mtume amemuona Jibrili upande wa Ajyaad, eneo ambalo ni mashariki mwa mji wa Makkah.

(24) **NA YEYE SI BAKHILI WA GHAIBU** Na Muhammad sio bahili wa habari za mbinguni. Hafanyi ubahili wa kufikisha Wahyi, na wala hafanyi uzembe katika kuufikisha. Bali anawafundisha viumbe maneno ya Mwenyezi Mungu na sheria zake.

(25) **NA HIYO SIO KAULI YA SHETANI MRUJUMIWA** Yaani: Qur'ani sio neno la shetani miongoni mwa mashetani wanaosikiliza kwa kuibia mbinguni kisha wakarushiwa vimondo na kuchomwa kwavyo. Kwa hiyo, Qur'ani sio ushairi wala ukuhani (uchawi) kama walivyosema Maquraish.

(26) **BASI MNAKWENDA WAPI?** Ni njia ipi mtakayopita iliyo wazi zaidi kuliko njia hii iliyowekwa wazi kwenu?

(27) **HAYAKUWA HAYO ISIPOKUWA TU NI MAWAIDHA KWA WALIMWENGU** Yaani: Qur'ani si chochote isipokuwa tu ni mawaidha kwa viumbe wote na ni ukumbusho kwao.

(28) **KWA ANAYETAKA, MIONGONI MWENU, KUFUATA NJIA ILIYONYOOKA** Qur'ani ni mawaidha kwa anayetaka kufuata njia iliyo juu ya haki, imani na utiifu.

(29) **NA HAMTATAKA ISIPOKUWA TU AKITAKA MWENYEZI MUNGU MOLA WA VIUMBE WOTE** Yaani: Hamtataka kuwa katika njia iliyonyooka na wala hamtaweza hivyo isipokuwa tu kwa kutaka Mwenyezi Mungu na kwa msaada wake.

# SURATUL – INFITWAAR (82)

*Ni ya Makka Aya zake ni kumi na tisa*

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنفَطَرَتْ ﴿١﴾ وَإِذَا ٱلْكَوَاكِبُ ٱنتَثَرَتْ ﴿٢﴾ وَإِذَا ٱلْبِحَارُ
فُجِّرَتْ ﴿٣﴾ وَإِذَا ٱلْقُبُورُ بُعْثِرَتْ ﴿٤﴾ عَلِمَتْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ
وَأَخَّرَتْ ﴿٥﴾ يَٰٓأَيُّهَا ٱلْإِنسَٰنُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ ٱلْكَرِيمِ ﴿٦﴾ ٱلَّذِى
خَلَقَكَ فَسَوَّىٰكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾ فِىٓ أَىِّ صُورَةٍ مَّا شَآءَ رَكَّبَكَ ﴿٨﴾
كَلَّا بَلْ تُكَذِّبُونَ بِٱلدِّينِ ﴿٩﴾ وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَٰفِظِينَ ﴿١٠﴾ كِرَامًا
كَٰتِبِينَ ﴿١١﴾ يَعْلَمُونَ مَا تَفْعَلُونَ ﴿١٢﴾ إِنَّ ٱلْأَبْرَارَ لَفِى نَعِيمٍ ﴿١٣﴾ وَإِنَّ
ٱلْفُجَّارَ لَفِى جَحِيمٍ ﴿١٤﴾ يَصْلَوْنَهَا يَوْمَ ٱلدِّينِ ﴿١٥﴾ وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَآئِبِينَ
﴿١٦﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا يَوْمُ ٱلدِّينِ ﴿١٧﴾ ثُمَّ مَآ أَدْرَىٰكَ مَا يَوْمُ ٱلدِّينِ
﴿١٨﴾ يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِّنَفْسٍ شَيْـًٔا ۖ وَٱلْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِّلَّهِ ﴿١٩﴾

آياتها ٣٦ — سُورَةُ ٱلْمُطَفِّفِينَ — ترتيبها ٨٣

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ إِذَا ٱكْتَالُوا۟ عَلَى ٱلنَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾
وَإِذَا كَالُوهُمْ أَو وَّزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾ أَلَا يَظُنُّ أُو۟لَٰٓئِكَ أَنَّهُم
مَّبْعُوثُونَ ﴿٤﴾ لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥﴾ يَوْمَ يَقُومُ ٱلنَّاسُ لِرَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٦﴾

(1) **WAKATI MBINGU ZITAKAPOPASUKA** Kupasuka kwa mbingu ni kuchanika kwake ili Malaika wapate kuteremka kutoka huko.

(2) **NA WAKATI NYOTA ZITAKAPOPUKUTIKA** Yaani: Nyota zitaanguka zikiwa zimetawanyika.

(3) **NA WAKATI BAHARI ZITAKAPOTIRIRISHWA** Yaani: Baadhi ya bahari zitachanganywa na baadhi nyingine na kuwa bahari moja. Bahari ya maji baridi itachanganyika na bahari ya maji chumvi. Mambo haya yatatokea muda mchache kabla ya Qiyama kama yalivyotangulia maelezo haya katika sura iliyo kabla ya hii.

(4) **NA WAKATI MAKABURI YATAKAPOTIFULIWA** Yaani: Mchanga wa makaburi utaondolewa na maiti waliomo humo watatolewa.

(5) **NAFSI ITAJUA ILICHOTANGULIZA NA ILICHOCHELEWESHA** Wakati wa kufunuliwa nyaraka za matendo, nafsi itaelewa ilichokitanguliza, iwe ni matendo ya kheri au ya shari. Pia itaelewa ilichokiacha, iwe ni mwenendo mzuri au mbaya.

(6) **EWE MWANADAMU, NI NINI KILICHOKUHADAA KWA MOLA WAKO MKARIMU?** Yaani: Ni kitu gani kilicho kulaghai na kukuhadaa hata ukamkufuru Mola wako ambaye: **a)** Amekufadhili hapa duniani kwa kulifanya zuri (kamilifu) umbile lako na njia zako za fahamu, na. **b)** Akakufanya mwenye akili timamu na mwenye kuelewa, na. **c)**Akakupa riziki, na. **d)** Akakuneemesha kwa neema ambazo huwezi kukanusha hata moja katika neema hizo? Yasemekana kuwa kilicho mdanganya mwanadamu ni msamaha wa Mwenyezi Mungu pale anapoacha kufanya haraka ya kumuadhibu hapa duniani kwa makosa atendayo kwa mara ya kwanza.

(7) **AMBAYE AMEKUUMBA, KISHA AKAKUWEKA SAWA, KISHA AKAKUNYOOSHA** Amekuumba kutokana na tone la maji ya uzazi, na ilhali kabla ya hapo hukuwa kitu chochote. Akakuweka sawa ukawa ni mtu unayesikia, unayeona na unayefahamu. Akakufanya umenyooka, umesimama na mwenye sura nzuri. Pia amevifanya viungo vyako vimelinganishwa sawa sawa, havikutofautiana.

(8) **KATIKA SURA ALIYOITAKA, AMEKUUMBA** Yaani: Amekuumba katika sura ile aliyoitaka yeye miongoni mwa sura tofauti. Wewe hukujichagulia sura yako mwenyewe.

(9) **MKOME! BALI MNAPINGA DINI** Ni kemeo na karipio la kutodanganyika na ukarimu wa Mwenyezi Mungu, na kuufanya ukarimu huo kuwa ndio sababu ya kufikia hatua ya kumkufuru. Dini ni malipo (kwa maana kwamba mnapinga malipo yatakayofanyika Siku ya Qiyama), au (maana yake ni kwamba) mnapinga dini ya Kiislam.

(10) (11) **NA ILHALI JUU YENU KUNA WANAOHIFADHI. WATUKUFU, WAANDISHI** Hao ni Malaika wanaohifadhi (matendo ya waja).

(12) **WANAJUA MNAYOYAFANYA** Anasema Mwenyezi Mungu: Nyinyi mnaipinga Siku ya Malipo ilhali Malaika wa Mwenyezi Mungu wamewekwa kwa ajili yenu. Wanaandika matendo yenu ili mhesabiwe kwayo Siku ya Qiyama.

(13) (14) **HAKIKA, WEMA WAMO NDANI YA NEEMA. NA HAKIKA, WAOVU WAMO NDANI YA MOTO**

(15) **WATAUINGIA MOTO HUO SIKU YA MALIPO** Yaani: Hiyo ni siku ya malipo ambayo makafiri walikuwa wanaipinga. Makafiri, siku hiyo, watalazimika kuuingia moto huo wakipambana na muwako na joto lake.

(16) **NA HAWATATENGANA NAO** Yaani: Makafiri hawatatengana na moto huo asilani na hawatakuwa mbali nao. Bali wao watabaki humo

milele na milele.

17 **NA NI NINI KILICHOKUJULISHA WEWE, NI NINI SIKU YA MALIPO?**

18 **KISHA NI NINI KILICHOKUJULISHA WEWE, NI NINI SIKU YA MALIPO?** Yaani: Siku ya Malipo ni siku ya malipo na hisabu. Mwenyezi Mungu amerudiarudia kuitaja ili kuonesha utukufu wa daraja lake na kulitukuza suala lake, na pia kutahadharisha jambo lake.

19 **SIKU AMBAYO NAFSI HAITAMILIKI KWA NAFSI NYINGINE KITU CHOCHOTE, NA MAMBO SIKU HIYO NI YA MWENYEZI MUNGU** Hataweza yeyote, vyovyote awavyo, kumfanyia mwengine jambo lolote la manufaa. Huko hakuna yeyote atakayetekeleza au kufanya chochote isipokuwa Mwenyezi Mungu tu Mola wa viumbe. Mwenyezi Mungu katika siku hiyo, hampi yeyote mamlaka ya kitu chochote kama alivyowapa mamlaka duniani.

## SURATUL MUTWAFFIFIINA (83)

*Ni ya Makka Ina aya thalathini na sita*

Imepokewa kutoka kwa Ibni-abbas akisema kuwa: "Wakati Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipofika mji wa Madina aliwakuta watu wa Madina ni watu wabaya mno kwa vipimo. Mwenyezi Mungu akateremsha (sura hii): *Wailul-lil Mutwaf-fina*. Baada ya hapo, wakawa wanapima vizuri".[1]

1 **ADHABU KALI KWA WENYE KUPUNGUZA PUNGUZA VIPIMO** Kupunguza kipimo ni kupunguza kitu kidogo katika ujazo au uzito. Kwa hiyo, mpunguza kipimo ni yule anayepunguza haki ya mwengine kwa kupunguza katika ujazo au uzito. Mara nyingine, yawezekana mmoja wao akawa na pishi mbili. Pishi moja anawauzia watu kwa kutumia pishi hiyo, na anaponunua yeye kutoka kwa mwengine anajipimia kwa kutumia ile pishi nyingine.

2 **AMBAO WANAPOPIMA KUTOKA KWA WATU, WANAPIMA KAMILI** Yaani: Ambao wanaponunua wao, wanapima kamili katika ujazo au uzito.

3 **NA WANAPOWAPIMIA WAO KWA UJAZO AU UZITO, WANAPUNGUZA** Yaani: Wanapouza kwa kuwapimia watu wengine kwa ujazo au uzito, wanapunguza.

4 **HIVI HAWADHANI HAO KUWA WATAFUFUFULIWA?** Maana ni kuwa haiingii akilini mwao kuwa wao watafufuliwa na, kwa hiyo, wataulizwa wanayoyafanya. Hivi ni kwa nini wasilielewe hilo wakalitafakari, kulichunguza na kuuacha mwisho wake mbaya wanaouhofia?

5 **KWA AJILI YA SIKU ADHIMU?** Hiyo ni siku ya Qiyama. Ni siku adhimu kwa sababu ya yale mambo makubwa yaliyomo ndani ya siku hiyo, ikiwa ni pamoja na kufufuliwa, kuhisabiwa, adhabu, watu wa peponi kuingia peponi na watu wa motoni kuingia motoni.

6 **SIKU WATU WATAKAPOSIMAMA KWA AJILI YA MOLA WA VIUMBE** Watu watasimama wakisubiri ima: **a)** Amri ya Mola wa viumbe au **b)** Malipo yake au **c)** Hisabu ili kuonesha ukubwa wa kosa la kupunguza kipimo, madhambi yake ya ziada na ukubwa wa adhabu yake. Yote hiyo ni kwa sababu katika tendo hilo, kuna kukosa uaminifu na kula haki ya mtu mwengine kwa dhulma

7 **NI KWELI. HAKIKA YA KITABU CHA WAOVU KIMO NDANI YA SIJJIINI** Yaani: Hakika ya waovu, wakiwemo wapunguzavipimo, wameandikwa katika daftari la watu wa motoni, au wamo katika kifungo na dhiki kubwa.

8 **NA NI NINI KILICHOKUJULISHA WEWE, NI NINI SIJJIINI?**

9 **NI KITABU KILICHOANDIKWA** Yaani: Kitabu hicho ambacho ndani yake mna majina yao (hao watu waovu) ni kitabu kilichoandikwa. Na yasemekana kuwa *Sijjiini* ni kitabu kilichokusanya matendo maovu yaliofanywa na mashetani, makafiri na watu waovu. Yasemekana pia kuwa neno *Sijjiini* asili yake ni *Sijjiil,* litokanalo na neno Sijl, yaani: Kitabu.

10 **ADHABU KALI SIKU HIYO NI KWA WENYE KUPINGA** Yaani: Adhabu kali siku ya Qiyama ni kwa yule aliyepinga kufufuliwa na aliyepinga yale mambo waliyokuja nayo Mitume.

11 **AMBAO WANAIPINGA SIKU YA MALIPO**

12 **NA HAIPINGI SIKU HIYO ISIPOKUWA TU KILA YULE ANAYEKIUKA MIPAKA, MWINGI WA MADHAMBI** Yaani : (Mkiuka mipaka na mwingi wa dhambi ni yule) : Muovu, dhalimu, mwenye kuvuka mipaka katika madhambi na mwenye kuzama katika sababu za maovu.

13 **WAKATI ANAPOSOMEWA AYA ZETU ANASEMA: NI VIGANO VYA WATU WA KALE** (Wakati akisomewa aya) Zilizoteremshwa kwa (Mtume) Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, anasema kuwa hayo ni mazungumzo ya watu wa kale na batili zao walizozipamba.

14 **AKOME. BALI YAMEJENGA KUTU JUU YA NYOYO ZAO YALE MAMBO WALIYOKUWA WANAYAFANYA** Ni kemeo na karipio kwa yule mwenye kukiuka mipaka, mwingi wa madhambi kwamba aache maneno hayo batili, na kuyakanusha maneno hayo.

---

*Ameipokea Hadithi hii Ibn-Maajah,Hadithi Na. 2214.*

كَلَّآ إِنَّ كِتَٰبَ ٱلْفُجَّارِ لَفِى سِجِّينٍ ﴿٧﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا سِجِّينٌ ﴿٨﴾ كِتَٰبٌ
مَّرْقُومٌ ﴿٩﴾ وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ يُكَذِّبُونَ بِيَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿١١﴾
وَمَا يُكَذِّبُ بِهِۦٓ إِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ﴿١٢﴾ إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ءَايَٰتُنَا قَالَ أَسَٰطِيرُ
ٱلْأَوَّلِينَ ﴿١٣﴾ كَلَّا ۖ بَلْ ۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا۟ يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾ كَلَّآ إِنَّهُمْ
عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ ﴿١٥﴾ ثُمَّ إِنَّهُمْ لَصَالُوا۟ ٱلْجَحِيمِ ﴿١٦﴾ ثُمَّ يُقَالُ
هَٰذَا ٱلَّذِى كُنتُم بِهِۦ تُكَذِّبُونَ ﴿١٧﴾ كَلَّآ إِنَّ كِتَٰبَ ٱلْأَبْرَارِ لَفِى عِلِّيِّينَ
﴿١٨﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا عِلِّيُّونَ ﴿١٩﴾ كِتَٰبٌ مَّرْقُومٌ ﴿٢٠﴾ يَشْهَدُهُ ٱلْمُقَرَّبُونَ
﴿٢١﴾ إِنَّ ٱلْأَبْرَارَ لَفِى نَعِيمٍ ﴿٢٢﴾ عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ يَنظُرُونَ ﴿٢٣﴾ تَعْرِفُ فِى
وُجُوهِهِمْ نَضْرَةَ ٱلنَّعِيمِ ﴿٢٤﴾ يُسْقَوْنَ مِن رَّحِيقٍ مَّخْتُومٍ ﴿٢٥﴾
خِتَٰمُهُۥ مِسْكٌ ۚ وَفِى ذَٰلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ ٱلْمُتَنَٰفِسُونَ ﴿٢٦﴾ وَمِزَاجُهُۥ
مِن تَسْنِيمٍ ﴿٢٧﴾ عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا ٱلْمُقَرَّبُونَ ﴿٢٨﴾ إِنَّ ٱلَّذِينَ
أَجْرَمُوا۟ كَانُوا۟ مِنَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يَضْحَكُونَ ﴿٢٩﴾ وَإِذَا مَرُّوا۟ بِهِمْ
يَتَغَامَزُونَ ﴿٣٠﴾ وَإِذَا ٱنقَلَبُوٓا۟ إِلَىٰٓ أَهْلِهِمُ ٱنقَلَبُوا۟ فَكِهِينَ ﴿٣١﴾
وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوٓا۟ إِنَّ هَٰٓؤُلَآءِ لَضَآلُّونَ ﴿٣٢﴾ وَمَآ أُرْسِلُوا۟ عَلَيْهِمْ
حَٰفِظِينَ ﴿٣٣﴾ فَٱلْيَوْمَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنَ ٱلْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿٣٤﴾

Yamekuwa mengi kwao maasi na madhambi hivyo yakazizingira nyoyo zao. Hizo ndio kutu zilizopo juu ya nyoyo zao. Amesema Alhasan kuwa: "Hiyo (kutu) ni kosa juu ya kosa mpaka moyo unakuwa mweusi kutokana na madhambi. Na kupiga muhuri (chapa) ni kuufumba moyo. Na kupiga muhuri ni hali mbaya zaidi kuliko kutu".

Amepokea Imam Ahamad na Tirmidhiy, ambaye amesema kuwa Hadithi hii ni sahihi pia amepokea Imam An-nasaai (wote) wakinakili kutoka kwa Abuhuraira naye akinakili kutoka kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akisema kuwa: "Hakika, mja anapofanya dhambi hukaa kwenye moyo wake doa jeusi. Iwapo atatubu, akakoma na kuomba msamaha, husafishika moyo wake. Na akirejea (tena kufanya dhambi), doa jeusi linaongezeka mpaka linaufinika moyo wake. Hiyo ndio kutu aliyoitaja Mwenyenzi Mungu Mtukufu katika Qur'ani".[1]

(15) **WAKOME. HAKIKA YA WAO SIKU HIYO NA MOLA WAO NI WENYE KUWEKEWA KIZUIZI** Yaani: Makafiri ni wenye kuzuiwa kumuona Mola wao Siku ya Qiyama; hawatamuona kama waumini watakavyomuona. Kama Mwenyezi Mungu alivyowazuia kumpwekesha yeye hapa duniani, atawazuia huko Akhera wasimuone. Na Mujahid amesema kuwa: "Makafiri watazuiwa kupata takrima zake (Mwenyezi Mungu)".

(16) **KISHA, HAKIKA YA WAO WATAUINGIA MOTO** Yaani: Makafiri watauingia moto, watabaki humo, hawatatoka. Na kuingia motoni ni jambo baya zaidi kuliko kufedheheshwa na kunyimwa takrima.

(17) **KISHA PATASEMWA: HAYA NDIO YALE MLIYOKUWA MNAYAPINGA** Yaani: (Malaika) Wahudumu wa motoni watawaambia makafiri kwa kuwaliza na kuwatahayarisha kwamba: Haya ndio yale mliyokuwa mnayapinga duniani. Basi yaoneni na yaonjeni.

(18) **WAKOME. HAKIKA YA KITABU CHA WEMA KIMO NDANI YA ILLIYYIIN** Yaani: Hakika ya hao waja wema wameandikwa katika watu wa *illiyyiin.* Na *Ill-yyiin* ni pepo tu, au ni pepo ya daraja ya juu. Wema ni wale watiifu (kwa Mwenyezi Mungu).

(19) **NA NI NINI KILICHOKUJULISHA WEWE NI NINI ILLIYYIIN?** Yaani: Ni nini kilichokujulisha ewe Muhammad, ni kitu gani *Illiyyiin*? Swali hili lina maana ya kuonesha hadhi na utukufu wa *Illiyyiin.*

[1] *Sunan Tirmidhiy, Hadithi Na. 3257. Musnad Imam Ahmad, Hadithi Na. 7611.*
*Assunan Al-kubraa, An-nasaaii, Hadithi Na. 11658.*

(20) **NI KITABU KULICHOANDIKWA** Yaani: Kitabu ambacho ndani yake yamo majina yao.

(21) **WANAKISHUHUDIA WALIOKARIBU** Maana ni kwamba: Malaika wanafika kwenye kitabu hicho kilichoandikwa na wanakiona. Na yasemekana kuwa Malaika watatoa ushahidi wa yaliyomo ndani ya kitabu hicho Siku ya Qiyama.

(22) **HAKIKA YA WEMA WAMO NDANI YA NEEMA** Yaani: Wenye kumtii Mwenyezi Mungu wamo ndani ya neema kubwa isiyo kadirika.

(23) **JUU YA VITANDA VILIVYOREMBWA WANAANGALIA** *Araa-ik* (vitanda vivyorembwa) ni vitanda ambavyo vina urembo. Kitanda hakiitwi *Ariika* isipokuwa tu kikiwa kimetiwa urembo. (Watu wema watakuwa) Wanaangalia takrima alizowaandalia Mwenyezi Mungu. Na yasemekana kuwa maana ni kwamba watakuwa wanaangalia uso wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

(24) **UTATAMBUA NYUSONI MWAO USTAWI WA NEEMA** Ukiwaona utatambua kuwa wao ni watu wa neema kwa sababu ya nuru, uzuri, weupe, furaha na mn'garo utakaouona katika nyuso zao. Hiyo ni kwa sababu, Mwenyezi Mungu ataongeza katika uzuri wao na rangi zao vitu ambavyo hakuna

msifiaji anayeweza kuvisifia.

(25) **WATANYWESHWA MVINYO ULIO FUNGWA** *Rahiiq* (Mvinyo) katika pombe ni pombe isiyo na udanganyifu (isiyo ghushiwa) wala isiyokuwa na kitu kinachoweza kuiharibu. *Makhtuum* (Iliyofungwa): Ni ile iliyofungwa kwa lakiri (kizibo madhubuti) isiyoweza kufunguliwa na yeyote mpaka hapo inapofunguliwa kwa Waja Wema.

(26) **MWISHO WAKE NI MISKI. NA KATIKA HAYO, WASHINDANE WENYE KUSHINDANA** Mwisho wa ladha yake ni harufu ya miski. Mnywaji anapoinua kinywa chake mwisho wa kunywa kwake, atakuta harufu yake ni kama harufu ya miski. Na yasemekana kuwa vyombo vya mvinyo huo, ikiwa ni glasi na birika zake, vimefungwa kwa lakiri ya miski.

Basi katika hayo, watake (kushindana) wenye kutaka (kushindana). Kushindana ni kugombea kitu, ili kila mmoja akipate yeye na kumsimanga nacho mwenzie.

(27) **NA MCHANGANYIKO WAKE UNATOKANA NA TASNIIM** Yaani: Mchanganyiko wa mvinyo huo unatokana na *Tasniim*. *Tasniim* ni kinywaji kitakacho wamiminikia kutokea juu. Na hicho ndicho kinywaji bora zaidi peponi.

(28) **CHEMCHEM WATAKAYO KUNYWA HUKO WALIO KARIBU** Yaani: Kinywaji cha mvinyo au *Tasniim* watakachopewa kinatokana na chemchem watakayochanganyia kwayo glasi zao.

(29) **HAKIKA YA WALE AMBAO WAMEFANYA MAOVU WALIKUWA WAKIWACHEKA WALE WALIOAMINI** Hakika ya makafiri wa Kiquraish na wanaokubaliana nao katika ukafiri walikuwa wanawafanyia waumini istihzai na dharau.

(30) **NA WAKATI WAKIWAPITIA, WANAKONYEZANA** Kukonyeza ni kitendo cha kuashiria kwa kope na nyusi. Wanafanya hivyo wakilenga kuwafedhehesha na kuwa-aibisha Waislamu kwa sababu ya Uislam (wao).

(31) **NA WAKATI WANAPORUDI KWA WATU WAO, WANARUDI WAKIWA WAMEFURAHI** Yaani: Makafiri wanaporudi wakitokea kwenye vikao vyao, wanafurahia hali waliyo nayo na kujisikia raha kwayo.Wanafurahia kuwataja waumini, kuwakashifu na kuwafanyia kejeli.

(32) **NA WAKATI WANAPOWAONA WANASEMA: HAKIKA YA HAWA WAMEPOTEA** Yaani: Wamepotea katika kumfuata kwao (Mtume) Muhammad, kushikamana kwao na yale aliyokuja nayo na kuacha kwao starehe za sasa.

(33) **NA HAWAKUPELEKWA WAKIWA NI WALINZI KWAO** Makafiri hawakutumwa na Mwenyezi Mungu kwa Waislamu wawe ni walinzi wao wanaotunza hali zao na matendo yao.

(34) **BASI LEO WALE WALIOAMINI WATAWACHEKA MAKAFIRI** Muradi wa "leo" ni Siku ya Mwisho. Yaani: Hakika ya waumini siku hiyo watawacheka makafiri pale watakapowaona wakiwa dhalili, waliohemewa, imewashukia adhabu.Waislamu watawacheka makafiri kama wao walivyowacheka Waislamu duniani.

(35) **WAKIWA JUU YA VITANDA VYENYE UREMBO WANAANGALIA** Yaani: Waumini, wakiwa wamestarehe juu ya vitanda vyenye urembo, watawaangalia maadui wa Mwenyezi Mungu wakiwa wanaadhibiwa motoni.

(36) **JE, MAKAFIRI WAMELIPWA MAMBO WALIYOKUWA WANAYAFANYA?** Yaani: Kwa yakini, makafiri wameyapata malipo ya yale waliyokuwa wanayafanya duniani ya kuwacheka waumini na kuwafanyia stihzai.

## SURATUL-INSHIQAQ (84)

*Ni ya Makka Ina aya ishirini na tano*

(1) **WAKATI MBINGU ZITAKAPOPASUKA** Kupasuka kwake ni miongoni mwa alama za Qiyama.

(2) **NA ZIKAMSIKILIZA MOLA WAKE. NA ZINA HAKI** Yaani: Zikamtii Mola wake. Kusikiliza ni kukitegea sikio kitu na kukisikiliza. (Zina haki, yaani): Zina haki ya kutii, kufuata na kusikiliza.

(3) **NA WAKATI ARDHI ITAKAPOKUNJULIWA** Yaani: Ardhi itakapokunjuliwa na kupondwa milima yake mpaka ikawa tambarare.

(4) **NA IKAVITUPA VILIVYOMO NDANI YAKE NA IKAWA TUPU** Yaani: Ardhi itatoa maiti na madini yaliyomo ndani yake na kuvitupa nje ya mgongo wake ikawa haina vitu hivyo. Ardhi itajitenga na wanadamu na matendo yao. Itajitenga nao ikielekea kwa Mola wake ili amri yake itekelezwe kwao.

(5) **NA IKAMSIKIA MOLA WAKE NA INA HAKI** Yaani: Itayasikia yale anayoiamuru Mola wake na kuyatii. Ina haki ya kuwa tupu na kusikiliza yale ambayo Mola wake anataka kuiamuru.

(6) **EWE MWANADAMU, HAKIKA YA WEWE NI MWENYE JUHUDI KUBWA KUELEKEA KWA MOLA WAKO, BASI UTAKUTANA NAYE** Anayekusudiwa (hapa kwa neno mwanadamu) ni jinsi ya mwanadamu. Kwa hiyo, anaingia Mwislamu na kafiri. Maana ni kwamba: Kwa yakini, wewe katika matendo yako umo katika harakati za kuelekea kwa Mola wako, au kuelekea kukutana na Mola wako. Basi hakuna budi kwamba utakutana na Mola wako kwa matendo yako.

عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ يَنظُرُونَ ٣٥ هَلْ ثُوِّبَ ٱلْكُفَّارُ مَا كَانُوا۟ يَفْعَلُونَ ٣٦

## سُورَةُ الانشِقَاق

ترتيبها ٨٤ — آياتها ٢٥

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنشَقَّتْ ١ وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ٢ وَإِذَا ٱلْأَرْضُ مُدَّتْ
٣ وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ ٤ وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ٥ يَٰٓأَيُّهَا
ٱلْإِنسَٰنُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَٰقِيهِ ٦ فَأَمَّا مَنْ أُوتِىَ
كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ ٧ فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا ٨ وَيَنقَلِبُ
إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ مَسْرُورًا ٩ وَأَمَّا مَنْ أُوتِىَ كِتَٰبَهُۥ وَرَآءَ ظَهْرِهِۦ ١٠ فَسَوْفَ
يَدْعُوا۟ ثُبُورًا ١١ وَيَصْلَىٰ سَعِيرًا ١٢ إِنَّهُۥ كَانَ فِىٓ أَهْلِهِۦ مَسْرُورًا ١٣
إِنَّهُۥ ظَنَّ أَن لَّن يَحُورَ ١٤ بَلَىٰٓ إِنَّ رَبَّهُۥ كَانَ بِهِۦ بَصِيرًا ١٥ فَلَآ أُقْسِمُ
بِٱلشَّفَقِ ١٦ وَٱلَّيْلِ وَمَا وَسَقَ ١٧ وَٱلْقَمَرِ إِذَا ٱتَّسَقَ ١٨
لَتَرْكَبُنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٍ ١٩ فَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ٢٠ وَإِذَا قُرِئَ
عَلَيْهِمُ ٱلْقُرْءَانُ لَا يَسْجُدُونَ ۩ ٢١ بَلِ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ يُكَذِّبُونَ
٢٢ وَٱللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوعُونَ ٢٣ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ٢٤
إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ٢٥

(7) **BASI AMA ATAKAYEPEWA KITABU CHAKE KWA MKONO WAKE WA KUUME** Hao ni waumini. Watapewa kwa mikono yao ya kuume vitabu vyao ambavyo ndani yake mna ufafanuzi wa mambo yao mema.

(8) **BASI ATAHISABIWA HISABU NYEPESI** Hisabu nyepesi ni kuoneshwa maovu yake kisha Mwenyezi Mungu atayasamehe bila ya hisabu hiyo kujadiliwa. Hiyo ndio hisabu nyepesi. Katika Sahiih Bukhaariy na Sahiih Muslim, imepokewa kutoka kwa Mama Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, akisema kuwa: " Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kwamba: Yeyote ambaye hisabu (yake) itajadiliwa, basi ataadhibiwa. Akasema (Mama Aisha): Nikasema (kumwambia Mtume): Hivi si Mwenyezi Mungu anasema:"ATAHISABIWA HISABU NYEPESI?". Akasema (Mtume): Huko sio kuhisabiwa, lakini ni kuoneshwa matendo tu. Yeyote ambaye hisabu (yake) itajadiliwa Siku ya Qiyama, basi ataadhibiwa" [1]

(9) **NA ATARUDI KWENYE FAMILIA YAKE AKIWA NA FURAHA** Yaani: Baada ya hisabu nyepesi, ataondoka kwenda kwenye familia yake ambayo iko peponi ikiwa ni pamoja na wake na watoto, au ataelekea kwa wale Mahurul-ain alioandaliwa na Mwenyezi Mungu peponi huku akifurahia kheri na takrima alizopewa.

(10) **NA AMA ATAKAYEPEWA KITABU CHAKE NYUMA YA MGONGO WAKE** Yaani: Atapewa kitabu chake nyuma ya mgongo wake kwa sababu mkono wake wa kuume umefungwa shingoni mwake, na mkono wake wa kushoto utakuwa nyuma yake.

(11) **BASI ATAOMBA KUANGAMIA** Yaani: Atakaposoma kitabu chake, atasema: Oo! Ole wangu! Nimeangamia!

(12) **NA ATAINGIA MOTONI** Yaani: Ataingia motoni na kuungua kwa joto na ukali wake.

(13) **HAKIKA, YEYE ALIKUWA KATIKA WATU WAKE NI MWEMYE FURAHA** Alikuwa mwenye furaha kwa kufuata na kuyapanda matamanio ya nafsi yake kwa sababu ya kiburi, kwa vile Akhera haikuingia akilini mwake.

(14) **KWA YAKINI, YEYE ALIDHANI KUWA HATARUDI** Maana ni kwamba: Sababu ya furaha yake ni dhana yake kwamba hatarejea kwa Mwenyezi Mungu, na kwamba hatafufuliwa kwa ajili ya hisabu na adhabu.

(15) **KWANI? HAKIKA YA MOLA WAKE ALIKUWA ANAMUONA** Yaani: Kwa yakini, atarejea na atafufuliwa. Mwenyezi Mungu alikuwa anamjua yeye na matendo yake. Katika hayo, hakuna kilichojificha kwake.

(16) **NINA APA KWA WEKUNDU WA JUA** Mwenyezi Mungu Mtukufu ana apia wekundu wa jua. Wekundu wa jua ni ule wekundu unaokuwepo baada ya kuzama kwa jua mpaka wakati wa Swala ya Isha.

(17) **NA USIKU NA ULICHOKUSANYA** Yaani: Usiku umekusanya kile kilichokuwa kimesambaa mchana katika harakati zake. Na hiyo ni kwa sababu usiku unapoingia, kila kitu kinaelekea kwenye makao yake.

(18) **NA MWEZI UNAPOKAMILIKA** Yaani: Mwezi unapokusanyika na kukamilika. Kukamilika kwa mwezi ni kujaa kwake, kukusanyika kwake na kuwa sawa sawa. Na hali hii inapatikana katikati ya siku za mwezi mwandamo.

(19) **KWA YAKINI, MTAPANDA TABAKA KWA TABAKA** Enyi watu, kwa yakini, mtapanda hali baada ya hali; utajiri na ufukara, kifo na uhai, kukusanywa na kuhisabiwa na kuingia peponi au motoni.

(20) **BASI WANA NINI HAO, HAWAAMINI?** Wana nini hawataki kumwamini Muhammad na

---

[1] *Sahih Bukhari, Hadithi Na. 6055. Sahih Muslim, Hadithi Na. 5122*

Qur'ani aliyokuja nayo, pamoja na kuwepo kwa mambo yanayowajibisha kuamini hayo?

(21) **NA WAKATI WANAPOSOMEWA QUR'ANI, HAWASUJUDU** Yaani: Ni kitu gani kinachowazuia wasisujudu na kunyenyekea wakati wa kusomwa Qur'ani? Na yasemekana kuwa kilichokusudiwa ni sijda ile ile inayojulikana kuwa ni *sijdatu-tilaawa* (inayoletwa na msomaji pia msikilizaji wakati inaposomwa Qur'ani).

(22) **BALI WALE AMBAO WAMEKUFURU WANAPINGA** Yaani: Wanakipinga kitabu ambacho ndani yake mna kumpwekesha Mwenyezi Mungu, kufufuliwa na thawabu na adhabu.

(23) **NA MWENYEZI MUNGU ANAYAJUA SANA WANAYOYAKUSANYA** Yaani: Mwenyezi Mungu anaujua ukafiri wanaouficha katika nafsi zao, na matendo mema na mabaya wanayoyakusanya.

(24) **BASI WAPE HABARI NJEMA ZA ADHABU YENYE KUUMIZA** Maneno haya yametoka katika muundo wa kuwakejeli wao (makafiri).

(25) **ISIPOKUWA TU WALE AMBAO WAMEAMINI NA WAKATENDA MEMA. HAO, WANA MALIPO YASIYO SIMBULIWA** Hawatasimangwa kwa malipo hayo.

## SUURATUL-BURUUJ (85)

*Ni ya Makka,na aya zake ni ishirini na mbili*

(1) **NINA'APA KWA MBINGU ZENYE BURUJI** Buruji ni nyota. Pia imesemwa kuwa Buruji ni vituo vya sayari, navyo ni vituo kumi na mbili vya sayari kumi na mbili.

(2) **NA SIKU ILIYOAHIDIWA** Yaani: Siku iliyoahidiwa kuwa itakuja nayo ni Siku ya Qiyama.

(3) **NA SHAHIDI NA KINACHOSHUHUDIWA** Muradi wa "shahidi" ni vile viumbe vitakavyotoa ushahidi katika siku hiyo ya Qiyama. Na muradi wa "kinachoshuhudiwa" ni yale maovu makubwa kabisa ambayo watu waovu waliwafanyia hao mashahidi wenyewe, ambao ni kila aliyeuliwa katika kuitetea dini ya Mwenyezi Mungu, kama ilivyo katika kisa cha watu waliowatesa Waislamu katika mahandaki, kisa ambacho maelezo yake yatakuja. Na Mwenyezi Mungu pia atakuwa shahidi juu yao, kama yatakavyokuja maelezo yake baadae. Na imesemwa pia kwamba "Shahidi" ni siku ya Ijumaa ambayo inamshuhudia kila mtu kwa kile alichokitenda katika siku hiyo. Na "Kinachoshuhudiwa" ni siku ya Arafa (siku ya Mwezi tisa, Mfungo Tatu). Siku hiyo watu wanashuhudia msimu wa Hija na pia Malaika hushuhudia.

(4) **WAMELAANIWA WATU WA MAHANDAKI** Watu wa mahandaki ni mfalme mmoja kafiri na majeshi yake. Baadhi ya raia wake walipoamini, waliwachimbia mashimo na kukoka moto ndani yake. Kisha wakawaambia Waislam hao kuwa:Yeyote katika nyinyi atakayeiacha dini yake (mpya), basi tutamwacha. Na ambaye hataiacha dini yake, tutamtia katika moto. Waislam (walikataa kuiacha dini yao na)Wakawa na subira [katika kushikamana na dini yao].Walitupwa kwenye moto, wakaungua na ilhali mfalme na watu wake wakitazama. Kisa hiki ni kirefu. *Kiangalie katika Sahihi Muslim, Juzuu ya 4, ukurasa wa 2299. (Hadithi Na.*

(5) **MOTO WENYE KUNI** Kuni ni kitu ambacho hukokewa moto kwacho.

(6) **WAKATI WAO JUU YAKE NI WENYE KUKAA** Yaani: Wamelaaniwa pale walipokuwa wakiuangalia moto hali ya kuwa wamekaa juu ya viti mbele ya yale mahandaki (wakifurahia kuwatesa Waislamu).

(7) **NA WAO KWA YALE WANAYOYAFANYA KWA WAISLAMU NI WENYE KUSHUHUDIA** Yaani: Mfalme na watu wake waliochimba mahandaki watashuhudia Siku ya Qiyama juu ya yale waliyoyafanya kwa Waislamu ambayo ni kuwatishia kuwachoma moto ili wapate kuingia kwenye dini yao (ya ukafiri). Halafu pia zitakuwa mashahidi ndimi zao, mikono na miguu yao.

(8) **NA HAWAKUWATESA ISIPOKUWA TU NI KWA KULE KUMWAMINI KWAO MWENYEZI MUNGU MWENYE NGUVU, MWENYE KUHIMIDIWA** Yaani: Hawa Waislam hawakutenda jambo baya lolote dhidi ya utawala mpaka wakateswa kiasi hicho isipokuwa tu kwamba wao wamemkubali Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda, Mwenye kusifiwa katika hali zote. Watawala hawakuona baya lolote kwao isipokuwa tu imani yao.

(9) **AMBAYE NI WAKE YEYE TU UFALME WA MBINGUNI NA ARDHINI. NA MWENYEZI MUNGU JUU YA KILA KITU NI SHAHIDI** Basi yule ambaye mambo yake ni haya, huyo ndiye mwenye haki ya kuaminiwa na kupwekeshwa. (Mwnyezi Mungu ni shahidi wa kila jambo), Ikiwa ni pamoja na vitendo vyao, watu wa mahandaki, walivyowafanyia Waislamu. Hakifichiki kitu chochote kwake. Katika haya, kuna makemeo makali sana kwa wale watu waliowatesa Waislamu katika mahandaki, na pia kuna ahadi ya kheri kwa wale Waumini walioteswa kwa sababu ya dini ya Mwenyezi Mungu.

(10) **HAKIKA, WALE AMBAO WALIWAFITINI WAUMINI WANAUME NA WAUMINI WANAWAKE KISHA WASITUBU, BASI WATAKUWA NA ADHABU YA JAHANNAMU NA WATAKUWA NA ADHABU YA KUUNGUA**

سُورَةُ ٱلۡبُرُوجِ — ترتيبها ٨٥ — آياتها ٢٢

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلسَّمَآءِ ذَاتِ ٱلۡبُرُوجِ ١ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡمَوۡعُودِ ٢ وَشَاهِدٖ وَمَشۡهُودٖ
٣ قُتِلَ أَصۡحَٰبُ ٱلۡأُخۡدُودِ ٤ ٱلنَّارِ ذَاتِ ٱلۡوَقُودِ ٥ إِذۡ هُمۡ عَلَيۡهَا
قُعُودٞ ٦ وَهُمۡ عَلَىٰ مَا يَفۡعَلُونَ بِٱلۡمُؤۡمِنِينَ شُهُودٞ ٧ وَمَا نَقَمُواْ
مِنۡهُمۡ إِلَّآ أَن يُؤۡمِنُواْ بِٱللَّهِ ٱلۡعَزِيزِ ٱلۡحَمِيدِ ٨ ٱلَّذِي لَهُۥ مُلۡكُ
ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ وَٱللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ شَهِيدٌ ٩ إِنَّ ٱلَّذِينَ
فَتَنُواْ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ ثُمَّ لَمۡ يَتُوبُواْ فَلَهُمۡ عَذَابُ جَهَنَّمَ وَلَهُمۡ
عَذَابُ ٱلۡحَرِيقِ ١٠ إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَهُمۡ
جَنَّٰتٞ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡكَبِيرُ ١١ إِنَّ بَطۡشَ
رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ١٢ إِنَّهُۥ هُوَ يُبۡدِئُ وَيُعِيدُ ١٣ وَهُوَ ٱلۡغَفُورُ ٱلۡوَدُودُ ١٤
ذُو ٱلۡعَرۡشِ ٱلۡمَجِيدُ ١٥ فَعَّالٞ لِّمَا يُرِيدُ ١٦ هَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ٱلۡجُنُودِ
١٧ فِرۡعَوۡنَ وَثَمُودَ ١٨ بَلِ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ فِي تَكۡذِيبٖ ١٩ وَٱللَّهُ مِن
وَرَآئِهِم مُّحِيطُۢ ٢٠ بَلۡ هُوَ قُرۡءَانٞ مَّجِيدٞ ٢١ فِي لَوۡحٖ مَّحۡفُوظِۭ ٢٢

سُورَةُ ٱلطَّارِقِ — ترتيبها ٨٦ — آياتها ١٧

Yaani: Wale waliowachoma Waislamu kwa moto na, katika kufanya hivyo, hawakuwapa hiyari isipokuwa tu kumkufuru Mwenyezi Mungu, na kwa hiyo wakawatesa kwa sababu ya dini yao ili waiache, kisha wasitubu kutokana na vitendo vyao viovu na kuacha kufuru zao na fitina (mateso) yao (kwa Waislamu), basi watapata adhabu ya Jahanamu huko Akhera kwa sababu ya kukufuru kwao.

Na pia watapata adhabu nyingine ya ziada mbali ya ile adhabu ya kukufuru kwao, na ambayo ni adhabu ya kuungua kwa sababu ya ule moto waliowachoma waumini (kwenye mahandaki).

11 **HAKIKA, WALE WALIOAMINI NA KUTENDA MEMA WATAPATA MABUSTANI YAPITAYO MITO MBELE YAKE. HUKO NDIKO KUFUZU KUKUBWA** Yaani: (Wale walioamini) Na miongoni mwao ni wale waliouvumilia moto wa kwenye mahandaki, wakawa imara katika dini yao na hawakuritadi (hawakutoka katika Uislamu wao), watapata mabustani kwa sababu ya imani na matendo mema. Hayo yaliyotajwa ndio kufaulu ambako hakulingani, hakukurubii wala hakusogelei kufaulu kokote.

12 **HAKIKA, KUTIA MKONONI KWA MOLA WAKO NI KUKUBWA** (Kuadhibu kwa Mola wako ni kukubwa) Kwa yule anayemuasi. Yaani: Kuwatia mkononi mwake watu majabari, jeuri na madhalimu ni kukubwa kabisa, kunaongezeka na kurudufika.

13 **HAKIKA, YEYE NDIYE ANAYEANZA NA KURUDISHA** Yaani: Yeye ndiye anayeumba viumbe kwanza hapa Duniani, na yeye ndiye atakayevirudisha (huko Akhera) vikiwa hai baada ya kufa.

14 **NAYE NI MSAMEHEVU SANA, MPENZI SANA** Yaani: Ni Msamehevu sana wa madhambi ya waja wake Waumini, hawafedheheshi kwa madhambi hayo. Ni Mwenye Mapenzi mno kwa waja wake watiifu.

15 **MWENYE ARSHI, MKARIMU** Yaani: Yeye Mtukufu ndiye Mola wa Arshi tukufu. Ukarimu ni ufadhili na takrima ya kiwango cha juu kabisa.

16 **MWINGI WA KUFANYA ATAKALO**

17 **JE, IMEKUFIKIA HABARI YA MAJESHI?** Yaani: Je, imekufikia, ewe Muhammad, habari ya makundi ya makafiri wenye kuwakadhibisha Mitume wao na ambao waliwakusanyia majeshi ili kupigana nao vita?

18 **FIRAUNI NA THAMUDI** Muradi wa habari yao ni ule upinzani na ukafiri wao walioufanya, na adhabu iliyowapata.

19 **BALI WALE AMBAO WAMEKUFURU WAMO KATIKA KUKADHIBISHA** Yaani: Bali hawa washirikina wa Kiarabu wamo katika kukukadhibisha sana wewe (Muhammad) na yale mambo uliyokuja nayo, na wala hawakupata onyo kwa yale yaliyowapata makafiri waliokuwa kabla yao.

20 **NA MWENYEZI MUNGU AMEWAZUNGUKA KOTE KOTE** Yaani: Mwenyezi Mungu anaweza kuwateremshia kama yale aliyowateremshia hao (makafiri waliokuwa kabla yao).

21 **BALI HIYO NI QUR'ANI TUKUFU** Yaani: Qura'ni ni kilele katika utukufu, heshima na baraka, na wala haiko kama vile makafiri wanavyosema kuwa ni ushairi, ukuhani na uchawi.

22 **IPO KATIKA UBAO ULIOHIFADHIWA** Yaani: Qur'ani imeandikwa katika ubao ambao ni asili ya kitabu. Umehifadhiwa na Mwenyezi Mungu, haufikiwi na mashetani.

## SUURATI THWAARIQ (86)

*Ni ya Makka Aya zake ni kumi na saba*

1 **NINA APA KWA MBINGU NA KIJACHOUSIKU** Mwenyezi Mungu ana'apa kwa mbingu na kijachousiku. Kijachousiku ni nyota. Nyota zimeitwa "Kijachousiku",kwa sababu hudhihiri wakati wa usiku na kujificha wakati wa mchana. Kila kitu kinachokujia usiku,

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ
وَٱلسَّمَآءِ وَٱلطَّارِقِ ١ وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا ٱلطَّارِقُ ٢ ٱلنَّجۡمُ ٱلثَّاقِبُ ٣ إِن كُلُّ
نَفۡسٖ لَّمَّا عَلَيۡهَا حَافِظٞ ٤ فَلۡيَنظُرِ ٱلۡإِنسَٰنُ مِمَّ خُلِقَ ٥ خُلِقَ مِن مَّآءٖ
دَافِقٖ ٦ يَخۡرُجُ مِنۢ بَيۡنِ ٱلصُّلۡبِ وَٱلتَّرَآئِبِ ٧ إِنَّهُۥ عَلَىٰ رَجۡعِهِۦ لَقَادِرٞ ٨
يَوۡمَ تُبۡلَى ٱلسَّرَآئِرُ ٩ فَمَا لَهُۥ مِن قُوَّةٖ وَلَا نَاصِرٖ ١٠ وَٱلسَّمَآءِ ذَاتِ ٱلرَّجۡعِ ١١
وَٱلۡأَرۡضِ ذَاتِ ٱلصَّدۡعِ ١٢ إِنَّهُۥ لَقَوۡلٞ فَصۡلٞ ١٣ وَمَا هُوَ بِٱلۡهَزۡلِ ١٤ إِنَّهُمۡ
يَكِيدُونَ كَيۡدٗا ١٥ وَأَكِيدُ كَيۡدٗا ١٦ فَمَهِّلِ ٱلۡكَٰفِرِينَ أَمۡهِلۡهُمۡ رُوَيۡدَۢا ١٧

## سُورَةُ الأَعۡلَى

ترتيبها ٨٧ — آياتها ١٩

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ
سَبِّحِ ٱسۡمَ رَبِّكَ ٱلۡأَعۡلَى ١ ٱلَّذِي خَلَقَ فَسَوَّىٰ ٢ وَٱلَّذِي قَدَّرَ فَهَدَىٰ
٣ وَٱلَّذِيٓ أَخۡرَجَ ٱلۡمَرۡعَىٰ ٤ فَجَعَلَهُۥ غُثَآءً أَحۡوَىٰ ٥ سَنُقۡرِئُكَ
فَلَا تَنسَىٰٓ ٦ إِلَّا مَا شَآءَ ٱللَّهُۚ إِنَّهُۥ يَعۡلَمُ ٱلۡجَهۡرَ وَمَا يَخۡفَىٰ ٧ وَنُيَسِّرُكَ
لِلۡيُسۡرَىٰ ٨ فَذَكِّرۡ إِن نَّفَعَتِ ٱلذِّكۡرَىٰ ٩ سَيَذَّكَّرُ مَن يَخۡشَىٰ ١٠
وَيَتَجَنَّبُهَا ٱلۡأَشۡقَى ١١ ٱلَّذِي يَصۡلَى ٱلنَّارَ ٱلۡكُبۡرَىٰ ١٢ ثُمَّ لَا يَمُوتُ
فِيهَا وَلَا يَحۡيَىٰ ١٣ قَدۡ أَفۡلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ١٤ وَذَكَرَ ٱسۡمَ رَبِّهِۦ فَصَلَّىٰ ١٥

basi hicho ni kijachousiku *"At-twariq"*.

(2) **NA NI NINI KITACHOKUJULISHA WEWE, NI KIPI HICHO KIJACHOUSIKU?**

(3) **NI NYOTA ITOBOAYO** Itoboayo ni inga'arayo na kutoa mwanga mkali kama kwamba inatoboa kwa nguvu giza la usiku.

(4) **HAKUNA NAFSI YOYOTE ILA TU INAYE MHIFADHI** Hili ni jibu la kiapo (kilichopo katika aya ya kwanza ya sura hii). Yaani: Hakuna nafsi yoyote ila inaye mhifadhi. Wahifadhi ni wale Malaika ambao wanahifadhi matendo ya watu, amali na kauli zao, na kudhibiti kheri au shari wanazotenda. Na kwa kweli mhifadhi hasa ni Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu na utukufu. Kuhifadhi kwa Malaika ni jumla ya kuhifadhi kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu kuhifadhi kwao huko ni kwa amri yake.

(5) **BASI HEBU MTU ATAZAME: NI KUTOKANA NA NINI AMEUMBWA?** Ni wajibu juu ya binadamu kutafakari mwanzo wa kuumbwa kwake, ili aweze kujua uwezo wa Mwenyezi Mungu juu ya kufufua walio kufa, jambo ambalo ni dogo kuliko huko kuumba kwa mara ya kwanza.

(6) **AMEUMBWA KUTOKANA NA MAJI YANAYORUKA** Yaani: Maji yanayomiminwa katika mfuko wa uzazi, nayo ni maji ya mwanaume na ya mwanamke, kwa sababu binadamu ameumbwa kutokana nayo. Lakini Mwenyezi Mungu ameyafanya yote hayo kuwa ni maji mamoja, kwa sababu ya kuchanganyika kwake (na kuwa kitu kimoja).

(7) **YATOKAYO KATI YA MIFUPA YA (UTI WA) MGONGO NA YA KIFUA** Yaani: Mgongo wa mwanaume na kifua cha mwanamke. Mifupa ya kifua *"At-Taraaib"* ni pale mahali panapokaa kidani katika kifua (cha mwanamke). Mtoto hawi isipokuwa tu kwa maji mawili (ya mke na ya mume). Na yasemekana kuwa: Maana ni kwamba maji hayo yanatoka kutoka katika sehemu zote za mwili (wa binaadamu).

(8) **HAKIKA , YEYE JUU YA KUMRUDISHA NI MUWEZA** Maana ni kuwa: Kwa hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kumrudisha binadamu kwa kumfufua baada ya kufa ni muweza. Naye Muqatil amesema kwamba: "Maana ni kuwa: (Mimi Mwenyezi Mungu) Nikitaka nitamrudisha kutoka katika utuuzima kwenda katika ujana, na kutoka ujana kwenda katika utoto, na kutoka katika utoto kwenda katika hali ya tone la manii.

(9) **SIKU SIRI ZITAKAPOWEKWA WAZI** Yaani: Mwenyezi Mungu atamrudisha binaadamu katika siku ambayo siri zitadhihirishwa, kwa maana ya kuwa zitachambuliwa na kujulikana. Siri zenyewe ni zile itikadi, nia na mambo mengine yanayofichwa katika nyoyo. Wakati huo, yaliyo mema katika hayo yatajitenga na yaliyo mabaya.

(10) **BASI HATAKUWA NA NGUVU ZOZOTE, WALA WA KUMNUSURU** Yaani: Mwanadamu hatakuwa na nguvu nafsini mwake ambazo kwazo anaweza kujizuia na adhabu ya Mwenyezi Mungu, wala hatakuwa na yeyote wa kumnusuru akaweza kumuokoa na yale yaliyomfika.

(11) **NINA APA KWA MBINGU YENYE REJEA** *"Arraj'u*, Rejea" ni mvua. Mvua imeitwa hivyo kwa sababu huja, hurudi na kurejea mara kwa mara.

(12) **NA ARDHI YENYE MPASUKO** Mpasuko ni ile mimea, matunda na miti ambayo ardhi hupasuka ili kuitoa.

(13) **HAKIKA, HIYO NI KAULI IPAMBANUAYO** Yaani: Qur'ani ni kauli inayopambanua kati ya haki na batili.

(14) **NA SIO MASKHARA** Yaani: Qur'ani haikuteremka kwa mchezo, bali ni kweli na sio mzaha.

(15) **HAKIKA, WAO WANAFANYA VITIMBI** Yaani: Wanafanya hila za kubatilisha dini ya haki aliyokuja nayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

(16) **NAMI NAFANYA VITIMBI VIKUBWA**

Yaani: Nawachukulia kidogo kidogo kwa namna ambayo hawaijui, na nitawalipa malipo ya vitimbi vyao.

17 **BASI WAPE MUDA MAKAFIRI. WAPE MUDA KIDOGO** Yaani: Waache na usimuombe Mwenyezi Mungu aharakishe kuwaangamiza. Tosheka na jinsi Mwenyezi Mungu anavyokupangia kuhusu masuala yao. Wape muda wangojee kidogo au muda mfupi.

# SURA AL-AALAA (87)

*Ni Ya Makkah Aya zake ni kumi na tisa*

1 **LITAKASE JINA LA MOLA WAKO MTUKUFU SANA** Yaani: Mtakase Mola wako na kila sifa isiyolingana naye kwa kusema: "SUBHAANA RAB-BIYAL-AALAA= UTAKASIFU NI WA MOLA WANGU MTUKUFU ZAIDI". Wakati ilipoteremka aya hii, alisema Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: "Iwekeni hiyo Tasbiih katika kusujudu kwenu (katika swala)". *(Ameipokea Hadithi hii Abudaauud, Na. 736).*

Na yasemekana kuwa maana ya aya hii ni: Litakase jina la Mola wako, na umtajapo Mola wako, usimtaje isipokuwa tu unapokuwa mnyenyekevu kwake, mwenye taadhima na kuheshimu utajo wake.

2 **AMBAYE AMEUMBA NA AKAWEKA SAWA** Amemuumba binadamu akiwa yuko sawa sawa, akakiweka vizuri kimo chake, akauweka sawa ufahamu wake na akamuandaa kwa ajili ya kubeba majukumu.

3 **NA AMBAYE AMEKADIRIA NA AKAONGOZA** Maana ni kwamba Mwenyezi Mungu amekadiria jinsi za vitu; aina zake, sifa zake, vitendo vyake, kauli zake na muda wake wa kuishi. Amekiongoza kila kimoja katika ya hivyo kwenye yale inayoyatenda na yanayotakikana kwake. Amekirahisishia kila kitu yale aliyokiumbia na kukipa *Il-hamu* (fahamu) katika mambo ya dini yake na dunia yake. Amekadiria riziki za viumbe na vyakula vyao, na akawaongoza katika mambo yao ya maisha kama ni binadamu, na malisho yao kama ni wanyama. Ameumba manufaa katika vitu, na akamuongoza binadamu njia ya kuyapata manufaa hayo kutoka katika vitu hivyo.

4 **NA AMBAYE AMETOA MALISHO** Yaani: Ameotesha nyasi na mimea ya kijani ambayo wanyama wanakula.

5 **KISHA AKAYAFANYA YENYE KUVUNJIKA VUNJIKA, MEUSI** Yaani: Akayafanya malisho hayo, baada ya kuwa ya rangi ya kijani, makavu, yenye kuvunjika vunjika na meusi. Hiyo ni kwa sababu, nyasi zinapokauka zinakuwa nyeusi.

6 **TUTAKUSOMESHA NA HIVYO HUTASAHAU** Tutakufanya msomaji kwa kukutia *Il-hamu* (fahamu) ya kusoma na hutasahau yale utakayosoma. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa anapomjia Jibrili na *wahyi* (ufunuo), huwa Jibrili hawahi kumaliza mwisho wa aya ila Mtume huyasema yale ya mwanzo wake, kwa kuchelea kuyasahau. Ndipo ikateremka aya hii: TUTAKUSOMESHA NA HUTASAHAU Mwenyezi Mungu akampa ufahamu Mtume na kumhifadhi asiisahau Qur'an.

7 **ILA TU ATAKALO MWENYEZI MUNGU. HAKIKA, YEYE ANAYAJUA YALIYODHAHIRI NA YALE YANAYOFICHIKA** Ila alitakalo Mwenyezi Mungu ulisahau, basi hilo utalisahau tu. Na yasemekana kuwa hii ina maana ya *Naskh* (Kufuta). Yaani: Isipokuwa tu analotaka Mwenyezi Mungu kulifuta katika yale yaliyofutwa kisomo chake, basi hilo utalisahau (kwa maana ya kuwa limefutwa).

Yaani: Mwenyezi Mungu anayajua ya dhahiri na ya ndani. Miongoni mwa yaliyo dhahiri ni kila afanyalo au kulisema mtu kwa dhahiri. Na miongoni mwa yanayojificha ni kila alifanyalo mtu kwa siri kati yake na nafsi yake katika mambo ambayo hapana ayajuaye ispokuwa tu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

8 **TUTAKURAHISISHIA YALIYO MEPESI** Yaani:Tutakufanyia wepesi wa matendo ya kukupeleka peponi, na tutakurahisishia ufunuo ili upate kuuhifadhi na kuutekeleza. Au maana ni kwamba: Tutakusaidia katika kufuata njia nyepesi ya dini na dunia katika kila jambo miongoni mwa mambo ya dini na dunia ambayo yanakukabili.

9 **BASI KUMBUSHA KAMA UTAFAA UKUMBUSHO** Yaani: Ewe Muhammad wape watu mawaidha kwa yale tuliyokufunulia, na waelekeze kwenye njia za kheri, na pia wajulishe sheria za dini, pale ambapo kukumbusha kutaonesha manufaa. Ama yule aliyekumbushwa na kubainishiwa haki kwa uwazi, baada ya hapo, akafuata matamanio ya nafsi yake na akashupalia maasi, hakuna haja ya kumkumbusha. Msimamo huu ni katika kukariri na kurudiarudia ulinganiaji. Ama ulinganiaji na ukumbusho wa mara ya kwanza ni wa jumla (hauangalii kufaa kwa ukumbusho au kutofaa).

10 **ATAONYEKA YULE AOGOPAYE** Yaani: Ataonyeka kwa mawaidha yako yule anayemuogopa Mwenyezi Mungu. Kwa ukumbusho huo, atazidi kumuogopa Mwenyezi Mungu na atazidi kuwa mtu mwema.

11 **NA ATAUKWEPA MWINGI WA MAOVU** Yaani: Ataukwepa ukumbusho huo na kuwa mbali nao yule aliye muovu zaidi katika makafiri, kwa sababu ya kung'ang'ania kwake kumkufuru Mwenyezi Mungu na kuzama kwake

بَلْ تُؤْثِرُونَ ٱلْحَيَوٰةَ ٱلدُّنْيَا ﴿١٦﴾ وَٱلْـَٔاخِرَةُ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰٓ ﴿١٧﴾ إِنَّ
هَٰذَا لَفِى ٱلصُّحُفِ ٱلْأُولَىٰ ﴿١٨﴾ صُحُفِ إِبْرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾

ترتيبها ٨٨ — سُورَةُ الْغَاشِيَةِ — آياتها ٢٦

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

هَلْ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ٱلْغَٰشِيَةِ ﴿١﴾ وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَٰشِعَةٌ ﴿٢﴾
عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٣﴾ تَصْلَىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٤﴾ تُسْقَىٰ مِنْ عَيْنٍ ءَانِيَةٍ ﴿٥﴾
لَّيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِن ضَرِيعٍ ﴿٦﴾ لَّا يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِى مِن جُوعٍ ﴿٧﴾
وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ ﴿٨﴾ لِّسَعْيِهَا رَاضِيَةٌ ﴿٩﴾ فِى جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿١٠﴾
لَّا تَسْمَعُ فِيهَا لَٰغِيَةً ﴿١١﴾ فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ﴿١٢﴾ فِيهَا سُرُرٌ مَّرْفُوعَةٌ ﴿١٣﴾
وَأَكْوَابٌ مَّوْضُوعَةٌ ﴿١٤﴾ وَنَمَارِقُ مَصْفُوفَةٌ ﴿١٥﴾ وَزَرَابِىُّ مَبْثُوثَةٌ ﴿١٦﴾
أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى ٱلْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿١٧﴾ وَإِلَى ٱلسَّمَآءِ كَيْفَ
رُفِعَتْ ﴿١٨﴾ وَإِلَى ٱلْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿١٩﴾ وَإِلَى ٱلْأَرْضِ كَيْفَ
سُطِحَتْ ﴿٢٠﴾ فَذَكِّرْ إِنَّمَآ أَنتَ مُذَكِّرٌ ﴿٢١﴾ لَّسْتَ عَلَيْهِم
بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٢﴾ إِلَّا مَن تَوَلَّىٰ وَكَفَرَ ﴿٢٣﴾ فَيُعَذِّبُهُ ٱللَّهُ ٱلْعَذَابَ
ٱلْأَكْبَرَ ﴿٢٤﴾ إِنَّ إِلَيْنَآ إِيَابَهُمْ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم ﴿٢٦﴾

katika maasi.

(12) **AMBAYE ATAUINGIA MOTO MKUBWA SANA** Yaani: Atauingia moto mkubwa wa kutisha. Na Moto mdogo ni moto wa duniani.

(13) **KISHA HATAKUFA HUMO NA HATAKUWA HAI** Hatakufa akapata kupumzika na adhabu aliyonayo,na hatakuwa na uhai atakaonufaika nao.

(14) **KWA HAKIKA, AMEFAULU YULE ALIYEJITAKASA** Yaani: Aliyejitakasa ni yule aliyejisafisha na ushirikina, na hivyo, akamwamini Mwenyezi Mungu, akampwekesha yeye tu na kuzitekeleza sheria zake. Na yasemekana pia kuwa muradi wa aya hii ni kujitakasa kwa kutoa zaka ya mali.

(15) **NA AKATAJA JINA LA MOLA WAKE NA HIVYO, AKASALI** Imesemwa kuwa maana ni mtu kutaja jina la Mola wake kwa ulimi wake akasimamisha swala tano. Na yasemekana kuwa maana ni kwamba: Akakumbuka kusimama kwake mbele ya Mola wake na kurejea kwake na, kwa ajili hiyo, akamwabudu Mwenyezi Mungu. Na Imesemwa pia kuwa muradi wa kujitakasa katika aya ya kwanza ni Zakaatul-fitri, na muradi wa kuswali ni Swala ya Iddi.

(16) **BALI MNAPENDA MNO MAISHA YA DUNIA** Yaani: Hamfanyi hayo (ya kuswali, kujitakasa n.k) bali mnakhiyari starehe za duniani zinazokwisha.

(17) **NA ILHALI AKHERA NI BORA ZAIDI NA YENYE KUBAKI** Akhera ni bora zaidi na yenye kudumu kuliko dunia. Malik Bin Diinar amesema kuwa: "Lau ingelikuwa dunia ni ya dhahabu inayokwisha, na Akhera ni ya vigae vya udongo unaodumu, basi ingelikuwa ni wajibu kukhiyari vigae vya udongo vyenye kudumu kuliko dhahabu yenye kwisha. Ni vipi basi (mtu apuuze Akhera) na ilhali Akhera ni ya dhahabu yenye kubaki, na dunia ni ya vigae vya udongo vyenye kwisha?".

(18) **HAKIKA, HAYA YAMO KATIKA VITABU VYA KWANZA** Haya yaliyotangulia; ya kufaulu Mwenye kujitakasa na yaliyo baada yake yamethibiti katika vitabu hivyo vya mwanzo.

(19) **VITABU VYA IBRAHIMU NA MUSA** Vitabu vya Mwenyezi Mungu vimeafikiana kwamba Akhera ni bora na inabaki kuliko dunia.

## SURA AL-GHASHIYAH (88)

*Ni ya Makkah Aya zake ni ishirini na sita.*

(1) **JE, IMEKUFIKIA HABARI YA KIFINIKACHO?** Yaani: Kwa yakini imekufikia, ewe Muhammad, habari ya tukio lifinikalo, ambalo ni Qiyama. Qiyama kimeitwa "Kifinikacho" kwa sababu kitawafinika viumbe kwa matukio yake ya kutisha.

(2) **NYUSO SIKU HIYO ZITAKUWA ZENYE KUDHALILIKA** Yaani: Kwa hakika, watu Siku ya Qiyama watakuwa makundi mawili. La kwanza nyuso zao zitakuwa dhalili, nyonge kwa sababu ya adhabu watakayokuwa nayo. Na imesemwa kuwa Mwenyezi Mungu hapa amekusudia hasa nyoso za Wayahudi na Wanaswara.

(3) **NI ZENYE KUFANYA AMALI, NI ZENYE KUTAABIKA** (Wenye nyuso hizo) Walikuwa wakijisumbua katika kufanya ibada na kujitaabisha kuzitekeleza ilhali hawana malipo yoyote juu ya ibada hizo, kwa sababu ya ukafiri na upotevu**2** walionao.

(4) **ZITAUINGIA MOTO MKALI SANA**

(5) **ZITANYWESHWA KATIKA CHEMCHEM ZENYE KUCHEMKA SANA** Yaani: Watakunywa maji yake. Al-aaniy: Ni maji ya kiwango cha juu katika kuchemka

(6) **HAWATAKUWA NA CHAKULA ISIPOKUWA MIBA TU** Adh-dharii: Katika lugha ya Waquraish ni aina ya miba ambayo inapokuwa mibichi inaitwa Al-Shabraq. Ikikauka, ndiyo huitwa Adh-dharii.

(7) **HAINENEPESHI NA HAIONDOI NJAA**

Yaani: Miba hiyo haimnenepeshi anayeila wala haimuondolei njaa aliyonayo.

8 **NYUSO SIKU HIYO NI ZENYE KUN'GARA** Yaani: Zitakuwa na neema na furaha. Nyuso hizi ni za watu wa kundi la pili (watu wema). Watakuwa hivyo kwa sababu ya mwisho wao mwema watakaouona.

9 **KWA AMALI ZAKE, ZITARIDHIKA** Yaani: Wataridhika na amali zao walizozitenda hapa duniani, kwa sababu watakuwa wamepewa malipo yaliyowaridhisha.

10 **ZITAKUWA KATIKA PEPO YA JUU**

11 **HAUTASIKIKA HUMO UPUUZI** Yaani: Katika maneno ya watu wa peponi, hapatasikika neno la kipuuzi, kwa sababu wao hawatazungumza ila maneno ya hekima na ya kumsifu Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya neema za kudumu alizowaruzuku.

12 **HUMO MNA CHEMCHEM ZINAZOTIRIRIKA** Maji yake yanatiririka, yanaruka na kutoa aina mbali mbali za vinywaji vyenye ladha nzuri.

13 **HUMO MNA VITI VYA FAHARI VILIVYOWEKWA JUU**

14 **NA GLASI ZILIZOWEKWA** Glasi ni bilauri ambazo ndani yake mna tembo. Zimewekwa mbele yao wanakunywa kwazo.

15 **NA MITO YA KUEGEMEA ILIYOPANGWA** Mito iliyopangwa kwa mistari, mmoja mbele ya mwingine.

16 **NA MAZULIA YALIYOTANDIKWA** *Azzaraabiyyu* ni mazulia yenye matamvua laini yakiwa yametandikwa katika mahala pengi tofauti pa kukaa.

17 **JE, HAWAWATAZAMI NGAMIA JINSI WALIVYOUMBWA?** Hivi hawatizami ngamia ambao ndio sehemu muhimu ya mifugo yao (Waarabu) na pia ni viumbe vikubwa mno wanavyoviona? Hivi hawatizami jinsi walivyo katika umbo zuri sana, ikiwa ni pamoja na ukubwa wa umbo lake, nguvu zake za ziada na sifa zake nyingine nzuri. Mwenyezi Mungu amewatanabahisha juu ya kiumbe kikubwa alichokiumba (ngamia) kwa kuwa amemfanya kuwa mtiifu hata kwa mtoto mdogo awezaye kumchunga, kumuinamisha, kumsimamisha na kumbebesha mizigo mizito akiwa amepiga magoti, kisha anainuka pamoja na uzito wa mzigo wake.

18 **NA MBINGU JINSI ILIVYOINULIWA?** (Hebu atizame mwanadamu) Jinsi mbingu ilivyoinuliwa juu ya ardhi bila ya nguzo, kwa namna ambayo fahamu na akili za binadamu haziwezi kufikia.

19 **NA MILIMA JINSI ILIVYOSIMAMISHWA?** Yaani: Milima jinsi ilivyosimamishwa juu ya ardhi. Imekitwa ikiwa imara; haiyumbi, haianguki wala haitoweki.

20 **NA ARDHI JINSI ILIVYOTANDAZWA?**

21 **BASI KUMBUSHA. HAKIKA, HAPANA VINGINE ILA WEWE NI MKUMBUSHAJI TU** Yaani: Wape mawaidha ewe Muhammad na watie woga (wa kumuogopa Mwenyezi Mungu). Wewe huna jukumu isipokuwa hilo tu.

22 **WEWE SI MWENYE MAMLAKA JUU YAO** (Huna mamlaka nao) Mpaka ufikie kuwalazimisha kuamini.

23 **LAKINI YULE ALIYERUDI NYUMA NA AKAKUFURU** Yaani : Lakini yule aliyegeuka na kupuuza mawaidha na ukumbusho

24 **BASI MWENYEZI MUNGU ATAMUADHIBU ADHABU KUBWA KABISA** Adhabu hiyo kubwa kabisa ni adhabu ya kudumu ya Jahanamu.

25 **HAKIKA, KWETU TU NDIO MAREJEO YAO** Yaani: Marejeo yao ni kwetu tu baada ya kufa.

26 **KISHA BILA SHAKA, NI JUU YETU HISABU YAO** Yaani: Mahesabu yao ni juu yetu, na kisha tutawalipa kwa mujibu wa matendo yao, baada ya kurudi kwao kwa Mwenyezi Mungu kwa kufufuliwa.

## SURATUL-FAJRI (89)

*Ni ya Makka Aya zake ni thalathini.*

1 **NINA APA KWA ALFAJIRI** Mwenyezi Mungu ameapa kwa Alfajri kwa kuwa huo ni wakati wa kupambazuka kiza kwa kuja mchana. Mujahid amesema kuwa:"Mwenyezi Mungu anakusudia Alfajri ya siku ya kuchinja (Mwezi kumi, mfunguo tatu, siku ya sikukuu ya *Idd Adhhaa*).

2 **NA SIKU KUMI** Yaani: Siku kumi za mwezi wa Mfungo Tatu (kumi la mwanzo).

3 **NA SHAF'I NA WAT'RI** Shaf'i ni vitu viwili viwili. Watri ni kimoja kimoja katika vitu vyote. Na yasemekana kuwa muradi wa *Shaf'i* ni siku mbili za *Tashriiq;* ya kwanza na ya pili (tarehe 11, 12, Mfungo Tatu) siku ambazo inaruhusiwa kwa mtu (aliyeko Mina kwa ibada ya Hija) kuharakisha kuondoka katika siku hizo. Na *Wat'ri* ni siku ile ya tatu (mwezi 13).

4 **NA USIKU UNAPOPITA** Yaani: Usiku unapokuja na kuingia kisha ukaondoka.

5 **JE, KATIKA HAYO KUNA KIAPO KWA MWENYE AKILI?** Mwenye akili na utambuzi atajua kuwa vitu alivyoviapia Mwenyezi Mungu miongoni mwa hivi vilivyotajwa vinastahiki kuapiwa.

6 **JE, HUKUONA ALIVYOFANYA MOLA WAKO KWA AAD?** *Aad* ni wale watu wa *Aad* wa Kwanza. Wale waliokuja baada yao, wanaitwa Aad wa Mwisho. Nabii wao alikuwa Huud. Walimkadhibisha na, hivyo, ukawakumba ukelele (wakaangamia wote).

7 **IRAM WENYE MAJUMBA MAREFU**

ترتيبها ٨٩ — سُورَةُ الفَجۡرِ — آياتها ٣٠

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلۡفَجۡرِ ١ وَلَيَالٍ عَشۡرٖ ٢ وَٱلشَّفۡعِ وَٱلۡوَتۡرِ ٣ وَٱلَّيۡلِ إِذَا يَسۡرِ
٤ هَلۡ فِي ذَٰلِكَ قَسَمٞ لِّذِي حِجۡرٍ ٥ أَلَمۡ تَرَ كَيۡفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ
٦ إِرَمَ ذَاتِ ٱلۡعِمَادِ ٧ ٱلَّتِي لَمۡ يُخۡلَقۡ مِثۡلُهَا فِي ٱلۡبِلَٰدِ ٨
وَثَمُودَ ٱلَّذِينَ جَابُواْ ٱلصَّخۡرَ بِٱلۡوَادِ ٩ وَفِرۡعَوۡنَ ذِي ٱلۡأَوۡتَادِ ١٠
ٱلَّذِينَ طَغَوۡاْ فِي ٱلۡبِلَٰدِ ١١ فَأَكۡثَرُواْ فِيهَا ٱلۡفَسَادَ ١٢ فَصَبَّ
عَلَيۡهِمۡ رَبُّكَ سَوۡطَ عَذَابٍ ١٣ إِنَّ رَبَّكَ لَبِٱلۡمِرۡصَادِ ١٤ فَأَمَّا
ٱلۡإِنسَٰنُ إِذَا مَا ٱبۡتَلَىٰهُ رَبُّهُۥ فَأَكۡرَمَهُۥ وَنَعَّمَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّيٓ أَكۡرَمَنِ
١٥ وَأَمَّآ إِذَا مَا ٱبۡتَلَىٰهُ فَقَدَرَ عَلَيۡهِ رِزۡقَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّيٓ أَهَٰنَنِ ١٦
كَلَّاۖ بَل لَّا تُكۡرِمُونَ ٱلۡيَتِيمَ ١٧ وَلَا تَحَٰٓضُّونَ عَلَىٰ طَعَامِ
ٱلۡمِسۡكِينِ ١٨ وَتَأۡكُلُونَ ٱلتُّرَاثَ أَكۡلٗا لَّمّٗا ١٩
وَتُحِبُّونَ ٱلۡمَالَ حُبّٗا جَمّٗا ٢٠ كَلَّآ إِذَا دُكَّتِ ٱلۡأَرۡضُ دَكّٗا
دَكّٗا ٢١ وَجَآءَ رَبُّكَ وَٱلۡمَلَكُ صَفّٗا صَفّٗا ٢٢ وَجِاْيٓءَ يَوۡمَئِذِۭ
بِجَهَنَّمَۚ يَوۡمَئِذٖ يَتَذَكَّرُ ٱلۡإِنسَٰنُ وَأَنَّىٰ لَهُ ٱلذِّكۡرَىٰ ٢٣

**SANA** *Iram* ni jina jingine la watu wa *Aad* wa Kwanza. Na yasemekana pia kwamba *Iram* ni babu yao. Na inasemwa pia kwamba *Iram* ni jina la mahali pao ambapo ni mji wa Damuscus (Dimashki) au mji mwingine huko *Ahqaaf*. Maana ya wao kuwa na majumba marefu, amesema Mujahid kwamba wao ni watu wa maguzo na mahema katika wakati wa masika. Inapostawi mimea, hurudi majumbani kwao. Yasemekana kuwa mji wao ulikuwa na majumba imara sana yenye maguzo marefu yaliyonakshiwa.

(8) **AMBAO HAUKUUMBWA MFANO WAO KATIKA MIJI** Yaani: Haukuumbwa mfano wa kabila hilo katika urefu, ukali na nguvu. Nao ni wale ambao walisema: "Ni nani Mwenye nguvu zaidi kuliko sisi?" Sura Haamiim Sajda 41, aya 15. Au maana ya aya hii ni kwamba haikuumbwa miji kama ile katika uimara wa majengo yake.

(9) **NA THAMUD AMBAO WAMECHONGA MAJABALI KATIKA VIWANJA** Walikuwa wakichonga majabali, kuyatoboa na kufanya yale matobo kuwa ni nyumba wanazoishi humo. Viwanja vyao ni *Hij-ri* au *Waadil-qura* katika njia iendayo Sham kutokea mji wa Madina Munawwara.

(10) **NA FIRAUNI MWENYE VIGINGI** Vigingi ni yale mapyramids waliyoyajenga watawala wa Misri ili yawe makaburi yao. Waliwadhalilisha watu wao katika kuyajenga. Na imesemwa pia kwamba maana yake Firauni mwenye majeshi yenye mahema mengi wanayoyafunga na kuyakaza kwa vigingi.

(11) **AMBAO WALIFANYA MAOVU KATIKA MIJI** Hii ni sifa ya *Aad, Thamud* na *Firaun*. Yaani: Kila kundi miongoni mwao lilifanya maovu, ukorofi na ujeuri katika nchi zao.

(12) **WAKAZIDISHA UOVU HUMO** Wamezidisha maovu kwa kufanya kufuru, kumuasi Mwenyezi Mungu na kuwafanyia dhuluma waja wake.

(13) **MOLA WAKO AKAWAMIMINIA BAKORA YA ADHABU** Yaani : Akayamiminia na kuyatupia adhabu makundi hayo, kama isemwavyo: "Nimemmiminia bakora mtu muovu". Yaani: Nimempiga mijeledi mikali sana.

(14) **HAKIKA, MOLA WAKO YUKO KATIKA MAVIZIO** Anadhibiti tendo la kila mtu, ili kwa jambo la kheri alilofanya amlipe kheri, na kwa shari amlipe shari. Na Alhasan amesema kuwa maana ni kwamba: "Kwake yeye tu ndio njia (marejeo) ya waja. Hamponyoki mtu yeyote".

(15) **AMA BINADAMU ANAPOJARIBIWA NA MOLA WAKE NA AKAMKIRIMU, BASI HUSEMA: MOLA WANGU AMENIKIRIMU** Yaani: Mwenyezi Mungu anapompa mtihani mwanadamu na kumjaribu kwa kumpa neema; akamkirimu kwa kumpa mali na kumkunjulia riziki yake, basi anakuwa na itikadi kwamba hiyo ni takrima huku akichekelea aliyoyapata na kufurahia yale aliyopewa, bila ya kumshukuru Mwenyezi Mungu juu ya hayo, na wala haimpitii katika moyo wake kwamba huo ni mtihani kwake kutoka kwa Mola wake.

(16) **NA AMA ANAPOMJARIBU AKAIFANYA NDOGO RIZIKI YAKE, BASI HUSEMA: MOLA WANGU AMENIDHALILISHA** Yaani: Mwenyezi Mungu anapomtia mwanadamu majaribuni na kumpa mtihani;
akaifanya finyu riziki yake, asiikunjue na asiipanue basi husema: Mola wangu amenitwisha madhila. Hii ni sifa ya kafiri ambaye haamini kufufuliwa baada ya kufa, kwa sababu yeye kwake haoni isipokuwa dunia tu na kukunjuliwa starehe zake. Na wala kwake haoni udhalili isipokuwa tu kuikosa dunia na kutoyafikia mapambo yake ayatakayo. Ama Mwislamu, heshima kwake ni kukirimiwa na Mwenyezi Mungu kwa kupata uwezo wa kumtii yeye na kuwezeshwa kutenda matendo ya Akhera. Na

madhila kwake ni kutowezeshwa na Mwenyezi Mungu kuwa mtiifu na kutenda matendo ya watu wa peponi. Wasaa wa dunia sio heshima kwake, na wala dhiki ya dunia sio madhila. Utajiri kwake hauna maana nyingine isipokuwa tu ni mtihani kwa tajiri kwamba je, atashukuru? Na ufukara pia ni mtihani kwa masikini kwamba je, atavumilia?

(17) **HAPANA, BALI NYINYI HAMUMFANYII UKARIMU YATIMA** Hili ni onyo na ni kemeo kwa yule mtu aliyesema aliyoyasema katika hali zote mbili (Ya kwanza ni pale anaponeemeshwa anasema: "Amehishimiwa", na ya pili ni pale asiponeemeshwa anasema: "Amedhalilishwa"). Hamufanyii ukarimu yatima katika ule utajiri aliokupeni Mwenyezi Mungu. Lau mngaelimfanyia ukarimu yatima, basi hiyo ingekuwa ni heshima kwenu mbele ya Mwenyezi Mungu.

(18) **NA HAMUHIMIZANI JUU YA KUWAPA CHAKULA MASIKINI** Yaani: Hamjihimizi nyinyi wenyewe, au baadhi yenu hawawahimizi wengine juu ya hilo. Hakuna anayeamuru hilo wala kulielekeza, na kwa hiyo masikini anabaki akiwa amehemewa, amezidiwa kati yenu na hanyooshewi mkono wa msaada.

(19) **NA MNAKULA MIRATHI ULAJI MKUBWA** Mirathi ni mali za Yatima, wanawake (wajane) na wanyonge. Yaani: Ulaji mkubwa kabisa. Mnazila ulaji mkubwa sana.

(20) **NA MNAPENDA MALI MAPENZI MAKUBWA**

(21) **HAPANA! ITAKAPOVUNJWA ARDHI VIPANDE VIPANDE** Yaani: Hivyo sivyo. Haitakiwi vitendo vyenu viwe hivi! *Dakk* (Kuvunjavunja): Ni kuvunja na kuponda. Maana ni kwamba: Kumbukeni itakapotetemeshwa ardhi na kutikiswa mtikisiko mmoja baada ya mwingine. Au maana ni kwamba: Kumbukeni itakapovunjwa milima mpaka ikawa sawa sawa (kama vile hapakuwa na milima).

(22) **NA AKAJA MOLA WAKO NA ILHALI MALAIKA WAMEJIPANGA SAFU** Atakuja Mola wako aliyetakasika ili kupitisha hukumu kati ya waja wake. Malaika nao watakuja wakiwa wamejipanga mistari.

(23) **NA SIKU HIYO ITALETWA JAHANAMU. SIKU HIYO ATAKUMBUKA MWANADAMU, NA LAKINI KUTAMFAA NINI KUKUMBUKA HUKO?** Jahanamu italetwa ikiwa imefungwa hatamu na ilhali Malaika wanaikokota. Mwanadamu atajuta kwa ule ukafiri na maasi aliyoyafanya duniani. Kukumbuka kungelimfaa kama tu angeliikumbuka haki kabla ya kufika mauti.

(24) **ATASEMA: "LAITI NINGEUTANGULIZIA UHAI WANGU"**

(25) **BASI SIKU HIYO, HAKUNA YEYOTE ATAKAYEADHIBU KAMA ANAVYOADHIBU YEYE** Yaani: Hakuna yeyote atakayeadhibu kama anavyoadhibu Mwenyezi Mungu.

(26) **NA HATAFUNGA PINGU YEYOTE KAMA KUFUNGA KWAKE** Yaani: Hakuna yeyote atakayemfunga kafiri kwa minyororo na pingu kama Mwenyezi Mungu anavyofunga.

(27) **EWE NAFSI ULIYETULIA** Ewe nafsi yenye yakini katika imani na kumpwekesha Mwenyezi Mungu, isiyochanganyika na mashaka, isiyopatwa na wasi wasi, iliyoridhika na hukumu ya Mwenyezi Mungu, iliyojua kuwa jambo lililomkosa halikupangwa kumfika na lililompata halikupangwa kumkosa. Nafsi hiyo siku ya Qiyama, itakuja ikiwa imetulia kwa sababu, wakati wa kufa na wakati wa kufufuliwa, ilikwishapewa habari njema ya kupata pepo.

(28) **REJEA KWA MOLA WAKO UKIWA NI MWENYE KURIDHIKA, MWENYE KURIDHIWA** Ni mwenye kuridhika na malipo ambayo Mola wako amekupa, ni mwenye kuridhiwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

(29) **BASI INGIA KATIKA WAJA WANGU** Yaani: Ingia katika kundi la waja wangu wema, na uwe miongoni mwao.

(30) **INGIA KATIKA PEPO YANGU** Yaani: Ingia katika pepo yangu pamoja na hao waja wangu wema. Hiyo ndiyo takrima na heshima ya kweli. Hakuna takrima na heshima zaidi ya hiyo.

# SURATUL BALAD (90)

*Ni ya Makka Aya zake ni ishirini.*

(1) **NINA APA KWA MJI HUU** Maana ni kwamba Mwenyezi Mungu ameapa kwa mji mtukufu, nao ni mji wa Makkah. Hiyo inatokana na kwamba Mwenyezi Mungu anataka kubainisha utukufu wa Mama wa Miji (Makka) na ubora wake mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu humo: **1)** Mna nyumba yake tukufu (*Al-kaaba*). **2)** Ni mji wa Mtume Ismail na Muhammad, Mwenyezi Mungu awafikishie rehema na amani. **3)** Kuna mwahala mwa matendo ya Hija.

(2) **NA WEWE NI MWENYE KUSHUKA KATIKA MJI HUU** Yaani: Ewe Muhammad, makafiri wa Makka wamehalalisha kukuudhi wewe katika Mji Mtukufu. Na Imesemwa pia kuwa maana ni kwamba: Nina apa kwa mji huu ambao wewe unaishi humo, ikiwa ni taadhima kwako na heshima ya hadhi yako, kwa sababu, mji huu umekuwa Mtukufu na wa heshima kwa kule kuishi kwako humo.

(3) **NA MZAZI NA ALICHOKIZAA** Mwenyezi Mungu ana apa kwa mzazi na watoto wake, kama vile Nabii Adam na wanawe waliozalikana naye, na pia ana apa kwa kila mzazi na alichokizaa, kwa wanyama wote ikiwa ni kutanabahisha juu ya ukubwa wa suala la kuzaa na

يَقُولُ يَٰلَيۡتَنِي قَدَّمۡتُ لِحَيَاتِي ﴿٢٤﴾ فَيَوۡمَئِذٖ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهُۥٓ أَحَدٞ ﴿٢٥﴾
وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُۥٓ أَحَدٞ ﴿٢٦﴾ يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفۡسُ ٱلۡمُطۡمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرۡجِعِيٓ
إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةٗ مَّرۡضِيَّةٗ ﴿٢٨﴾ فَٱدۡخُلِي فِي عِبَٰدِي ﴿٢٩﴾ وَٱدۡخُلِي جَنَّتِي ﴿٣٠﴾

## سُورَةُ ٱلۡبَلَدِ

ترتيبها ٩٠ — آياتها ٢٠

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

لَآ أُقۡسِمُ بِهَٰذَا ٱلۡبَلَدِ ﴿١﴾ وَأَنتَ حِلُّۢ بِهَٰذَا ٱلۡبَلَدِ ﴿٢﴾ وَوَالِدٖ وَمَا وَلَدَ
﴿٣﴾ لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِي كَبَدٍ ﴿٤﴾ أَيَحۡسَبُ أَن لَّن يَقۡدِرَ عَلَيۡهِ
أَحَدٞ ﴿٥﴾ يَقُولُ أَهۡلَكۡتُ مَالٗا لُّبَدًا ﴿٦﴾ أَيَحۡسَبُ أَن لَّمۡ يَرَهُۥٓ أَحَدٌ
﴿٧﴾ أَلَمۡ نَجۡعَل لَّهُۥ عَيۡنَيۡنِ ﴿٨﴾ وَلِسَانٗا وَشَفَتَيۡنِ ﴿٩﴾ وَهَدَيۡنَٰهُ
ٱلنَّجۡدَيۡنِ ﴿١٠﴾ فَلَا ٱقۡتَحَمَ ٱلۡعَقَبَةَ ﴿١١﴾ وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا ٱلۡعَقَبَةُ ﴿١٢﴾
فَكُّ رَقَبَةٍ ﴿١٣﴾ أَوۡ إِطۡعَٰمٞ فِي يَوۡمٖ ذِي مَسۡغَبَةٖ ﴿١٤﴾ يَتِيمٗا ذَا مَقۡرَبَةٍ
﴿١٥﴾ أَوۡ مِسۡكِينٗا ذَا مَتۡرَبَةٖ ﴿١٦﴾ ثُمَّ كَانَ مِنَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَتَوَاصَوۡاْ
بِٱلصَّبۡرِ وَتَوَاصَوۡاْ بِٱلۡمَرۡحَمَةِ ﴿١٧﴾ أُوْلَٰٓئِكَ أَصۡحَٰبُ ٱلۡمَيۡمَنَةِ ﴿١٨﴾ وَٱلَّذِينَ
كَفَرُواْ بِـَٔايَٰتِنَا هُمۡ أَصۡحَٰبُ ٱلۡمَشۡـَٔمَةِ ﴿١٩﴾ عَلَيۡهِمۡ نَارٞ مُّؤۡصَدَةُۢ ﴿٢٠﴾

## سُورَةُ ٱلشَّمۡسِ

ترتيبها ٩١ — آياتها ١٥

kuzaliana, na jinsi linavyoonesha uwezo wa Mwenyezi Mungu, hekima na ujuzi wake.

4 **KWA HAKIKA, TUMEMUUMBA MWANADAMU KATIKA KUPAMBANA** Mwanadamu hatoacha kuwa katika kupambana na dunia na na tabu zake mpaka anapokufa. Akisha kufa, anapambana na shida za kaburini na maisha ya *Barzakh* (maisha kati ya kufa hadi kufufuliwa) na matukio yake ya kutisha. Halafu mbele yake, kuna shida za Akhera.

5 **HIVI ANADHANI KUWA HAKUNA YEYOTE AMUWEZAYE?** Yaani: Hivi mwanadamu anadhani kwamba hapana yeyote atakayemuweza wala kumuadhibu hata Mola wake Mtukufu, japo akitenda maovu kiasi gani?

6 **ANASEMA: NIMETEKETEZA MALI NYINGI SANA** Yaani: Nimetumia mali nyingi sana iliyorundikana, isiyohofiwa kwisha kwake, kwa sababu ya wingi wake.

7 **HIVI ANADHANI KUWA HAKUNA YEYOTE ALIYEMUONA?** Je, anadhani kuwa Mwenyezi Mungu aliyetakasika hamuoni na hatamuuliza kaichumaje mali hiyo na pia ameitumiaje?

8 **HIVI HATUKUMJAALIA MACHO MAWILI?** Macho ambayo anaona kwayo?

9 **NA ULIMI NA MIDOMO?** Ulimi anaotamka kwao na midomo anayoficha kwayo kinywa chake?

10 **NA TUKAMBAINISHIA NJIA MBILI?** Maana yake ni kuwa: Hivi hatukumtambulisha njia ya kheri na njia ya shari zilizo bayana kama zilivyo njia mbili zilizoinuka juu?

11 **JE, AMEKIVUKA KIKWAZO?** Yaani: Si ingekuwa vyema kwa mwanadamu akachangamka na kuvivuka vikwazo vilivyopo kati yake na kati ya kumtii Mwenyezi Mungu, ikiwa ni pamoja na ushawishi wa nafsi, kufuata matamanio ya nafsi na pia kumfuata shetani. Qatada amesema kuwa: "Kwa hakika, hivyo ni vikwazo vigumu mno. Basi vivukeni kwa kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu".

12 **NA NINI KILICHOKUJULISHA WEWE NI NINI KIKWAZO?**

13 **NI KUACHA HURU MTUMWA** Yaani: Ni kumpa uhuru mtumwa na kumuokoa kutoka katika kudhalilishwa katika utumwa.

14 **AU KULISHA CHAKULA KATIKA SIKU YENYE NJAA** Yaani: Siku yenye njaa ambayo chakula katika siku hiyo ni kitu adhimu.

15 **(KUMPA CHAKULA) YATIMA MWENYE UNDUGU** Yaani: Kumpa chakula yatima. Yatima ni mtoto mdogo ambaye hana baba, na akawa yatima huyu ni miongoni mwa ndugu wa huyu mvukaji kikwazo.

16 **AU MASIKINI MWENYE MCHANGA** Yaani: Masikini mwenye mchanga ni hohe hahe ambaye hana kitu, kama kwamba ameganda kwenye mchanga kwa sababu ya ufukara wake. Mujahid amesema kuwa: "Huyu ni yule mtu ambaye hana nguo wala kitu chochote kingine cha kumkinga na mchanga. Basi yule mtu atakayewapa chakula aina mbili ya watu hawa katika siku za njaa ambazo humfadhaisha binadamu na kumfanya asishughulikie isipokuwa tu nafsi na familia yake, basi hayo ayafanyayo yanakuwa yametokana na ari yake juu ya kumtii Mwenyezi Mungu na kuwanufaisha waja wake. Mtu huyo anastahiki kuwa miongoni mwa watu wa kuliani (Peponi)".

17 **HALAFU AKAWA NI MIONGONI MWA WALE WALIOAMINI NA WAKAUSIANA KUWA NA SUBIRA NA WAKAUSIANA KUWA NA HURUMA** Kwa hakika, ibada hizi za kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu zinakuwa na manufaa zikiwa pamoja na imani na iwapo zitafanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Wakausiana kuwa na subira katika kumtii Mwenyezi Mungu, kuwa na subira katika kuepuka kumuasi na kuwa na subira katika balaa na masaibu yanayowasibu. Wakawa na huruma kwa waja wa Mwenyezi Mungu. Iwapo

watafanya hivyo, bila shaka watamhurumia yatima na masikini, na watafanya mambo mengi ya kheri kwa kutoa sadaka.

(18) **HAO NI WATU WA KULIANI** Kuliani ni Peponi. Mwenyezi Mungu amewataja watu wa upande wa kulia na zile neema alizowaandalia na kuyaweka wazi zaidi hayo kwa ukamilifu kabisa katika *Suratul waaqi'a* (56), aya 26-40. Rejea tafsiri yake huko.

(19) **NA WALE WALIOZIKUFURU AYA ZETU HAO NDIO WATU WA KUSHOTONI** Yaani: Waliokufuru aya za kuteremshwa (maandiko) na aya za kimaumbile hao ni watu wa kushoto. Kushoto ni Moto mbaya. Ufafanuzi wa yale mambo ambayo Mwenyezi Mungu amewaandalia watu wa kushoto umewekwa wazi pia katika *Suratul waaqi'a* (56), aya 41-56.

(20) **JUU YAO UPO MOTO ULIOFUNGIWA** Yaani: Moto ulio katika tabaka, umefungwa (watafungiwa humo, hawataweza kukimbia).

# SURATUSH-SHAMS (91)

*Ni ya Makka Ina aya kumi na tano*

(1) **NINA APA KWA JUA NA MWANGAZA WAKE** Mwangaza wa jua (Dhuhaa) unaokusudiwa ni ule wakati jua linapopanda baada ya kuchomoza kwake, pindipo mwangaza wake ukitimia.

(2) **NA MWEZI PINDI UNAPOLIFUATIA** Yaani: Na mwezi unapolifuata jua. Na hilo linakuwa katika zile siku nyeupe, ambazo ni usiku wa mwezi kumi na nne, mwezi kumi na tano na mwezi kumi na sita. Mwezi katika siku hizo, huchomoza kutoka mashariki baada ya kuzama jua huku ukiwa umejaa (umekamilika).

(3) **NA MCHANA UNAPOLIDHIHIRISHA JUA** Yaani: Mchana unapolidhihirisha jua. Na hiyo ni kwamba mchana unaposambaa, jua linadhihiri kwa ukamilifu zaidi.

(4) **NA USIKU UNAPOLIFINIKA** Usiku unalifinika jua na, kwa hiyo, unauondosha mwangaza wake na matokeo yake jua linazama na anga kufunga kiza.

(5) **NA MBINGU NA ALIYEZIJENGA** Yaani: Nina apa kwa mbingu na Mwenyezi Mungu aliyezijenga.

(6) **NA ARDHI NA ALIYEITANDAZA** Yaani: Ameitandaza kila upande.

(7) **NA NAFSI NA ALIYEIWEKA SAWA** (Mwenyezi Mungu) Ameianzisha nafsi na kuvisawazisha viungo vyake, ametia roho ndani yake, ameweka ndani yake nguvu kubwa za nafsi na hisia za ajabu za ufahamu. Na ameifanya nafsi kuwa ni yenye kunyooka juu ya maumbile asilia, kama ilivyo katika Hadithi kwamba "Kila mwenye kuzaliwa anazaliwa akiwa juu ya maumbile ya asili. Sasa, wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi au awe Mnaswara (Mkristo)". *Ameipokea Hadithi hii Imam Bukhariy, Hadithi Na. 1296. Ahmad, Hadithi Na. 6884. Abuudaud, Hadithi Na. 4091.*

(8) **AKAIFAHAMISHA UOVU WAKE NA UCHAMUNGU WAKE** Ameifahamisha na kuitambulisha hali ya kumcha Mwenyezi Mungu na hali ya kumuasi, na pia wema na uovu uliomo ndani yake.

(9) **HAKIKA, AMEFAULU YULE ALIYEITAKASA** Mwenye kuitakasa nafsi yake na akaiendeleza na kuikweza juu kwa kumcha Mwenyezi Mungu, basi amefaulu kwa kupata kila linalotakiwa na linalopendwa. Imepokewa kutoka kwa Mama Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba yeye alimkosa (hakumuona) Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika sehemu yake ya kulala. (Alipomtafuta kwa kupapasa) Akamgusa kwa mkono wake uliomkuta akiwa amesujudu- na ilhali anasema: "Ewe Mola wangu, ipe nafsi yangu uchamungu wake. Na itakase, wewe ndiye Mbora wa kuitakasa. Wewe ndiye wa kuinusuru, na Mtawala wake". *Ameipokea Hadithi hii Imam Ahmad, Hadithi Na. 24575.*

(10) **NA HAKIKA, AMETOKA PATUPU ALIYEIZAMISHA** Yaani: Amepata hasara mwenye kuipoteza nafsi, akaipotosha, akaidumaza na asiitangaze kwa utiifu na matendo mema.

(11) **THAMUD WAMEKADHIBISHA KWA SABABU YA KUVUKA KWAO MIPAKA** Yaani: Wamekadhibisha kwa sababu ya kupindikia mipaka. Kupindukia mipaka ndiko kulikowapelekea kwenye kukadhibisha. Na kupindikia mpaka *Thughyan* ni kuvuka mipaka katika maasi.

(12) **WAKATI ALIPOJITUMA MUOVU WAO** Yaani: Aliposimama muovu wa kabila la *Thamud*, au kiumbe muovu ambaye ni Qudar bin Salif, akamkata miguu ngamia. Na maana ya kujituma ni kwamba alijiteua mwenyewe kwa ajili ya suala hilo la kumkata miguu ngamia na kulitekeleza.

(13) **MJUMBE WA MWENYEZI MUNGU AKAWAAMBIA: MWACHENI NGAMIA WA MWENYEZI MUNGU NA KINYWAJI CHAKE** Saleh, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, aliwaambia kuwa: Mwacheni ngamia wa Mwenyezi Mungu. Aliwatahadharisha na ngamia huyo na unywaji wake wa maji. Aliwaambia kuwa msiyaingilie maji siku ya zamu yake ya kunywa maji.

(14) **WAKAMKADHIBISHA NA WAKAMKATA MIGUU NGAMIA. MOLA WAO AKAWAANGAMIZA KWA SABABU YA MADHAMBI YAO NA AKAYAFANYA SAWA MAANGAMIZI** Wakamkadhibisha

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴿١﴾ وَالْقَمَرِ إِذَا تَلَاهَا ﴿٢﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّاهَا ﴿٣﴾
وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿٤﴾ وَالسَّمَاءِ وَمَا بَنَاهَا ﴿٥﴾ وَالْأَرْضِ وَمَا طَحَاهَا
﴿٦﴾ وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿٧﴾ فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ﴿٨﴾ قَدْ
أَفْلَحَ مَن زَكَّاهَا ﴿٩﴾ وَقَدْ خَابَ مَن دَسَّاهَا ﴿١٠﴾ كَذَّبَتْ ثَمُودُ
بِطَغْوَاهَا ﴿١١﴾ إِذِ انبَعَثَ أَشْقَاهَا ﴿١٢﴾ فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ
نَاقَةَ اللَّهِ وَسُقْيَاهَا ﴿١٣﴾ فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ
عَلَيْهِمْ رَبُّهُم بِذَنبِهِمْ فَسَوَّاهَا ﴿١٤﴾ وَلَا يَخَافُ عُقْبَاهَا ﴿١٥﴾

ترتيبها ٩٢ — سُورَةُ اللَّيْلِ — آياتها ٢١

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ﴿٢﴾ وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٣﴾
إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّىٰ ﴿٤﴾ فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ ﴿٥﴾ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿٦﴾
فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْيُسْرَىٰ ﴿٧﴾ وَأَمَّا مَن بَخِلَ وَاسْتَغْنَىٰ ﴿٨﴾ وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَىٰ
﴿٩﴾ فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْعُسْرَىٰ ﴿١٠﴾ وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّىٰ ﴿١١﴾ إِنَّ عَلَيْنَا
لَلْهُدَىٰ ﴿١٢﴾ وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ ﴿١٣﴾ فَأَنذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّىٰ ﴿١٤﴾

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kuwahadharisha. Yule muovu alimkata miguu ngamia na ilhali wote wakiridhia kitendo alichofanya. Mwenyezi Mungu aliwaangamiza na kuwafinika kwa adhabu. Maangamizi yalikuwa sawa kwao na kuwaenea wote; mdogo kwa mkubwa. Pamesemwa pia kuwa maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu aliisawazisha ardhi juu yao akawaweka chini ya mchanga.

(15) **NA HAOGOPI MWISHO WAKE** Mwenyezi Mungu amewafanyia hayo bila ya kuogopa hatima wala kufuatiliwa.

## SURATUL-LAYL ( 92)

*Ni ya Makka Inaa ya ishirini na moja*

(1) **NINA APA KWA USIKU UNAPOFINIKA** Mwenyezi Mungu mtukufu ana'apa kwa usiku wakati unapofinika, kwa kiza chake, kila kilichokuwa kinaangaza.

(2) **NA MCHANA UNAPODHIHIRI** Na hiki ni kiapo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuapia mchana pale unapodhihiri, kuangaza na kuwa wazi kutokana na kuondoka kwa kiza kilichokuwepo usiku.

(3) **NA KUUMBWA KWA MWANAMUME NA MWANAMKE** Na hiki pia ni kiapo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu akiapia kuumba kwake jinsia mbili za kike na kiume kwa binadamu na viumbe vingine.

(4) **HAKIKA, MATENDO YENU NI YENYE KUTOFAUTIANA** Hakika, matendo yenu ni yenye kutofautiana. Katika hayo, kuna matendo ya peponi na kuna matendo ya motoni. Kuna Mwenye kuhangaika katika kuiokoa nafsi yake, na mwenye kuhangaika katika kuiangamiza.

(5) **AMA YULE AMBAYE ATATOA NA AKAMCHA MUNGU** Ama yule aliyetoa mali yake katika njia za kheri, na akajikinga na mambo ya haramu ambayo Mwenyezi Mungu ameyakataza.

(6) **NA AKASADIKISHA JAMBO ZURI** Akaisadikisha ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyoahidi kwamba anayetoa atampa badala ya kile alichotoa.

(7) **BASI TUTAMRAHISISHIA YALIYO MEPESI** Tutamrahisishia kutoa katika njia za kheri na kuwa mtiifu kwa Mwenyezi Mungu. Zilishuka aya hizi kwa (Swahaba) Abubakar Siddiq, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, wakati aliponunua Waislamu sita ambao walikuwa katika mikono ya watu wa Makkah wakiwatesa kwa sababu ya Imani yao. Aliwanunua na kuwaacha huru.

(8) **NA AMA YULE AMBAYE ATAFANYA UBAHILI NA AKATOSHEKA** Ama aliyeifanyia ubahili mali yake na asiitoe katika njia za kheri, akapuuza malipo na thawabu, akatosheka na anasa za dunia na kuzipuuza neema za akhera.

(9) **NA AKAKADHIBISHA YALIYO MAZURI** Akakadhibisha badali itolewayo na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

(10) **BASI TUTAMRAHISISHIA YALIYO MAZITO** Tutamuandaa kwa ajili ya jambo zito. Tutalirahisisha kwake, mpaka sababu za kufanya kheri na wema ziwe nzito kwake, na awe mnyonge kuzitenda, hatimae hilo limpelekee kwenda motoni. Ameeleza Bukhari na Muslim, wakinakili kutoka kwa (Swahaba) Ali bin bin Abi-twaalib, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, akisema kuwa: "Tulikuwa pamoja na Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika mazishi. Akasema: Hapana yeyote katika nyinyi ila ni kwamba yamekwishaandikwa makao yake peponi na makao yake motoni. (Swahaba) Wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hivi kwa nini tusikae tu (tukategemea maandishi hayo)? Akasema: Tendeni, kwani kila mmoja wenu amerahisishiwa lile ambalo ameumbiwa. Ama atakayekuwa ni katika watu wema, huyo atarahisishiwa kutenda matendo ya watu wema. Na ama atakayekuwa ni katika watu waovu, huyo atarahisishiwa kutenda matendo ya watu waovu.

Kisha Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akazisoma aya hizi: AMA YULE AMBAYE ATATOA NA AKAMCHA MUNGU, NA AKASADIKISHA YALIYO MAZURI, mpaka neno lake Mwenyezi Mungu: BASI HUYO TUTAMRAHISISHIA YALIYO MAZITO ". *Ameipokea Hadithi hii Imam Bukhari, Hadithi Na. 4564, na Imam Muslim, Hadithi Na. 4787.*

11 **NA HAITAMSAIDIA MALI YAKE PINDI ATAKAPO POROMOKA** Haitamsaidia kitu mali yake ambayo ameifanyia ubahili pindi atakapoangamia na kuangukia katika moto wa Jahanamu, kwa kuwa mali ambayo anaiacha nyuma yake hana malipo yoyote ndani yake madamu hakuwaachia watoto wanaoihitaji. Ama mali ambayo ameitanguliza (ameitumia) yeye mwenyewe, hiyo ndiyo ambayo itamfaa siku ya Qiyama.

12 **HAKIKA, NI JUU YETU TU KUONGOZA** Ni juu yetu kuiweka wazi njia ya uongofu tukaitenganisha na njia ya upotevu. Amesema Alfarraa' kuwa: "Mwenye kufuata uongofu, basi ni juu ya Mwenyezi Mungu njia yake". Amesema: "Mwenye kumtaka Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu yuko njiani. Mwenye kumtaka, ataongoka kuelekea kwake. Na huu ni mfano".

13 **NA HAKIKA, NI MILIKI YETU AKHERA NA DUNIA** Ni yetu sisi yote yaliyopo Akhera na yote yaliyopo Duniani. Tunafanya humo tutakavyo.

14 **KWA HIYO, NIMEKUTAHADHARISHENI MOTO UNAOWAKA** Nimekutahadharisheni moto unaowaka na kutoa miali.

15 **HATAUINGIA ILA TU MTU MUOVU** Muovu ni kafiri. Atachomwa na joto lake.

16 **AMBAYE AMEKADHIBISHA NA AKAPANYONGO** Maana ni: Kafiri ambaye ameikadhibisha haki ambayo wamekuja nayo Mitume, na akapuuza imani na utiifu.

17 **NA ATAEPUSHWA NAO MCHAMUNGU SANA** Na ataepushwa na moto huo yule mwenye kujikinga na ukafiri kinga ya juu sana. Amesema Alwaahidiy kuwa: "Katika kauli ya wafasiri wote wa Qur'an, Mchamungu sana ni Abuubakar Assiddiq, kwa maana kwamba aya hii imeshuka ikimzungumzia yeye. Na pamoja na hayo, hukumu yake inawahusu watu wote. Na Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi".

18 **AMBAYE ANATOA MALI YAKE AKIJITAKASA** Anatoa mali yake na kuitumia katika njia za kheri, akitaka awe msafi mbele ya Mwenyezi Mungu. Hataki kujionesha wala kusifiwa.

19 **NA KWAKE HAKUNA YEYOTE MWENYE NEEMA YOYOTE INAYOLIPWA** Yeye sio katika wale wanaotoa sadaka mali yao kwa mtu yeyote ili walipwe kutokana na sadaka yao hiyo. Hakuna jingine isipokuwa tu kwamba kwa sadaka yake hiyo, anataka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

20 **ISIPOKUWA TU KUTAKA RADHI YA BWANA WAKE ALIYE MTUKUFU SANA** Hatoi ila tu kwa kutaka radhi ya Bwana wake, na sio kwa ajili ya kulipwa neema zake.

21 **NA KWA YAKINI, PUNDE HIVI ATARIDHIA** Nina apa kwa Mwenyezi Mungu kuwa punde hivi ataridhia ukarimu na malipo makubwa tutakayompa.

## SURATUDH-DHUHAA ( 93)

*Ni ya Makkah Ina aya kumi na moja*

Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliumwa na, kwa hiyo, hakuweza kusimama kwa kusali Swala za usiku kwa muda wa siku mbili au tatu. Mwanamke mmoja akamwendea na kumwambia: "Ewe Muhammad, sioni ila shetani wako amekuacha (amekukimbia) tu. Hajakusogelea kwa muda wa siku mbili au tatu". Mwenyezi Mungu akateremsha sura hii:

1 **NINA APA KWA DHUHAA** *Dhuhaa* ni jina la wakati wa kupanda jua.

2 **NA USIKU UNAPOFINIKA** Amesema Al-asma'iyy kuwa: "Kufinika kwa usiku ni kuufunika kwake mchana, kama mtu anavyofinikwa kwa nguo".

3 **HAKUKUACHA MOLA WAKO NA HAKUKUCHUKIA** Hili ndio jibu la kiapo. Maana ni kwamba hakukukata Mola wako kukata kwa Mwenye kuaga, hakukukatia ufunuo na hajakuchukia.

4 **NA, KWA HAKIKA, AKHERA NI BORA ZAIDI KWAKO KULIKO ULIMWENGU** Pepo ni bora zaidi kwako kuliko dunia. Hii ni pamoja na ule utukufu wa Utume ambao Mtume amepewa hapa duniani, utukufu ambao unakuwa mdogo mbele yake kila utukufu. Na kila utukufu hapa ulimwenguni, ukilinganishwa na utukufu huo, unakuwa mdogo.

5 **NA, KWA YAKINI KABISA, ATAKUPA MOLA WAKO NA KWA HIYO UTARIDHIKA** Mwenyezi Mungu atampa Mtume wake ushindi katika dini, thawabu, birika na kuombea umma wake huko Akhera.

6 **HIVI HAKUKUKUTA UKIWA YATIMA AKAKUHIFADHI?** Alikukuta ukiwa yatima; huna baba, akakuwekea hifadhi uliyoiegemea.

7 **NA HAKUKUKUTA UMEDANGANA AKAKUONGOZA?** Alikukuta ukiwa huifahamu imani; hujui imani ni nini. Au alikukukuta ukiwa umeghafilika na yale mambo ya utume ambayo yanatakiwa kwako; hukuwa unajua Qur'an wala sheria. Mwenyezi Mungu

لَا يَصْلَىٰهَآ إِلَّا ٱلْأَشْقَى ﴿١٥﴾ ٱلَّذِى كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٦﴾ وَسَيُجَنَّبُهَا
ٱلْأَتْقَى ﴿١٧﴾ ٱلَّذِى يُؤْتِى مَالَهُۥ يَتَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾ وَمَا لِأَحَدٍ عِندَهُۥ مِن
نِّعْمَةٍ تُجْزَىٰٓ ﴿١٩﴾ إِلَّا ٱبْتِغَآءَ وَجْهِ رَبِّهِ ٱلْأَعْلَىٰ ﴿٢٠﴾ وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ﴿٢١﴾

## سُورَةُ الضُّحَىٰ

ترتيبها ٩٣ — آياتها ١١

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلضُّحَىٰ ﴿١﴾ وَٱلَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾ مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾
وَلَلْءَاخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ ٱلْأُولَىٰ ﴿٤﴾ وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ
فَتَرْضَىٰٓ ﴿٥﴾ أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَـَٔاوَىٰ ﴿٦﴾ وَوَجَدَكَ ضَآلًّا
فَهَدَىٰ ﴿٧﴾ وَوَجَدَكَ عَآئِلًا فَأَغْنَىٰ ﴿٨﴾ فَأَمَّا ٱلْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ
﴿٩﴾ وَأَمَّا ٱلسَّآئِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾ وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

## سُورَةُ الشَّرْحِ

ترتيبها ٩٤ — آياتها ٨

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾ وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ﴿٢﴾ ٱلَّذِىٓ
أَنقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٣﴾ وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ﴿٤﴾ فَإِنَّ مَعَ ٱلْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥﴾ إِنَّ
مَعَ ٱلْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾ فَإِذَا فَرَغْتَ فَٱنصَبْ ﴿٧﴾ وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَٱرْغَب ﴿٨﴾

akakuongoza kwenye hayo.

**8 NA HAKUKUKUTA UKIWA MUHITAJI AKAKUTOSHELEZA?** Alikukuta ukiwa fukara, mwenye familia, huna mali akakutosheleza kwa riziki aliyokupa. Mwenyezi Mungu alimtosheleza Mtume kwa miji aliyoikomboa. Na pamesemwa kuwa Mwenyezi Mungu amemtosheleza Mtume kwa kufanya kwake biashara katika mali ya mkewe, Bibi Khadija binti Khuwailid.

**9 BASI YATIMA USIMDHALILISHE** Usimtawale kwa kumdhulumu kwa sababu ya unyonge wake. Bali mpe haki yake, na kumbuka uyatima wako. Na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa akimfanyia mema na mazuri yatima na kuusia kuwajali yatima.

**10 NA MUOMBAJI USIMFOKEE** Usimfokee muombaji pindi akikuomba, kwani nawe ulikuwa fukara. Sasa ima mpe aliyekuomba au mjibu majibu ya upole.

**11 NA NEEMA YA MOLA WAKO IZUNGUMZE** Mwenyezi Mungu Mtukufu amemwamrisha Mtume kuzizungumza neema za Mwenyezi Mungu alizozineemesha kwake; azidhihirishe na kuzitangaza kwa watu. Na kuzizungumza neema za Mwenyezi Mungu ndio kushukuru. Na imesemwa kuwa muradi wa neema hapa ni Qur'an. Mwenyezi Mungu amemwamrisha Mtume kuisoma Qur'an na kuizungumzia.

## SURATUL-INSHIRAAH (94)

*Ni ya Makka Ina aya nane*

**1 HIVI HATUKUKIKUNJUA KIFUA CHAKO?** Maana ni kwamba: Ewe Muhammad, tumekikunjua kifua chako ili uweze kupokea utume. Kutokea hapa, Mtume aliweza kutekeleza mahubiri aliyotekeleza, na aliweza kubeba majukumu ya utume na kuhifadhi *wahyi* (ufunuo).

**2 NA KUKUONDOLEA MZIGO WAKO?** Tumekufutia yaliyotangulia kwako kabla ya kuja Uislamu.

**3 AMBAO UMEUELEMEA MGONGO WAKO?** Maana yake ni kwamba mzigo huo ungekuwa unabebeka mgongoni, ingesikika sauti ya kunesa kwa mgongo wake. Na imesemwa kuwa mzigo huo ni mzigo wa majukumu ya utume. Mwenyezi Mungu ameurahisisha mpaka ukawa mwepesi kwake.

**4 NA KUKUNYANYULIA UTAJO WAKO?** Mwenyezi Mungu ameunyanyua utajo wake duniani na Akhera kwa mambo mengi. Katika hayo ni haya: **1)** Kuwalazimisha waumini wanaposema: **أشهد أن لا إله إلا الله** Nashuhudia kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba hapana Mola mwenye kupasa kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu tu, amewalazimisha kusema: **وأشهد أن محمدا رسول الله**, Nashuhudia kwa Moyo na kutamka kwa ulimi kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. **2)** Kutajwa kwa Mtume katika Adhana. **3)** Kumuombea rehema na amani. **4)** Mwenyezi Mungu ameamrisha kumtii.

**5 KWA HAKIKA, PAMOJA NA UZITO PANA WEPESI**

**6 HAKIKA, PAMOJA NA UZITO PANA WEPESI** Hakika pamoja na uzito huo ambao umetajwa hapo nyuma, pana wepesi mwingine. Katika maneno yaliyohusishwa kwa Mtume, imepokewa kutoka kwa Ibni-masoudi akisema, kwamba: "Lau kama uzito ungekuwa ndani ya jiwe, basi wepesi ungeufuatia mpaka uingie ndani yake na uutoe. Na uzito mmoja hautashinda wepesi muwili, kwani Mwenyezi Mungu anasema: "Hakika, pamoja na uzito pana wepesi. Hakika, pamoja na uzito pana wepesi". *Ameipokea Hadithi hii Hakim, Na. 3010.*

**7 BASI UKIMALIZA, JITAHIDI** Yaani: Ukimaliza kuswali au kuufikisha ujumbe au kupigana vita, basi jitahidi katika kuomba. Na omba kwa Mwenyezi Mungu tu mahitaji yako. Au maana ni kwamba fanya bidii katika ibada.

**8 NA KWA MOLA WAKO TU, ELEKEA**

Yaelekeze matakwa yako kwa Mwenyezi Mungu peke yake huku ukiwa na hofu ya kuogopa moto na matarajio ya kupata pepo.

## SURATUT-TIIN ( 95)

*Ni ya Makka Ina aya nane*

1 **NINA APA KWA TINI NA ZAITUNI** *Tini* ambayo Mwenyezi Mungu ameiapia hapa ni ile ambayo inaliwa na watu. Na *Zaituni* ni ile ambayo watu wanakamua mafuta kutokana nayo. *Tini* na *Zaituni* (zilizotajwa katika sura hii) ni fumbo la kufumbia miji mitakatifu ambayo imekuwa mashuhuri kwa kuotesha Tini na Zaituni. Mwenyezi Mungu ameapa kwa *Tini* kwa sababu ni tunda lililotakaswa na mchanganyiko wenye madhara. Wataalamu wengi wa tiba wamesema kuwa tunda la *Tini* lina manufaa mengi kwa mwili wa mwanadamu, na lina viini lishe vingi sana. Ama *Zaituni,* tunda hilo hukamuliwa mafuta kutokana nalo, mafuta ambayo ni kichovyeo kikuu cha vyakula vya baadhi ya watu wa miji, na ndio mafuta yao. Na Zaituni pia inaingia katika kutengeneza dawa nyingi.

2 **NA MLIMA SININ** Huo ni mlima ambao juu yake Mwenyezi Mungu alizungumza na Mtume Mussa juu yake iwe amani ya Mola, nao ni Mlima wa Sinai.

3 **NA HUU MJI WENYE AMANI** Mwenyezi Mungu anakusudia mji wa Makkah. Ameuita kuwa ni Wenye Amani kwa sababu una amani. Yaelekea kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ameziapia sehemu hizo tatu kwa sababu sehemu hizo ni mashukio ya ufunuo wa Mwenyezi Mungu juu ya wale Mitume waliopewa majukumu makubwa. Kutoka katika sehemu hizo, uliangaza uongofu kwa wanadamu.

4 **KWA YAKINI, TUMEMUUMBA MWANADAMU KATIKA ULINGANIFU WA UMBILE LILILO ZURI SANA** Mwenyezi Mungu amekiumba kila kiumbe chenye roho kikiwa kimeinama juu ya uso wake, ila tu mwanadamu. Kwani Mwenyezi Mungu, kwa hakika, amemuumba mwanadamu akiwa katika kimo kilichonyooka, anachukua chakula chake kwa mkono wake. Amemuumba akiwa mwenye kujua, mwenye kusema, mwenye kupanga mambo, mwenye hekima. Kwa sifa hizo,Mwenyezi Mungu amemuezesha kuwa Khalifa wake katika dunia kama alivyomtakia hilo.

5 **KISHA TUTAMRUDISHA CHINI ZAIDI YA WALIO CHINI** Yaani: Tutamrudisha katika umri ulio dhaifu sana, nao ni ukongwe na unyonge baada ya ujana na nguvu, mpaka awe kama mtoto mdogo. Akili yake itatetereka na kupungua. Watu walio chini ni wale wanyonge, wenye magonjwa ya kudumu na watoto wadogo. Mzee mkongwe ni mnyonge zaidi wa hao wote. Imesemwa pia kuwa maana ya aya hii ni kwamba: Hakika, mwanadamu ambaye Mwenyezi Mungu amemuumba akiwa katika hali na sura nzuri, atarudishwa akiwa ni mbaya zaidi kuliko kila mnyama na katika hali mbaya zaidi kuliko kila hali, kwa sababu yeye atarudishwa kupelekwa kwenye daraja za chini zaidi, katika daraja za chini za moto ikiwa atamuasi mola wake.

6 **ILA TU WALE AMBAO WAMEAMINI NA WAKATENDA MATENDO MEMA. HAO, WANA MALIPO YASIYOKATIKA** Hao hawatarudishwa chini zaidi ya walio chini. Bali, kwa sababu ya utiifu wao, watapelekwa kwenye pepo za Mwenyezi Mungu zilizo pana, zilizo za juu, ambazo ni malipo ya kudumu na yasiyokatika.

7 **NI LIPI BASI LINALOKUFANYA UKADHIBISHE DINI BAADA YA HAYO?** Yaani: Ukishajua, ewe mwanadamu, kwamba Mwenyezi Mungu amekuumba katika umbile lililo zuri sana na kwamba yeye atakurudisha chini ya walio chini, sasa ni jambo gani tena linalokufanya ukanushe kufufuliwa na kulipwa? Na imesemwa kuwa matamshi haya anaambiwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Maana ikiwa ni kwamba: Ni jambo gani, ewe Muhammad, litakalokufanya ukadhibishe baada ya kudhihiri dalili zenye kutamka? Basi, pamoja na yale yaliyokujia kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kuwa na yakini kwamba yeye Mwenyezi Mungu ndio Mwenye hekima zaidi ya wenye hekima.

8 **HIVI MWENYEZI MUNGU HAKUWA NI HAKIMU ZAIDI YA MAHAKIMU?** Maana ni kwamba Mwenyezi Mungu, kwa hukumu na uadilifu, ni hakimu zaidi ya mahakimu pale alipolifanya zuri sana umbile la mwanadamu, kisha amewafidikiza wale waliomkufuru katika daraja za chini zaidi za moto, na kuwaweka daraja za juu za pepo wale ambao wamemwamini.

## SURATUL-ALAQ ( 96)

*Ni ya Makka Ina aya kumi na tisa*

Aya tano za mwanzo wa sura hii ndio Qur'an ya mwanzo kushuka.

1 **SOMA KWA JINA LA MOLA WAKO AMBAYE AMEUMBA** Yaani: Soma ukianza kwa jina la Mola wako. Na imesemwa pia kwamba: Soma ukiomba msaada kwa jina la Mola wako ambaye ameumba. Mwenyezi Mungu Mtukufu amejisifu kwetu kwa sifa hii ya kuumba ili kukumbusha neema. Kwani neema ya kuumbwa ndio neema ya kwanza kabisa, na ndio neema kubwa sana.

2 **AMEMUUMBA MWANADAMU KUTOKANA NA PANDE LA DAMU** Yaani:

## سُورَةُ التِّينِ

ترتيبها ٩٥ — آياتها ٨

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

وَالتِّينِ وَالزَّيْتُونِ ﴿١﴾ وَطُورِ سِينِينَ ﴿٢﴾ وَهَٰذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ﴿٣﴾
لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾ ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ
﴿٥﴾ إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦﴾
فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالدِّينِ ﴿٧﴾ أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمِ الْحَاكِمِينَ ﴿٨﴾

## سُورَةُ الْعَلَقِ

ترتيبها ٩٦ — آياتها ١٩

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ﴿١﴾ خَلَقَ الْإِنسَانَ مِنْ عَلَقٍ ﴿٢﴾ اقْرَأْ وَرَبُّكَ
الْأَكْرَمُ ﴿٣﴾ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ﴿٤﴾ عَلَّمَ الْإِنسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٥﴾ كَلَّا إِنَّ
الْإِنسَانَ لَيَطْغَىٰ ﴿٦﴾ أَن رَّآهُ اسْتَغْنَىٰ ﴿٧﴾ إِنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ الرُّجْعَىٰ ﴿٨﴾ أَرَأَيْتَ
الَّذِي يَنْهَىٰ ﴿٩﴾ عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰ ﴿١٠﴾ أَرَأَيْتَ إِن كَانَ عَلَى الْهُدَىٰ ﴿١١﴾ أَوْ أَمَرَ
بِالتَّقْوَىٰ ﴿١٢﴾ أَرَأَيْتَ إِن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٣﴾ أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ اللَّهَ يَرَىٰ ﴿١٤﴾ كَلَّا لَئِن
لَّمْ يَنتَهِ لَنَسْفَعًا بِالنَّاصِيَةِ ﴿١٥﴾ نَاصِيَةٍ كَاذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ﴿١٦﴾ فَلْيَدْعُ نَادِيَهُ
﴿١٧﴾ سَنَدْعُ الزَّبَانِيَةَ ﴿١٨﴾ كَلَّا لَا تُطِعْهُ وَاسْجُدْ وَاقْتَرِب ۩ ﴿١٩﴾

Amewaumba wanadamu. Pande la damu ni damu iliyoganda. Iwapo damu itachirizika, basi hiyo ni damu yenye kumwagika. Pande la damu ni hatua katika hatua za kuumbwa kwa mwanadamu tumboni mwa mama. Kwani huanza kuumbwa akiwa ni tone la manii, kisha hubadilika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kuwa pande la damu lililo kama donge la damu iliyoganda. Kisha anakuwa kama pande la nyama iliyotafunwa. Kisha hudhihiri katika nyama hiyo maumbile kamili.

**(3) SOMA NA ILHALI MOLA WAKO NDIYE TU MKARIMU SANA** Tekeleza jambo la kusoma uliloamrishwa. Na Mola wako ambaye amekuamrisha kusoma ndiye mkarimu sana. Miongoni mwa ukarimu wake ni kukuwezesha wewe kusoma ilhali hukuwa ukijua kuandika wala kusoma kilichoandikwa.

**(4) AMBAYE AMEFUNDISHA KWA KALAMU** Mwenyezi Mungu amemfundisha mwanadamu kuandika kwa kalamu. Kalamu ni neema kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwani lau kama si kalamu, dini isingesimama na maisha yasingetengemaa. Mwenyezi Mungu, kwa kalamu, amewatoa watu kutoka katika kiza cha ujinga kwenda kwenye mwangaza wa elimu. Elimu, hekima, habari za watu wa zamani na maneno yao, vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyoteremshwa havikukusanywa, havikuandikwa na kudhibitiwa, ila tu kwa kuandika. Lau wewe ungeutafakari ulimwengu ambao hauna kalamu wala kuandika wala vitabu, basi usingeweza kuona ila ulimwengu ambao ujinga umekita vigingi vyake ndani yake. Haziwezi kuhama ndani ya ulimwengu huo elimu za watu wa zamani, majaribio yao, ufasaha na fikra zao kwenda kwa watu wengine. Pia, hayo hayawezi kuhama kutoka katika mji kwenda mji mwingine ila kwa uchache sana, pamoja na upungufu na upotoshaji. Kisha yatakoma na kwisha kadiri zama zinavyokwenda, na hayatakuwepo kabisa. Ama unapokuwepo uandishi, basi elimu na maarifa ya jamii hubaki na kisha huendelezwa na kuongezeka mpaka kiwango ambacho Mwenyezi Mungu anakitaka. Na kwa hiyo, maendeleo yanakua, fikra zinapanuka, dini zinahifadhiwa na uongofu unasambazwa. Bila shaka, ni kwa ajili hiyo ndio Mwenyezi Mungu Mtukufu, alianzisha mahubiri ya Uislam kwa kuwaita watu kwenye: **1)** Kusoma na kuandika. **2)**Kuwahimiza juu ya hayo. **3)** Kuweka wazi kuwa mawili hayo ni katika alama za uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake na ni rehema yake kwao. **4)** Kuweka wazi kuwa Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ambaye ni Mwarabu asiyeweza kuandika wala kusoma kilichoandikwa, amekuja. Muujiza wake ni Qur'an inayosomwa na kitabu kinachoandikwa na kwamba yeye kwa hayo atauhamisha umma wake kutoka katika hali ya ujinga kwenda kwenye hali ya elimu kwa fani zake zote, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu akidhihirisha neema yake kwa hilo aliposema kuwa:"Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyempeleka, kwa watu ambao hawajui kusoma wala kuandika, Mjumbe miongoni mwao, akiwasomea aya zake na akiwatakasa, na akiwafundisha kitabu na hekima. Kwa hakika, kabla ya hapo walikuwa katika upotevu ulio wazi". *Sura Al-jum'a 62, aya 2.*

**(5) AMEMFUNDISHA MWANADAMU MAMBO AMBAYO HAKUYAJUA** Amemfundisha kwa njia ya kalamu mambo ambayo hakuwa akiyaelewa.

**(6) KWA HAKI,. HAKIKA, MWANAADAMU HUVUKA MIPAKA** Mwanadamu anavuka mipaka na kuonesha kiburi kwa Mola wake.

**(7) KWA VILE KUJIONA AMEJITOSHA** Mwanadamu huvuka mpaka kwa kujiona ametosheka kwa sababu ya mali yake na nguvu zake.

**(8) HAKIKA , NI KWA MOLA WAKOTU MAREJEO** Ni kwa Mwenyezi Mungu tu marejeo si kwa mwengine.

(9) (10) **JE, UMEMUONA AMBAYE ANAMKATAZA MJA PINDI ANAPOSWALI?** Ambaye anakataza ni Abuujahl, na mja (anayekatazwa) ni Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.
(11) **JE, UNAONAJE IKIWA YUKO JUU YA UONGOFU?** Mwenyezi Mungu hapa anamkusudia mja anayekatazwa wakati anaposwali, naye ni Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.
(12) **AU AKIAMRISHA UCHAMUNGU?** Yaani: Au akiamrisha kufanya utakaso, kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kutenda matendo mema, mambo ambayo kwayo mtu hujikinga na moto (wa Jahanamu).
(13) **JE, UNAONAJE IKIWA ATAKADHIBISHA NA AKAKATAA?** Mwenyezi Mungu hapa anamkusudia Abuujahl aliyekadhibisha yale aliyokuja nayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na akakataa kuamini.
(14) **HIVI HAJUI KUWA MWENYEZI MUNGU ANAONA?** Maana ni kwamba: Hivi hajui kuwa Mwenyezi Mungu anazifahamu vyema hali zake zote, na kwahiyo, atamlipa juu ya hayo? Sasa kama ni hivyo, vipi afanye ujasiri wa kufanya hayo aliyothubutu kuyafanya?
(15) **NA AKOME. NINA APA KUWA KAMA HATOKOMA, TUTAMKOKOTA KWA UTOSI WAKE** Yaani: Nina'apa kwa Mwenyezi Mungu kuwa akitokoma na kutoacha hayo aliyonayo, basi tutamshika utosi wake na kumkokota kumpeleka motoni. Utosi (Naaswia) ni nywele za mbele za kichwa.
(16) **UTOSI ULIO MRONGO, WENYE MAKOSA** Mwenye utosi huo ni muongo, mwenye makosa, mzembe wa kufanya madhambi.
(17) **BASI NA AITE WANACHAMA WAKE** Yaani: Awaite watu wa klabu yake. Klabu ni Baraza ambayo watu wanakaa, na ndugu na jamaa wanakusanyika. Maana ni kwamba: Na awaite hao watu wake ili wamsaidie na wamnusuru. Yasemekana kwamba Abuujahl alimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa: "Hivi unanitisha na ilhali mimi, kati ya watu wa jangwa hili, nina Baraza ya watu wengi sana?". Kwa sababu hiyo, ikashuka aya hii.
(18) **TUTAWAITA MAZABANIA** Maana: Tutawaita malaika wakali na wenye nguvu, ili wamkamate na kumtumbukiza katika moto mkali sana.
(19) **HAPANA. USIMTII NA SWALI NA JIKURUBISHE** Usimtii katika jambo la kuacha Swala analokuitia. Swali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, usimjali yeye na usiyajali makatazo yake. Jikurubishe kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kumtii na kumwabudu.

سُورَةُ القَدۡرِ — آياتها ٥ — ترتيبها ٩٧

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ فِي لَيۡلَةِ ٱلۡقَدۡرِ ١ وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا لَيۡلَةُ ٱلۡقَدۡرِ ٢
لَيۡلَةُ ٱلۡقَدۡرِ خَيۡرٞ مِّنۡ أَلۡفِ شَهۡرٖ ٣ تَنَزَّلُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ
فِيهَا بِإِذۡنِ رَبِّهِم مِّن كُلِّ أَمۡرٖ ٤ سَلَٰمٌ هِيَ حَتَّىٰ مَطۡلَعِ ٱلۡفَجۡرِ ٥

سُورَةُ البَيِّنَةِ — آياتها ٨ — ترتيبها ٩٨

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

لَمۡ يَكُنِ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِنۡ أَهۡلِ ٱلۡكِتَٰبِ وَٱلۡمُشۡرِكِينَ مُنفَكِّينَ
حَتَّىٰ تَأۡتِيَهُمُ ٱلۡبَيِّنَةُ ١ رَسُولٞ مِّنَ ٱللَّهِ يَتۡلُواْ صُحُفٗا مُّطَهَّرَةٗ ٢
فِيهَا كُتُبٞ قَيِّمَةٞ ٣ وَمَا تَفَرَّقَ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ إِلَّا مِنۢ
بَعۡدِ مَا جَآءَتۡهُمُ ٱلۡبَيِّنَةُ ٤ وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ
لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ
ٱلۡقَيِّمَةِ ٥ إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِنۡ أَهۡلِ ٱلۡكِتَٰبِ وَٱلۡمُشۡرِكِينَ
فِي نَارِ جَهَنَّمَ خَٰلِدِينَ فِيهَآۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمۡ شَرُّ ٱلۡبَرِيَّةِ ٦ إِنَّ
ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ أُوْلَٰٓئِكَ هُمۡ خَيۡرُ ٱلۡبَرِيَّةِ ٧

# SURATUL QADR (97)

*Ni ya Makka Ina aya tano*

(1) **HAKIKA, SISI TUMEITEREMSHA KATIKA USIKU WA HADHI** Maana ya iliyoteremshwa ni Qur'an. Qur'an iliteremshwa yote kutoka katika Ubao Uliohifadhiwa kuja kwenye mbingu iliyo karibu na dunia katika usiku wenye hadhi kubwa. Qur'an, katika kipindi cha miaka ishirini na tatu, ilikuwa ikishuka kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwa vipande vipande kulingana na mahitaji. Usiku wenye hadhi ni usiku katika usiku wa mwezi wa Ramadhani ambao Qur-an iliteremshwa ndani yake. Hadithi za Mtume zimetofautiana katika kuuainisha usiku huo.
(2) **NI LIPI LILILOKUFAHAMISHA, NI UPI HUO USIKU WA HADHI?** Usiku huo umeitwa " Usiku wa Hadhi" kwa sababu: **1)** Mwenyezi Mungu Mtukufu anakadiria ndani yake mambo anayoyataka mpaka mwaka unaofuata. Pia imesemwa kuwa umeitwa kwa jina hilo kwa sababu ya: **2)** Ukubwa wa hadhi na utukufu wake.
(3) **USIKU WA HADHI NI BORA KULIKO MIEZI ELFU** Maana ni kwamba: Kufanya amali

njema ndani yake, na ilhali usiku huo ni mmoja tu, ni bora kuliko kutenda amali katika miezi elfu.

(4) **HUSHUKA MALAIKA NA ROHO NDANI YAKE KWA IDHINII YA MOLA WAO KWA AJILI YA KILA JAMBO** Malaika wanashuka na kila jambo kutoka mbinguni kuja ardhini. Roho ni Jibril Amani iwe juu yake.

(5) **NI AMANI TUPU USIKU HUO MPAKA KUCHOMOZA KWA ALFAJIRI** Haukuwa usiku huo ila ni salama tu. Usiku wote ni kheri, hamna ubaya ndani yake. Amesema Mujahidi kuwa: "Huo ni usiku ulio salama. Shetani hawezi kufanya ndani yake ubaya wala maudhi yoyote". Na Ash-sha'biy amesema kuwa: "Maana ya amani hiyo ni Malaika kuwaombea amani watu wa misikitini tokea kuzama kwa jua mpaka kuchomoza kwa alfajiri". Hakusiti kushuka kwao kundi baada ya kundi jingine mpaka kuchomoza kwa alfajiri.

# SURATUL-BAYYINA (98)

*Ni ya Makka Ina aya nane*

(1) **WALE AMBAO WAMEKUFURU KATIKA WATU WA KITABU NA WASHIRIKINA HAWATAJINASUA MPAKA IWAJIE HOJA ILIYO WAZI** Watu wa kitabu ni Wayahudi na Wanaswara. Washirikina ni washirikina wa Kiarabu wanaoabudu masanamu. Hoja iliyo wazi ni kila kinachoiweka wazi haki, na maana yake hapa ni: **1)** Qur'an au. **2)** Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.

Maana ya aya ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anaeleza habari za makafiri kwamba wao hawataacha: **1)** Ukafiri wao. **2)** Kumshirikisha kwao Mwenyezi Mungu. **3)** Kutofautiana kwao katika dini mpaka Mwenyezi Mungu awapelekee kile ambacho: **a)** Kitawawekea wazi haki ikawa mbali na batili katika itikadi na dini zao, na. **b)**Kitawawekea wazi upotofu wao na kuwa mbali kwao na usahihi kwa sababu ya: **1)** Muda kuwa mrefu. **2)** Umbali wao na zama za Mitume, na. **3)**Kupotosha vitabu vya mbinguni vilivyokuwa mikononi mwao.

Hoja hiyo iliyo wazi ni Mtume Muhammad pamoja na kitabu alichokuja nacho. Kitabu hicho kimewawekea wazi upotofu na ujinga wao na kuwaita kwenye imani.

(2) **MJUMBE ATOKAYE KWA MWENYEZI MUNGU ANAYESOMA NYARAKA TAKATIFU** Mjumbe mwenyewe ni Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliyewajia akiwa ametumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtume alikuwa anawasomea Qur'an iliyokuwa imeandikwa katika nyaraka hizo. Alikuwa akiwasomea kwa kuhifadhi kwa moyo na sio kwa kusoma maandishi. Nyaraka hizo zimetakaswa na uongo, utata na ukafiri. Bali humo mna haki iliyo wazi, inayowabainishia watu wa kitabu na washirikina kila jambo la dini linalowatatiza. Katika nyaraka hizo, hamna upotoshaji au utata, bali yaliyomo humo ni maneno ya Mwenyezi Mungu ya kweli.

(3) **HUMO MNA MAANDISHI YALIYO NYOOKA** Muradi wa maandishi ni aya na sheria ambazo zimeandikwa humo. Maandishi yaliyo nyooka maana yake ni kwamba maandishi hayo yamenyooka, yamekaa sawasawa, yako madhubuti na hayana kuukwepa ukweli. Bali yote yaliyomo ndani yake ni wema, uogofu na hekima kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa:"Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu ambaye amemteremshia Mja wake kitabu, na hakukifanya kikawa na utenge, kikiwa kimenyooka, ili kitoe onyo la adhabu kali itokayo kwake na kiwape habari njema waumini ambao wanafanya mema kwamba watapata malipo mazuri". *Sura Al-kahf 18, aya 1-2.* Mwenye kuzifuata aya hizo atakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu iliyonyooka.

(4) **NA WALE AMBAO WAMEPEWA KITABU, HAWAKUFARAKANA ILA TU BAADA YA KUJIWA NA HOJA ILIYO WAZI** Maana ni kwamba: Kufarakana na kutofautiana kwao hakukutokana na kutatizwa na mambo, bali kulipatikana baada ya haki na sawa kudhihiri na kuwa wazi. Halafu Mwenyezi Mungu alimpeleka Mtume Muhammad. Sasa Mtume alipopelekwa, walifarakana kuhusu yeye na wakatofautiana. Baadhi yao wakamwamini na wengine wakamkana. Walitakiwa wawe juu ya njia moja ya kufuata dini ya Mwenyezi Mungu na kumfuata Mtume ambaye amewajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu, akiwa anasadikisha yale waliyo nayo.

(5) **NA HAWAKUAMRISHWA ILA TU WAMWABUDU MWENYEZI MUNGU (MMOJA) WAKIMTAKASIA YEYE TU DINI, WAKIZIEPUKA DINI ZOTE POTOFU NA KUELEKEA KWENYE DINI ILIYO SAWA, NA WADUMISHE SALA NA WATOE ZAKA. NA HIYO NDIYO DINI ILIYO NYOOKA** Maana ni kwamba: Hapana vingine isipokuwa kwamba imewajia wao Qur'an kutoka kwa Mwenyezi Mungu ili: **1)** Washikamane na kumwabudu Mwenyezi Mungu. **2)** Ibada zao ziwe safi. **3)** Wasikishirikishe na Mwenyezi Mungu kitu chochote. **4)** Wazifanye nafsi zao ni zenye kutakata katika dini kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. **5)** Waziache dini zote waelekee kwenye Uislamu. **6)** Watekeleze swala katika nyakati zake katika njia ambayo Mwenyezi Mungu anairidhia. **7)** Watoe zaka kwa wanaostahiki kupewa.

جَزَآؤُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ جَنَّٰتُ عَدْنٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ
فِيهَآ أَبَدًا ۖ رَّضِىَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ لِمَنْ خَشِىَ رَبَّهُۥ ﴿٨﴾

## سُورَةُ الزَّلْزَلَةِ

ترتيبها ٩٩ — آياتها ٨

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا زُلْزِلَتِ ٱلْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴿١﴾ وَأَخْرَجَتِ ٱلْأَرْضُ أَثْقَالَهَا
﴿٢﴾ وَقَالَ ٱلْإِنسَٰنُ مَا لَهَا ﴿٣﴾ يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿٤﴾
بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ﴿٥﴾ يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ ٱلنَّاسُ أَشْتَاتًا
لِّيُرَوْا۟ أَعْمَٰلَهُمْ ﴿٦﴾ فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا
يَرَهُۥ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُۥ ﴿٨﴾

## سُورَةُ العَادِيَاتِ

ترتيبها ١٠٠ — آياتها ١١

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلْعَٰدِيَٰتِ ضَبْحًا ﴿١﴾ فَٱلْمُورِيَٰتِ قَدْحًا ﴿٢﴾ فَٱلْمُغِيرَٰتِ صُبْحًا
﴿٣﴾ فَأَثَرْنَ بِهِۦ نَقْعًا ﴿٤﴾ فَوَسَطْنَ بِهِۦ جَمْعًا ﴿٥﴾ إِنَّ ٱلْإِنسَٰنَ
لِرَبِّهِۦ لَكَنُودٌ ﴿٦﴾ وَإِنَّهُۥ عَلَىٰ ذَٰلِكَ لَشَهِيدٌ ﴿٧﴾ وَإِنَّهُۥ لِحُبِّ
ٱلْخَيْرِ لَشَدِيدٌ ﴿٨﴾ ۞ أَفَلَا يَعْلَمُ إِذَا بُعْثِرَ مَا فِى ٱلْقُبُورِ ﴿٩﴾

Haya ambayo wameamrishwa yanahitaji kuungana na kuafikiana, na sio kugombana na kutengana. Kwani Mtume Muhammad amekuja na mfano wa yale ambayo Mitume wengine wameamrishwa kwayo. Dini hiyo ya kuitakasa ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kuacha vile vyote vinavyoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu, kutekeleza swala kwa ajili ya Mwenyezi Mungu katika nyakati zake na kutoa zaka kwa waja wa Mwenyezi Mungu wenye shida, hii ndio dini ya mila iliyonyooka.

(6) **HAKIKA, WALE WALIOKUFURU KATIKA WATU WA KITABU NA WASHRIKINA WATAKUWA KATIKA MOTO WA JAHANAMU WAKIISHI MILELE HUMO. HAO TU NDIO VIUMBE WABAYA** Yaani: Marejeo yao ni motoni, hawatatoka humo na hawatakufa. Wao ni viumbe waovu hivi sasa kwa sababu wameiacha haki kwa husda na kwa dhulma, na kwa hiyo watakuwa viumbe wabaya huko mwisho.

(7) **HAKIKA, WALE AMBAO WAMEAMINI NA KUTENDA MATENDO MEMA, HAO TU NDIO VIUMBE WEMA** Hao ni viumbe wema hivi sasa na baadae.

(8) **MALIPO YAO MBELE YA MOLA WAO NI BUSTANI ZA UKAAZI WA MILELE, INAYOPITA CHINI YAKE MITO WAKIISHI MILELE HUMO. MWENYEZI MUNGU AMEWARIDHIA NA WAO WAMEMRIDHIA. HAYO NI KWA YULE AMBAYE AMEMUOGOPA MOLA WAKE** Malipo yao, kulingana na imani na matendo mema waliyofanya, ni bustani za ukaazi ambazo chini ya miti na nyumba zake inapita mito. Hawatatoka humo, hawatahama na hawatakufa. Bali wao watadumu katika neema zake, wataendelea kuburudika katika ladha zake milele na milele. Neema zao hazina ukomo. Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nao kwa sababu wametii maamrisho yake na kuzikubali sheria zake. Na wao wamemridhia Mwenyezi Mungu kwakuwa, katika mambo waliyokuwa wakiyataka, wamepata mambo ambayo hakuna jicho ambalo limewahi kuyaona, wala hapana sikio ambalo limewahi kuyasikia na wala hayajapita katika fikra za mtu yeyote. Malipo na radhi hizo atazipata yule ambaye kumepatikana kwake kumuogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu hapa duniani, na akaacha kumuasi kwa sababu ya kuogopa huko.

## SURATUZ-ZILZALA (99)

*Ni ya Makka Ina aya nane*

(1) **PINDI ARDHI ITAKAPOTETEMESHWA KUTETEMESHWA KWAKE** Pindi Ardhi itakapotetemeshwa kutetemeshwa kwa nguvu. Kwani itatetemeka mpaka kila kitu kilicho juu yake kivunjike.

(2) **NA ARDHI IKATOA MIZIGO YAKE** Ardhi itatoa nje maiti, vitu mbali mbali vilivyozikwa ndani yake na yote yaliyotendwa juu ya mgongo wake. Amepokea Imam Muslim (Hadithi Na. 1683) na Tirmidhy (Hadithi Na. 2134) na kunakili kutoka kwa Abuuhrairah, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, akisema kuwa: "Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: Itatapika ardhi vipande vya ini lake mfano wa sahani za dhahabu na fedha. Na atakuja muuaji na kusema: Kwa sababu ya hii, niliua. Na atakuja mkataji wa udugu na kusema: Kwa sababu ya hii, nimeukata udugu wangu. Na atakuja mwizi na kusema: Kwa sababu ya hii, ulikatwa mkono wangu. Kisha wataacha na hawatachukua kitu chochote". Ama maiti, ardhi itawatoa katika Mpulizio wa pili.

(3) **NA AKASEMA MWANAADAMU: INA NINI?** Atasema kila mmoja katika watu, kutokana na kufazaishwa na kushtushwa na jambo la Qiyama, kwamba: Ni kwa sababu gani ardhi imetetemeshwa na kutoa nje mizigo yake?

(4) **SIKU HIYO ITASIMULIA HABARI**

**ZAKE** Ardhi itaeleza habari zake na itazizungumza kheri na shari zilizotendwa juu yake. Mwenyezi Mungu ataitamkisha ardhi ili iwe shahidi juu ya waja.

5 **KWA SABABU MOLA AMEIPA WAHYI** Ardhi itazungumza habari zake kwa wahyi (ufunuo) wa Mwenyezi Mungu na kuipa kwake idhini izungumze na ishuhudie.

6 **SIKU HIYO WATU WATATOKA WAKIWA TOFAUTI ILI WAONESHWE MATENDO YAO** Watu watatoka makaburini mwao kwenda mahali pa kuhisabiwa, wakiwa katika hali tofauti. Baadhi yao watakuwa katika amani, na baadhi wengine watakuwa katika hofu. Baadhi yao watakuwa na rangi nyeupe ya watu wa pepo, na baadhi wengine watakuwa na rangi nyeusi ya watu wa motoni. Baadhi yao wataondoka kuelekea upande wa kulia, na baadhi wengine wataelekea upande wa kushoto, pamoja na kugawanyika na kutofautiana kwao katika dini na matendo, ili Mwenyezi Mungu awaoneshe bayana matendo yao. Na imesemwa kuwa: Ili waone malipo ya matendo yao.

7 **BASI ATAKAYETENDA KHERI UZITO WA CHEMBE, ATAIONA** Yaani: Atakayefanya kheri hapa duniani hata iwe ndogo kiasi gani ataiona kheri hiyo Siku ya Qiyama katika kitabu chake, na ataifurahia. Au ataiona kheri kwa macho yake ikiwa imetandazwa mbele yake.

8 **NA ATAKAYETENDA SHARI UZITO WA CHEMBE, ATAIONA** Na vilevile atakayefanya shari hapa duniani hata iwe ndogo kiasi gani, ataiona shari hiyo siku ya Qiyama na itamhuzunisha. Na inawezekana Mwenyezi Mungu akasamehe. Chembe (*Dharra*) ni lile vumbi linaloonekana katika mionzi ya jua. Amesimulia Ibnujariir na Ibnu abii Hatim *(Al-ahaadiith Al-mukhtaara, Hadithi Na. 2243)* wakisema kuwa: "Alisema Abuubakar: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hivi mimi nitaiona shari ya uzito wa chembe niliyotenda? Mtume akasema: Ewe Abubakar, je, umeyaona yale ambayo unayachukia hapa duniani ambayo unayaona? Yakiwa katika viyasi vikubwa vya vitu vidogo katika shari, na utawekewa akiba viyasi vingi vya vitu vidogo katika kheri, mpaka ulipwe siku ya Qiyama.

*Na amesimulia Bukhari (Hadithi Na. 2648) na Muslim (Hadithi Na. 1647)* wakinakili kutoka kwa Abuu Hurairah kwamba: "Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: Farasi ni wa watu watatu: **1)** Kwa mtu ni malipo, na **2)** Kwa mtu ni Sitara, na **3)** Kwa mtu ni madhambi". Isome hadithi hiyo. Na katika hiyo hiyo, amesema (Abuu Huraira kuwa): Aliulizwa (Mtume) kuhusu punda, akasema: Haikuteremshwa juu yangu kuhusu punda isipokuwa tu aya hii ambayo imekusanya maana mengi na ya pekee: "Atakayetenda matendo ambayo ni kiasi cha (uzito wa) kitu kidogo sana kheri ataiona, na atakayetenda matendo yenye kulingana na kiasi cha (uzito wa) kitu kidogo sana shari ataiona".

## SURATUL-AADIYAAT (100)

Ni ya Makka Ina aya kumi na moja

1 **NINA APA KWA WENYE KWENDA MBIO HUKU WANAHEMA** Muradi wa hao wenye kwenda mbio ni farasi, wakiwa na wapandaji wake wanaoipigania dini ya Mwenyezi Mungu, wanaokwenda mbio kuwafuata maadui wa kikafiri wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na imesemwa pia kuwa muradi wake ni ngamia ambao wanakwenda mwendo wa kasi wakiwa wamewachukua mahujaji kutoka Arafa kuelekea Muzdalifah mahali ambapo mahujaji wote wanakusanyika. Kauli ya kwanza ndio sahihi zaidi. Dhabhan (Kwenda mbio) ni aina ya mwendo na ukimbiaji. Amesema Alfarraa'i kuwa: Dhab'han (Kuhema) ni sauti ya pumzi za farasi pindi wanapokwenda mbio.

2 **HALAFU WENYE KUPIGA KWATO ZAO WAKIWASHA MOTO** Hao ni farasi wakati, wakiipiga kwa kwato zao ardhi iliyo ngumu, wanawasha moto na kutoka cheche katika kwato hizo.

3 **KISHA WENYE KUSHAMBULIA GHAFLA ASUBUHI** Ambao wanawashambulia maadui wakati wa asubuhi.

4 **WAKATIFUA VUMBI WAKATI HUO** Vumbii lenyewe ni vumbi ambalo wamelitimua katika uso wa maadui wakati wa vita.

5 **WAKALIINGILIA KATI KUNDI KWA VUMBI HILO** Kutokana na kwenda mbio kwao, wamekuwa katikati ya maadui wakiwa wamekusanyika mahali hapo kwa wingi.

6 **KWA HAKIKA, MWANADAMU NI MKAIDI SANA KWA MOLA WAKE** Mwenye kukaidi ni yule mwenye kukufuru na kuzikana sana neema za mola wake.

7 **NA HAKIKA, YEYE JUU YA HILO NI MWENYE KUSHUHUDIA** Kwa hakika, mwanada mu juu ya ukaidi wake ni shuhuda anayeishuhudia nafsi yake ukanushaji na ukafiri, kwa sababu ya kuonekana dhahiri athari ya ukanushaji huo juu yake.

8 **NA HAKIKA, YEYE KWA KUPENDA MALI NI MWENYE NGUVU** Maana ni kwamba: Kwa hakika, mwanadamu kutokana na kupenda mali ni mwenye nguvu. Anafanya juhudi kubwa katika kutafuta na kuihangaikia

وَحُصِّلَ مَا فِي ٱلصُّدُورِ ﴿١٠﴾ إِنَّ رَبَّهُم بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيرٌۢ ﴿١١﴾

## سُورَةُ القَارِعَةِ

ترتيبها ١٠١ — آياتها ١١

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

ٱلْقَارِعَةُ ﴿١﴾ مَا ٱلْقَارِعَةُ ﴿٢﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا ٱلْقَارِعَةُ
﴿٣﴾ يَوْمَ يَكُونُ ٱلنَّاسُ كَٱلْفَرَاشِ ٱلْمَبْثُوثِ ﴿٤﴾
وَتَكُونُ ٱلْجِبَالُ كَٱلْعِهْنِ ٱلْمَنفُوشِ ﴿٥﴾ فَأَمَّا
مَن ثَقُلَتْ مَوَٰزِينُهُۥ ﴿٦﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ
﴿٧﴾ وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَٰزِينُهُۥ ﴿٨﴾ فَأُمُّهُۥ هَاوِيَةٌ
﴿٩﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا هِيَهْ ﴿١٠﴾ نَارٌ حَامِيَةٌۢ ﴿١١﴾

## سُورَةُ التَّكَاثُرِ

ترتيبها ١٠٢ — آياتها ٨

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

أَلْهَىٰكُمُ ٱلتَّكَاثُرُ ﴿١﴾ حَتَّىٰ زُرْتُمُ ٱلْمَقَابِرَ ﴿٢﴾ كَلَّا سَوْفَ
تَعْلَمُونَ ﴿٣﴾ ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٤﴾ كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ
عِلْمَ ٱلْيَقِينِ ﴿٥﴾ لَتَرَوُنَّ ٱلْجَحِيمَ ﴿٦﴾ ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا
عَيْنَ ٱلْيَقِينِ ﴿٧﴾ ثُمَّ لَتُسْـَٔلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ ٱلنَّعِيمِ ﴿٨﴾

mali na hutoa juhudi zake zote katika hilo.

(9) **HIVI HAJUI WAKATI VITAKAPOFUKULIWA VILIVYO MAKABURINI?** Maiti walio makaburini watafukuliwa, kutafutwa na kutolewa

(10) **NA YAKAPAMBANULIWA YALIYO KATIKA NYOYO** Kheri na shari zilizomo ndani ya nyoyo zitapambanuliwa na kutenganishwa.

(11) **HAKIKA, MOLA WAO SIKU HIYO NI MWENYE KUWAJUA VILIVYO** Maana ni kwamba: Hakika, Mola wa wenye kufufuliwa anawajua vizuri. Jambo lao lolote halijifichi kwake katika siku hiyo na siku nyinginezo. Bali atawalipa siku hiyo. Maana ni kwamba: Iwapo wanalielewa hilo, hakitakiwi kupenda mali kuwashughulishe wasimshukuru Mola wao, kumwabudu na kutenda matendo kwa ajili ya siku ya kufufuliwa.

## SURATUL-QAARIAH (101)

*Ni ya Makka Ina aya kumi na moja*

(1) **KIGONGACHO** *Al-qaariah* (Kigongacho) ni mojawapo ya majina ya Siku ya Qiyama, kwa vile Qiyama kitazigonga nyoyo kwa fazaa, au kitawagonga maadui wa Mwenyezi Mungu kwa adhabu.

(2) **NI NINI KIGONGACHO?** Swali hili lina lengo la kuonesha ukubwa na uzito wa suala la Qiyama. Yaani: Ni kitu gani hicho?

(3) **NA NI NINI KILICHOKUJULISHA, NI NINI KIGONGACHO?** Swali hili ni sisitizo la kuonesha ukubwa wa msukosuko wa Qiyama na tishio lake kubwa. Maana ni kwamba: Na ni kitu gani kilichokujulisha, ni nini hali ya hicho kigongacho?

(4) **SIKU WATU WATAKAPOKUWA KAMA VIPEPEO WALIOSAMBAZWA** Vipepeo ni wadudu maarufu wanaoruka. Pia yasemekana kuwa wanaingia katika neno hilo wadudu wote wanaoruka, kama vile mbu na nzige. Muradi wa waliosambazwa ni waliotawanyika na kuzagaa. Na huu ni ufananisho wa hali ya watu itakavyokuwa wakati wa kutoka kwao makaburini. Watatembea kila upande bila ya muelekeo kutokana na ukubwa wa msukosuko mpaka watakapokusanywa kwenye kisimamo.

(5) **NA MILIMA ITAKAPOKUWA KAMA SUFI ILIYOTIWA NAKSHI** Yaani: Milima itakuwa kama sufi iliyotiwa rangi mbali mbali ambayo imechambuliwa kwa *nadfu* (mashine ndogo ya mkononi) Hii ni kwa sababu milima itapasuka pasuka na kupeperuka, kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika kauli yake isemayo kwamba "Na milima itakapoendeshwa (itakapo peperushwa)", Sura Attakwiir 81, aya 3, na kauli yake "Na milima ikawa rundo la mchanga ulioachana" Sura Al-muzzammil 73, aya14. Kisha Mwenyezi Mungu akazielezea hali za watu kwa jumla na kugawanyika kwao makundi mawili, akasema kwamba:

(6) **BASI AMA YULE AMBAYE MIZANI YAKE ITAKUWA NZITO** Mizani hiyo ni matendo yake mema. Na kilichokusudiwa ni kuwa matendo yake mema yatakuwa mazito na kuuzidi upande wa mizani ya matendo yake maovu.

(7) **BASI HUYO ATAKUWA KATIKA MAISHA YANAYORIDHISHA** Yaani: Atakuwa katika maisha maridhawa atakayoyaridhia atakaye yapata. Neno "maisha" ni tamko lenye kukusanya neema zilizoko Peponi.

(8) **NA AMA YULE AMBAYE MIZANI YAKE ITAKUWA NYEPESI** Yaani: Ama mtu ambaye maovu yake yamekuwa mazito kuliko mema yake, au alikuwa hana mema yanayoweza kuzingatiwa.

(9) **BASI MAMA YAKE NI SHIMO (LA JAHANNAM)** Yaani: Makazi yake ni Jahannamu. Mwenyezi Mungu ameiita Jahanamu "Mama Yake", kwa sababu mtu huyo muovu atakimbilia humo kama mtoto anavyokimbilia kwa mama yake. Na Jahannamu imeitwa "Shimo", kwa sababu mtu huyo muovu atatumbukia humo pamoja na urefu wa kina chake.

(10) **NA NI NINI KILICHOKUJULISHA, NI**

**NINI SHIMO HILO?** Swali hili ni kwa ajili ya kutisha na kuhofisha kwa kubainisha kuwa shimo hilo haliko katika hali ya kawaida iliyo zoelezeka kiasi kwamba uhalisia wake haujulikani.

(11) **NI MOTO MKALI SANA** Joto na uchomaji wake vimefikia kiwango cha juu kabisa.

## SURATU -TTAKAATHUR (102)

*Ni ya Makka Ina aya nane*

*Amepokea Muslim (Hadithi Na. 5258), At-tirmidhyu (Hadithi Na. 2264) na An-nasaaiy (Hadithi Na. 3555)* wakinukulu kutoka kwa Abdallah Bin Ash-shikh-khiir akisesema kuwa: "Nilifika kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, nikamkuta anasoma ***"Al-haakumu t-takaathur"***. Na katika mapokezi mengine, amenukuliwa (Abdallah Bin Ash-shikh-khiir) akisema kuwa: " Nikamkuta (Mtume) ameteremshiwa ***"Al-haakumu t-takaathur"*** na ilhali anasema: Eti mwanadamu anasema: Mali yangu, mali yangu! Kwani wewe (mwanadamu), katika ulivyomiliki, una mali zaidi ya ulivyokwisha kula ukamaliza?".

(1) **UMEKUSHUGHULISHENI WINGI** Yaani: Umekushughulisheni kujifaharisha kwa wingi wa mali na watoto, kushindana na kutoa juhudi nyingi katika kuyatafuta, na mkaacha kumtii Mwenyezi Mungu na kufanya matendo ya Akhera.

(2) **MPAKA MKAYAZURU MAKABURI** Yaani: Mmeshughulika na hayo mpaka kifo kikawafika ilhali mkiwa mmo katika hali hiyo.

(3) **HAPANA. PUNDE MTAJUA** Hili ni kemeo kwao ili waache kuuhangaikia wingi huo, pia ni uzinduzi kuwa wataujua mwisho mbaya wa tendo hilo siku ya Qiyama.

(4) **KISHA HAPANA. PUNDE MTAJUA** Kurudia huku ni kwa ajili ya kutia uzito na kusisitiza.

(5) **HAPANA. LAU KAMA MNGELIJUA UJUZI WA YAKINI** Yaani: Lau kama mngelilijua ujuzi wa yakini jambo mnaloliendea kama mnavyoyajua kwa yakini mambo yenu ya duniani, basi hilo lingelikushughulisheni na mngeacha kutafuta wingi na kujifaharisha, na msingeacha kulishughulikia jambo hilo kubwa la kumtii Mwenyezi Mungu.

(6) **KWA YAKINI, MTAIONA JAHANAMU** Mtauona moto huko akhera.

(7) **KISHA MTAIONA KWA JICHO LA YAKINI** Yaani: Kisha mtauona moto kuuona kwa yakini; kwa macho yenu. Yasemekana kuwa maana ya maelezo haya ni kwamba hii taarifa ya kubaki kwao motoni, kwa maana kuwa uonaji huo ni wa kudumu, unaoendelea.

(8) **KISHA , KWA YAKINI, MTAULIZWA SIKU HIYO KUHUSU NEEMA** Yaani: Mtaulizwa kuhusu neema za hapa duniani ambazo zimekushughulisheni na mkaacha matendo ya Akhera. Na yasemekana kuwa watu wataulizwa kuhusu amani, afya, muda, vyakula na vinywaji vitamu, vinywaji baridi, vivuli vya makazi na neema nyingine zisizokuwa hizo. Amepokea Ibnu-abiy Shaiba *(Musnad Ibn-abii Shaiba, Hadithi Na. 34345)* na Ahmad *(Hadithi Na. 22532)* wakinukulu kutoka kwa Mahmoud Bin Lubaid akisema: kuwa ilipoteremka " UMEKUSHUGHULISHENI WINGI ", Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliisoma (sura hii) mpaka akafika "KISHA MTAULIZWA SIKU HIYO KUHUSU NEEMA". (Swahaba) Walisema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ni neema zipi tutakazoulizwa? Kwani hakuna vingine isipokuwa kwamba (hivyo tulivyo navyo) ni vyeusi viwili; maji na tende, na panga zetu ziko shingoni mwetu, na adui yupo. Ni neema zipi tutaulizwa? (Mtume) Akasema: Mtaulizwa hayo.

Na amepokea Muslim na Watunzi wa vitabu vya Sunna wakinukulu kutoka kwa Abuu Hurairah akisema kuwa: "Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alitoka. Ghafla, akakutana na Abubakar na Omar na kuwauliza: Ni nini kilichokutoeni majumbani mwenu wakati huu? Wakasema: Ni njaa ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mtume akasema: Nina apa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba hicho kilichokutoeni ndicho nami kimenitoa Basi twendeni. Wakaondoka pamoja naye. Walimfuata mtu mmoja katika Answari, lakini hakuwepo nyumbani kwake. Mke (wa Answari huyo) alipomuona Mtume, alimwambia: Karibu. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akasema : Fulani yuko wapi? (Yule mwanamke) Akasema: Amekwenda kututafutia maji. Mara akafika yule Answari, akamtazama Mtume na Swahaba wake wawili na kusema: "Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu. Leo hakuna aliyepata ugeni bora zaidi yangu". Akatoka na kurudi na kole la tende zinazoaanza kuiva (tosa) na akawaambia: Kuleni hizi. Kisha akachukua kisu. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akamwambia: (Kama unakwenda kuchinja) Usichinje mnyama anayenyonyesha. Akawachinjia, wakala mbuzi na lile kole la tende na wakanywa. Waliposhiba na kukata kiu, Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akamwambia Abuubakar na Omar kwamba: Nina apa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba kwa yakini mtaulizwa neema hii Siku ya Qiyama".
*Sahih Muslim, Hadithi Na. 3799. Tirmidhiy, Hadithi Na. 2292.*

## SURATUL-ASRI (103)

*Ni ya Makka Ina aya tatu*

(1) **NINA'APA KWA ALASIRI** Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kwa alasiri ambayo ni muda, kwa sababu ya mazingatio yaliyomo ndani yake kutokana na kupita kwa usiku na mchana kwa mpangilio, kupishana kwa kiza na mwanga na kutengemaa kwa maisha na maslahi ya viumbe hai kunakotoka na hali hiyo. Kwani katika hayo, kuna ushahidi wa wazi unaomtambulisha Mtengeneza (Muumba) Mtukufu na kwamba yeye yu pekee. Muqatil amesema kuwa:"Kilichokusudiwa kwa neno "Alasiri" ni Swala ya Alasiri.

(2) **HAKIKA YA MWANADAMU YUMO KATIKA HASARA** Neno hasara ni upungufu na kupotea kwa rasilimali (mtaji). Maana ni kwamba: Kila mwanadamu katika biashara, mihangaiko na kuutumia umri katika mambo ya dunia yumo katika upungufu na kujitenga na haki mpaka anaondoka duniani. Na hakuna yeyote anayetoka katika hasara hiyo isipokuwa tu wale waliotajwa katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa:

(3) **ISIPOKUWA WALE WALIOAMINI NA WAKATENDA MEMA NA WAKAUSIANA HAKI NA WAKAUSIANA UVUMILIVU** Yaani: Isipokuwa wale ambao wamekusanya kati ya kumwamini Mwenyezi Mungu na kufanya mema. Hao wamo katika faida na si katika hasara, kwa sababu wametenda matendo ya akhera, na mambo ya dunia hayakuwafanya waache mambo ya akhera. Hawa ni kila muumini mwanaume na muumini mwanamke. Pia wakausiana wao kwa wao kushikamana na haki ambayo inawajibika kuisimamia na ambayo ni: **1)** Kumwamini Mwenyezi Mungu. **2)** Kumpwekesha Mwenyezi Mungu. **3)** Kutekeleza na kuzisimamia sheria alizoziweka Mwenyezi Mungu na. **4)** Kujiepusha na yale aliyoyakataza Mwenyezi Mungu.

**Pia wakausiana kushikamana na: 1)**Uvumilivu wa kuacha kumuasi Mwenyezi Mungu Mtukufu. **2)** Uvumilivu wa kutekeleza mambo yake ya faradhi (wajibu). **3)** Uvumilivu juu ya mambo yanayouma ambayo Mwenyezi Mungu ameyakadiria kutokea.

Uvumilivu ni miongoni mwa mambo ya haki. Uvumilivu umetajwa baada ya kutajwa kwa kuusiana na mambo ya haki kwa sababu: **1)**Uvumilivu una hadhi zaidi ya hayo. **2)** Daraja ya uvumilivu iko juu zaidi ya hayo. **3)** Watu wengi wanaosimamia haki hufanyiwa uadui, hivyo uvumilivu unahitajika.

سُورَةُ الْعَصْرِ — ترتيبها ١٠٣ — آياتها ٣

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَٱلۡعَصۡرِ ١ إِنَّ ٱلۡإِنسَٰنَ لَفِي خُسۡرٍ ٢ إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ
وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَتَوَاصَوۡاْ بِٱلۡحَقِّ وَتَوَاصَوۡاْ بِٱلصَّبۡرِ ٣

سُورَةُ الْهُمَزَةِ — ترتيبها ١٠٤ — آياتها ٩

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

وَيۡلٞ لِّكُلِّ هُمَزَةٖ لُّمَزَةٍ ١ ٱلَّذِي جَمَعَ مَالٗا وَعَدَّدَهُۥ ٢
يَحۡسَبُ أَنَّ مَالَهُۥٓ أَخۡلَدَهُۥ ٣ كَلَّاۖ لَيُنۢبَذَنَّ فِي ٱلۡحُطَمَةِ ٤
وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا ٱلۡحُطَمَةُ ٥ نَارُ ٱللَّهِ ٱلۡمُوقَدَةُ ٦ ٱلَّتِي تَطَّلِعُ
عَلَى ٱلۡأَفۡـِٔدَةِ ٧ إِنَّهَا عَلَيۡهِم مُّؤۡصَدَةٞ ٨ فِي عَمَدٖ مُّمَدَّدَةِۭ ٩

سُورَةُ الْفِيلِ — ترتيبها ١٠٥ — آياتها ٥

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

أَلَمۡ تَرَ كَيۡفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصۡحَٰبِ ٱلۡفِيلِ ١ أَلَمۡ يَجۡعَلۡ كَيۡدَهُمۡ
فِي تَضۡلِيلٖ ٢ وَأَرۡسَلَ عَلَيۡهِمۡ طَيۡرًا أَبَابِيلَ ٣ تَرۡمِيهِم
بِحِجَارَةٖ مِّن سِجِّيلٖ ٤ فَجَعَلَهُمۡ كَعَصۡفٖ مَّأۡكُولِۭ ٥

## SURA TUL-HUMAZAH (104)

*Ni ya Makka Ina aya tisa*

(1) **ADHABU NI KWA KILA MTETAJI, MSENGENYAJI** Maana ni kwamba: Fedheha au adhabu au hilaki ni kwa mtetaji. Mtetaji ni yule anayemsengenya mtu ilhali mwenyewe yupo. Na msengenyaji ni yule anayemteta mtu ilhali mwenyewe hayupo. Yasemekana kuwa Alhumazah ni yule anayewaudhi watu anaokaa nao kwa matamshi mabaya, na Allumazah ni yule anayepindisha jicho lake kwa mtu aliyekaa naye na kutoa ishara kwa mkono wake au kichwa au nyusi zake (ikiwa ni ishara ya kiburi,dharau na kejeli).

(2) **AMBAYE AMEKUSANYA MALI NA KUZIHESABU** Huu ni ufafanuzi wa sababu za usengenyaji, utetaji na ukonyezaji wake. Sababu ni kiburi chake kilichotokana na utajiri wake, na kudhani kwake kwamba utajiri wake umempatia ubora na kwa hiyo watu wengine anawaona kuwa duni.

(3) **ANADHANI KUWA MALI YAKE ITAMBAKISHA MILELE** Yaani: Anadhani kuwa mali yake itamuacha hai, atadumu milele na hafi, kwa sababu ya ukubwa wa kiburi chake cha

mali anazochuma. Kamwe hayatafakari yatakayotokea baada ya kufa. Na yasemekana kuwa hiyo ni ishara isiyokuwa ya moja kwa moja kwenye matendo mema na kwamba matendo hayo mema ndiyo yatakayomfanya ayatendaye aishi milele katika maisha ya milele na sio mali.

(4) **SI HIVYO. KWA YAKINI, ATATUPWA KATIKA KIVUNJAVUNJA** Mambo hayako kama anavyodhani. Bali atatupwa yeye na mali yake katika moto unaovunjavunja kila kinachotupwa humo na kukiteketeza.

(5) **NA NI NINI KILICHOKUJULISHA, NI NINI KIVUNJAVUNJA?** Yaani: Ni kitu gani hicho? Kama vile hicho ni kitu kisichofahamika na akili.

(6) **NI MOTO WA MWENYEZI MUNGU ULIOWASHWA** Yaani: Huo ni moto wa Mwenyezi Mungu uliowashwa barabara kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

(7) **AMBAO UNAPANDA JUU YA NYOYO** Yaani: ukali wa Joto lake unafika kwenye nyoyo na kuzifunika. Zimetajwa mahsusi nyoyo pamoja na kuwa moto utaifinika miili yao yote, kwa sababu nyoyoni ndipo mahali palipo na yale malengo potofu, nia chafu na tabia mbaya, kikiwemo kiburi na kuwadharau watu wema.

(8) **MOTO HUO UMEFINIKWA JUU YAO** Yaani: Moto huo umewafinika, wamefungiwa milango yake yote. Hawawezi kutoka humo.

(9) **KATIKA NGUZO NDEFU** Yaani: Watakuwa wamefungwa katika nguzo ndefu. Muqatil amesema kuwa: "Watafungiwa milango kisha milango hiyo itakazwa kwa vigingi vya chuma. awatafunguliwa mlango na haitaingia kwao raha yoyote".

## SURATUL -FIIL (105)

*Ni ya Makka Ina aya tano*

(1) **HIVI HUKUONA NAMNA MOLA WAKO ALIVYOWAFANYA WENYE NDOVU?** Wenye ndovu ni wale watu wa Uhabeshi (Abisynia) waliokusudia kuibomoa Al-Kaaba. Yaani: Kwa yakini umelielewa, ewe Muhammad wewe pamoja na watu wa wakati wako na watakaokuja baada yao, tukio la Wenye Tembo, na jinsi Mwenyezi Mungu alivyowafanya! Wana nini basi hawa jamaa zako hawataki kumwamini Mwenyezi Mungu? Na Wenye Tembo ni Wakristo Wakihabeshi waliotawala Yemen. Walitoka Yemen wakikusudia kuibomoa Al-kaaba. Walipofika Makkah, Mwenyezi Mungu aliwapelekea ndege waliotajwa ndani ya sura hii wakawateketeza. Ilikuwa ni dalili, alama, muujiza. Tukio hilo lilitokea kabla Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, hajapewa utume kwa miaka arobaini. Baadhi ya walioliona tukio hilo, walikuwa wako hai wakati Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, anapewa utume.

(2) **HIVI MWENYEZI MUNGU HAKUZIFANYA NJAMA ZAO KUPOTEA BURE?** Yaani: Je, Mwenyezi Mungu hakuvifanya vitimbi na juhudi zao za kutaka kubomoa *Al-kaaba* na kuvunja hadhi ya watu wake kutofanikiwa na kile walichokusudia mpaka wakashindwa kufika iliko *Al-kaaba* na kushindwa kufikia kukifanya kile walichokusudia? Bali Mwenyezi Mungu aliwateketeza, kama anavyoeleza katika sura hii. Maana ni kwamba: Ikiwa jamaa zako wanayaelewa haya, wana nini basi hawaogopi Mwenyezi Mungu kuwateremshia adhabu yake, ilhali wao wanampinga Mjumbe wake na kitabu chake, na wanawazuia watu kuamini?.

(3) **NA AKAWAPELEKEA NDEGE MAKUNDI KWA MAKUNDI?** Aliwapelekea makundi yaliyosambaa. Makundi hayo ni ya ndege weusi waliotokea upande wa baharini wakiwa makundi kwa makundi. Kila ndege amechukua mawe matatu. Mawili yako miguuni, na moja liko mdomoni mwake. Jiwe hilo haligusi kitu ila linakiteketeza.

(4) **WANAWADONDOSHEA MAWE YA MOTO** Wanachuoni wamesema kuwa hayo ni mawe ya udongo uliofinyangwa kwa moto wa Jahanamu. Katika mawe hayo, yameandikwa majina ya Wenye Ndovu. Linapompata mmoja wao jiwe katika mawe hayo, unamtoka upele. Ukubwa wa jiwe ulikuwa kama ngano na zaidi ya dengu.

(5) **YAKAWAFANYA WAKAWA KAMA MAJANI YALIYOTAFUNWA**. Wakawa kama jani la mmea pale mnyama anapolitafuna na kulitema chini. Na yasemekana kuwa maana ni kwamba: Wakawa kama jani la mmea lililotafunwa na mnyama na kusalia bua.

## SURATU QURAISH (106)

*Sura hii pia huitwa "Suratul-iilaaf"*
*Ni ya Makka Ina aya nne*

(1) **KWA AJILI YA MAZOWEA YA WAQURAISH** Mazoea yenyewe ni kwamba Waquraish ambao ni kabila la Mtume Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, walikuwa wakitoka kwenda katika biashara zao katika kipindi cha kabla ya Uislamu na walikuwa hawashambuliwi kwa sababu Waarabu walikuwa wakisema: Waquraishi ni watu wa nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu (Hivyo haifai kuwadhuru. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu akawaamuru Waquraish wamwabudu yeye tu kwa sababu ya kuzowea kwao kwenda safari hizi mbili (bila ya madhara yoyote), kwani Mwenyezi Mungu ndiye aliyewafanya wazowee misafara hiyo miwili na kuifanya iwe myepesi kwao.

(2) **KUZOWEA KWAO MSAFARA WA KUSI NA KASKAZI** Moja ya misafara hii ilikuwa ni kwenda Yemen katika kipindi cha baridi, kwa vile Yemen ni nchi ya joto. Na msafara mwingine ulikuwa ni kwenda Sham (Syria, Lebanon, Jordan na Palestine) katika kipindi cha joto, kwa vile Sham ni nchi ya baridi. Waquiraish walikuwa wakiishi kwa biashara. Kama si misafara hii miwili, ilikuwa kwao hakuna maisha. Na kama si usalama kwa sababu ya kuishi kwao jirani na nyumba ya Mungu, wasingeliweza kuifanya misafara yao.

(3) **BASI WAMWABUDU MOLA WA NYUMBA HII** Yaani: Kama hawako tayari kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa ajili ya neema zake nyingine, basi wamwabudu kwa ajili ya neema hii maalum iliyotajwa. Nyumba ni Al-kaaba. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajulisha kuwa yeye ndiye Bwana wa nyumba hii, kwa sababu walikuwa na masanamu wanayoyaabudu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu akajitenganisha na masanamu hayo. Kwa sababu ya Al-kaaba, Waquraish wamepata heshima kuliko Waarabu wengine.

(4) **AMBAYE AMEWAPA CHAKULA KUTOKANA NA NJAA NA AKAWASALIMISHA NA HOFU** Yaani: Kwa misafara hii miwili, amewapa chakula na kuwaokoa kutoka kwenye njaa kali waliyokuwa nayo kabla ya misafara hii. Waarabu walikuwa wanashambuliana na kutekana. Lakini Waquraish walisalimika na hali hiyo kwa heshima ya Msikiti Mtukufu. Pia Mwenyezi Mungu alikwishawasalimisha na hofu ya Wahabeshi waliokuwa na tembo.

## SURATUL-MAA'UUN (107)

*Pia yaitwa "Suratuddiin"*
*Ni ya Makka Ina aya saba*

(1) **JE, UMEMUONA AMBAYE ANAKANUSHA DINI?** Yaani: Je, umemuona anayekanusha hesabu na malipo (ya Akhera)?

(2) **BASI HUYO NI YULE ANAYEMSUKUMA YATIMA** Yaani: Ukimtafakari au ukimtafuta, basi huyo ni yule anayemsukuma kwa nguvu yatima akamkosesha haki yake. Katika mila za Waarabu wa wakati kabla ya Uislam walikuwa hawawapi mirathi wanawake na watoto.

(3) **NA HAHIMIZI KUMPA CHAKULA MASIKINI** Yaani: Hajihimizi yeye mwenyewe wala familia yake wala watu wengine kufanya hivyo, kwa sababu ya ubahili wa mali.

(4) **BASI ADHABU KALI ITAWAPATA WENYE KUSWALI**

(5) **AMBAO SWALA ZAO WANAZIPUUZA** Wanaopuuza: Hawana habari na sala, hawaijali. Wanaposwali, hawatarajii thawabu kwa kuswali kwao, na wanapoacha kuswali hawaogopi

سُورَةُ قُرَيْشٍ — ترتيبها ١٠٦ — آياتها ٤

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

لِإِيلَٰفِ قُرَيْشٍ ﴿١﴾ إِۦلَٰفِهِمْ رِحْلَةَ ٱلشِّتَآءِ وَٱلصَّيْفِ
﴿٢﴾ فَلْيَعْبُدُوا۟ رَبَّ هَٰذَا ٱلْبَيْتِ ﴿٣﴾ ٱلَّذِىٓ أَطْعَمَهُم
مِّن جُوعٍ وَءَامَنَهُم مِّنْ خَوْفٍۭ ﴿٤﴾

سُورَةُ المَاعُونِ — ترتيبها ١٠٧ — آياتها ٧

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

أَرَءَيْتَ ٱلَّذِى يُكَذِّبُ بِٱلدِّينِ ﴿١﴾ فَذَٰلِكَ ٱلَّذِى
يَدُعُّ ٱلْيَتِيمَ ﴿٢﴾ وَلَا يَحُضُّ عَلَىٰ طَعَامِ ٱلْمِسْكِينِ ﴿٣﴾
فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ
﴿٥﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ يُرَآءُونَ ﴿٦﴾ وَيَمْنَعُونَ ٱلْمَاعُونَ ﴿٧﴾

سُورَةُ الكَوْثَرِ — ترتيبها ١٠٨ — آياتها ٣

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِنَّآ أَعْطَيْنَٰكَ ٱلْكَوْثَرَ ﴿١﴾ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ﴿٢﴾
إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلْأَبْتَرُ ﴿٣﴾

adhabu. Kwa hiyo, wao huipuuza swala mpaka wakati wake ukatoka. Wanapokuwa pamoja na waumini wanaswali ili waonekane kuwa nao wanaswali, na kama hawako pamoja na waumini, basi hawaswali kabisa.

(6) **AMBAO WAO WANAJIONESHA** Yaani: Wanawaonesha watu Swala zao wanaposwali, au wanawaonesha watu kila matendo mema wanayoyafanya ili watu wawasifie.

(7) **NA WANAZUIA MAAUUN** *Maauun* ni jina la kila kitu wanachoazimishana watu kati yao, kama vile ndoo, jembe na chungu. Pia ni jina la kila kitu kisichonyimwa, kama vile maji na chumvi. asemekana pia kuwa Maauun ni Zaka. Yaani: Wanazuia zaka za mali zao.

## SURATUL-KAUTHAR (108)

*Ni ya Makka Ina aya tatu*

(1) **KWA YAKINI, SISI TUMEKUPA KAUTHAR** *Kauthar* ni mto ulioko Peponi. Mwenyezi Mungu ameufanya mto huo kuwa ni takrima kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na umma wake. Amepokea *Imam Ahmad (Hadithi Na. 11558) na Muslim (Hadithi Na. 607)* wakinukuu kutoka kwa

Anas akisema kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema: "Je, mnajua ni nini Kauthar? (Swahaba) Wakasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wanaojua zaidi. (Mtume) Akasema: Huo ni mto alionipa Mola wangu Peponi. Juu ya mto huo kuna kheri nyingi. Umma wangu utakunywa katika mto huo siku ya Qiyama. Vyombo vyake ni kama idadi ya nyota. Atakuja fukuzwa mtoni hapo mja miongoni mwa umma wangu, na kwa hiyo nitasema: Ewe Mola wangu, yule ni miongoni mwa umma wangu. (Mwenyezi Mungu) Atasema: Hujui alichokizusha (katika dini) baada yako". *Kauthar* katika Lugha ya Kiarabu ni kheri nyingi iliyofikia kilele cha wingi. Na yasemekana kuwa *Kauthar* ni Qur'an. Pia yasemekana kuwa *Kauthar* ni wingi wa wenzi (marafiki) na umma.

(2) **BASI SWALI KWA AJILI YA MOLA WAKO NA CHINJA (KWA AJILI YAKE)** Kilichoamriwa ni kudumisha Swala za wajibu. Walikuwepo watu waliokuwa wanaswali na kuchinja lakini sio kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu akamuamuru Mtume wake, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba kuswali na kuchinja kwake kuwe kw ajili yake. Qatada, Atwaa na Ikrima wemesema kuwa muradi (wa kuswali kulikotajwa katika aya hii ) ni (kuswali) Swala ya Idd na kuchinja Udh-hiya.(Udh-hiya ni mnyama anayechinjwa katika kipindi cha Idd El-hajj).

(3) **KWA YAKINI, ATAKAYEKUBUGHUDHI NDIYE TU ALIYEKATIKIWA** Yaani: Atakayekubughudhi, basi huyo ndiye aliyekatikiwa na kheri za Dunia na Akhera, au huyo ndiye ambaye jina lake halitabaki baada ya kufa kwake. Aliyekatikiwa katika wanaume ni mtu asiyekuwa na mtoto. Mtoto wa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipofariki mmoja katika makafiri alisema: "Muhammad amekatikiwa". Kwa ajili hiyo, ikateremka sura hii.

## SURA AL-KAAFIRUUN (109)

*Ni ya Makka Aya zake ni sita*

Imethibiti kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliisoma sura hii *(Al-kaafiruun)* na *Qulhuwal-llahu Ahad (Al-ikhlaas)* katika: **1)** Rakaa mbili za Twawafu (kuzunguka Al-kaaba wakati wa ibada ya Hija na Umra -*Tirmidhiy, Hadithi Na. 797).* **2)**Rakaa mbili za (sunna ya kabla ya sala ya) Alfajiri. *(Sahih Muslim, Hadithi Na. 1195).* **3)**Rakaa mbili (za sunna ya ) baada ya (sala ya) Magharibi. *(An-nasai, Hadithi Na. 982).*

Pia Mtume alikuwa anaswali swala ya Witri kwa kusoma *Sabbih*(Sura Al-aalaa 87 katika rakaa ya kwanza), na *Qul-yaa ay-yuhal- kaafiruun* (sura Al-kaafiruun109 katika rakaa ya pili), na *Qul-huwal-laahu Ahad* (sura Al-ikhlaas 112) katika rakaa ya pekee ya mwisho. *(Tirmidhiy, Hadithi Na. 424).*

(1) **SEMA: ENYI MAKAFIRI** Sababu ya kuteremka kwa sura hii ni kwamba makafiri walimtaka Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aabudu miungu wao (masanamu) kwa muda wa mwaka mmoja, na wao wamuabudu Mungu wake mwaka mmoja. Mwenyezi Mungu Mtukufu akamuamuru Mtume wake awambie kuwa:

(2) **SIABUDU MNACHOKIABUDU** Yaani: Sitafanya mnachotaka nikifanye; cha kuabudu masanamu mnayoyaabudu. Yaani: Hivi sasa siabudu miungu wenu.

(3) **NA NINYI SI WENYE KUABUDU NINACHOKIABUDU** Yaani: Na nyinyi, madamu mmo katika ushirikina na ukafiri wenu, hamumuabudu Mwenyezi Mungu ninayemuabudu.

(4) **NA MIMI SI MWENYE KUABUDU MNACHOKIABUDU** Yaani: Siku zangu za baadae na umri wangu ujao sitaabudu chochote katika Miungu wenu mnaowaabudu.

(5) **NA NYINYI SI WENYE KUABUDU NINACHOABUDU** Yaani: Katika siku zenu za baadae hamtamwabudu Mwenyezi Mungu madamu mmo katika ukafiri wenu na kuabudu kwenu masanamu, kwa sababu ibada ya mtu mwenye kumkufuru na kumshirikisha Mwenyezi Mungu haikubaliki na haitambuliwi. Na yasemekana kuwa ndani ya sura hii kuna kurudiarudia, lengo likiwa ni kuzikata tamaa za makafiri kuwa Mtume atawakubalia ombi walilomuomba la yeye aabudu Miungu wao.

(6) **MNA DINI YENU NA NINA DINI YANGU** Yaani: Ikiwa mko radhi na dini yenu, basi na mimi niko radhi na dini yangu. Dini yenu ambayo ni ushirikina ni yenu nyinyi, haivuki ikafika kwangu, na dini yangu ambayo ni ya *Tawhiid* (kumwabudu Mwenyezi Mungu mmoja) ni yangu mimi, hainikiuki ikapatikana kwenu.

## SURATUN-NASR (110)

*Pia sura hii inaitwa Suratit-taudii'*
*Ni ya Makka Aya zake ni tatu*

Amepokea Imam Ahmad na Ibn-jariir wakinukuu kutoka kwa Ibni-Abbaas akisema kuwa Ilipoteremka *"Idhaa Jaa-a Nasrul-llaahi Walfat-hu"*, Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alisema: "Nimetangaziwa kifo changu". *Ahmad, Hadithi Na. 1777. Ibn-jariir At-tabariy, Juzuu 30, Uk. 334.*

(1) **ITAKAPOKUJA NUSRA YA MWENYEZI MUNGU NA UKOMBOZI** Yaani: Itapokufikia, ewe Muhammad, nusra ya Mwenyezi Mungu dhidi

ya Waquraish wanaokufanyia uadui na akakufungulia (akakukombolea mji wa) Makkah. Nusra ni msaada ambao kwao kunapatikana kuwazidi, kuwashinda na kuwatawala maadui. Ufunguzi (ukombozi) ni ufunguzi wa makazi ya maadui, kuingia majumbani mwao na kuzifungua nyoyo zao ili ziikubali haki.

(2) **NA UKAWAONA WATU WANAINGIA KATIKA DINI YA MWENYEZI MUNGU MAKUNDI KWA MAKUNDI** Yaani: Ukawaona watu, Waarabu na wasiokuwa Waarabu, wanaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu aliyokutuma kwayo, wakiwa makundi kwa makundi. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipoingia Makka, Waarabu walisema: "Kwakuwa Muhammad ameweza kuwashinda watu wa Mji Mtukufu (Makka) na ilhali Mwenyezi Mungu aliwalinda dhidi ya Watu wa Tembo, basi ni kweli yuko katika haki, na wala hamtamuweza". Kwa sababu hiyo, Waarabu wakawa wanaingia katika Uislamu makundi mengi, badala ya kuwa wanaingia mmoja mmoja na wawili wawili. Pia ikawa kabila zima linaingia katika Uislamu.

(3) **BASI MTAKASE MOLA WAKO KWA KUMSHUKURU NA MUOMBE MSAMAHA. KWA YAKINI, YEYE NI MWINGI WA KUKUBALI TOBA** Katika maelezo haya kuna kukusanya kati ya kumtakasa Mwenyezi Mungu kunakoruhusu kuyastaajabu mambo ambayo Mwenyezi Mungu amemrahisishia Mtume Muhammad na ambayo hakuyatazamia yeye wala mtu mwengine yeyote, na kati ya kumshukuru Mola wake juu ya jambo zuri alilomfanyia, neema kubwa aliyomneemesha kwa kumpa nusra na ukombozi wa Mama wa Miji (Makka). Muombe msamaha: Maana yake ni: Muombe msamaha kwa makosa yako, ikiwa ni kuonesha unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu na kuonesha kasoro za matendo yako. Yeye ni Mwingi wa kukubali toba: Yaani: Mwenyezi Mungu ni sifa yake kuwasamehe wanaomuomba msamaha. Anakubali toba zao na kuwarehemu kwa kukubali toba zao hizo. Amepokea Imam Bukhari na maimamu wengine wakinukuu kutoka kwa Ibn-Abbas akisema kuwa: "Omar Bin Alkhat-twaab alikuwa ananiingiza (katika baraza nikae) pamoja na wazee walioshiriki vita vya Badri. Baadhi yao wakawa hawaridhiki. Siku moja akawaita, na akaniingiza pamoja nao. Ibn-Abbas akasema: "Sikudhani isipokuwa tu kwamba Omar siku hiyo aliniita nijumuike nao ili awaoneshe (jambo)". Akasema Omar: "Mnasemaje kuhusu neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu "ITAKAPOKUJA NUSRA YA MWENYEZI MUNGU NA UKOMBOZI"? Baadhi yao walisema: "Mwenyezi Mungu ametuamuru

سُورَةُ الكَافِرُونَ
ترتيبها ١٠٩ — آياتها ٦

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ يَٰٓأَيُّهَا ٱلْكَٰفِرُونَ ١ لَآ أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ٢
وَلَآ أَنتُمْ عَٰبِدُونَ مَآ أَعْبُدُ ٣ وَلَآ أَنَا۠ عَابِدٌ مَّا عَبَدتُّمْ ٤
وَلَآ أَنتُمْ عَٰبِدُونَ مَآ أَعْبُدُ ٥ لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ٦

سُورَةُ النَّصْرِ
ترتيبها ١١٠ — آياتها ٣

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

إِذَا جَآءَ نَصْرُ ٱللَّهِ وَٱلْفَتْحُ ١ وَرَأَيْتَ ٱلنَّاسَ
يَدْخُلُونَ فِى دِينِ ٱللَّهِ أَفْوَاجًا ٢ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ
وَٱسْتَغْفِرْهُ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ تَوَّابًۢا ٣

سُورَةُ المَسَدِ
ترتيبها ١١١ — آياتها ٥

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ١ مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُۥ وَمَا
كَسَبَ ٢ سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ٣ وَٱمْرَأَتُهُۥ
حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ٤ فِى جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍۭ ٥

anapotunusuru na kutufungulia, tumshukuru na tumuombe msamaha". Wengine wakanyamaza na hawakusema kitu. Omar akaniuliza: Je, na wewe Ibn-abbas unasema hivyo hivyo? Nikasema: Hapana. Omar akasema: Unasemaje? Nikasema: Hicho ni kifo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amemjulisha Mtume wake kifo hicho akasema "ITAKAPOKUJA NUSRA YA MWENYEZI MUNGU NA UKOMBOZI". Kwa hiyo, hiyo ni alama ya kwisha kwa umri wako "BASI MTAKASE MOLA WAKO KWA KUMSHUKURU NA MUOMBE MSAMAHA. KWA YAKINI, YEYE NI MWINGI WA KUKUBALI TOBA". Omar akasema: Hakuna ninachokifahamu katika sura hiyo isipokuwa tu hayo unayoyasema". *Bukhariy, Hadithi Na. 4588.*

# SURATUL- MASAD (111)

*Ni ya Makka Aya zake ni tano*

(1) **IMEANGAMIA MIKONO YA ABII-LAHAB NA AMEANGAMIA** Yaani: Imehiliki mikono yake, imekhasirika na kutoka patupu, na yeye mwenyewe amehiliki. Yaani: Kile alichokiomba kimemuangukia mwenyewe. Abu-Lahabi ni Ami (ndugu wa kiume wa baba) yake

Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na jina lake ni Abdul-uzza.

(2) **MALI YAKE NA VITU ALIVYOVICHUMA HAVITAMKINGA** Yaani: Mali alizokusanya, cheo na faida alizopata hazitamkinga na maangamizi na adhabu ya Mwenyezi Mungu itakayomkumba na kumshukia.

(3) **ATAUINGIA MOTO WENYE MIALI** Yaani: Punde tu ataadhibiwa katika moto unaobimbirika, utakaounguza ngozi yake. Moto huo unawaka mno, nao ni moto wa Jahannamu.

(4) **NA MKEWE MWENYE ALIKUWA AKIBEBA KUNI** Yaani: Na mkewe pia atauingia moto unaowaka. Mkewe ni Ummu-jamiil Binti Harbi dada wa Abu-sufiyani. Ummu-jamiil alikuwa akibeba miba na kuitupa usiku kwenye njia apitayo Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.

(5) **SHINGONI MWAKE KUNA KAMBA YA SUMBA** Sumba ni ndifu ambayo hutengezwa kwayo kamba. Ummu-jamiil alikuwa na kidani cha madini ya fahari, akasema: "Nina apa kwa Lata na Uzza (masanamu ya makafiri wa Makka) kuwa kwa yakini kabisa nitakitoa kidani hiki katika kumfanyia uadui Muhammad". Kwa hiyo,hilo litakuwa ni adhabu mwilini mwake Siku ya Qiyama.

## SURATUL-IKHLAAS (112)

*Ni ya Makka Aya zake ni nne*

Amepokea Imam Ahmad, Bukhari na maimamu wengine katika Hadithi aliyoisimulia Abu-Saiidi akisema kuwa: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema kuwaambia Swahaba wake kwamba: Hivi mmoja wenu anashindwa kusoma theluthi ya Qur'ani ndani ya usiku mmoja? Hilo likawa gumu kwao na wakasema: Ni yupi miongoni mwetu anayeweza hilo? (Mtume)Akasema: "Qul-huwal-laahu ahad (*Sura Al-ilhlaas*) " ni theluthi ya Qur'ani". *Ameipokea Hadithi hii:* **1.***Bukhariy, Hadithi Na. 4627* **2.***Muslim, Hadithi Na. 1344* **3.***Tirmidhiy, Hadithi Na. 2821*

(1) **SEMA: ILIVYO NI KWAMBA ALLAH NI WA PEKEE** Washrikina walisema (kumwambia Mtume) Muhammad kuwa: "Ewe Muhammad, tutajie nasaba ya Mungu wako", ikateremka sura hii. Kwa hiyo, maana ni kwamba: Kama mnataka kuwekewa bayana nasaba yake basi yeye ni Mwenyezi Mungu wa pekee.Yaani ni mmoja, asiye na mshirika.

(2) **MWENYEZI MUNGU TU NDIYE MKUSUDIWA** Mkusudiwa ni yule anayekusudiwa katika shida. Yaani: Anakusudiwa kwa vile ni mwenye uwezo wa kuzitatua shida hizo. Imepokewa kutoka kwa Ibni-abbas akisema kuwa: Mkusudiwa ni Bwana aliyekamilika katika ubwana wake,
Mtukufu ambaye amekamilika katika utukufu wake, Muadhama ambaye amekamilika katika uadhama wake,
Mpole ambaye amekamilika katika upole wake,
Tajiri ambaye amekamilika katika utajiri wake, Shupavu ambaye amekamilika katika ushupavu wake, Mjuzi ambaye amekamilika katika ujuzi wake na Mwenye hekima ambaye amekamilika katika hekima zake.
Mwenye sifa hizo ni Mwenyezi Mungu Mtakatifu. Hizi ni sifa ambazo hakuna anayezistahiki ila yeye tu asiyekuwa na mfano. Amesema Azzajjaj kuwa: Mkusudiwa ni Bwana ambaye ni kilele cha ubwana, hakuna Bwana zaidi yake.

(3) **HAKUZAA NA HAKUZALIWA** Yaani: Kwake hakutoka mtoto, na yeye hakutokea kwenye chochote, kwa sababu: **1)** Yeye hafanani na chochote. **2)** Ni muhali kunasibisha kwake "kutokuwepo" wakati uliopita na ujao. Kwa sababu, mwenye kuzaliwa alikuwa hayupo kabla hajazaliwa. Yaani: Mwenyezi Mungu Mtukufu hana baba hata anasibishwe kwa baba huyo, na hana watoto hata wanasibishwe kwake. Qatada amesema kuwa: "Washirikina wa Kiarabu walisema kuwa: Malaika ni mabinti wa Mwenyezi Mungu *(Qur'ani, sura 16, aya 57. Sura 37, aya 149).* Na Wayahudi walisema kuwa: Uzeri ni Mwana wa Mwenyezi Mungu (*Qur'ani, sura 9, aya 30*). Na Wakristo wamesema kuwa: Masihi ni Mwana wa Mwenyezi Mungu *(Qur'ani, sura 9, aya 30).* Mwenyezi Mungu akawaambia (wote hao) kuwa ni warongo, akasema: "Hakuzaa na Hakuzaliwa".

(4) **NA HAKUNA YEYOTE ALIYE MFANAO WAKE** Hakuna yeyote aliye sawa na yeye na kufanana naye , na hakuna anayeshirikiana naye katika chochote.

## SURATUL - FALAQ (113)

*Ni ya Makka Aya zake ni tano*

Amepokea Imam Al-baihaqiy na Tirmidhy na kusema kuwa mapokezi haya yako katika daraja la "Hasan" wakinukulu kutoka kwa Abu-said Al-khudriy akisema kuwa: "Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa akiomba kinga ya jicho la husda la majini na jicho la husda la watu. Ziliposhuka sura mbili za kinga, alikamatana nazo na kuacha yasiyokuwa hayo". Naye Imam Malik katika kitabu chake *"Muwat-ta'"* amemnukuu Aisha akisema kuwa: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alipokuwa akiumwa, alikuwa anajisomea sura mbili za kujilinda na kujipulizia. Ugonjwa wake ulipozidi, nikawa ninamsomea na ninamfutafuta kwa mkono wake, ili kutaraji baraka zake".

(1) **SEMA: NINAOMBA KINGA KWA BWANA WA AL-FALAQ** Alfalaq ni asubuhi, kwa sababu usiku unatanzuka kwa asubuhi. Na yasemekana kuwa Alfalaq ni kila kilichotokana na

سُورَةُ الإِخْلَاص — آياتها ٤ — ترتيبها ١١٢

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ
وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾

سُورَةُ الفَلَق — آياتها ٥ — ترتيبها ١١٣

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ﴿١﴾ مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ﴿٢﴾ وَمِن
شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ﴿٣﴾ وَمِن شَرِّ ٱلنَّفَّٰثَٰتِ فِى
ٱلْعُقَدِ ﴿٤﴾ وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ﴿٥﴾

سُورَةُ النَّاس — آياتها ٦ — ترتيبها ١١٤

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ﴿١﴾ مَلِكِ ٱلنَّاسِ ﴿٢﴾ إِلَٰهِ
ٱلنَّاسِ ﴿٣﴾ مِن شَرِّ ٱلْوَسْوَاسِ ٱلْخَنَّاسِ ﴿٤﴾ ٱلَّذِى
يُوَسْوِسُ فِى صُدُورِ ٱلنَّاسِ ﴿٥﴾
مِنَ ٱلْجِنَّةِ وَٱلنَّاسِ ﴿٦﴾

vitu vyote alivyoviumba Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama vile wanyama, asubuhi, nafaka, kokwa na kila kitu; iwe ni mmea au kinginecho. Yasemekana pia kuwa: Muradi ni kuashiria kwamba yule aliye na uwezo wa kuondoa kiza hiki kinene akakiondoa katika ulimwengu wote, basi ana uwezo wa kumuondolea anayetaka kinga kwake yale yote anayoyaogopa na kuyahofu.

(2) **KUTOKANA NA SHARI YA VITU ALIVYOUMBA** Yaani: Ninataka hifadhi kwa Mwenyezi Mungu anikinge na shari ya viumbe vyake vyote alivyoviumba.

(3) **NA KUTOKANA NA SHARI YA USIKU UNAPOINGIA** Yaani: Sema: Na ninaomba hifadhi kwake anikinge na shari ya usiku unapoingia. Wanazuoni wamesema kuwa hii ni kwa sababu usiku ndio wakati wanyama wakali wanatoka mafichoni mwao, wadudu wanaotambaa wanatoka mle walimo, watu waovu wanachangamka kufanya uovu na uhalifu. Na yasemekana kuwa Ghaasiq ni mwezi unapochomoza.

(4) **NA SHARI YA WANAWAKE WANAOTABANA KATIKA MAFUNDO** Yaani: Na ninaomba kinga ya shari ya wanawake wachawi. Hiyo ni kwa vile wanawake hao walikuwa wanapulizia katika mafundo ya nyuzi wanaporoga kwa kutumia nyuzi hizo.

(5) **NA SHARI YA HASIDI ANAPOFANYA HUSUDA** Husuda maana yake ni mtu kutamani kuondoka neema ambazo Mwenyezi Mungu amezineemesha kwa mwenzie anayemfanyiwa husuda.

## SURATUN-NAAS (114)

*Ni ya Makka Aya zake ni sita*

(1) **SEMA: NINAOMBA KINGA KWA BWANA WA WATU** Bwana wa watu ni Mwenyezi Mungu, Muumba wao, Mpangaji mambo yao na Mtengenezaji hali zao.

(2) **MFALME WA WATU** Ana ufalme uliokamilika na utawala wenye nguvu.

(3) **MOLA WA WATU** Yaani: Muabudiwa wao, kwa sababu mfalme anaweza kuwa Mungu; na anaweza asiwe Mungu. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu akabainisha kuwa jina la Mungu linamuhusu yeye tu, hakuna yeyote anayeshirikiana naye katika jina hilo.

(4) **KUTOKANA NA SHARI YA MWENYE WASIWASI, MWINGI WA KURUDI NYUMA** Mwenye wasiwasi ni shetani. Yaani: Ndiye mwenye wasiwasi. Mwingi wa kurudi nyuma: Kila anapotajwa Mwenyezi Mungu, shetani anarudi nyuma na ananywea. Na asipotajwa Mwenyezi Mungu, anajitanua juu ya moyo.

(5) **AMBAYE ANATIA WASIWASI KATIKA NYOYO ZA WATU** Kutia wasiwasi kwa shetani ni wito wake wa kutaka watu wamtii, wito anaoutoa kwa sauti iliyojificha, ifikayo ndani ya nyoyo bila ya kusikika sauti. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akafafanua kuwa wanaotia wasiwasi wako namna mbili; ni majini na wanadamu, akasema:

(6) **KATIKA MAJINI NA WATU** Ama shetani jini, yeye anatia wasiwasi katika vifua vya watu, kama ilivyotangulia kuelezwa. Ama shetani binaadamu, wasiwasi wake katika nyoyo za watu ni kwamba yeye anajionesha kama mtoa nasaha mwenye huruma. Kwa hiyo, kutokana na maneno yake aliyoyatoa kwa mtindo wa nasaha, anaingiza katika moyo yale yale anayoyainigiza shetani jini katika moyo kwa kutia wasiwasi wake.

Na yasemekana kuwa Ibilisi anatia wasiwasi katika nyoyo za majini kama anavyotia wasiwasi katika nyoyo za wanaadamu. Imepokewa kutoka kwa Ibni-Abbas akisema kuwa: "Hakuna yeyote aliyezaliwa isipokuwa kwamba juu ya moyo wake kuna shetani. Anapomkumbuka Mwenyezi Mungu, shetani anarudi nyuma, na anaposahau, shetani anatia wasiwasi". *Bukhariy, Kitaab Tafsiir Qur'an.*

*Tunamuomba Mwenyezi Mungu atukinge na hila za shetani na wasiwasi wake.*

# MASWALI MUHIMU KATIKA MAISHA YA MWISLAMU

**1. Je, Mwislamu anachukua wapi itikadi yake?** Mwislamu anachukua itikadi yake katika kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na Sunna sahihi za Mtume wake ambaye hatamki kutokana na mapenzi ya nafsi. ***"Hayakuwa hayo (ayatamkayo) isipokuwa tu ni Wahyi unaofunuliwa"***. **Sura An-najm (53), aya 4.** Uchukuaji huo unatakiwa uwe kwa mujibu wa walivyofahamu Swahaba na Wema Waliotangulia (Assalaf Asswaalih), Mwenyezi Mungu awawiye radhi.

**2. Endapo tutatofautiana, tunarejea kwenye ni nini?** Tunarejea kwenye sheria tukufu. Hukumu katika hilo ni kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Ikiwa mtazozana katika jambo, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)"***. **Sura An-nisaa (4), aya 59.** Naye Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Nimeacha kwenu mambo mawili. Hamtapotea madamu mmekamatana nayo: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake"*. **Muwatta'i.**

**3. Ni lipi kundi litakalo okoka Siku ya Kiyama?** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "**...***na umma wangu utagawanyika katika mila sabini na tatu. Wote watakuwa katika moto, isipokuwa (watu wa) kundi moja tu. (Swahaba) Waliuliza: Na ni nani kundi hilo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mtume alisema: Ni ile mila niliyonayo mimi na Swahaba wangu"* **Ahmad.** Haki ni yale mambo aliyokuwa nayo Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na Swahaba wake. Kwa hiyo, jilazimishe kufuata na jiepushe kuzusha kama unataka kupona na kukubaliwa amali (zako).

**4. Ni yapi masharti ya kukubaliwa kwa matendo mema?** Masharti yake ni haya: **1)** Kumwamini Mwenyezi Mungu na kumpwekesha. Haikubaliwi amali kwa mshirikina. **2)** Ikhlaas; kwa maana ya kukusudiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa hayo matendo mema yafanywayo. **3)** Kumuiga Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika mema hayo; kwa maana ya kuwa yawe yanaafikiana na yale aliyoyaleta. Kwa hiyo, haabudiwi Mwenyezi Mungu isipokuwa tu kwa yale aliyoyaweka Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). Endapo amali itakosa mojawapo ya masharti hayo, basi itarudishwa (haikubaliwi). Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Na tutaiendea amali yoyote ile waliyotenda na tutaifanya (iwe) vumbi lililo peperushwa"***. **Sura Al-furqaan (25), aya 23.**

**5. Daraja za dini ni ngapi?** Daraja za dini ni tatu: **1)** Uislamu **2)** Imani **3)** Ihsaan.

**6. Uislamu ni nini, na nguzo zake ni ngapi?** Uislamu ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kumpwekesha, kumnyenyekea kwa kumtii na kujitenga na ushirikina na washirikina. Nguzo zake ni tano. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amezitaja nguzo hizo katika kauli yake isemayo kuwa: *"Umejengwa Uislamu juu mambo matano:* **1)** *Kukiri kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu na kwamba Muhammad ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, na* **2)** *Kusimamisha Sala na* **3)** *Kutoa zaka na* **4)***Kuhiji Nyumba (ya Mwenyezi Mungu Tukufu huko Makka) na* **5)** *Kufunga (mwezi wa) Ramadhani"*. Ameipokea Hadithi hii Bukhariy na Muslim.

**7. Imani ni nini, na nguzo zake ni ngapi?** Imani ni itikadi ya moyoni na kauli ya ulimini na vitendo vya viungo. Imani inaongezeka kwa utiifu na inapungua kwa

kufanya maasi. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"...ili waongezeke kiimani pamoja na imani yao".*** **Sura Al-fat'h (48), aya 4.** Na Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Imani ni matawi sabini na ushei. Tawi lake la juu zaidi ni kauli ya Laa ilaaha illallah, na tawi lake la chini zaidi ni kuondoa kero njiani. Kuwa na haya ni tawi katika Imani*". Muslim. Haya yanatiwa mkazo na ule uchangamfu anaouhisi Mwislamu katika nafsi yake katika kufanya ibada wakati wa misimu ya kheri, na uvivu anaouhisi nafsini mwake humo katika kufanya ibada baada ya kufanya maasi. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***" Kwa yakini, mazuri yanaondosha mabaya ".*** **Sura Hud (11), aya 114.**

**Nguzo za imani ni sita.** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amezitaja nguzo hizo katika kauli yake isemayo kuwa: " **(***Imani)* *Ni kumwamini* **1)***Mwenyezi Mungu na* **2)***Malaika wake na* **3)***Vitabu vyake na* **4)***Mitume wake na* **5)** *Siku ya Mwisho na* **6)** *Qadari; kheri yake na shari yake*". Bukhariy.

**8. Ni nini maana ya LAA ILAAHA IL-LAL-LAAH?** Ni kukanusha kustahiki kuabudiwa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kuthibitisha kuwa anayestahiki kuabudiwa ni Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee.

**9. Je, Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi?** Ndio, Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi kwa ujuzi wake, usikiaji wake, uonaji wake, ulinzi wake na ueneaji wake (wa kukifikia na kukitawala kila kitu), uwezo wake na utashi wake. Ama dhati yake, haichanganyiki na dhati nyingine, na hakuna kiumbe chochote kinachomzunguka. (yaani kumuelewa jinsi alivyo)

**10. Je, inawezekana Mwenyezi Mungu Mtukufu kuonekana kwa macho?** Waislamu wamekubaliana kwamba: Mwenyezi Mungu haonekani hapa duniani, na kwamba: Waumini watamuona Mwenyezi Mungu huko Akhera katika kukusanywa (kwa ajili ya kuhukumiwa) na pia Peponi. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "***Nyuso siku hiyo ni zenye kumeremeta. Ni zenye kumuangalia Mola wake***". Sura Al-qiyaama 75, aya 22 – 23.

**11. Ni nini faida ya kujua majina na sifa za Mwenyezi Mungu?** Faradhi ya mwanzo kabisa aliyoifaradhisha Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake ni kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Watu wakimjua Mwenyezi Mungu, watamwabudu vilivyo. Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa amesema kuwa: ***"..hivyo, jua kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, na omba msamaha kwa makosa yako"*** Sura Muhammad (47), aya 19. Kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa rehema yake pana, kunawajibisha matarajio (ya kupata rehema hizo), na kukumbuka adhabu yake kali kunawajibisha kuogopa (adhabu yake hiyo), na kukumbuka kuwa yeye pekee ndiye mwenye kuneemesha kunawajibisha kushukuru. Makusudio ya kuabudu kwa majina na sifa za Mwenyezi Mungu ni kuhakikisha kuyajua, kujua maana yake na kuyatumia. Miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake kuna ambazo mja husifiwa kwa kuwa nazo, kama elimu, huruma na uadilifu. Na miongoni mwa sifa hizo kuna ambazo mja hushutumiwa kwa kusifika nazo, kama uungu, ujabari na kiburi. Mja anazo sifa anazosifiwa kwazo na anazoamriwa kuwa nazo, kama uja, uhitaji, udhalili, kuomba na nyinginezo. Lakini Mwenyezi Mungu hawezi kusifika kwa sifa hizi. Kiumbe anayependwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni yule anayesifika kwa sifa ambazo

Mwenyezi Mungu anazipenda, na kiumbe anayechukiwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni yule ambaye anasifika kwa sifa ambazo Mwenyezi Mungu anazichukia

**12. Ni yapi majina mazuri ya Mwenyezi Mungu?** Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa: ***"…na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri. Kwa hiyo, muombeni kwayo"***. **Sura Al-aaraaf (7), aya 180.** Imethibiti kunukuliwa kutoka kwa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa amesema kwamba: *"Kwa yakini, Mwenyezi Mungu Mtukufu ana majina tisini na tisa; mia kasoro moja. Mwenye kuyahifadhi, ataingia peponi"*. Bukhariy na Muslim. **Makusudio ya kuyahifadhi majina hayo ni: 1)**Kuhifadhi matamshi yake na idadi yake. **2)**Kufahamu maana yake, madhumuni yake na kuyaamini. Kwa hiyo, mja anapomtaja Allah kuwa ni "Mwenye hekima", anatakiwa kuyasalimisha mambo yake yote kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu mambo hayo yote yanatokea kwa mujibu wa hekima zake. Mja anapomtaja Allah kuwa ni "Al-qudduus = Mtakatifu sana", anatakiwa kuweka akilini mwake kwamba Mwenyezi Mungu ametakasika na hana mapungufu ya aina zote. **3)**Kumuomba Mwenyezi Mungu kwayo. Maombi ni aina mbili: **a)**Dua ya kusifu na ibada. **b)** Dua ya maombi. Mwenye kufuatilia Qur'ani na Sunna sahihi ataweza kuyakusanya majina hayo, na ambayo ni haya:

| JINA | MAANA YAKE |
|---|---|
| أَللَّهُ **Al-laah** | **Mola** Mwenye Uungu na utumishi kwa viumbe wake wote. Yeye ndiye Mola muabudiwa ambaye ananyenyekewa, anainamiwa, anasujudiwa na kufanyiwa yeye aina zote za ibada. |
| الرَّحمَنُ **Ar-rahmaan** | **Mwingi wa rehema** Ni jina linaloelezea upana wa rehema zake na zinavyowaenea viumbe wote. Ni jina linalomhusu Mwenyezi Mungu tu, na haifai asiyekuwa Mwenyezi Mungu kuitwa kwa jina hilo. |
| الرَّحِيمُ **Ar-rahiim** | **Mwenye kurehemu** Mwenye rehema, Msamehevu kwa waumini duniani na Akhera. Amewaongoza kwenye kumuabudu duniani, naye atawakirimu kwa kuwapa pepo yake Akhera. |
| العَفُوّ **Al-afuwu** | **Mwingi wa msamaha** Ni ambaye anafuta dhambi na kuzisamehe. Hatoi adhabu kwa dhambi hizo pamoja na kuwa mja anastahiki adhabu. |
| الغَفُورُ **Al-ghafuur** | **Mwenye kusamehe sana** Ni anayemsitiri mwenye kutenda dhambi; hamfedheheshi na hamuadhibu kwa dhambi hiyo. |
| الغَفَّارُ **Alghaffaru** | **Msamehevu sana** Ni jina linaloelezea msamaha mwingi wa Mwenyezi Mungu kwa mja wake mwenye kufanya dhambi na kuomba msamaha. |
| الرَّءوفُ **Arrauufu** | **Mpole sana** Jina hili linatokana na upole ambao ni huruma ya kiwango cha juu sana. Upole huu unavienea viumbe vyote duniani na unavihusu baadhi ya viumbe hivyo akhera nao ni waumini. |
| الحَلِيمُ **Al-halim** | **Rahimu** Ni ambaye hafanyi haraka kuwaadhibu waja wake pamoja na kuwa na uwezo wa kuwaadhibu. Anawasamehe wamuombapo msamaha. |
| التَّوابُ **Attawwab** | **Mwingi wa kukubali toba** Ni ambaye anawawezesha kutubu waja wake awatakao na kuwakubalia ktubu kwao. |
| السِّتِّيرُ **Assittiyr** | **Mwenye kusitiri sana** Ni ambaye anamsitiri mja wake na, kwa hiyo, hamfedheheshi mbele ya viumbe wake. Naye pia ni Mwenye kumpenda mja wake anayejisitiri na anayewasitiri wengine na anayesitiri sehemu zake za siri. |
| الغَنِيُّ **Al-ghaniyyu** | **Mkwasi** Ni ambaye hamhitaji kiumbe wake yeyote kwa sababu ya ukamilifu wake mpana na ukamilifu wa sifa zake. Viumbe vyote vinamhitaji yeye na vinahitaji neema zake na msaada wake. |

| | |
|---|---|
| الكَرِيمُ<br>**Al-karim** | **Mkarimu** Mwingi wa kheri na kutoa. Anatoa atakacho kumpa amtakaye kwa namna atakayo kwa kuomba na bila ya kuomba. Anasamehe dhambi na kusitiri kasoro. |
| الأَكْرَمُ<br>**Al-ak'ramu** | **Mkarimu sana** Aliyefikia ukomo wa ukarimu, asiyekuwa na wa kufanana naye katika hilo asilani. Kheri zote zinatoka kwake. Anawalipa waumini kwa fadhila zake na anawapa muda wapinzani na kuwahesabu kwa uadilifu wake. |
| الوَهَّابُ<br>**Al-wahhabu** | **Mwingi wa kutoa** Mwingi wa kutoa. Anatoa bila ya mbadala, anatoa bila ya lengo na ananeemesha bila ya kuombwa. |
| الجَوَادُ<br>**Al-jawadu** | **Mpaji sana** Mwingi wa fadhila na utoaji kwa viumbe wake. Wanaomwamini yeye wana fungu kubwa zaidi la ukarimu na ufadhili wake. |
| الوَدُودُ<br>**Al-waduud** | **Mwenye upendo** Anawapenda wafuasi wake na kujipendekeza kwao kwa msamaha na neema na kwahiyo, huwa radhi nao, hukubali matendo yao na kuwafanya wakubalike duniani. |
| المُعْطِى<br>**Al-mutwii** | **Mtoaji** Anampa amtakaye katika viumbe wake kitu atakacho katika hazina yake. Wafuasi wake wana fungu kubwa zaidi la utoaji wake. Yeye ndiye aliyekipa kila kitu umbile lake na sura yake. |
| الوَاسِعُ<br>**Al-wassiu** | **Mwenye kuenea** Mwenye sifa pana. Hakuna yeyote anayefikia ukomo wa kumsifia. Ni mwenye utukufu na utawala mpana, ni mwenye msamaha na rehema pana, ni mwenye fadhila na hisani pana. |
| المُحْسِنُ<br>**Almuhsin** | **Mwenye uzuri** Yeye ni mwenye uzuri uliokamilika katika dhati yake, majina yake, sifa zake na matendo yake. Kila kitu amefanya umbile lake kuwa zuri, na amefanya mazuri kwa viumbe wake. |
| الرَازِقُ<br>**Arraaziq** | **Mtoaji riziki** Yeye ndiye anayewapa riziki viumbe wote na amezipanga riziki zao kabla ya kuwaumba na amedhamini kuzikamilisha hata kama ni baada ya muda. |
| الرَزَّاقُ<br>**Arrazzaaq** | **Mwingi wa kuruzuku** Ni jina linaloelezea wingi wa riziki zake kwa viumbe wake. Yeye Mola Mtukufu anawaruzuku viumbe kabla ya wao kumuomba. Pia anawaruzuku hata pale wanapomuasi. |
| اللَّطِيفُ<br>**Al-llatwiifu** | **Mjuzi wa yasiyojulikana** Yeye ni mjuzi wa mambo ya ndani. Kwake halijifichi la kujificha. Anafikisha kheri na manufaa kwa waja wake kwa njia za uficho |
| الخَبِيرُ<br>**Al-khabiir** | **Mjuzi wa ya dhahiri** Yeye ni ambaye ujuaji wake umevizingira vitu vya ndani na vilivyofichikana kama ulivyovizingira vya dhahiri. |
| الفَتَّاحُ<br>**Al-fataahu** | **Mfunguaji** Yeye ndiye anayefungua atakacho katika hazina ya ufalme wake, rehema zake na riziki zake kwa namna ambayo hekima yake na ujuzi wake umetaka. |
| العَلِيمُ<br>**Al-alym** | **Mwenye elimu kubwa** Yeye ni ambaye kujua kwake kumezingira mambo ya dhahiri na ya ndani, ya siri na bayana, yaliyopita, ya sasa na yajayo. Kwake hakifichiki kitu chochote. |
| البَرُّ<br>**Al-barru** | **Mwema** Yeye ni mpana katika kuwafanyia mazuri viumbe wake. Anatoa na hakuna yeyote anayeweza kuzihesabu neema zake au kuzikokotoa. Yeye ni mkweli katika ahadi zake, na ambaye anamsamehe mja wake, anamnusuru, anamlinda, anakubali kidogo kutoka kwake na kukikuza. |
| الحَكِيمُ<br>**Al-hakam** | **Mwenye hekima** Ni ambaye anaweka vitu katika sehemu zake, na mipango yange haiingiliwi na makosa au kuteleza. |
| الحَكَمُ<br>**Mwamuzi** | Ni ambaye anahukumu baina ya viumbe wake kwa uadilifu, hamdhulumu yeyote kati yao. Naye ndiye aliyeleta ktabu chake kitukufu ili kiwe hakimu baina ya watu. |

| | |
|---|---|
| الشَّاكِرُ<br>**Ash-shakiru** | **Mwenye shukurani** Anamsifu anayemtii na kumsifia. Anatoa malipo kwa amali iliyofanywa hata kama ni ndogo. Anazikabili shukurani za neema kwa kuziongeza neema hizo duniani na kuziwekea malipo Akhera. |
| الشَّكُورُ<br>**Ash-shakuur** | **Mwingi wa shukurani** Kwake amali ndogo za waja zinakua na kuwarudufishia malipo. Mwenyezi Mungu kumshukuru mja ni kumlipa kwa shukurani hizo na kukubali ibada zake. |
| الجَمِيلُ<br>**Aljamiilu** | **Mzuri** Yeye ni mzuri katika dhati yake, majina yake, sifa zake na matendo yake uzuri mpana. Kila uzuri uliopo kwa viumbe wake unatoka kwake yeye aliyetakasika. |
| المَجِيدُ<br>**Al-majiid** | **Mwenye kutukuzwa** Yeye ndiye ambaye ni stahiki yake fahari, ukarimu, utukufu, hadhi mbinguni na duniani. |
| الوَلِيُّ<br>**Al-waliyyu** | **Mtawalia** Ni msimamizi wa mambo ya viumbe wake na kuuendesha utawala wake. Yeye ndiye mwenye nusura na mwenye msaada kwa wapenzi wake. |
| الحَمِيدُ<br>**Al-hamiid** | **Msifiwa** Yeye ndiye mwenye kusifiwa juu ya majina yake, sifa zake na matendo yake. Yeye ndiye asifiwaye kwa yanayofurahisha na yanayodhuru na katika shida na raha. Yeye ndiye mwenye kustahiki sifa na shukurani kwa hali zote kwakuwa yeye ndiye mwenye kusifika kwa kila ukamilifu. |
| المَوْلَى<br>**Al-mawlaa** | **Mola** Yeye ni mlezi, mfalme, bwana, mwenye nusura na mwenye msaada kwa wapenzi wake. |
| النَّصِيرُ<br>**Annaswiiru** | **Mwenye kunusuru** Yeye ndiye ambaye anampa nguvu kwa nusura yake amtakaye. Hakuna wa kumshinda aliyemnusuru na hakuna wa kumnusuru aliyemfedhehesha. |
| السَّمِيعُ<br>**Assamiiu** | **Mwenye kusikia** Usikiaji wake umezingira kila siri na mnon'gono, kila bayana na dhahiri, lakini pia sauti zote vyovyote ziwavyo; ndogo au kubwa. Yeye ndiye mwenye kumjibu anayemuomba. |
| البَصِيرُ<br>**Al-baswiiru** | **Mwenye kuona** Yeye ni ambaye kuona kwake kumevizingira vitu vyote vilivyopo katika ulimwengu wa visivyoonekana na vinavyoonekana, vyovyote vinavyojificha au kudhihiri na vyovyote vinavyokuwa vidogo au vikubwa. |
| الشَّهِيدُ<br>**Ash-shahiid** | **Shahidi** Yeye ni mwangalizi wa viumbe wake. Anajishuhudia yeye mwenyewe kwa umoja na uadilifu, na anashuhudia ukweli wa waumini pindi wanapompwekesha. Pia anawashuhudia Mitume wake na Malaika wake. |
| الرَّقِيبُ<br>**Arraqiibu** | **Mwangalizi** Yeye ni mwenye kuwajua viumbe wake na mwenye kuyajua vyema matendo yao. Halimpiti kopeso la mwenye kutazama wala fikra impitiayo mwenye kufikiri. |
| الرَّفِيقُ<br>**Arrafiiqu** | **Rafiki** Ni mwenye upole mwingi katika matendo yake. Yeye, akiwa ametakasika, anakuwa mtulivu na kwenda hatua kwa hatua katika kuumba kwake na katika mambo yake. Pia anahusiana na waja wake kwa upole na ulaini na, kwa hiyo, hawkalifishi jambo wasiloliweza. Naye, akiwa ametakasika, anampenda mja wake mpole. |
| القَرِيبُ<br>**Al-qariib** | **Aliye karibu** Yu karibu na viumbe wake wote kwa elimu yake na uwezo wake, na yu karibu na waja wake waumini kwa upole wake na msaada wake. Pia yeye, pamoka na hayo, yuko juu ya Arshi yake. Dhati yake haichanganyikani na viumbe. |
| المُجِيبُ<br>**Al-mujiib** | **Mwenye kujibu** Yeye ndiye ambaye anajibu maombi ya wanao omba kwa namna ambayo elimu yake na hekima yake inataka. |

| | |
|---|---|
| الْمُقِيتُ<br>**Al-muqiit** | **Mlishaji** Yeye ndiye ambaye ameumba vyakula na riziki na kudhamini kuzifikisha kwa viumbe. Naye ndiye mwenye kuzitunza na pia matendo ya waja bila ya upungufu. |
| الحَسِيبُ<br>**Al-hasiib** | **Mwenye kuhesabu** Yeye ndiye mwenye kuwatosheleza waja wake yote muhimu yanayowahusu katika mambo ya dini yao na dunia yao. Wanaomwamini yeye wana fungu kubwa zaidi la utoshelezaji wake. Naye, akiwa ametakasika, ni mwenye kuwahesabu waja juu ya yale waliyoyatenda duniani. |
| الْمُؤْمِنُ<br>**Al-muuminu** | **Muumini** Mwenye kuwasadikisha Mitume na wafuasi wao kwa kuwashuhudulia wao kuwa ni wakweli na pia kwa hoja anazozisimamisha juu ya ukweli wao. Kila amani iliopo duniani au akhera, yeye ndiye mwenye kuileta. Yeye ndiye mwenye kuwaahidi amani wenye kumwamini yeye kwamba hatawadhulumu au kuwaadhibu au kuwapa hofu siku ya Kiyama. |
| الْمَنانّ<br>**Al-mannan** | **Mwingi wa neema** Mtoaji sana, Mneemeshaji mkubwa na mwenye kuwatendea mengi mazuri viumbe wake. |
| الطَّيِّبُ<br>**Attwayyibu** | **Mwema/ Msafi** Yeye ni msafi na aliyesalimika na kila kasoro na upungufu. Yeye ndiye ambaye ni wake yeye tu uzuri na ukamilifu wote. Yeye ni mwenye kheri nyingi kwa viumbe wake. Yeye, akiwa ametakasika, hakubali katika tendo na sadaka isipokuwa tu ile ambayo ni safi, halali na halisi kwa ajili yake. |
| الشّافى<br>**Ashshafiy** | **Mponyaji** Ambaye anaponya nyoyo na miili iondokane na magonjwa yake. Kilichopo mkononi mwa mwanadamu si kingine isipokuwa tu ni dawa ambazo Mwenyezi Mungu amewarahisishia. |
| الحَفيظُ<br>**Al-hafiidh** | **Mhifadhi** Yeye ndiye ambaye anahifadhi na kulinda waja wake na matendo yao kwa fadhila zake. Pia anachunga na kulinda viumbe vyote kwa uwezo wake. |
| الوَكيلُ<br>**Al-wakiilu** | **Mdhamini** Yeye ndiye amewadhamini walimwengu na kuwatawalia kwa kuumba na usimamizi. Yeye ndiye mwenye kudhamini viumbe wake kwa kuumba na kusaidia. Pia yeye ni mdhamini wa waumini ambao wameyaegemeza kwake mambo kabla ya kushughulika kwao, wameomba kwake msaada wakati wa kutafuta kwao riziki, wamemsifia kwa shukurani baada ya kuwasaidia na wameridhika na alichowapangia baada ya kuwapa mitihani. |
| الخَلاّقُ<br>**Al-khallaqu** | **Muumbaji sana** Hili ni jina linaloelezea wingi wa yale ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anayaumba. Yeye pia anaendelea kuumba na bado ataendelea kuwa na sifa hii kubwa. |
| الخَالقُ<br>**Alkhaaliqu** | **Muumba** Yeye ndiye mbunifu wa kuumba viumbe vyote bila ya kuwepo mfano uliotangulia. |
| البَارِئُ<br>**Albaariu** | **Mletaji** Yeye ndiye aliyeleta viumbe alivyopanga na kuamua na kuvileta ulimwenguni. |
| الْمُصَوِّرُ<br>**Almuswawwiru** | **Mtiaji sura** Yeye ndiye ambaye amevifanya viumbe vyake view katika sura aliyovichagulia kwa mujibu wa hekima yake, elimu yake na rehema zake. |
| الرَّبّ<br>**Arrabbu** | **Mlezi** Yeye ndiye anayewalea viumbe wake kwa neema zake na kuwakuza hatua kwa hatua. Pia yeye ndiye anayewalea wapenzi wake kwa mambo yanayozifanya nyoyo zao kuwa njema. Yeye ndiye muumba, mmiliki na Bwana. |
| العَظِيمُ<br>**Al-adhwim** | **Mtukufu** Yeye tu ndiye mwenye utukufu usiokuwa na mpaka katika dhati yake, majina yake na sifa zake. Kwa sababu hiyo, imekuwa wajibu kwa |

| | |
|---|---|
| | viumbe wake kumtukuza, kumheshimu na kuheshimu maamrisho yake na makatazo yake. |
| القاهِر **Al-qaahir** / القهار **Al-qahhaaru** | **Mwenye nguvu** Yeye ndiye mwenye kuwafanya waja wake kuwa dhalili, mwenye kuwatumikisha na aliye juu yao. Naye ndiye mshindi ambaye nyoyo na nyuso zinamnyenyekea yeye. |
| المُهَيْمِنُ **Almuhayminu** | **Mwenye kuwa juu** Mwenye kulisimamia jambo, Mwenye kulitunza, Mwenye kulishuhudia na mwenye kulitawala. |
| العَزِيزُ **Al-aziizu** | **Mwenye ezi** Maana zote za ezi na shani ni zake yeye tu; ezi ya nguvu na kwa hiyo hakuna wa kumshinda, ezi ya kujitosha na kwa hiyo hamhitaji yeyote, ezi ya nguvu na udhibiti na kwa hiyo halitokei jambo isipokuwa tu kwa idhini yake. |
| الجَبَّارُ **Aljabbaaru** | **Jabari (Asiyeshindwa kufanya atakalo)**Ambaye ana utashi usiozuilika. Viumbe vyote vimedhibitiwa naye; vinatii utukufu wake, vinafuata kanuni zake. Naye ndiye anayemuunga aliyekatikiwa, asiyenacho anampa cha kutosha, zito analifanya jepesi, anaponya mgonjwa na kumsaidia mwenye tatizo. |
| المُتَكَبِّرُ **Almutakabbiru** | **Mtukufu sana** Ni Mtukufu aliyetakasika na kila uovu na upungufu, aliyetakasika na kudhulumu waja wake, aliye na nguvu kubwa za kuwatenza nguvu viumbe wake waasi. Yeye ni mwenye kusifika kwa kiburi, na mwemye kukinzana naye katika hilo, anamvunjavunja na kumwadhibu. |
| الكَبِيرُ **Al-kabiiru** | **Mkubwa** Ni mtukufu katika dhati yake, katika sifa zake na katika vitendo vyake. Hakuna kitu kikubwa zaidi kuliko yeye. Kila kisichokuwa yeye ni kidogo mbele ya utukufu wake na ukubwa wake. |
| الحَيِيُّ **Al-hayiyu** | **Mwenye haya** Yeye ndiye mwenye haya zinazolingana na utukufu wa uso wake na utukufu wa utawala wake. Haya za Mwenyezi Mungu ni haya za ukarimu, wema, utoaji na utukufu. |
| الحَيُّ **Al-hayy** | **Aliye hai** Ni ambaye ana uhai kamili, wa kudumu na usalio usiokuwa na mwanzo wala mwisho. Kila uhai uliopo ulimwenguni unatoka kwake yeye tu aliye Mtakatifu. |
| القَيُّومُ **Al-qayyuum** | **Mwenye kusimamia** Yeye ni mwenye kujisimamia mwenyewe, asiyehitaji viumbe wake. Yeye ni msimsmizi wa wote waliopo mbinguni na ardhini. Wao wanamhitaji yeye. |
| الوارِثُ **Al-waarith** | **Mrithi** Yeye ni mwenye kubaki baada ya viumbe kutoweka. Vitu vyote vitarejea kwake baada ya kutoweka kwa wenyewe. Vyote vilivyopo mikononi mwetu ni amana tu, kuna siku vitarudi kwa mmiliki wake; Mwenyezi Mungu Mtukufu. |
| الديّانُ **Addayyan** | **Mlipaji** Yeye ndiye ambaye wamemnyenyekea na kumtii, mwenye kuwalipa waja wake juu ya yale waliyoyatenda. Yakiwa kheri anayarudufisha, na yakiwa shari anaadhibu juu ya hayo au anasamehe. |
| المَلِكُ **Al-maliku** | **Mfalme** Ni ambaye ni miliki yake kuamuru, kukataza na kushinda. Yeye ndiye mwenye kufanya atakayo kwa viumbe vyake kwa amri zake na vitendo vyake. Hakuna yeyote mwenye fadhila kwake katika kuwepo kwa ufalme wake na uchungaji wake. |
| الْمالِكُ **Al-maaliku** | **Mwenye kumiliki** Umiliki wake unatokana na ustahiki na uhalisia. Umiliki ni wake yeye tu wakati wa kuumba viumbe, kwa kuwa hakuwepo yeyote isipokuwa yeye tu. Aidha umiliki ni wake yeye tu wakati wa mwisho, pale viumbe watakapo toweka. |
| المَلِيكُ | **Mfalme mkubwa** Hili ni jina linalo onesha ufalme mpana. Jina hili lina |

| | |
|---|---|
| Al-maliiku | maana zaidi ya mfalme. |
| السُّبوحُ Assubbuhu | **Mtukufu** Mwenye kutakasika na kila kasoro na upungufu, kwa sababu yeye ndiye mwenye sifa za ukamilifu na uzuri wote. |
| القُدّوسُ alquduus | **Mtakatifu** Mwenye kutakasika na kila kasoro na upungufu kwa namna yoyote ile. Hiyo ni kwa sababu yeye ndiye pekee mwenye sifa za ukamilifu wote na, kwa hiyo, hapigiwi mifano. |
| السّلامُ As-ssalaam | **Salama** Mwenye kusalimika na kila kasoro na upungufu katika dhati yake au katika sifa zake, majina yake na vitendo vyake. Kila amani iliopo duniani na akhera inatoka kwake yeye mtukufu. |
| الحَقّ Al-haqu | **Haki** Yeye ndiye ambaye hana shaka wala utata katika dhati yake, katika majina yake na sifa zake na katika uungu wake. Yeye ndiye tu mwabudiwa wa haki na hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa yeye tu |
| المُبينُ Al-mubiinu | **Mwenye kupambanua** Mambo yake yako wazi, katika upekee wake, hekima zake na rehema zake. Yeye ni mwenye kuwawekea wazi waja wake njia za uongofu ili wazifuate na njia za upotofu uili waziache. |
| القَوىّ Al-qawiyyu | **Mwenye nguvu** Yeye ndiye mwenye uwezo wote pamoja na utashi ulio kamili. |
| المَتينُ Al-matiin | **Madhubuti** Yeye ni imara katika nguvu zake na uwezo wake. Katika kutenda kwake, hapatwi na ugumu, uzito wala uchovu. |
| القَادرُ Al-qaadiru | **Mwenye kuweza** Mwenye uwezo wa kila jambo. Hashindwi na jambo ardhini na mbinguni. Yeye ndiye mkadiriaji wa kila jambo. |
| القَديرُ Al-qadiiru | **Mwenye uwezo mkubwa** Jina hili lina maana ya mwenye kuweza ila tu lina maana zaidi katika kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu. |
| المُقْتَدرُ Al-muq'tadir | **Muweza sana** Ni jina linalo onesha kiwango kikubwa cha uwezo wa Mwenyezi Mungu katika kutekeleza yaliyokadiriwa na kuumbwa kama ilivyokuja katika ujuzi wa Mwenyezi Mungu wa kitambo. |
| العَليّ Al-aliyyu<br>الأعْلَى Al-aalaa | **Mtukufu aliye juu zaidi** Yeye ndiye ambaye mambo yake yako juu, uwezo wake uko juu na dhati yake iko juu. Kila kitu kiko chini ya uwezo wake na utawala wake, na hakuna kitu kilichoko juu yake. |
| المُتَعَالُ Al-mutaalu | **Aliyejiweka juu** Yeye ni ambaye kila kitu kimekuwa dhalili mbele ya utukufu wake, na kamwe, juu yake hakuna kitu chochote. Kila kitu kiko chini yake na chini ya uwezo wake na utawala wake. |
| المُقَدِّمُ al-mutaqadimu | **Mtangulizaji** Yeye ndiye atangulizaye mambo na kuyaweka mahali pake kwa mujibu wa utashi wake na hekima zake. Baadhi ya viumbe huwaweka mbele ya wengine kwa mujibu wa ujuzi wake na fadhila zake. |
| المُؤخِرُ Al-muakhir | **Muwekaji nyuma** Yeye huyaweka mambo mahali pake. Huyaweka mbele ayatakayo na huyaweka nyuma ayatakayo kwa hekima zake. Pia huwaahirishia adhabu waja wake ili watubu na kurejea kwake. |
| المُسَعِّرُ Al-musairu | **Mtiaji thamani** Yeye ni ambaye anaongeza thamani ya vitu, nafasi yake na athari zake na kupunguza. Vitu vinakuwa ghali au vinakuwa rahisi kwa namna ambayo hekima zake na ujuzi wake unataka. |
| القَابضُ Al-qaabidh | **Mkamataji** Yeye ndiye ambaye anazikamata roho. Naye ndiye anayezuia riziki kumnyima amtakaye katika viumbe vyake kwa hekima zake na uwezo wake ikiwa ni kuwapa mtihani. |
| البَاسطُ Al-baasitu | **Mkunjuaji** Ni ambaye anakunjua riziki kwa waja wake kwa ukarimu wake na rehema zake, na kwa kufanya hivyo, huwapa mtihani kwa jinsi hekima zake zinavyotaka. Pia hukunjua mikono yake kwa kumkubalia toba aliyefanya maovu. |

| | |
|---|---|
| الأَوَّلُ<br>**Al-awwalu** | **Wa mwanzo** Ni ambaye hakikuwepo kitu chochote kabla yake. Viumbe vyote vimepatikana kwa yeye kuviumba. Ama yeye Mwenyezi Mungu mtukufu hana mwanzo wa kupatikana kwake. |
| الآخِرُ<br>**Al-aákhiru** | **Wa mwisho** Ni ambaye hakuna kitu baada yake. Yeye ndiye mwenye kubaki. Wote waliopo juu ya ardhi watatoweka na halafu watarejea kwake. Yeye hana mwisho wa kuwepo kwake. |
| الظَّاهِرُ<br>**Adh-dhwaahiru** | **Wa dhahiri** Ni aliye juu ya kila kitu. Hakuna kitu kilicho juu yake. Naye ni mwenye kukidhibiti na kukizingira kila kitu. |
| البَاطِنُ<br>**Albaátwinu** | **Wa siri** Ni ambaye hakuna kitu kijifichacho kwake. Yeye ni wa karibu, anayezingira, asiyeonekana na macho ya waja duniani. |
| الوِتْرُ<br>**Al-witr** | **Witiri** Ni mmoja asiye na mshirika, na wa pekee asiye na wa kufanana naye. |
| السَّيِّدُ<br>**Assaiyyidu** | **Bwana** Ni ambaye ana ubwana wote kwa viumbe wake. Yeye mmiliki wao na Mola wao, nao ni waja wake na watumishi wake. |
| الصَّمَدُ<br>**Asw-swamad** | **Mkusudiwa** Ni bwana aliyekamilika katika ubwana wake. Naye pia ni ambaye viumbe wanamkusudia katika mahitaji yao yote, kwa sababu uhitaji wao mkubwa kwake. Yeye ndiye alishaye na halishwi. |
| الوَاحِدُ<br>**Al-waahidu** | **Mmoja, wa pekee** Ni ambaye ni mmoja na wa pekee kwa ukamilifu wote. Hana mshirika wa kushirikiana naye katika ukamilifu huo, na hakuna kitu kilicho kama mfano wake. Haya yanalazimisha kumfanyia yeye pekee ibada, kwa kuwa hana mshirika. |
| الأَحَدُ<br>**Al-ahad** | |
| الإِلَهُ<br>**Al-ilaahu** | **Mola** Ni mwabudiwa wa kweli, anayestahiki kuabudiwa yeye peke yake, na si mwenginewe. |

**13. Kuna tofauti gani kati ya majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake?** Majina na sifa za Mwenyezi Mungu zinashirikiana katika kufaa kuomba kinga na kuapa kwayo. Lakini baina yao kuna tofauti. Muhimu zaidi ya tofauti hizo ni hizi: **Tofauti Ya Kwanza:** Inafaa kujinasibisha uja na kuomba kwa kutumia majina ya Mwenyezi Mungu na sio kwa sifa zake. Mfano wa kujinasibisha ni kujiita jina la "*Abdul-kariim* = Mja wa Mkarimu". Ama kujiita "*Abdul-karam* = Mja wa ukarimu", haifai. Mfano wa kuomba dua ni "*Yaa Kariim* = Ewe Mkarimu", na haifai kuomba: "*Yaa karamallah* = Ewe ukarimu wa Allah". **Tofauti Ya Pili:** Ni kwamba zinachukuliwa sifa kutoka katika majina ya Mwenyezi Mungu. Kwa mfano: Jina la " *Ar-rahmaan* = **Mwingi wa Rehema**", huchukuliwa kutoka katika jina hilo sifa ya "*Ar-rahma* = **Rehema**". Ama majina ambayo hayakuthibiti kunukuliwa, hayachukuliwi kutoka katika sifa. Kwa mfano: Sifa ya "**Kulingana sawa**", haisemwi kuwa ni miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu jina la "**Mwenyekulingana sawa**". **Tofauti Ya Tatu:** Majina ya Mwenyezi Mungu ambayo hayakuthibiti kunukuliwa hayachukuliwi kutoka katika vitendo vyake. Ni katika vitendo vya Mwenyezi Mungu kitendo cha "**kukasirika**". Kwa hiyo, haisemwi kuwa ni miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu jina la "**Mwenyekukasirika**". Ama sifa zake, zinachukuliwa kutoka katika vitendo vyake. Kwa hiyo, tunaithibitisha sifa ya "**Kukasirika**" kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni katika matendo ya Mwenyezi Mungu kwamba **anakasirika**.

**14. Ni nini maana ya kuamini Malaika?** Ni imani thabiti ya Kuamini kuwepo kwao, na kwamba Mwenyezi Mungu amewaumba kwa ajili ya kumwabudu yeye na

kutekeleza amri zake "*Waja watukufu. Hawamtangulii kwa kauli na wao wanatekeleza amri zake tu*". Sura Al-anbiyaa' (21), aya 26 - 27.

**Kuwaamini Malaika kunajumuisha mambo manne: 1)** Kuamini kuwepo kwao. **2)** Kuwaamini wale ambao majina yao tumeyajua, kama vile Jibrili. **3)** Kuziamini sifa zao tulizozijua, kama vile ukubwa wa maumbile yao. **4)** Kuyaamini majukumu yao tuliyoyajua na ambayo yanawahusu, kama vile Malaika wa Mauti.

**15. Qur'ani ni nini?** Qur'ani ni maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambayo hufanywa ibada kuyasoma. Kwake yameanzia na kwake yanaishia. Mwenyezi Mungu ameyatamka kwa hakika; kwa herufi na sauti. Jibrili ameyasikia kutoka kwake, halafu yeye akayafikisha kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Vitabu vyote vya mbinguni ni maneno ya Mwenyezi Mungu.

**16. Je, tunaweza kutosheka na Qur'ani tukaacha Sunna za Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani?** Haifai, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamuru kutumia Sunna, katika kauli yake isemayo kuwa: ***"…na alichokuleteeni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kichukueni na alichokukatazeni kiacheni"***. Sura Al-hashr (59), aya 7. Sunna zimekuja zikiwa zinaifasiri Qur'ani, na mchanganuo wa dini kama vile sala hauwezi kujulikana isipokuwa tu kwa Sunna hizo. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Ee, kwa yakini, mimi nimepewa Kitabu (Qur'ani) na mfano wake pamoja nacho. Ee, unakaribia wakati wa kuwepo mtu aliyeshiba akiwa juu ya kiti chake akisema: Kamataneni na hii Qur'ani tu. Ya halali mtakayoyakuta humo yahalalisheni, na ya haramu mtakayoyakuta humo yaharamisheni".*** Abuudaud.

**17. Ni nini maana ya kuamini Mitume?** Ni imani thabiti ya kuamini kwamba: **1)** Mwenyezi Mungu ametuma katika kila umma Mjumbe miongoni mwao akiulingania umma huo kwenye kumwabudu Mwenyezi Mungu pekee, kukataa vyote vinavyoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu, na kwamba: **2)** Mitume wote ni wakweli, wanaoaminika, waongofu, wenye heshima, watenda mema, wachamungu, waaminifu, viongozi, walio ongoka na kwamba: **3)**Wao wameufikisha ujumbe wao, na kwamba: **4)** Wao ni viumbe bora zaidi, na kwamba: **5)** Wao wameepushwa na ushirikina wa kumshirikisha Mwenyezi Mungu tangu kuzaliwa kwao mpaka kufa kwao.

**18. Ni zipi aina za Maombezi Siku ya Kiyama?** Ni aina nyingi. Kubwa zaidi ya aina hizo ni **1)** Maombezi Makubwa. Maombezi hayo yatakuwa katika kusimama kwa Kiyama baada ya kuwa watu wamesimama miaka hamsini elfu wakisubiri kuhukumiwa. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ataomba kwa Mola wake ili ahukumu kati ya watu. Maombezi hayo yanamhusu Bwana wetu Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na ndio ile Hadhi ya Kusifiwa (Al-maqaam Al-mahmuud) ambayo Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ameahidiwa. **2)** Aina ya pili ni maombezi katika kufunguliwa kwa mlango wa peponi. Wa kwanza kabisa atakayeingia mlango wa peponi ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wetu Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na Umma wa kwanza kabisa utakaoingia peponi ni Umma wake. **3)** Aina ya tatu ni Maombezi watakayo ombewa watu waliokwisha amriwa kuingia motoni. Wataombewa wasiingie motoni. **4)** Aina ya nne ni maombezi watakayo

ombewa waumini waliofanya maasi ambao wameingia motoni. Wataombewa watolewe motoni. **5)** Aina ya tano ni maombezi ya kuzipandisha daraja za watu wa peponi. Aina hizi tatu za karibuni (3, 4, 5) hazimhusu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wetu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, pekee. Lakini yeye ndiye atakaye tangulia kuomba, halafu baada yake wataomba Manabii (wengine), Malaika, Watu Wema na Mashahidi. **6)** Aina ya sita ni maombezi ya kuwaombea watu waingie peponi bila ya kuhesabiwa. **7)** Aina ya saba ni maombezi ya kuomba kupunguzwa kwa adhabu ya baadhi ya makafiri. Maombezi haya yanamhusu Mtume wetu tu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, atakayemuombea Ami yake Abutwaalib (ndugu wa baba yake) apunguziwe adhabu yake. Aina ya nane ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa rehma zake, atawatoa motoni watu waliokufa wakiwa katika Tawhiid (kumwamini na kumpwekesha Allah) bila ya uombezi wowote. Hakuna anayewafahamu hao isipokuwa Allah tu na ,kwa hiyo, Allah atawaingiza peponi kwa rehema zake.

**19. Je, inafaa kuomba msaada au uombezi kwa watu walio hai?** Ndio, inafaa. Kwa yakini, sheria imeshawishi kumsaidia mwengine. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"na saidianeni katika wema na uchamungu"***. **Sura Al-maaidah (5), aya5.** Aidha Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishierehma na amani, amesema kuwa: ***"…na Mwenyezi Mungu yupo katika kumsaidia mja madamu mja (huyo) yupo katika kumsaidia ndugu yake".*** Muslim. Fadhila za maombezi, ambayo ni kuingilia kati, ni kubwa.. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Yeyote atakayeombea maombezi mema, atapata sehemu katika (maombezi) hayo"***. **Sura An-nisaa' (4), aya 85.** Na Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Ombeeni mtalipwa*". Bukhariy. **Hayo yote ni kwa masharti haya: 1)** Maombi ya msaada au kuombewa yawe yanaombwa kwa aliye hai. Kumtaka msaada maiti au kuombea kunaitwa maombi, na maiti hamsikii anayemuomba. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "*Ikiwa mtawaomba, hawasikii maombi yenu, na hata wangesikia wasingekujibuni*". Sura Faatir (35), aya 14. Vipi anaombwa maiti na ilhali yeye anahitaji maombi ya walio hai?. Kwa kufa kwake, matendo yake yamekatika, isipokuwa tu malipo yanayomfikia kwa maombi na mambo mengine. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Mwanadamu anapokufa, matendo yake yanakatika isipokuwa yanayotokana na mambo matatu: Sadaka endelevu au elimu inayotoa manufaa au mtoto mwema anayemuombea*". Muslim. **2)** Kuyafahamu yale atamkiwayo. **3)** Linalo ombwa liwe lipo. **4)** Uombezi uwe katika jambo linalowezekana. **5)** Uombezi uwe katika mambo ya duniani. **6)**Uombezi uwe katika jambo linalofaa, lisilokuwa na madhara.

**20. Mafungu ya Tawassul ni mangapi?** Tawassul ni mafungu mawili. **Fungu la kwanza: Ni Tawassul inayofaa**. Tawaasul hii ina aina tatu: **1)** Kutawassal kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa majina yake na sifa zake. **2)** Kutawassal kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia baadhi ya matendo memo, kama ilivyo katika lile tukio la watu watatu waliokuwa katika pango. **3)** Kutawassal kwa Mwenyezi Mungu kwa kutumia dua ya Mwislamu mwema, aliye hai, aliyepo na ambaye kuna matarajio makubwa ya dua yake kukubaliwa. **Fungu la pili: Ni Tawassul haramu**. Tawassul hii ina aina mbili: **1)** Kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa

kutumia Jaha (hadhi) ya Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishierehema na amani, au Walii, kama vile mtu kusema, kwa mfano,: Ewe Mola wangu, nakuomba kwa Jaha ya Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wako au kwa jaha ya Hussein. Ni sahihi kwamba Jaha ya Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, na kadhalika jaha ya Watu Wema. Lakini Swahaba, ambao ni watu wenye ari zaidi ya kheri, pale ardhi ilipokumbwa na ukame hawakutawassal kwa Jaha ya Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, pamoja na kuwepo kwa kaburi lake kwao. Hawakufanya vingine isipokuwa tu walitawassal kwa kutumia dua ya baba yake mdogo Abbas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, **2)** Mja kuomba shida yake kwa Mola wake akiapia kwa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wake au Walii wake, kama mtu kusema: Ewe Mola wangu, nakuomba jambo fulani kwa (kupitia kwa) Walii wako fulani au kwa haki ya Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wako fulani. Hii ni kwa sababu, kiumbe kuapia kwa kiumbe imekatazwa, na kwa Mwenyezi Mungu imekatazwa zaidi. Halafu pia, mja hana haki yoyote kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu tu ya utiifu wake kwake.

**21. Ni nini maana ya kuamini Siku ya Mwisho?** Ni imani thabiti ya kuamini kutokea kwa siku hiyo. Inaingia katika hilo kuamini: **1)** Mauti na yatakayotokea baada yake, ikiwemo **a)** Mtihani wa kaburini **b)** Adhabu ya kaburini au neema zake. **2)**Kupulizwa kwa Parapanda. **3)** Kusimama watu kwa ajili ya Mola wao. **4)**Kufunuliwa kwa madaftari (ya matendo ya waja). **5)** Kuwekwa kwa Mizani, Njia (Siraat), Birika, (bwawa) Maombezi (Shafaa'a) na hatimae (watu): **6)** Kwende peponi au motoni.

**22. Ni zipi alama kubwa za Kiyama?** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Kwa yakini, Kiyama hakitasimama (hakitatokea) mpaka muone alama kumi kabla yake. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akataja: Moshi na (Masiih) Dajjaal na Daabba (Mnyama) na kuchomoza kwa jua kutokea magharibi yake na kushuka kwa Issa Mwana wa Mariamu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na (kutokea kwa) Yaajuuj na Maajuuj na kupatwa kwa jua mara tatu; kupatwa kumoja mashariki, kupatwa kwingine magharibi na kupatwa kwingine katika Kisiwa cha Arabuni. Mwisho kabisa wa alama hizo ni moto utakaotokea Yemen na utakaowachunga watu kuelekea mahali pao pa kukusanywa (na kuhukumiwa)".*** Muslim.

**23. Ni (fitna) mtihani upi mkubwa utakaowatokea watu?** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Kati ya kuumbwa kwa Adam mpaka kusimama kwa Kiyama, hakuna jambo kubwa sana kuliko (kutokea kwa Masihi) Dajjali".*** Muslim. *Huyo* ni mtu miongoni mwa wanadamu. Atatokea zama za mwisho (wa maisha ya duniani) huku machoni mwake kukiwa kumeandikwa (herufi hizi:) ك – ف – ر . Kila muumini atazisoma herufi hizo. Yeye ana chongo ya jicho la kulia. Jicho lake liko kama zabibu iliyo jitokeza (juu katika kole). Mwanzo kabisa wa kutokea kwake, atadai kuwa yeye ni mtu mwema na (halafu) Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) na (hatimae) Mungu. Atakwenda kwa watu na kuwahubiria. Watamkana na kumkatalia maneno yake. Atawaacha na (lakini) mali zao zitamfuata na, kwa hiyo, watakuwa hawana kitu. Atakwenda kwa watu wengine na kuwahubiria. Watamwamini na kumkubalia. Ataziamrisha mbingu zinyeshe mvua

na ardhi ioteshe mazao na itaotesha. Atawafuata watu huku akiwa ameshika moto na maji. Moto wake ni maji na maji yake ni moto. **Inatakiwa kwa Mwislamu:** Aombe kinga kwa Mwenyezi Mungu ya kujilinda na fitina yake mwisho wa kila sala, amsomee aya za mwanzo za Sura Alkahf ikiwa mtu atapata kukutana naye na. ajiepushe kukutana naye, kwa kuogopa fitna. Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Yeyote atakayemsikia Dajal,i amuepuke. Nina'apa kwa Mwenyezi Mungu kuwa mtu atamwendea na ilhali anadhani kuwa yeye (Dajali) ni muumini na hivyo atamfuata kutokana na Shubuhaat (itikadi tata) atakazozisambaza".*** Abudaud. Dajali atakaa duniani siku arobaini. Siku (ya kwanza) ni kama mwaka, na siku (ya pili) ni kama mwezi, na siku (ya tatu) ni kama wiki. Siku zake nyingine ni kama siku zetu hizi. Hatoacha mji au nchi ila ataingia, isipokuwa tu miji mitukufu ya Makka na Madina. Halafu atashuka (Nabii) Issa, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, na kumuua Dajali.

**24. Je, Pepo na Moto ni vitu vipo?** Ndio, na, kwa yakini kabisa, Mwenyezi Mungu ameumba Pepo na Moto kabla ya kuumba watu. Pepo na moto daima hazitatoweka na hazitaharibika. Pepo ameiumbia watu kwa fadhila zake na moto ameuumbia watu wengine kwa uadilifu wake. Kila mtu anarahisishiwa (kufanya) yale ambayo ameumbwa kwa hayo.

**25. Ni nini maana ya kuamini Qadari?** Ni imani thabiti ya kuamini kwamba: Kila kheri au shari inatokea kwa maamuzi ya Mwenyezi Mungu na mpango wake, na kwamba yeye hufanya ayatakayo. Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Lau kama Mwenyezi Mungu angewaadhibu waliomo katika mbingu zake na waliomo katika ardhi yake, basi angewaadhibu na ilhali si mwenye kuwadhulumu. Na lau kama angewapa rehema, basi rehema zake zingekuwa kheri kwao kutokana na vitendo vyao. Na lau kama ungetoa dhahabu mfano wa mlima Uhud katika kuiendeleza dini ya Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu asingeyakubali hayo kwako mpaka:* **a)** *Uamini Qadari na* **b)** *Ufahamu kuwa yaliyokufika hayakupangwa kukukosa na kwamba yaliyokukosa hayakupangwa kukufika. Na lau kama ungekufa ukiwa katika imani isiyokuwa hii, basi ungeingia motoni".* Ahmad, Abudaud. **Kuamini Qadari kunajumuisha mambo manne: 1)**Kuamini kwamba Mwenyezi Mungu anakijua kila kitu kwa jumla na kwa mchanganuo. **2)** Kuamini kwamba Mwenyezi Mungu ameandika hayo katika Ubao Uliohifadhiwa. Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Mwenyezi Mungu ameandika mipangilio ya viumbe kabla hajaumba mbingu na ardhi kwa miaka elfu hamsini)".* Muslim. **3)** Kuamini utashi wa Mwenyezi Mungu unaoendelea na ambao hakuna kitu kinachoweza kuuzuia, na uwezo wake ambao hakuna kitu kinachoweza kuushinda. Analotaka Mwenyezi Mungu ndio linalokuwa na asilolitaka haliwi. **4)** Kuamini kuwa Mwenyezi Mungu tu ndiye Muumba na Mletaji wa vitu vyote, na vyote visivyokuwa yeye vimeumbwa kwa ajili yake.

**26. Je, viumbe wana uwezo na utashi wa hakika?** Ndio. Mwanadamu anao utashi na uhuru wa kuchagua, lakini uchaguzi na utashi huo hautoki nje ya utashi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"..na***

*hamtaki ila tu akitaka Mwenyezi Mungu"*. Sura Al-insaan (76), aya 30. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, naye amesema kuwa: *"Fanyeni amali, kwani kila mmoja ni mwenye kurahisishiwa (kufanya) yale aliyoumbwa kwayo"*. Bukhariy na Muslim. Mwenyezi Mungu ametupa akili, masikio na macho ili tutofautishe kati ya jema na baya. Hivi kuna mwenye akili anayeiba halafu akasema: Mwenyezi Mungu ameniandikia hivyo? Hata kama angesema hayo, watu hawawezi kumsamehe, bali ataadhibiwa na kuambiwa: Mwenyezi Mungu pia amekuandikia adhabu hiyo. Kutoa hoja na visingizio kwa Qadar haifai na ni kukufuru. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Watasema wale ambao wameshirikisha (kuwa): Lau kama Mwenyezi Mungu angetaka, tusingeshirikisha; sisi wala baba zetu, na tusingeharamisha kitu chochote. Kama hivyo, walikadhibisha wale ambao walikuwepo kabla yao"***. Sura Al-an'aam (6), aya 148.

**27. Ih-saan ni nini?** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliulizwa kuhusu Ihsaan akasema kuwa: *"(Ihsaan) Ni wewe kumwabudu Mwenyezi Mungu kama unamuona. Kwani ikiwa wewe humuoni, basi yeye anakuona"*. Muslim. Ihsaan ni daraja ya juu zaidi katika daraja tatu za dini.

**28. Mafungu ya Tawhiid ni mangapi?** Mafungu yake matatu: **1)Tawhiid Rubuubiyya**. Tawhidi hii ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu (kuamini kwamba Mwenyezi Mungu yu pekee) katika matendo yake, kama kuumba, kutoa riziki, kuleta uhai n.k. Makafiri, kabla Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) hajapewa utume, walikuwa wanalikubali fungu hili la Tawhiid. **2) Tawhiid Uluuhiyya**. Tawhiid hii ni kumpwekesha (kumkusudia Mwenyezi Mungu pekee) kwa ibada, kama kuswali, kuweka nadhiri, kutoa sadaka n.k. Kwa ajili ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa ibada ndio Mitume walitumwa na vitabu kuteremshwa. **3) Tawhiid Al-asmaa Wassifaat**. Tawhiid hii ni kuthibitisha majina mazuri na sifa tukufu alizozithibitisha Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake, bila ya kubadilisha au kupotosha matamshi au kuainisha au kufananisha namna.

**29. Walii ni nani?** Ni muumini, mwema, mchamungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Ee, kwa yakini, mawalii (wapenzi) wa Mwenyezi Mungu hawana hofu na wao hawatahuzunika. Ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu"*. **Sura Yunus (10), aya 62–63.** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) naye, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Kwa yakini, hakuna vingine isipokuwa kwamba walii wangu ni Mwenyezi Mungu na waumini wema"*. Bukhariy na Muslim.

**30. Ni lipi lililo wajibu kwetu kuhusu Swahaba wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani?** La wajibu ni kuwapenda, kuwaombea radhi, nyoyo na midomo yetu iwe salama kwao (kwa maana ya kuwa tusiwaseme vibaya au kuamini kuwa wao ni waovu), kutangaza mema yao, kutotangaza tofauti zilizojitokeza baina yao. Wao sio watakatifu wasiofanya makosa na lakini walijitahidi. Aliyepatia katika wao, ana malipo mara mbili na aliyekosea ana malipo mara moja kwa kujitahidi kwake, na makosa yake yanasameheka. Wana mema yanayofuta kasoro zilizotokea kwao. Nao wanazidiana ubora. Walio bora zaidi kwao ni kumi: **Abubakar, halafu Omar, halafu Othman, halafu Ali, Zubeir, Abdulrahman Bin Auf, Saad Bin Abii-waqqaas, Said Bin Zubeir na Abu-obaidah Bin Aljarraah.** Halafu wanafuatia Muhajirina wote (waliohamia

Madina), halafu waliokuwepo kwenye vita vya Badr, halafu Ansaar waliosalia, halafu Swahaba waliobaki. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Msiwatukane Swahaba wangu, kwani nina'apa kwa (Mwenyezi Mungu) ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba: Lau kama mmoja wenu angetoa (sadaka ya) dhahabu mfano wa mlima Uhud basi asingefikia mema ya kadiri ya kiganja cha mmoja wao wala nusu yake"*. **Bukhariy na Muslim.**

Pia amesema kuwa: *"Yeyote aliyewatukana Swahaba wangu, imshukie laana ya Mwenyezi Mungu na Malaika na watu wote"*. Tabaraaniy.

**31. Je, tunaweza kupindukia mipaka katika kumsifu Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, tukavuka hadhi ambayo Mwenyezi Mungu amempa?** Hakuna shaka kwamba Bwana wetu Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni mtukufu zaidi katika viumbe wa Mwenyezi Mungu na ni bora zaidi yao wote. Lakini haifa kuzidisha katika kumsifu kama Wakristo walivyozidisha katika kumsifu Issa Mwana wa Mariamu, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, kwa sababu Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ametukataza hilo, kwa kauli yake isemayo kuwa: "*Msichupe mipaka katika kunisifu kama walivyochupa mipaka Wakristo katika kumsifu (Issa) Mwana wa Mariamu. Hakuna vingine isipokuwa kwamba mimi ni mja tu. Kwa hiyo, semeni: Mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake*". **Bukhariy.**

**32. Je, Watu wa Kitabu ni waumini?** Wayahudi, Wakristo na wafuasi wa dini nyingine ni makafiri, hata kama walikuwa wanafuata dini ambayo asili yake ni sahihi. Mtu ambaye hakuiacha dini yake baada ya utume wa Mtume Muhammad, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ***"..halitokubaliwa kwake (hilo) na yeye Akhera ni miongoni mwa watakaopata hasara"***. **Sura Aal-imraan (3), aya 85.** Mwislamu asipoitakidi ukafiri wa makafiri hao au akiutilia mashaka ukafiri wao, anakuwa kafiri yeye, kwa sababu amepingana na hukumu ya Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake katika kuwakufurisha makafiri. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"….na yeyote anayemkufuru (anayemkataa Mtume Muhammad) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) katika makundi (ya watu wa dini) basi moto (wa Jahanamu) ndio ahadi yake"***. **Sura Huud (11), aya 17.** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) naye, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Nina apa kwa (Mwenyezi Mungu) ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba hanisikii mimi mtu yeyote katika umma huu; si Myahudi wala Mkristo halafu asiniamini isipokuwa tu atakuwa miongoni mwa watu wa motoni"*. Muslim.

**33. Je, inafaa kumdhulumu kafiri?** Uadilifu ni wajibu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Kwa yakini, Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na kufanya mazuri"*. Sura Annahl (16), aya 90. Dhuluma ni haramu, kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "*Kwa yakini, mimi nimejiharamishia dhuluma, na nimeifanya haramu kwenu. Kwa hiyo, msidhulumiane"*. Muslim. Aliyedhulumiwa atachukua haki yake Siku ya Kiyama kwa aliyemdhulumu. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Je, mnajua ni nani aliyefilisika? (Swahaba) Walisema: Aliyefilisika kwetu ni yule asiyekuwa na fedha wala rasilimali. Akasema: Kwa yakini, mwenye kufilisika katika umma wangu atakuja Siku ya Kiyama akiwa na*

*sala, saumu na zaka, na atakuja na ilhali amemtukana huyu na amemsingizia huyu na amekula mali ya huyu na amemwaga damu ya huyu na amempiga huyu. Kwa hiyo, huyu atapewa katika mema yake na huyu atapewa katika mema yake. Mema yake yakimalizika kabla ya kulipwa anayodaiwa, yatachukuliwa katika madhambi yao na kutupiwa yeye na halafu atatupwa motoni".* Muslim.

**34. Bid'a ni nini?** Ibn-Rajab, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: "*Muradi wa Bid'a ni jambo lililozushwa, lisilokuwa na msingi katika sheria unaoelekeza kwenye jambo hilo. Ama jambo ambalo katika sheria lina msingi unaoelekeza kwenye jambo hilo, basi hilo sio Bid'a kisheria hata kama litakuwa Bid'a katika lugha*".

**35. Je, katika dini kuna Bid'a nzuri na Bid'a mbaya?** Zimekuja aya na Hadithi katika kushutumu Bid'a kwa maana yake ya kisheria ambayo ni: **Jambo lililozushwa na lisilokuwa na msingi katika sheria** pale Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliposema kuwa: *"Na yeyote aliyefanya amali (ambayo), katika amali hiyo, hamna amri yetu, basi amali hiyo ni yenye kurudishwa".* Bukhariy na Muslim. Pia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kwamba: *"...kila kilichozushwa ni Bid'a na kila Bid'a ni upotofu".* Abudaud. Imam Malik, Mwenyezi Mungu amrehemu, katika kuelezea maana ya kisheria ya Bid'a, amesema kuwa: ***"Na yeyote aliyezusha katika Uislamu Bid'a anayoiona kuwa ni nzuri, basi huyo amedai kuwa Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ameufanyia hiyana utume, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa: Leo nimekukamilishieni dini yenu na nimetimiza kwenu neema yangu".*** Sura Al-maaida (5), aya 3. **Zimekuja baadhi ya Hadithi zikisifu Bid'a kwa maana yake ya kilugha ambayo ni: Jambo ambalo sheria imelileta na lakini limesahauliwa**, na kwa hiyo, Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akatoa sisitizo la kuwakumbusha watu jambo hilo, kama ilivyo katika kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: *"Mwenye kuanzisha (kukumbusha) njia nzuri katika Uislamu, atapata thawabu zake na thawabu za watakaoitumia njia hiyo baada yake bila ya kupungua kitu katika thawabu zao".* Muslim. **Kwa maana hii, ndio ilikuja kauli ya (Swahaba) Omar, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, isemayo kuwa: "Bid'a bora ni hii"** akikusudia sala ya Tarawehe. Sala ya Tarawehe ilikuwepo kisheria na Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliihimiza, aliisali kwa siku tatu halafu akaiacha kwa kuchelea isije ikafaradhishwa. Kwa hiyo, (Swahaba) Omar, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, aliisali na kuwajumuisha watu waisali jamaa.

**36. Je, unafiki ni aina ngapi?** Ni aina mbili: **1)Unafiki wa itikadi (Unafiki Mkubwa).** Unafiki huu ni wa mtu kuonesha imani ilhali moyoni anaficha ukafiri. Unafiki huu unamtoa mtu katika dini. Mwenye unafiki huu iwapo atakufa na ilhali ameun'gan'gania, basi atakufa akiwa kafiri. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"...kwa yakini, wanafiki watakuwa katika tabaka la chini sana katika moto".*** Sura An-nisaa' (4), aya 145. **Miongoni mwa sifa za wanafiki ni** kwamba wanamfanyia hadaa Mwenyezi Mungu na Waislamu, wanawadharau Waislamu, wanawasaidia makafiri dhidi ya Waislamu na wanapofanya mambo yao mema, wanakusudia

kupata faida za kidunia. **2) Unafiki wa kiutendaji (Unafiki Mdogo)** ambao mwenye nao haumtoi katika Uislamu, lakini asipotubu, atakuwa yupo katika hatari ya unafiki huo kumfikisha kwenye ule unafiki mkubwa. Mwenye unafiki huu ana sifa nyingi, miongoni mwake ni hizi: Akizungumza anasema uongo, anapotoa ahadi hatekelezi, anapogombana anakuwa na lugha chafu, anapoingia katika makubaliano (mkataba) anayavunja na anapoaminiwa anafanya hiyana (anavunja uaminifu). Kwa sababu hiyo, Swahaba, Mwenyezi Mungu awawiye radhi, walikuwa wakiuogopa unafiki wa vitendo. Ibn-abii Mulaika, Mwenyezi Mungu amrehemu, anasema kuwa: "Niliwahi kukutana na Swahaba thalathini wa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wa Mwenyezi Mungu. Wote walikuwa wakiuogopa unafiki wasiwe nao". Ibrahim Attaimiy, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: " Sijapambanisha kauli zangu na vitendo vyangu isipokuwa niliogopa nisije nikawa muongo". Hassana Albasriy, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kwamba: "Hauogopi unafiki isipokuwa tu mtu Muumini, na hana hofu na unafiki isipokuwa tu mnafiki". Omar alimwambia Hudhaifa, Mwenyezi Mungu awawiye radhi wote, kwamba: "Naomba nikuulize kwa jina la Mwenyezi Mungu, hivi Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wa Mwenyezi Mungu hajanitaja kwako kwamba mimi ni katika wao? Anakusudia wanafiki. Hudhaifa akasema: Hapana, na simsafishi yeyote baada yako".

**37. Ni dhambi ipi nzito na kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu?** Ni kumfanyia shirk (ushirika) Mwenyezi Mungu Mtukufu. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa: ***"…kwa yakini, Shirki ni dhuluma kubwa".*** Sura Luqman (31), aya 13. Wakati Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipoulizwa: Ni dhambi gani kubwa zaidi? Alisema kuwa: *"Ni wewe kumfanyia Mwenyezi Mungu mshirika na ilhali yeye amekuumba".* **Bukhariy na Muslim.**

**38. Je, aina za Shirk (Ushirika) ni ngapi?** Ni aina mbili: **1) Ushirika Mkubwa** unaomtoa mtu katika Uislamu, na Mwenyezi Mungu hamsamehe mwenye nao. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Kwa yakini, Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa naye na anasamehe (madhambi) yaliyo chini ya hayo kwa amtakaye".*** Sura An-nisaa' (4), aya 48. Mafungu ya Shirki hii ni manne: **a)**Ushirika wa kuomba. **b)** Ushirika wa nia, utashi na makusudio kwa maana ya mtu kufanya mema kwa kutomkusudia Mwenyezi Mungu. **c)** Ushirika wa utiifu, kwa maana ya mtu kuwatii wanachuoni (viongozi wa dini) katika kuharamisha aliyoyahalalisha Mwenyezi Mungu au kuhalalisha aliyoyaharamisha. **d)** Ushirika wa kupenda, kwa maana ya mtu kumpenda mwengine kama anavyompenda Mwenyezi Mungu. **2) Ushirika Mdogo,** usiomtoa mtu katika Uislamu. Huo nao uko katika mafungu mawili: **a)** Ushirka wa wazi, sawasawa uwe umefungamana na kauli kama vile kuapia asiye kuwa Mwenyezi Mungu, au kusema: Akitaka Mwenyezi Mungu na wewe, au kusema: Lau kama si Mwenyezi Mungu na fulani, au uwe umefungamana na vitendo, kama vile kuvaa kikuku (bangili) au uzi, kwa ajili ya kuondoa balaa au kuikinga balaa, na kama vile kutundika hirizi kwa ajili ya kuogopa kijicho, au mikosi kupitia ndege, majina fulani, matamshi fulani na maeneo fulani n.k). **b)** Ushirika uliojificha, na ambao ni ushirika katika nia na makusudio, kama vile kufanya jambo ili uonekane na kutaka kusikika.

**39. Ni ipi tofauti kati ya Ushirika Mkubwa na Mdogo?** Miongoni mwa tofauti kati yao ni hizi: Mwenye Shirki Kubwa anahukumiwa kuwa ametoka katika Uislamu hapa duniani, na atawekwa milele motoni huko akhera. Ama mwenye Shirki Ndogo, hahukumiwi kuwa ametoka katika Uislamu hapa duniani na hatawekwa milele motoni huko akhera. Shirki Kubwa pia inaharibu matendo yote wakati ambapo Shirki Ndogo inaharibu ile amali iliyokutana nayo tu. Linabaki suala lenye mvutano. Suala hilo ni hili: Je, Shirki Ndogo haisamehewi isipokuwa kwa kutubu tu kama Shirki Kubwa, au ni kama dhambi nyinginezo kubwa na ambazo ziko chini ya utashi wa Mwenyezi Mungu? Kwa kauli zote mbili, jambo hili ni hatari sana!

**40. Je, Shirki Ndogo ina kinga isitokee au kafara iwapo imeshatokea?** Ndio. Kinga ya Ria inapatikana kwa mtu kumkusudia Mwenyezi Mungu kwa matendo yake. Ama Ria ndogo, inakingwa kwa maombi (dua). Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Enyi watu, iepukeni Shirki hii (ndogo), kwa sababu ni yenye kujificha sana kuliko utambaaji wa sisimizi. (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Aliulizwa: Na tutaiepuka vipi na ilhali ni yenye kujificha sana kuliko utambaaji wa sisimizi, ewe Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu? Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alisema: Semeni:* ***Allaahumma Innaa Nauudhu Bika Annushrika Bika Shai-an-naalamuhuu. Wanastaghfiruka Limaa Laa Naalamuhuu****. = Ewe Mola wangu, kwa yakini, sisi tunakuomba utukinge kukishirikisha nawe kitu tunachokijua na tunakuomba msamaha kwa (kukishiriksha nawe kitu) tusichokijua".* **Ahmad.** Ama kafara ya kuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu, Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Yeyote aliyeapia (sanamu la) Lata na Uzzaa aseme:* ***Laa Ilaaha Illallah*** *= Hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu".* Bukhariy na Muslim. **Ama kafara ya kuona mkosi, Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa:** *"Yeyote ambaye kuona mkosi kumemrudisha asikidhi haja, kwa yakini amefanya Shirki. (Swahaba) Waliuliza: Iwapo ni hivyo, kafara ya hayo ni nini? (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Alisema: (Kafara yake) Ni kusema:* ***Allahumma Laa Khaira Illaa Khairuk Walaa Twaira Illaa Twairuk Walaa Ilaaha Ghairuk.*** *Ewe Mola wangu, hakuna kheri isipokuwa kheri yako tu na hakuna ndege isipokuwa ndege wako tu na hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa wewe tu".* Ahmad.

**41. Je, ukafiri ni aina ngapi?** Ni aina mbili: **a) Ukafiri Mkubwa** unaomtoa mtu katika Uislamu. Ukafiri huo upo katika mafungu matano: **1)** Ukafiri wa kukanusha. **2)** Ukafiri wa kiburi pamoja na kuwepo kwa imani. **3)** Ukafiri wa shaka. **4)** Ukafiri wa kupinga. **5)** Ukafiri wa unafiki. **b) ukafiri Mdogo**, Ukafiri huo ni wa kuasi usiomtoa mtu katika Uislamu, kama vile (Mwislamu) kumuua Mwislamu (mwenzake).

**42. Ni nini hukumu ya kuweka Nadhiri?** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amechukia kuweka Nadhiri, na kusema kuwa: "..*kwa yakini, hiyo (Nadhiri) haileti kheri*". Bukhari. Hii ni pale Nadhiri hiyo itakapokuwa halisi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Ama Nadhiri ikiwa sio kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kama mtu anayeweka Nadhiri kwa ajili ya kaburi au Walii, basi hiyo ni Nadhiri haramu, haifai na pia haifai kuitekeleza.

**43. Je, ni nini hukumu ya kwenda kwa mpiga ramli au kuhani (mganga)?** Ni haramu. Iwapo mtu atawaendea akitaka msaada wao na lakini asiwaamini katika wanayoyasema, basi sala yake haitakubaliwa kwa siku arobaini, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: *"Yeyote atakayemwendea mpiga ramli akamuuliza jambo, basi haitakubaliwa swala yake siku arobaini".* Muslim. Na kama mtu atawaendea na kuwaamini katika madai yao ya kujua mambo yaliyojificha, basi ameyakufuru yale yaliyoteremshwa kwa Mtume Muhammad, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: *"Yeyote atakayemwendea mpiga ramli au kuhani (mganga) akayasadiki(akayaamini) yale wanayoyasema, basi ameyakufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad".* Abudaud.

**44. Ni wakati gani kuomba mvua kwa kutumia nyota kunakuwa Ushirika Mkubwa na wakati gani kunakuwa Ushirika Mdogo?** Anayekuwa na itikadi kwamba nyota ina athari, bila ya utashi wa Mwenyezi Mungu, na kwa sababu hiyo anaihusisha mvua na nyota uhusishaji wa kuitengeneza na kuileta, basi huu ni **Ushirika Mkubwa**. Ama anayekuwa na itikadi kwamba nyota, kwa utashi wa Mwenyezi Mungu, ina athari na kwamba Mwenyezi Mungu ameifanya nyota hii kuwa sababu ya kunyesha kwa mvua na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka kawaida ya kunyesha kwa mvua wakati wa kuchimbuka kwa nyota hiyo, itikadi hii ni haramu na ni **Ushirikina Mdogo** kwa sababu amefanya hivyo bila ya hoja ya kisheria au utambuzi na hali halisi au akili sahihi. Ama kutafuta mwongozo kwa kutumia nyota hizo juu ya vipindi vya mwaka na nyakati za kutegemewa kunyesha kwa mvua, ni jambo linalofaa.

**45. Ni lipi la wajibu kuwafanyia viongozi wa Waislamu?** La wajibu kuwafanyia ni usikivu na utiifu katika kupenda na kuchukia. Haifai kuwaasi hata kama wakifanya udhalimu. Hatuwaombei mabaya na hatuuondoi utiifu wetu kwao. Tunawaombea wapate wema, waondokewe na mabaya na wafanye yaliyo sahihi. Tunaona kuwa kuwatii ni katika kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu, madamu hawaamrishi maasi. Ikiwa wataamrisha maasi, ni haramu kuwatii katika maasi hayo, na ni wajibu kuwatii, kwa wema, katika amri nyingine zisizokuwa hizo za maasi. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Utakuwa msikivu na mtiifu kwa kiongozi. Na hata ukipigwa mgongo wako na mali yako kuchukuliwa, wewe sikia na tii".* Muslim.

**46. Je, inafaa kuuliza hekima ya Mwenyezi Mungu katika maamrisho na makatazo?** Ndio, lakini kwa sharti la kutoegemeza imani na utekelezaji kwenye kujua hekima na kuridhika nayo. Kujua hekima kunatakiwa kuwe ni ongezeko tu la uimara wa muumini katika haki. Utiifu wa jumla na kutouliza (hekima) ni ushahidi wa ukamilifu wa utumishi na imani kwa Mwenyezi Mungu na hekima zake kamilifu, kama walivyokuwa Swahaba, Mwenyezi Mungu awawiye radhi.

**47. Ni nini makusudio ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "*Zuri lolote lililokufika linatokana na Mwenyezi Mungu, na baya lolote lililokufika linatokana na nafsi yako*"?** Sura An-nisaa'(4), aya 79. Makusudio ya "**zuri**" hapa ni neema, na makusudio ya "**baya**" ni balaa (majaribu). Yote

yamepangwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Jema limehusishwa na Mwenyezi Mungu, kwa kuwa yeye ndiye aliyelifadhili. Ama baya, ameliumba kwa hekima fulani, na kwa kuizingatia hekima hiyo, baya hilo ni katika ufadhili wake pia, kwani Mwenyezi Mungu hafanyi mabaya. Yote ayafanyayo ni mazuri. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Na kheri yote iko mikononi mwako na shari haiko kwako"***. **Muslim.** Vitendo vya wanadamu vimeumbwa na Mwenyezi Mungu, na wakati huo huo ni chumo la wanadamu wenyewe. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Basi ama aliyetoa na kuwa mchamungu, na akaamini (jambo) zuri, tutamrahisishia (njia) nyepesi (kwenda peponi). Na ama aliyefanya ubahili na akatosheka, na akalikataa (jambo) zuri, tutamrahisishia (njia) nzito (kwenda motoni)"***. **Sura Al-Lail (92), aya 5 – 10.**

**48. Je, inafaa kusema: "Mtu fulani ni shahidi"?** Kumhukumu yeyote maalum kuwa ni shahidi ni kama kumhukumu kuwa amepata pepo. Madhehebu ya Watu wa Sunna (Ahlus-sunna) ni kwamba hatumuelezei Muislamu yeyote maalum kwamba yeye ni katika watu wa peponi au ni katika watu wa motoni, isipokuwa tu wale ambao Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amewaelezea kuwa ni miongoni mwa watu wa mojawapo kati ya pepo au moto. Hii ni kwa sababu, ukweli umejificha na hatuyajui vizuri yote ambayo mwanadamu amekufa nayo. Amali zinazingatiwa kwa (kuangalia) mwisho, na ujuzi wa nia uko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini sisi tunataraji thawabu kwa afanyaye mazuri na tunakuwa na hofu ya adhabu kwa afanyaye mabaya.

**49. Je, inafaa kumhukumu Muislamu maalum kuwa ni kafiri?** Haifai kumhukumu Muislamu kuwa ni kafiri wala mshirikina wala mnafiki, madamu halijaonekana kwake jambo linaloshuhudia hivyo, na kukawa hakuna pingamizi. Tunamwachia Mwenyezi Mungu Mtukufu dhamira yake ya ndani.

**50. Je, inafaa kutufu (kuzunguka kwa nia ya ibada) pasipokuwa Al-kaaba?** Hakuna mahali popote duniani panapofaa kutufu isipokuwa Al-kaaba tu. Haifai kuifananisha sehemu yoyote na Al-kaaba, vyovyote utukufu wake uwavyo. Yeyote atakayetufu sehemu isiyokuwa Al-kaaba kwa taadhima, basi amemuasi Mwenyezi Mungu**.**

# MATENDO YA NYOYO

Mwenyezi Mungu ameuumba moyo akaufanya mfalme na viungo jeshi lake. Mfalme anapokuwa mzuri na jeshi linakuwa zuri. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Na kwa yakini, katika moyo kuna kipande cha nyama (ambacho) kikiwa chema na mwili wote unakuwa mwema na kikiwa kiovu na mwili wote unakuwa muovu. Ee!Kipande hicho cha nyama ni moyo "*. **Bukhariy, Muslim.** Moyo ni mahali pa imani na uchamungu au ukafiri, unafiki na ushirika. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Uchamungu ni hapa, na alionesha ishara kwenye kifua chake mara tatu "*. **Muslim.**

❖ Imani ni itikadi, kauli na vitendo; itikadi ya moyoni, kauli ya ulimi na vitendo vya moyo na viungo. Moyo unaamini na kukubali na, kwa hiyo, unazalisha kutamka shahada kwa ulimi. Halafu moyo unafanya kazi yake ya kupenda, kuogopa na kutumaini, na hivyo, unafanya kazi ya kutamka na kusoma Qur'ani na viungo vinafanya kazi ya kusujudu, kurukuu na kutenda mema yanayomuweka mtu karibu na Mwenyezi Mungu. Mwili unaufuata moyo. Hakikai kitu moyoni ila hudhihiri athari yake mwilini japo kwa namna yoyote ile.

❖ Makusudio ya matendo ya moyoni: Ni matendo ambayo mahali pake ni moyoni, na yanahusiana na moyo.Tukufu zaidi ya matendo hayo ni kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu imani ambayo inakuwa moyoni. Ni katika imani hiyo: kuamini, kufuata na kukubali. Hii ni pamoja na yanayotokea katika moyo wa mja kwa ajili ya Mola wake ikiwa ni pamoja na upendo, hofu, matumaini, kujirudi, kutegemea, subira, yakini, unyenyekevu na yasiyokuwa hayo.

Kila kitendo katika vitendo vya moyo, kinyume chake ni ugonjwa. Ikhlasi (uhalisi) kinyume chake ni Ria (mtu kufanya jambo kwa kutaka aonekane). Yakini, kinyume chake ni shaka. Upendo, kinyume chake ni chuki. Tukijisahau kuzifanya njema nyoyo zetu zitajirundikana dhambi juu yake na, hivyo, kuziangamiza. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Kwa yakini, mja afanyapo dhambi hubandikwa doa katika moyo wake. Akijirudi na akaomba msamaha na akatubu doa hilo hukwatuliwa (husafishwa). Na akirudi (katika dhambi) linaongezwa mpaka linakaa juu yake, na hiyo ndio kutu aliyoitaja Mwenyezi Mungu katika kauli yake isemayo kuwa: "**Sivyo, bali yametia kutu juu ya nyoyo zao yale waliyokuwa wakiyachuma**"* .**Sura Mutaffifiin (83), aya 14". Tirmidhiy.**

Pia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mitihani (majaribu) hutandazwa juu ya nyoyo kama zulia; moja baada ya nyingine. Moyo wowote unaoifyonza mitihani hiyo (unaoipokea na kuikubali) hubandikwa doa jeusi. Na moyo wowote unaoikataa, hubandikwa doa jeupe mpaka inakuwa juu ya mioyo miwili: mweupe kama jiwe litelezalo na, kwa hiyo, hakuna mtihani unaoudhuru moyo huo madamu mbingu na ardhi zipo. Na moyo mwingine ni mweusi, kijivu, kama kopo ukiwa umepinda, haujui jambo wala haukatai jambo baya isipokuwa yale matamanio yake uliokwisha yafyonza,"*. **Muslim.**

❖ Kuzijua ibada za moyoni ni jambo la lazima sana na la muhimu zaidi kwa mja kuliko kujua matendo ya viungo, kwa sababu ibada za moyoni ndio shina na matendo ya viungo ni matawi yake, yanayakamilisha na ni matunda yake. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Kwa yakini, Mwenyezi Mungu hatazami sura zenu na mali zenu, na lakini anatazama nyoyo zenu na matendo yenu,"*. **Muslim.** Moyo ndio mahali pa elimu,

mazingatio na kutafakari. Kwa sababu hiyo, ndio kumekuwepo kuzidiana kati ya watu kwa kiasi cha imani, yakini na ikhlasi zilizopo katika moyo, na mfano wa hayo. Hassan Albasriy, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "Nina'pa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hakukushindeni Abubakar, mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwa sababu ya sala wala saumu. Hakuna vingine isipokuwa kwamba amekushindeni kwa sababu ya imani iliyotuama katika moyo wake".

❖ Matendo ya moyo yanayazidi ubora matendo ya viungo, kwa njia nyingi: 1)Kutetereka kwa ibada ya moyoni kunaweza kuibomoa ibada ya viungo, kama vile Ria pamoja na vitendo. 2)Matendo ya moyo ndio msingi. Tamko lolote linalotamkwa au kitendo chochote kinachofanyika bila ya kukusudia hakizingatiwi. 3)Matendo ya moyo ndio sababu ya kupata daraja za juu peponi, kama vile Zuhudi. (Zuhudi ni kutoyaweka mbele mambo ya kidunia). 4)Matendo ya moyo ni magumu zaidi na mazito zaidi kuliko matendo ya viungo. Ibn Almunkadir, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, anasema kuwa: "Nilisumbuana na nafsi yangu miaka arobaini mpaka ikaninyookea". 5)Matendo ya moyo yana matokeo mazuri sana, kama vile kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. 6)Matendo ya moyo yana malipo makubwa sana. Abu-dardaa', Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "Kufikiri saa moja ni bora zaidi kuliko kusali usiku mzima". 7)Matendo ya moyo ni yenye kuviendesha viungo. 8)Matendo ya moyo yanayafanya malipo ya ibada za viungo yawe makubwa au kuyapunguza au kuyapoteza, kama vile unyenyekevu katika kusali. 9)Matendo ya moyo yanaweza kuwa mbadala wa ibada ya viungo, kama kunuia kutoa sadaka pamoja na kukosa mali. 10)Malipo ya matendo ya moyo hayana ukomo, kama vile subira. 11)Malipo ya matendo ya moyo yanaendelea pamoja na viungo kusimama au kushindwa kufanya kazi. 12)Matendo ya moyo yanakuwa kabla ya matendo ya viungo na pamoja nayo.

Moyo unapitia hali kadhaa kabla ya viungo kutenda: 1)Haajis. Hii ni wazo mwanzo linapotua moyoni. 2)Khaatira. Hii ni lile wazo linalokaa moyoni. 3)Mazungumzo ya nafsi. Hii ni kusita; je, mtu afanye au aache. 4)Shauku. Ni kuwa na nguvu zaidi kwake hali ya kutenda. 5)Azma. Hii ni nguvu ya makusudio na uamuzi thabiti wa kutenda. Hali tatu za mwanzo hazina malipo katika jambo jema, wala dhambi katika maasi. Ama **Shauku,** kwa jambo zuri mtu ataandikiwa jambo zuri, na kwa jambo baya hatoandikiwa baya. Halafu Shauku inapokuwa Azma, ikiwa ni katika kufanya jambo zuri mtu atalipwa, na ikiwa ni katika kufanya maasi atapata dhambi hata kama hakufanya, kwa sababu utashi pamoja na uwezo unalazimisha kupatikana kwa linalowezekana. Mwenyezi Mungu mtukufu amesema kuwa: *"Kwa yakini, wale ambao wanapenda machafu yaenee kwa ambao wameamini, watapata adhabu iumizayo".* **Sura Annuur (24), aya 19.** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Waislamu wawili wakikutana kwa panga zao, basi muuaji na aliyeuliwa watakuwa motoni. Nilisema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, huyu aliyeua sawa. Sasa ana kosa gani yule aliyeuliwa? Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alisema: Yeye alikuwa na bidii yakutaka kumuua mwenzake".* **Bukhariy.**

**Mtu akiacha maasi baada ya kuazimia kuyafanya, yuko katika mafungu manne:**
**1)** Ni kuyaacha kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu. Huyu atapewa thawabu. **2)**Ni kuyaacha kwa ajili ya kuwaogopa watu. Huyu atapata dhambi, kwa sababu

kuacha maasi ni ibada, na ibada lazima ifanyike kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. **3)**Ni kuyaacha kwa kushindwa bila ya kutumia nyenzo ambazo zinafikisha kwenye maasi hayo. Huyu pia atapata dhambi kwa sababu ya ile nia thabiti. **4)** Ni kuyaacha kwa kushindwa pamoja na kutumia nyenzo ambazo zinafikisha kwenye maasi hayo, lakini makusudio yake hayakutimia. Huyu ataandikiwa dhambi za mafanyaji kamili, kwa sababu utashi thabiti ambao pamoja nao limeletwa jambo linaloweza kufanywa, mwenye utashi huo anahesabika kuwa mfanyaji kamili, kama ilivyotangulia kutajwa katika Hadithi iliyopita. Wakati wowote kutenda kunapoambatana na shauku, inatolewa adhabu juu ya hilo, sawa kutenda kutatangulia au kutakuja baadae. Yeyote aliyefanya jambo la haramu mara moja halafu akaazimia kulifanya tena wakati wowote akiwa na uwezo nalo, huyo atakuwa ni mwenye kuendelea na maasi na ataadhibiwa kwa sababu ya nia hii, hata kama hakurudia kitendo chake.

## Baadhi ya matendo ya nyoyo:

❖ **Nia:** Hiyo ni kwa maana ya utashi na kukusudia. Tendo haliwi sahihi na halikubaliwi isipokuwa tu kwa nia hiyo. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Hakuna vingine isipokuwa kwamba matendo yanazingatiwa kwa nia, na hakuna vingine isipokuwa kwamba kila mtu atapata aliyonuia".* **Bukhariy, Muslim.** Ibni-mubarak, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: "Inawezekana nia ikaifanya nyingi amali ndogo, na inawezekana nia ikaifanya ndogo amali kubwa". Fudhail naye, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: "Hakuna vingine isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka kwako nia yako na utashi wako. Tendo likiwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huitwa Ikhlasi; kitendo kinakuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, mwenginewe hana sehemu katika kitendo hicho. Kitendo kikiwa kwa ajili ya asiyekuwa Mwenyezi Mungu, huitwa Ria (Kujionesha) au Unafiki au majina yasiyokuwa hayo.

**FAIDA:**Watu wote wameangamia isipokuwa tu wenye elimu, na wenye elimu wote wameangamia isipokuwa tu wenye kutenda, na wenye kutenda wote wameangamia isipokuwa tu wenye Ikhlasi. Kazi ya kwanza kwa kila mja anayetaka kumtii Mwenyezi Mungu ni kujifunza nia, halafu aifanye iwe sahihi kwa kutenda, baada ya kufahamu hakika ya ukweli na ikhlasi. Kutenda bila ya nia ni usumbufu, na nia bila ikhlasi ni Ria, na ikhlasi bila ya kuithibitisha imani ni vumbi.

**Matendo ni aina tatu:** 1)Maasi: Nia nzuri katika maasi haiyageuzi maasi hayo kuwa ibada, kwa sababu ya nia hiyo nzuri. Lakini maasi yakiongezewa nia mbaya dhambi zake zinarudufishwa. 2)Mubaha (mambo yenye kuruhusiwa): Hakuna jambo katika mambo ya ruhusa ila tu katika jambo hilo kuna nia moja au nia nyingi. Mtu lau anataka inawezekana jambo hili kuwa ibada. 3)Ibada: Nazo zinafungamana na nia katika msingi wa kusihi kwake na kurudufishwa malipo yake[1]. Akinuia kujionesha, inakuwa maasi na Shirk (ushirika) ndogo na inaweza

---

[1] Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mwenye kukusudia kufanya jambo zuri na asilifanye, Mwenyezi Mungu kwake atamuandikia zuri kamili. Akilikusudia na akalifanya, Mwenyezi Mungu kwake atamuandikia mazuri kumi mpaka mara mia saba mpaka mara nyingi. Na mwenye kukusudia jambo baya na asilifanye, Mwenyezi Mungu kwake atamuandikia zuri kamili, na ikiwa atalikusudia na akalifanya Mwenyezi mungu atamuandikia baya moja".* **Bukhariy na Muslim.** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) pia, Mwenyezi Mungu amfikishie

ikafikia kuwa shirk kubwa, nayo ni namna tatu: 1)Sababu ya kufanya ibada kimsingi ni kuwaonesha watu. Huu ni ushirika na ibada ni batili. 2)Matendo yanakuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, halafu nia ya Ria (kujionesha) ikayaingilia. Kama mwanzo wa Ibada haujengeki juu ya mwisho wake kama vile sadaka, basi mwanzo wake ni sahihi na mwisho wake ni batili. Kama mwisho wa ibada unajengeka juu ya mwisho wake, kama vile sala, basi ibada hiyo iko katika mojawapo ya hali mbili: 1)Mtu kupigana vita na Ria. Katika hali hii, Ria haitakuwa na athari katika ibada. 2)Mtu kuiridhia Ria. Ibada yote itabatilika. 3)Kutokea Ria baada ya ibada. Huu ni wasiwasi usiokuwa na athari yoyote juu ya ibada na juu ya mfanyaji ibada. Kuna aina nyingine nyingi za Ria zilizojificha. Inapasa kuzijua na kujihadhari nazo. Ama makusudio ya mtu katika kufanya jambo jema ikiwa ni dunia aitafutayo, basi malipo yake au dhambi zake ni kwa kadiri ya nia yake. Hali hii ni aina tatu: 1)Sababu ya kufanya jambo jema ni dinia, kama mtu anayewaongoza watu katika sala ili apate pesa. Huyu anapata dhambi. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mwenye kujifunza elimu katika mambo ambayo kwayo anakusudiwa Mwenyezi Mungu, (lakini) mtu hajifunzi elimu hiyo isipokuwa tu kwa kutaka apate kwayo masilahi ya kidunia, hatanusa harufu ya pepo Siku ya Kiyama".* Abudaud. 2)Mtu kufanya jambo jema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya dunia. Huyu ni mpungufu wa imani na Ikhlasi, kama vile mtu anayekwenda kuhiji kwa ajili ya Hija na kwa ajili ya biashara. Malipo yake yatakuwa kwa kadiri ya Ikhlasi yake. Mtu kufanya jambo jema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke yake, lakini akawa anachukua posho inayomsadia kufanya jambo hilo. Huyu malipo ni kamili, hayapungui kwa sababu ya posho anayochukua. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Kwa yakini, kitu chenye haki zaidi katika vitu mlivyovichukulia ujira ni kitabu cha Mwenyezi Mungu".* Bukhariy. Fahamu kuwa wafanyao mema wenye Ikhlasi wako katika daraja. 1)Daraja ya chini ni kufanya ibada kwa ajili ya kupata thawabu au kuogopa adhabu. 2) Daraja ya katikati ni kufanya ibada kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kutii amri zake.

---

rehema na amani, amesema: *"Mfano wa umma huu ni kama mfano wa watu wanne: Mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa mali na elimu, kwa hiyo, anaitumia mali yake katika elimu yake; anaitumia katika haki yake. Na mtu mwengine Mwenyezi Mungu amempa elimu na hakumpa mali. Yeye anasema: Lau kama ningekuwa na mfano wa aliyo nayo huyu ningeifanyia mfano wa anavyofanya. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu akasema: Wawili hao katika malipo ni sawa. Na mtu mwengine Mwenyezi Mungu amempa mali na hakumpa elimu na, kwa hiyo, yeye anakwenda hovyo katika mali yake; anaitumia katika isiyokuwa haki yake. Na mtu mwengine Mwenyezi Mungu hakumpa elimu wala mali. Yeye anasema: Lau kama ningekuwa na mfano wa huyu ningefanya mfano wa ambayo anafanya. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu akasema: Wawili hao katika dhambi ni sawa".* Tirmidhiy. Kauli ya mtu wa pili na wa nne katika Hadithi imeletwa kwa linalowezekana, nayo ile nia pamoja na kutamani. Hilo limedhihiri kwa kauli yao: "Lau kama ningekuwa na mfano wa huyu ningefanya mfano wa ambayo anafanya.". Kwa sababu hiyo, kila mmoja ameunganishwa na swahiba wake katika thawabu au dhambi. Ibn-rajab amesema kuwa: "Kauli yake (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) katika Hadithi: "Wawili hao katika malipo ni sawa" inaonesha kuwa wao wako sawa katika msingi wa malipo ya kutenda bila ya kurudufishwa kwa malipo hayo. Kurudufishwa kunamhusu yule aliyetenda na sio aliyekusudia kutenda na asitende. Wao kama wangekuwa sawa kwa kila njia, yule aliyekusudia kufanya jambo zuri na asilifanye angeandikiwa mazuri kumi, na hilo ni tofauti na matamshi yote ya sheria.

3)Daraja ya juu ni kufanya ibada kwa ajili ya kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu, kumtukuza, kumuadhimisha na kumuogopa. Hii ni daraja ya Wakweli.[1]

❖ **TOBA:** Toba ni wajibu daima, na kufanya dhambi ni maumbile ya mwanadamu. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Kila mwanadamu ni mfanyaji makosa sana, na bora zaidi ya wafanyao makosa sana ni wanaotubu sana".* **Tirmidhiy.** Pia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Lau kama msingefanya dhambi, Mwenyezi Mungu angekuondosheni na angeleta watu (wengine) wafanyao makosa na, kwa sababu hiyo, wakamuomba msamaha Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu akawasamehe".* Muslim. Kuahirisha kutubu na kuendelea na dhambi ni makosa. Shetani anakusudia kumshika mwanadamu kwa kikwazo miongoni mwa vikwazo saba. Kikimshinda kimoja anahamia cha baada yake. Vikwazo hivyo ni hivi: 1)Kikwazo cha Ushirika na ukafiri. 2)Akishindwa, anatumia kikwazo cha Bid'a katika itikadi na katika kuacha kumuiga Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na Swahaba wake. 3)Akishindwa, anatumia kikwazo cha kutenda Dhambi Kubwa. 4)Akishindwa, anatumia kikwazo cha kufanya sana Dhambi Ndogo. 5)Akishindwa, anatumia kikwazo cha kutenda sana mambo ya ruhusa. 6)Akishindwa, anatumia kikwazo cha kufanya ibada ambazo badala yake ni bora na zina malipo makubwa zaidi kuliko hizo afanyazo. 7)Akishindwa, anatumia kikwazo cha kumshakizia mashetani wa kijini na wa kibinadamu.

**Maasi ni mafungu mengi:** 1)Makubwa. Hayo ni yale maasi ambayo yana adhabu duniani, au makemeo makali akhera, au hasira au laana au kukataliwa kwa imani. 1)Madogo. Hayo ni yale maasi yaliyo chini ya hayo makubwa. Kuna sababu zinazoyafanya maasi madogo kuwa makubwa. Muhimu zaidi ya sababu hizo ni hizi: kudumu kuyafanya, au kurudiarudia kuyafanya, au kuyaona kuwa ni madogo, au kuona fahari kuyafanya, au kuyatangaza.

Ni sahihi kutubu kwa kila aina ya dhambi. Kutubu kupo mpaka jua litakapochomoza kutokea magharibi (mpaka Siku ya Kiyama), au roho inapokuwa katika Sakratil Maut (wakati wa kukata roho). Malipo ya mwenye kutubu ni maovu yake kubadilishwa kuwa mema, hata kama kwa wingi wake yatafikia urefu wa mbingu. **Ili Toba ikubaliwe, kuna masharti, nayo ni haya: 1)**Kuiacha dhambi. **2)**Kujuta juu ya dhambi zilizopita. **3)**Kuweka azma madhubuti ya kutorudia dhambi wakati ujao. **1)**Kama dhambi inahusiana na haki za watu, ni lazima haki hiyo iliyodhulumiwa irudishwe kwa wenyewe.[2] **Watu katika Toba ni tabaka**

---

[1] Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Na nimefanya haraka kuja kwako ewe Mola wangu ili uwe radhi".*** **Sura Taha (20), aya 84.** Mtume Musa, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie amani, amekuwa na ari ya kukutana haraka na Mwenyezi Mungu ili Mwenyezi Mungu awe radhi naye, na sio tu kwa kukitii amri zake. Ni miongoni mwa hali hiyo kuwatendea mema wazazi. Daraja ya chini ni kuwafanyia mema kwa ajili ya kuogopa adhabu ya kuwaudhi na kwa ajili ya kutafuta thawabu wa kutendea mema. Daraja ya katikati kuwatendea mema wazazi kwa ajili ya kumtii Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya kuyalipa mema waliyokufanyia; kwa kule kukulea ukiwa mdogo na kwa vile walikuwa sababu ya wewe kuja kwako duniani. Daraja ya juu ni kuwafanyia mema wazazi kwa kuheshimu amri ya Mwenyezi Mungu kwako katika kuwafanyia mema wazazi, na kwa ajili kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumheshimu.

[2] Imepokewa kwamba Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: " Madaftari kwa Mwenyezi amungu ni matatu: Kuna daftari ambalo hatalijali kitu, na kuna daftari ambalo

**nne: 1)**Kuna mwenye kutubu aliye na msimamo katika Toba mpaka mwisho wa umri wake. Haiambii nafsi yake kurudi katika dhambi, isipokuwa tu makosa madogo ambayo mwanadamu hawezi kuyaepuka. Huu ndio msimamo katika Toba, na mwenye Toba hii, ndiye mwenye kutangulia katika kheri. Toba hii inaitwa Toba Ya Kweli, na hii ndio Nafsi Iliyotulia.[1] **2)**Kuna mwenye kutubu aliye na msimamo katika kufanya ibada kubwa, isipokuwa tu yeye hayaachi madhambi yanayomtokea, sio kwa makusudi, lakini amepewa mtihani (majaribu) kwayo bila ya yeye kutanguliza azma ya kutaka kuyafanya. Kila afanyapo jambo katika madhambi hayo, anailaumu nafsi yake, na kujuta kwa kutojikinga na sababu zinazopelekea kwenye madhambi hayo. Hii ndio Nafsi Yenye Kulaumu Sana.[2] **3)**Kuna anayetubu na kuwa na msimamo katika muda fulani, halafu matamanio yake katika dhambi fulani yanamshinda na, kwa hiyo, anazitenda dhambi hizo, isipokuwa tu, pamoja na hayo, anaendelea kufanya ibada. Yeye ameacha dhambi nyingi tu pamoja na kuwa na uwezo wa kuzifanya, ila tamanio moja au mawili yamemshinda nguvu, na yakishatimia anajuta. Lakini, anaiahidi nafsi yake kuwa atatubu na kuacha dhambi hizo. Hii ndio Nafsi Itakayohojiwa. Hatima yake ni hatari, kwa sababu ya kuahirisha kwake, kwani anaweza kufa kabla ya kutubu. Matendo yanazingatiwa kwa mwisho. **4)**Kuna anayetubu na kuwa na msimamo katika muda fulani, halafu anarudi katika kufanya madhambi huku akijimwaga katika madhambi hayo, bila ya kuiambia nafsi yake kuhusu Toba, na bila ya kujuta kwa kuyatenda. Hii ndio Nafsi Inayoamrisha Maovu.[3] Kuna hofu ya mtu huyu kuwa na mwisho mbaya.

❖ **UKWELI:** Ukweli ndio msingi wa matendo yote ya nyoyo. Neno ukweli linatumika maana sita: 1)Ukweli katika kauli. 2)Ukweli katika utashi na makusudio (Ikhlasi). 3)Ukweli katika azma. 4)Ukweli katika kutekeleza azma. 5)Ukweli katika kutenda; kwa maana ya yaliyo ndani yake yaafikiane na yaliyo nje yake, kama unyenyekevu katika sala. 6)Ukweli katika kuthibitisha daraja zote za dini. Hiyo ndio daraja ya juu zaidi na tukufu zaidi, kama ukweli katika hofu, kutaraji, kutukuza, kutokuwa na pupa ya dunia (Zuhudi), kuridhika, kutegemea, kupenda na matendo mengine ya nyoyo. Yeyote aliyesifika na ukweli katika yote yaliyotajwa, basi huyo ndiye Mkweli Sana, kwa sababu amefikia kiwango cha juu cha ukweli. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Jilazimisheni ukweli, kwa sababu ukweli unaongoza kwenda kwenye wema, na wema unaongoza kwenda Peponi. Na mtu ataendelea kuwa mkweli na kuukusudia ukweli mpaka aandikwe kwa Mwenyezi Mungu kuwa ni Mkweli Sana".*

---

hatoacha kitu, na kuna daftari ambalo hatalisamehe. Ama daftari ambalo hatalisamehe ni Ushirika wa kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Kwa yakini, ilivyo ni kwamba yeyote anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu ameharamisha kwake Pepo, na makazi yake ni motoni"*. Sura ..aya…. Na ama daftari ambalo hatajali kitu, ni mja kujidhulumu mwenyewe katika yale mambo yaliopo baina yake yeye na Mola wake. Mwenyezi Mungu atasamehe akitaka. Na ama daftari ambalo hataacha kitu ni dhuluma wanazofanya waja kuwafanyia wenzao. Hapa ni kulipa kisasi, hakuna ujanja". Ahmad, na Hadithi hii ina udhaifu.

[1] Sura Alfajri ( 89), aya 27.

[2] Sura Alqiyama (75), aya 2.

[3] Sura Yusuf (12), aya 53.

Bukhariy, Muslim. Mtu ambaye imetatizika kwake haki na, kwa sababu hiyo, akawa mkweli kwa Mwenyezi Mungu katika kuitafuta, bila ya mapenzi potofu katika nafsi yake, basi aghlabu huwa anawezeshwa kuipata haki. Kama hakuipata, Mwenyezi Mungu humsamehe. Kinyume cha ukweli ni uongo. Mwanzo wa uongo unavyotembea katika nafsi ni kulekea kwenye ulimi na kuuharibu. Halafu unaelekea kwenye viungo na kuharibu matendo yake, kama uluvyouharibia ulimi maneno yake. Kwa sababu hiyo, uongo unaenea maneno yake, vitendo vyake na hali zake na, kwa hiyo, uovu unamtawala.

❖ **KUPENDA:** Kwa kumpenda Mwenyezi Mungu, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake na waumini unapatikana utamu wa imani. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mambo matatu, mtu ambaye atakuwa nayo, atapata kwayo utamu wa imani:* **1)***Mwenyezi Mungu na Mtume* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *wake wawe wanapendwa zaidi kwake kuliko wasiokuwa wao, na* **2)***Kumpenda mtu (ambaye) hampendi isipokuwa tu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, na* **3)***Kuchukia kurejea kwenye ukafiri baada ya kuwa Mwenyezi Mungu amemuokoa katika ukafiri huo, kama mtu anavyochukia kutumbukizwa katika moto".* **Bukhariy, Muslim.**

Mti wa upendo ukipandwa katika moyo na ukamwagiliwa kwa maji ya Ikhlasi na kumuiga Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, utazaa aina mbali mbali za matunda na kutoa mazao yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake. Aina za upendo ni nne: 1)Kumpenda Mwenyezi Mungu. Huu ndio msingi wa imani. 2)Kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kupenda huku ni wajibu.[1] 3)Kupenda pamoja na Mwenyezi Mungu. Mapenzi haya ni kumshirikisha asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika mapenzi ya wajibu, kama washirika waipendavyo miungu yao. Mapenzi hayo ndio msingi wa Ushirika. 4)Mapenzi ya maumbile, kama kuwapenda wazazi, watoto, chakula n.k. Mapenzi hayo yanafaa. Ili Mwenyezi Mungu akupende, usiipapatikie

---

[1] Watu kwa mujibu wa kupendwa na kuchukiwa (Alwalaa Walbaraa) ni mafungu matatu: 1)Kuna wanaopendwa mapenzi safi yasiyokuwa na kuchukia. Hao ni waumini halisi, kama vile Mitume na Wakweli wakiongozwa na Bwana wetu Muhammad, wake zake, mabinti zake na Swahaba wake. 2)Kuna wanaochukiwa wakati wote. Hao ni makafiri, wafanyao ushirika na wanafiki. 3)Kuna wanaopendwa kwa upande fulani na kuchukiwa kwa upande mwingine. Hao ni waumini wafanyao maasi. Wanapendwa kwa sababu ya imani waliyonayo, na wanachukiwa kwa sababu ya maasi waliyonayo. Kuwapenda makafiri ni namna mbili: 1)Kuna mapenzi yanayolazimisha kuritadi na kutoka katika Uislamu. Haya ni mapenzi ya kuwapenda kwa ajili ya dini yao. 2)Kuna mapenzi ambayo ni haramu, lakini hayamtoi mtu katika Uislamu. Haya ni mapenzi ya kuwapenda makafiri kwa sababu ya mambo ya dunia yao. Wakati mwingine kunatokea kuchanganya na kutatizika kati ya kuishi vizuri na makafiri (Wasio katika Vita na Waislamu) na kati ya kuwachukia na kuwakata. Ni lazima kutofautisha kati ya mambo hayo mawili. Kuwatendea haki, kuishi nao vizuri bila ya mapenzi ya ndani, kama kumuonea huruma mnyonge wao, kuwa na kauli nzuri kwao kwa njia ya kuwa mpole kwao na kuwa na huruma, ni jambo linalofaa. Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu jambo hilo amesema kuwa: *"Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuhusu wale ambao hawakupigeni katika dini na hawakukutoeni katika nyumba zenu, (hakukatazeni) kuwafanyia wema na kuwafanyia uadilifu".* **Sura Almumtahina (60), aya 8.** Ama kuwachukia na kuwafanya adui ni jambo jingine. Jambo hilo ameliamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kauli yake isemayo kuwa: *"Enyi ambao mmeamini, msiwafanye maadui wangu na maadui wenu wapenzi mnaokutana nao kwa upendo".* **Sura Almumtahina (60), aya 1.** Kwa hiyo, inawezekana kufanya uadilifu katika kushirikiana nao pamoja na kuwachukia na kutowapenda, kama alivyofanya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa Wayahudi wa Madina.

dunia. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Usiipapatikie dunia, Mwenyezi Mungu atakupenda"*. Ibnimaajah.

❖ **KUTEGEMEA:** Ni kuuegemeza moyo na kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kupata jambo linalotakwa, na kuondoa jambo linalokera, pamoja na kuwa na imani na Mwenyezi Mungu na kutumia sababu zinazoruhusiwa kisheria. Kuacha kuuegemeza moyo ni kuitia dosari imani ya kumwamini Mungu mmoja (Tauhiid), na kuacha kutumia sababu zinazoruhusiwa kisheria ni uzembe na upungufu katika akili. Mahali pa kutegemea ni kabla ya kutenda, na ndio matunda ya imani. Aina za kutegemea ni tatu: 1)Utegemezi wajibu. Huu ni utegemezi wa kumtegemea Mwenyezi Mungu katika jambo ambalo hakuna aliwezaye ila Mwenyezi Mungu tu, kama kuponya wagonjwa. 2)Utegemezi haramu. Utegemezi huu uko katika aina mbili: a)Ushirika Mkubwa. Huu ni ushirika wa kuzitegemea moja kwa moja sababu, na kwamba sababu hizo pekee ndizo zenye kuathiri katika kuleta manufaa au kuondoa madhara[1]. b)Ushirika Mdogo, kama kumtegemea mtu katika riziki, bila ya kuwa na itikadi kwamba yeye pekee ndiye mwenye kusababisha, lakini mafungamano yake na riziki hiyo ni zaidi ya itikadi kwamba ni sababu tu. 3)Utegemezi unaofaa. Huu ni utegemezi wa mtu kumuwakilisha mtu mwengine na kumtegemea katika kutenda jambo analoliweza, kama kuuza na kununua. Lakini haifai kumwambia: Nimemtegemea Mwenyezi Mungu halafu nimekutegemea wewe. Bali amwambie: Nimekuwakilisha.

❖ **KUSHUKURU:** Ni kuonekana athari ya neema za Mwenyezi Mungu kwa mja; katika moyo wake kwa kuamini, na katika ulimi wake kwa kusifia, na katika viungo vyake kwa kufanya ibada. Kushukuru ndio muradi wa nafsi yake na subira

---

[1] Je, kutegemea kunapingana na kutumia sababu? Kuna aina: 1)Kutafuta manufaa yaliyokosekana, na yako katika namna tatu: a)Sababu yenye yakini, kama kuoa kwa ajili ya kutaka mtoto. Kuacha kutumia sababu hii ni wendawazimu, na kamwe, sio katika kumtegemea Mwenyezi Mungu. b)Sababu zisizokuwa na yakini, lakini aghlabu matokeo hayapatikani bila ya sababu hizo, kama mtu anayesafiri jangwani bila ya mahitaji muhimu. Kitendo chake hiki sio kutegemea, na kuchukua kwake mahitaji muhimu ni jambo lililo amrishwa, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu aliposafiri alibeba huduma muhimi na kukodi muongozaji wa kumuelekeza mji wa Madina. c)Sababu zinazodhaniwa kufikisha kwenye matokeo bila ya yakini ya wazi, kama mtu ambaye anamaliza juhudi zote katika maandalizi ya kina katika kutafuta riziki na njia zake. Huyu hajatoka katika kumtegemea Mwenyezi Mungu. Kuacha kutafuta riziki, kamwe sio katika kumtegemea Mwenyezi Mungu. Omar, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "Mtegemeaji ni yule ambaye anapanda mbegu halafu anamtegemea Mwenyezi Mungu". 2)Kuhifadhi kitu kilchopo. Mtu ambaye amepata chakula halali, kukihifadhi kwake chakula hicho hakumtoi katika kutegemea, hasa kama ana familia. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa akiuza tende za Banin-nadhiir kuitengea familia yake chakula cha mwaka wao mzima. 3)Kuzuia madhara ambayo hayajatokea. Kuacha sababu za kuzuia madhara sio sharti la kutegemea, kama kuvaa nguo za vita, kumfunga ngamia. Katika hayo yote mtu anategemea msababishaji na sio sababu, na anakuwa radhi na yote ambayo Mwenyezi Mungu atamhukumia. 4)Kuondoa madhara yaliyokwisha tokea. Aina hii iko katika mafungu matatu: a)Sababu kuwa haina mjadala, kama vile maji yenye kuondosha kiu. Kuacha kuyanywa, kamwe sio katika kutegemea. b)Sababu kuwa inadhaniwa tu, kama vile kupiga chuku, na mfano wake. Kuifanya hakupingani na kutegemea, kwa sababu Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ametumia dawa, na ameamrisha kutumia dawa. c)Sababu kuwa inafikirika tu, kama vile kujitibu kwa moto wakati wa uzima, ili mtu asije akaugua. Kufanya hivi kunapingana utegemezi kamili.

ndio nyenzo kwa mwenginewe. Shukurani zinakuwa kwa moyo, ulimi na viungo. Maana ya kushukuru ni kuitumia neema katika kumtii Mwenyezi Mungu.

❖ **SUBIRA:** Ni kuacha kulalamika kutokana na maumivu ya tatizo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kuyapeleka malalamiko hayo kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Hakuna vingine isipokuwa kwamba wenye subira hupewa malipo yao bila ya hisabu".*** **Sura Azzumar (39), aya 10.** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Mwenye kutaka kuvumilia, Mwenyezi Mungu humuwezesha kuvumilia, na hakuna yeyote aliyepewa tuzo bora zaidi na kunjufu zaidi kuliko subira".* Bukhariy, Muslim. Omar, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "Sikupewapo mtihani wa tatizo lolote isipokuwa kwamba katika tatizo hilo Mwenyezi Mungu ana neema nne kwangu: wakati haukuwa katika dini yangu, na wakati haukuwa mkubwa sana, na wakati sikunyimwa kuridhika nao, na wakati nataraji kupata thawabu kwa ajili yake". Subira ni daraja nyingi. Ya chini zaidi ni kuacha kulalamika pamoja na kuchukia. Ya katikati ni kuacha kulalamika pamoja na kuridhika. Ya juu zaidi ni kumshukuru Mwenyezi juu ya tatizo. Aliyedhulumiwa akimuombea mabaya aliyemdhulumu, amejilipizia kisasi na kuchukua haki yake, na hakuwa na subira. **Subira** ni aina mbili: 1)Ya mwili, na hii sio makusudio yetu hapa. 2)Ya nafsi juu ya matamanio ya maumbile na mahitajio ya mapenzi ya nafsi.[1] Yote yanayomkuta mwanadamu duniani hayaachi kuwa mojawapo ya aina mbili hizi: a)Kuna yanayoafikiana na mapenzi ya nafsi. Inahitajika subira katika kutekeleza haki ya Mwenyezi Mungu katika mambo hayo, ikiwemo kushukuru na kutofanya lolote katika hayo katika kumuasi Mwenyezi Mungu. a)Kuna yasiyoafikiana na mapenzi ya nafsi, na hayo ni mafungu matatu: 1)Uvumilivu katika kumtii Mwenyezi Mungu. Lililo wajibu katika uvumilivu huu ni kutenda ya faradhi, na la kupendekezwa ni kufanya ya suna. 2)Uvumilivu katika kuacha kumuasi Mwenyezi Mungu. Lililo wajibu katika uvumilivu huu ni kuacha ya haramu, na la kupendekezwa ni kuacha ya makuruhu. 3)Uvumilivu juu ya mipango ya Mwenyezi Mungu. Lililo wajibu katika hayo ni kuuzia ulimi usilalamike, na kuuzia moyo usipinge na kuchukia alilolipanga Mwenyezi Mungu, na kuvizuia viungo visijiingize katika yale yasiyomridhisha Mwenyezi Mungu, ikiwa ni pamoja na kumlilia maiti kwa mayowe, kuchana nguo, kujipiga usoni na yasiyokuwa hayo. La kupendekezwa katika hayo ni ridhaa ya moyoni ya kuridhika na aliyoyapanga Mwenyezi Mungu. **Yupi kati ya wawili hawa ni bora zaidi? Tajiri mwenye kushukuru na fukara mvumilivu?** Tajiri atumiapo mali yake katika kumtii Mwenyezi Mungu au akaiweka akiba mali hiyo kwa ajili ya hilo, huyo ni bora zaidi kuliko masikini. Kama matumizi yake mengi ni katika mambo ya ruhusa, basi masikini ni bora zaidi. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema

---

[1] Subira ya aina hii ikiwa ni ya kujizuia na matamanio ya tumbo na tupu huitwa Iffah (kujizuia kwa heshima), na ikiwa katika vita huitwa ushujaa, na ikiwa katika kuzuia hasira huitwa upole, na ikiwa katika kuficha jambo huitwa kuficha siri, na ikiwa katika maisha ya ziada huitwa zuhudi (kutopapatikia dunia), na ikiwa katika kuacha baadhi ya anasa za dunia huitwa kukinai (kuridhika).

na amani, amesema kuwa: *"Mlishaji mwenye kushukuru yuko katika daraja ya mfungaji mwenye subira"*. Ahmad.

❖ **KURIDHIKA:** Ni kukinai kitu na kutosheka nacho. Mahali pake ni baada ya kitendo. Kuridhika na hukumu ya Mwenyezi Mungu ni miongoni mwa daraja za juu sana za watu waliokribu na Mwenyezi Mungu (Muqarrabiin), na ni katika matunda ya upendo na kutegemea. Kumuomba Mwenyezi Mungu aondoshe jambo linalokera hakupingani na kuridhika nalo.

❖ **UNYENYEKEVU:** Ni heshima, ulegevu na udhalili. Hudhaifa, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "Jihadharini na unyenyekevu wa kinafiki. Aliulizwa: Na ni upi unyenyekevu wa kinafiki? Alisema: Ni kuuona mwili mnyenyekevu, na moyo sio mnyenyekevu". Pia Hudhaifa, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "La kwanza kabisa mtakalolipoteza katika dini yenu ni unyenyekevu". Ibada yoyote ambayo inatakiwa ndani yake uwepo unyenyekevu, basi malipo kwa ajili ya ibada hiyo ni kwa kadiri ya unyenyekevu uliopo ndani yake, kama vile sala. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kumuelezea mwenye kusali kwamba anaweza asipate katika sala yake isipokuwa tu nusu yake, robo yake, khumsi yake (sehemu yake ya tano), ushri yake (sehemu yake ya kumi). Pia inawezekana asipate kitu chochote katika sala yake, kwa sababu ya kutokuwepo kwa unyenyekevu kamili.

❖ **KUTARAJI:** Ni kuitazamia rehema pana ya Mwenyezi Mungu. Kinyume chake ni kukata tamaa. Kufanya ibada kwa kutaraji rehema ni jambo tukufu zaidi kuliko kufanya ibada kwa kuogopa adhabu, kwa sababu kutaraji kunarithisha kumdhania vizuri Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa: *"Mimi niko kwenye dhana ya mja wangu kwangu"*. Muslim. Kutaraji ni daraja mbili: **Daraja ya Juu:** Huyu ni yule aliyefanya ibada na kutaraji thawabu za Mwenyezi Mungu. Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu: "*Na wale ambao wanatoa vile walivyopewa na ilhali nyoyo zao ni zenye woga*". Sura Almuuminun (23), aya 60. Je, huyu ni ambaye anaiba na anazini na anakunywa pombe na ilhali yeye anamuogopa Mwenyezi Mungu? Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alisema: Hapana ewe Binti wa (Abubakar) Assiddiik. Na lakini hao ni wale ambao wanasali na wanafunga na wanatoa sadaka na ilhali wao wanachelea (ibada hizo) kutokubaliwa kwao "*Hao wanafanya haraka katika mambo ya kheri*". Sura Almuuminun (23), aya 61.". Tirmidhiy. **Daraja ya Chini:** Ni yule mwenye dhambi anayetubu, huku akitaraji msamaha wa Mwenyezi Mungu. Ama mfanyaji maasi, anaye endelea na maasi, aliyeacha kutubu na anataraji rehema ya Mwenyezi Mungu, huko ni kutamani na sio kutaraji. Aina hii inashutumiwa, na ile ya kwanza inasifiwa. Muumini amekusanya kufanya mazuri na kuogopa, na mnafiki amekusanya kufanya maovu na amani.

❖ **HOFU: Ni kero inayoipata nafsi kwa kutegemea kutokea jambo la kuchukiza**. Likithibitika jambo la kuchukiza, huitwa woga, na kinyume chake ni amani. Hofu sio kinyume cha kutaraji, lakini ni sababu kwa njia ya kuogopa , na kutaraji ni sababu kwa njia ya utashi. Ni lazima kukusanya baina ya kupenda, kuogopa na kutaraji. Ibnil-qayyim amesema kuwa: "Moyo katika kwenda kwake kuelekea kwa Mwenyezi Mungu ni kama ndege. Upendo ndio kichwa chake, na

hofu na kutaraji ndio mabawa yake. Hofu ikikaa moyoni, inaunguza sehemu za matamanio, na kuifukuza itoke humo". Hofu ya wajibu ni ile inayosababisha kutenda ya wajibu na kuacha ya haramu. Hofu inayopendekezwa ni ile inayosababisha kutenda ya suna, na kuacha ya makuruhu. Hofu ni aina nyingi: 1)Hofu ya kificho na ya uungu. Aina hii inapasa iwe kwa Mwenyezi Mungu pekee. Kuielekeza sehemu ya hofu hii kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni Ushirika Mkubwa, kama kuwaogopa miungu wa washirika kudhuru au kuleta jambo la kuudhi. 2)Hofu ya haramu. Hii ni hofu ya kuacha jambo la wajibu, au kufanya jambo la haramu kwa kuwaogopa watu. 3)Hofu inayofaa, kama hofu ya maumbile ya kumuogopa mbwamwitu, na wenginewe.

❖ **ZUHUDI:** Ni kuuondoa utashi katika kitu ili kukiendea kilichokuwa bora zaidi kuliko hicho. Kuipa nyongo dudia, kunaupa raha moyo na mwili, na kuipapatikia dunia kunaongeza kero na huzuni. Kuipenda dunia ndio msingi wa kila dhambi, na kuichukia ndio sababu ya kila ibada. Kuipa nyongo dunia ni kuitoa dunia moyoni mwako, na sio kuitoa mkononi mwako pamoja na kuwa moyo wako umefungamana nayo, jambo ambalo ndio Zuhudi ya wajinga. Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "***Mali njema ni ile ilioko kwa mtu mwema***". **Ahmad**. **Fukara pamoja na mali ana hali tano:** **1)**Anakimbia kuchukua mali kwa kuichukia na kujilinda na shari yake na kushughulishwa nayo. Mwenye hali hii anaitwa "Mwenye Zuhudi". **2)** Hana furaha kwa kuipata mali, na hakereki kero ambayo anapata maudhi kwayo. Mwenye hali hii anaitwa "Mwenye kuridhika". **3)** Kupata mali ni jambo analolipenda zaidi kuliko kuikosa kwa kuwa anaitaka, lakni kuitaka kwake hakumfanyi aitafute. Lakini ikimjia hivi hivi anaichukua na kuifurahia. Kama ikihitaji usumbufu katika kuitafuta, hajishughulishi na usumbufu huo. Mwenye hali hii anaitwa "Mwenye kukinai". **4)** Kuacha kwake kuitafuta mali ni kwa sababu ya kushindwa, vinginevyo ni kwamba anaitaka sana. Kama angepata njia ya kuipata kwa usumbufu angeitafuta. Mwenye hali hii anaitwa "Mwenye Pupa". **5)** Kuwa na ulazima wa mali anayoikusudia, kama mtu mwenye nja, na kama mtu aliye uchi ambao wanahitaji chakula na mavazi. Mwenye hali hii anaitwa "Mwenye kushikika /Muhitaji".

# MAHOJIANO TULIVU

Mtu mmoja, jina lake likiwa ni *Abdallah* (Mja wa Mwenyezi Mungu), alikutana na mtu mwengine ambaye jina lake ni *Abdun-nabiy* (Mja wa Mtume). (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Abdallah alilipinga jina hili (la Abdun-nabiy) nafsini mwake na kusema: Vipi mja anaunasibisha uja wake kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu? Halafu akamwambia Abdun-nabiy akisema: Je, wewe unamwabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu? Abdun-nabiy akasema: Hapana. Mimi siabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Mimi ni Mwislamu na ninamwabudu Mwenyezi Mungu pekee.

**Abdallah** Alisema**:** Kwa hiyo, ni la nini jina hili linalofanana na majina ya Wakristo katika kujiita kwao kwa majina ya Mja wa Kristo? Na hakuna la kushangaza, kwani Wakristo wao wanamwabudu Issa, Mwenyezi Mungu amfikishie amani. Atakayelisikia jina lako, itamjia haraka akilini mwake kwamba wewe unamwabudu Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na ilhali hii sio itikadi ya Mwislamu.

**Abdun-nabiy** akasema: Lakini Mtume Muhammad, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni kiumbe bora zaidi na ni Bwana wa Mitume. Sisi tunajiita jina hili kwa kutaka baraka na kutaka kuwa karibu na Mwenyezi Mungu kwa kutumia cheo cha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake na nafasi yake kwake. Kwa hiyo, tunaomba kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, *Shafaa'* (Uombezi) kwa sababu ya nafasi yake kwa Mola wake Mtukufu. Usishangae, kwani kaka yangu jina lake ni *Abdul-hussein* (Mja wa Hussein) na kabla yake baba yangu jina lake ni Abdur-rasul (Mja wa Mtume). (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Kuitana majina haya ni jambo la zamani na limeenea kwa watu. Tumewakuta wazazi wetu wakiwa na haya. Usiwe na msimamo mkali katika suala hili, kwani jambo lenyewe ni dogo na dini ni nyepesi.

**Abdallah** alisema: Hili ni jambo jingine baya na kubwa zaidi kuliko lile la kwanza. Jambo hilo baya zaidi ni kule kuomba kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu jambo ambalo hakuna aliwezaye ila Mwenyezi Mungu tu; sawa huyu anayeombwa awe ni Mtume Muhammad, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, au mtu mwengine mwema, kama Hussein au mwenginewe. Jambo hilo linapingana na Tawhiid na linapingana na maana ya "Laa ilaaha illallaah". Nitakuuliza baadhi ya maswali ili ukubainikie ukubwa wa jambo lenyewe na athari za kujiita jina hili na mfano wake. Sina lengo na makusudio isipokuwa tu: **1)** Haki na kuifuata. **2)**Kubaini batili na kuiepuka. **3)** Kuamrisha mema na kukataza maovu. Mwenyezi Mungu tu ndiye muombwa msaada na mtegemewa. Hakuna hila (ujanja wa kuepuka maovu) wala nguvu (za kufanya mema) isipokuwa tu kwa msaada wa Mwenyezi Mungu tu. Lakini, ninakukumbusha kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Kwa yakini, hakuna vingine isipokuwa kwamba kauli ya waumini wanapolinganiwa (wanapohubiriwa waelekee) kwa Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake ili watoe hukumu baina yao inatakiwa iwe (hivi): Tumesikia na kutii".*** **Sura Annuur 24, aya 51.** Na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Ikiwa mtazozana katika jambo (lolote) basi lirejesheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume ikiwa nyinyi mnamwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho".*** **Sura An-nisaa 4, aya 59.**

**Abdallah**:Wewe umesema kuwa unampwekesha Mwenyezi Mungu na kukiri kuwa *Laa ilaaha illallah* (Hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Mwenyezu Mungu tu).

Je, unaweza kunifafanulia maana yake?

**Abdun-nabiy**: Tawhiid ni kuamini kwamba: **1)** Mwenyezi Mungu yupo. **2)** Yeye ndiye ambaye ameumba mbingu na ardhi. **3)** Yeye ndiye mletaji uhai na mauti. **4)** Yeye ndiye mwendesha ulimwengu. **5)** Yeye ndiye Mtoaji riziki, Mjuzi, Mjuzi zaidi na Muweza.

**Abdallah**: Ingekuwa hii tu ndio tafsiri ya Tawhiid, basi Firauni na watu wake, Abujahli na wengineo wangekuwa waumini, kwa sababu waliyajua haya. (uliyoyataja) kama walivyo washirikina wengine. Firauni ambaye alidai uungu, alikuwa anakiri na kuamini nafsini mwake kwamba Mwenyezi Mungu yupo na yeye ni mwendeshaji ulimwengu. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Na wakazikanusha (aya, alama, ishara na dalili zetu) kwa dhulma na kiburi na ilhali nafsi zao zimezikubali"***. Sura An-namli 27, aya 14. Kukubali huku kulijitokeza wazi wakati gharika ilipomkumba Firauni (Sura Yunus 10, aya 90)

Kwa hakika Tawhiid ambayo kwa ajili yake Mitume waliletwa, vitabu viliteremshwa na Waquraishi kupigana nao vita kwa sababu ya Tawhidi hiyo ni: Kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa ibada. Ibada ni neno linalokusanya kila jambo analolipenda Mwenyezi Mungu na kuliridhia; iwe ni kauli au vitendo; vya dhahiri au vya siri. Neno "anayestahiki kuabudiwa" katika "*Laa ilaaha illaLlah* = Hapana anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu" lina maana ya: Muabudiwa ambaye ibada haifai kufanywa isipokuwa kwa ajili yake tu.

**Abdallah**: Je, unajua ni kwa nini Mitume, na wa mwanzo wao akiwa Nuh, Mwenyezi Mungu awafikishie amani, waliletwa duniani?

**Abdun-nabiy**: Mitume waliletwa ili wawalinganie washirikina wamwabudu Mwenyezi Mungu pekee na kuacha kila kinachoshirikishwa naye.

**Abdallah**: Na ni ipi sababu ya ushirikina wa watu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Nuh?

**Abdun-nabiy**: Sijui.

**Abdallah**: Mwenyezi Mungu alimtuma Nuh kwa watu wake pale walipokiuka mipaka katika kuwatukuza watu wema; akina Wadi, Suwaa', Yaghuuth, Yauuk na Nasri.

**Abdun-nabiy**: Hivi una maana kwamba Wadi, Suwaa', Yaghuuth, Yauuk na Nasri ni majina ya watu wema na sio majina ya mabeberu makafiri?

**Abdallah**: Ndio. Haya ni majina ya watu wema ambao watu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Nuh waliwafanya Miungu na Waarabu kuwafuata katika hilo. Ushahidi wa hayo ni yale aliyoyasimulia Bukhariy akinukulu kutoka kwa Ibn-abasi, Mwenyezi Mungu awawiye radhi yeye na baba yake, akisema kuwa: ***"Masanamu ambayo yalikuwa kwa watu wa Nuhu yakawa kwa Waarabu baadae. Ama Wadi lilikuwa ni (sanamu) la (kabila la) Kalb huko Daumat-aljandal. Na ama Suwaa' lilikuwa ni (sanamu) la (kabila la) Hudhail. Na ama Yaghuuth lilikuwa ni (sanamu) la (kabila la) Murad halafu likawa la (kabila la) Bani-ghutaif huko Al-jouf katika (sehemu za) Sabai. Na ama Yauuk lilikuwa la (kabila la) Hamadan. Na ama Nasr lilikuwa la (kabila la) Himyar katika familia ya Dhil-kalaai. Haya ni majina ya watu wema katika watu wa (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Nuh. Walipofariki, shetani aliwashawishi watu wao kuwa: Jengeni masanamu katika makazi yao waliyokuwa wakikaa, na yapeni masanamu hayo majina yao. Kwa hiyo, walifanya hivyo na lakini masanamu hayo hayakuabudiwa. Walipofariki hao (walioyajenga) na elimu kutoweka, masanamu hayo yaliabudiwa"***. Bukhariy.

**Abdun-nabiy**: Haya ni maneno ya ajabu.

**Abdallah**: Unaonaje, nikuambie ya ajabu zaidi kuliko hayo? Fahamu kuwa Mwenyezi Mungu alimtuma Muhammad Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa mwisho, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwa watu wanao omba msamaha, wanaofanya ibada, wanaotufu, wanaofanya Saa'yi, wanaohiji na wanaotoa sadaka. Lakini walikuwa wanavifanya baadhi ya viumbe kuwa viombezi (mediators) baina yao na baina ya Mwenyezi Mungu wakisema kwamba: Tunataka kwa viumbe hivyo vituweke karibu na Mwenyezi Mungu na tunataka uombezi wao kwake. Viumbe hivyo ni kama vile Malaika, (Mtume) Issa, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie amani na watu wema wengine. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu alimtuma Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akawafundishe upya dini ya baba yao Ibrahimu, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, na kuwafahamisha kuwa itikadi na hali hii ya kutaka kuwa karibu (na Mwenyezi Mungu) ni haki halisi ya Mwenyezi Mungu. Yoyote kati ya hizo haifai kuelekezwa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Yeye pekee asiye na mshirika ndiye Muumba. Hakuna anayetoa riziki ila yeye tu. Mbingu zote saba na vilivyomo ndani yake, na ardhi zote saba na vilivyomo ndani yake ni viumbe vyake na viko chini ya udhibiti na umiliki wake. Hata Miungu ambao washirikina wanawaabudu wanakiri kuwa wako chini ya udhibiti na ufalme wake.

**Abdun-nabiy**: Haya ni maneno hatari na ya ajabu. Hivi, yana hoja yoyote?

**Abdallah**: Hoja ni nyingi. Miongoni mwa hoja hizo ni hizi: **1)** Kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu isemayo kuwa: "***Sema: Ni nani anayekupeni riziki kutoka mbinguni na ardhini? Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona? Na ni nani anayetoa kilicho hai kutoka katika kilichokufa na anayetoa kilichokufa kutoka katika kilicho hai? Na ni nani anaye endesha mambo? Watasema: Ni Mwenyezi Mungu. Sema: Mbona hamumchi Mungu?***". Surat Yunus 10, aya 31. **2)** Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "***Sema: Ni ya nani ardhi na vilivyomo ndani yake ikiwa nyinyi mnajua? Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Sema: Mbona hamkumbuki?. Sema: Ni nani Mola wa mbingu saba na Mola wa Arshi Tukufu?. Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Sema: Mbona hamumchi Mungu? Sema: Ni nani ambaye uko mkononi mwake ufalme wa kila kitu na ilhali yeye analinda na halindwi, ikiwa nyinyi mnajua? Watasema: (Uwezo huo) Ni wa Mwenyezi Mungu. Sema: Vipi basi mnarogwa?***'. Suratul-Muuminun 23, aya 84-89.

**3)**Washirikina walikuwa wakileta Talbiyah katika Hija kwa kusema: "*Labbaykallaahumma labbayk. Labbayka laa shariika lak. Illaa shariikan huwalak. Tamlikuhuu wamaamalak= Nimekuitika ewe Mola wangu. Nimekuitika. Nimekuitika. Huna mshirika, isipokuwa mshirika wako unayemmiliki yeye na anachokimiliki*".

Kukiri kwa washirikina kwamba Mwenyezi Mungu tu ndiye mwendeshaji wa ulimwengu – kukiri ambako kunaitwa Tawhiid rubuubiyya – hakukuwaingiza washirikina hao katika Uislamu. Aidha kuwakusudia kwao Malaika au Mitume au Mawalii wakitaka Uombezi wao na kutaka kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, ndio jambo ambalo lilihalalisha damu zao na mali zao. Kwa sababu hii, inakuwa wajibu: **a)** Kuelekeza dua zote kwa Mwenyezi Mungu. **b)** Kuelekeza Nadhiri zote kwa Mwenyezi Mungu. **c)** Kuelekeza uchinjaji wote kwa Mwenyezi Mungu. **d)** Kuelekeza maombi yote ya msaada kwa Mwenyezi Mungu, na pia aina nyingine zote za ibada zielekezwe kwa Mwenyezi Mungu.

**Abdun-nabiy**: Ikiwa Tawhiid sio kukubali kwamba Mwenyezi Mungu yupo na

ndiye mwendeshaji ulimwengu kama unavyodai, Tawhiid ni ipi?

**Abdallah**: Tawhiid ambayo kwa ajili yake Mitume walitumwa na washirikina wakakataa kuikubali ni: Kumpwekesha Mwenyezi Mungu (kumkusudia Mwenyezi Mungu pekee) kwa ibada. Aina yoyote ya ibada haitakiwi kuelekezwa isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu tu; kama vile kuomba, kuweka Nadhiri, kuchinja, kuomba msaada, kuomba wokovu nk.. Tawhiid hii ndio maana ya kauli yako: *"Laa ilaaha illallaah* = Hakuna (Mola) anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Mola kwa washirikina wa Kiquraishi ni yule ambaye anakusudiwa kwa mambo haya yaliyopita kutajwa; sawa awe ni Malaika au Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) au Walii au mti au kaburi au Jini. Waquraishi hawakuwa wakikusudia kwamba Mola ni: Muumbaji, Mtoaji riziki, Mwendesha ulimwengu. Wao wanajua, kwa yakini kabisa, kwamba hayo ni ya Mwenyezi Mungu pekee kama nilivyokwisha tangulia kukueleza. Kwa hiyo, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliwaendea akiwahubiria tamko la Tawhiid ambalo ni: "Laa ilaaha illallaah = Hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, na makusudio ni maana yake na sio kulitamka tu.

**Abdun-nabiy**: Kama vile unataka kusema kwamba washirikina wa Kiquraishi walikuwa wanajua zaidi maana ya *Laa ilaaha illallaah* kuliko Waislamu katika wakati wetu huu?

**Abdallah**: Ndio. Hii ndio hali yenyewe inayouma! Makafiri wajinga wanajua kwamba makusudio ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika tamko hili ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu kwa ibada, kuvikataa vingine vinavyoabudiwa badala ya Mwenyezi Mungu na kujitenga navyo. Pamoja na kuamini kwa washirikina kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mwendeshaji ulimwengu, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alipowaambia: Semeni: *Laa ilaaha illallaah, walisema: "**Hivi amefanya Miungu wote kuwa Mungu mmoja? Bila shaka, hili ni jambo la ajabu sana!**"*.Surat Saad 38, aya 5. Ikiwa makafiri wajinga wanajua hivyo, ajabu ni kwa anayedai kuwa yeye ni Mwislamu na ilhali hajui ile maana waliyoijua makafiri wajinga katika tafsiri ya tamko hili. Bali anadhani kwamba maana hiyo ni kutamka tu herufi zake bila ya moyo kuitakidi maana yoyote. Aliye mwerevu katika hao, wanaodai kuwa ni Waislamu, anadhani kuwa maana yake ni kwamba: Hakuna atoaye riziki isipokuwa Mwenyezi Mungu tu na hakuna anaye endesha mambo isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Hakuna kheri yoyote kwa watu wanaodai kuwa ni Waislamu na ilhali makafiri wa Kiquraishi walio wajinga wanaijua zaidi maana ya Laa ilaaha illallaah kuliko wao!

**Abdun-nabiy**: Lakini mimi simfanyii ushirikina Mwenyezi Mungu. Bali ninakiri moyoni na kutamka kinywani kwamba hakuna anayeumba, kutoa riziki, kunufaisha na kudhuru isipokuwa Mwenyezi Mungu tu na kwamba Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, hana uwezo wa kumiliki madhara au manufaa kwa nafsi yake achilia mbali Ali, Hussein, Abdulqadir na wengineo. Lakini mimi ni mwenye dhambi na Watu Wema wanayo hadhi mbele ya Mwenyezi Mungu, na mimi namuomba Mwenyezi Mungu kwa hadhi yao hiyo kwake.

**Abdallah**: Nakujibu tena kwa yale yale niliyotangulia kukujibu kwamba wale ambao Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipigana nao vita walikuwa wanakubali hayo uliyoyataja, na pia wanakubali kuwa masanamu yao hayana uwezo wa kufanya chochote, isipokuwa tu walikusudia hadhi na uombezi.

Tulitangulia kukupa hoja za hayo kutoka katika Qur'ani.

**Abdun-nabiy**: Lakini aya hizi zilishuka kwa watu waliokuwa wakiabudu masanamu. Sasa vipi mnawafanya Watu Wema na Mitume kuwa masanamu?

**Abdallah**: Tulikwisha kubaliana kwamba baadhi ya masanamu haya yalipewa majina ya watu wema kama ilivyokuwa kwa watu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Nuh, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, na kwamba makafiri hawakutaka kwa watu wema hao isipokuwa tu uombezi mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa wana hadhi kwake. Hoja ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Na wale ambao wamefanya wapenzi (Miungu) badala yake (Mwenyezi Mungu, walipotakiwa kutofanya hivyo, walisema:) Hatuwaabudu isipokuwa tu kwa kutaka watuweke karibu na Mwenyezi Mungu".*** **Suratiz-zumar 39, aya 3.**

**Ama kauli yako kwamba: Vipi mnawafanya Mitume kuwa masanamu? Tunakuambia kwamba: 1)** Makafiri ambao Mwenyezi Mungu aliwapelekea Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, miongoni mwao kuna waliokuwa wakiwaomba Mawalii ambao Mwenyezi Mungu amewaelezea kwa kusema: ***"Hao (mawalii= miungu) ambao (makafiri) wanawaomba, (wao wenyewe) wanatafuta cha kuwaweka karibu na Mola wao; Ni nani wao wa karibu zaidi, na wanataraji rehema yake na wanaogopa adhabu yake. Kwa yakini, adhabu ya Mola wako imekuwa ya kuogopwa".*** Surat Bani-israil 17, aya 57.

**2)** Miongoni mwa makafiri hao kuna waliokuwa wakimuomba Issa, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema, yeye na mama yake. Mwenyezi Mungu amesema kuwa: ***"Na (eleza) wakati Mwenyezi Mungu aliposema: Ewe Issa Mwana wa Mariamu, hivi wewe ulisema kuwaambia watu (kuwa): Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa miungu badala ya Mwenyezi Mungu?".*** Suratul-Maidah 5, aya 117. **3)** Miongoni mwa makafiri hao kuna waliokuwa wakiwaomba Malaika. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa: ***"Na (eleza) siku atakapowakusanya wote halafu atawaambia Malaika: Hivi hawa ndio waliokuwa wakikuabuduni nyinyi?".*** Suratu Saba-i 34, aya 40.

Zitafakari vyema aya hizi. Mwenyezi Mungu katika aya hizo amewahukumu ukafiri wale waliokusudia masanamu. Pia amewahukumu ukafiri wale waliowakusudia watu wema, wakiwemo Mitume, Malaika na Mawalii kwa pamoja. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu alipigana nao vita, na katika hilo hakuwatofautisha.

**Abdun-nabiy**: Lakini makafiri walikuwa wanaomba kwao manufaa, na lakini mimi ninakiri kuwa Mwenyezi Mungu tu ndiye Mwenye kunufaisha, Mwenye kudhuru, mtengenezaji mambo, na hayo siyaombi isipokuwa kwake tu. Watu wema hawana uwezo wowote, lakini nawakusudia nikitaraji kwa Mwenyezi Mungu kukubaliwa kwa uombezi wao.

**Abdallah**: Kauli yako hii ni sawasawa na kauli ya makafiri. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Na wanaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu, vitu ambavyo haviwadhuru na haviwanufaishi na wanasema: Hawa ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu".*** Surat Yunus 10, aya 18.

**Abdun-nabiy**: Lakini mimi siabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Huku kuwaelekea hao tunaowaelekea na kuwaomba sio ibada.

**Abdallah**: Lakini mimi ninakuuliza: Je, unakiri kwamba Mwenyezi Mungu amefaradhisha kwako kumtakasia yeye tu ibada, na ni haki yake kwako kama

ilivyo katika kauli yake isemayo kuwa: ***"Na hawakuamrishwa isipokuwa tu wamwabudu Mwenyezi Mungu wakimtakasia yeye dini, wakiacha dini zote potofu"***? Suratul-Bayyinah 98, aya 5.

**Abdun-nabiy**: Ndio. Mwenyezi Mungu amefaradhisha hilo kwangu.

**Abdallah**: Na mimi nakuomba uniwekee wazi hili jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelifaradhisha kwako na ambalo ni kuitakasa ibada.

**Abdun-nabiy**: Sijafahamu, una maana gani kwa swali hili? Niwekee wazi?

**Abdallah**: Nisikilize nikuwekee wazi. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa: ***"Muombeni Mola wenu kwa kunyenyekea na kwa siri. Kwa yakini, yeye hawapendi wenye kupindukia mipaka"***. Suratul-A'raaf 7, aya 55. Je, dua ni kumwabudu Mwenyezi Mungu au laa?

**Abdun-nabiy**: Naam. Dua ni kumwabudu Mwenyezi Mungu, na ndio msingi wa ibada kama ilivyo katika Hadithi isemayo kuwa: ***"Dua ndio ibada"***. Ameipokea Hadithi hii Abudaud.

**Abdallah**: Madamu unakiri kuwa dua ni kumwabudu Mwenyezi Mungu, na ukamuomba Mwenyezi Mungu shida fulani usiku au mchana kwa kuhofu na kutaraji rehema halafu katika shida hiyo hiyo ukamuomba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) au Malaika au Mtu Mwema aliyeko kaburini mwake je, utakuwa umefanya ushirikina katika ibada hii?

**Abdun-nabiy**: Ndio. Nitakuwa nimefanya ushirikina. Haya ni maneno sahihi na yaliyo wazi.

**Abdallah**: Chukua mfano mwingine. Iwapo umeijua kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Basi swali kwa ajili ya Mola wako na chinja (kwa ajili ya Mola wako)"***. Suratul-Kauthar 108, aya 2. na ukaitii amri hii itokayo kwa Mwenyezi Mungu na, kwa hiyo, ukachinja kwa ajili yake. Je, huku ni kumwabudu Mwenyezi Mungu?

**Abdun-nabiy**: Ndio. Huko ni kuabudu.

**Abdallah**: Ikiwa utachinja kwa ajili ya kiumbe; Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) au jini au kiumbe mwenginewe pamoja na kumkusudia Mwenyezi Mungu, je utakuwa umemshirikisha asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika ibada hii?

**Abdun-nabiy**: Ndio. Bila shaka, huu ni ushirikina.

**Abdallah:** Mimi nimekutolea mfano wa dua (kuomba) na kuchinja kwa sababu: **1)** Dua ni aina nzito zaidi katika aina za ibada za kauli. **2)** Kuchinja ni aina nzito zaidi katika aina za ibada za vitendo. Lakini sio kwamba ibada ni hizo tu. Ibada ni zaidi ya hizo. Huingia katika ibada kuweka nadhiri, kuapa, kuomba kinga, kuomba wokovu na nyinginezo. Lakini je, washirikina ambao Qur'ani ilishuka kwao walikuwa wakiabudu Malaika, Watu Wema, Lata na wasiokuwa hao au laa?

**Abdun-nabiy**: Ni kweli. Walikuwa wakifanya hivyo.

**Abdallah**: Ibada yao kwao haikuwa katika mambo mengine isipokuwa tu ilikuwa katika dua, kuchinja, kuomba kinga, kuomba msaada na kuomba hifadhi. Vinginevyo ni kwamba walikuwa wanakiri kwamba wao ni waja wa Mwenyezi Mungu na wako chini ya utawala wake na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye ambaye anaendesha mambo ya ulimwengu. Lakini waliwaomba (hao waliokuwa wakiomba) kwa sababu ya hadhi na uombezi. Hili liko wazi sana.

**Abdun-nabiy**: Je, unakanusha, ewe Abdallah, uombezi wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na unaukataa?

**Abdallah**: Hapana. Mimi siukanushi na siukatai. Yeye Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi

Mungu amfikishie rehema na amani, nikiwa tayari kumtetea kwa hali na mali, ndiye Muombeaji, Mkubaliwa uombezi wake. Mimi nataraji uombezi wake. Lakini uombezi wote ni wa Mwenyezi Mungu kama alivyosema kuwa: ***"Sema: Ni wa Mwenyezi Mungu tu uombezi wote"***. **Suratuz-Zumar 39, aya 44.** Uombezi hautakuwa ila tu baada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kutoa idhini, kama alivyosema kuwa: ***"Ni nani huyu ambaye ataombea kwake bila ya idhini yake?"***. **Suratul-Baqara 2, aya 255.** Hataombewa yeyote isipokuwa tu baada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kumtolea idhini, kama alivyosema kuwa: ***"Na hawataombea isipokuwa tu kwa yule ambaye (Mwenyezi Mungu) amekuwa radhi (naye)"***. **Sura Al-anbiyaa 21, aya 28.** Mwenyezi Mungu haridhii isipokuwa Tawhiid tu, kama alivyosema kuwa: ***"Na yeyote anayetaka usiokuwa Uislamu kuwa dini (yake), hatokubaliwa na yeye huko Akhera atakuwa miongoni mwa wenye hasara"***. **Sura Aal-imraan 3, aya 85.**

**Iwapo: 1)** Uombezi wote ni wa Mwenyezi Mungu. **2)** Uombezi hauwi ila tu baada ya idhini ya Mwenyezi Mungu. **3)** Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, wala mwengine yeyote hawatamuombea ila yule tu aliyeidhinishwa na Mwenyezi Mungu. **4)** Mwenyezi Mungu hakubali maombezi ila kwa watu wa Tauhidi tu imebainika wazi kuwa uombezi wote ni wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hiyo, mimi nauomba uombezi huo kwake na kusema: Ewe Mola wangu, usininyime uombezi wake (Mtume). (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Ewe Mola wangu, ukubali uombezi wa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wako kwangu.

**Abdun-nabiy**: Tumekubaliana kwamba: **1)** Haifai kumuomba yeyote jambo lolote asilolimiliki, na kwamba: **2)** Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, uombezi na kwamba: **3)**Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amempa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) uombezi, basi ndio amemmilikisha. Kwa msingi huu, inafaa kumuomba Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) jambo analolimiliki, na hilo haliwi ushirikina.

**Abdallah**: Ndio. Haya ni maneno sahihi kama Mwenyezi Mungu asingekuzuia kufanya hivyo. Lakini Mwenyezi Mungu anasema kuwa: ***"…kwa hiyo, usimuombe yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu"***. Suratul-Jinn 72, aya 18. Kuomba uombezi ni maombi (dua), na ambaye amempa Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, uombezi ni Mwenyezi Mungu naye ndiye ambaye amekuzuia kuomba uombezi huo kwa asiyekuwa yeye vyovyote awavyo muombwaji huyo. Aidha uombezi umetolewa kwa wengine wasiokuwa Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*).

**Ni sahihi kwamba**: **1)** Malaika wataombea. **2)** Watoto (watoto ambao wamekufa kabla ya kufikia umri wa kubalehe) wataombea. **3)** Watu Wema wataombea.

Je, utasema kuwa: Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewapa hawa uombezi, basi nauomba uombezi huo kutoka kwao? Endapo utasema hivi, basi utakuwa umerudi kwenye kuwaabudu Watu Wema, kuabudu ambako Mwenyezi Mungu Mtukufu amekutaja katika kitabu chake. Endapo utasema: La! basi ile kauli yako kwamba "Mwenyezi Mungu amewapa wao uombezi basi nami nauomba kutoka kwao" itakuwa batili.

**Abdun-nabiy**: Lakini mimi simshirikishi Mwenyezi Mungu, na kujiegemeza kwa Watu Wema sio ushirikina.

**Abdallah**: Hivi unakubali kuwa Mwenyezi Mungu ameharamisha ushirikina zaidi

kuliko alivyoharamisha zinaa na kwamba hausamehe ushirikina?

**Abdun-nabiy**: Ndio. Nalikubali hilo, na liko wazi katika maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**Abdallah**: Wewe sasa hivi umejisafisha kwamba huna ushirikina ambao Mwenyezi Mungu ameuharamisha. Sasa, kwa jina la Mwenyezi Mungu, hebu niambie: Ni ushirikina upi wa kumshirikisha Mwenyezi Mungu na ambao wewe hujaingia humo na umejisafisha nao?

**Abdun-nabiy**: Ushirikina ni kuabudu masanamu; kuyakusudia, kuyaomba na kuyaogopa.

**Abdallah**: Ni nini maana ya kuabudu masanamu? Hivi unadhani kwamba makafiri wa Kiquraishi walikuwa na itikadi kwamba miti na mawe hayo yanaumba, yanatoa riziki na kutengeneza mambo ya wanaoyaomba? Wao hawana itikadi hiyo kama nilivyokuambia.

**Abdun-nabiy**: Mimi pia sina itikadi hiyo. Lakini yule anayekusudia mti au jiwe au jengo lililo kaburini au sehemu nyingine akiliomba au kuchinjia kwa ajili yake na kusema: Hilo linatuweka karibu na Mwenyezi Mungu na kwa baraka zake Mwenyezi Mungu hutuondolea madhara. Huko ndio kuabudu masanamu ambako ninakukusudia.

**Abdallah**: Umesema kweli. Hivi ndivyo mnavyofanya kwenye mawe, majengo, vyumba vilivyopo makaburini na sehemu nyingine. Aidha unaposema: "Ushirikina ni kuabudu masanamu", je, makusudio yako ni kwamba ushirikina unamhusu anayefanya hivyo tu na kwamba kuwategemea watu wema na kuwaomba hakuingii katika jumla ya ushirikina?

**Abdun-nabiy**: Ndio. Haya ndio niliyoyakusudia.

**Abdallah**: Kwa hiyo basi, unaziangaliaje aya nyingi ambazo Mwenyezi Mungu katika aya hizo ametaja kuharamisha kuwategemea Watu Wema, kujiegemeza kwa malaika na viumbe wengine na amewataja wanaofanya hivyo kuwa ni makafiri, kama nilivyotangulia kukuambia na kukutolea ushahidi?

**Abdun-nabiy**: Lakini wale ambao waliwaomba Malaika na Mitume hawakuwa makafiri kwa sababu hii. Wao wamekuwa makafiri pale waliposema kuwa: **1)** Malaika ni mabinti wa Mwenyezi Mungu. Sura An-nahl 16, aya57. **2)** Masiah ni Mwana wa Mungu. **Sura At-tawbah 9,aya 30.**

Lakini sisi hatukusema kuwa Abdulkadir ni Mwana wa Mungu au Zainabu ni Binti wa Mungu.

**Abdallah**: Ama kumnasibisha mtoto kwa Mwenyezi Mungu, huo ni ukafiri unaojitosheleza. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "***Sema: Ilivyo ni kwamba Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu ndiye tu Mkusudiwa***". Suratul-Ikhlas 112, aya 1-2. **Wa pekee:** Ni ambaye hana wa kufanana naye. **Mkusudiwa:** Ni yule anayekusudiwa katika shida. Kwa hiyo, yeyote anayekanusha haya amekufuru, hata kama hakukanusha mwisho wa Sura. Halafu Mwenyezi Mungu amesema kuwa: "***Mwenyezi Mungu hakufanya mtoto yeyote na hakuna Mungu yeyote pamoja naye. Ingekuwa hivyo, kila Mungu angeondoka na alichoumba, na baadhi yao wangewakalia juu baadhi nyengine***". Suratul-Muuminun 23, aya 91. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu ametofautisha kati ya kufuru mbili. Ushahidi wa haya pia ni kwamba: **1)** Wale waliokufuru kwa sababu ya kumuomba Lata pamoja na kuwa ni Mtu Mwema hawakumfanya kuwa ni Mwana wa Mungu. **2)** Wale waliokufuru kwa sababu ya kuabudu Majini pia hawakuwafanya hivyo. **3)** Aidha, madhehebu manne yanataja

katika mlango wa Murtadi (mtu aliyetoka katika Uislamu) kwamba endapo Mwislamu atadai kuwa Mwenyezi Mungu ana mtoto basi yeye ni Murtadi (ametoka katika Uislamu na kuwa kafiri). Kwa hiyo, wanachuoni wanatofautisha kati ya aina mbili za ukafiri.

**Abdun-nabiy**: Lakini Mwenyezi Mungu anasema kuwa: "***Ee! Kwa yakini, Wapenzi (Mawalii) wa Mwenyezi Mungu hawana hofu na wao hawahuzuniki***". Surat Yunus 10, aya 62.

**Abdallah**: Na sisi tunaamini kwamba hayo ni kweli na tunasema hayo hayo. Lakini Mawalii hawaabudiwi. Sisi hatukanushi isipokuwa tu kuabudiwa kwao pamoja na Mwenyezi Mungu na kushirikishwa kwao pamoja naye. Kinyume na hivyo, ni wajibu kwako: **1)** Kuwapenda. **2)** Kuwaiga. **3)** Kukiri karama zao.

Hawakatai karama za Mawalii isipokuwa tu Watu wa Bidaa (uzushi). Dini ya Mwenyezi Mungu ipo katikati kati ya pande mbili; uongofu kati ya upotofu wa aina mbili, na haki kati ya batili mbili.

**Abdun-nabiy**: Wale ambao ilishuka kwao Qur'ani walikuwa: **1)** Hawakiri kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu tu. **2)** Wanamkataa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. **3)** Wanakanusha kufufuliwa. **4)** Wanaipinga Qur'ani na kuifanya kuwa ni uchawi.

Sisi tunakiri kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu tu na kwamba Muhammad ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, tunaiamini Qur'ani, tunaamini kufufuliwa, tunaswali na kufunga. Sasa vipi mnatufanya sisi kama wao?

**Abdallah**: Hakuna tofauti kati ya wanachuoni wote kwamba mtu atakapomwamini Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu katika jambo fulani na akampinga katika jambo jingine amekuwa kafiri na hayumo katika Uislamu. Vile vile, mtu atakapoamini baadhi ya Qur'ani na kuipinga baadhi nyingine, kama vile mtu kuamini upekee wa Mwenyezi Mungu na akakanusha kuswali au kukiri upekee wa Mwenyezi Mungu na kuswali akakanusha wajibu wa kutoa zaka au kuyaamini yote haya na akakanusha kufunga au kukiri yote haya na akakanusha wajibu wa kuhiji. Watu fulani wakati wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, walipokataa kuhiji, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha kuwahusu wao maneno yafuatayo: ***"Na ni (haki) ya Mwenyezi Mungu kwa watu kuhiji Nyumba (Tukufu ya Al-kaaba) mwenye kuweza kuiendea, na anayekufuru (anayekanusha) basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na walimwengu"***. Surat Aal-imran 3, aya 97.

Ikiwa mtu akanusha kufufuliwa atakuwa kafiri, kwa mujibu wa makubaliano ya wanachuoni wote. Kwa sababu hiyo, Mwenyezi Mungu ameweka wazi katika kitabu chake kwamba anayeamini baadhi na kukanusha baadhi nyingine huyo ndiye kafiri kweli. Mwenyezi Mungu ameamrisha uchukuliwe Uislamu wote. Anayechukua jambo fulani na kuacha jingine, huyo amekuwa kafiri. Je, unakubali kuwa anayeamini baadhi ya mambo na kukataa baadhi nyingine amekufuru?

**Abdun-nabiy**: Ndio. Nayakubali hayo. Hayo yako wazi ndani ya Qur'ani Tukufu.

**Abdallah**: Ikiwa unakubali kwamba aliyemwamini Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika jambo fulani na akakanusha wajibu wa sala au akayakubali yote isipokuwa kufufuliwa, basi yeye ni kafiri kwa mujibu wa makubaliano ya madhehebu yote. Qur'ani imelitamka hilo, kama tulivyotangulia kueleza. Fahamu kuwa Tauhidi ni faradhi kubwa sana katika faradhi alizokuja nazo Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na ni kubwa

zaidi kuliko Sala, Zaka na Hija. Vipi basi mtu akikanusha jambo katika mambo haya awe kafiri hata kama atatekeleza yote aliyokuja nayo Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na mtu huyo anapoikanusha Tauhidi ambayo ndio dini ya Mitume wote asiwe kafiri? Ametakasika Mwenyezi Mungu! Huu ni ujinga wa ajabu sana! Aidha, hebu tafakari Swahaba wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, pale walipopigana vita na Bani-hanifah na ilhali walikuwa wamesilimu pamoja na Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, wanakiri kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, wanaswali na kuadhini.

**Abdun-nabiy**: Lakini hao Bani-hanifa walikuwa wanaamini kuwa Musailamah ni Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na sisi tunasema kuwa hakuna Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) baada ya Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.

**Abdallah**: Lakini nyinyi mnamtukuza Ali, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, au Abdulkadir au viumbe wengineo wakiwemo Mitume au Malaika na kuwafikisha daraja ya (Mwenyezi Mungu) Jabari wa mbinguni na ardhini. Ikiwa aliyemtukuza mtu na kumfikisha daraja ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, anakuwa kafiri na kuwa halali damu na mali yake na Shahada yake na Sala yake isimsaidie, basi yule anayemtukuza mtu na kumfikisha daraja ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni bora zaidi yeye kuwa kafiri. Pia, wale ambao Ali, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, aliwachoma moto, wote walidai kuwa ni Waislamu, ni wafuasi wa Ali na kujifunza elimu kwa Swahaba. Lakini walikuwa na itikadi kwa Ali kama ile itikadi yenu kwa Abdulkadir na wengineo. Vipi basi Swahaba wote walikubaliana kuwakufurisha na kuwapiga vita? Hivi unadhani kuwa Swahaba wanawakufurisha Waislamu? Au unadhani kuwa itikadi kwa Sayyid (Sharifu) na mfano wake haidhuru na itikadi hiyo hiyo kwa Ali, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, ndio inakufurisha?

**Inasemwa pia kuwa:** Ikiwa wale wa mwanzo hawakuingia katika ukafiri isipokuwa tu kwa sababu walikusanya kati ya ushirikina na kumkanusha Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, Qur'ani, kukanusha kufufuliwa na mengine yasiyokuwa hayo, ni ipi basi maana ya mlango (chapter) ambao wanachuoni katika kila madhehebu wameutaja na ambao ni: "Mlango wa hukumu ya Murtadi"? Murtadi ni Mwislamu ambaye anakuwa kafiri baada ya kuwa Mwislamu. Halafu wanachuoni hao wametaja mambo mengi, kila jambo kati ya mambo hayo linakufurisha, linamotoa mtu katika uislamu. Wamefikia kutaja hata mambo madogo kwa anayeyafanya, mfano wa neno linalomchukiza Mwenyezi Mungu na analolitaja mtu kwa ulimi wake bila ya moyo wake kuliamini au neno analolitamka kwa njia ya mzaha na mchezo. Vile vile kuna wale ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaelezea kwa kusema: ***"Sema: Hivi mnamfanyia mzaha Mwenyezi Mungu na aya zake na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake? Msitoe udhuru. Hakika, mmekufuru baada ya kuamini kwenu"***. **Suratut Tawbah 9, aya 66.** Hawa ambao Mwenyezi Mungu ameeleza wazi kwamba wamekuwa makafiri baada ya kuamini kwao, na ilhali wao wako pamoja na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika vita vya Tabuk, walisema maneno waliyoyatolea hoja kwamba waliyasema kwa mzaha tu.

Aidha, husemwa: Yale yaliyonukuliwa kwa Wana wa Israili kwamba, pamoja Uislamu,

elimu na wema wao, walisema kumwambia Mussa kwamba: ***"Tufanyie Mungu, kama wao walivyo na Mungu"***. Suratul A'araf 7, aya 138. Pia kauli ya watu miongoni mwa Swahaba wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) waliposema: *"Tufanyie Dhaat-anwaat kama ambavyo wao wana Dhaat-anwaat"*. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Menyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliapa kwamba kauli hii ni sawa na kauli ya Wana wa Israili: ***"Tufanyie Mungu, kama wao walivyo na Miungu"***. Suratul-A'raf 7, aya 138.

**Abdun-nabiy**: Lakini Wana wa Israili na wale ambao walimuomba Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, awafanyie Dhaat-anwaat hawakuwa makafiri kwa sababu hiyo.

**Abdallah**: Jibu ni kwamba Wana wa Israili na wale waliomuomba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) hawakuwahi kufanya. Lau kama wangefanya hivyo, wangekuwa makafiri. Na wale ambao Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliwakataza wasingemtii na wangefanya Dhaat-anwaat baada ya kukatazwa, wangekuwa makafiri.

**Abdun-nabiy**: Lakini mimi nina tatizo jingine. Ni kisa cha Usama bin Zaid, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, wakati alipomuua yule aliyetamka "Laa ilaaha illallah" Bukhari na Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kumkemea na kumwambia: "*Ewe Usama, hivi umemuua baada ya kuwa ametamka: Laa ilaaha illallah?" Muslim*. Pia kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: "*Nimeamrishwa nipigane vita na watu mpaka waseme: Laa ilaaha illallah"*. Vipi nitaoanisha kati ya uliyoyasema na kati ya hizi Hadithi mbili? Nipe mwongozo, nawe Mwenyezi Mungu atakuongoza.

**Abdallah**: Ni miongoni mwa mambo yanayojulikana kwamba: **1)** Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipigana vita na Wayahudi na kuwateka ilhali wao wanasema: Laa ilaaha illallah. **2)** Swahaba wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, walipigana vita na Bani-hanifa na ilhali Bani-hanifa hao wanatamka: Laa ilaaha illallah na kwamba Muhammad ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu na wanaswali. **3)** Vile vile wale ambao Ali, Mwenyezi mungu amuwiye radhi, aliwachoma moto walikuwa hivyo hivyo.

**Wewe unakubali kuwa: 1)** Anayekanusha kufufuliwa anakuwa kafiri na anatakiwa kuuawa hata kama anasema: Laa ilaaha illallah. **2)** Anayekanusha jambo katika nguzo za Uislamu anakuwa kafiri na kutakiwa kuuawa hata kama anatamka hiyo Laa ilaaha illallah.

Sasa vipi Laa ilaaha illallah isimsaidie mtu anapokanusha jambo katika matawi (masuala mepesi ya dini) na lakini imsaidie anapokanusha Tauhidi ambayo ndio msingi na kichwa cha dini ya Mitume? Inawezekana kwamba hukufahamu maana ya Hadithi hizi.

Ama Hadithi ya Usama, ni kwamba alimuua mtu aliyedai kuwa yeye ni Mwislamu, kwa sababu alidhani kuwa mtu huyo alidai kuwa ni Mwislamu kwa ajili tu ya kuchelea damu na mali yake. Mtu anayeonesha dhahiri Uislamu ni wajibu kutomgusa mpaka yabainike kwake mambo yaliyo kinyume na hivyo. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "***Enyi ambao mmeamini, mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu (mtakapokuwa katika Jihadi), basi thibitisheni***". Suratun-Nisaa 4, aya 94.

**Aya inaonesha kwamba ni wajibu: 1)** Kutomgusa. **2)** Kufanya uhakiki.

Yakibainika baada ya hapo mambo yanayopingana na Uislamu, anauawa kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa *" …thibitisheni".* Suratun-Nisaa 4, aya 94. Ingekuwa hauawi aitamkapo hiyo Laa ilaaha illallah, uhakiki usingekuwa na maana yoyote.

Aidha maana ya ile Hadithi nyingine ni hivyo hivyo kwamba mtu anayeonesha dhahiri Tauhidi na Uislamu ni wajibu kutomgusa isipokuwa tu yatakapobainika kwake yanayopingana na hayo. Ushahidi wa haya ni kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliposema: "…*hivi umemuua baada ya kuwa ametamka: Laa ilaaha illallah?"*. Pia aliposema: "*Nimeamrishwa nipigane vita na watu mpaka waseme: Laa ilaaha illallah*" ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) huyo huyo aliyesema kuhusu Khawaarij kwamba: *"Popote mtakapowakuta waueni"Bukhari*... pamoja na kuwa Khawaarij walikuwa ni wafanyaji ibada sana na watamkaji sana wa Laa ilaaha illallah mpaka Swahaba walikuwa wakijiona duni wanapoziona ibada za watu hawa. Watu hawa walikuwa wamepata elimu yao kwa Swahaba. Laa ilaaha illallah, ibada zao nyingi na kudai kwao kuwa ni Waislamu haikuwazuia wasiuawe pale kulipobainika wazi kwao kuipinga sheria.

**Abdun-nabiy**: Unasemaje kuhusu yale yaliyothibiti kunukuliwa kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: "*Watu Siku ya Kiyama watamuomba wokovu Adam halafu Nuh halafu Ibrahim halafu Mussa halafu Issa. Wote watatoa udhuru mpaka maombi hayo yatamfikia Mtume* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani"*. Hii inaonesha kwamba kumuomba wokovu asiyekuwa Mwenyezi Mungu sio ushirikina.

**Abdallah**: Huku ni kuchanganya mambo. Hatukanushi kumuomba wokovu kiumbe aliyepo na aliye hai, katika jambo analoliweza, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema kuwa: ***" …hivyo, akamuomba wokovu (msaada) yule ambaye ni katika jamaa zake dhidi ya yule ambaye ni katika maadui wake".*** Suratul-Qasas 28, aya 15. Kama ambavyo mtu anaweza kuwaomba wokovu wenzake katika vita na sehemu nyingine katika mambo ambayo kiumbe anayaweza. Sisi tunakanusha kuomba wokovu ambako ni ibada, mnakokufanya kwenye makaburi ya Watu Wema au kuwaomba Watu Wema wenyewe wasipokuwepo, katika mambo ambayo hakuna ayawezaye isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Watu watawaomba wokovu Mitume Siku ya Kiyama; wakiwataka wamuombe Mwenyezi Mungu awahesabu watu ili watu wa peponi waondokane na mateso ya kisimamo. Haya yanafaa duniani na Akhera; wewe kumuendea Mtu Mwema anayeketi nawe, anayesikia maneno yako na kumwambia: Niombee Mungu, kama Swahaba wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, walivyokuwa wakimuomba Mtume katika uhai wake. Ama baada ya kufa kwake, haikuwa hivyo. Hawakumuomba hayo kaburini kwake, bali Wahenga Wema wamemkemea mtu anayekusudia kumuomba Mwenyezi Mungu kwenye kaburi.

**Abdun-nabiy**: Unasemaje kuhusu kisa cha Mtume Ibrahim, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie amani, wakati alipotumbukizwa katika moto na jibrili kumjia angani na kumuuliza: Je, una shida yoyote? Mtume Ibrahim, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie amani, akajibu: Ama kwako, hapana. Lau kama kumuomba wokovu Jibrili ingekuwa ni ushirikina, Jibrili asingemuuliza Ibrahim.

**Abdallah**: Utata huu ni aina ya utata ule ule wa kwanza. Hiyo Athar sio sahihi.

Lakini hata tukichukua kauli isemayo kuwa ni sahihi, Jibrili, Mwenyezi Mungu amfikishie amani, alimuonesha Ibrahim nia ya kutaka kumsaidia kwa jambo analoliweza. Jibrili, kama alivyomuelezea Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni "***Mwenye nguvu sana***" Sura An-najm 53, aya 5. Lau kama Mwenyezi Mungu angelimruhusu Jibrili kuchukua moto, ardhi na milima ilioko kando kando ya moto huo na kuitupa mashariki au magharibi lisingemshinda hilo. Mfano huu ni kama mfano wa mtu tajiri aliyemuonesha mtu mwenye shida nia ya kutaka kumkopesha mali ili atimize shida yake, lakini mtu huyo mwenye shida akakataa na kuamua kuvumilia mpaka Mwenyezi Mungu Mtukufu ampe riziki isiyokuwa na masimbulizi kutoka kwa yeyote. Sasa liwapi hili na uombaji wokovu wa ibada na ushirikina ufanywao hivi sasa?

Fahamu ndugu yangu kwamba ushirikina wa wale watu wa mwanzo ambao Bwana wetu Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alitumwa kwao ni mdogo zaidi kuliko ushirikina wa watu wa wakati wetu, na hiyo ni kwa kuzingatia mambo matatu: **1) Jambo la kwanza** ni kwamba watu wa zamani hawakuwa wakikishirikisha na Mwenyezi Mungu kitu kingine isipokuwa tu katika raha. Ama katika matatizo, wanaitakasa dini (unyenyekevu) kwa Mwenyezi Mungu. Ushahidi ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: "***Basi wapandapo katika majahazi (na wakafikwa na misukosuko) humuomba Mwenyezi Mungu wakimtakasia yeye dini. Wakati akiwaokoa (na) kuwafikisha bara (nchi kavu) mara wao hufanya ushirikina***".Suratul-Ankabuut 29, aya 65. Pia Mwenyezi Mungu amesema kuwa: "***Na yanapowafinika mawimbi kama mawingu, humuomba Mwenyezi Mungu wakimtakasia yeye tu dini (unyenyekevu). Na anapowaokoa (na) kuwafikisha bara, basi miongoni mwao kuna wenye msimamo wa kati. Na hazikanushi aya zetu isipokuwa tu kila mdanganyifu sana, kafiri mkubwa***". Surat Luqman 31, aya 32. Washirikina ambao Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alipigana nao vita walikuwa wanamuomba Mwenyezi Mungu na wanawaomba (Miungu) wengine katika raha. Ama katika matatizo, hawamuombi isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee na kuwasahau Mabwana zao. Ama washirikina wa wakati wetu, wanamuomba Mwenyezi Mungu na wanawaomba wengine katika raha na shida. Mmoja wao anapopata shida, husema: Ewe Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, ewe Hussein! Lakini yuko wapi anayelifahamu hilo?

**2) Jambo la pili** ni kwamba wale watu wa zamani walikuwa wanaomba, pamoja na Mwenyezi Mungu, watu wengine walio karibu na Mwenyezi Mungu; ima ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) au Walii au Malaika au kwa uchache jiwe au mti, vitu ambavyo vinamtii Mwenyezi Mungu na havimuasi. Watu wa wakati wetu wanaomba, pamoja na Mwenyezi Mungu, watu ambao ni miongoni mwa watu waovu sana. Ambaye ana itikadi kwa kiumbe chema na ambacho hakifanyi maasi, kama jiwe na mti ni afadhali zaidi kuliko yule aliye na itikadi kwa mtu ambaye uovu na ubaya wake unaonekana wazi.

**3) Jambo la tatu** ni kwamba ushirikina wa washirikina wote wa wakati wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ulikuwa katika Tauhidi ya *Uluuhiyya* (Tawhidi ya kuabudu) na haukuwa katika Tawhidi ya *Rubuubiyya* (Tauhidi ya Vitendo), tofauti na ushirikina wa watu waliokuja baadae. Ushirikina wa

watu wa sasa upo kwa wingi katika *Uluuhiyya,* kama ambavyo upo kama hivyo katika *Rubuubiyya*. Wao, kwa mfano, wanayafanya maumbile kuwa ndiyo yanayoendesha mambo katika ulimwengu, ikiwemo kuleta uhai na kuleta mauti n.k.
Pengine nimalizie maneno yangu haya kwa kutaja suala moja kubwa linalofahamika kutokana na yale yaliyopita; kwamba hakuna tofauti kwamba Tauhidi lazima iwe kwa: **a)**Kauli, matendo ya moyoni na mdomoni. **b)**Kufanya sababu kwa matendo ya viungo. Ikikosekana moja kati ya mawili haya, mtu hawezi kuwa Mwislamu. Ikiwa mtu anaijua Tauhidi na asiitumie, basi huyo ni kafiri mpinzani, kama vile Firauni na Ibilisi. Watu wengi wanalikosea jambo hili na kusema: Haya ni kweli, lakini hatuwezi kuyatekeleza na hayafai kwa watu wa nchi yetu na kwamba ni lazima kukubaliana nao na kwenda nao kwa kuogopa shari yao. Masikini huyu hajui kwamba aghlabu ya vigogo wa ukafiri wanaijua haki na hawakuiacha isipokuwa tu kwa kutoa mojawapo ya udhuru, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema kuwa: ***"Wamenunua kwa aya za Mwenyezi Mungu thamani ndogo na hivyo, wakazuia njia yake. Kwa yakini, ni mabaya sana waliyokuwa wakiyafanya"***. Surat-Tawba 9, aya 9.

Anayeitekeleza Tauhidi utekelezaji wa nje na ilhali haielewi wala haiamini kwa moyo wake, basi huyo ni mnafiki. Mnafiki ni mbaya zaidi kuliko kafiri safi, kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: ***"Kwa yakini, wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini sana katika moto"***. Suratun-Nisaa 4, aya 145.

Suala hili litakubainikia wazi utakapolizingatia katika midomo ya watu: Utamuona anayeijua haki na kuacha kuitekeleza kwa kuogopa kupungukiwa na dunia yake, kama Karuni au kuogopa kupungukiwa na hadhi yake kama Haman au kuogopa kupungukiwa na utawala wake kama Firauni. Pia utamuona anayeitekeleza Tawhidi kwa nje tu na sio kwa ndani, kama wanafiki. Ukimuuliza kuhusu itikadi anayoiamini katika moyo wake, haijui.

**Lakini jitahidi kuzifahamu aya mbili zilizomo katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, nazo ni hizi: a)** Aya ya kwanza ni ile kauli ya Mwenyezi Mungu iliyopita kwamba: ***"Msitoe udhuru. Hakika, mmekufuru baada ya kuamini kwenu"***. Suratit Taubah 9, aya 66. Ukijua kwamba baadhi ya wale ambao, wakiwa pamoja na Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, walipigana vita na Warumi, walikufuru kwa sababu ya neno walilolitamka kwa njia ya mchezo na mzaha, itakubainikia kuwa mtu ambaye anatamka ukafiri au kuutumia kwa kuogopa kupungukiwa na mali au hadhi au kumbembeleza yeyote ni mbaya zaidi kuliko anayetamka neno akilifanyia mzaha. Kwa sababu, anayefanya mzaha mara nyingi hayaamini katika moyo wake yale anayoyatamka kwa ulimi wake ili kuwachekesha watu. Ama anayetamka ukafiri au kuutumia kwa hofu au tamaa ya yaliyoko kwa kiumbe, atakuwa: **1)** Amemhakikishia shetani ahadi yake: ***"Shetani anakuahidini ufukara na kukuamrisheni mambo machafu"***. Suratul-Baqara 2, aya 268. **2)** Ameogopa kitisho cha shetani. ***"Hakuna vingine isipokuwa kwamba huyo ni shetani anakutisihieni wapenzi wake"***. Suratu Aal-imran 3, aya 175. **3)** Hakuiamini ahadi ya Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema: ***"Na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha kutoka kwake na fadhila"***. Suratul-Baqara 2, aya 268. **4)** Hakuogopa kitisho cha Mwenyezi Mungu Jabari: ***"…Basi msiwaogope na niogopeni mimi"***. Surat Aal-imran 3, aya 175.
Je, mtu ambaye hali yake ndio hii anastahiki kuwa miongoni mwa Mawalli (Wapenzi)

wa Mwenyezi Mungu au anastahiki kuwa miongoni mwa Mawalii wa shetani?

Aya ya pili ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Yeyote anayemkufuru Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake, (adhabu kubwa inamngojea) isipokuwa yule aliyelazimishwa na ilhali moyo wake umetulizana kwa imani. Na lakini wale waliovikunjulia ukafiri vifua vyao, basi hao iko juu yao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na watakuwa na adhabu kubwa"***. Suratun-Nahli 16, aya 106. Mwenyezi Mungu hakukubali udhuru wa watu hawa isipokuwa tu kwa yule aliyelazimishwa na ilhali moyo wake ukawa umeridhika na imani. Ama asiyeshurutishwa, anakuwa kafiri; sawa ameyafanya hayo kwa hofu au tamaa au kumpendezesha yeyote au kutetea nchi yake, familia yake, jamaa zake, mali yake au ameyafanya hayo kwa mzaha au kwa malengo mengine yasiyokuwa hayo, isipokuwa tu aliyeshurutishwa. Aya inaonesha kuwa mtu hashurutishwi isipokuwa tu katika kutenda na kutamka. Ama itikadi ya moyoni, hakuna yeyote anayeshurutishwa. Kauli ya Mwenyezi Mungu: ***"Hiyo ni kwa sababu wao waliyapenda maisha ya dunia kuliko akhera na kwamba Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri"***. Suratun-Nahl 16, aya 107. Mwenyezi Mungu ameweka wazi kwamba adhabu haikuwa kwa sababu ya itikadi, ujinga, kuichukia dini au kuupenda ukafiri, isipokuwa tu sababu yake ni kwamba katika hilo kuna sehemu ya upenzi wa mambo ya kidunia na kwa hiyo mtu akayakhiyari hayo kuliko dini.
Mwenyezi Mungu ndiye tu Mjuzi zaidi.

Baada ya yote haya, hivi hakujawadia kwako kutubu na kurejea kwa Mola wako na kuacha itikadi uliyo nayo? Mambo, kama ulivyosikia, ni hatari sana! Suala ni zito na mambo ni mazito!

**Abdun-nabiy**: Namuomba msamaha Mwenyezi Mungu na kutubu kwake. Ninakiri na kutamka kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu na ninakiri na kutamka kuwa Muhammad ni Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wa Mwenyezi Mungu. Ninavikana vyote nilivyokuwa nikiabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu anisamehe yote yaliyopita, anichukulie kwa upole wake, msamaha na rehema zake, anipe msimamo thabiti katika Tauhidi na itikadi sahihi mpaka nitakapokutana naye. Ninamuomba Mwenyezi Mungu akulipe kheri, ewe ndugu yangu Abdallah, kwa nasaha zako hizi, kwani ***"Dini ni nasaha".*** Pia nakushukuru kwa kukemea jambo baya nililokuwa nalo la jina langu la Abdun-nabiy. Nakupa habari kuwa jina hilo nimelibadlisha na kuwa Abdul-rahman (Mja wa Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema). Pia nakushukuru kwa kukemea jambo baya la ndani na ambalo ni itikadi potofu ambayo lau kama ningekutana na Mwenyezi Mungu na ilhali nina itikadi hiyo nisingepona asilani. Lakini ninaomba ombi la mwisho kwako. Naomba unitajie baadhi ya mambo mabaya ambayo watu huyakosea sana.

**Abdallah**: Hakuna ubaya. Niazime tu masikio yako.

✸ Jihadhari kauli mbaya yako isiwe "Kufuata masuala yenye tofauti" katika Qur'ani au katika Sunna kwa kutaka fitna au kupotosha. Kwa hakika, hakuna anayejua tafsiri yake isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Kauli mbiu yako iwe ni ile kauli ya waliobobea katika elimu ambao wanasema katika masuala yenye utata: ***"Tumeyaamini. Yote yanatoka kwa Mola wetu"***.**Suratu Aal-imran 3, aya 7.** Katika mambo yenye tofauti, kauli mbiu yako iwe: **1)** Kauli ya Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) wa Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Acha yanayokutia***

*shaka ufanye yasiyokutia shaka".* **Ahmad na Tirmidhiy.** 2) Kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Basi anayejitenga na mambo yenye kutatiza, bila shaka ameitakasa dini yake na heshima yake. Na anayejitumbukiza katika mambo yenye kutatiza, bila shaka ametumbukia katika haramu"*.** **Bukhariy na Muslim.** 3) Kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa: ***"Na dhambi ni lile jambo linalotia kigegezi katika nafsi yako na ukachukia watu kulifahamu (kuwa unalifanya)".*** **Muslim.** 4) Kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kuwa ***Uulize moyo wako na iulize nafsi yako (Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alitamka mara tatu). Wema ni lile jambo ambalo nafsi imetulia kwake na dhambi ni jambo linalotia kigegezi katika nafsi na kusita katika moyo, hata kama watu watakutaka Fat'wa na kukupa Fat'wa"*** **Ahmad.**

✸ Jihadhari kufuata mapenzi ya nafsi, kwani Mwenyezi Mungu amelihadharisha hilo kwa kauli yake isemayo kuwa: ***"Hivi umemuona yule aliyeyafanya mapenzi yake ya nafsi kuwa Mungu wake?*** Suratul-Furqan 25, aya 43.

✸ Jihadhari na kujifunga (kuegemea) kwa watu, maoni na mambo waliyokuwa nayo wazee. Jambo hilo linaweka kizuizi kati ya mtu na haki. Haki ni "Kitu kilichompotea muumini. Popote aikutapo, basi yeye ana haki zaidi ya haki hiyo". Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa: ***Na wakati wakiambiwa kuwa: Fuateni yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wanasema: Bali tunafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Hivi hata kama baba zao hawajui kitu na hawaongoki (wanawafuata tu)?".*** Sura Al-baqara 2, aya 170.

✸ Jihadhari kuwaiga makafiri, kwa kuwa huo ndio msingi wa kila balaa. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Yeyote anayejifananisha na watu (fulani) basi yeye ni katika wao* **Abudaud.**

✸ Jihadhari kumtegemea asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Na yeyote anayemtegemea Mwenyezi Mungu, basi yeye ni tosha yake".*** **Suratut-Talaaq 65, aya 3.**

✸ Usimtii kiumbe yeyote katika kumuasi Mwenyezi Mungu. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Hakuna kumtii kiumbe yeyote katika kumuasi Muumba" tirimidhy.*

✸ Jihadhari kumdhania vibaya Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Hadithi Qudsiy amesema kuwa: ***"Mimi niko kwenye dhana ya mja wangu kwangu"*.** **Bukhariy na Muslim.**

✸ Jihadhari kuvaa kikuku, uzi au mfano wa hivyo kwa lengo la kuzuia balaa kabla halijatokea au kuondoa balaa baada ya kutokea.

✸ Jihadhari kutundika (kufunga) hirizi kwa ajili ya kijicho (zongo), kwani jambo hilo ni ushirikina. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Mwenye kutundika kitu, huegemezwa kwenye kitu hicho".*** **Tirmidhiy.**

✸ Jihadhari kutafuta baraka kwa kutumia mawe, miti, vitu vya kale na majengo, kwakuwa huo ni ushirikina.

✸ Jihadhari kuamini kuwepo nuksi ya kitu chochote, kwani huo ni ushirikina. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Nuksi ni ushirikina, Nuksi ni ushirikina (Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliyasema hayo) mara tatu".***
Ahmad na Abu-daud.

✷ Jihadhari kuwaamini wachawi na wanajimu (watabiri wa nyota) wanaodai kujua mambo yaliyojificha *(ghaibu)* na kutangaza sayari katika magazeti na habari njema au mbaya za wenye sayari hizo. Kuwaamini katika hayo ni ushirikina, kwa sababu hakuna anayejua ghaibu (mambo yaliyojificha) isipokuwa Mwenyezi Mungu tu.

✷ Jihadhari kuhusisha kunyesha kwa mvua kwenye nyota na miongo, kwani huo ni ushirikina. Hakuna vingine isipokuwa kwamba kunyesha kwa mvua kunahusishwa kwa Mwenyezi Mungu tu.

✷ Jihadhari kuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu; vyovyote awavyo anayeapiwa; kama vile kuapia kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) au uaminifu au heshima au dhamana au uhai. Kufanya hivyo ni ushirikina. Imekuja katika Hadithi kwamba: ***"Yeyote anayeapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, amekufuru au amefanya ushirikina"***. **Ahmad na Abu-daud.**

✷ Jihadhari kutukana wakati, upepo, jua, baridi au joto, kwakuwa kufanya hivyo ni kumtukana Mwenyezi Mungu aliyeviumba vitu hivyo.

✷ Jihadhari na neno "Lau" linapokupata jambo baya. Neno hilo linafungua matendo ya shetani. Katika neno hilo, kuna kupinga Qadari (mipango) ya Mwenyezi Mungu. Lakini linapokupata jambo hilo baya, sema: ***"Hiyo ni Qadari (mipango) ya Mwenyezi Mungu. Na atakayo, hufanya"***.

✷ Jihadhari kuyafanya makaburi misikiti (sehemu za ibada). Ilivyo ni kwamba haitakiwi kuswali katika msikiti ambao ndani yake kuna kaburi. Imekuja katika Sahih Bukhariy na Sahih Muslim ikinukuliwa kutoka kwa Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akiwa katika sakaratilmaut (hali ya kufikwa na mauti) amesema kwamba: ***"Laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie Wayahudi na Wakristo. Wameyafanya makaburi ya Mitume wao misikiti (sehemu za ibada). (Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliyasema hayo) akihadharisha yale Wayahudi na Wakristo waliyofanya. Amesema Aisha kuwa: Lau kama sio onyo hilo, watu wangelinyanyua kaburi lake (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)"***. Bukhariy na Muslim. Pia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Kwa yakini, waliokuwepo kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao na Watu Wema wao misikiti. Kwa hiyo, msiyafanye makaburi misikiti. Mimi nakukatazeni hilo"***. **Abu-uwana.**

✷ Jihadhari kuziamini Hadithi ambazo waongo wanazihusisha na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika kuhimiza kutawasali kwa dhati ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) au Watu Wema katika umma wake, na ilhali Hadithi hizo zimebuniwa na kuzuliwa. Miongoni mwa Hadithi hizo ni hizi: **1)** "*Tawasalini kwa cheo changu, kwani cheo changu kwa Mwenyezi Mungu ni kikubwa*". **2)** "*Yakikukwazeni mambo, kumbatieni watu walio makaburini (maiti)*". **3)** "*Mwenyezi Mungu humuweka Malaika katika kaburi la kila Walii atimize shida za watu*". **4)** "*Lau kama mmoja wenu angekuwa na dhana nzuri katika jiwe, lingemsaidia*". Kuna Hadithi nyingine nyingi zisizokuwa hizo.

**Jihadhari kusherehekea kile kinachoitwa Sherehe za Kidini, mfano: 1)** Maulidi ya Mtume. (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) **2)**Israi na Miraji. **3)**Usiku wa tarehe 15 ya mwezi wa Shabani. Hayo ni mambo yaliyozushwa, na hayana hoja yoyote iliyonukuliwa kutoka kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, wala kwa Swahaba ambao wanampenda zaidi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kuliko sisi, na wana ari zaidi ya kheri kuliko sisi. Mambo hayo yangekuwa kheri, wangetutangulia kuyafanya.

# KUKIRI KUWA HAKUNA ANAYE STAHIKI KUABUDIWA ISIPOKUWA MWENYEZI MUNGU TU

Tamko hili linakusanya nguzo mbili: **Ya kwanza: Ni *Laa ilaaha*** (Hakuna anayestahiki kuabudiwa) ambayo ni kuukanusha uungu wa kweli kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu. **Ya pili: Ni *illallaah*** (isipokuwa Mwenyezi Mungu tu), ambayo ni kuuthibitisha uungu wa kweli kwa Mwenyezi Mungu pekee. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Na (kumbuka) Ibrahimu aliposema kumwambia baba yake na watu wake kuwa: Kwa yakini, mimi najitenga na vile mnavyoviabudu. Isipokuwa (mimi namwabudu) yule ambaye ameniumba, kwa sababu yeye ataniongoza".* Kwa hiyo, haitoshi kumwabudu Mwenyezi Mungu, lakini inatakiwa awe anaabudiwa yeye peke yake. Kuamini upekee wa Mwenyezi Mungu hakuwi sahihi isipokuwa tu kwa kujumuisha kati ya imani hiyo na kujiepusha na ushirika na washirika. Imepokewa katika Athar kuwa ufunguo wa Pepo ni ***Laa ilaaha illallaah*** (Hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu). Lakini je, kila anayetamka neno hilo anastahiki kufunguliwa Pepo? Wahab Bin Munabbih, Mwenyezi Mungu amrehemu, aliulizwa kuwa: Hivi laa ilaaha illallaah si ndio ufunguo wa Pepo? Alijibu: "Ilivyo ndio hivyo. Lakini hakuna ufunguo isipokuwa tu una meno. Ukija na ufunguo wenye meno utakufungulia, vinginevyo hautakufungulia". Zimenukuliwa Hadithi nyingi kutoka kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ambazo zote zinafafanua meno ya ufunguo huu. Mfano ni kauli ya Mtume isemayo kuwa: "*Yeyote anayetamka Laa ilaaha illallaah akiwa na ikhlasi......"*, na kauli yake isemayo kuwa: "*Yeyote anayetamka Laa ilaaha illallaah akiwa na yakini nayo...,*" na kauli yake isemayo kuwa: "*Yeyote anayetamka Laa ilaaha illallaah akiitamka kwa ukweli kutoka moyoni mwake......."*. Hadithi hizi, na nyinginezo, zimeweka masharti ya kuingia Peponi kwa kujua maana ya *Laa ilaaha illallaah*, kuwa imara katika Laa ilaaha illallah mpaka mtu anapokufa, kuwa na unyenyekevu kwenye maelekezo yake. Kutokana na mjumuika wa hoja, wanachuoni wameweka masharti amabayo, pamoja na kutokuwepo vikwazo vingine, ni lazima yapatikane ili Laa ilaaha illallaah iwe ufunguo wa Pepo. Masharti haya ndio meno ya ufunguo, nayo ni haya:

**❶ ELIMU:** Kila tamko lina maana. Ni wajibu kujua maana ya Laa ilaaha illallaah ujuzi usiokuwa na ujinga. Neno hilo linakanusha uungu kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kuuthibitisha uungu huo kwa Mwenyezi Mungu tu; kwa maana kuwa hakuna anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "***..... isipokuwa tu wale wanaoikiri haki na ilhali wao wanaijua***". Sura Azzukhruf (43), aya 86. *Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "Yeyote aliyekufa na ilhali anajua kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, ataingia Peponi".* Muslim.

**❷ YAKINI:** Hiyo ni wewe kuwa na yakini thabiti juu ya maana ya Laa ilaaha illallah, kwa sababu tamko hilo halikubali shaka, dhana, kusitasita au wasiwasi. Inapaswa tamko hilo lisimame juu ya yakini imara na madhubuti. Mwenyezi Mungu Mtukufu, akiwasifu waumini, amesema kuwa: "***Kwa yakini, hakuna vingine isipokuwa kwamba waumini ni wale tu waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake kisha wasiwe na shaka na wakatoa juhudi kwa mali zao na nafsi zao***

***katika (kutetea, kuihami, kuiendeleza) njia (dini) ya Mwenyezi Mungu. Hao tu ndio wakweli".*** Sura Al-hujuraat 49, aya 15. Kutamka kutupu hakutoshi. Ni lazima moyo uwe na yakini. Iwapo yakini hii haitapatikana, basi huo ni unafiki halisi. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Ninakiri kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu na kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mja hatakutana na Mwenyezi Mungu na yakini mbili hizo akiwa hana shaka nazo isipokuwa tu ataingia Peponi".* Muslim.

❸ **KUKUBALI**: Ukishajua na ukawa na yakini, elimu hii ya yakini inatakiwa iwe na athari yake. Hilo linapatikana kwa kukubali, kwa moyo na ulimi, yale yanayotakiwa na tamko hili. Yeyote anayekataa wito wa Tauhidi na asiukubali, anakuwa kafiri; sawa kutokubali huko kuwe ni kwa sababu ya kiburi au upinzani au husda.  Mwenyezi Mungu Mtukufu, akiwaelezea makafiri ambao walilikataa tamko la Tauhidi kwa kiburi, amesema kwamba: ***"Hakika ya wao wanapoambiwa: Hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, walikuwa wanafanya kiburi".*** Sura Saaffaat (37), aya 35.

❹ **KUTII**: Tauhidi inatakiwa iwe na uitiifu kamili. Huu ndio msingi wa hakika na ndio mandhari ya vitendo vya imani. Hili linapatikana kwa kutekeleza yale aliyoyaweka Mwenyezi Mungu na kuacha yale aliyoyakataza, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema kuwa:***"Na yeyote anayejisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na ilhali yeye ni mwenye kufanya yaliyo mazuri, basi ameshikamana na kishiko madhubuti, na ni kwa Mwenyezi Mungu tu mwisho wa mambo (yote)".*** Sura Luqman (31), aya 22. Huu ndio utiifu kamili.

❺ **UKWELI**: Mtu anatakiwa kuwa mkweli katika kutamka tamko la Tauhidi; ukweli usiokuwa na uongo. Mwenye kutamka Laa ilaaha illallah kwa ulimi wake tu na ilhali moyo wake unaikataa, huyo ni mnafiki. Hoja ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kuwashutumu wanafiki isemayo kuwa: ***"Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwemo katika nyoyo zao".*** Sura Al-fat'h (48), aya 11.

❻ **UPENDO:** Muumini anatakiwa kulipenda tamko hili, kupenda kuufanyia kazi muktadha wake, kuwapenda waumini wake wanaolitekeleza. Alama ya mja kumpenda Mola wake ni: kuyapa kipaumbele mambo anayoyapenda Mwenyezi Mungu, hata kama yanapingana na mambo anayoyapenda, kuwapenda wanaompenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kuwafanya maadui wanaomfanyia uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kumfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani; kufuata nyayo zake na kukubali mwongozo wake.

❼ **IKHLAS:** Ikhlas inapatikana kwa mtu kutokusudia kwa kutamka tamko hilo isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Na hawakuamrishwa isipokuwa tu wamwabudu Mwenyezi Mungu wakimhalisia (wakimtakasia) yeye tu dini, wakiziacha dini zote potofu".*** Sura Albayyina (98), aya 5. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Kwa yakini, Mwenyezi Mungu ameharamisha kuingia motoni mtu aliyetamka Laa ilaaha illallaah akimkusudia Mwenyezi Mungu kwa hilo".* Bukhari.

# KUKIRI KUWA MUHAMMAD NI MTUME WA MWENYEZI MUNGU

Maiti kaburini anatahiniwa na kuulizwa maswali matatu. Akiyajibu, ataokoka na akishindwa kuyajibu, ataangamia. Miongoni mwa maswali hayo ni hili: **Ni nani Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wako?** Hatalijibu swali hilo isipokuwa tu yule ambaye Mwenyezi Mungu amemuwezesha duniani kutekeleza masharti yake, akamuimarisha na kumpa utambuzi kaburini mwake na, kwa hiyo, kukiri kwake huko kukamsaidia Akhera; siku ambayo haitafaa mali wala watoto. Masharti hayo ni haya:

❶ **Kumtii Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika yale aliyoamuru:** Mwenyezi Mungu ametuamuru kumtii Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na kusema kuwa: ***"Yeyote anayemtii Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa hakika amemtii Mwenyezi Mungu".*** Sura Annisaa (4), aya 80. Aidha, Mwenyezi Mungu amesema kuwa: ***"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, nifuateni atakupendeni Mwenyezi Mungu".*** Sura Aal-imran (3), aya 31. Ujumla wa kuingia Peponi unafungamana na ujumla wa kumtii Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Umma wangu wote utaingia Peponi isipokuwa yule aliyekataa. (Swahaba) Walisema: Ewe Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, na ni nani anayekataa? (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Akasema: Aliyenitii, ataingia Peponi na aliyeniasi amekataa (kuingia Peponi)".*** Bukhariy. Yeyote anayempenda Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) hana budi kumtii, kwa sababu utiifu ndio matunda ya kupenda, na ndio ushahidi wa vitendo wa kupenda.

❷ **KUMWAMINI KATIKA YALE ALIYOYAELEZA**: Yeyote anayekanusha jambo lililo sahihi kunukuliwa kutoka kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa sababu ya umashuhuri au mapenzi ya nafsi, basi huyo amemkanusha Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake, kwa sababu Mtume amehifadhiwa kufanya makosa na kusema uongo. ***"Na hatamki kutokana na mapenzi ya nafsi. Hayakuwa hayo (atamkayo) isipokuwa tu ni wahyi (ufunuo) ufunuliwao".*** **Sura Annajmi (53), aya 3 – 4.**

❸ **Kuyaepuka mambo aliyoyakataza:** Kuanzia madhambi makubwa sana na ambayo ni shirk, kupitia madhambi makubwa na yanayoangamiza na kuishia madhambi madogo na yanayochukiza. **Kwa kiasi cha mtu kumpenda Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake, ndivyo imani yake inavyo ongezeka**. Imani ya mtu inapo ongezeka, Mwenyezi Mungu humfanya apende mambo mema na kumfanya achukie ukafiri, uovu na uasi.

❹ **Kutoabudiwa Mwenyezi Mungu isipokuwa tu kwa yale aliyoyaweka Mwenyezi Mungu kupitia mdomo wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake**: Msingi katika ibada ni kukatazwa. Kwa hiyo, haifai kumwabudu Mwenyezi Mungu isipokuwa tu kwa yale yaliyonukuliwa kwa Mtume. (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mtume amesema kuwa: *"Yeyote aliyefanya amali ambayo katika amali hiyo hakuna amri yetu, amali hiyo ni yenye kurudishwa".* Muslim. Maana ni kuwa amali hiyo atarudishiwa mwenyewe.

►**Faida:** Fahamu kwamba kumpenda Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na kuyapenda yale aliyokuja nayo ni wajibu. Yeyote

aliyechukia jambo katika yale aliyokuja nayo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) hata kama atalifanya, huyo atakuwa amekufuru. Haitoshi kupenda tu, **bali hakuna budi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) awe mpendwa zaidi kwako kuliko kila kitu; kuliko hata nafsi yako**. Anayekipenda kitu, hukipa kipaumbele na hutanguliza kukiafiki. Mkweli katika kumpenda Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni yule ambaye zinaonekana wazi kwake alama za mapenzi hayo kwa: kumuiga, kufuata mwenendo wake kwa kauli na vitendo, kutii amri zake na kuyaepuka aliyoyakataza, kufuata maadili yake katika uzito wake na wepesi wake, katika kufurahi kwake na kukereka kwake. **Utiifu na kuiga ndio matunda ya kupenda**, na bila ya hayo, mapenzi sio ya kweli. Kumpenda Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuna alama nyingi. Miongoni mwa alama hizo ni hizi: **1)** Kumtaja sana na kumuombea rehema sana. Anayekipenda kitu, hukitaja sana. **2)** Kuwa na shauku ya kukutana naye. Kila apendaye, huwa na shauku ya kukutana na mpenzi wake. **3)** Kumtukuza na kumheshimu wakati wa kumtaja. Is-haq, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: "Swahaba wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, baada yake walikuwa hawamtaji isipokuwa kwamba wanakuwa wanyenyekevu, ngozi zao husisimka na wanalia. **4)** Kuwachukia wale ambao Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliwachukia. **5)** Kuwafanya adui wale ambao walimfanyia uadui Mtume. (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) **6)** Kuwatenga wanaopinga Suna zake na kuanzisha Bid'a (uzushi) katika dini yake; ambao ni watu wa Bid'a na wanafiki. **7)** Kuwapenda wale ambao Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliwapenda, na ambao ni wake zake, wanafamilia wake na Swahaba wake; Muhajirina na Ansaar. **8)** Kuwafanya adui wale waliowafanya adui watu hao ambao Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliwapenda, na kuwachukia waliowachukia na kuwatukana. **9)** Kuiga tabia zake tukufu, kwani Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa mtu karimu sana, hata Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, alisema kuwa: "Tabia za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu zilikuwa Qur'ani"; kwa maana kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alijilazimisha kutofanya isipokuwa tu yale ambayo Qur'ani imemuamrisha.

**Ama sifa za Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ni kwamba: 1)** Alikuwa shujaa sana. Ushuja wake ulikuwa zaidi wakati wa vita vikali. **2)** Alikuwa mkarimu sana. Ukarimu wake ulikuwa zaidi katika mwezi wa Ramadhani. **3)** Alikuwa mtoaji nasaha sana kwa watu. **4)** Alikuwa mtu mpole sana. Hakupatapo kulipiza kisasi kwa ajili ya nafsi yake. **5)** Alikuwa mtu mkali sana katika amri za Mwenyezi Mungu. **6)** Alikuwa mtu mnyenyekevu sana, mwenye heshima. **7)** Alikuwa mwenye haya sana kuliko binti bikira awapo nyumbani kwake. **8)** Alikuwa mwema sana kwa familia yake. **9)** Alikuwa kiumbe mwenye huruma sana kwa viumbe (wenzake). Kuna sifa nyingine nyingi zaidi ya hizo.

# TWAHARA

Sala ni ya pili katika nguzo za Uislamu. Sala haisihi isipokuwa tu kwa Twahara, na Twahara haiwi isipokuwa tu kwa maji au mchanga.

**AINA ZA MAJI: 1) Maji Twahara.** Haya ni maji ambayo yenyewe ni Twahara na yanatwaharisha kitu kingine. **2) Maji Najisi.** Haya ni maji yaliyokutana na najisi, iwapo maji hayo ni machache, au imebadilika ladha yake au rangi yake au harufu yake kwa najisi, iwapo maji hayo ni mengi.

**UZINDUSHI:** Maji mengi hayawi najisi isipokuwa tu najisi itakapobadilisha mojawapo ya sifa zake; rangi yake au ladha yake au harufu yake. Maji machache yanakuwa najisi kwa kukutana na najisi. Maji yanaitwa mengi pale yatakapokuwa zaidi ya Kullataini. Kullataini ni takriban lita mia mbili na kumi (210).

**VYOMBO:** Vyombo vyote ni twahara, ni halali kuwa navyo na kuvitumia, isipokuwa tu vyombo vya dhahabu na fedha. Twahara kwa kutumia vyombo vya dhahabu na fedha inakuwa sahihi, pamoja na kupata dhambi. Vyombo na nguo za makafiri ni halali isipokuwa tu tukijua kuwa ni najisi.

**NGOZI YA MNYAMA MFU:** Ngozi ya mnyama mfu kwa jumla ni najisi. Mnyama mfu ni mojawapo ya aina mbili: **1)** Mfu ambaye nyama yake kwa hali yoyote hailiwi. **2)** Mfu ambaye nyama yake inaliwa na lakini hakuchinjwa.
Mnyama ambaye nyama yake inaliwa na hakuchinjwa iwapo ngozi yake itasafishwa, inafaa kuitumia katika matumizi ya vitu vikavuvikavu na sio vitu vya majimaji.

**KUSTANJI:** Kustanji ni kusafisha kilichotoka katika tupu ya mbele au ya nyuma. Iwapo usafishaji utafanyika kwa maji, unaitwa Istinjai (kustanji), na ikiwa utafanyika kwa jiwe au karatasi na mfano wake unaitwa Istijmari (kupangusa). Inashartiwa kwa Istijmari tu, ili ifae, iwe: **1)** Kwa kitu twahara, halali, kinachosafisha, kisicholiwa. **2)** Kwa mawe matatu au zaidi. Istinjai na Istijmari ni wajibu kwa kila kinachotoka.

**Ni haramu kwa anayekwenda haja: 1)** Kukaa katika hali yake hiyo zaidi ya kiasi cha haja yake. **2)** kukidhi haja kubwa au ndogo katika chanzo cha maji au njia inayotumika au chini ya kivuli chenye faida au chini ya mti wenye matunda. **3)** Kuelekea Kiblah katika jangwa.

**Ni makuruhu [haipendezi] kwa anayekwenda haja: 1)** Kuingia chooni na kitu ambacho kina jina la Mwenyezi Mungu. **2)** Kuzungumza wakati wa kukidhi haja. **3)** Kukojoa katika ufa na mfano wake. **4)** Kushika tupu kwa mkono wake wa kulia. **5)** Kuelekea Kiblah katika choo kilichojengwa. Haya yaliyotajwa yanaweza kufaa kufanyika kwa dharura.

**Inapendekezwa kwa anayekwenda haja: 1)** Kufanya witri katika idadi za kuosha au kupangusa. **2)** Kufanya kwa pamoja; kupangusa na kuosha kwa maji.

**MSWAKI:** Ni suna kupiga mswaki kwa mti laini, kama mpilipilitawa. Kupiga mswaki kunasisitizwa wakati wa: **1)** Kusali. **2)** Kusoma Qur'ani. **3)** Kutawadha, kabla ya kusukutua. **4)** Kuamka kutoka usingizini. **5)** Kuingia msikitini au nyumbani. **6)** Kubadilika kwa harufu ya kinywa.

**Ni suna** kuanza upande wa kulia katika kupiga mswaki na katika Twahara.

**Na ni suna** kutumia mkono wa kushoto katika kuondoa visivyopendeza.

**UDHU**: **Nguzo Zake: 1)** Kuosha uso, na ni miongoni mwa kuosha uso kusukutua na kupandisha maji puani. **2)** Kuosha mikono miwili kuanzia ncha za vidole mpaka

kwenye fundo (kongo). **3)** Kupaka maji kichwa chote pamoja na masikio. **4)** Kuosha miguu pamoja na nguyu (fundo). **5)** Kupangilia. **6)** Kufululiza.

**Suna Zake: 1)** Kupiga mswaki na kuosha viganja mwanzo wa udhu. **2)** Kutanguliza kusukutua na kupandisha maji puani kabla ya kuosha uso. **3)** Kufikisha maji mbali zaidi katika kusukutua na kupandisha maji puani kwa mtu ambaye hakufunga. **4)** Kupitisha vidole (kuatulia) katika ndevu nyingi. **5)** Kupitisha vidole (kuatulia) katika vidole (vya mikono na miguu). **6)** Kupaka maji masikio. **7)** Kuanza kuosha kiungo cha kulia kabla ya cha kushoto. **8)** Kuosha viungo mara mbili na mara tatu. **9)** Kupandisha maji puani kwa mkono wa kulia na kuyapumua kwa mkono wa kushoto. **10)** Kusu`gua viungo. **11)** Kutawadha vizuri (viungo kuvieneza maji vizuri). **12)** Kuomba dua zilizothibiti baada ya kutawadha.

**Wajibu Wake: 1)** Kusema *Bismillahi* kabla ya kutawadha. **2)** Kuosha viganja vya mikono mara tatu kwa aliyeamka kutoka usingizi wa usiku kabla ya kuviingiza viganja hivyo katika maji.

**Makuruhu Yake (mambo yasiyopendeza): 1)** Kutawadha kwa maji sana baridi au moto sana. **2)** Kuzidisha kuosha kiungo kimoja zaidi ya mara tatu. **3)**Kukung'uta maji viungoni. **4)** Kuosha ndani ya macho. Ama kukausha viungo baada ya kutawadha, ni jambo linalofaa.

**ANGALIZO:** Ni lazima kuyatikisa maji ndani ya mdomo katika kusukutua. Pia ni lazima kuyaingiza maji puani kwa kupumua na sio kwa mdomo katika kupandisha maji puani, na hivyo hivyo pia katika kuyapumua maji. Kusukutua, kupandisha maji puani na kuyapumua hakuwi sahihi isipokuwa kwa namna hii tu.

**NAMNA YA KUTAWADHA:** Ni mtu kunuwia kwa moyo wake. Halafu atasema: Bismillaah (Kwa jina la Mwenyezi Mungu), na kuosha viganja vya mikono yake. Halafu atasukutua na kupandisha maji puani. Halafu ataosha uso wake. Mpaka wa uso ni kuanzia kwenye maoteo ya kawaida ya nywele za kichwa mpaka kwenye kidevu kwa urefu, na kuanzia sikio mpaka sikio kwa upana. Halafu ataosha mikono yake pamoja na *dhiraa* na kongo (fundo) zake. Halafu atapaka maji sehemu yote ya nje ya kichwa chake, kuanzia mpaka wa uso hadi kichogoni mwake. Weupe uliopo juu ya masikio ni sehemu ya kichwa. Ataingiza vidole vyake vya shahada katika pande za ndani za mikunjo ya masikio yake, na atapaka maji kwa vidole vya gumba sehemu za nje za masikio hayo. Halafu ataosha miguu yake pamoja na nguyu (fundo) zake.

**ANGALIZO:** Ndevu zikiwa kidogo, ni wajibu kuosha ngozi iliopo chini yake. Ndevu zikiwa nyingi, zinaoshwa juu yake.

**KUPAKA MAJI KHOFU:** Khofu ni vazi la mguuni (kama kiatu), iwe ni ngozi au mfano wake. Vazi hilo likiwa ni la sufi na mfano wake, huitwa *soksi.* Kupaka maji juu yake inafaa katika Hadathi ndogo tu.

**Kupaka maji inafaa kwa masharti: 1)** Mtu kuvaa Khofu akiwa katika Twahara kamili (baada ya kuosha mguu wa pili katika udhu). **2)** Twahara yake iwe imefanyika kwa maji. **3)** Khofu ziwe zimefinika sehemu ya wajibu (kuoshwa) **4)** Khofu ziwe halali. **5)** Ziwe zimetengenezwa kwa kitu Twahara.

**KILEMBA:** Inafaa kupaka maji juu ya kilemba kwa masharti: **1)** Kilemba kiwe cha mwanaume. **2)** Kilemba kiwe kimefinika sehemu ya kawaida ya kichwa. **3)** Upakaji maji uwe kwa sababu ya Hadathi Ndogo. **4)** Twahara iwe kwa maji.

**USHUNGI:** Inafaa kupaka maji ushungi kwa masharti: **1)** Ushungi uwe wa mwanamke.**2)** Ushungi uwe umezungushwa kuanzia chini ya koo. **3)** Upakaji maji uwe kwa sababu ya Hadathi Ndogo. **4)** Twahara iwe kwa maji. **5)** Ushungi uwe umefinika sehemu ya kawaida ya kichwa.

**MUDA WA KUPAKA:** Kwa mkazi ni siku moja, na kwa msafiri anaesafiri safari ambayo masafa yake yameruhusiwa kisheria kupunguza swala (85km) ni siku tatu(michana mitatu na usiku wake).

**MWANZO WA KUPAKA:** Muda unaanza tokea upakaji wa kwanza baada ya Hadathi iliyotokea baada ya kuvaa Khofu, mpaka muda huo huo kwa kesho yake kwa mkazi (yaani saa 24).

**FAIDA:** Mtu ambaye amepaka akiwa safarini halafu akawa mkazi, au alipaka akiwa mkazi halafu akawa safarini, au akiwa na shaka ya muda wa kuanza kupaka, atapaka kama mkazi.

**KIWANGO KINACHOPAKWA KATIKA KHOFU:** Kiwango chake cha juu zaidi ni kuanzia vidole vya miguu yake mpaka kwenye muundi wake. Upakaji unatakiwa uwe kwa vidole vya mikono yake huku vikiwa vimetenganishwa.

**KICHANJA:** Kichanja ni vijiti ambavyo mifupa (iliyovunjika) na mfano wake huungwa kwavyo. Inafaa kupaka maji kichanja kwa masharti: **1)** Kichanja kiwe kinahitajika. **2)** Kichanja kiwe hakikuvuka sehemu yenye tatizo. **3)** Kuwepo mfululizo kati ya kupaka maji kichanja na kati ya kuosha viungo vingine katika kutawadha. Endapo kichanja kitavuka sehemu yenye tatizo, itawajibika kuiondoa sehemu iliyozidi katika kichanja hicho. Akichelea madhara kwa kufanya hivyo, itamtosha kupaka maji juu yake.

**FAIDA:** ✸ Jambo bora zaidi ni kupaka maji Khofu zote kwa pamoja bila ya kutanguliza ya kulia. ✸ Sio sheria kupaka maji chini ya Khofu wala kisigino chake. ✸ Ni makuruhu kuosha Khofu badala ya kupaka, na pia kurudiarudia kupaka. ✸ Kilemba na ushungi ni wajibu kupaka sehemu yake nyingi zaidi.

**MAMBO YANAYOTENGUA UDHU:** **1)** Kinachotoka katika njia ya mkojo na kinyesi, sawa kinachotoka kiwe ni twahara kama vile hewa na manii,au kiwe ni najisi kama vile mkojo na madh-yi. **2)** Kuondokwa na utambuzi kwa kulala au kuzirai isipokuwa usingizi mdogo mtu akiwa amekaa au amesimama, kwani usingizi huo hautengui udhu. **3)** Kutoka kwa mkojo au kinyesi katika sehemu isiyokuwa yake. **4)** Kutoka kwa kitu najisi (sio mkojo wala kinyesi) katika mwili wake kikiwa ni kibaya kama vile damu nyingi. **5)** Kula nyama ya ngamia. **6)**Kushika tupu (sehemu ya siri) bila ya kizuizi kwa mkono. **7)** Kushika kiungo cha siri cha mwanaume kwa mwanamke au kinyume chake kwa kutamani na bila ya kinga. **8)** Kutoka katika dini (Kuritadi).

Aliye na yakini (hakika) ya Twahara na (halafu) akawa na shaka ya Hadathi au kinyume chake, ataegemea kwenye yakini.

**JOSHO (KUOGA) MAMBO YANAYOWAJIBISHA KUOGA: 1)** Kutokwa kwa Manii kwa matamanio au kutoka kwa Manii kwa matamanio au bila ya matamanio kwa mtu aliyelala. **2)** Kuingiza kichwa cha kiungo cha siri cha mwanaume katika tupu ya mwanamke, hata kama *Manii* hayakutoka. **3)** Kafiri kuingia katika Uislamu, hata kama alikuwa murtadi. **4)** Kutoka kwa damu ya Hedhi. **5)** Kutoka kwa damu ya uzazi *(Nifasi)*. **6)** Mwislamu kufa.

**FARADHI ZA KUOGA:** Inatosha kuueneza maji mwili wote kwa niya ya kuoga na ndani ya pua na mdomo. Kuoga kikamilifu kunapatikana kwa kufanya mambo tisa: **1)** Kunuia. **2)** Kusema: *Bismillah* = Kwa jina la Mwenyezi Mungu naanza kuoga. **3)** Mtu kuosha mikono yake kabla ya kuiingiza katika chombo. **4)** Mtu kuosha sehemu zake za siri na sehemu nyingine zilizochafuka. **5)** Kutawadha. **6)** Kumimina maji kichwani mwake mara tatu. **7)** Kuumiminia maji mwili wake. **8)** Kusugua mwili wake kwa mikono yake. **9)** Kuanza upande wa kulia.

**YALIYO HARAMU KWA MWENYE HADATHI NDOGO: 1)** Kugusa Msahafu. **2)** Kuswali. **3)** Kutufu (Al-kaabah).

**YALIYO HARAMU KWA MWENYE HADATHI KUBWA:** Ni haramu kwa mwenye Hadathi kubwa pamoja na yaliyotangulia: **4)** Kusoma Qur'ani. **5)** Kukaa msikitini.

**Ni makuruhu kwa mwenye Janaba: 1)** Kulala bila ya Udhu. **2)** Kufanya ubadhirifu katika kuoga.

**KUTAYAMAMU: MASHARTI YAKE: 1)**Kushindikana kwa maji. **2)**Kutayamamu kufanyike kwa mchanga twahara, halali, wenye vumbi na usiochomwa.

**NGUZO ZAKE: 1)** Kupaka uso wote, halafu. **2)** Kupaka mikono (viganja) mpaka kwenye fundo zake mbili. **3)** Kupangilia. **4)** Kufululiza.

**YANAYOBATILISHA: 1)** Kila jambo linalobatilisha Udhu. **2)** Kupatikana kwa maji ikiwa mtu alitayamamu kwa kukosa maji. **3)** Kuondoka kwa jambo lililoruhusu kutayamamu huko, kama vile mtu aliyetayamamu kwa sababu ya ugonjwa na akawa amepona.

**SUNA ZAKE: 1)** Kupangilia na kufululiza kwa kutayamamu kunakotokana na Hadathi Kubwa. **2)** Kuahirisha kutayamamu mpaka mwisho wa wakati (wa ibada anayokusudia kuifanya). **3)** Kuleta uradi wa Udhu baada ya kutayamamu.

**YALIYO MAKURUHU:** Kurudiarudia mapigo (kwenye mchanga).

**NAMNA YA KUTAYAMAMU:** Ni mtu kunuia halafu kusema Bismillah. Kwa mikono yake, atapiga kwenye mchanga pigo moja. Halafu atapaka uso wake kwanza kwa kupitisha sehemu ya ndani ya viganja vyake juu ya uso wake na ndevu zake. Halafu atapaka viganja vyake; sehemu ya juu ya kiganja chake cha kulia kwa kutumia sehemu ya ndani ya kiganja chake cha kushoto, na sehemu ya juu ya kiganja cha kushoto kwa sehemu ya ndani ya kiganja cha kulia.

**KUSAFISHA NAJISI: Vitu ni aina tatu**: **1) Wanyama.** Nao ni mafungu mawili: **a)** Wanyama najisi, nao ni mbwa na nguruwe na aliyezaliwa nao. Pia ndege na wanyama ambao nyama zao haziliwi na ambao kwa umbo ni zaidi ya paka ni najisi. Mkojo, kinyesi, mate (ute), jasho, manii, maziwa, kamasi na matapishi ya wanyama wa fungu hili ni najisi. **b)** Wanyama twahara. Wanyama hawa ni aina tatu: **1-** Mwanadamu. Manii yake, jasho lake, mate yake, maziwa yake, kamasi zake, balaghamu yake, majimaji ya sehemu ya siri ya mwanamke ni twahara. Kadhalika, viungo vyake vyote na vitu vyote vitokavyo mwilini mwake ni twahara isipokuwa mkojo, kinyesi, madh-yi, wad-yi na damu. Hivyo ni najisi. **2-** Kila mnyama ambaye nyama yake inaliwa. Mkojo wake, kinyesi chake, manii yake, maziwa yake, jasho lake, ute wake, kamasi zake, matapishi yake, madh-yi na wad-yi yake ni twahara. **3-** Wanyama ambao ni vigumu kujichunga nao, kama punda, paka, panya na mfano wake. Ute na jasho lao tu ni twahara.

**2) Wafu.** Wafu wote ni najisi isipokuwa maiti ya mwanadamu, samaki, nzige na mfu asiyekuwa na damu inayochuruzika, kama n'ge, chunguchungu na mbu.

**3) Vitu visivyokuwa na uhai.** Vitu hivi ni twahara, kama vile ardhi, mawe na mfano wake. (Huopolewa katika vitu visivyokuwa na uhai kila kitu kisichokuwa na uhai ikiwa kitu hicho kitakuwa katika vile vitu vilivyotangulia).

**FAIDA:** ✸ Damu na usaha ni najisi. Najisi hii inasamehewa katika swala na sehemu nyengine iwapo itakuwa chache na ikiwa inatokana na mnyama twahara. ✸ **Damu ni twahara katika vitu vya aina mbili**: **1)** Samaki. **2)** Damu iliyobaki katika nyama na mishipa ya mnyama aliyechinjwa. ✸ Sehemu iliyokatwa ya mnyama anayeliwa na ilhali yuko hai, pande la nyama na pande la damu (litokalo katika mfuko wa uzazi wa mwanamke) vyote hivyo ni najisi. ✸ Kusafisha najisi hakuhitaji kunuia. Najisi kama imeondoka kwa mvua, kwa mfano, twahara imepatikana. ✸ Kugusa najisi kwa mkono au kuikanyaga hakutengui Udhu, isipokuwa tu inapasa kuisafisha na kusafisha sehemu ya mwili na nguo iliyokutana nayo. ✸ **Najisi inasafishika kwa masharti**: **1)** Ioshwe kwa maji twahara. **2)** Kinacho oshwa kikamuliwe nje ya maji, ikiwa kitu kama hicho kinakamulika. **3)** Najisi isafishwe kwa kusugua na mfano wake ikiwa kuosha hakutoshi. **4)** Najisi ioshwe mara saba na mojawapo iwe kwa mchanga au sabuni, ikiwa najisi hiyo ni ya mbwa.

**ANGALIZO:** ✸ Najisi iliopo ardhini, ikiwa ni ya kitu majimaji kama vile mkojo, inatosha kuimiminia maji mpaka najisi yenyewe, harufu yake na rangi yake iondoke. Kama najisi hiyo ni kitu kama vile kinyesi, ni lazima kusafisha kitu najisi chenyewe na pia kusafisha athari yake. ✸ Najisi ikikataa kusafishika isipokuwa kwa maji tu, ni wajibu kuisafisha kwa maji. ✸ Mahali penye najisi pakijificha, pataoshwa mahali hapo mpaka iyakinike kuwa pameoshwa. ✸ Aliyetawadha kwa ajili ya kusali sunna inafaa kusali faradhi kwa Udhu huo. ✸ Sio wajibu kwa aliyelala au kutokwa na hewa kustanji (kujisafisha), kwa sababu hewa ni twahara. Lililo wajibu kwake tu ni kutawadha, ikiwa anataka kusali au kufanya ibada nyingine mfano wake.

# SHERIA ZA MWANAWAKE

## SHERIA ZA DAMU ZA MAUMBILE ZA MWANAWAKE

### KWANZA: HEDHI NA ISTIHADHA

| SUALA | SHERIA |
|---|---|
| **Udogo na ukubwa wa umri ambao mwanamke anapata Hedhi** | Udogo wake ni miaka tisa. Ikitoka damu katika sehemu zake za siri kabla ya umri huo, hiyo ni *Istihadha*[1]. Ukubwa wake hauna kikomo. |
| **Uchache wa siku ambazo damu ya Hedhi inaendelea** | Ni siku moja (saa 24). Ikiwa chini ya hapo, hiyo ni Istihadha |
| **Wingi wa siku ambazo Hedhi inaendelea** | Siku kumi na tano. Damu itokayo ikizidi idadi hii, basi hiyo ni Istihadha |
| **Twahara kati ya Hedhi mbili** | Siku kumi na tatu. Ikitoka damu kabla ya kutimia siku hizo, basi hiyo ni Istihadha |
| **Aghlabu ya Hedhi kwa wanawake** | Siku sita au saba |
| **Aghlabu ya twahara kwa wanawake** | Siku ishirini na tatu au ishirini na nne |
| **Je, damu wakati wa mimba ni Hedhi?** | Kitokacho kwa mwanamke mwenye mimba, iwe ni damu nyekundu au ya Majimaji Kahawia[2] au Majimaji Manjano[3], ni Istihadha |
| **Wakati gani mwanamke mwenye Hedhi anajua kuwa sasa ametwaharika?** | Wanawake ni aina mbili: **1)**Atatwaharika kwa Majimaji Meupe[4] ikiwa atayaona. **2)**Atatwaharika kwa kukauka damu nyekundu au ya kahawia au ya manjano katika tupu yake, ikiwa yeye ni katika wale wasioona maji meupe. |
| **Vitu vya majimaji vitokavyo katika tupu ya mwanamke wakati wa twahara** | Kikiwa ni chepesi au cheupe kinachonata, basi hicho ni twahara. Kikiwa ni damu nyekundu au ya kahawia au ya manjano, basi hiyo ni najisi. Vyote vinabatilisha Udhu. Vikiendelea kutoka, basi hiyo ni Istihadha. |
| **Damu ya kahawia au manjano katika tupu** | Ikiwa imeambatana na Hedhi kabla yake au baada yake, hiyo ni Hedhi. Ikiwa imetengana, hiyo ni Istihadha. |
| **Ambaye ana siku maalum anazopata Hedhi kila mwezi na akaona twahara kabla ya kutimia siku hizo** | Atachukuliwa hukumu kuwa yuko twahara ikiwa damu imekatika na akaona twahara, hata kama siku zake za Hedhi alizozoea kuona damu hazijakwisha. |
| **Kutangulia au kuchelewa kwa Hedhi katika wakati** | Zikibainika sifa za Hedhi, hiyo ni Hedhi wakati wowote kwa sharti tu la kuwepo kwa siku kumi na tatu (uchache wa |

---

[1] Istihadha: Ni damu ya ugonjwa inayochuruzika kutoka katika mshipa uliopo chini ya mfuko wa uzazi. Tofauti kati ya Hedhi na Istihadha ni kwamba: **1)** Damu ya Hedhi ni nyekundu; wekundu wa damu ya mzee inayoelekea kwenye weusi. Damu ya Istihadha ni nyekundu iliyoiva, kama vile damu ya ugonjwa wa kutoka damu puani. **2)** Damu ya Hedhi ni nzito. Wakati mwingine inakuwa na madonge madonge. Ama damu ya Istihadha ni nyepesi inayochuruzika kama vile jeraha linalotweta. **3)** Damu ya Hedhi ina harufu mbaya, aghlabu inanuka. Ama harufu ya damu ya Istihadha ni kama harufu ya damu ya kawaida. Ama kwa upande wa sheria ni kwamba yanakuwa haramu kwa mwanamke mwenye Hedhi yale ambayo ni haramu kwa mwenye Hadathi Kubwa, kama vile kusali,kumuingilia mwanamke katika tupu,talaka,twafu,nakushika musihafu, kukaa msikitini, kusoma Qur'ani, kufunga na mengineyo.

[2] Kud –ra (Majimaji Kahawia): Ni damu inayochuruzika, inayotoka katika tupu. Rangi yake ni ya kahawia iliyokoza.

[3] Sufra (Majimaji Manjano): Ni damu inayochuruzika, inayotoka katika tupu. Rangi yake inamili kwenye manjano.

[4] Qassa Baidhaa(Majimaji Meupe): Ni majimaji meupe yatokayo katika tupu wakati wa twahara. Maji haya ni twahara, lakini yanatengua Udhu.

| | |
|---|---|
| **wake wa kawaida** | twahara) kati ya damu mbili. Vinginevyo, hiyo ni Istihadha. |
| **Hedhi ikizidi au ikipungua katika idadi yake ya kawaida** | Hiyo ni Hedhi kwa sharti isizidi wingi wa Hedhi (Siku kumi na tano) |
| **Damu ikiendelea kutoka kwa mwanamke kwa muda mrefu; mwezi mzima au zaidi** | Atakuwa na hali zifuatazo: **1)** Kuna anayejua: muda wa Hedhi yake kila mwezi, idadi ya siku zake na kutofautisha kati ya Hedhi na damu nyingine. Hapa itatumika idadi na muda wa kawaida na sio sifa za damu. **2)**Kuna anayejua muda wa Hedhi yake kila mwezi na idadi ya siku zake, lakini damu yake iko katika namna moja. Huyu atakaa kiasi cha Hedhi yake kwa muda na idadi. **3)**Kuna anayejua muda wa Hedhi yake kila mwezi, lakini hajui idadi ya siku zake. Huyu atakaa siku sita au saba (Aghlabu ya Hedhi) kwa siku zile zile zinazojulikana. |

## PILI: NIFASI

| SUALA | SHERIA |
|---|---|
| **Mwanamke atakapozaa na asione damu** | Hatatumia sheria za mwanamke mwenye Nifasi, na sio wajibu kwake kuoga na saumu yake haibatiliki. |
| **Mwanamke akiona dalili za uzazi** | Damu, maji pamoja na uchungu atakaouona kabla ya kuzaa kwa muda, haitachukua sheria ya Nifasi, bali hiyo ni *Istihadha.* |
| **Damu itokayo kwa mwanamke wakati wa kuzaa** | Damu hii ni ya Nifasi, hata kama mtoto hajatoka wote au kama ametoka baadhi yake. Sio wajibu kwa mwanamke kulipa sala iliyompita katika muda huu. |
| **Ni wakati gani zinaanza kuhesabiwa siku za Nifasi?** | Baada ya mtoto wote kutoka kuja duniani. |
| **Ni upi uchache wa Nifasi?** | Hakuna ukomo wa uchache wake. Kama mwanamke amezaa halafu damu yake ikakatika mara tu baada ya kuzaa, ni wajibu kuoga na kusali na hatangojea kukamilika kwa siku arobaini. |
| **Ni upi wingi wa Nifasi?** | Ni siku arobaini. Ikizidi, haitoangaliwa, itapasa kuoga na kusali isipokuwa tu ikikutana na kipindi cha Hedhi yake kabla ya mimba. Hapo, itazingatiwa kuwa ni Hedhi. |
| **Aliyezaa pacha wawili au zaidi** | Hesabu ya siku za Nifasi itaanza baada ya mwanamke kuzaa mtoto wa kwanza. |
| **Damu baada ya kipomoko** | Ikiwa umri wa kipomoko ni siku (80) au chini ya hapo, damu baada yake ni Istihadha. Ikiwa umri ni baada ya siku (90), damu baada yake ni Nifasi. Ikiwa umri ni kati ya siku (80) na (90), sheria itafungamana na maumbile. Ikiwa kipomoko hicho kina umbile la mwanadamu, damu baada yake ni Nifasi. Ikiwa kipomoko hakijaumbika, basi hiyo ni Istihadha. |
| **Mwanamke akitwaharika ndani ya siku arobaini halafu damu ikamrudia kabla ya kutimia siku arobaini** | Twahara atakayoiona mwanamke ndani ya siku arobaini za Nifasi, ni twahara. Mwanamke ataoga kwa twahara hiyo na ataswali. Ikimrudia damu ndani ya siku arobaini, damu hiyo itachukua sheria za Nifasi. Itakuwa hivyo hivyo, mpaka siku arobaini zimalizike. |

**ANGALIZO:** ✸ Ni wajibu kwa mwanamke mwenye Istihadha kusali, lakini tu atakuwa **akitawadha kwa kila sala**. ✸ Mwanamke mwenye Hedhi au Nifasi akitwaharika kabla ya jua kuchwa, itamlazimu kusali sala ya Adhuhuri na ya Alasiri ya mchana huu. Akitwaharika kabla ya alfajiri kuchimbuka, atasali sala ya Isha na ya Magharibi ya usiku huu. ✸ Ukimfikia mwanamke wakati wa sala halafu akapata Hedhi au Nifasi kabla ya kuisali sala hiyo, haimlazimu kuilipa. ✸ Ni wajibu kwa mwanamke kufumua nywele zake wakati wa kuoga josho la Hedhi

au Nifasi, na sio wajibu kufumua nywele katika josho la Janaba. ✸ Ni haramu kumjamii (kumuingilia)mke mwenye Hedhi au Nifasi katika tupu yake, na inafaa kustarehe naye katika sehemu isiyokuwa tupu. ✸ Ni makuruhu kumjamii mke mwenye Istihadha katika tupu yake, na ni halali wakati mume akihitaji kufanya hivyo. ✸ Inapendekezwa kwa mwanamke mwenye Istihadha kuoga kwa kila sala. Akishindwa, atakusanya sala ya Adhuhuri na ya Alasiri kwa josho moja, na sala ya Magharibi na ya Isha kwa josho moja, na ataoga kwa ajili ya sala ya Alfajiri. Kwa jumla, yatakuwa majosho matatu katika siku moja. Akishindwa, ataoga mara moja kwa siku na atatawadha kwa kila sala. Akishindwa, atatawadha kwa kila sala baada ya kuoga kwake josho la Hedhi. ✸ Inafaa kwa mwanamke kutumia dawa inayozuia Hedhi kwa muda ili kufanya matukio ya ibada ya Hija na Umra au kukamilisha kufunga Ramadhani, kwa sharti la kuwa dawa hiyo haitamdhuru.

**MWANAMKE KATIKA UISLAMU:** Mwanamke ni kama mwanaume katika malipo na ubora mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa kiasi cha imani na utendaji. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Hakuna vingine isipokuwa kwamba wanawake ni ndugu wa wanaume".*** Abudaud. Mwanamke anayo haki ya kudai haki yake au kuondoa udhalimu anaofanyiwa. Hiyo ni kwa sababu: **1)** Matamshi ya dini yanamhusu mwanaume na mwanamke kwa pamoja, isipokuwa tu yale matamshi yananayo onesha kutofautisha kati yao, na ambayo ni sheria chache ukilinganisha na sheria za dini zilizobaki, na **2)** kwa sababu sheria imezingatia weledi wa mwanaume na mwanamke, kwa mujbu wa maumbile na uwezo. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Hivi hajui yule aliyeumba na ilhali yeye ni Mjuzi wa visivyo onekana, Mjuzi wa vinavyo onekana?".*** Sura Almulk (67), aya 14. Mwanamke ana majukumu yanayomhusu, na mwanaume ana majukumu yake yanayomhusu. Uingiliaji katika yanayomhusu mwengine, unaleta madhara katika mizani ya maisha. Mwanamke amepewa malipo kama ya mwanaume na ilhali yuko nyumbani kwake. Imepokewa kutoka kwa Asmaa Bint Yaziid kwamba alikwenda kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani na ilhali yupo na Swahaba wake, na kumwambia: *"Mimi ni mjumbe wa wanawake kwako,- na ninaijuza nafsi yangu utetezi wako-. Ilivyo ni kwamba hakuna mwanamke yeyote aliyeko mashariki na magharibi amesikia kuja kwangu huku au hakusikia isipokuwa kwamba yeye yupo na muono kama wangu. Kwa yakini, Mwenyezi Mungu amekutuma kwa haki ufikishe ujumbe kwa wanaume na wanawake. Tumekuamini wewe na Mungu wako aliyekutuma. Sisi, mjumuiko wa wanawake, tumedhibitiwa, tumefungwa; ni wakaaji wa nyumba zenu na wakidhiji wa matamanio yenu na wabebaji mimba za watoto wenu. Nyinyi, mjumuiko wa wanaume, mmekuwa bora kwetu kwa kusali sala za Ijumaa na za Jamaa na kuwatembelea wagonjwa na kuhudhuria mazishi na kuhiji mara nyingi. Bora zaidi ya hayo ni kushiriki Jihadi katika dini ya Mwenyezi Mungu. Na mwanaume miongoni mwenu akienda Hija au Umra na akienda vitani, sisi tunakulindieni mali zenu na tunakushoneeni nguo zenu na tunakuleleeni watoto wenu. Hivi hatushirikiani nanyi katika malipo ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Mtume,* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *aligeuka kwa uso wake wote na kuwaelekea Swahaba wake, halafu akasema:* ***"Je, mmewahi***

***kusikiapo maneno ya mwanamke yaliyokuwa mazuri sana katika kuuliza kwake mambo ya dini yake kuliko ya mwanamke huyu?*** *(Swahaba)Walisema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hatukudhani kuwa mwanamke anaweza kuwa na mawazo ya uongofu kama haya. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aligeuka kumwelekea yule mwanamke, halafu akamwambia:* ***"Nenda zako, ewe mwanamke, na wajulishe wanawake walioko nyuma yako kwamba kujipamba kwa mmoja wenu kwa ajili ya mume wake na kuhangaika kwake kumridhisha na kufuata kwake anayoyaafiki, kunalingana na yote hayo (uliyoyataja awali)".*** Baihaqiy. Walikuja wanawake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na kusema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wanaume wamepata ubora kwa kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Je, na sisi hatuna amali (ya kufanya) ambayo kwayo tutafikia amali ya wanaopigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu? Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu alisema: ***"Kazi za mmoja wenu nyumbani kwake, zinafikia amali ya wanaopigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu".*** Baihaqiy. Mwenyezi Mungu pia amefanya kumtendea mazuri ndugu mwanamke ni jambo lenye malipo makubwa. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Mwenye kutoa huduma kwa watoto (wake) wawili wa kike au ndugu (zake) wawili wa kike au wanawake wawili wenye udugu akikusudia kulipwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwahudumia huko, mpaka Mwenyezi Mungu awatoshe au awape uwezo kutokana na fadhila zake, wawili hao watakuwa siatara ya moto kwake".*** Ahmad, Tabaraniy.

## BAADHI YA SHERIA ZA WANAWAKE:

- Ni haramu mwanaume kukaa faragha na mwanamke asiyekuwa na maharimu[1]. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Asikae faragha, asikae faragha, asikae faragha Mwanaume na mwanamkea isipokuwa tu mwanamke anapokuwa pamoja na maharimu".*** Bukhariy, Muslim.

- Inafaa kwa mwanamke kusali msikitini. Iwapo kutakuwa na hofu ya mtihani (wa mambo machafu), inakuwa jambo lisilopendeza. Aisha (mke wa Mtume), (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: ***"Lau kama Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, angediriki kuyaona waliyoyazusha wanawake, angewazuia kwenda misikitini, kama walivyozuiwa wanawake wa Wanaisraeli".*** Bukhariy, Muslim. Kama ambavyo kusali kwa mwanaume msikitini kunarudufisha thawabu, ni hivyo hivyo kusali kwa mwanamke nyumbani kwake. Mwanamke mmoja alikwenda kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na kumwambia: *"Mimi napenda kusali na wewe. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akasema:*

---

[1] Maharimu wa mwanamke ni wale watu ambao inakuwa haramu kwao kumuoa mwanamke huyo uharamu wa kudumu. Hao ni: Baba, babu na kwenda juu. Mtoto wa kiume, mjukuu wa kiume na kwenda chini. Ndugu wa kiume na watoto wake. Watoto wa ndugu wa kike. Baba mdogo au mkubwa, mjomba, baba wa mume na kwenda juu. Mtoto wa kiume wa mume na kwenda chini. Baba, mtoto wa kiume na ndugu wa kiume wa kunyonya. Mume wa mtoto wa kike na mume wa mama.

***"Nimeshajua kwamba wewe unapenda kusali pamoja nami, na (lakini) kusali kwako chumbani kwako ni bora zaidi kuliko kusali kwako nyumbani kwako, na kusali kwako nyumbani kwako ni bora zaidi kuliko kusali kwako mtaani kwako, na kusali kwako mtaani kwako ni bora zaidi kulikokusali kwako katika msikiti wa watu wako, na kusali kwako katika msikiti wa watu wako ni bora zaidi kuliko kusali kwako katika msikiti wangu".*** Ahmad. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Misikiti bora zaidi ya wanawake ni nyumba zao".*** Ahmad.

✸Sio wajibu kwa mwanamke kwenda Hija na Umra isipokuwa tu atakapopata maharimu atakaye fuatana naye. Haruhusiwi kusafiri bila ya maharimu, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: ***"Asisafiri mwanamke zaidi ya siku tatu isipokuwa tu (atakapokuwa) pamoja na maharimu".*** Bukhariy, Muslim.

✸Ni haramu kwa mwanamke kuzuru makaburi na kusindikiza Jeneza, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: ***"Mwenyezi Mungu anawalaani wanawake wanaozuru sana makaburi".*** Ahmad, Tirmidhiy. Mama Atiyyah, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: ***"Tulikatazwa kusindikiza Jeneza na (hilo) halikutiliwa mkazo kwetu".*** Muslim.

✸Inaruhusiwa kwa mwanamke kupaka rangi yoyote nywele za kichwa chake, na ni makuruhu kupaka rangi nyeusi, kwa sharti la kutokuwepo kumdanganya anayetaka kuchumbia katika kufanya hivyo.

✸Ni wajibu mwanamke kupewa sehemu yake ya mirathi ambayo Mwenyezi Mungu amempangia, na ni haramu kumnyima. Imepokewa kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam ) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba amesema: ***"Yeyote aliyezuia mirathi ya mrithi wake, Mwenyezi atamnyima mirathi yake ya peponi Siku ya Kiyama".*** Ibn-maajah.

✸Ni wajibu kwa mume kumhudumia mke wake. Huduma ni kila kitu ambacho mkewe hana budi nacho kwa wema (kawaida inayokubalika), kama: chakula, kinywaji, nguo na makazi. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Atoe (huduma) mwenye uwezo kutokana na uwezo wake. Na yule ambaye riziki yake imekuwa ndogo, atoe katika kile ambacho Mwenyezi Mungu amempa".*** Sura Attalaaq (65), aya 7. Kama mwanamke hana mume, wajibu wa kumhudumia unakuwa juu ya baba yake au ndugu yake wa kiume au mtoto wake wa kiume. Ikiwa mwanamke hana ndugu, inapendekezewa huduma itoke kwa watu wengine, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: ***"Mwenye kumhangaikia mjane na masikini, anakuwa kama mwenye kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu au kama mtu ambaye anasali usiku na kufunga saumu mchana".*** Bukhariy, Muslim.

✸Mwanamke ndiye mwenye haki zaidi ya kumlea mtoto wake mdogo, madamu hajaolewa, na ni wajibu wa baba yake kutoa huduma kumpa mama yake, madamu mtoto huyo yuko katika mikono ya mama yake huyo.

✸Haipendekezwi kuanza kumsalimia mwanamke, hasa anapokuwa msichana au ukihofiwa mtihani (wa kupelekea mambo machafu).

✸Inapendekezwa kunyoa (nywele za) kinena, kunyonyoa (nywele za) kwapa na kukata kucha, kila siku ya Ijumaa. Ni makuruhu kuacha kufanya hayo zaidi ya siku arobaini.

✸Ni haramu kunyonyoa nywele za uso, na ni miongoni mwa nywele hizo nyusi, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: ***"Mwenyezi Mungu amemlaani (mwanamke mwenye kunyonyoa nywele za uso na mwenye kunyonyolewa"***.Abudaud.

✸ **KUOMBOLEZA:** Ni haramu kwa mwanamke kuomboleza zaidi ya siku tatu kwa ajili ya maiti isipokuwa tu kwa ajili ya mume, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: ***"Sio halali kwa mwanamke anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuomboleza kwa ajili ya maiti zaidi ya siku tatu isipokuwa tu kwa ajili ya mume wake"***.Muslim. Kwa hiyo, ni wajibu kwake kuomboleza kwa ajili ya mumewe miezi minne na siku kumi. Katika kuomboleza huko, ni wajibu kwake kuacha mapambo na manukato, kama Zafarani, kuvaa vito japo ni pete, nguo zenye rangi ya mapambo kama nyekundu na manjano, kujipamba kwa hina au rangi, kujipaka wanja mweusi na mafuta mazito yanayonukia. Inaruhusiwa kwake kukata kucha, kunyonyoa (nywele za) kwapa na kuoga. Sio wajibu kuvaa nguo ya rangi maalum, kama nyeusi. Ni wajibu kukaa eda katika nyumba ambayo mumewe amefariki na ilhali yeye yumo humo, na ni haramu kuondoka humo isipokuwa tu kwa dharura. Hatakiwi kutoka nyumbani kwake mchana isipokuwa kwa dharura.

✸Ni haramu kwa mwanamke kunyoa nywele za kichwa chake bila ya dharura, na inaruhusiwa kuzipunguza kwa sharti la kutojifananisha na wanaume, kwa mujibu wa Hadithi hii: ***"Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu amewalaani wanawake wanaojifananisha na wanaume na wanaume wanaojifananisha na wanawake"***. Tirmidhiy. Pia ni haramu kujifananisha na makafiri, kwa mujibu wa Hadithi hii: ***"Na yeyote aliyejifananisha na watu, basi yeye ni katika wao"***.Abudaud.

✸Ni wajibu kwa mwanamke atokapo nyumbani mwake kuvaa buibui ambalo yanapatikana ndani yake masharti yafuatayo: **1)** Lifinike mwili wote. **2)** Lenyewe lisiwe urembo. **3)** Liwe zito lisilo onesha. **4)** Liwe pana lisilo bana. **5)** Lisiwe limewekwa manukato. **6)** Lisifanane na nguo za wanaume. **7)** Lisifanane na nguo za makafiri. **8)** lisiwe vazi la ufahari.

✸Ni haramu kuvaa vazi ambalo lina picha ya binadamu au mnyama na kuitundika, kufinika ukuta kwayo na kuiuza. **Uchi wa mwanamke akiwa pamoja na mtu mwengine ni aina tatu: 1)** Mume. Yeye anaruhusiwa kuona kwa mkewe atakacho. **2)**Wanawake wenziwe na maharimu. Wao wanaruhusiwa kuona sehemu ambazo aghlabu zinakuwa wazi, kama uso, nywele, shingo, mkono, mguu na mfano wa hayo. **3)**Wanaume waliosalia (sio mume na maharimu). Hawa hawatakiwi kuona chochote kwa mwanamke, isipokuwa tu kwa dharura, kama kuchumbia au matibabu na mfano wa hayo, kwa sababu mtihani wa mwanamke unapatikana kwa uso wake. Fatma Bint Mundhir, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: ***"Wasafiri walikuwa wakipita kwetu na ilhali sisi tuko pamoja na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu. Wanapotuelekea, mmoja wetu anateremsha nguo yake kuanzia kichwani mwake mpaka kwenye uso wake. Wakitupita, tunaifunua"***. Abudaud.

✸ **EDA:** Ni aina nyingi: **1)Mwenye mimba:** Eda ya kuachwa na ya kufiwa inakwisha kwa kuzaa mimba yake. **2)Mwenye kufiwa na mumewe:** Eda yake ni miezi minne na siku kumi. **3)Aliyachwa na ilhali ana kawaida ya kupata hedhi:** Eda yake ni Hedhi tatu. Eda itakwisha kwa twahara itakayotokana na Hedhi ya tatu. **4)Ambaye hana kawaida ya kupata Hedhi:** Eda yake ni miezi mitatu. Mwanamke aliyemo ndani ya eda inayotokana na kuachwa Talaka Rejea, anawajibika kukaa na mumewe wakati wa Eda, na inaruhusiwa kwa mume kuona kwa mkewe huyo akitakacho na kukaa naye faragha, pengine Mwenyezi Mungu anaweza kuleta muafaka baina yao. Kurejea hakuhitaji ridhaa ya mwanamke, kama Talaka ni ya rejea. Kurejea kunapatikana kwa mume kusema: Nimekurejea au kwa kujamiiana.

✸Mwanamke hawezi kujiozesha mwenyewe. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Mwanamke yeyote aliyeolewa bila ya idhini ya Walii wake, ndoa yake ni batili".*** Abudaud.

✸Ni haramu kwa mwanamke kuunganisha nywele zake kwa nywele nyingine na kuchora (kwa kutoboa) sehemu yoyote katika mwili wake. Vitendo hivi viwili ni katika dhambi kubwa, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: ***"Mwenyezi Mungu amemlaani mwanamke mwenye kuunganisha nywele na mwenye kuunganishwa, na mwenye kuchora kwa (kutoboa) na mwenye kuchorwa".*** Bukhariy, Muslim.

✸Ni haramu kwa mwanamke kumomba Talaka mume wake bila ya sababu, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) isemayo kuwa: ***"Mwanamke yeyote aliyemuomba mumewe Talaka bila ya uovu wowote, ni haramu kwake harufu ya Pepo".*** Abudaud.

✸Ni wajibu kwa mwanamke kumtii mume wake kwa wema, hasa amuitapo kitandani. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Mtu atakapomuita mkewe kitandani akakataa kwenda na kwa hiyo mume akalala ilhali amekasirika, Malaika wanamlaani mwanamke huyo mpaka afikapo asubuhi".*** Bukhariy, Muslim.

✸Ni haramu kwa mwanamke kujifukiza manukato iwapo anajua kuwa njiani kwake apitako atakutana na wanaume kando (sio mume na sio maharimu), kwa mujibu wa Hadithi hii: ***"Mwanamke ajitiapo manukato na hivyo akajipitisha kwa wanaume ili wanuse harufu yake, yeye ni hivi na hivi; yaani: Ni mzinifu".***Abudaud.

# SALA

**ADHANA NA IQAMA:** Kuadhini na Kuqimu mjini ni *faradhi kifaya* (ya kutoshelezana) kwa wanaume. Ni suna kwa anayesali peke yake na msafiri. Ni makuruhu kwa wanawake. Sio sahihi kuadhini na kuqimu kabla ya wakati (wa sala) isipokuwa tu alfajiri. Ni sahihi kuadhini Adhana ya kwanza ya sala ya Alfajiri baada ya nusu ya usiku.

**MASHARTI YA SALA:** **1)** Uislamu. **2)** Akili timamu. **3)** Utambuzi. **4)** Twahara pamoja na kuweza. **5)** Kuingia kwa wakati. **Wakati wa sala ya Adhuhuri** ni kuanzia kupinduka kwa jua mpaka kivuli cha kila kitu kiwe mfano wake. Halafu unaingia **wakati wa sala ya Alasiri**. Muda wa hiyari katika wakati huo ni mpaka kivuli cha kila kitu kiwe mara mbili yake. Halafu unaingia wakati wa dharura ambao unaendelea mpaka kuchwa kwa jua. Halafu unafuatia **wakati wa sala ya Magharibi** unaoendelea mpaka kupotea kwa mawingu mekundu. Halafu unaingia **wakati wa sala ya Isha.** Muda wa hiyari katika wakati huo ni mpaka nusu ya usiku. Halafu unaingia wakati wa dharura unaoendelea mpaka kuchimbuka kwa alfajiri. Halafu unaingia **wakati wa sala ya Alfajiri** unaoendelea mpaka kuchimbuka kwa jua. **6)** Kusitiri uchi.[1] **7)** Kutokuwepo najisi katika mwili wake, katika nguo yake na katika eneo lake (analosali), pamoja na kuweza. **8)** Kuelekea Kibla pamoja na kuweza. **9)** Kunuia.

**NGUZO ZA SALA:** Ni kumi na nne. **1)** Kusimama katika sala ya faradhi, pamoja na kuweza. **2)** Takbira ya kuanzia sala. **3)** Kusoma sura Alfatiha. **4)** Kurukuu katika kila rakaa. **5)** Kunyanyuka kutoka katika kurukuu. **6)** Kuitadili baada ya kurukuu huku mtu akiwa amesimama. **7)** Kusujudu juu ya viungo saba. **8)** Kitako kati ya sijda mbili. **9)** Tashahudi ya mwisho. **10)** Kitako kwa ajili ya Tashahudi ya mwisho. **11)** Kumsalia Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, katika Tashahudi ya mwisho. **12)** Salamu ya kwanza. **13)** Utulivu katika nguzo za vitendo. **14)** Kuzipangilia nguzo hizi.

Bila ya nguzo hizi, sala haiwi sahihi, na rakaa inakuwa batili kwa kuacha nguzo mojawapo; sawa iwe ni kwa makusudi au kwa kusahau.

**WAJIBU WA SALA:** Ni mambo manane: **1)** Takbira zote, isipokuwa tu Takbira ya kuanzia sala. **2)** Kusema "***Samiallahu Liman-hamidah***" kwa Imamu na mtu anayesali peke yake. **3)**Kusema "***Rabbanaa walakal hamdu***" katika kunyanyuka kutoka kurukuu. **4)** Kusema "***Sub-haana Rabbiyal-'adhiim***" katika kurukuu, mara moja. **5)** Kusema "***Sub-haana Rabbiyal-a'alaa***" mara moja katika kusujudu.**6)** Kusema "***Rabbighfir-lii***" kati ya mara mbili za kusujudu. **7)** Tashahudi ya kwanza. **8)** Kukaa kwa ajili ya hiyo Tashahudi ya kwanza. Mtu akiyaacha kwa makusudi masuala haya ya wajibu, sala yake itabatilika, na akiyaacha kwa kusahau atasujudu kwa ajili ya kusahau.

---

[1] Uchi: Ni utupu wa mwanadamu na ambao anaona aibu kuonwa. Uchi wa mwanaume aliyefikia umri wa miaka saba ni zile tupu mbili tu. Aliyefikia miaka kumi ni sehemu iliopo kati ya kitovu na goti. Mwanamke muungwana na aliye balehe, mwili wake wote ni uchi, isipokuwa tu uso wake. Ni makuruhu kuufinika uso wake huo katika sala, isipokuwa tu wakiwepo wanaume kando, hapo inakuwa wajibu kuufinika. Iwapo mwanamke atasali au atatufu na ilhali kuna sehemu ya mwili wake iko wazi kama mguu wake kwa mfano, ibada yake ni batili; sio sahihi. Uchi Mzito (Utupu wa mbele na wa nyuma) ni wajibu kuufinika hata nje ya sala, na ni makuruhu kuufunua bila ya dharura, hata kama ni gizani au faragha.

Mambo haya ya wajibu wa sala kama mtu akiyaacha kwa makusudi, sala yake itabatilika. Kama mtu akiyaacha kwa kusahau, atasujudu kwa ajili ya kusahau.

**SUNA ZA SALA:** Kuna suna za kauli na za vitendo. Sala haibatiliki kwa kuacha jambo katika suna hizo, hata kama kuacha huko ni kwa makusudi.

**SUNA ZA KAULI:** **Ni kusoma** dua ya kuanzia sala **– Kusema** "***Auudhu Billahi Minash-shaitaanir-rajiim***" **– Kusema** "***Bismillahir-rahmanir-rahiim***" **– Kusema** *"Aamiin"* – **Kuisema** *"Aamiin"* kwa sauti ya kusikika katika sala ya kusoma kwa sauti ya kusikika – **Kusoma** sehemu chache ya Qur'ani baada ya *Suratul-Faatihah* **– Kusoma** Qur'ani kwa sauti ya kusikika kwa Imamu (Maamuma anakatazwa kusoma kwa sauti ya kusikika, na ayesali peke yake ana hiyari. **Kusema** "***Hamdan Kathiiran Twayyiban Mubaarakan Fiih Mil-assamaawaati Wamil-al-ardhi…***" baada ya kusema "***Rabbanaa walakalhamdu***" **– Kuzidisha zaidi** ya mara moja Tasbihi za kurukuu na kusujudu na kuzidisha kusema "***Rabbighfirlii***" – **Kuleta** dua kabla ya kutoa Salaam. **SUNA ZA VITENDO: Ni kunyanyua mikono** wakati wa kuletaTakbira ya kuanzia sala, wakati wa kurukuu, wakati wa kunyanyuka kutoka katika kurukuu na wakati wa kunyanyuka kutoka katika kikao cha Tashahudi ya kwanza **– Kuweka mkono** wa kulia juu ya wa kushoto chini ya kifua wakati wa kusimama **– Kuangalia mahali** pake pa kusujudu **– Kutenganisha** miguu yake wakati mtu amesimama **– Kuanza kuweka magoti yake** halafu mikono yake halafu paji la uso na pua yake katika kusujudu kwake **– Kuepusha** kwapa zake zisiguse mbavu zake na tumbo lake lisiguse mapaja yake na mapaja yake yasiguse miguu yake **– Kutenganisha magoti** yake **– Kusimamisha miguu** yake ikiwa imetenganishwa na kufanya matumbo ya vidole vyake yaguse ardhi **– Kuweka mikono yake** mkabala na mabega yake ikiwa imekunjuliwa na vidole vikiwa vimekutanishwa **– Kusimama kwa kuegemea** vifua vya nyayo za miguu yake na kuegemea magoti yake kwa kutumia mikono yake **– Kukaa Iftirashi** katika kitako kati ya sijida mbili na katika Tashahudi ya Kwanza **– Kukaa Tawaruki** katika Tashahudi ya Pili **– Kuweka mikono** juu ya mapaja ikiwa imekunjuliwa viganja na vidole vikiwa vimekutanishwa katika sijida mbili na pia katika Tashahudi; isipokuwa tu katika mkono wa kulia atakunja kidole kidole na kinachofuatia pamoja na kidole gumba na cha kati na ataashiria kwa kidole cha shahada wakati wa kumtaja Mwenyezi Mungu na kumuomba, ikiwa ni ishara ya kuonesha upekee wa Mwenyezi Mungu **– Kugeuka kulia na kushoto** wakati wa kutoa kwake Salaam **– Kuanza upande wa kulia** wakati wa kugeuka.

**KUSUJUDU KWA KUSAHAU: Ni suna** Kusujudu kwa Kusahau ikiwa mtu atafanya, kwa kusahau, jambo la sheria katika mahali pasipokuwa pake; kama kusoma Qur'ani katika kusujudu. Inafaa Kusujudu kwa Kusahau ikiwa mtu ataacha jambo la suna. **Ni wajibu** Kusujudu kwa Kusahau ikiwa mtu atazidisha kurukuu, kusujudu, kusimama au akitoa salamu kabla ya sala kukamilika au akifanya kosa la usomaji linalopotosha maana au akiacha wajibu au akitilia mashaka ziada wakati wa kuifanya ziada hiyo. Sala itabatilika kwa kuacha kwa makusudi Kusujudu kwa Kusahau ambako ni wajibu. Mtu akitaka anaweza kusujudu sijida mbili za kusahau

kabla ya kutoa salamu au baada yake. Mtu akisahau kusujudu mpaka kipindi kikawa kirefu, kusujudu huko kutafutika.

**NAMNA YA KUSALI:** Mtu atakaposimama kwa ajili ya kuswali, ataelekea Kiblah na kusema: ***Allahu Akbar***. Imamu ataisema Takbira hiyo na Takbira nyinginezo kwa sauti ya juu ili awasikilizishe walioko nyuma yake waisikie. Asiyekuwa imamu, ataisema Takbira hiyo kwa sauti ya chini. Atanyanyua mikono yake wakati wa kuanza kuleta Takbira mpaka mkabala wa mabega yake. Halafu atashika, kwa mkono wake wa kulia, kiganja cha mkono wake wa kushoto na kuiweka mikono hiyo chini ya kifua chake, na macho yake yakiangalia mahali pake pa kusujudu. Halafu ataanza kwa kusoma baadhi ya nyiradi zilizothibiti katika Sunna, mfano: ***Sub-haanakal-laahumma wabihamdik. Tabaarakasmuk, wataalaa jad-duk, walaa ilaaha ghairuk*** = Umetakasika ewe Mola wangu na umesifika. Limetukuka jina lako, na umekuwa juu utukufu wako, na hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa wewe tu. Halafu atasoma *Istiadha* "***Auudhu Bil-laahi Minash-shaitwaanir-rajiim*** = Naomba kinga kwa Mwenyezi Mungu anilinde na shetani aliye mbali na rehema". Halafu atasoma *Basmalah* "***Bismil-laahir-rahmaanir-rahiim*** = Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu". (atasoma yote hayo yaliyopita kimoyomoyo bila kutoa sauti). Halafu atasoma *Suratul-Faatiha*. Inapendekezwa kwa maamuma kuisoma *Suratul-Faatiha* katika: **1)** Nyakati za kunyamaza kwa Imamu, na. **2)** Katika sala ambazo Imamu hasomi kwa sauti ya juu.

Ni wajibu kusomwa *Suratul-Faatiha* katika sala za kusoma kimya kimya.

Halafu atasoma sehemu chache ya Qur'ani. Inapendekezwa katika sala ya Alfajiri asome katika Sura Ndefu *(Twiwaal Mufassal),* na katika sala ya Magharibi asome katika Sura fupi *(Qisaar Mufassal),* na katika sala nyinginezo asome katika Sura za Kati. Sura Ndefu ni kuanzia Surat Qaaf (50) mpaka *Suratin Naba-i* (78). Sura za Kati ni kuanzia *Suratin Naba-i* (78) mpaka *Suratu-Dhuhaa* (93). Sura Fupi ni kuanzia *Suratu-Dhuhaa* (93) mpaka *Suratun-Naas* (114). Imamu atasoma kwa sauti ya juu katika sala ya Alfajiri na katika rakaa mbili za mwanzo katika sala ya Magharibi na sala ya Isha. Atasoma kwa sauti ya chini katika sala na rakaa zisizokuwa hizo.

Halafu ataleta *Takbira,* atarukuu, atanyanyua mikono yake kama alivyonyanyua wakati wa Takbira ya kuanzia sala. Ataweka mikono yake juu ya magoti yake na kuvitawanya vidole vyake. Ataunyoosha mgongo wake na kukiweka kichwa chake usawa wa mgongo wake. Halafu atasema: ***Sub-haana Rab-biyal-adhiim*** mara tatu. Halafu atanyanyua kichwa chake huku akisema: ***Samiallaahu Liman-hamidah***, na atanyanyua mikono yake kama alivyonyanyua wakati wa Takbira ya kufunga sala. Akishasimama sawasawa, atasema: ***Rabbanaa Walakal-hamdu. Hamdan Kathiiran Twayyiban Mubaarakan Fiih Mil-assamaawaati Wamil-al-ardhi Wamil-a Maashi-ita Min-shai-in Baadu***. Halafu atainama kwenda kusujudu huku akileta Takbira. Mikono yake ataitenganisha isiguse mbavu zake, na pia tumbo lake lisiguse mapaja yake. Ataiweka mikono yake mkabala na mabega yake. Atakuwa amesimama juu ya kingo za nyayo za miguu yake, huku akivielekeza vidole vya miguu na mikono yake upande wa Kiblah. Halafu atasema: ***Sub-haana Rabbiyal-aalaa*** mara tatu. Anaweza kuongeza baadhi ya nyiradi zilizothibiti au kuomba dua

atakayo. Halafu atanyanyua kichwa chake huku akileta Takbira. Atautandaza mguu wake wa kushoto na kuukalia. Atausimamisha unyayo wa mguu wa kulia na kuvikunja vidole vyake kuvielekeza upande wa Kiblah. Au atazisimamisha nyayo zote za miguu yake na vidole vyake kuvielekeza Kiblah na kukalia visigino vyake. Atasema: ***Rab-bighfir-lii*** mara tatu. Anaweza kuongeza: ***War-hamnii, Waj-burnii, War-faanii, War-zuqnii, Wansurnii, Wahdinii, Wa-aafinii, Wa-fu an-nii***. Halafu atasujudu mara ya pili kama alivyosujudu mara ya kwanza. Halafu atanyanyua kichwa chake huku akileta Takbira. Atanyanyuka akisimamia vifua vya nyayo za miguu yake. Atasali Rakaa ya pili kama alivyosali Rakaa ya kwanza.

Akimaliza kusali Rakaa mbili hizo, atakaa kwa ajili ya *Tashahudi* huku akiwa ameitandaza miguu yake. Ataweka mkono wake wa kushoto juu ya paja lake la kushoto, na mkono wake wa kulia atauweka juu ya paja lake la kulia. Katika mkono huo wa kulia, atakunja kidole kidogo cha mwisho na kinachofuatia pia **kidole gumba na cha kati na kutoa ishara kwa kidole cha shahada akisema:** ***At-tahiy-yaatu Lillaah. Was-swalawaat Wat-tway-yibaat. Assalaamu alaika Ay-yuhan-nabiy-yu Warahmatu-llaahi Wabarakaatuh. Assalaamu alainaa Wa-alaa Ibaadil-laahis-swaalihiin. Ash-hadu Al-laa ilaaha il-lallaah. Wa-ash-hadu An-na Muhammadan Ab-duhuu Warasuuluh.***

Halafu atanyanyuka katika sala yenye rakaa tatu na yenye rakaa nne akileta Takbira na kunyanyua mikono yake. Atasali rakaa zilizobaki kama hivyo isipokuwa tu hatasoma kwa sauti ya juu, na atasoma *Suratul-Faatihah* tu.

Halafu atakaa kwa ajili ya *Tashahudi* ya mwisho akiwa amekaa kikao cha *Tawarruk*; atautandaza mguu wake wa kushoto na kuutoa upande wake wa kulia. Atausimamisha unyayo wa mguu wa kulia na tako lake juu ya ardhi. Kukaa Tawarruk katika kikao cha mwisho ni kwa sala ambayo ina *Tashahudi* mbili.

**Halafu atasoma *Tashahudi* ya Kwanza, na halafu atasema:** ***Allaahumma swal-li alaa Muhammad Wa-alaa aali Muhammad Kamaa Swal-laita alaa Ibraahiim Wa-alaa Aali Ibraahiim, in-naka Hamiidun Majiid. Allaahumma baarik Alaa Muhammad Wa-alaa aali Muhammad Kamaa baarakta Alaa Ibraahiim Wa-alaa aali Ibraahiim in-naka Hamiidun Majiid.***

**Ni suna kusema:** ***Auudhu Bil-laahi Min Adhaabin-naar, Wamin adhaabil-qabri, Wamin-fitnatil-mahyaa Wal-mamaat, Wafit-natil-masiihid-dajjaal*** na dua nyinginezo zilizothibiti kunukuliwa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).

Halafu atatoa salamu mara mbili. Atazungusha kichwa upande wake wa kulia akisema: ***Assalaamu Alaykum Warahmatullaahi***. Halafu atafanya hivyo upande wa kushoto.

Baada ya salamu, ni suna kuleta dua zilizothibiti kunukuliwa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).[1]

---

[1] **Kusema:** ***Astaghafirullaahi*** mara tatu.
*Allaahumma antas-salaamu,waminkas-salaamu,tabaarakta yaadhaljalaali wal-ikraami.laailaaha il-lallaahu wahdahuu laashariika lahu,lahul-mulku walahul-hamdu wahuwa alaakul-li shay in qadiiru. Laahaula walaa quwwata il-laa bil-laahi. Laa ilaaha il-lallaahu walaa naabudu il-laa iyyaahu,lahun-niimatu walahul-fadhlu walahuth-thanaaul-hasan.Laa ilaaha il-lallaahu mukhliswiina lahuddiina walau karihalkaafiruuna. Allaahumma laamaania lima aatwayta, walaa*

**SALA YA MGONJWA:** Ikiwa kusimama kunamzidishia mgonjwa ugonjwa wake au hawezi kusimama, atasali akiwa amekaa. Akishindwa kukaa, atasali akiwa amelalia ubavu wake. Hilo likiwa zito kwake, atasali akiwa amelala chali. Akishindwa kurukuu na kusujudu, ataashiria tu. Ni wajibu kwake kulipa sala zilizompita. Ikimuwia uzito kutekeleza kila sala katika wakati wake, anaweza kukusanya kati ya sala za Adhuhuri na Alasiri na kati ya Magharibi na Isha katika wakati wa sala mojawapo.

**SALA YA MSAFIRI:** Ikiwa umbali wa safari ya mtu takriban ni zaidi ya kilomita thamanini (80km) na safari yake ikawa ni ya halali, anaweza kuipunguza sala yenye rakaa nne na kuwa ya rakaa mbili. Msafiri, wakati wa safari yake, akinuia kukaa katika mahali zaidi ya siku nne (sala 20 za faradhi), atasali sala kamili tangu kufika kwake na hatapunguza. Msafiri akimfuata (akiwa maamuma nyuma ya) mkazi au akisahau sala ya uenyejini akaikumbuka akiwa safarini au akiisahau sala ya safarini akaikumbuka akiwa uenyejini, ni wajibu kwake kuisali kamili sala hiyo katika hali zote hizo zilizotangulia. Msafiri anaweza kusali kamili, na kupunguza ni bora zaidi.

**SALA YA IJUMAA:** Sala ya Ijumaa ni bora zaidi kuliko ya Adhuhuri. Hii ni sala inayojitegemea na sio Adhuhuri iliyopunguzwa. Haifai kuisali rakaa nne, na haifungamani (haisihi) kuisali kwa nia ya Adhuhuri. Haifai kuijumuisha pamoja na Alasiri kwa hali yoyote, hata kama itakuwepo sababu ya kujumuisha.

**WITRI:** Witri ni suna. Wakati wake ni kuanzia sala ya Isha mpaka kuchimbuka kwa alfajiri. Uchache wake ni rakaa moja, na wingi wake ni rakaa kumi na moja; akitoa salamu kila baada ya rakaa mbili, na kufanya hivyo ni bora zaidi. Au anaweza kusali rakaa nne au sita au nane kwa pamoja. Halafu atawitirisha kwa rakaa moja baada ya kila rakaa mbili mbili. Au atasali rakaa tatu au tano au saba au tisa kwa pamoja. Ukamilifu wa chini zaidi ni rakaa tatu kwa salamu mbili. Inafaa baada ya witri kusali rakaa mbili huku mtu akiwa amekaa.

**JENEZA:** Kumuosha maiti Mwislamu, kumvalisha sanda, kumsalia, kumbeba na kumzika ni Faradhi ya Kutoshelezana, isipokuwa Shahidi wa vitani. Yeye haoshwi na havalishwi sanda. Inafaa kumswalia. Anazikwa akiwa katika hali yake aliyokufa nayo. Maiti mwanaume huvalishwa sanda ya mapande matatu ya nguo yaliyo

---

*muutwiya lima manaata,walaa yanfau dhaljaddi minkal jaddu*. **Baada ya sala ya Alfajiri na Magharibi atasema, pamoja na hayo yaliyotangulia**.

**Baada ya sala ya Alfajiri na Magharibi atasema, pamoja na hayo yaliyotangulia,:** *Laailaaha il-lallaahu wahdahuu laa shariika lahu lahul-mulku walahul hamdu yuhyii wayumiitu wahuwa alaa kul-li shay in qadiiru*. (mara kumi).

Halafu baada ya hayo atasema: ***Subhaana llaahu*** (mara 33), ***Alhamdulillahi*** (mara 33), ***Allaahu akbaru*** (mara 33) na atasema katika kukamilisha mara mia moja: *Laailaaha il-lallaahu wahdahuu laa shariika lahu lahul-mulku walahul hamdu yuhyii wayumiitu wahuwa alaa kul-li shay in qadiiru*. **Halafu atasoma Aya Kursiy:** *Allahu laailaaha i-laahuwal hayyulqayyuum. Laataakhudhuhu sinatun walaa nauum. Lahuu mafias-maawati wamaafil-ardhi,mandhal-ladhii indahu i-laa biidhinihi, Yaalamu maabaina aidiihim wamaa khalfaham,walaa yuhiitwuuna bishai in min ilmihii il-laa bimaa shaa-a, wasia kur-siyyuhus-samaawati wal-ardhwa,walaa yauuduhu hifdhuhumaa wahuwal-aliyyul-adhwiim.* (Aya ya 255 katika sura Albaqara 2). Halafu atasoma: **Sura Al-ikhlas, Alfalaq na Annas** Atarudia kuzisoma sura hizi mara tatu baada ya sala ya Alfajiri na Magharibi.

meupe, na mwanamke nguo tano nyeupe; shuka, ushungi, gauni na mapande mawili ya kuzungushia. **Ni suna** (wakati wa kumsalia maiti) kwa Imamu na anayeswalia peke yake kusimama mkabala wa kifua cha mwanaume na makabala wa sehemu ya kati ya mwanamke. Ataleta Takbira nne akinyanyua mikono yake pamoja na kila Takbira. Ataanza sala kwa Takbira ya kwanza, ataomba kinga (Istiadha), ataleta Basmala (Bismillahi) na kusoma Sura Alfaatiha tu kimya kimya. Ataleta Takbira ya pili na kumsalia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Halafu ataleta Takbira ya tatu na kumuombea dua maiti. Halafu ataleta Takbira ya nne na kunyamaza kidogo. Halafu atatoa salamu moja upande wa kuliani kwake. **Ni haramu** kulinyanyua kaburi zaidi ya shubiri, kulipaka rangi, kulibusu, kulifukiza ubani, kuliandika, kulikalia au kutembea juu yake. **Ni haramu** kuyawekea taa makaburi, kutufu (kuzunguka) kando kando yake, kujenga msikiti makaburini au kuzika msikitini. **Ni wajibu** kuvunja makuba yalioko makaburini.

- Katika matamshi ya *Taazia* (kutoa pole) hakuna marufuku. Miongoni mwa matamshi hayo ni mtoa pole kusema: "Aadhwamallaahu ajraka,wa ahsana azaa-aka,waghafara limayyitika."Mwenyezi Mungu ayafanye makubwa malipo yako, ayafanye mazuri majonzi yako na ampe msamaha maiti wako. Katika kumpa pole Mwislamu kwa kufiwa na kafiri, atasema: "Aadhwamallaahu ajraka wa ahsana azaa-aka" Mwenyezi Mungu ayafanye makubwa malipo yako, ayafanye mazuri majonzi yako. Ni haramu kumpa *Tazia* kafiri japo kwa kufiwa na Mwislamu.
- Ni wajibu kwa anayejua kuwa iwapo atakufa watu wake watalia kwa mayoe kuwausia kuacha. Vinginevyo, ataadhibiwa kwa kilio chao.
- Imam Shaafii, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: “Ni makuruhu kukaa kwa ajili ya Tazia, na hiyo ni kukusanyika kwa wenye maiti katika nyumba ili wanaotaka kuwafariji wawafuate. Inatakiwa waondoke kwenda kwenye shughuli zao; sawa wawe ni wanaume au wanawake”.
- Ni suna kuwapikia chakula wenye maiti. Ni makuruhu kula chakula chao au kuwapikia chakula wanaokusanyika kwa wenye msiba.
- Ni suna kuzuru kaburi la Mwislamu bila ya kusafiri. Inafaa kuzuru kaburi la kafiri. Kafiri hazuiwi kuzuru kaburi la Mwislamu.
- Ni suna kwa anayefika makaburini kusema: "Assalamu alaykum daara qaumin muuminiina, ahlad-diyaaariminal muuminiina,wainnaa inshaallaahu bikum lalaahiquun, yarhamullaahul-mustaqdimiina minnaa walmustaakhiriina,,nas-alullaha lanaa walakumul-aafiyata.allaahumma laa tahrimnaa ajrahum,walaa taftinnaa baadahum,waghfir lanaa walahum"
- Ni haramu kuandika Qur'ani katika sanda, kwa: Kuchelea kuitia najisi, kwa kuwa jambo hilo ni kuidhalilisha na pia jambo hilo halikuthibiti.
- Dua bora ya kumuombea maiti. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema katika kumuombea Mungu maiti: "Allaahumma ighfir lahuu warhamhuuu,waafihii,waafu anhuu,wa-akrim nuzulahuu,wawas-sii mudkhalahuu, waghsil hu bil-maai wath-thalji walbaradi,wanaqqihii minalkhatwaayaa kamaa naqqaytath-thaubal-abyadhwa

minaddanasi,wa-abdilhu daaran khairan min daarihi,wa ahlan khayran min ahlihii,wazaujan khayran min zaujihi,wa adkhilhuljannata,wa aidh-hu min adhaabilqabri wamin adhaabin-naari." Amaeipokea Hadithi hii Muslim

**SALA YA IDI:** Sala ya Idi ni *Faradhi* ya Kutosheleza. Wakati wake ni wakati wa sala ya Dhuha. Idi ikifahamika baada ya jua kupinduka katika usawa wa anga, patasaliwa kesho yake, ikiwa ni kulipa. Masharti yake ni kama ya sala ya Ijumaa isipokuwa hotuba mbili. Ni makuruhu kusali suna kabla yake na baada yake katika mahali pa kusalia. **Namna yake** ni rakaa mbili. Ataleta Takbira sita katika rakaa ya kwanza baada ya Takbira ya kuanzia sala na kabla ya kuomba kinga. Katika rakaa ya pili, kabla ya kusoma, ataleta Takbira tano huku akinyanyua mikono yake pamoja na kila Takbira.. Halafu ataomba kinga na kisha sura Alfatiha kwa sauti ya kusikika. Atasoma sura Al-aalaa (87) katika rakaa ya kwanza, na sura Al-ghaashiya (88) katika rakaa ya pili. Akishatoa salamu, atahutubu hotuba mbili kama hotuba za sala ya Ijumaa, lakini inasuniwa katika hotuba za sala ya Idi kuleta Takbira kwa wingi. Mtu akisali sala ya Idi kama sala ya suna ni sahihi, kwa sababu Takbira za ziada na nyiradi baina yake ni suna.

**SALA YA KUPATWA KWA JUA/MWEZI** Sala ya kupatwa kwa jua/mwezi ni suna. Wakati wake ni kuanzia kupatwa kwa jua/mwezi mpaka kutanzuka kwake. Sala hii hailipwi, ikiwa sababu yake imeondoka. Sala hii ni rakaa mbili. Katika rakaa ya kwanza, atasoma sura Alfatiha na sura nyingine ndefu kwa sauti ya kusikika. Halafu atarukuu kurukuu kurefu. Halafu atasimama na kusema "samiallahu liman hamida"na "Rabbanaa walakalhamdu"na hatasujudu, bali atasoma sura Alfatiha na sura nyingine ndefu. Halafu atarukuu kurukuu kurefu. Halafu atanyanyuka. Kisha atasujudu sijida mbili ndefu. Halafu atasali rakaa ya pili kama rakaa ya kwanza. Halafu atasoma Tashahudi na kutoa salamu. Akija maamuma baada ya rukuu ya mwanzo, hakuipata rakaa.

**SALA YA KUOMBA MVUA** Sala ya kuomba mvua inakuwa suna pale ardhi inapokuwa kame na mvua zikawa haba. Wakati, namna na sheria zake ni kama sala ya Idi, isipokuwa tu imamu atawahutubia waumini hotuba moja baada ya sala. Ni suna kuigeuza nguo ya kujitanda mwishoni mwake ikiwa ni matarajio mema ya hali kubadilika.

**ZALA ZA SUNA:** Imethibiti kwamba Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa akisali, sio faradhi, rakaa kumi na mbili kila siku. Hizo ni: rakaa mbili kabla ya sala ya Alfajiri, rakaa nne kabla ya sala ya Adhuhuri, rakaa mbili baada ya sala ya Adhuhuri, rakaa mbili baada ya sala ya Magharibi na rakaa mbili baada ya sala ya Isha. Zimepokewa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) sala nyingine za suna zisizokuwa hizo.

**Nyakati zilizokatazwa kusali:** Ni haramu kusali suna baadhi ya sala ya suna katika nyakati ambazo

✸ Sala ya Jamaa ni wajibu kwa wanaume, hata safarini ikiwezekana. Anatiwa adabu na kuadhiriwa mwenye kuiacha au kuyamethibiti makatazo ya kusali suna katika nyakati hizo. Nyakati hizo ni hizi: 1)Tangu kutokea kwa alfajiri mpaka kuchomoza kwa jua, mpaka jua lipande kiasi cha mkuki. 2)Wakati wa jua kuwa katikati ya mbigu mpaka limili. 3)Baada ya sala ya Alasiri mpaka kuzama kwa jua.

**Ama sala zenye sababu:** Inasihi kuzisali katika nyakati hizi, kama sala ya kuingia msikitini, rakaa mbil za kutufu alkaaba, rakaa mbili za suns ya Alfajiri, sala ya Jeneza, rakaa mbili za Udhu, sijida ya kusoma na sijida ya kushukuru.

✸ **SHERIA ZA MISIKITI:**Ujenzi wa misikiti ni wajibu kwa kiasi cha mahitaji. Misikiti ni maeneo yanayopendwa sana na Mwenyezi Mungu, na ni haramu kuimba, kupiga makofi, kupig nzumari (firimbi), kuimba mashairi ya haramu, mchanganyiko wa wanaume na wanawake, mume na mke kujamiiana na kufanya biashara (na ni suna kumwambia anayefanya biashara msikitini: *"Mwenyezi Mungu asiipe faida biashara yako"*. Pia ni haramu kutangaza kitu kilichopoptea, na ni suna kumwambia anayetangaza kitu kilichopotea: *"Mwenyezi Mungu asikirudishe kwako kitu hicho"*. Inaruhusiwa kuwafundisha watoto wadogo wasiokuwa na madhara, kufungisha ndoa, kuamua ugonvi, kuimba mashairi halali, kulala kwa aliyeko katika Itikafu na asiyekuwa katika Itikafu, kulala mgeni na mgonjwa, kujipumzisha. Ni suna kuilinda misikiti isiwe na zogo, uhasama, maongezi mengi, kupaza sauti kwa jambo lisilopendeza na kufanya njia bila ya dharura. Ni jambo lisilopendeza kuzungumza mazungumzo mengi ya kidunia, kutumia mazulia yake au taa zake au umeme wake kwa ajili ya harusi na msiba.

# ZAKA

**AINA ZA ZAKA** Inakuwa wajibu kutoa zaka katika aina nne (za mali): Aina ya kwanza ni wanyama wanaofugwa (wanyama hoa). Aina ya pili ni mali itokayo ardhini (madini). Aina ya tatu ni thamani. Aina ya nne ni bidhaa za biashara.

**MASHARTI YA KUWAJIBIKA** Zaka haiwi wajibu isipokuwa tu kwa kuwepo masharti matano: Sharti la kwanza ni Uislamu. Sharti la pili ni Uhuru. Sharti la tatu ni kufikia kiwango. Sharti la nne ni umiliki kamili. Sharti la tano ni kutimia mwaka, isipokuwa kwa mali itokayo ardhini.

**ZAKA YA WANYAMA WAFUGWAO** Aina za wanyama hao ni tatu: Ngamia, n'gombe, mbuzi na kondoo.Ili iwe wajibu kutoa zaka katika wanyama hao, ni lazima yawepo masharti mawili: **1)** Wawe wamefugwa kiasi cha mwaka au zaidi. **2)** Wawe wamefugwa kwa ajili ya maziwa na ufugaji (kupata mifugo mingi) na sio kwa ajili ya kazi.

**ZAKA YA NGAMIA**

| Idadi | 1 - 4 | 5 - 9 | 10 - 14 | 15 - 19 | 20 - 24 | 25 - 35 | 36 - 45 | 46 - 60 | 61 - 75 | 76 - 90 | 91- 120 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zaka yake | Hakuna zaka | Shaat mmoja | Shaat wawili | Shaat watatu | Shaat wanne | Bintimakhadh | Bintilabun | Hiqqa | Jadh'a | Bintimakhadh 2 | Bintilabun 2 |

*Shaat* ni mbuzi au kondoo *Binti Makhaadh* ni yule ngamia aliyefikia umri wa mwaka mmoja. *Binti Labuun* ni yule aliyefikia umri wa miaka miwili. *Hiqqa* ni yule aliyefikia umri wa miaka mitatu. *Jidh-a* ni yule aliyefikia umri wa miaka mine. Ngamia wakizidi idadi ya 120, basi katika kila hamsini atatoa Hika, na katika kila arobaini atatoa Binti Labuun.

**ZAKA YA N'GOMBE** Zaka ya n'gombe ni:

| Idadi | 1-29 | 30-39 | 40-59 |
|---|---|---|---|
| Zaka yake | Hakuna zaka | *Tabii* jike au dume | *Musini* jike au dume |

*Tabii* jike au dume ni yule n'gombe aliyekamilisha mwaka mmoja. *Musini* jike au dume ni yule aliyekamilisha miaka miwili. N'gombe wanapofika 60 na zaidi, inawajibika katika kila thalathini kutoa Tabii na katika kila arobaini kutoa Musini.

**ZAKA YA MBUZI NA KONDOO** Zaka ya mbuzi/kondoo ni:

| Idadi | 1-39 | 40-120 | 121-200 | 201-399 |
|---|---|---|---|---|
| Zaka yake | Hakuna zaka | Shaat mmoja | Shaat wawili | Shaat watatu |

Wakifika 400 na zaidi, katika kila mia atatolewa mbuzi mmoja. Shaat akiwa ni wa kondoo ni yule aliyetimiza miezi sita, na huitwa Jadh-a. Akiwa ni wa mbuzi, ni yule aliyetimiza mwaka mmoja, na huitwa *Than-yi*.

Katika zaka ya mbuzi/kondoo, wafuatao hawatolewi zaka: Beberu la mbegu, mkongwe (mzee sana), mwenye ulemavu, anayelea mtoto wake, mwenye mimba na wenye thamani kubwa.

**ZAKA YA MALI ITOKAYO ARDHINI:** Inawajibika zaka katika mimea katika kila nafaka na matunda kwa masharti matatu: **1)** Mmea uwe katika aina zinazopimwa kwa pishi na kuwekwa akiba, kama shairi na ngano katika nafaka, na kama tende na zabibu katika matunda. Ama mimea isiyopimika na isiyowekeka

akiba kama mboga mboga na mfano wake, haina zaka. **2)** Kufikia kiwango. Kiwango ni kilogramu 653 na zaidi. **3)** Mmea uwe unamilikiwa na mtoaji wakati wa kuwajibika kwa zaka. Ikiwa ni matunda, yawe yamekuwa mekundu au manjano. Ikiwa ni nafaka, ziwe zimekomaa na kukauka. Inawajibika kutoa asilimia kumi **(10%)** katika mimea iliyomwagiliwa maji bila ya tabu yoyote, kama ile inayomwagiliwa maji kwa mvua na mito. Inawajibika kutoa nusu ya asilimia kumi **(5%)** kwa mimea iliyomwagiliwa maji kwa gharama na usumbufu, kama maji yaliyotolewa katika visima na mfano wake. Ama mimea iliyomwagiliwa kwa usumbufu katika baadhi ya siku za mwaka na bila ya usumbufu katika baadhi ya siku za mwaka huo, itazingatiwa wingi wa siku. Hesabu itazingatia idadi ya siku za usumbufu na zisizokuwa za usumbufu.

**ZAKA YA THAMANI: Thamani** ni aina mbili: **1) Dhahabu,** na hakuna zaka katika dhahabu mpaka ifike gramu (85). **2) Fedha**, na hakuna zaka katika fedha mpaka ifike gramu (595). Hakuna zaka katika sarafu na fedha za karatasi mpaka thamani yake wakati wa kutoa zaka ifike kiwango cha chini cha dhahabu na fedha. Kiwango cha zaka ya thamani ni robo ya asilimia kumi **(2.5%)**. Hakuna zaka katika mapambo halali yaliyotayarishwa kwa ajili ya matumizi. Ama mapambo yaliyotayarishwa kwa ajili ya kukodisha au kuweka akiba, inawajibika zaka. Ni halali kwa wanawake kuvaa dhahabu na fedha katika kiwango ambacho kwa kawaida imezoeleka kuvaa. Pia ni halali kuweka fedha kidogo katika vyombo. Inafaa kwa wanaume kuvaa fedha kidogo ikiwa peke yake, kama pete, miwani na mfano wake. Ama dhahabu ni haramu kuweka hata kidogo katika vyombo. Inafaa kwa wanaume kutumia dhahabu kidogo ikiwa inategemea kitu kingine bila ya kujifananisha na wanawake, kama kifungo katika nguo na mshipi wa kufungia jino.

Mtu ambaye ana mali inayo ongezeka na kupungua na ikawa uzito kwake kutoa zaka ya kila mali katika mwaka wake, atatoa zaka katika siku atakayoipanga katika mwaka. Katika siku hiyo, ataangalia ni kiasi gani anamiliki na atatoa **(2½%)**, hata kama baadhi ya mali zake hazijafikia mwaka. Mtu ambaye ana mshahara au ana kitu anachokodisha kama nyumba na ardhi, ikiwa haweki akiba katika hayo hakuna zaka, hata kama ni nyingi. Ikiwa anaweka akiba, atatoa zaka katika akiba hiyo ikipitiwa na mwaka. Ikiwa itamuwia uzito, atajiwekea siku katika mwaka ya kutoa zaka, kama ilivyotangulia kuelezwa.

**ZAKA YA DENI:** Mtu ambaye ana deni analolidai kwa mtu mwenye uwezo au anayo mali anayoweza kuichukua, ni wajibu kwake kuitolea zaka atakapoipata kwa miaka iliyopita hata kama ni mingi. Ikiwa ni vigumu kulipata deni hilo, kama deni liliopo kwa mtu aliyefilisika, halina zaka kwa sababu mali hiyo haiwezekani kutumiwa.

**ZAKA YA BIDHAA ZA BIASHARA:** Hakuna zaka katika bidhaa za biashara isipokuwa tu kwa masharti manne: **1)** Mtu kuwa anazimiliki. **2)** Anuwie biashara kwa bidhaa hizo. **3)** Thamani yake ifikie kiwango. Kiwango chake ni kile kiwango cha chini cha dhahabu na fedha. **4)** Kutimia kwa mwaka. Masharti haya yakipatikana, atatoa zaka katika thamani yake. Ikiwa mtu atakuwa na dhahabu au fedha au sarafu, ataijumuisha kwenye bidhaa za biashara ili kukamilisha kiwango. Mtu atakaponuia

kutumia katika bidhaa za biashara kama nguo, nyumba, gari na mfano wake, hakuna zaka. Halafu ikiwa atanuia biashara kwa bidhaa hizo baada ya hapo, atazianzia mwaka (kwa maana ya kuwa atazitolea zaka na atahisabu mwaka kuanzia wakati huo aliponuia kufanya biashara)[1]. Kiwango cha bidhaa za biashara ni sawa na thamani ya kiwango cha dhahabu gramu 85 au thamani ya kiwango cha fedha gramu 595. Anaweza kutoa kiwango cha chini kati ya viwango hivyo wakati wa kutoa zaka.

**ZAKATUL-FITRI:** Ni wajibu kwa kila Mwislamu atakapomiliki mali ya ziada ya chakula chake na chakula cha familia yake siku ya Idi. Kiwango chake ni kilogramu mbili na robo **(2¼)** ya chakula kinachotumika katika mji, kwa kumtolea mtu mmoja; sawa awe ni mwanaume au mwanamke. Mtu ambaye analazimika kujitolea Zakatul-fitri, analazimika kumtolea kila ambaye analazimika kumhudumia siku ya Idi, iwapo atamiliki cha kulitekeleza hilo. Inapendekezwa kutoa Zakatul-fitri siku ya Idi kabla ya kusali. Haifai kuiahirisha baada ya sala ya Idi. Inafaa kutanguliza kuitoa kabla ya siku ya Idi kwa siku moja au mbili. Inafaa kumpa mtu mmoja Zakatul-fitri ya wengi na pia inafaa kuwapa wengi Zakatul-fitri ya mtu mmoja.

**KUTOA ZAKA:** Ni wajibu kutoa zaka haraka. Walii (mlezi) analazimika kumtolea zaka mtoto mdogo na mwendawazimu. Ni suna kuitangaza na mtoaji kuigawa yeye mwenyewe. Kwa mtu balehe, inashartiwa nia katika kutoa zaka. Haitatosha mtu kunuia sadaka ya kawaida, hata kama atatoa sadaka mali yake yote. Jambo bora zaidi ni kuwapa zaka ya mali yake fukara wa mjini mwake. Inafaa kuihamisha zaka na kuipeleka mji mwingine kwa masilahi. Inafaa na ni sahihi kuiharakisha zaka kwa miaka miwili, ikiwa kiwango kimekamilika

**WANAOPEWA ZAKA:** Ni aina nane: **1)** Fukara. **2)** Masikini. **3)** Watumishi wa zaka **4)** Wanaolainishwa nyoyo zao. **5)** Watumwa. **6)** Wenye madeni. **7)** Katika njia ya Mwenyezi Mungu. **8)** Msafiri. Wote watapewa zaka kwa kiasi cha shida, isipokuwa mtumishi wa zaka. Yeye atapewa kwa kiasi cha ujira wake, hata kama ni tajiri. Inatosha kuwapa zaka Khawaarij (waasi) na wavamizi, ikiwa watatawala mji wake. Inatosha zaka ikiwa mtawala ataichukua kwa nguvu au kwa hiari; sawa mtawala huyo amefanya uadilifu katika zaka hiyo au hakufanya uadilifu. Haitoshi kumpa zaka kafiri, mtumwa, tajiri, mtu ambaye zinamlazimu mtoa zaka huduma zake, watoto wa Hashim (familia ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)). Mtu akitoa zaka kuwapa wasiostahiki na ilhali hajui, halafu akajua, haitatosha. Lakini mtu akitoa zaka kumpa mtu anayemdhania kuwa fukara na ikabainika kuwa ni tajiri, zaka hiyo itatosha.

**SADAKA YA HIYARI:** Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Kwa yakini, miongoni mwa yatakayomfuata muumini katika matendo yake na mazuri yake baada ya kufa kwake, ni elimu aliyoifundisha na kuisambaza na mtoto mwema aliyemuacha na msahafu aliourithisha au msikiti alioujenga au nyumba ya wasafiri aliyoijenga au mto alioupitisha au sadaka aliyoitoa katika mali yake katika uzima wake na uhai wake. (Yote hayo) Yatamfuata baada ya kufa kwake".*** Ibn-majah.

---

[1] Kiwango cha bidhaa ni = gramu 85 (kiwango cha dhahabu) au gramu 595 (kiwango cha fedha). Anaweza kutoa cha chini zaidi katika viwango hivyo wakati wa kutoa zaka.

# KUFUNGA SAUMU

Ni wajibu kufunga samu ya Ramadhani kwa kila Mwislamu, mwenye akili timamu, balehe, mwenye kuweza kufunga, asiye katika *Hedhi* na asiye katika *Nifasi (*damu ya uzazi). Mtoto anaamrishwa kufunga ikiwa ataweza ili aizoee saumu.

**Kuingia kwa Ramadhani kunajulikana kwa mojawapo ya mambo mawili:** **1)** Kuonekana kwa mwezi mwandamo, kwa ushahidi wa mtu mwadilifu, *mukallaf* (mtu anayetakiwa kutekeleza amri za kisheria), hata kama ni mwanamke. **2)**Kuukamilisha mwezi wa Shabani kwa siku thalathini. Wajibu wa kufunga unaanza tangu kuchimbuka kwa alfajiri ya kweli mpaka kuzama kwa jua. Ni lazima kuhudhurisha nia kabla ya alfajiri kwa saumu ya faradhi.

**YANAYOHARIBU SAUMU: 1)** Kujamiiana kupitia sehemu za siri. Inamuwajibikia mtu kulipa na kutoa kafara. Kafara ni kuacha huru mtumwa. Ambaye hakuweza (kuacha huru mtumwa), ni kufunga miezi miwili mfululizo. Ambaye hakuweza (kufunga miezi miwili), ni kuwapa chakula masikini sitini (60). Ambaye hakupata kitu, hana wajibu wowote. **2)** Kutoa manii kwa sababu ya kubusu au kugusa au kujitoa manii kwa mkono. Hakuna kitu kwa aliyeota. **3)** Kula na kunywa kwa makusudi. Ikiwa amesahau, saumu yake ni sahihi. **4)** Kutoa damu kwa kuumika (kupiga chuku) au kujitolea damu. Ama damu chache iliyotolewa kwa ajili ya kupima au iliyotoka bila ya utashi, kama jeraha na ugonjwa wa kutoka damu ya pua, haiharibu saumu. **5)** Kutapika kwa makusudi.

Vumbi likipeperuka na kuingia kooni mwake au mtu alisukutua au kupandisha maji puani na kwa hiyo maji yakafika kooni mwake au alifikiri na kwa hiyo akashusha manii au aliota na kushusha manii au alitapika bila ya hiari, haikuharibika saumu yake. Aliyekula akidhani kuwa ni usiku na ikabainika kuwa ni mchana, ni wajibu kwake kulipa. Aliyekula usiku akiwa na shaka ya kuchimbuka kwa alfajiri, haikuharibika saumu yake. Ikiwa amekula mchana akiwa na shaka ya kuzama kwa jua, ni wajibu kwake kulipa.

**HUKUMU ZA WANAORUHUSIWA KUTOFUNGA: Ni haramu** kutofunga katika Ramadhani kwa asiyekuwa na udhuru. **Ni wajibu** kutofunga kwa mwanamke aliye katika Hedhi na mwenye Nifasi na mtu ambaye anahitajika ili kuokoa kiumbe kilichohifadhika kisiangamie. **Ni suna** kutofunga kwa msafiri wakati wa mchana, mwanamke mwenye mimba na anayenyonyesha ikiwa watajihofia wao wenyewe au kuhofia mtoto. Ni wajibu kwao kulipa tu. Mwanamke mwenye mimba na anayenyonyesha wanaongeza kumpa chakula masikini kwa kila siku ikiwa watahofia mtoto tu. Aliyeshindwa kufunga kwa sababu ya uzee au ugonjwa usiotarajiwa kupona, atatoa chakula kumpa masikini kwa kila siku moja, na hana wajibu wa kulipa. Aliyecheleweshà kulipa kwa udhuru mpaka ikamkuta Ramadhani nyingine, hana wajibu isipokuwa wa kulipa tu. Ikiwa amefanya uzembe katika kulipa, atatoa chakula, pamoja na kulipa, kumpa masikini kwa kila siku moja. Akiacha kulipa kwa udhuru akafa, hana wajibu wowote. Ikiwa aliacha kulipa bila ya udhuru, atatolewa chakula na kupewa masikini kwa kila siku moja. Ni suna kwa ndugu yake kumfungia saumu ya kulipa aliyoifanyia uzembe, saumu yake ya Nadhiri na kulipia kila Nadhiri ya ibada.

Aliyeacha kufunga kwa udhuru halafu udhuru wake ukaondoka ndani ya mchana wa Ramadhani, itamlazimu kujizuia. Kafiri akisilimu au mwanamke mwenye Hedhi akitwaharika au mgonjwa akipona au msafiri akirejea au mtoto akibalehe au mwendawazimu akipona katika mchana wa Ramadhani na ilhali hawakufunga, itawalazimu kulipa hata kama watafunga sehemu ya siku iliyobaki. Haifai kwa ambaye anaruhusiwa kutofunga katika Ramadhani kufunga saumu nyingine katika Ramadhani hiyo.

**SAUMU YA SUNA:** Saumu bora zaidi ni: Kufunga siku moja na kutofunga siku inayofuata. Halafu, kufunga siku za Alhamisi na Jumatatu kila wiki. Halafu, kufunga siku tatu kila mwezi, na jambo bora zaidi ni siku hizo ziwe Siku Nyeupe (tarehe 13, 14 na 15 za mwezi mwandamo). **Ni suna** kufunga siku nyingi za mwezi wa Muharami na Shabani, siku ya Ashura, siku ya Arafa na siku sita za Mfungo Tatu. **Ni makuruhu** kutenga siku zifuatazo kwa kufunga: Mwezi wa Rajabu, siku ya Ijumaa, siku ya Jumamosi na kufunga siku ya shaka ambayo ni siku ya thalathini ya mwezi wa Shabani, kama anga litakuwa safi. **Ni haramu** kufunga siku ya Idi Elfitri, *Idi al-adh'haa* (Idd Alhaj) na siku za Tashriki, isipokuwa tu kwa mtu ambaye ana wajibu wa kuchinja mnyama wa Tamattui au Qirani.

**ANGALIZO:**

✸ Mtu ambaye ana Hadathi Kubwa, kama mtu mwenye Janaba na mwanamke aliye katika Hedhi na aliye katika Nifasi, akitwaharika kabla ya alfajiri, inafaa kwao kuahirisha kuoga mpaka baada ya Adhana ya sala ya Alfajiri na kutanguliza kula daku kabla ya kuoga, na saumu itakuwa sahihi.

✸ Inafaa mwanamke kutumia dawa ili kuahirisha Hedhi yake katika Ramadhani kwa lengo la kushirikiana na Waislamu wenzake katika ibada zao, ikiwa hakuna madhara.

✸ Inafaa kwa mwenye saumu kumeza mate au kohozi ikiwa liko ndani (kooni).

✸ Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Watu hawataacha kuwa katika kheri madamu wanafanya haraka kufuturu na kuchelewesha kula daku*". Ahmad. Pia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Dini haitaacha kuwa na nguvu madamu watu wanafanya haraka kufuturu, kwani Wayahudi na Wakristo wanachelewesha*". Abudaud.

✸ Inapendekezwa kuomba dua wakati wa kufuturu. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "*Mfungaji wakati wa kufuturu kwake, anayo maombi yasiyorudishwa*". Ibn-majah. Miongoni mwa dua zilizonukuliwa wakati wa kufuturu ni kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: "Dhahabadh-dhwamau wabtal-latil-uruuqu,wathabatal-ajru inshaallah".Ameipokea Hadithi hii Abudaud.

✸ Suna ni kufuturu kwa Tende tosa. Akikosa, iwe kwa Tende mbivu. Akikosa, iwe kwa maji.

✸ Inatakikana kwa mfungaji kujiepusha kupaka wanja na dawa za matone katika macho au masikio wakati wa kufunga, ili kuepuka makindano (mzozo). Ikiwa

atahitaji kama tiba, hakuna ubaya hata kama ladha ya dawa hiyo itafika kooni mwake, na saumu yake ni sahihi.

✷ Ni suna kupiga mswaki nyakati zote za funga bila ya makuruhu, katika kauli iliyo sahihi.

✷ Ni wajibu kwa mfungaji kuacha kusengenya, fitina, kusema uongo na mfano wake. Ikiwa atatokea mtu na kumtukana, aseme: "Mimi nimefunga". Kwa kulinda ulimi wake na viungo vyake vingine visifanye dhambi, mtu atailinda saumu yake. Imekuja kwamba Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: *"Ambaye hakuacha kusema uzushi na kuutumia, hakuna haja kwa Mwenyezi Mungu katika kuacha chakula chake na kinywaji chake"*.Ahmad.

✷ Ni suna kwa aliyealikwa chakula na akawa amefunga kumuombea dua aliyemwalika chakula. Kama hakufunga, ni suna ale.

✷ *Lailatul-Qadri* (usiku wa hadhi) ni usiku bora zaidi katika mwaka. Kupatikana kwake kunahusika na kumi la mwisho katika Ramadhani. Usiku wenye mategemeo zaidi ni usiku wa mwezi ishirini na saba. Amali njema (ifanywayo) katika usiku huo ni bora zaidi kuliko amali (ifanywayo) katika miezi elfu moja. Lailatul-kadri ina alama nyingi. Miongoni mwa alama hizo ni hizi: Kuchimbuka kwa jua asubuhi yake likiwa jeupe lisilokuwa na miali mingi, hali yake ya hewa kuwa tulivu. Lailatul-kadri inaweza kumkuta Mwislamu na ilhali hajui. Linalotakiwa kwa Mwislamu ni kufanya juhudi katika ibada katika Ramadhani, na hasa katika kumi la mwisho. Pia afanye bidii ya kutoupoteza usiku wowote bila ya kusali. Iwapo atasali Tarawehe katika Jamaa, asiondoke mpaka imamu amalize kusali sala ya Tarawehe ikiwa kamili, ili aandikiwe kisimamo cha usiku.

✷ Mtu ambaye ameingia katika kufunga saumu ya suna, ni suna kwake kuikamilisha na sio wajibu. Akikusudia kuibatilisha, hana dhambi na hawajibiki kulipa.

**ITIKAFU** *Itikafu* ni Mwislamu mwenye akili timamu kujilazimisha kukaa msikitini kwa ibada. Inashartiwa kwa anayekaa Itikafu awe ametwaharika na Hadathi Kubwa. Mwenye kukaa Itikafu hatakiwi kutoka (msikitini) isipokuwa tu kwa jambo ambalo hana budi nalo, kama kwa mfano: Kula, kwenda haja na kuoga ambako ni wajibu. Itikafu inabatilika kwa kutoka bila ya dharura na kwa kujamiiana. Itikafu ni suna wakati wote, na katika Ramadhani inasisitizwa zaidi. Ramadhani inayosisitizwa zaidi ni kumi la mwisho. Muda wa chini zaidi wa Itikafu ni saa moja. Inapendekezwa isipungue siku moja. Mwanamke hakai Itikafu isipokuwa tu kwa idhini ya mumewe. Ni suna kwa mwenye kukaa Itikafu kujishughulisha na ibada, kuacha kukithirisha mambo ya **mubaha**, kujiepusha na mambo yasiyomhusu.

# HIJA NA UMRA

Ni wajibu kuhiji na kufanya Umra mara moja tu katika umri. Masharti ya kuwajibika kwa Hija na Umra ni: **1)** Uislamu. **2)** Akili timamu. **3)** Kubalehe. **4)** Uhuru. **5)** Uwezo; mtu kupata chakula na usafiri. Mwanamke anaongeza sharti la sita ambalo ni: Kuwepo mumewe au maharimu wake, naye ni yule mtu ambaye kwake anakuwa haramu daima kumuoa. Aliefanya uzembe mpaka akafa, zitatolewa katika mali yake gharama za Hija na Umra. Hija na Umra haisihi kwa kafiri au mwendawazimu. Hija na Umra inasihi kwa mtoto mdogo na mtumwa na (lakini) haiwatoshelezi wajibu. Mtu asiyekuwa na uwezo, kama fukara, akikopa na kuhiji hija yake itakuwa sahihi. Aliyemhijia mtu mwengine na ilhali yeye mwenyewe hajahiji Hija ya wajibu, hija hiyo itakuwa faradhi yake yeye.

**KUHIRIMIA (KUNUIA):** Ni suna kwa anayetaka kuhirimia: Kuoga, kujisafisha, kujipaka manukato, kuepuka kuvaa vitu vilivyoshonwa na kuvaa shuka na rubega nyeupe na safi. Halafu atahirimia kwa kusema: **Labbayka allaahumma umratan**"au **"Labbayka allahumma hajjan"** au **"Labbayka allaahumma hajjan waumratan"**. Ikiwa atachelea kuzuiwa na jambo lolote, inashartiwa kusema: "**Fa in habasanii haabisun famahil-lii haythu habastanii' =** Likinizuia la kunizuia, mwisho wa ibada yangu ni pale uliponizuia.

**Mwenye kuhiji ana hiari ya kufanya mojawapo ya aina tatu za ibada ya Hija:** **1)** *Tamattu'i.* **2)** *Ifradi.* **3)** *Qirani.* Iliyo bora zaidi ya aina hizo ni *Tamattu'i*. *Tamattu'i* ni kuhirimia kufanya Umra katika miezi ya Hija na kuhitimisha. Halafu atahirimia kufanya Hija katika mwaka huo huo. Ifradi ni kuhirimia kufanya Hija peke yake. Kirani ni kuhirimia kufanya Hija na Umra au kuhirimia kufanya Umra halafu akaichanganyia Hija. Mwenye kutaka kuhiji akishakaa vizuri katika chombo chake cha usafiri, ataleta *Talbiya* kwa kusema: "labbayka llaahumma labbayka,labbayka laa shariika laka labbayka,innal hamda wanniimata laka walmulku laashariika laka"Inapendekezwa kuisema sana hiyo Talbiya na kuileta kwa sauti ya juu kwa wasiokuwa wanawake.

**YALIYOKATAZWA KWA SABABU YA KUHIRIMIA:** Ni mambo tisa: **1)** Kunyoa nywele. **2)** Kukata kucha. **3)** Kuvaa vazi lililoshonwa, kwa mwanaume, isipokuwa tu kama hakupata shuka. Hapo, anaweza kuvaa suruali, au kama hakupata kanda mbili. Hapo, atavaa Hofu (buti),na kuzikata ili ziwe juu ya vifundo viwili vya mguu na hatawajibika kutoa fidia. **4)** Kufinika kichwa, kwa mwanaume. **5)** Kujitia manukato katika mwili wake na katika nguo zake. **6)** Kuua wanyamapori, nao ni wanyama walio halali kuliwa na wanaoishi porini. **7)** Kufunga ndoa. Jambo hilo ni haramu na halina fidia. **8)** Kukumbatia kwa matamanio katika sehemu isiyokuwa ya siri. Fidia yake ni Shaat au kufunga siku tatu au kuwapa chakula masikini sita. **9)** Kujamiiana. Ikiwa kujamiiana kutafanyika kabla ya *Tahaluli* ya kwanza, hija yake itaharibika, atawajibika kuikamilisha na kuilipa mwaka unaofuatia pamoja na kuchinja ngamia atakaegawiwa kwa masikini wa Makka. Ikiwa kujamiiana kutafanyika baada ya *Tahaluli* ya kwanza, Hija yake haitaharibika na atawajibika kuchinja ngamia. Ikiwa mtu atajamiiana katika Umra, kujamiiana huko kutaiharibu umra, atawajibika kuchinja Shaat na atawajibika kuilipa Umra hiyo. Hija na Umra haziharibiki kwa jambo ambalo sio kujamiiana.

Mwanamke ni kama mwanaume isipokuwa kwamba yeye anaruhusiwa kuvaa nguo iliyoshonwa, na lakini havai Nikabu na glovu (soksi za mkononi).

**FIDIA:** Fidia iko katika mafungu mawili: **1)** Ya hiyari. Hiyo ni fidia ya kunyoa au kujitia manukato au kukata kucha au kufinika kichwa na kuvaa vazi lililoshonwa, kwa mwanaume. Ana hiari kati ya: **a)** Kufunga siku tatu, au **b)** Kuwapa chakula masikini sita. Kila masikini mmoja atampa nusu ya pishi (kilo moja na nusu), au **c)** Kuchinja Shaat (Kondoo aliyetimiza miezi sita au mbuzi aliyetimiza mwaka mmoja). Fidia ya mnyamapori ni mfano wa mnyama aliyemuua katika wanyama wa kufuga, kama mnyama pori huyo anaye wa kufanana naye. Kama hana wa kufanana naye, atatoa thamani yake. **2)** Aina ya pili ni fidia ya mpangilio. Hiyo ni fidia ya anayefanya Hija ya Tamatui, ambayo ni kuchinja Shaat, na ya anayefanya Hija ya Kirani ambayo ni kuchinja ngamia. Asipopata mnyama wa kuchinja, atafunga siku tatu akiwa katika Hija na siku saba atazifunga atakaporudi. Wanyama wanaochinjwa na chakula havigawiwi isipokuwa tu kwa masikini wa Makka.

**KUINGIA MAKKA** Mwenye kufanya Hija aingiapo Msikiti Mtukufu *(Al-kaaba),* atasoma uradi wa kisheria wa kuingia misikitini. Halafu ataanza kutufu Tawafu ya Umra ikiwa anafanya Hija ya Tamatui au ataanza Tawafu ya kuingia Makka ikiwa anafanya Hija ya Ifradi au Kirani. Atajifunga rubega nguo yake na, hivyo, ataiweka sehemu ya kati ya nguo yake chini ya kwapa lake la kulia na ncha zake ataziweka juu ya bega lake la kushoto. Ataanzia Jiwe Jeusi; atalishika, atalibusu au ataliashiria na atasema: ***Bismillahi Wallahu Akbar***. Atafanya hivyo katika kila mzunguko. Halafu ataiweka Alkaaba upande wake wa kushoto na kutufu mara saba akienda mwendo wa matiti. (Kwenda matiti ni kwenda mwendo wa haraka haraka na hatua za miguu kuwa karibu karibu) katika mizunguko mitatu ya mwanzo kiasi atakavyoweza. Atatembea mwendo wa kawaida katika mizunguko iliyosalia. Kila atakapoikabili nguzo ya Alyamaaniy, ataishika iwapo ataweza. Atasema baina ya nguzo mbili: "***Rabbanaa aatinaa fidduniyaa hasanatan wafil-aakhirati hasanatan waqinaa adhaabannaari***" Katika mizunguko mingine, ataomba dua apendayo. Halafu atasali rakaa mbili nyuma ya Maqaam Ibrahim ikiwa ataweza. Katika rakaa mbili hizo, atasoma *Suratul-Kaafiruun* (109) na *Suratul-Ikhlas* (112). Halafu atakunywa maji ya Zamzam, na anywe mengi. Atarudi kwenye Jiwe Jeusi na kuligusa ikiwa itamuia wepesi. Halafu ataomba dua *Multazam* ambayo ni sehemu iliopo kati ya Jiwe Jeusi na Mlango (wa Alkaaba). Halafu atatoka kuelekea (kilima cha) Swafaa. Atapanda na kusema: **Ninaanza kwa kile ambacho Mwenyezi Mungu ameanza kwacho** na atasoma kauli ya Mwenyezi mungu: "***Innas-swafaa walmaruwata min shaa iril-laahi,faman hajjal bayta awiitamara falaa junaaha alayhi an yat-twawwafa bihimaa,waman tatwawwaa khairan fa-innallaaha shaakirun aliim***".Ataleta *Takbira* na *Tahlila.* Ataielekea Alkaaba, atanyanyua mikono yake na kuomba. Halafu atateremka na kutembea mwendo wa kawaida mpaka kwenye alama ya kijani. Halafu atatembea mwendo wa haraka mpaka kwenye alama nyingine ya kijani. Halafu atatembea mwendo wa kawaida mpaka afike kwenye (kilima cha) Marwa. Hapo, atafanya kama alivyofanya katika (kilima cha) Swafaa. Halafu atateremka na kutembea mwendo wa kawaida katika

sehemu ya kutembea mwendo wa kawaida na atatembea mwendo wa haraka haraka katika sehemu ya kutembea mwendo wa haraka haraka mpaka akamilishe mizunguko saba. Kutoka Swafaa mpaka Marwa ni mzunguko mmoja, na kutoka Marwa mpaka Swafaa ni mzunguko mmoja. Halafu atapunguza nywele zake au atazinyoa. Kunyoa ni bora zaidi isipokuwa kwa anayefanya hija ya *Tamattui,* kwakuwa yeye atafanya Hija baada ya kufanya kwake Umra. Ama anayefanya Hija ya Kirani na ya Ifradi, hatoki katika ibada yake baada ya Tawafu ya kuingia Makka mpaka akitupa mawe Jamra *Al-akaba* siku ya Idi. Mwanamke ni kama mwanaume isipokuwa kwamba mwanamke hatembei mwendo wa haraka haraka katika kufanya *Tawafu* (kuzunguka Alkaaba) na katika kufanya *Sa'yi* (kutembea kati ya Swafaa na Marwa).

**NAMNA YA KUHIJI:** Ifikapo siku ya Tarwiya (tarehe nane ya Mfungotatu), yule aliyekuwa ametoka katika ibada ya Umra (amefanya Tawafu, amefanya Sa'yi na kunyoa nywele au kupunguza), atahirimia kutoka nyumbani kwake hapo Makka. Atatoka kuelekea Mina ambapo atalala huko usiku wa mwezi tisa. Jua likichimbuka asubuhi ya mwezi tisa, atakwenda Arafa. Halafu ukifika wakati wa adhuhuri, atasali sala ya Adhuhuri na ya Alasiri akizisali kwa pamoja (*Jam-u Takdiim)* na kwa kupunguza (kusali rakaa mbili mbili badala ya nne nne). Arafa yote ni sehemu ya kusimama isipokuwa bonde la *Urana*. Atasema sana: "***Laa ilaha il-lallaahu wahdahuu laa shariika lahu lahul-mulku walahulhamdu biyadihil khairu wahuwa alaa kul-li shay in qadiiru***" Atajitahidi sana kuomba dua na rehema za Mwenyezi Mungu. Jua litakapokuchwa, ataondoka haraka kuelekea Muzdalifa kwa utulivu na upole huku akileta *Talbiya* na akimtaja Mwenyezi Mungu. Akifika Muzdalifa, atasali hapo sala ya Magharibi na ya Isha kwa pamoja na kwa kupunguza. Halafu atalala hapo Muzdalifa. Halafu atasali sala ya Alfajiri mwanzo wa wakati wake. Atabaki hapo Muzdalifa akiomba dua mpaka kupambazuke vizuri. Halafu ataondoka haraka kabla ya jua kuchomoza. Akifika bonde la Muhassir, atakaza mwendo sana ikiwa ataweza mpaka afike Mina. Ataanza kuutupia vijiwe mnara wa *Jamratul-Aqaba*. Atautupia vijiwe saba vilivyo katika ukubwa kama mbwewe (kati ya dengu na lozi). Ataleta *Takbira* pamoja na kila kijiwe na kunyanyua mkono wake katika kila utupaji. Inashartiwa kijiwe kitumbukie katika shimo hata kama hakikulenga mnara. Ataacha kuleta *Talbiya* kwa kuanza kutupa vijiwe.

**Halafu: 1)** Atachinja mnyama wake. **2)** Atanyoa kichwa chake au kupunguza. Kunyoa ni bora zaidi. Kwa kutupa vijiwe na kunyoa, inakuwa halali kwake kufanya kila kitu isipokuwa wanawake. Na hii ndio *Tahaluli* ya Kwanza. Halafu ataelekea Makka na kufanya Tawafu Ifadha. Hii ndio Tawafu ya wajibu ambayo kwayo Hija hukamilika. Halafu atafanya Sa'yi kati ya Swafaa na Marwa ikiwa mtu anafanya hija ya Tamatui au ikiwa hakufanya Sa'yi wakati wa kutufu Tawafu ya kuingia Makka (Tawaf Kudum). Kwa kufanya kwake Tawafu Ifadha, inakuwa halali kufanya kila kitu hata wanawake. Na hii ndio *Tahaluli* ya Pili. Halafu atarudi Mina na kulala hapo ikiwa ni wajibu. Hapo Mina, ataitupia mawe minara (yote mitatu) baada ya jua kumili kuelekea magharibi (wakati wa adhuhuri) katika siku

zote. Kila mnara atautupia vijiwe saba. Ataanzia mnara wa kwanza na kuutupia vijiwe saba, halafu atakwenda mbele, atasimama na kuomba dua. Halafu atauendea mnara wa kati, atautupia vijiwe kama ule wa mwanzo na kuomba dua baada yake. Halafu atautupia vijiwe mnara wa Al-akaba na hatasimama hapo. Halafu atatupa vijiwe kama hivyo katika siku ya pili. Ikiwa atapenda kuondoka haraka katika siku mbili, atatoka Mina kabla ya jua kuchwa. Jua likichwa siku ya mwezi kumi na mbili na ilhali mtu bado yupo Mina, itamlazimu kulala hapo Mina na kutupa vijiwe kesho yake, isipokuwa kama msongamano utamzuia wakati tayari aliazimia kutoka, hapo hakuna ubaya yeye kutoka hata baada ya jua kuchwa. Anayefanya Hija ya Kirani ni kama anayefanya Hija ya Ifradi, isipokuwa kwamba anayefanya Kirani ana wajibu wa kuchinja kama ilivyo wajibu kwa anayefanya Tamatui. Akitaka kusafiri kurudi kwenye familia yake, hatatoka mpaka aiage Alkaaba kwa kutufu ili jambo lake la mwisho iwe *(kutufu)* Alkaaba. Kwa mwanamke mwenye Hedhi na mwenye Nifasi, inawaondokea Tawaf Wadai (Tawafu ya kuaga). Iwapo mtu atajishughulisha na biashara baada ya kutufu Tawafu Wadai, atairudia tena. Ambaye ametoka kabla ya Tawafu Wadai, atarudi kama yupo karibu (na Makka). Kama atakuwa yuko mbali, ni wajibu kwake kuchinja.

**NGUZO ZA HIJA** Nguzo za Hija ni nne: **1)** Kuhirimia; kunuia kuingia katika ibada ya Hija. **2)** Kusimama (kuwepo) Arafa. **3)** Tawafu ya Ziara (Ifadha). **4)** Sa'yi ya Hija.

**WAJIBU WAKE** Wajibu wake ni mambo saba: **1)** Kuhirimia (kunuia kuingia katika ibada ya Hija) katika Mikati (vituo maalum). **2)** Kusimama (kuwepo) Arafa mpaka usiku. **3)** Kulala Muzdalifa mpaka baada ya nusu ya usiku. **4)** Kulala Mina siku za Tashriki **5)** Kuitupia mawe minara (*Jamaraat*). **6)** Kunyoa au kupunguza. **7)** Tawafu ya kuaga (*Tawafu Wadai*).

**NGUZO ZA UMRA** Nguzo za Umra ni tatu: **1)** *Kuhirimia*. **2)** *Tawafu* ya Umra. **3)** *Sa'yi*

**WAJIBU WA UMRA** Wajibu wa Umra ni mambo mawili: **1)** Kuhirimia katika *Miiqati* (vituo maalum). **2)** Kunyoa au kupunguza

Aliyeacha nguzo, **ibada haikamiliki isipokuwa kwa nguzo hiyo**. Aliyeacha wajibu, **ibada inaungwa kwa kuchinja mnyama**. Aliyeacha suna, **hana la kumlazimu**.

**Masharti ya kusihi kutufu Alkaaba ni kumi na tatu:** **1)** Uislamu. **2)** Akili timamu. **3)** Nia maalum. **4)** Kuingia kwa wakati wa kutufu. **5)** Kusitiri uchi kwa anayeweza. **6)** Kutwaharika na Hadathi, sio kwa mtoto. **7)** Kukamilisha mizunguko saba kwa uhakika. **8)** Kuiweka Alkaaba kushotoni mwake. Ataurudia mzunguko ambao ameukosea. **9)** Kutotembea kinyumenyume. **10)** Kutembea kwa miguu kwa anayeweza. **11)** Kufululiza kati ya mizunguko. **12)** Kutufu kuwe ndani ya Msikiti Mtukufu. **13)** Mwanzo uwe kuanzia Jiwe Jeusi.

**Masharti ya kusa'yi ni tisa:** **1)** Uislamu. **2)** Akili timamu. **3)** Kunuia. **4)**Kufululiza. **5)** Kutembea kwa miguu kwa anayeweza. **6)** Kukamilisha mizunguko saba. **7)** Kuyakamilisha vizuri masafa yaliyopo baina ya vilima viwili (Swafa na Mar'wa). **8)** Kusa'yi kunatakiwa kuwe baada ya kutufu ambako ni sahihi. **9)** Kuanza Witri kutokea Swafa, na kanza Shaf'i kutokea Mar'wa.

**Suna za kusa'yi ni:** Kutwaharika na Hadathi na najisi, kusitiri uchi, kuleta uradi na kuomba dua wakati wa kusa'yi, kwenda haraka na kutembea kwa miguu katika sahemu zake, kupanda vilima viwili, kufululiza kati ya kusa'yi na kati ya kutufu.

**ANGALIZO:** Jambo bora zaidi ni kutupa mawe katika siku ile ile. Kama ataahirisha siku ya kutupa mpaka kesho yake au kama ataahirisha siku zote za kutupa mpaka siku ya mwisho katika siku za Tashriki, itatosha.

**UDH'HIYA:** Ni suna iliyosisitizwa. Zikiingia siku kumi za Mfungotatu, ni haramu kwa anayetaka kuchinja Udh'hiya kutoa kitu katika nywelezake au kucha zake au ngozi yake mpaka achinje mnyama wake wa Udh'hiya.

**AKIKA:** Ni suna. Mtoto wa kiume anachinjiwa mbuzi wawili na mtoto wa kike mbuzi mmoja. Huchinjiwa katika siku yake ya saba ya kuzaliwa kwake. Ni suna katika siku ya saba: kunyoa kichwa cha mtoto wa kiume na kutoa sadaka ya fedha kwa thamani ya uzito wa nywele zake na kumpa jina katika siku hiyo. Majina mazuri zaidi ni Abdallah (Mja wa Mwenyezi Mungu), Abdulrahman (Mja wa Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma). **Ni haramu** kwa uja wa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kama *Abdunnabiy* (Mja wa Nabii) na *Abdulrasul* (Mja wa Mtume). (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Ukikutana wakati wa Akika na *Udh'hiya,* inatosha mojawapo kuitosheleza nyingine.

**Huu ni muhtasari wa matendo ya Hija kwa mpangilio:**

| Ibada | Tamatui | Kirani | Ifradi |
|---|---|---|---|
| Mwanzo: *Ihram* na *Talbiya* | *Labbaika* Umra nikifanya *Tamattui* kuelekea Hija | *Labbaika* Hija na Umra | *Labbaika* Hija |
| Halafu | Tawafu ya Umra | *Tawaf* ya Kufika (Makka) | *Tawaf* ya Kufika (Makka) |
| Halafu | *Saa'yi* ya Umra | *Saa'yi* ya Hija | *Saa'yi* ya Hija |
| Halafu | Kupunguza nywele (Tahaluli Kamili) | Atabaki katika Ihramu yake | Atabaki katika Ihramu yake |
| Siku ya 8 kabla ya Adhuhuri | Kunuia Hija kutokea Makka halafu kwenda Mina | Kwenda Mina | Kwenda Mina |
| Siku ya 9 baada ya jua kuchomoza | Kwenda Arafa na kusali Adhuhuri na Alasiri kwa kujumuisha na kupunguza (*Jam'i Takdim*) halafu kujishughulisha na dua mpaka jua kuchwa | | |
| Baada ya jua kuchwa | Kuelekea Muzdalifa na kusali Magharibi na Isha kwa kupunguza wakati wa kufika na kulala hapo mpaka nusu ya usiku na ni suna mpaka Alfajiri | | |
| Siku ya kuchinja 10 (Idi) baada ya Alfajiri kabla ya jua kuchomoza | Kuelekea Mina na kuutupia mawe Mnara wa Akaba | | |
| | Kuchinja mnyama | Kuchinja mnyama | = = = = = = = |
| | Kunyoa au kupunguza halafu *Tawafu Ifadha* Kwa kufanya mawili kati ya haya matatu, imetimia Tahaluli ya Kwanza na kwa kufanya yote matatu inatimia Tahaluli ya Pili | | |
| | *Sa'yi* ya Hija | = = = = = = = | = = = = = = = |
| Siku 11,12 na 13 kwa aliyechelewa | Kutupia mawe minara mitatu; mdogo halafu wa kati halafu wa mwisho baada ya jua kupinduka (kutoka usawa wa dunia) | | |
| Wakati wa kuondoka Makkah | *Tawafu* ya kuaga (*Tawaf Wadai*) na *Tawafu* hii inamwondokea mwanamke aliye katika *Hedhi* na aliye katika *Nifasi* | | |

# FAIDA MBALI MBALI

**Maovu:** Yanafutwa kwa kufanya mambo mengi. Miongoni mwa hayo ni: Toba ya kweli, kuomba msamaha, kufanya mambo mazuri, kupata majaribu ya misiba (majanga), kutoa sadaka, kuombewa dua na mtu mwengine. Ikiwa litabaki jambo na Mwenyezi Mungu ikawa hakulisamehe, mtu ataadhibiwa kwa jambo hilo kaburini au Siku ya Kiyama au katika moto wa Jahanamu, mpaka asafike nalo. Halafu ataingia Peponi kama alikufa akiwa katika Tauhidi. Kama alikufa akiwa katika ukafiri au Shirki au unafiki, atawekwa milele katika moto wa Jahanamu. Maasi na madhambi yana athari nyingi kwa mwanadamu. Athari yake katika moyo ni kwamba yanarithisha upweke, giza, udhalili, maradhi na yanamfanya mtu kuwa mbali na Mwenyezi Mungu. Athari yake katika dini ni kwamba yanarithisha mfano wa madhara yanayopatikana katika moyo, yanazuia utiifu, yanazuia maombi ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Malaika na Waumini. Athari yake katika riziki ni kwamba yanazuia riziki, yanaondoa neema na baraka ya mali. Athari yake kwa mtu mwenyewe ni kwamba yanaondoa baraka ya umri, yanarithisha tabu na mambo kuwa magumu. Athari yake kwa jamii ni kwamba yanaondoa neema ya amani, inaleta ughali (wa bidhaa na maisha), uovu wa watawala na maadui, kutonyesha kwa mvua na mengineyo. Athari yake katika ibada ni kwamba yanazuia kukubaliwa kwa ibada.

**KERO ZA NAFSI:** Raha, furaha ya moyo na kuondoka kwa kero zake ni jambo analolitafuta kila mtu. Kwa hayo, yanapatikana maisha mazuri. Ili yapatikane hayo, kuna sababu za kidini, kimaumbile na za kiutendaji. Zote hazijumuiki isipokuwa kwa muumini tu. Miongoni mwa sababu hizo ni hizi: **1)** Kumwamini Mwenyezi Mungu. **2)** Kufanya mambo yalioamrishwa na kuyaepuka yaliokatazwa. **3)** Kuwafanyia mazuri viumbe wengine kwa kauli, vitendo na aina mbali mbali za mambo mema.**4)** Kujishughulisha na kazi au taaluma zenye manufaa; za kidini au za kidunia. **5)** Kutofikiria mambo yajayo au yaliyopita. Bali mtu anatakiwa ajishughulishe na amali zake za kila siku. **6)** Kumkumbuka na kumtaja sana Mwenyezi Mungu. **7)** Kuzizungumza neema za Mwenyezi Mungu za dhahiri na zisizo za dhahiri. **8)** Kumtizama aliye chini zaidi kuliko sisi na kutomtizama ambaye amepewa fadhila zaidi kuliko sisi kwa mambo ya kidunia. **9)** Kuchukua hatua za kuondoa sababu ziletazo kero za nafsi na kutafuta sababu ziletazo furaha. **10)**Kumuelekea Mwenyezi Mungu kwa baadhi ya maombi ili kuondoa kero za nafsi. **FAIDA:** Ibrahim Alkhawas, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: *"Dawa ya moyo ni mambo matano: Kusoma Qur'ani kwa mazingatio, Kutoshiba sana, Kusali usiku, kunyenyekea (kwa Mwenyezi Mungu) nyakati za usiku wa manane na kukaa na watu wema".*

Aliyeingia msikiti wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ataanza kusali rakaa mbili za maamkizi ya msikiti. Halafu atakwenda kwenye kaburi tukufu (la Mtume). (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Atasimama mbele ya uso wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, huku akikipa mgongo Kiblah, moyo ukiwa umejaa haiba ya heshima kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kama vile anamuona. Atamsalimu akisema:"Assalaamu alaika yaa rasuulallaahi" Kama ataongeza zaidi zaidi ya hapo ni vizuru. Halafu atachipuka upande wa kulia kiasi cha dhiraa moja na kusema: "Assalamu alayka yaa abaabakris-

swiddiiq,assalaamu alayka yaa umarulfaaruuq, allaahummajzihimaa an nabiyyihimaa waanil-islaami khayraa".Amani iwe kwako ewe Abubakar Siddik, amani iwe kwako ewe Omar Alfaruk. Ewe Mola wetu, walipe kheri kwa kumtumikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wao na kwa kuutumikia Uislamu. Halafu atarudi eneo la raudhwa tukufu kisha ataelekea Kiblah huku Chumba (alichozikwa mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) humo na Swahaba wake wawili) kikiwa kushotoni mwake na ataomba.

✸ **NDOA: Ni suna** kuoa kwa mtu mwenye kutamani, asiyechelea zinaa. Kuoa ni jambo linalofaa kwa mtu ambaye hana matamanio. Kuoa **ni wajibu** kwa mtu anayechelea zinaa, na kutapewa kipaumbele kuliko kuhiji ambako ni wajibu. **Ni haramu** kumtazama mwanamke, kumtazama mwanamke mzee kwa kumtamani, kumtazama mwanaume mwenye sura nzuri, kukaa faragha na kumtazama mnyama anayemtamani.

**MASHARTI YA NDOA:** Inasihi mwanaume kumuoa mwanamke kwa masharti. **1)** Kuwaainisha wanao oana. Haitakuwa sahihi kwa Walii kusema (kumwambia muoaji): Nimekuozesha mmojawapo wa binti zangu, huku akiwa na binti zaidi ya mmoja. **2)** Ridhaa ya mwanaume Mukallaf (balehe), mwongofu na ridhaa ya mwanamke huru, mwenye akili timamu. **3)** Kuwepo Walii. Haisihi mwanamke kujiozesha mwenyewe. Pia hawezi kumuozesha mwanamke mtu asiyekuwa walii, isipokuwa tu ikiwa Walii atakataa kumuozesha mwanamke kwa mtu ambaye ni muafaka kwake. Mwenye haki zaidi ya kumuozesha mwanamke ni baba halafu babu na kwenda juu. Halafu mtoto wa kiume wa mwanamke,halafu mjukuu wake wa kiume na kwenda chini. Halafu ndugu wa kiume (kaka) wa baba mmoja mama mmoja. Halafu ndugu wa kiume wa baba mmoja. Halafu mtoto wa kiume wa ndugu wa kiume, n.k. **4)** Ushahidi. Ni lazima kuwepo kwa mashahidi wawili wanaume, balehe, wenye akili timamu na waadilifu. **5)** Mwanaume na mwanamke wasiwe na pingamizi, kama kunyonya, nasaba au ukwe.

**WALIO HARAMU KUOLEWA: AINA YA KWANZA**: Ni walio haramu daima. Hao ni mafungu mengi. **1)** Walio haramu kwa sababu ya nasaba. Hao ni mama, bibi na kwenda juu, mtoto wa kike (binti), mtoto wa kike wa mtoto wa kiume na kwenda chini, ndugu wa kike(dada) wa vyovyote (baba mmoja mama mmoja au baba mmoja au mama mmoja), mtoto wa kike wa ndugu wa kiume, binti wa mtoto wa kiume wa dada au binti yake, binti wa kaka wa vyovyote, wajukuu wao, wajukuu wa watoto wao wa kiume au dada zao na kwenda chini, shangazi, ndugu wa kike wa mama na kwenda juu. **2)** Walio haramu kwa sababu ya kunyonya. Walio haramu kwa sababu hii ni kama wale walio haramu kwa nasaba, hata ukwe. **3)** Walio haramu kwa ukwe. Hao ni mama wa mkewe na bibi zake, wake wa wazazi wa nasaba yake, watoto wa kike wa mke na kwenda chini.

**AINA YA PILI:** Ni walio haramu kwa kipindi maalum. Hao ni mafungu mawili. **1)** Walio haramu kwa sababu ya kukutana pamoja, kama vile kuoa dada wawili kwa pamoja,mwanamke na shangazi yake au mama yake mdogo. **2)** Walio haramu kwa sababu ya jambo lililozuka na linaloweza kuondoka, kama mke wa mtu mwengine.

**FAIDA:** Haifai kwa wazazi wa mwanaume kumlazimisha kuoa mke asiyemtaka, sio wajibu kuwatii katika hilo na kwa kufanya hivyo mwanaume huyo hatakuwa amewaasi wazazi.

✸ **TALAKA:** Ni haramu kumpa talaka mke akiwa katika Hedhi au Nifasi au katika twahara ambayo amemuingilia kimwili katika twahara hiyo, na lakini Talaka inakuwa sahihi. **Ni makuruhu** kutaliki bila ya sababu (ya kisheria). **Ni halali kutaliki** kwa sababu, na **ni suna** kwa anayepata madhara kutokana na ndoa. Sio wajibu kuwatii wazazi katika Talaka. Anayetaka kumtaliki mkewe, ni haramu kwake kumtaliki zaidi ya Talaka moja. Inapasa mke apewapo Talaka, awe katika twahara ambayo mume hakumuingilia kimwili mkewe katika twahara hiyo. Atamtaliki Talaka moja na kumuacha bila ya kuongeza talaka nyingine mpaka eda yake ishe. Ni haramu kwa mke ambaye Talaka yake ni Rejea kutoka katika nyumba yake au mumewe kumtoa katika nyumba hiyo kabla ya Eda yake kukamilika. Talaka inapatikana kwa kutamka na, kwa hiyo, haipatikani kwa nia pekee.

✸ **VIAPO:** Ili Kafara iwe wajibu katika kuapa, kuna masharti manne: **1) Kudhamiria tendo la kuapa**. Kiapo hakifungamani ikiwa mtu atakitamka kiapo kwa ulimi wake bila ya kukusudia kiapo, kama kusema wakati wa mazungumzo: “Wallahi (Kwa jina la Mwenyezi Mungu) sio” au “Wallahi (Kwa jina la Mwenyezi Mungu) ndio”. Hiki kinaitwa: Kiapo cha Upuuzi. **2) Kiapo kiwe kinaapia jambo la baadaye linalowezekana.** Kiapo hakifungamani katika jambo lililopita huku muapaji akiwa hajui au akidhani kuwa anasema kweli au akijua kuwa anasema uongo. Hiki ni Kiapo cha Gharika na ni miongoni mwa madhambi makubwa. Pia kiapo hiki ni mtu kuapa katika jambo la baadaye akidhani kuwa anasema kweli na ikadhihirika kinyume chake. **3) Muapaji awe anaapa kwa hiari;** asiyelazimishwa. **4) Kutovunja kiapo chake** kwa kufanya jambo aliloapa kuliacha au kuacha jambo aliloapa kulifanya. Aliyeapa na akaopoa, sio wajibu kwake kutoa Kafara kwa masharti mawili: **1.** Uopoaji ushikane na kiapo. **2.** Mtu adhamirie kukiambatanisha kiapo na uopoaji, kama kusema: “Wallahi akitaka Mwenyezi Mungu…….”.

Mwenye kuapa juu ya jambo fulani na akaona kuwa manufaa yanataka kinyume chake, ni suna kukitolea Kafara kiapo chake na afanye lile jambo ambalo ni bora.

**KAFARA YA KIAPO:** Ni kuwapa chakula masikini kumi. Kila masikini apewe nusu Pishi (kilo moja na nusu) ya chakula au kuwapa nguo au kuacha huru mtumwa. Ambaye hakupata (hayo), ni wajibu kwake kufunga siku tatu mfululizo. Aliyefunga pamoja na kuwa na uwezo wa kuwapa chakula masikini au kuwapa nguo, dhima yake haitamtoka. Inafaa kutoa Kafara kabla ya kuvunja Kiapo au baada yake. Aliyeapa zaidi ya mara moja juu ya jambo moja, inamtosha Kafara moja. Kama mambo aliyoapa ni mengi, Kafara pia zitakuwa nyingi.

✸ **NADHIRI:** Nadhiri ni aina nyingi. **1) Nadhiri ya Jumla,** kama kusema: “Nitamfanyia Mwenyezi Mungu Nadhiri (jambo) ikiwa nitapona” na akanyamaza bila ya kukusudia Nadhiri maalum. Atawajibika kutoa Kafara ya Kiapo iwapo atapona. **2) Nadhiri ya malumbano na hasira.** Nadhiri hiyo ni kuihusisha Nadhiri na sharti kwa nia ya kujizuia kufanya jambo au kujilazimisha kulifanya jambo hilo, kama mtu kusema: “Nikikusemesha, nitafunga mwaka mmoja”. Hukumu yake ni

kwamba mtu ana hiari kati ya kulifanya jambo alilojilazimisha au kutoa Kafara ya Kiapo endapo atamsemesha. **3) Nadhiri Halali.** Mfano: Nina wajibu kwa Mwenyezi Mungu kuvaa nguo yangu". Hukumu yake ni kwamba mtu ana hiari kati ya kuvaa nguo au kutoa Kafara ya Kiapo. **4) Nadhiri Karaha.** Mfano: "Ni juu yangu kwa Mwenyezi Mungu kumtaliki mke wangu". Hukumu yake ni kwamba ni suna kwa mtu aliyesema hayo kutoa Kafara na asiitekeleze Nadhiri aliyoiweka. Iwapo ataitekeleza Nadhiri hiyo, hawajibiki kutoa Kafara. **5) Nadhiri ya Maasi.** Mfano: "Ni wajibu wangu kwa Mwenyezi Mungu kuiba". Hukumu yake ni kwamba ni haramu kuitekeleza Nadhiri hiyo, na atalazimika kutoa Kafara ya Kiapo. Ikiwa ataitekeleza, atapata dhambi na hawajibiki kutoa Kafara. **6) Nadhiri ya Utiifu.** Mfano: "Ni wajibu wangu kwa Mwenyezi Mungu kusali rakaa …..", kwa lengo la kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Ikiwa ataihusisha Nadhiri hiyo na sharti, kama kupona kwa mgonjwa, itawajibika kuitekeleza Nadhiri hiyo pale sharti litakapopatikana. Kama Nadhiri hiyo hakuihusisha na sharti, ni wajibu kuitekeleza Nadhiri hiyo vyovyote iwavyo.

✸ **KUNYONYESHA:** Yanakuwa haramu kwa kunyonya yale yanayokuwa haramu kwa nasaba, kwa masharti matatu: **1)** Maziwa yawe yanatokana na uzazi na si jambo jingine. **2)** Unyonyaji wa mtoto uwe ndani ya miaka miwili ya mwanzo ya kuzaliwa. **3)** Mara za kunyonyesha ziwe tano na zaidi kwa uhakika. Makusudio ya mara ya kunyonyesha ni mtoto kufyonza ziwa mpaka aliache, na sio kushiba. Haithibiti kwa kunyonyesha huduma na mirathi.

✸ **USIA: Usia unakuwa wajibu** baada ya kufa, kwa mtu ambaye ana haki (ya mtu mwengine) bila ya kuwepo kwa ushahidi. Anatakiwa ausie haki hiyo apewe mwenyewe. **Usia unakuwa suna** kwa mtu aliyeacha mali nyingi. Inapendekezwa ausie sehemu ya tano ya mali yake itolewe sadaka apewe ndugu masikini asiyerithi. Kama hakuna ndugu fukara asiyerithi, ausie kupewa masikini, mwanachuoni au mtu mwema. Kwa mtu fukara mwenye watu wanaomrithi, **ni makuruhu kutoa Usia,** isipokuwa kama warithi hao watakuwa wanajitosha (wana uwezo). Hapo, **Usia utakuwa halali**. **Ni haramu kuusia** zaidi ya theluthi ya mali kupewa mtu kando (asiyekuwa ndugu). Ni haramu kuusia mrithi apewe kitu hata kama ni kidogo, isipokuwa kama warithi wengine wataliruhusu hilo baada ya kufa kwake. **Usia unakuwa batili** kwa muusiaji kusema: Nimejirudi au nimebatilisha au nimeghairi na mfano wa hayo. Inapendekezwa aandike mwanzo wa Usia wake: *Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Haya ndio aliyousia kwamba yeye anakiri kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, pekee, asiye na mshirika na kwamba Muhammad ni Mja wake na ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake, na kwamba Pepo ni kweli na moto ni kweli, na kwamba Kiyama kinakuja hakina shaka, na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walioko makubirini. Ninawausia ndugu zangu niliowaacha kwamba wamuogope Mwenyezi Mungu na waishi vizuri, wamtii Mwenyezi Mungu na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wake kama wao kweli ni waumini. Ninawausia yale ambayo (Nabii Ibrahimu) aliwausia watoto wake na pia (Nabii) Yakubu: "Enyi wanangu, kwa*

*yakini, Mwenyezi Mungu amekuchagulieni dini. Kwa hiyo, msife ila nyinyi ni Waislamu".* **Sura Albaqara (2), aya 132.**

✸ Inapendekezwa anapoombewa rehema Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, yajumuishwe maombi hayo na kumuombea amani. Isiishie kwenye maombi mamoja tu. Wasiokuwa Mitume, hawaanzwi kuombewa rehema. Haisemwi: Abubakar, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani au: Imfikie amani. Hilo ni makuruhu karaha ya kutakasa (itikadi). Kwa makubaliano ya wanachuoni, inafaa kuwafanya wasiokuwa Mitume wakiwafuatia Mitume kwa kusema: Ewe Mola wetu, mfikishie rehema na amani Muhammad na Familia ya Muhammad na Swahaba wake na wake zake na kizazi chake. **Inapendekezwa kuwaombea radhi na rehema Swahaba**, Taabi'iina na wanachuoni, wafanya ibada na watu wema wengine waliokuja baada yao. Kama Abuhanifa, Malik, Shaafii na Ahmad, Mwenyezi Mungu awawiye radhi au kusema: Mwenyezi Mungu awarehemu.

✸ **KUCHINJA:** Ni wajibu kumchinja mnyama ili iwe halali kumla. Inashartiwa katika mnyama: **1)** Awe halali kuliwa. **2)** Awe anashikika. **3)** Awe mnyama wa nchi kavu.

Kuchinja kuna masharti manne: **1)** Mchinjaji awe mwenye akili timamu. **2)** Zana ya kuchinjia isiwe jino au kucha, kwani haifai kuchinja kwa zana hizo. **3)** Kukata koo, mishipa miwili ya pembeni mwa shingo au mmoja wao na mrija wa chakula. **4)** Kusema: *Bismillahi* wakati wa kitendo cha mkono kuchinja. *Bismillahi* inasameheka kwa kusahau, na inafaa kusemwa kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu. Ni suna pamoja na *Bismillahi* kuleta *Takbira.*

✸ **UWINDAJI:** Inashartiwa kwa mnyama anayekusudiwa kuwindwa masharti yafuatayo: **1)** Mnyama awe halali kuliwa. **2)** Awe ni mnyama wa porini kwa maumbile. **3)** Awe hashikiki. **Hukumu ya kuwinda**: Ni halali kwa anayekusudia kuwinda. Ni makuruhu kuwinda kwa kujiliwaza au kucheza. Ikiwa mtu atawakera watu kwa kumfuatilia mnyama anayemuwinda, kuwinda kutakuwa haramu. **Inafaa kuwinda kwa masharti manne: 1)** Muwindaji awe miongoni mwa wale wanaoruhusiwa kuchinja. **2)** Zana ya kuwindia ziwe miongoni mwa zile zana ambazo ni halali kuchinja kwa zana hizo. Hilo litapatikana kwa zana hiyo kuwa kali, kama mkuki, mshale na mfano wake. Ikiwa uwindaji unafanyika kwa kutumia mnyama anayejeruhi, kama kipanga au mbwa, inashartiwa mnyama huyo awe amefundishwa. **3)** Kusudio la kutenda; kutupa zana kwa makusudio ya kuwinda. Ama aala[1] ikiwinda bila ya mwenye ala hiyo kukusudia kuwinda, mnyama huyo aliyewindwa si halali kuliwa. **4)** Kusema: *Bismillahi* wakati wa kuituma zana (ya kuwindia). *Bismillahi* hapa haisameheki hata kama ni kwa kusahau na, kwa hiyo, ni haramu kula mnyama aliyechinjwa bila ya *Bismillahi.*

✸ **CHAKULA:** Chakula ni kila kitu kinacholiwa na kinachonywewa. Asili katika vitu hivyo ni halali. Kila chakula ni halali kwa masharti matatu: **1)** Chakula kiwe twahara. **2)** Chakula kiwe hakina madhara. **3)** Chakula kisiwe uchafu. **Ni haramu** kila chakula najisi, kama damu na mzoga. Pia ni haramu chakula chenye madhara,

---

[1] *Nyenzo za kuwindia.*

kama sumu, na uchafu kama kinyesi, mkojo, chawa na kiroboto. **Ni haramu** katika wanyama wa nchi kavu: Punda wafugwao, wanyama wanaowinda kwa kutumia meno yao kama simba, chui, duma, mbwa, nguruwe, nyani na paka hata kama ni paka wa porini, kicheche, kuchakuro, isipokuwa fisi. Katika ndege, **ni haramu** wale ambao wanawinda kwa kutumia kucha zao kama tai, mwewe, kipanga, shorewanda, bundi na wanaokula mizoga kama tai na kila wanyama na ndege ambao watu wa miji wanawaona kuwa wabaya, kama poponundu, panya, nyuki, nzi, kipepeo, hudihudi, nungunungu na nyoka. **Ni haramu** pia wadudu, kama funza au minyoo, mende, mjusi. na kila mdudu ambaye sheria imeamuru auliwe, kama n'ge au mdudu ambaye sheria imekataza kumuua kama sisimizi. Pia ni haramu mnyama aliyezaliwa kutokana na mnyama anayeliwa na asiyeliwa kama vile mnyama ambaye amezaliwa kutokana na mbwa mwitu na fisi. Si haramu mnyama aliyezaliwa kutokana na wanyama wawili halali, kama nyumbu na pundamilia na farasi. Mnyama ambaye watu hawamjui na hakutajwa katika sheria, atarejeshwa kwenye mnyama anayefanana naye kwa karibu. Akifanana na mnyama halali, naye atakuwa halali. Na akifanana na mnyama haramu, naye atakuwa haramu. Ikiwa atafanana na mnyama halali na haramu, utapewa uzito upande wa haramu. Wanyama wasiokuwa hao **ni halali**, kama vile wanyama wa kufuga (Ngamia, n'gombe, mbuzi na kondoo) na farasi. Pia ni halali wanyama pori, kama twiga, sungura, kenge, paa. Pia ni halali ndege, kama mbuni, kuku, tausi, kasuku, njiwa, chiriku, bata na batamzinga. Ndege wa majini wote na wanyama wa baharini, ni halali isipokuwa chura, nyoka na mamba. Mazao yaliyomwagiliwa au kutiwa mbolea kwa najisi, yanafaa kuliwa isipokuwa tu ikiwa ladha au harufu ya najisi itajitokeza wazi. Hapo, itakuwa haramu. Ni makuruhu kula mkaa na mchanga. Pia ni makuruhu kula kitunguu maji, kitunguu saumu na mfano wake isipokuwa baada ya kupikwa. Ikiwa mtu atakuwa na njaa na akashikika, atakula kiasi kitakacho okoa uhai wake tu, ikiwa ni wajibu kufanya hivyo.

✸ Ni haramu kuwapongeza makafiri katika sikukuu zao au kuhudhuria. Pia ni haramu kuanza kuwasalimu. Ikiwa wataanza kutusalimia, ni wajibu kujibu kwa kusema: ***Wa alaykum.*** Ni haramu kuwasimamia na pia kumsimamia mwenye kufanya Bid'a. Ni makuruhu kupeana nao mikono. Ama kuwapa pole na rambirambi na kuwasalimia wagonjwa wao ni haramu, isipokuwa tu kwa maslahi ya kisheria.

# RUQ-YA KISHERIA

Anayezitafakari kanuni za Mwenyezi Mungu atajua, kwa yakini, kuwa kupata mtihani (balaa, maafa, majaribu) ni kanuni miongoni mwa kanuni za Mwenyezi Mungu za kidunia na zilizopangwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa: ***"Na, kwa yakini, tutakupeni mtihani mdogo wa hofu na njaa na upungufu wa mali na nafsi na matunda, na wape habari njema wenye subira".*** Suratul-Baqara 2, aya 155. Anafanya makosa anayedhani kuwa waja wema wa Mwenyezi Mungu ndio watu walioko mbali zaidi na misiba na balaa. Majaribu ni dalili ya imani. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, aliulizwa: Ni watu gani wenye mtihani zaidi? Alisema: ***"Ni Mitume, halafu watu wema, halafu watu walio afadhali halafu walio afadhali. Mtu atapewa mtihani kwa kadiri ya dini yake. Mtu akiwa na umadhubuti katika dini yake, huongezewa katika mtihani wake. Na akiwa na ulaini katika dini yake, hufanyiwa tahfifu".*** Ibnimaajah. Kupewa mitihani ni miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu kumpenda mja. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Na Mwenyezi Mungu akiwapenda watu, huwapa mitihani".*** Ahmad. Hilo pia ni miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu kumtakia kheri mja wake. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Mwenyezi Mungu akimtakia kheri mja wake, humharakishia mateso duniani, na Mwenyezi Mungu akimtakia shari mja wake hujizuia naye kwa madhambi yake ili amlipe kwayo Siku ya Kiyama".*** Tirmidhiy. Mitihani ni kafara ya madhambi, hata kama ni madogo. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Hakuna Mwislamu yeyote anayepatwa na adha ya mwiba na zaidi isipokuwa kwamba, kwa mwiba huo, Mwenyezi Mungu humfutia madhambi yake kama mti unavyodondosha majani yake".*** Bukhariy na Muslim. Kwa ajili hiyo, Mwislamu aliyepata mtihani akiwa ni mwema basi mtihani huo ni kufuta maovu yaliyopita au kupandishwa daraja. Na akiwa ni mfanya maasi, mtihani huo ni kufuta maovu na ukumbusho wa hatari yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Umedhihiri uovu katika bara (nchi kavu) na katika bahari kwa sababu ya yale ambayo mikono ya watu imeyachuma ili (Mwenyezi Mungu) awaonjeshe baadhi ya yale waliyoyatenda, huenda wakarejea".*** Sura arruum (30), aya 41.

**AINA ZA MITIHANI:** Kuna mtihani wa kheri, kama kuongezeka kwa mali, na kuna mtihani mbaya, kama hofu, njaa na kupungua kwa mali. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa: ***"Na nitakujaribuni kwa shari na kheri ikiwa ni mtihani".*** **Sura Alanbiyaa (21), aya 35.** Miongoni mwa mtihani huo mbaya ni mtihani wa maradhi na mauti, mtihani ambao kubwa ya sababu zake ni kijicho na uchawi unaotokana na husda. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Wengi zaidi wa wanaokufa katika uma wangu baada ya hukumu ya Mwenyezi Mungu na mipango yake ni kwa sababu ya kijicho".*** Twayaalisiy.

**KINGA YA JICHO NA UCHAWI :** Kinga ni bora zaidi kuliko tiba. Kwa hiyo, ni wajibu kwetu kufanya bidii ya kujikinga. Miongoni mwa kinga muhimu zaidi ni hizi: ✸ Kuipa nguvu nafsi kwa Tauhidi (kumpwekesha Mwenyezi Mungu) na kuamini kwamba mwenye kuendesha mambo ulimwenguni ni Mwenyezi Mungu. ✸ Kufanya sana mambo mazuri. ✸ Kuwa na dhana nzuri kwa Mwenyezi Mungu na kumtegemea. Mtu asiwe na hofu ya fikra kuwa ugonjwa na kijicho ni kwa ajili ya jambo lolote lililojitokeza, hofu ya fikra yenyewe ni ugonjwa.[1] ✸ Ikitangazika

[1] Madaktari na wataalamu wanasema kuwa karibu theluthi mbili ya magonjwa ya mwili yanatokana na sababu za kisaikolojia kwa kudhani kuugua na wakati ugonjwa haupo kamwe.

kwamba mtu fulani ana kijicho au ni mchawi anatengwa, kwa msingi wa kuchukua sababu (za tahadhari) na sio kwa kuogopa (uovu wake). ✸ Mtu kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba baraka wakati wa kuona jambo linalomfurahisha. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Atakapoona mmoja wenu kwake mwenyewe au katika mali yake au kwa ndugu yake jambo linalomfurahisha, basi aombe baraka, kwani kijicho ni kweli".*** Haakim. Kuomba baraka ni kusema: Baarakallahu laka = Mwenyezi Mungu akubariki, na sio kusema: Tabaarakallah = Ametukuka Mwenyezi Mungu. ✸Kufungua kinywa asubuhi kwa kula tende saba katika tende za Mji wa Mtume (Madina). ✸Kumkimbilia Mwenyezi Mungu, kumtegemea, kuwa na dhana nzuri kwake na kumuomba kinga ya kijicho na uchawi, na kudumu kusoma nyiradi za kila siku; asubuhi na jioni[1]. Nyiradi hizi zina athari inayozidi na kupungua kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kwa mambo mawili: **1)** Kuamini kwamba yaliyomo katika nyiradi hizo ni haki na kweli na kwamba yana manufaa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. **2)** Ulimi wa mtu utamke nyiradi hizi na ilhali masikio yake yanazisikiliza na moyo wake uwe hadhiri (makini), kwa sababu nyiradi hizi ni dua (maombi), na dua itokayo katika moyo ulioghafilika na kupuuza haijibiwi, kama hilo lilivyosihi kunukuliwa kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.

**WAKATI WA NYIRADI NA KUOMBA KINGA:** Nyiradi za asubuhi zinasomwa baada ya sala ya Alfajiri. Ama nyiradi za jioni zinasomwa baada ya sala ya Alasiri. Mwislamu akighafilika au akisahau kuzisoma, azisome wakati wa kukumbuka.

**DALILI ZA KUPATWA NA KIJICHO NA MENGINEYO:** Hakuna kupingana kati ya tiba (za kisasa) na tiba ya kisheria (Ruq-ya). Ndani ya Qur'ani, kuna tiba ya magonjwa ya mwili na magonjwa ya kiroho. Mwanadamu anapokuwa hana magonjwa ya kimwili, aghlabu dalili za magonjwa zinakuwa katika mtindo wa: Kuumwa kichwa kunakohamahama au rangi ya manjano usoni, kutokwa na jasho sana na kukojoa sana, kutokuwa na hamu ya kula, kutokwa majipu au kusikia joto au baridi katika viungo, mapigo ya moyo kwenda mbio, maumivu yanayohama hama chini ya mgongo na mabegani, huzuni na kupumua kwa tabu, kukosa usingizi usiku, hasira kali zitokanazo na hofu na ghadhabu zisizokuwa za kawaida, kuteuka sana, kuvimba tumbo (zongo), kupenda kujitenga (mtu kukaa peke yake), uchovu na uvivu, kupenda kulala na matatizo mengine ya kiafya yasiyokuwa na sababu za kidaktari. Dalili hizi zinaweza kupatikana zote au baadhi yake kwa kadiri ya nguvu ya ugonjwa na udhaifu wake.

**Ni lazima kwa Mwislamu awe na imani yenye nguvu na moyo shupavu** ili asiingiliwe na wasiwasi kwa kuitia hofu nafsi yake kuwa amepatwa na ugonjwa fulani kwa kuhisi tu kuwa ana mojawapo ya dalili hizi. Maradhi ya wasiwasi ni mojawapo ya magonjwa magumu sana kutibika. Dalili hizi zinaweza kuwepo kwa baadhi ya watu na ilhali wao ni wenye afya nzuri. Pia dalili hizi zinaweza zikawepo na ilhali sababu ni maradhi ya viungo vya mwili. Pia zinaweza kuwepo na ilhali sababu ya dalili hizo ni imani dhaifu, mfano: Kubanwa kifua, kupata riziki ndogo, huzuni, uchovu na mengineyo. Ni wajibu wake mtu kuuchunguza uhusiano wake na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

---

[1] Angalia nyiradi za asubuhi na jioni, ukurasa wa .....

**Ugonjwa ukiwa umesababishwa na Jicho (kijicho)[1], tiba, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, inakuwa kwa kufanya mojawapo ya mambo mawili yafuatayo**: **1)** Ikiwa umemjua aliyefanya kijicho, utamuamuru aoge na kuyachukua maji haya au mabaki yake[2] halafu utaoga kwayo na kuyanywa. **2)** Ikiwa aliyefanya kijicho hajulikani, tiba inakuwa kwa Ruq-ya, dua na kuumika (kupiga chuku).

**Ugonjwa ukiwa ni uchawi[3], tiba, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, inakuwa kwa kufanya mojawapo ya mambo kadhaa**: **1) Kujua mahali ulipo uchawi. Akiukuta**, atafungua vifundo vyake huku akisoma sura mbili za kinga (sura Alfalaq 113 na sura Annas 114) na kisha kuuchoma moto. **2) Kusoma Ruq-ya** ya Kisheria kwa kutumia aya za Qur'ani, na hasa kwa kutumia sura mbili za kinga na dua. Utakuja ufafanuzi wa Ruq-ya. **3) Nushra.** Nayo iko katika aina mbili : **a) Nushra haramu**. Hii ni Nushra ya kuuondoa uchawi kwa kutumia uchawi na kwenda kwa wachawi ili kuondoa uchawi. **b) Nushra inayofaa**. Miongoni mwa Nushra hii ni: Kuchukua majani saba ya mti wa Mkunazi na kuyaponda. Halafu kuyasomea sura Alkaafirun (109) na sura Al-ikhlas (112) na sura Alfalaq (113) na sura Annas (114) mara tatu. Halafu kuyatia katika maji. Halafu kuyanywa na kuyaoga. Atarudia kufanya hivyo mpaka atakapopona Mwenyezi Mungu akipenda. Ameyasimulia haya Abdulrazak katika kitabu chake Musannaf. **4) Kutoa uchawi:** kwa kusafisha tumbo kwa dawa za kuharisha ikiwa uchawi uko tumboni, na kwa kupiga chuku[4] ikiwa uchawi uko sehemu nyingine isiyokuwa tumbo.

**RUQ-YA MASHARTI YAKE:** **1)** *Ruq-ya* iwe kwa aya za Qur'ani na dua za kisheria. **2)** Ruq-ya iwe kwa lugha ya Kiarabu. Dua zinafaa kwa lugha nyingine. **3)**Kuwa na itikadi kwamba Ruq-ya haiathiri yenyewe, na kwamba tiba inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kuzidisha taathira ya Ruq-ya, inatakiwa kusoma Qur'ani kwa nia ya tiba na mwongozo[5] kwa binadamu na majini. Qur'ani imeshuka ikiwa ni mwongozo na tiba. Haisomwi kwa nia ya kumuua jini ila baada kushindikana kutoka kwa njia zilizotangulia.

---

[1] Kijicho: Ni madhara yatokanayo na jini yanayompata mkusudiwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya sifa na husda ya mfanyaji kijicho na ambaye amefikiwa na mashetani na pasiwepo kinga (kama uradi, sala na kinga nyinginezo). Ushahidi wa hayo ni Hadithi isemayo "Jicho ni kweli". Ameipokea hadithi hii Bukhariy. Pia kuna upokezi mwingine usemao: "Jicho ni haki (ambayo) inahudhuriwa na shetani na husda ya binadamu". Amaeipokea Hadithi hii Ahmad na Haithamiy ameisahihisha. Pia Hadithi hii ina ushahidi mwingine. Ametaja jicho kwa sababu ndio zana ya kusifia na sio kwamba ndilo linaloleta madhara, kwa ushahidi kwamba mtu kipofu anamdhuru mwengine na ilhali hamuoni.

[2] Mabaki: Ni kitu chochote alichokigusa mwenye kufanya kijicho, kama mabaki ya kinywaji alicho kunywa au chakula alicho kula au kitu alicho kigusa. Yatachukuliwa mabaki hayo yatapanguswa kwa kitambaa na kuongezewa maji halafu amwagiwe aliepatwa na kijicho na anywe baadhi yake.

[3] Uchawi ni vifundo, visomo na maneno yanayotamkwa au kufanywa kitu kinacholeta taathira moja kwa moja katika mwili wa mtu aliyerogwa au moyo wake au akili yake. Uchawi una ukweli. Kuna uchawi unaoua, kuna unaosababisha kuugua, kuna unaomfanya mtu ashindwe kujamiiana na mkewe, kuna unaotenganisha kati ya mke na mume. Kuna uchawi ambao ni ushirikina na ukafiri na kuna ambao ni madhambi makubwa.

[4] Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "Dawa bora mliyojitibia ni kuumika (kupiga chuku)". Mwenyezi Mungu katika matukio ya kweli ameponya magonjwa ya viungo kwa kuumika na magonjwa yaliyo sababishwa na jicho, uchawi, kama saratani.

[5] **Nia ya mwongozo** ni kumhubiria anayeisikia Qur'ani afuate dini ya Mwenyezi Mungu, atende kheri na aache maovu. Nia hii ina taathira kubwa kwa majaribio. Aghlabu majini wanaathirika na Qur'ani na haraka huacha kumdhuru mgonjwa, kinyuma cha nia ya kuua ambayo inampa jini kiburi, upinzani na kumdhuru mgonjwa na msomaji Ruq-ya. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema: "Mwenyezi Mungu ni mpole, anapenda upole. Anatoa katika upole mambo ambayo hayatoi katika nguvu".

**Masharti ya anayesoma Ruq-ya: 1)** Awe Mwislamu mwema, mwenye uchamungu. Kadiri anavyokuwa mwema zaidi, ndipo taathira inakuwa na nguvu zaidi. **2)** Wakati wa kusoma Ruq-ya, amwelelekee Mwenyezi Mungu kwa ukweli kwa namna ambayo moyo uwe pamoja na ulimi. Jambo bora zaidi ni mtu kujisomea mwenyewe Ruq-ya, kwa sababu: **a)** Moyo wa mtu mwengine aghlabu unakuwa umeshughulishwa na **b)** Hakuna yeyote anayehisi shida na mahitaji yake mtu kama anavyohisi yeye mwenyewe. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameahidi kuwajibu wenye shida.

**Masharti ya anayesomewa: 1)** Inapendekezwa awe Mwislamu mwema. Kwa kadiri ya imani, ndivyo taathira inavyokuwa kubwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: ***"Na tunateremsha katika Qur'ani yale ambayo ni tiba na rehema kwa waumini. Na (Mwenyezi Mungu) hawazidishii madhalimu isipokuwa hasara tu"***. Sura Al-israa (17), aya 82. **2)** Kumwelekea Mwenyezi Mungu kwa ukweli ili amponye. **3)**Kutoona tiba inachelewa, kwa sababu, Ruq-ya ni maombi (dua). Muombaji akitaka kujibiwa haraka, anaweza asijibiwe. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Atajibiwa mmoja wenu madamu hafanyi haraka akisema: Nimeomba na sikujibiwa"***. Ameipokea Hadithi hii Bukhariy na Muslim.

**Ruq-ya ina njia nyingi: 1)** Kusoma Ruq-ya pamoja na kutabana (kutema cheche ndogo ndogo za mate). **2)** Kusoma bila ya kutabana. Kuweka mate katika kidole halafu kuyachanganya na mchanga na kuyapaka katika sehemu yenye maumivu. **3)** Kusoma Ruq-ya pamoja na kupapasa sehemu yenye maumivu.

## AYA NA HADITHI AMBAZO KWAZO MGONJWA HUFANYIWA RUQ-YA:

Suratul-fatiha , Ayatulkursiy :

﴿ ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلۡحَيُّ ٱلۡقَيُّومُۚ لَا تَأۡخُذُهُۥ سِنَةٞ وَلَا نَوۡمٞۚ لَّهُۥ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلۡأَرۡضِۗ مَن ذَا ٱلَّذِي يَشۡفَعُ عِندَهُۥٓ إِلَّا بِإِذۡنِهِۦۚ يَعۡلَمُ مَا بَيۡنَ
أَيۡدِيهِمۡ وَمَا خَلۡفَهُمۡۖ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيۡءٖ مِّنۡ عِلۡمِهِۦٓ إِلَّا بِمَا شَآءَۚ وَسِعَ كُرۡسِيُّهُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضَۖ وَلَا يَـُٔودُهُۥ حِفۡظُهُمَاۚ وَهُوَ ٱلۡعَلِيُّ ٱلۡعَظِيمُ ﴾

***Allahu laailaaha i-laahuwal hayyulqayyuum.Laataakhudhuhu sinatun walaa nauum. Lahuu mafias-maawati wamaafil-ardhi,mandhal-ladhii indahu i-laa biidhinihi, Yaalamu maabaina aidiihim wamaa khalfaham,walaa yuhiitwuuna bishai in min ilmihii il-laa bimaa shaa-a, wasia kur-siyyuhus-samaawati wal-ardhwa,walaa yauuduhu hifdhuhumaa wahuwal-aliyyul-adhwiim.***

﴿ ءَامَنَ ٱلرَّسُولُ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيۡهِ مِن رَّبِّهِۦ وَٱلۡمُؤۡمِنُونَۚ كُلٌّ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ لَا نُفَرِّقُ بَيۡنَ أَحَدٖ مِّن رُّسُلِهِۦۚ وَقَالُواْ
سَمِعۡنَا وَأَطَعۡنَاۖ غُفۡرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيۡكَ ٱلۡمَصِيرُ ٢٨٥ لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفۡسًا إِلَّا وُسۡعَهَاۚ لَهَا مَا كَسَبَتۡ وَعَلَيۡهَا مَا ٱكۡتَسَبَتۡۗ رَبَّنَا لَا
تُؤَاخِذۡنَآ إِن نَّسِينَآ أَوۡ أَخۡطَأۡنَاۚ رَبَّنَا وَلَا تَحۡمِلۡ عَلَيۡنَآ إِصۡرٗا كَمَا حَمَلۡتَهُۥ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِنَاۚ رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلۡنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا
بِهِۦۖ وَٱعۡفُ عَنَّا وَٱغۡفِرۡ لَنَا وَٱرۡحَمۡنَآۚ أَنتَ مَوۡلَىٰنَا فَٱنصُرۡنَا عَلَى ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡكَٰفِرِينَ ﴾

***Aamanarrasuulu bimaa unzila ilayhi min rabbihii walmuuminuuna,kl-lun aamana bil-laahi wamalaaikatihi wakutubihi warusulihi,laanufarriqu baina ahadin min rusulihi,waqaalu saamiina wa-atwaana,ghufuraanaka rabbana wailaikalmaswiiru. Laayukallifullahu nafsan i-laa wus-aha,lahaa maakasabat waalaihaa maktasabat, rabbana laatuaakhidhna in nasiinaa au akhtwaana,rabbana walaatuhammil-alainaa iswuran kamaa hamaltahuu alal-ladhiina minqablinaa,rabbana walatuhammilnaa maala twaaqata lanaa bihi,waafuannaa,waghafirlanaa,warhamnaa,anta maulaanaa fansurnaa alalqaumilkaafiriina.***

﴿ فَسَيَكۡفِيكَهُمُ ٱللَّهُۚ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ ﴾ ***Fasayakfiikahumullahu wahus-samiiul-aliimu.***

﴿ يَٰقَوۡمَنَآ أَجِيبُواْ دَاعِيَ ٱللَّهِ وَءَامِنُواْ بِهِۦ يَغۡفِرۡ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمۡ وَيُجِرۡكُم مِّنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ ﴾ ***Yaa qaumanaa ajiibuu daaiyallaahi wa-aaminuu bihii,yaghfirlakum mindhunuubikum,wayujirkum min adhaabin aliim.***

﴿ وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴾ ***Wanunazzilu minal-qur-aani maahuwa shifaaun warhmatun lil-muuminiina,walaa yaziidudh-dhwaalimiina il-laa khasaara.***

﴿ أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ﴾ ***Am yahsuduunan-naasa alaa maa-aataahumullaahu min fadhlihi.***

﴿ وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ ﴾ ***Waidhaa maridhtu fahuwa yashfiini.***

﴿ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ ﴾ ***Wayashfi suduura qaumin muuminiina.***

﴿ قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءٌ ﴾ ***Qul huwa li-ladhiina aamanuu hudan washifaau.***

﴿ لَوْ أَنْزَلْنَا هَٰذَا الْقُرْآنَ عَلَىٰ جَبَلٍ لَرَأَيْتَهُ خَاشِعًا مُتَصَدِّعًا مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ ﴾ ***Lau anzal-naa haadhalqur-aana alaa jabalin lara-aitahuu khaashian mutaswaddian min khashiatil-lahi.***

﴿ فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِنْ فُطُورٍ ﴾ Far-jiil-baswara haltaraa minfutuuri.

﴿ وَإِنْ يَكَادُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَيُزْلِقُونَكَ بِأَبْصَارِهِمْ لَمَّا سَمِعُوا الذِّكْرَ وَيَقُولُونَ إِنَّهُ لَمَجْنُونٌ ﴾ ***Wa in yakaadul-ladhiina kafaruu layuzliquunaka biabswaarihim,lammaa samiudh-dhikra wayaquuluuna innahuu lamajnuun.***

﴿ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ (١١٧) فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ (١١٨) فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ ﴾

***Wa auhaynaa alaa muusaa an-alqi aswaaqa,faidhaa hiya talqafu maa ya-afikuun.Fawaqaalhaqqu wabatwala maakaanuu yaamaluuna.Faghulibuu unaalika wanqalabuu swaaghiriina.***

﴿ قَالُوا يَا مُوسَىٰ إِمَّا أَنْ تُلْقِيَ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَىٰ (٦٥) قَالَ بَلْ أَلْقُوا فَإِذَا حِبَالُهُمْ وَعِصِيُّهُمْ يُخَيَّلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنَّهَا تَسْعَىٰ (٦٦) فَأَوْجَسَ فِي
نَفْسِهِ خِيفَةً مُوسَىٰ (٦٧) قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَىٰ (٦٨) وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴾

***Qaalu yaa muusaa immaa antulqiya waimmaa annakuuna awwala man-alqaa.Qaala bal-alquu,faidhaa hibaaluhum waiswiyyuhum yukhayyalu ilaihi minsihrihim annahaa tas-aa.Fa-aujasa fii nafsihii khiifatan muusaa.Qulnaa laatakhaf innaka antal-aalaa.wa-alqimaa fiiyamiinika talqafu maaswanauu,innamaa swanauu kaidu saahirin,walaa yuflihus-saahiru haithu ataa.***

﴿ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴾ ***Thumma anzalallahu sakiinatahuu alaa rasuulihiii waalalmu-uminiina.***

﴿ فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا ﴾ ***Fa anzalallahu sakiinatahu alayhi wa-ayyadahu bijunuudin lam tarauhaa.***

﴿ فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَىٰ ﴾ ***Faanzalallaahu sakiinatahu alaa rasuulihii waalal-muuminiina wa-alzamahum kalimatattaquwaa.***

﴿ لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴾ **Laqad** ***radhwiyallahu anil muuminiina idh yubaayiunaka tahtash-shajarati,faalima maa fiiquluubuhim fa-anzalas-sakiinata alayhim wa-athaabahum fat-han qariibaa.***

﴿ هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ السَّكِينَةَ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ لِيَزْدَادُوا إِيمَانًا مَعَ إِيمَانِهِمْ ﴾ ***Huwal-ladhi anzalas-sakiinata fii quluubul-muuminiina,liyazdaaduu iimaanan maa iimaanihim.***

**HADITHI:**

**أسأل الله العظيم رب العرش العظيم أن يشفيك** = ***As-alullahal-adhiim Rab-bal-arshil-adhiim an-yashfiyaka*** = Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa Arshi Tukufu akuponye. Atasoma hayo mara saba.

أعيذك بكلمات الله التامة من كل شيطان وهامة ومن كل عين لامة = ***U-iidhuka Bikalimaatil-lahit-taamma Min-kulli Shaitwaan Wa-haamma Wamin-kulli ainin Laamma*** = Ninakuombea kinga kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyo kamili akukinge na kila shetani na …….na kila jicho lenye lawama. Atasema hayo mara tatu.

اللهم رب الناس أذهب الباس، واشف أنت الشافي، لا شفاء إلا شفاؤك، شفاء لا يغادر سقما = ***Allahumma Rabban-nas Adh-hibilba's Washfi Antash-shaafii laa shifaa-an il-laa shifaa-uka, Shifaa-an Laa Yughaadiru Saqama*** = Ewe Mola wangu, Mola wa watu: Ondoa ubaya, na ponya. Wewe tu ndiye mponyaji. Hakuna uponyaji isipokuwa uponyaji wako tu. Ponya uponyaji usioacha ugonjwa. Atasoma hivyo mara tatu.

اللهم أذهب عنه حرها وبردها ووصبها ، حسبي الله لا إله إلا هو عليه توكلت وهو رب العرش العظيم = *Allahumma Adh-hib An-hu Harrahaa Wabardahaa Wawasbahaa. Hasbiyallahu Laa ilaaha illaa huu. Alaihi Tawakkaltu Wahuwa Rabbul-arshil-adhiim* = Ewe Mola wangu, muondoshee joto lake na baridi yake na…….Tosha yangu ni Mwenyezi Mungu tu. Hakuna anayestahiki kuabudiwa ila yeye tu, na yeye ni Mola wa Arshi Tukufu. Atasema hayo mara saba.

بسم الله أرقيك، من كل داء يؤذيك، ومن شر كل نفس أو عين حاسد، الله يشفيك بسم الله أرقيك = ***Bismi Llaahi arqiika minkulli daai yu-udhiika, waminsharri kulli nafsi au ayn haasidi, allahu yashfiika Bismi Llaahi arqiika***.

Unaweka mkono wako juu ya sehemu yenye maumivu na kusema: **a)** بسم الله *Bismi Llaahi*. mara tatu. **b)** أعوذ بعزة الله وقدرته من شر ما أجد وأحاذر ***Auudhu biizzati llahi waqudratihi minsharri maa ajidu wa-uhaadhir***. mara saba.

**ANGALIZO:**

1. Haifai kuamini uzushi katika masuala yanayohusu kukabiliana na mtu mwenye kijicho, kama kunywa mkojo wake na kwamba taathiri yake haina manufaa kama atajua.
2. Haifai kuweka hirizi za ngozi, vikuku (bangili) na vidani juu ya kitu ambacho mtu anahofia kupatwa na kijicho. Mtume, (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: ***"Mwenye kutundika kitu, huegemezwa kwenye kitu hicho".*** Tirmidhiy. Ikiwa vitu hivyo vinatokana na Qur'ani, kuna tofauti (baina ya wanazuoni), na kuacha ni bora zaidi.
3. Haifai kuandika "ما شاء الله", ***maashaa-allaah***"بارك الله" ***baarakallahu*** au kuchora upanga au kisu au kuchora jicho au kuweka Qur'ani katika gari au kutundika baadhi ya aya (za Qur'ani) katika nyumba. Mambo yote hayo, hayaondoi kijicho. Wakati mwingine, yanaweza kuwa ni miongoni mwa hirizi haramu.
4. Ni wajibu kwa mgonjwa kuamini kuwa atajibiwa, na asione kuwa anachelewa kupona. Lau kama mgonjwa ataambiwa kuwa tiba ya dawa za kisasa zinatakiwa kutumika maisha, haoni huzuni. Lakini Ruqya ikimchukua muda mrefu, anakereka, pamoja na kuwa kila herufi anayoisoma ni jambo zuri. Jambo zuri moja ni kwa mazuri kumi mfano wake. Ni wajibu kwa mgonjwa kuomba dua, kuomba msamaha na kutoa sadaka sana, kwani hayo ni miongoni mwa mambo yanayotakiwa kujitibu kwayo.
5. Kisomo cha kikundi kinapingana na Sunna (mafundisho ya Mtume), (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) na taathira yake ni dhaifu. Aidha kutosheka na kinasia sauti (kama Radio Kaseti) katika *Ruq-ya* ni kinyume na Sunna, kwa sababu nia haipatikani katika chombo hicho, na nia ni sharti kwa anayesoma *Ruq-ya*, japokuwa katika kukisikiliza chombo hicho kuna kheri. Ama kurudia rudia aya za *Ruq-ya* na kuomba dua kwa idadi maalum bila ya hoja, si jambo sahihi.

6 Kuna baadhi ya alama ambazo zinaweza kuchukuliwa kuwa ni dalili; ama zote au baadhi yake; kwamba msomaji *Ruq-ya* huyu anatumia uchawi na sio Qur'ani. Yasikuhadae mambo ya dini. Anaweza kuanza kisomo chake kwa Qur'ani na mara hubadilisha. Anaweza kuwa ni miongoni mwa watu wanaoingia sana misikitini kwa kuwalaghai watu. Inawezekana ukamuona anamtaja sana Mwenyezi Mungu mbele yako. Hilo lisikuhadae. Zinduka!

**Baadhi ya alama za wachawi na wanajimu:** ✸ Kumuuliza mgonjwa jina lake au jina la mama yake. Kujua jina au kutolijua hakubadilishi chochote katika tiba. ✸ Kumtaka mgonjwa alete kitu katika mavazi yake, kama kanzu au fulana. ✸ Anaweza, mara nyigine, kumtaka mgonjwa alete mnyama mwenye wasifu maalum ili awachinjie Majini. Anaweza kumpaka mgonjwa damu ya mnyama huyo. ✸ Kuandika au kusoma Talasimu zisizofahamika na zisizokuwa na maana. ✸ Kumpa mgonjwa karatasi ambayo ndani yake mna michoro ya pembe nne na ambayo ndani yake mna herufi na tarakimu na huitwa Hijabu (kinga/hirizi). ✸ Kumuamuru mgonjwa ajitenge (asionane) na watu kwa muda fulani katika chumba chenye giza na jambo hilo huitwa Hujba (kutiwa junguni). ✸ Kumwamuru mgonjwa asiguse maji katika muda maalum. ✸ Kumpa mgonjwa kitu akizike ardhini au karatasi aichome moto na kujifukiza kwayo. ✸ Kumwambia mgonjwa baadhi taarifa zake binafsi ambazo hakuna yeyote anayezijua au jina lake na mji wake na ugonjwa wake kabla mgonjwa mwenyewe hajasema. ✸ Kuichambua hali ya mgonjwa kwa kuingia tu au kwa simu au kwa barua.

7 Madhehebu ya Watu wa Sunna ni kwamba Majini wanaweza kumuingia mwanadamu. Hoja ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo kwamba: ***"Ambao wanakula riba hawasimami ila tu kama anavyosimama yule ambaye anapelekeshwa na shetani kutokana na kushikwa na Jini".*** Sura Albaqara (2), aya 275. Wafasiri wamekubaliana kwamba maana ya kushikwa katika aya hii ni wazimu wa kishetani unaomzukia mtu kwa sababu ya kuingiwa na Jini.

**HITIMISHO**: **UCHAWI:** Uchawi upo, na kuathiri kwake kumethibiti kwa Qur'ani na Sunna. Uchawi ni haramu na ni dhambi kubwa, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: ***"Yaepukeni mambo saba yaangamizayo. (Swahaba) Waliuliza:Na ni yapi mambo hayo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Alisema: Kumshirikisha Mwenyezi Mungu na uchawi.......".*** Bukhariy, Muslim. Pia uchawi ni haramu kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: ***"Na kwa yakini, walijua kuwa mwenye kuuchagua (uchawi) hana fungu lolote Akhera".*** Sura Albaqara (2), aya 102. Uchawi uko katika mafungu mawili: **1)** Mafundo na visomo ambavyo vinamfikisha mchawi kwenye kuwatumia mashetani katika yale ambayo kwayo anakusudia kumdhuru anayerogwa. **2)** Dawa zinazosababisha taathira katika mwili wa anayerogwa, akili yake, utashi wake na mwelekeo wake. Kwa hiyo, aliyerogwa anaweza kupitiwa akilini kwamba jambo hili limebadilika au kitu hiki kinatembea na mfano wa hayo. Aina ya kwanza ya uchawi kuifanya ni kushirikisha, kwa sababu mashetani hamhudumii mchawi mpaka amkufuru Mungu. Ama aina ya pili ni jambo linalo angamiza na ni katika madhambi makubwa sana. Yote hayo, yanatokea kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

# DUA

Viumbe wote wanamhitaji Mwenyezi Mungu na vilivyopo kwake, naye hawahitaji viumbe na hana shida nao. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajibisha kwa waja wake kuomba. Amesema: *"Niombeni nikujibuni. Kwa yakini, wale wanaotakabari wakaacha kuniabudu (kuniomba) wataingia Jahanamu wakiwa dhalili"*. Sura Al-muumin (40), aya 60. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) naye amesema kuwa: *"Yeyote asiyemuomba Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humkasirikia"*. Ibnimaaja. Pamoja na haya, Mwenyezi Mungu hufurahi kwa waja wake kumuomba, huwapenda wanaosisitiza maombi yao kwake na huwafanya wawe karibu naye. Swahaba wa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu awafikishie rehema na amani, walilitambua jambo hili na hivyo: **1)**Hakuna yeyote kati yao aliyedharau jambo analomuomba Mwenyezi Mungu. **2)**Hakuna yeyote aliyepeleka maombi yake kwa kiumbe yeyote wa Mwenyezi Mungu. Hayo si kwa jingine isipokuwa tu kwa sababu ya kufungamana kwao na Mwenyezi Mungu, ukaribu wao kwake na ukaribu wake kwao, ikiwa ni kuitekeleza kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: *"Na waja wangu watakapokuuliza kuhusu mimi, kwa yakini mimi niko karibu"*. Sura Albaqara (2), aya 186.

Dua ina nafasi kubwa kwa Mwenyezi Mungu, kwani ni jambo adhimu sana kwake, na inaweza kurudisha hukumu. Mwenyezi Mungu anamjibu kila anayemuomba, iwapo zitapatikana sababu na kutokuwepo vizuizi. Muombaji anapewa mojawapo ya mambo aliyoyataja Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwa kauli yake kuwa: *"Hakuna Mwislamu yeyote anayeomba dua ambayo haina dhambi wala kukata udugu isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu, kwa dua hiyo, atampa mojawapo ya mambo matatu: Ama* **1)** *Kujibiwa haraka maombi yake na ama* **2)** *Mwenyezi Mungu kumwekea akiba maombi hayo Akhera na ama* **3)** *Kumuondolea katika mambo mabaya mfano wa maombi yake. Swahaba wakasema: Kwa hiyo, tutaomba sana. Mtume* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *akasema: Mwenyezi Mungu ni mwingi sana"*. Ahmad.

**AINA ZA DUA:** Ni aina mbili: **1) Dua ya ibada,** kama sala na saumu. **2) Dua ya maombi.**

**KUZIDIANA KWA AMALI:** Je, kusoma Qur'ani ni bora zaidi au *dhikiri* (kumtaja Mwenyezi Mungu) au dua? Kusoma Qur'ani ni amali bora sana, halafu dhikiri na kumsifu Mwenyezi Mungu, halafu dua na kuomba. Hii ni kwa jumla. Lakini inaweza ikaitokea amali iliyozidiwa jambo linaloifanya iwe bora zaidi kuliko ile iliyoizidi. Dua siku ya Arafa ni amali bora zaidi kuliko kusoma Qur'ani. Kusoma nyiradi zilizothibiti kunukuliwa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) baada ya sala za faradhi ni bora zaidi kuliko kusoma Qur'ani.

**SABABU ZA DUA KUKUBALIWA:** Kuna sababu za dhahiri na sababu za ndani:

**1) Sababu za dhahiri: 1.** Kutanguliza kufanya mambo mema, kama sadaka, udhu, sala na kufunga. **2.** Kuelekea Qiblah. **3.** Kunyanyua mikono. **4.** Kumsifu Mwenyezi Mungu kwa sifa anazostahiki. **5.** Kutumia majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake zinazohusiana na jambo linaloombwa. Dua ikiwa ni ya kuomba pepo, atanyenyekea kwa fadhila na rehema za Mwenyezi Mungu. Ikiwa atamuapiza dhalimu, hatatumia sifa za Rahman (Mwenye rehema) au Karim (mkarimu), bali atatumia majina ya Jabbar (Mwenye nguvu kubwa), Kahari (Asiyeshindwa), Al-aziz (Mwenye ezi). **6.** Kumsalia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani,

mwanzo wa dua, katikati yake na mwisho wake. **7.** Kuungama dhambi. **8.** Kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake. **9.** Kuomba na kujibidiisha kutumia dua zinazokusanya mambo mengi. **10.** Kutumia fursa za nyakati bora ambazo umekuja ushahidi kwamba nyakati hizo ni matarajio ya dua kujibiwa. Nyakati hizo ni nyingi. Miongoni mwa hizo ni hizi: ✸ **KATIKA SIKU:** Theluthi ya mwisho ya usiku, wakati Mwenyezi Mungu Mtukufu anaposhuka mpaka mbingu ya karibu, wakati uliopo baina ya Adhana na Iqama, baada ya kutawadha, katika kusujudu, kabla ya kutoa salamu ya kumalizia sala, baada ya sala za faradhi, wakati wa kuhitimisha kusoma Qur'ani, wakati wa mlio wa jogoo, safarini, dua ya mtu aliyedhulumiwa, dua ya aliye katika matatizo, dua ya mzazi kwa mtoto wake, dua ya Mwislamu kwa ndugu yake Mwislamu aliye mbali naye na wakati wa kukabiliana na adui vitani. ✸**KATIKA WIKI:** Siku ya Ijumaa, na hasa saa ya mwisho (ya siku hiyo). ✸**KATIKA MIEZI:** Mwezi wa Ramadhani, wakati wa kufuturu, Lailatul-qadr na usiku wa manane. ✸**KATIKA SEHEMU TUKUFU:** Misikiti kwa jumla, mbele ya Alkaaba na hasa mbele ya Multazam na mbele ya Maqaam Ibrahim, juu ya (kilima) Swafaa na (kilima) Marwa, Arafa, Muzdalifa na Mina katika siku za Hija, wakati wa kunywa maji ya Zamzam.

**2) Sababu za ndani: 1.** Kabla ya maombi: Kutanguliza toba ya kweli na kurudisha vitu vya dhulma. **2.** Chakula, vinywaji, mavazi na makazi yawe yanatokana na kipato halali. **3.** Kufanya sana ibada. **4.** Kujiepusha na mambo ya haramu. **5.**Kujitenga na mambo ya tuhuma na ya anasa. Wakati wa maombi: Moyo kuwa makini, kuwa na imani na Mwenyezi Mungu (kwamba atajibu maombi), kuwa na matarajio na marejeo yenye nguvu kwa Mwenyezi Mungu, kunyenyekea, kubembeleza, kuyaegemeza mambo yote kwa Mwenyezi Mungu na kutomtaraji asiyekuwa yeye na kuwa na uhakika wa kujibiwa.

**VIZUIZI VYA DUA KUKUBALIWA:** Mtu anaweza kuomba na asijibiwe au majibu yakachelewa. Sababu ni nyingi. Miongoni mwa sababu hizo, ni hizi:✸ Kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu pamoja na Mwenyezi Mungu.✸ Ufafanuzi katika dua; kama kuomba kinga ya joto la Jahanamu na mbano wake na giza lake, pamoja na kuwa ilikuwa inatosha katika dua hii kuomba kinga ya moto tu. ✸ Mwislamu kujiombea mwenyewe au kumuombea mtu mwengine dua mbaya kwa dhulma ✸ Kuomba dhambi na kukata udugu.✸ Kuiwekea dua sharti la utashi, kama kusema: Ewe Mola wangu, nisamehe ukitaka.✸ Kutaka kujibiwa haraka, pale mtu anaposema: Nimeomba na sijajibiwa.✸Kukata tamaa; kwa maana ya kuacha kuomba dua kwa kuchoka au kukimwa.✸Kuomba dua kwa moyo ulioghafilika, usiojali.✸ Kutokuwa na adabu mbele ya Mwenyezi Mungu. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alimsikia mtu mmoja akiomba dua katika sala yake na hakumsalia Mtume. (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mtume alisema: *"Huyu amefanya haraka". Halafu alimwita na kumwambia yeye au mtu mwengine kwamba: "Mmoja wenu akiomba, aanze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu. Halafu amsalie Mtume. (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Halafu baada ya hapo, aombe anachotaka"*. Tirmidhiy.✸ Kuomba jambo lisilowezekana, kama kuomba kuishi milele duniani.✸Kuleta vina vya ushairi vya kulazimisha katika dua. Mwenyezi Mungu

Mtukufu amesema kuwa: *"Muombeni Mola wenu kwa kunyenyekea na kimyakimya (sauti ndogo). Kwa yakini, yeye hawapendi wanaopindukia mipaka"*. Sura Al-aaraaf (7), aya 55. Ibn-abbas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi yeye na mzazi wake, amesema kuwa: "*Angalia vina vya ushairi katika dua. Viepuke. Mimi sikumzoea Mtume* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *wa Mwenyezi Mungu na Swahaba wake isipokuwa kwamba walikuwa hawafanyi ila hilo (la kujiepusha na vina vya ushairi katika kuomba dua)*". Bukhariy. ✸Kupindukia mpaka katika kupaza sauti katika dua. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: *"Na usiyanyanyulie sauti ya juu maombi yako na usiyafiche. Na fuata baina ya hapo njia (ya wastani)"*. Sura Bani-israili (17), aya 110. Aisha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: "*Aya hii imeshushwa kuhusiana na dua*".

**Inapendekezwa kwa muombaji ayapangilie maombi yake kama ifuatavyo:** **KWANZA:** Kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifu. **PILI:** Kumsalia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. **TATU:** Kutubu na kuungama dhambi. **NNE:** Kumshukuru Mungu kwa neema zake. **TANO:** Kuingia katika maombi na kujibidiisha kutumia zile dua zinazokusanya mambo mengi na ambazo zimethibiti kunukuliwa kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezimmungu amfikishie rehema na amani, au kwa Wema Waliotangulia. **SITA:** Kuihitimisha dua kwa kumsalia Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu anfikishie rehema na amani.

**DUA MUHIMU AMBAZO INATAKIWA KUZIHIFADHI NA KUOMBA KWAZO:**

| MNASABA WA DUA | DUA: Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: |
|---|---|
| **Kabla na baada ya kulala na Akiamka atasema** | ***"Bismika allahumma ahyaa wa amuutu". "Al-hamdulillahi lladhiy ahyaanaa baada maa amaatanaa wa ilaihi nnushuur".*** |
| **Anayeshituka usingizini** | ***"Audhu bikalimaatil-laahi taammaati min ghadhwabihi wa min sharri ibaadihi wamin hamazaati shayaatwiin wa an- yah-dhuruun".*** |
| **Aliyelala akiota** | *"Aotapo mmoja wenu ndoto anayoipenda, ndoto hiyo inatokana na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, amshukuru Mungu na aisimulie ndoto hiyo. Akiota jambo asilolipenda kinyume cha ndoto hiyo (ya awali), ndoto hiyo inatokana na shetani. Aombe kinga ya shari yake na asimsimulie yeyote, kwani ndoto hiyo haitamdhuru".* |
| **Kutoka nyumbani** | ***"Allahhumma inniy audhubika an adhwilla au udhwal-la au azil-la au uzal-la au adhwlim au udhwlama au aj'hala au yuj'hala alayya" "Bisimillahi tawakkaltu alaa-llah laa haula walaa quwwata il-laa bil-laah".*** |
| **Kuingia msikitini** | Mtu akiingia msikitini, atatanguliza mguu wake wa kulia na kusema: ***"Bisimil-lahi was-salamu alaa rasuli l-laahi allahumma igh'firliy dhunuubiy waf'tah liy ab-waaba rahmatik".*** |
| **Kutoka nsikitini** | Mtu akitoka msikitinim, atatanguliza mguu wake wa kushoto na kusema: ***"Bisimillahi wassalamu alaa rasuli l-lahi allahumma ighfirliy dhunubiy waf'tah liy ab-waaba fadh-lik".*** |
| **Muoaji/muole waji mpya** | "Baaraka llahu laka wabaaraka alaika wajama'a bainakumaa fii khayr". |
| **Anayesikia mlio wa jogoo au punda** | *"Mtakaposikia mlio wa punda, ombeni hifadhi kwa Mwenyezi Mungu akukingeni na shetani, kwa kuwa yeye ameona shetani. Na msikiapo mlio wa jogoo, muombeni Mwenyezi Mungu katika fadhila zake, kwakuwa yeye ameona Malaika". "Msikiapo kubweka kwa mbwa na mlio wa punda usiku, ombeni kinga kwa Mwenyezi Mungu".* |

| | |
|---|---|
| **Aliyekujulisha kuwa anakupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu** | Imepokewa kutoka kwa Anas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba *"Mtu mmoja alikuwa kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na akapita mtu. Yule mtu (aliyekuwa kwa Mtume) akasema: Mimi kwa yakini ninampenda huyu (mtu apitaye). Mtume akamwambia: Je, umemfahamisha? Akasema: Hapana. Mtume akamwambia: Mfahamishe. Yule mtu akamfuata na kumwambia: Kwa yakini, mimi nakupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Akasema: Akupende Mwenyezi Mungu ambaye umenipenda kwa ajili yake".* |
| **Akipiga chafya ndugu yako Mwislamu** | *"Apigapo chafya mmoja wenu, aseme: (**alhamdullahi**), na ndugu yake au swahiba wake amwambie: (**yar'hamka llah**) Akiambiwa (**yar'hamka llah**), yeye aseme*: (***yahhadykum llahu wa yuswl'hu baalakum***)". Kafiri akipiga chafya na akasema: (al hamdulillahi)mwambie: (yahdiikum llah), na usimwambie: (yar'hamuka llah). |
| **Dua ya matatizo** | "Laa ilaha il-la llahul-adhwiimul-halymu, laa ilaha il-la llahu rabbul arshil adhwim,laa ilaha il-la-llahu rabbu-ssamaawaati wa rabbul-ardhwi wa rabbul-arshil-kariim.". "Allahu rabbiy laa ush'riku bihi shay-an". "Yaa hayyu yaa qayyuum, birahmatika as'taghiith". "Subhaana llahil adhwiim" |
| **Kuwaapiza maadui** | ***"Allahumma mujriyas-sahaab, mun'zilal kitaab, sariial–hisab, Ih'zimil-ahzaab, allahumma Ihzimhum wa zalzilhum".*** |
| **Mambo yawapo magumu** | ***Allahumma laa sahla il-laa maa jaaltahuu sahalan,wa anta taj'alul – hazana idhaa shi'ta sahalaa.*** |
| **Dua ya kulipa deni** | Allahumma inniy audhubika minalhhami,wal hazani,wal ajizi wal-kasal,wal-jubni,wal-bukhul,wadhwalau ddayin waghalabati rrijaal. |
| **Chooni** | Mtu akiingia chooni, aseme: (**allahumma iny audhubika minal khubuthi wal khabaaithi**)na akitoka chooni, aseme: (**ghufuraanaka**) |
| **Wasiwasi wa sala** | "Huyo ni shetani anayeitwa "Khanzab". Ukimhisi, muombe hifadhi Mwenyezi Mungu akukinge naye na tabana kushotoni kwako mara tatu" |
| **Katika kusujudu** | Allahumma igh'firiliy dhambiy kulahu,diqqahuu wajil-lahu,wa awwalahuu wa aakh'rahu,wa alaaniyyatahu wasirrahu<br>Subhaanaka rabbiy wabihamdika allahhumma igh'firiliy<br>Allahumma audhu biridhwaaka min sakhatwika wabimuâafaatika min uquubaatika wa auhubika min'ka laa uhswii thaanaa-an alayka an'ta kamaa ath'nayta alaa nafsika |
| **Sijda ya kusoma** | Allahumma laka sajad'tu wabika aaman'tu,walaka as'lamtu,sajada wajihiy lil-ladhii khalaqahu waswwarahu,washaqqa sam'âhu wabaswarahuu tabaaraka llahu ahasanul-khaaliqiina. |
| **Kuanza sala** | Allahumma baaid bainiy wabaina khatwaayaaya kama baâd'ta bainal-mashriki wal-maghrib,Allahumma naqqiniy min khatwayaaya kamaa yunaqqaa thaubul-ab'yadhwa mina ddanasi allahumma igh'silniy bil maa-I wathal'ji walbaradi |
| **Mwisho wa sala** | Allahumma innii dhwalamtu nafsiy dhulman kathiiran walaa yaghafiru dhunuuba il-laa an'ta faghafiriliy maghafiratan min indika war'hamniy innaka an'tal ghafuurur-rahiim. |
| **Baada ya sala** | Allahumma ainiy alaa dhikirika washukurika wahusuni ibaadatika<br>Allahumma inniy audhubika minal kufuri wal faq'ri wa adhabil qabri |
| **Aliyefanya jema** | *"Aliyetendewa jambo jema na akamwambia aliyemtendea: {**Jazaakallahu khairan**} Mwenyezi Mungu akulipe kheri, hakika amefikia kiwango cha juu katika kushukuru. Aliyeshukuriwa ajibu kwa kusema: Nawe Mungu akulipe, au: Na wewe pia.* |
| **Mtu aonapo** | {**Allaahumma swayyiban naafian**}mara mbili au tatu. "Tumepata mvua kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema zake". Mtu aombe dua atakayo, kwani |

| | |
|---|---|
| **mvua** | dua ni zenye kukubaliwa wakati wa kunyesha kwa mvua. |
| **Upepo ukivuma** | **“***Ewe Mola wangu, mimi ninakuomba kheri yake na kheri ya vilivyomo ndani yake na kheri ya yale ambayo upepo huo umetumwa kwayo. Na ninakuomba unikinge na shari yake na shari ya vilivyomo ndani yake na shari ya yale ambayo umetumwa kwayo”.* |
| **Mtu auonapo mwezi mwandamo** | *“Ewe Mola wangu, uandamishe kwetu kwa baraka na imani na salama na Uislamu. Mwezi wa kheri na uongofu. Mola wangu na Mola wako ni Mwenyezi Mungu”* |
| **Mtu anayemuaga msafiri** | *“Namuomba Mwenyezi Mungu hifadhi ya dini yako na uaminifu wako na hatima ya amali zako***”.** *Msafir naye atamjibu kwa kusema: “Namuomba Mwenyezi Mungu ambaye amana zake hazipotei akuhifadhi***”.** |
| **Dua ya Msafiri** | Allahu ak'bar, allahu ak'bar (subhaana lladhiy sakhara lanaa hadhaa wamaa kunnaa lahu muq'riniina, wa innaa ilaa rabbina lamuniqalibuuna) allahuma innaa nas'aluka fii safarinaa haadhaa al birra wattaquwaa waminal amali maatar'dhwaa,allahumma hawwin alainaa safaranaa haadhaa watwuwi anaa buu'dahu,allahumma anta sswaahibu fis-safari wal khalifatu fil-ahali,allahumma inniy audhubika min waâthaa-issafari, wakaabatil man'dhwari, wasuu-il mun'qalabi filmaali wal ahali<br>**Akirudi safari atayasema hayo na kuongezea:** Aayibuuna taaibuuna Aabiduuna lirabbinaa haamiduna. |
| **Dua ya kulala** | Allahumma inniy as'lamtu nafsiy ilaika wafawadhtu amriy ilaika, wa al-ja'tu dhwahariy ilaika, rahabatan waraghabatan ilaika, laa mal'jaa walaa man'jaa minka il-laa ilaika, Aaman'tu bikitaabika alladhiy an'zalita, wabinabiyyikal-ladhiy ar'salta .<br>Al-hamdulillahi ladhiy atwaamana, wasaqaanaa,wakafaanaa, wa aawaanaa, fakam minman laa kaafiya lahu walaa ma'waa.<br>Allahumma qiniy adhaabaka yauma tub'athu ibaadaka<br>Subhannaka allahumma rabbiy ,bika wadhwa'tu jan'biy wabika ar'fauhu, in am'sak'ta nafsiy faghaf'rilahaa,wa in ar'saltaha fah'fadhuhaa bimaa tahafadhu bihi ibaadaka swaalihiina.<br>**“**(Mtume alikuwa) Akitabana mikononi mwake na kusoma sura mbili za kinga (sura Alfalaq na sura An-nas) na kujipangusa mwili kwa mikono hiyo”**.** **“**(Mtume alikuwa) Halali kila usiku mpaka asome (sura) Alif Laam Miim (Assajda) na Tabaaraka (Almulk)”**.** |
| **Kutoka kwa ajili ya kwenda kusali** | Allahummaj-al fii qalbiy nuuran,wa fii lisaaniy nuuran,wafiisam'I nuuran wafii baswariy nuran, wamin fauqii nuuran, wa ani yaminiiy nuuran wa an shimaliy nuuran, wamin amaamiy nuuran,wamin khalfiy nuuran,waj'al fii nafsiy nuuran, wa aadhwim liy nuuran wa adh-dhwim liy nuuran waj'al liy nuuran,waj'aliny nuuran,allahumma aatwiniy nuuran,waj'al fi aswabiy nuuran wafilahamiy nuuran wa adhwim liy nuuran wafidamiy nuuran wafisahaariy nuuran,wafi bashari nuuran |

| | |
|---|---|
| **DUA YA KUOMBA KHERI** | **"Mmoja wenu akusudiapo kufanya jambo, aswali rakaa mbili zisizokuwa za faradhi halafu aseme:** *Allahumma inniy astakhiiruka bi-ilmika, wa-astaqdiruka biqudratika, wa-as'aluka min fadhwilika, fa-innaka taq'dir walaa aq'dir, watalam walaa aalam, wa an'ta âllamul-ghyuub. Allahumma inkun'ta taalam anna haddhal-amra( kisha anaitaja haja yake) khayiral-liy fiidiiniy wamaashiy wa aaqibati amriiy au Aajilihii wa Aajilihii faq'durhu liiy wayassirhu liiy, thumma baarik-liy fiihi,wa in kun'ta taalam anna hadhal-amra sharrul-liy fiiy diiniy wamaashiy waaqibati amriy –au qaala fi Ăajil wa Aajilihi faswrifhu anniy waswrifniy an'hu waq'durhu liy al khayira haythu kana thumma radhwiniy bihi.*<br>Ewe Mola wangu nakuomba kheri kwa ujuzi wako na nakuomba uwezo kwa uwezeshaji wako na ninakuomba katika fadhila zako, kwani wewe unaweza, nami siwezi. Nawe unajua, nami sijui na wewe ni Mjuzi sana wa yaliyofichikana. Ewe mola wangu, ikiwa unalijua jambo hili (na ataliainisha kwa kulitaja) kuwa ni kheri kwangu katika hali yangu ya sasa na ya baadae (au alisema: Katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa hali yangu) likadirie kwangu na lifanye liwe jepesi kwangu halafu nibarikie katika jambo hilo. Ewe Mola wangu, na ikiwa unajua kwamba jambo hilo ni baya kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa hali yangu, niepushe nalo na nikadirie kheri popote ilipo halafu niridhishe nayo**"**. |
| **Dua zinazojumuisha mambo mengi alizoziomba Mtume(s.a.w)** | Allahumma inniy audhu bika min suu-il qadhwaa-i, wamin daraki sha-shaqaa-i' wamin shamatati al aadaai wamin kuli jahadil balaa-i<br>Allahumma igh'firiliy khatwiiatiy,wajahaliy,wais'raafiy fii-amriy,wamaa an'ta aalam bihi minniy, allahumma ighfiriliy jiddiy wa haz'liy,wakhatwa'iy,wa amdiy,wakul-lu dhaalika indiy,allahumma ighifiriy maa qaddamtu wa maa akhartu wamaa as'rar'tu,wamaa aalan'tu,wamaa an'ta aalam bihi minniy an'tal muqadim wa an'tal muakh'r,wa an'ta alaa kul shayi-ini qadiir.<br>Allahumma asw'lih liy diiniy alladhiy huwa isumatu, wa asw'lihu liy duniyaya allatiy fiiha maashiy,wa aswil'h liy aakhiratiy allatiy fiha maadiy waj'al hayata ziyadata liy fi kul khayiri waj'al-maiti rahataliy min kul sharri<br>Allahumma inniy as'alukal-hudaa,watuqaa wal-afafu<br>Allahumma Aati nafsiy taquwaaha, wazakiha an'ta khayiru man zakkaha an'ta waliyyuhaa wamaulahaa,allahumma inniy audhubika min ilim laa yan'faa,wamin qalib laa yakhashaâ, wamin nafsi laa tash'baâ wamin daawati laa yus'tajaba lahaa<br>Allahumma inniy audhubika min zawali niimatika watahawwuli aafiyatika wafajaati niqimatika wajamiiâ sakhatwika. |

# BIASHARA YENYE FAIDA

Mwenyezi Mungu amemfanya mwanadamu kuwa bora kuliko viumbe wengine na kumhusisha yeye tu kwa neema ya kuzungumza. Mwenyezi Mungu pia ameufanya ulimi kuwa nyenzo ya kuzungumza. Ulimi ni neema itumikayo katika kheri na katika shari. Anayeutumia ulimi kwa kheri, utamfikisha kwenye wema wa duniani na daraja za juu peponi. Atakayeutumia ulimi katika mambo yasiyokuwa hayo, utamuingiza katika maangamizi ya duniani na akhera. Jambo bora zaidi ambalo wakati unatumika kwalo baada ya kusoma Qur'ani, ni kumtaja Mwenyezi Mungu.

**UMUHIMU WA KUMTAJA MWENYEZI MUNGU:** Zimekuja Hadithi nyingi katika kulihimiza hilo. Miongoni mwa Hadithi hizo ni hizi: **1)** Kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: "*Je, nikufahamisheni bora zaidi ya amali zenu na safi zaidi kwa Mfalme wenu na ya juu zaidi katika daraja zenu na bora zaidi kwenu kuliko kutoa dhahabu na fedha na bora zaidi kwenu kukabiliana na maadui wenu mkawaua nao wakakuueni? (Swahaba) Walisema: Tuambie, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. (Mtume)* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *Alisema: Ni kumtaja Mwenyezi Mungu*". Tirmidhiy. **2)** Kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: *"Mfano wa ambaye anamtaja Mola wake na ambaye hamtaji Mola wake ni mfano wa aliye hai na maiti"*. Bukhariy, Muslim. **3)** Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Hadithi Qudsiy isemayo kuwa: "*Mimi niko pale ilipo dhana ya mja wangu kwangu, na mimi niko pamoja naye pale anitajapo. Akinitaja nafsini mwake, nami namtaja nafsini mwangu. Na akinitaja katika kundi, nami namtaja katika kundi bora zaidi kuliko wao. Na akijikurubisha kwangu kwa shubiri, nami najikurubisha kwake kwa pima"*. Bukhariy. **4)** Kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: "*Wametangulia Mufarradun. (Swahaba) Waliuliza: Ni akina nani Mufarradu ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? (Mtume)* (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) *Alisema: Ni wanaume na wanawake wanaomtaja sana Mwenyezi Mungu*". Muslim. **5)** Kauli ya Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akimuusia Swahaba wake mmoja na kumwambia: "*Ulimi wako usiache kuwa maji maji kutokana na kumtaja Mwenyezi Mungu"*. Tirmidhiy.

**KURUDUFISHWA KWA MALIPO:** Malipo ya matendo mema yanarudufishwa kama yanavyorudufishwa malipo ya kusoma Qur,ani. Hayo ni kwa kuzingatia mambo mawili: **1)** Kiwango cha imani, *ikhlas* (utakaso), kumpenda Mwenyezi Mungu na viambata vyake katika moyo. **2)** Kiwango cha moyo unavyotafakari utajo wa Mwenyezi Mungu na unavyoshughulika na utajo huo. Kumtaja Mwenyezi Mungu isiwe kwa ulimi tu. Yakikamilika hayo, Mwenyezi Mungu humfutia mtu makosa yake yote na kumpa malipo yake kamili. Upungufu wa malipo ni kwa mujibu wa kiwango cha utajo.

**FAIDA ZA KUMTAJA MWENYEZI MUNGU:** Sheikhul-islam amesema kuwa: "Utajo (wa Mwenyezi Mungu) kwa moyo ni kama maji kwa samaki. Inakuwaje hali ya samaki akitoka majini?"

- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunarithisha kumpenda Mwenyezi Mungu, kuwa karibu naye, kupata radhi zake, kumuogopa, kurejea kwake na kunasaidia kumtii.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunaondoa kero na jekejeke moyoni, kunaleta furaha na kunaupa moyo uhai, nguvu na usafi.
- Katika moyo kuna mahitaji ambayo hakuna kinachoweza kuyakidhi isipokuwa kumtaja Mwenyezi Mungu tu. Pia katika moyo kuna ugumu ambao hakuna kinachoweza kuulainisha isipokuwa kumtaja Mwenyezi Mungu tu.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu ni tiba ya moyo, dawa ya moyo, nguvu ya moyo na ni ladha ya utamu wake ladha ambayo hailingani na ladha yoyote nyingine. Mghafala ni maradhi ya moyo.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kwa uchache ni dalili ya unafiki. Kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi ni dalili ya nguvu ya imani na ukweli wa kumpenda Mwenyezi Mungu, kwa sababu anayekipenda kitu hukitaja sana.
- Mja anapojitambulisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kumtaja katika raha, Mwenyezi Mungu naye humtambua mja huyo katika shida, na hasa wakati wa kifo na vitangulizi vyake.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu ni sababu ya kumuokoa mtu na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Pia ni sababu ya kushushwa kwa utulivu, kumiminika kwa rehema na maombi ya Malaika.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunaufanya ulimi uache kujishughulisha na upuuzi, kusengenya, fitina, uongo na mambo mengine haramu na ya karaha.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu ni ibada rahisi sana, ni bora sana, ni tukufu sana na ni zao la peponi.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunamvalisha mtajaji vazi la haiba, utanashati na uso kunawiri. Kumtaja Mwenyezi Mungu ni nuru duniani, kaburini na akhera.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunawajibisha rehema ya Mwenyezi Mungu na maombi mema ya Malaika kwa mtajaji. Mwenyezi Mungu anajifaharisha mbele ya Malaika wake kwa wanaomtaja.
- Watu bora zaidi wa kila amali ni wale ambao katika amali hiyo wanamtaja sana Mwenyezi Mungu. Wafungaji bora zaidi ni wale wanaomtaja sana Mwenyezi Mungu katika saumu yao.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunayafanya mambo magumu na mazito kuwa mepesi, kunapunguza mashaka, kunavuta riziki na kuupa nguvu mwili.
- Kumtaja Mwenyezi Mungu kunamfukuza shetani, kunamfedhehesha na kumdhalilisha.

# NYIRADI ZA KILA SIKU, ASUBUHI NA JIONI

| Na. | URADI WA SIKU (WA KUSEMA) | WAKATI NA IDADI | ATHARI NA UMUHIMU WAKE |
|---|---|---|---|
| 1 | Ayatul Kursiyyu[1] | Asubuhi na jioni, kabla ya kulala na baada ya sala za faradhi | Mtu hatasogelewa na shetani na ni sababu ya kuingia peponi |
| 2 | Aya mbili za mwisho za sura Albaqarah [2] | Mara moja usiku, na pia huso,wa nyumbani wakati wowote | Zinakinga shari ya kila kitu |
| 3 | Sura Ikhlas, Falaq, Annas | Mara 3 asubuhi na mara 3 jioni | Zinamkinga mtu na kila kitu |
| 4 | Bismillaahil- ladhiy laa yadhuru maâ ismihi shay-un fil ardhi walaa fissamaa-i wa hhuwas-ssamiiul- alym. | Mara 3 asubuhi na mara 3 jioni | Halitampata mtu balaa kwa ghafla na hakiwezi kumdhuru kitu chochote |
| 5 | Audhu bikalimatil-laahit-taammati min-sharri maa khalaq | Mara 3 asubuhi na jioni, na mtu akifika sehemu | Ni kinga ya sehemu dhidi ya kila madhara |
| 6 | Hasbiyal-laau, laa ilaaha illa Huwa, alaihi tawakkaltu wa Huwa rabbul-arshil adhwiim**.** | Mara 7 asubuhi na mara 7 jioni | Mwenyezi Mungu atamtosheleza na mambo ya dunia na ya akhera yanayomkera |
| 7 | Radhwiitu billahi rabban, wabil-islaami diinaan, wabi Muhammadin swallallaahu alaihi wasallama nabiyyan. | Mara 3 asubuhi na mara 3 jioni | Ni haki kwa Mwenyezi Mungu kumridhisha ailiyeyasema hayo |
| 8 | Allaahumma bika asbahnaa, wabika amsaynaa, wa bika nah-yaa, wabika namuutu, wailaikal maswiir. **Wakati wa jioni atasema:** Allaahumma bika amsaynaa, wabika asbahnaa, wa bika nah-yaa, wabika namuutu, wailaikal maswiir. | Asubuhi na jioni | Yamekuja mahimizo juu ya dua hii |
| 9 | Asbahnaa âlaa fitratil-islaam,wakalimatil –ikhlaas,wadini nabiyyinaa Muhammadin swalla-llahu alaihi wasallam, wamillati abiinaa Ibraahiim haniifan, Musliman, wamaa kaana minalmushrikiin. | Wakati wa asubuhi | Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa akiomba kwa kutumia dua hii |
| 10 | Allaahumma, Maa asbaha bii min niimatin, au bi-ahadin min-khalqika, famin'ka wahdaka, laa shariika laka, falakal-hamdu walakash-shukr. **Wakati wa jioni atasema:** Allahumma maa amsaa bii min-niimatin, au bi-ahadin min- khalqika, famin'ka wahdaka, laa shariika laka, falakal-hamdu walakash-shukr. | Asubuhi na jioni | Mtu atakuwa ametimiza shukurani za siku yake hiyo |

[1] "Allahu laailaaha i-llaahuwal-hayyulqayyuum. Laataakhudhuhuu sinatun walaa nauum. Lahuu maafis-maawati wamaafil-ardhi, mandhal-ladhii yashfau indahuu il-laa bi-idhnihi, Yaalamu maabaina aidiihim wamaa khalfahum,walaa yuhiitwuuna bishai-in min-ilmihii il-laa bimaa shaa-a, wasia kur-siyyuhus-samaawati wal-ardhwa,walaa yauuduhu hifdhuhumaa wahuwal-aliyyul-adhwiim".

[2] "Aamanarrasuulu bimaa unzila ilayhi min rabbihii walmuuminuuna, kul-lun aamana bil-laahi wamalaaikatihii wakutubihii warusulihii, laanufarriqu baina ahadin min-rusulihi, waqaalu saamiina wa-atwaana, ghufraanaka rabbana wailaikalmaswiir. Laayukallifullahu nafsan il-laa wus-ahaa, lahaa maakasabat wa-alaihaa maktasabat, rabbana laatuaakhidhnaa in-nasiinaa au akhtwa'ana, rabbanaa walaatahmil-alainaa iswran kamaa hamaltahuu alal-ladhiina minqablinaa, rabbana walatuhammilnaa maalaa twaaqata lanaa bih, waafuannaa, waghfirlanaa, warhamnaa, anta maulaanaa fansurnaa alalqaumilkaafiriin".

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11 | Allahumma inniy asbah'tu ushhiduka wa ush'hidu hamalata arshika wa malaaikataka, wa anibiyaa-aka wajamiią khalqika, bi-annaka an'ta-llahu, laa ilaaha illa an'ta, wa-anaa Muhammadan Abduka warasuluka. **Wakati wa jioni atasema:** Allahumma inniy amsaytu ushhiduka wa ush'hidu hamalata arshika wa malaaikataka, wa anibiyaa-aka wajamiią khalqika, bi-annaka an'ta-llahu, laa ilaaha illa an'ta, wa-anaa Muhammadan Abduka warasuluka. | Mara 4 asubuhi na mara 4 jioni | Mwenye kuisoma dua hii mara 4 Mwenyezi Mungu atamkinga na moto |
| 12 | Allahumma faatwira-ssamawaati wal-ardhwi, Ăalimal-ghaibi wash-shahaada, rabba kul-li shay-in wamaliikahu, ash-hadu allaa ilaaha illaa an'ta, auudhubika min sharri nafsiy, wamin sharri sh-shaitwaani washirkihi, wa an-aqtarifa âlaa nafsiy suuan, au ajurrahuu ilaa Muslim. | Asubuhi na jioni na wakati wa kulala. | Inamkinga mtu na wasiwasi wa shetani. |
| 13 | Allahumma inniy auudhu bika minalhammi walhazan,wa auudhubika minal-aj'zi walikasal,wa auudhubika minaljub-ni walbukhl,wa auudhu bika min ghalabatid-dayni wa qahrir-rijaal. | Mara moja asubuhi na mara moja jioni. | Inamuondoshea mtu kero yake, huzuni yake na kulipa deni lake |
| 14 | Allahumma an'ta rabbii, laa ilaaha illaa anta, khalaqtaniy wa ana abduka, wa ana alaa ahdika, wa waadika mastata'atu, auudhubika min-sharri maa swanaâtu, abuu-u laka biniimatika alayya, wa abuu-u laka bidhambiy, faghfirliy, fainnahuu laa yaghfirudh-dhunuba illaa an'ta . | Ni Maombi Makubwa Ya Msamaha. Mara moja asubuhi na mara moja jioni. | Anayesoma dua hii mchana huku akiwa na yakini nayo na akafa katika mchana huo, au anayeisoma usiku na akafa katika usiku huo, atakuwa miongoni mwa watu wa peponi |
| 15 | Yaa hayyu yaa qayyuum, birahmatika astaghiith, Aslih lii sha'nii kullahu, walaa takilniy ilaa nafsiy twarfata-ain. | Asubuhi na jioni | Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alimuusia Fatma dua hii. |
| 16 | Allahumma Ăafiniy fiy badaniy, allahumma Ăafiniy fii sam-ii, allahumma Ăafiniy fiibaswariy, allahumma inniy auudhubika minalkufri wal-faq'ri, allahumma inniy audhubika min-adhaabil qabri, laa ilaaha illaa an'ta. | Mara 3 asubuhi na mara 3 jioni | Imekuja kwamba Mtume alikuwa akiomba dua hii |
| 17 | Allahumma inniy as'alukal-aafiyata fiidiiniy waduniyaaya, wa-ahliy, allahummastur âuraatiy wa Aamin rauaâtiy, allahumma ih-fadhniy min baini yadaiyya, wamin-khalfiy, wa-ani yamiiniy, wa an-shimaliy, wa min-fauqiy, wa-auudhu bi-adhamatika an-ughtalaa min-tahtiy. | Asubuhi na jioni | Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, alikuwa haachi kuomba dua hii wakati wa asubuhi na wakati wa jioni. |
| 18 | Sub-hanaallah wabihamdihii, adada khalqihii, waridhwaa nafsihi, wazinata arshihii, wamidaada kalimaatihi. | Mara 3 asubuhi | Ni bora zaidi kuliko kukaa kuanzia asubuhi hadi jioni kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu. |

# KAULI NA VITENDO AMBAVYO NDANI YAKE KUNA MALIPO MAKUBWA

| N | KAULI AU TENDO BORA | MALIPO YAKE KATIKA SUNA Kama alivyosema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam). |
|---|---|---|
| 1 | *Laa ilaaha illallaahu, wahdahuu laa shariika lah, lahulmulku walahulhamdu, wahuwa alaa kullishay-in qadiir* | "Mwenye Kusema: *Laa ilaaha illallaah, wahdahuu laa shariika lah, lahulmulku walahulhamdu, wahuwa alaa kullishay-in qadiir,* mara mia moja katika siku, kwake itakuwa sawa na kuacha huru watumwa kumi, na ataandikiwa mazuri kumi, na atafutiwa mabaya kumi, na kwake itakuwa kinga ya shetani katika siku yake hiyo mpaka imfikie jioni. Na hajaletapo yeyote jambo bora zaidi ya aliyoleta yeye ila tu aliyefanya zaidi ya hayo" |
| 2 | Kusoma sura Ikhlas | "Sura Ikhlas (قل هو الله أحد) inalingana na theluthi ya Qur'ani". |
| 3 | *Subhaanal-lahi wabihamdihi, subhaanal-lahil-adhwiim* | "Atakayesema wakati wa asubuhi na wakati wa jioni: ***Subhaana llaha wabihamdihi*** mara mia moja **yatafutwa madhambi yake** hata kama yatakuwa (mengi) mfano wa povu la bahari. Na hajaleta yeyote Siku ya Kiyama yaliyo bora zaidi kuliko aliyoleta yeye isipokuwa tu yule aliyesema mfano wa aliyosema au akaongeza". "Ni maneno mawili; mepesi juu ya ulimi, mazito katika mizani, yanapendwa na (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema". |
| 4 | *laahawla walaa quwwata illaabillaahi* | "Je, nikufahamishe hazina miongoni mwa hazina za peponi? Nilisema: Nifahamishe. **Mtume** (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) **akasema**: ***laa hawla, walaa quwwata illaa billahi*** |
| 5 | Kafara ya kikao | "Aliyekaa katika kikao yakawa mengi maongezi katika kikao hicho na akasema kabla ya kuondoka katika kikao chake hicho: ***Sub-haanakal-laahumma wabihamdik, ash-hadu allaa ilaaha illaa anta,astaghfiruka wa-atuubu ilayka*** husamehewa yale (makosa) yaliyotokea katika kikao chake hicho" |
| 6 | **Kumsalia Mtume** (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) | "Mwenye kunisalia mara moja, Mwenyezi Mungu humrehemu mara kumi na humfutia madhambi kumi na humpandisha daraja kumi". Katika mapokezi mengine, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: "Na huandikiwa mazuri kumi kwa mara moja yake hiyo". |
| 7 | **Kusoma baadhi ya aya za Qur'ani Tukufu** | "Mwenye kusoma aya hamsini katika siku moja hatoandikwa miongoni mwa walioghafilika. Na mwenye kusoma aya mia moja ataandikwa miongoni mwa wenye kuabudu. Na mwenye kusoma aya mia mbili, Qur'ani haitamuwia hoja dhidi yake Siku ya Kiyama. Na mwenye kusoma aya mia tano ataandikiwa rundo la malipo" |
| 8 | **Kuhifadhi aya katika sura Alkahf** | "Mwenye kuhifadhi aya kumi za mwanzo za sura Alkahf atalindwa dhidi ya Dajali". |
| 9 | **Ujira wa waadhini** | "Hasikii upeo wa sauti ya Mwadhini jini wala binadamu wala kitu chochote isipokuwa kwamba (sauti ya mwadhini) itakuwa shahidi wake Siku ya Kiyama". "Waadhini ni wenye shingo ndefu zaidi Siku ya Kiyama". |
| 10 | **Kumuiga mwadhini wakati wa kuadhini na kuomba dua baada ya Adhana** | "Anayesema wakati akisikia Adhana: ***Allahumma Rabba haadhihi d-daawatit-taamma, waswalaatilqaa-imah, aati Muhammadan Alwasiilata walfadhwiila, wab-ath'huu maqaaman mahmuudan Alladhii wa-adtahu***, utamuia halali uombezi wangu Siku ya Kiyama" |
| 11 | **Kutawadha vizuri** | "Aliyetawadha na Udhu wake akaufanya vizuri, yatatoka madhambi yake kutoka mwilini mwake mpaka kupitia chini ya kucha zake" |
| 12 | **Dua baada ya Udhu** | "Hakuna yeyote kati yenu anayetawadha akakamilisha au akaueneza Udhu vyema, halafu akasema: ***Ash-hadu Al-laa ilaaha il-lallaah. Wa-anna Muhammadan Abdullahi Warasuuluh*** isipokuwa kwamba atafunguliwa milango minane ya pepo ili aingie kupitia mlango wowote autakao" |

| | | |
|---|---|---|
| 13 | Kusali rakaa mbili baada ya Udhu | “Hakuna yeyote miongoni mwenu anayetawadha na akaufanya vizuri Udhu wake halafu akasimama na kusali rakaa mbili akazizingatia kwa moyo wake na uso wake isipokuwa kwamba itakuwa wajibu kwake (kupata) Pepo”. |
| 14 | Hatua nyingi kuelekea msikitini | "Mwenye kwenda mapema msikiti wa Jamaa, hatua inafuta dhambi na hatua inaandikiwa zuri; anapokwenda na anaporudi" |
| 15 | Kwenda msikitini | "Mtu yeyote anapokwenda msikitini au anaporudi, Mwenyezi Mungu humuandalia dhifa Peponi; kila anapokwenda na anaporudi" |
| 16 | Suna ya Ratiba kabla ya Alfajiri na Faradhi ya Alfajiri | "Rakaa mbili za Alfajiri ni bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake" "Aliyesali (sala ya) Asubuhi yuko katika dhima ya Mwenyezi Mungu" |
| 17 | Kuwahi Takbira ya kuanzia sala | "Yeyote aliyesali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu siku arobaini katika Jamaa akiwahi Takbira ya kwanza, ataandikiwa kinga mbili: Kinga ya moto na kinga ya unafiki" |
| 18 | Kusali faradhi Jamaa | “Sala ya Jamaa inaizidi sala ya mtu peke yake kwa daraja ishirini na saba |
| 19 | Kusali Isha na Alfajiri katika Jamaa | "Aliyesali Isha katika Jamaa ni kama kwamba amesali nusu ya usiku. Na aliyesali Asubuhi katika Jamaa, ni kama kwamba amesali usiku wote" |
| 20 | Kusali safu ya kwanza | “Lau kama watu wangejua yaliyopo katika Adhana na safu ya kwanza halafu wasipate (nyenzo ya kuwahi kutekeleza mwanzo) isipokuwa kupiga kura, wangepiga kura” |
| 21 | Mwenye kudumu kusali suna za Ratiba | "Mwenye kusali rakaa kumi na mbili katika siku, atajengewa nyumba peponi. Rakaa nne kabla ya (sala ya) Adhuhuri na rakaa mbili baada yake. Rakaa mbili baada ya (sala ya) Magharibi, na rakaa mbili baada ya (sala ya) Isha na rakaa mbili kabla ya (sala ya) Alfajiri" |
| 22 | Mwanamke kusali nyumbani kwake | "Mwanamke mmoja alikuja kwa Mtume na kusema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwa yakini, mimi napenda kusali pamoja nawe. (Mtume) Akasema: Nimejua hasa kwamba wewe unapenda kusali pamoja nami, na sala yako chumbani kwako ni bora kuliko sala yako nyumbani kwako, na sala yako nyumbani kwako ni bora kuliko sala yako katika eneo la nyumba yako. Na sala yako katika eneo la nyumba yako ni bora kuliko sala yako katika msikiti wa watu wako. Na sala yako katika msikiti wa watu wako ni bora kuliko sala yako katika msikiti wangu” |
| 23 | Sala ya Dhuhaa | "Inakuwepo sadaka juu ya viungo vyote vya mmoja wenu. Kila Tasbihi ***Subhaana llaahu*** ni sadaka, na kila Tahmidi ***Alhamdulillahi*** ni sadaka, na kila Tahlili ***Laa ilaaha il-lallaahu*** ni sadaka, na kila Takbira ***Allaahu akbaru*** ni sadaka, na kaumrisha mema ni sadaka, na kukemea maovu ni sadaka. Na yote hayo yanatoshwa na rakaa mbili atakazozisali mtu katika (wakati wa) dhuhaa (jua linapochomoza na kupanda kidogo)" |
| 24 | Aliyekaa katika mahali pake aliposali akimtaja Mwenyezi Mungu | "Malaika wanamuombea rehma (dua njema) mmoja wenu madamu yupo katika mahali pake aliposali na madamu hajahuduthi (Udhu wake haujatenguka kwa kutokwa na hewa); wanasema: Ewe Mola wetu, msamehe. Ewe Mola wetu, mpe rehma" |
| 25 | Kumtaja Mwenyezi Mungu baada ya kusali Alfajiri katika Jamaa mpaka jua lichomoze kisha kusali rakaa mbili | "Aliyesali Asubuhi katika Jamaa kisha akaketi akimtaja Mwenyezi Mungu mpaka jua likachomoza kisha akasali rakaa mbili, kwake itakuwa kama malipo ya Hija na Umra kamili, kamili, kamili". |
| 26 | Aliyeamka akisali | "Aliyeamka usiku na akamuamsha mkewe na wakasali rakaa |

| | | |
|---|---|---|
| | usiku na akamuamsha mkewe | mbili kwa pamoja, wataandikwa kuwa ni miongoni mwa wanaume na wanawake wanaomtaja sana Mwenyezi Mungu". |
| 27 | Aliyenuia kusali usiku na usingizi ukamshinda | "Hakuna mtu yeyote ambaye ana sala ya usiku na usingizi ukaikwaza sala hiyo isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu atamuandikia mtu huyo malipo ya sala yake na usingizi wake huo utakuwa sadaka". |
| 28 | Dua kwa aliyeweweseka usiku (aliyeamka usiku) | "**Aliyeweweseka usiku akasema**: *Laailaaha illallaahu wahdahuu laashariika lahu lahulmulku walahulhamdu ,wahuwa alaa kulli shay-in qadiir Alhamdulillahi wasubhaana llaaha walaailaaha illallaahu ,wallaahu akbaru,walaahaula walaaquwwata illaabillaahil-aliyyul-adhwiim.* halafu akasema: Ewe Mola wangu, nisamehe au akaomba (dua yoyote) atakubaliwa. Ikiwa atatawadha na kusali, sala yake itakubaliwa" |
| 29 | ***Subhaana llaahu...*** mara 33 na kuhitimisha kwa ***Laa ilaaha il-lallaahu…*** baada ya sala ya faradhi | "Mwenye kumsabihi Mwenyezi Mungu ***Subhaana llaahu*** mara 33 baada ya kila sala, na akamhimidi Mwenyezi Mungu ***Alhamdulillahi*** mara 33, na akamkabiri Mwenyezi Mungu ***Allaahu akbaru*** mara 33. Hizo ni mara 99. Na akasema katika kukamilisha mara mia (100): ***Laa ilaaha il-lallaahu wahdahuu laa shariika lahu,lahulmulku walahul-hamdu wahuwa alaakul-li shy-in qadiir***. yatasamehewa madhambi yake hata kama yalikuwa (mengi) kama povu la bahari" |
| 30 | Kusoma aya Kursiy baada ya sala ya faradhi | “Mwenye kusoma aya Kursiy baada ya kila sala ya faradhi, hakuna cha kumzuia kuingia peponi isipokuwa kifo tu” |
| 31 | Kumtembelea mgonjwa | "Hakuna Mwislamu yeyote anayemtembelea Mwislamu (mgonjwa) asubuhi isipokuwa kwamba Malaika elfu sabini wanamuombea rehema mpaka ifike jioni. Na akimtembelea (mgonjwa) jioni Malaika elfu sabini wanamuombea rehema mpaka ifike asubuhi na atakuwa na bustani (ya matunda) Peponi" |
| 32 | Mwenye kutamka neno la Tauhidi na akafa juu ya neno hilo | "Hakuna mja yeyote aliyetamka ***Laailaaha illallaahu*** halafu akafa juu ya tamko hilo isipokuwa kwamba ataingia Peponi" |
| 33 | Kuosha maiti na kuficha aibu zake | "Aliyemuosha maiti na akaficha aibu zake, Mwenyezi Mungu atamsamehe mtu huyo mara arobaini" |
| 34 | Kujenga misikiti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu | "Yeyote aliyejenga msikiti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu japo (mdogo) kama kiota cha ndege, Mwenyezi Mungu atamjengea mtu huyo nyumba Peponi" |
| 35 | Kutoa | “Hakuna siku yoyote waamkapo waja katika siku hiyo isipokuwa kwamba Malaika wawili hushuka na mmoja wao kusema: Ewe Mola wetu, mpe mtoaji badala. Na mwengine husema: Ewe Mola wetu: Mpe mzuiaji hilaki” |
| 36 | **Sadaka** | “Sadaka haipunguzi mali yoyote. Na Mwenyezi Mungu hamzidishii mja kwa kusamehe isipokuwa utukufu tu. Na hajanyenyekea yeyote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu isipokuwa tu Mwenyezi Mungu humpandisha daraja” “Dirhamu moja huzishinda Dirhamu elfu mia moja (laki moja). Swahaba waliuliza: Inakuwaje? Mtume akasema: Mtu ana Dirhamu mbili; akachukua mojawapo ya Dirhamu hizo akatoa sadaka. Na mtu mwengine ana mali nyingi, akachukua katika pambizoni mwake (sehemu ndogo ya mali yake) elfu mia moja.(laki moja) akatoa sadaka" |
| 37 | Mkopo bila ya faida | "Hakuna Mwislamu yeyote anayempa Mwislamu (mwenzake) mkopo mara mbili isipokuwa kwamba ni kama kutoa sadaka mara moja" |
| 38 | Kumsamehe mwenye | "Alikuwepo mtu anayewadai watu. Alikuwa akimwambia kijana wake: Ukimkuta mtu mwenye matatizo, msamehe, huenda Mwenyezi Mungu |

| | | |
|---|---|---|
| | matatizo | akatusamehe. (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Akasema: (Yule mtu) Akakutana na Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu akamsamehe" |
| 39 | Kuondosha kero njiani | "Kwa yakini, nimemuona mtu anatanua (ananeemeka) Peponi kwa sababu ya mti alioukata katikati ya njia na uliokuwa ukiwakera watu" |
| 40 | Kufunga siku tatu kila mwezi, siku ya Arafa na siku ya Ashura | "Kufunga siku tatu kila mwezi na Ramadhani mpaka Ramadhani ni funga ya milele" "Na (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliulizwa kuhusu funga ya Arafa akasema: Inafuta (dhambi za) mwaka uliopita na uliobaki" "Na (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) aliulizwa kuhusu funga ya siku ya Ashura akasema: Inafuta (dhambi za) mwaka uliopita" |
| 41 | Kufunga siku sita za Mfungomosi | "Mwenye kufunga Ramadhani halafu akaifuatishia kwa kufunga siku sita za Mfungomosi, inakuwa kama saumu ya mwaka" |
| 42 | Kusali Tarawehe pamoja na Imamu mpaka amalize | "Kwa yakini, mtu anaposali pamoja na Imamu mpaka akamaliza, huandikiwa kisimamo cha usiku" |
| 43 | Hija Timamu | "Aliyehiji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; asifanye tendo la ndoa na asifanye maovu, atarudi (akiwa msafi) kama siku alipozaliwa na mama yake". |
| 44 | Umra katika Ramadhani | "Umra katika Ramadhani inalingana na Hija au (inalingana na) Hija (ya kuhiji) pamoja na mimi" |
| 45 | Matendo mema katika siku kumi za mwanzo wa Mfungotatu | "Hakuna siku ambazo matendo mema katika siku hizo yanapendwa zaidi na Mwenyezi Mungu kuliko siku hizi (akikusudia siku za kumi la mwanzo). (Swahaba) Walisema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hata kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu? (Mtume) Akasema: Hata kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa mtu ambaye ametoka kwa nafsi yake na mali yake na asirejee na chochote katika hayo". |
| 46 | Udh-hiya (mnyama anayechinjwa siku ya sikukuu ya Mfungotatu) | "Swahaba wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wa Mwenyezi Mungu walisema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hizi Udh-hiya ni nini? (Mtume) (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Alisema: Ni suna ya Baba yenu (Mtume) Ibrahimu. (Swahaba) walisema: Tunapata nini sisi katika suna hiyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? (Mtume) Alisema: Kwa kila unyoya kuna zuri moja. (Swahaba) Walisema: Na sufi nayo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? (Mtume) Alisema: Kwa kila unyoya mmoja katika sufi kuna zuri moja". |
| 47 | Nia njema inamfikisha Muumini daraja za juu Peponi pamoja na kufanya matendo yawezekanayo | "Mfano wa umma huu ni kama watu wanne: Mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa mali na elimu. Yeye anaitumia elimu yake katika mali yake anayoitumia katika haki yake. Na mtu mwengine Mwenyezi Mungu amempa elimu na hakumpa mali. Yeye anasema: Lau ningelikuwa na mfano wa aliyonayo huyu ningelifanya mfano wa anayofanya. Akasema Mtume: **Wawili hao katika thawabu wako sawa**. Na mtu mwengine Mwenyezi Mungu amempa mali na hakumpa elimu. Yeye anaharibu katika mali yake; anaitumia katika isiyokuwa haki yake. Na mtu (mwengine) Mwenyezi Mungu hakumpa elimu wala mali. Yeye anasema: Laiti Mwenyezi Mungu ningelikuwa na mfano wa aliyonayo huyu, ningefanya mfano wa anayofanya. Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: **Wawili hao katika makosa wako sawa**". |
| 48 | Malipo ya Shahidi (aliyekufa katika vita vya Jihadi) | "**Shahidi kwa Mwenyezi Mungu ana mambo sita:** 1) Anasamehewa (dhambi zake) katika tone la kwanza kabisa (la damu yake) na kuoneshwa makazi yake ya Peponi, na 2) Atakingwa na adhabu ya kaburini, na 3) Atasalimika na Fazaa (hofu) kubwa (ya Siku ya Kiyama), na 4) Litawekwa juu ya kichwa chake taji la heshima; Yakuti moja iliyomo katika taji hilo ni bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake, na 5) Ataozeshwa wake sabini na mbili katika Huri Ain, na 6)Atakubaliwa maombezi yake kwa watu sabini katika ndugu zake" |

| | | |
|---|---|---|
| 49 | Mwenye kuacha tiba ya moto na kusoma Ruq-ya na kuacha jambo kwa itikadi ya nuksi | "Mataifa yalioneshwa kwa Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, akiwa usingizini, akauona umma wake na ilhali miongoni mwao kuna watu elfu sabini wanaingia Peponi bila ya kuhesabiwa wala kuadhibiwa. Na hao ni wale ambao hawajitibu kwa moto na hawasomi Ruq-ya na hawaachi jambo kwa itikadi ya nuksi na wanamtegemea Mola wao tu" |
| 50 | Kumtembelea mgonjwa | "Hakuna Mwislamu yeyote anayemtembelea Mwislamu (mgonjwa) asubuhi isipokuwa kwamba Malaika elfu sabini wanamuombea rehema mpaka ifike jioni. Na akimtembelea (mgonjwa) jioni Malaika elfu sabini wanamuombea rehema mpaka ifike asubuhi na atakuwa na bustani (ya matunda) Peponi" |
| 51 | Jeraha katika njia ya Mwenyezi Mungu | "Nina'apa kwa (Mwenyezi Mungu) ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba hajeruhiwi yeyote katika njia ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye amjuaye zaidi aliyejeruhiwa katika njia yake, isipokuwa kwamba atakuja Siku ya Kiyama (na ilhali) rangi ni rangi ya damu na harufu ni harufu ya Miski" |
| 52 | Ulinzi katika njia ya Mwenyezi Mungu | "Ulinzi wa siku moja katika njia ya Mwenyezi Mungu ni bora kuliko dunia na vilivyopo juu yake, na mahali pa bakora (silaha) ya mmoja wenu katika Pepo ni bora kuliko dunia na vilivyopo juu yake" |
| 53 | Mwenye kumuandaa mpiganaji katika njia ya Mwenyezi Mungu | "Mwenye kumuandaa mpiganaji, kwa yakini naye amepigana. Na mwenye kumuakilisha mpiganaji katika familia yake (kuihudumia familia yake), kwa yakini naye amepigana" |
| 54 | Kumuomba Mwenyezi Mungu Shahada | "Mwenye kumuomba Mwenyezi Mungu Shahada (kufa katika vita vya kidini) kwa ukweli, Mwenyezi Mungu atamfikisha daraja za Mashahidi, hata kama alikufa kitandani kwake" |
| 55 | Kulia kutokana na kumuogopa Mwenyezi Mungu na ulinzi katika njia yake | "Macho mawili hayataguswa na moto; jicho lililolia kutokana na kumuogopa Mwenyezi Mungu na jicho lililokesha likilinda katika njia ya Mwenyezi Mungu" |
| 56 | Malipo ya mwenye kufiwa na watoto wadogo | "Hakuna Mwislamu yeyote katika watu anayefiwa na watoto watatu ambao hawakufikia balehe isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu atamuingiza Peponi tu" |
| 57 | Kukosa kuona na kulivumilia hilo | "Kwa yakini, Mwenyezi Mungu amesema kuwa: Nimpapo mtihani mja wangu katika vipenzi vyake viwili akavumilia, ninampa Pepo badala yake; akikusudia (kwa neno: vipenzi vyake viwili) macho yake" |
| 58 | Kuacha jambo kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu | "Kwa yakini, wewe hutaacha jambo kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu atakupa jambo bora zaidi kuliko hilo" |
| 59 | Kuzitunza sehemu za siri na ulimi | "Yeyote anayenipa dhamana ya kutunza (kiungo) kilichopo kati ya mataya yake na (kiungo) kilichopo kati ya miguu yake, mimi nampa dhamana ya kupata Pepo; akikusudia ulimi na sehemu za siri" |
| 60 | Kusema ***bismillaahi*** wakati wa kuingia nyumbani na wakati wa kula | "Mtu aingiapo nyumbani kwake na akamtaja Mwenyezi Mungu wakati wa kuingia kwake na wakati wa (kula) chakula chake, shetani husema (kuwaambia wafuasi wake kuwa): Hamna malazi nyinyi wala chakula. Na aingiapo bila ya kumtaja Mwenyezi Mungu wakati wa kuingia kwake, shetani husema (kuwaambia wafuasi wake kuwa): Mmewahi malazi. Na asipomtaja Mwenyezi Mungu wakati wa (kula) chakula chake, shetani husema: Mmewahi malazi na chakula" |

| | | |
|---|---|---|
| 61 | Kumshukuru Mwenyezi Mungu baada ya kula, kunywa na kuvaa nguo mpya | **"Mwenye kula chakula na kusema:** ***Alhamdulillaahil-ladhii atwamanii haadhaa warazaqaniyhi minghayri hawlin minny walaaquwwata***, husamehewa dhambi zake zilizopita". **Na anapovaa nguo mpya husema:** ***Alhamdulillaahi lladhiy kasaaniy*** |
| 62 | Mtu ambaye anataka Mwenyezi Mungu ampunguzie uchovu (uzito) wa kazi yake | "Fatma, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, alimuomba Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ampe mtumishi. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akamwambia Fatma: Je, nikufundisheni yaliyokuwa bora kuliko hayo mliyoniomba? Mkitaka kulala, mlete Takbira ***allaahu akbaru*** mara (34), na mlete Tahmidi ***Alhamduli-laahi*** mara (33), na mlete Tasbihi ***subuhaanallaahi*** mara (33). Hayo ni bora kwenu kuliko mtumishi" |
| 63 | Dua kabla ya kujamiiana | **"Lau kama mmoja wao akitaka kukutana na mke wake atasema:** ***Bismillahi,Allaahumma jannibna sh-shaytwaani wajannibish-shaytwaana maarazaqtanaa***. basi kama itapangwa baina yao kupata mtoto katika hilo, shetani yoyote hatamdhuru mtoto huyo asilani" |
| 64 | Kumdhamini Yatima | "Mimi na mdhamini wa Yatima Peponi (tutakuwa) kama hivi; na alisema (hivyo) kwa (kuashiria kwa) vidole vyake viwili; kidole cha shahada na cha kati" |
| 65 | Mke kumridhisha mumewe | "Mwanamke anaposali sala zake tano, na akafunga mwezi wake (wa Ramadhani), na akahifadhi sehemu yake ya siri (asifanye uzinzi), na akamtii mume wake (katika mambo yasiyokuwa ya haramu), ataambiwa: Ingia peponi kupitia mlango wowote wa Peponi uutakao". "Mwanamke yeyote aliyefariki na ilhali mumewe yu radhi naye, ataingia Peponi" |
| 66 | Kuunga udugu | "Anayependa kukunjuliwa katika riziki yake na kuzidishiwa katika umri wake, basi aunge ndugu zake" |
| 67 | Tabia nzuri | "Kwa yakini, Muumini, kwa tabia zake nzuri, anafikia daraja ya mfungaji, msimamaji (usiku kwa kusali)". "Mimi ni mwenye kudhamini nyumba Peponi kwa mtu ambaye tabia zake zimekuwa nzuri". |
| 68 | Kuwahurumia viumbe | "Na hakuna vingine isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu huwahurumia katika waja wake wale wenye huruma. Wahurumieni walioko duniani atakuhurumieni aliyeko mbinguni" |
| 69 | Kupenda Waislamu wapate kheri | "Hawi Muumini mmoja wenu mpaka apende ndugu yake apate yale anayopenda yeye mwenyewe apate" |
| 70 | Haya | "Haya haileti isipokuwa kheri tu". "Haya ni miongoni mwa Imani". "Mambo manne ni miongoni mwa suna za Mitume: **1)** Kuona haya na **2)**Kujipaka manukato na **3)** Kupiga mswaki na **4)** Kuoa". |
| 71 | Kuanza kusalimia | "Mtu mmoja alikwenda kwa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na kumwambia: ***Assalamu alaikum***. Mtume akasema: Kumi. Halafu akaja mtu mwengine na kusema: ***Assalaamu alaikum warahmatullaahi.*** Mtume akasema: Ishirini. Halafu (mtu) mwengine na kusema: ***Assalaamu alaikum warahmatullaahi wabarakatuh***. Mtume akasema: Thalathini." Mtume alikusudia mambo mazuri katika idadi hizo. |
| 72 | Kupeana mikono wakati wa kukutana | "Hakuna Waislamu wawili wanaokutana na wakapeana mikono isipokuwa kwamba watasamehewa (dhambi zao) kabla hawajaachana" |
| 73 | Kutetea heshima ya Mwislamu | "Mwenye kutetea heshima ya ndugu yake, Mwenyezi Mungu atauepushe uso wake (usiunguzwe) na moto Siku ya Kiyama" |
| 74 | Kuwapenda watu wema na kukaa nao | "Wewe utakuwa pamoja na unayempenda". Anas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, alisema: Swahaba hawakuwahi kufurahishwa na jambo kama walivyofurahishwa na Hadithi hii. |

| | | |
|---|---|---|
| 75 | Wanaopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu | "Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: Wanaopendana katika utukufu wangu watapata majukwaa ya nuru. Manabii na mashahidi watawaonea gere". |
| 76 | Mwenye kumuombea ndugu yake Mwislamu | "Mwenye kumuombea ndugu yake akiwa hayupo mbele yake, Malaika aliyewakilishwa kwake husema: Aamiin, nawe utapata mfano (wake)" |
| 77 | Kuwaombea msamaha Waislamu wanawake na wanaume | "Mwenye kuwaombea msamaha Waumini wanaume na Waumini wanawake, Mwenyezi Mungu atamuandikia zuri moja kwa kila Muumini mmoja wa kiume na wa kike". |
| 78 | Kuacha ubishi na uongo | "Mimi nadhamini nyumba ya kifahari katika viunga vya Peponi kwa mwenye kuacha ubishi hata kama ana haki, na (nadhamini) nyumba ya kifahari katikati ya Pepo kwa mwenye kuacha kusema uongo hata kama anafanya mzaha" |
| 79 | Kuzuia hasira | "Mwenye kuzuia hasira na ilhali anaweza kuitekeleza, Mwenyezi Mungu atamuita mbele ya halaiki Siku ya Kiyama ili ampe hiari ya kuchagua ni wanawake gani wa Peponi (Huur Al-ain) atakao" |
| 80 | Kusifia kheri au shari | "Yeyote mliyemsifia kheri, imewajibika kwake kupata Pepo. Na yeyote mliyemsifia shari, imewajibika kwake kuingia motoni. Nyinyi ni mashahidi wa Mwenyezi Mungu duniani" |
| 81 | Kumuondolea uzito Mwislamu, kumsaidia na kumsitiri | "Mwenye kumuondolea Muumini tatizo katika matatizo ya duniani, Mwenyezi Mungu atamuondolea mateso katika mateso ya siku ya Kiyama. Na Mwenye kumuwepesia aliyefikwa na mazito, Mwenyezi Mungu humfanyia wepesi duniani na Akhera. Na mwenye kumsitiri Mwislamu, Mwenyezi Mungu atamsitiri duniani na akhera. Na Mwenyezi Mungu yupo katika kumsaidia mja madamu mja huyo yupo katika kumsaidia ndugu yake. Na anayefuata njia akitafuta elimu katika kufuata kwake njia hiyo, Mwenyezi Mungu humrahisishia, kwa hilo, njia ya kuelekea peponi. Na hawakusanyiki watu katika nyumba miongoni mwa nyumba za Mwenyezi Mungu wakikisoma kitabu cha Mwenyezi Mungu na kukidurusu baina yao isipokuwa kwamba utulivu unawashukia, rehema inawafinika na Malaika huwazunguka na Mwenyezi Mungu huwataja pamoja na wale walioko kwake. Na ambaye amali zake zimemcheleweshа (zimemuweka nyuma), nasaba yake haiwezi kumpeleka haraka " |
| 82 | Kuitanguliza Akhera | "Yeyote ambaye Akhera ndio lengo lake, Mwenyezi Mungu atajaalia utajiri wake katika moyo wake na atamnyooshea mambo yake na itamjia dunia itake isitake (hali yake ya maisha itakuwa nzuri)" |
| 83 | Uadilifu wa mtawala, kijana kuwa mwema, kujihusisha na misikiti, kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu | "Watu saba Mwenyezi Mungu atawafinika katika kivuli chake siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa kivuli chake tu: **1)** Kiongozi mwadilifu, na **2)** Kijana aliyekulia katika kumwabudu Mola wake, na **3)**Mtu ambaye moyo wake umefungamana katika misikiti, na **4)** Watu wawili waliopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; wameungana kwa ajili hiyo na kutengana kwa ajili hiyo, na **5)** Mwanaume aliyeombwa na mwanamke mwenye hadhi na uzuri (ili afanye naye zinaa akakataa na) akasema: Mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, na.**6)** Mtu aliyetoa sadaka akaificha mpaka mkono wake wa kushoto usijue kile mkono wake wa kulia ulichokitoa, na **7)** Mtu aliyemkumbuka Mwenyezi Mungu akiwa faragha mpaka akalia" |

# MAMBO YALIYOKATAZWA

| N | JAMBO LILILOKATAZWA | HADITHI (ALIVYOSEMA MTUME (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).) |
|---|---|---|
| 1 | Kiburi | "Hataingia peponi ambaye katika moyo wake kuna chembe cha kiburi" Na kiburi ni kuwadharau watu na kuikana haki |
| 2 | Kujionesha (Riya) na kutaka sifa (Sum'a) | "Mwenye kutaka sifa, Mwenyezi Mungu humfedhehesha. Na mwenye kujionesha, Mwenyezi Mungu huuweka wazi undani wake (Mwenyezi Mungu humuumbua) |
| 3 | Uovu | "Kwa yakini, mtu mwenye daraja mbaya sana mbele ya Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama ni mtu ambaye watu wanamtenga au kumsusa kwa kujikinga na uovu wake" |
| 4 | Uongo | "Ole wake anayezungumza mazungumzo ili kwa mazungumzo hayo awachekeshe watu na kwa hiyo anasema uongo. Ole wake, Ole wake" |
| 5 | Dhambi na mitihani | "Nyoyo huoneshwa mitihani (dhambi) kama (kamba za) mkeka; moja moja. Moyo wowote utakaonyweshwa (utakaotenda), huota ndani yake doa jeusi" |
| 6 | Ujasusi | "Mwenye kusikiliza mazungumzo ya watu na ilhali wao wanamchukia au wanamkimbia, utamiminwa katika masikio yake uji wa risasi iliyoyayushwa Siku ya Kiyama" |
| 7 | Picha | "Kwa yakini, watakaoadhibiwa sana na Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama ni watengenezaji picha". "Malaika hawaingii nyumba ambayo ndani yake kuna mbwa na picha" |
| 8 | Fitina | "Haingii peponi mtu fitina" Kufitini ni kunakili maneno kati ya watu kwa madhumuni ya uharibifu" |
| 9 | Kusengenya | "Je, mnajua, ni nini kusengenya? Swahaba walisema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wanaojua zaidi. Mtume alisema: Ni wewe kumsema ndugu yako kwa anayoyachukia. Palisemwa: Unaonaje kama hayo niyasemayo ndugu yangu anayo? Mtume alisema: Ikiwa anayo hayo usemayo, kwa yakini umemsengenya. Na kama hana, kwa yakini umemzulia" |
| 10 | Kulaani | "Kumlaani Muumini ni kama kumuua" "Wenye kulaani sana hawawi waombezi wala mashahidi Siku ya Kiyama" |
| 11 | Kutangaza siri | "Kwa yakini, miongoni mwa watu wenye daraja ovu sana mbele ya Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama ni mwanaume anayekutana na mkewe (kimwili) naye mke akakutana naye halafu akatangaza siri yake" |
| 12 | Mwanamke kutoka akiwa na manukato | "Kila jicho ni lenye kuzini. Na mwanamke anapojipaka manukato halafu akapita kwenye baraza (ya watu waliokaa), basi yeye ni kadhaa wa kadhaa; ikiwa na maana ni mwenye kuzini" |
| 13 | Kumtuhumu Mwislamu kwa ukafiri | "Mtu yeyote aliyemwambia ndugu yake: Ewe kafiri, yamemrejea mmoja wao maneno hayo; ikiwa ni kama alivyosema, sawa. Vinginevyo, maneno hayo yatamrejea mwenyewe" |
| 14 | Kujinasibu na baba asiyekuwa wake | "Mwenye kujipa nasaba ya asiyekuwa baba yake na ilhali anajua, Pepo kwake ni haramu". "Yeyote mwenye kumkataa baba yake, huo ni ukafiri" |
| 15 | Kumtia hofu Mwislamu | "Haiwi halali kwa Mwislamu kumtia hofu Mwislamu (mwenzake)". "Mwenye kumuashiria (kumuelekeza) ndugu yake kwa chuma (silaha), Malaika wanamlaani mpaka akiache chuma hicho" |
| 16 | Kumuita mnafiki "Bwana" | "Msimwite mnafiki: Sayyid (Bwana), kwani kama akiwa Bwana, mtakuwa mmemkasirisha Mola wenu" |
| 17 | Wanawake Kuzuru Makaburi | "Mwenyezi Mungu amewalaani wanawake wanaozuru sana makaburi" "Mama Atiyah, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema kuwa: Tulikatazwa kusindikiza Jeneza na (lakini hilo) halikutiliwa mkazo kwetu" |

| | | |
|---|---|---|
| 18 | **Mwanamke Kumsusia Mumewe** | "Mwanaume atakapomwita mkewe kitandani kwake na akakataa kwenda, Malaika wanamlaani mwanamke huyo mpaka asubuhi" |
| 19 | **Kuwahadaa Raia** | "Hakuna mja yeyote anayepewa dhamana na Mwenyezi Mungu ya kuongoza watu akafa siku ya kufa na ilhali yeye anawafanyia hiyana watu wake isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu ameiharamisha Pepo kwa mtu huyo" |
| 20 | **Kutoa Fat'wa Bila Ya Elimu** | "Mwenye kupewa Fat'wa bila ya elimu, dhambi zake zinakuwa kwa yule aliyempa Fat'wa" |
| 21 | **Mwanamke Kuomba Talaka** | "Mwanamke yeyote aliyemuomba mumewe Talaka bila ya tatizo lolote, ni haramu kwake harufu ya pepo" |
| 22 | **Kuwafunga Wanyama Kengele** | "Malaika hawasuhubiani na msafara ambao ndani yake kuna mbwa au kengele". "Kengele ni firimbi za shetani" |
| 23 | **Kuacha (Sala Ya) Ijumaa Kwa Dharau** | "Mwenye kuacha Ijumaa mara tatu kwa dharau (bila ya udhuru wa kisheria), Mwenyezi Mungu ataupiga chapa moyo wake (kuwa yeye ni mnafiki)". |
| 24 | **Kupora ardhi** | "Mwenye kuchukua kipande cha ardhi kiasi cha shubiri kwa dhuluma, Mwenyezi Mungu atamtwisha shingoni kipande hicho Siku ya Kiyama kutokea ardhi saba" |
| 25 | **Maneno yanayomkasirisha Mwenyezi Mungu** | "Na, kwa yakini, mja hutamka neno la kumkasirisha Mwenyezi Mungu asilitilie maanani likamtumbukiza katika Jahanamu miongo sabini" |
| 26 | **Kusema sana bila ya kumtaja Mwenyezi Mungu** | "Msiseme sana bila ya kumtaja Mwenyezi Mungu, kwa sababu kusema sana bila ya kumtaja Mwenyezi Mungu ni ususuwavu wa moyo" |
| 27 | **Waungaji nywele na wakwaruzaji ngozi** | "Mwenyezi Mungu amemlaani mwanamke muungaji nywele na muungwaji, na mwenye kuweka urembo kwa kukwaruza ngozi na mwenye kuwekwa urembo kwa kukwaruza ngozi" |
| 28 | **Kuwekeana shonde baina ya Waislamu** | "Haiwi halali kwa Muumini kumsusa ndugu yake zaidi ya siku tatu" "Mwenye kumsusa ndugu yake mwaka ni kama kumwaga damu yake" |
| 29 | **Mwenye kujifananisha na jinsia isiyokuwa yake** | "Mtume wa Mwenyezi Mungu amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake na wanawake wanaojifananisha na wanaume" |
| 30 | **Mwenye kurejea katika alichotoa** | "Mwenye kurejea katika alichotoa ni kama mbwa; anatapika halafu anarudi katika matapishi yake". "Sio halali kwa mtu kutoa kitu halafu akarejea katika kitu hicho" |
| 31 | **Kutafuta elimu kwa ajili ya dunia** | "Mwenye kujifunza elimu katika yale ambayo kwayo inatakiwa akusudiwe Mwenyezi Mungu, (lakini) hajifunzi elimu hiyo isipokuwa tu kwa lengo la kupata kwayo kitu cha dunia, hatapata harufu ya Pepo Siku ya Kiyama" |
| 32 | **Kutazama Yaliyohara mishwa** | "Mwanadamu ameandikiwa sehemu yake katika Zinaa. litamkuta hilo; hakuna pingamizi. Zinaa ya macho ni kutazama, na Zinaa ya masikio ni kusikiliza, na Zinaa ya ulimi ni mazungumzo, na Zinaa ya mkono ni kushika, na Zinaa ya mguu ni hatua (kutembea), na moyo unapenda na kutamani, na sehemu ya siri inathibitisha hayo au kuyakataa" |
| 33 | **Kukaa faragha na mwanamke wa kando** | "Mmoja wenu asikae faragha kabisa na mwanamke, kwani shetani atakuwa watatu wao" |
| 34 | **Mwanamke kuolewa bila ya Walii** | "Mwanamke yeyote aliyeolewa bila ya idhini ya Walii wake, ndoa yake ni batili, ndoa yake ni batili, ndoa yake ni batili" |
| 35 | **Ndoa ya Shighari (kubadilishana)** | "Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amekataza (ndoa ya) Shighari". Shighari ni mtu kumuozesha binti yake kwa mtu kwa msingi kwamba yule mtu mwengine naye amuozeshe binti yake bila ya kuwepo mahari kati yao. |

| | | |
|---|---|---|
| 36 | **Kuwakusudia watu kwa amali** | "Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: Mimi ni katika washirika wasiokuwa na haja zaidi ya ushirika. Yeyote aliyefanya amali (ambayo) amemshirikisha badala yangu pamoja nami, ninamuacha yeye na ushirika wake". |
| 37 | **Mwanamke kusafiri bila ya Maharimu** | "Si halali kwa mwanamke anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kusafiri masafa ya siku moja isipokuwa tu awe pamoja na Maharimu" |
| 38 | **Kuomboleza kwa mayowe** | "Kwa yakini, Mwenye kuombolezwa kwa mayowe, ataadhibiwa kwa yale aliyoombolezwa kwayo Siku ya Kiyama". "Maiti anaadhibiwa katika kaburi lake kwa sababu ya kuombolezwa kwa mayowe" |
| 39 | **Kuwakera wanaosali** | "Aliyekula kitunguu maji na kitunguu saumu na Kurathi (mmea kama kitunguu una tumba nyeupe), asiusogolee kabisa msikiti wetu, kwani Malaika wanakereka na yale ambayo wanadamu wanakereka nayo" |
| 40 | **Kuapia asiyekuwa Mwenyezi Mungu** | "Aliyeapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, amekufuru au amefanya ushirikana". "Anayeapa, aape kwa Mwenyezi Mungu au anyamaze" |
| 41 | **Kiapo cha uongo** | "Mwenye kuapa akichukua kwa kiapo hicho mali ya Mwislamu na ilhali yeye kwa kiapo hicho ni muovu (muongo), atakutana na Mwenyezi Mungu na ilhali ni Mwenye kumkasirikia" |
| 42 | **Kuapa katika biashara** | "Jihadharini na kuapa sana katika biashara, kwani hilo linaifanikisha biashara na (lakini) linaiondolea baraka". "Kuapa kunafanikisha bidhaa (kuuzika) kunaondoa baraka" |
| 43 | **Kuwaiga makafiri** | "Yeyote aliyejifananisha na watu (fulani), basi yeye ni katika wao". "Si katika sisi aliyejifananisha na wasiokuwa sisi". |
| 44 | **Husuda** | "Jihadharini na husuda, kwa sababu husuda inakula mazuri kama moto unavyokula kuni", au alisema: "nyasi". |
| 45 | **Kujenga juu ya kaburi** | "Mtume wa Mwenyezi Mungu amekataza kulipaka jasi (chokaa/rangi) kaburi na kukaa juu yake na kujenga juu yake" |
| 46 | **Hadaa na Hiyana** | "Mwenyezi Mungu atakapowakusanya (viumbe) wa mwanzo na wa mwisho Siku ya Kiyama, kila aliyefanya hiyana atawekewa bendera na kusemwa: Hii ni hadaa ya fulani bin fulani" |
| 47 | **Kukaa juu ya kaburi** | "Kwa yakini, kukaa kwa mmoja wenu juu ya kaa la moto likaunguza nguo zake na kufika kwenye ngozi yake ni bora kuliko kukaa juu ya kaburi" |
| 48 | **Kuacha mapambo kwa ajili ya msiba** | "Haiwi halali kwa mwanamke anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuacha mapambo kwa ajili ya maiti zaidi ya siku tatu isipokuwa tu kwa mume" |
| 49 | **Kuomba bila ya dharura** | "Mambo matatu ninayaapia na ninakuhadithieni mazungumzo (makubwa). Hivyo, yahifadhini: **1)** Haipungui mali ya mja kwa (kutoa) sadaka, na **2)** Hakudhulumiwa mja dhuluma (yoyote) akasubiri isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu humzidishia enzi (nguvu na heshima), na **3)** Hakufungua mja mlango wa kuomba isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu humfungulia mlango wa ufukara" |
| 50 | **Kutia filisi katika biashara** | "Mtume wa Mwenyezi Mungu amekataza mtu wa mjini kumuuzia mtu wa shamba, na msitiliane filisi (kwa kuongeza thamani ya kitu ilhali muongezaji hataki kukinunua kitu hicho), na mtu asifanye biashara juu ya biashara ya ndugu yake" |
| 51 | **Kutangaza msikitini kitu kilichopotea** | "Atakayemsikia mtu anayetangaza kitu kilichopotea msikitini, aseme: "Tunamuomba Mwenyezi Mungu asikurudishie kitu hicho", kwa sababu misikiti haikujengwa kwa (madhumuni) haya" |

| | | |
|---|---|---|
| 52 | **Kupita mbele ya anayesali** | "Lau kama anayepita mbele ya anayesali angejua ni nini kilicho juu yake, ingekuwa kusimama arobaini ni bora kwake kuliko kupita mbele yake" |
| 53 | **Kuacha sala ya Alasiri** | "Yeyote aliyeacha (kusali) sala ya Alasiri, imepomoka (imepotea bure) amali yake". |
| 54 | **Kuzembea sala** | "Ahadi iliopo kati yetu (Waislamu) na kati yao (makafiri) ni sala. Mwenye kuacha sala, amekufuru". "Kati ya mtu na kati ya ukafiri ni kuacha sala". |
| 55 | **Kuhubiri upotofu** | "Na mwenye kulingania (kuhubiri) upotofu, atapata katika dhambi mfano wa dhambi za waliomfuata. Hilo halitapunguza kitu katika dhambi zao" |
| 56 | **Kunywa kwa kusimama na katika mdomo wa chombo cha kunywea** | "Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amekataza kunywa katika mdomo wa kiriba au chombo cha kunywea". "Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amekemea mtu kunywa akiwa amesimama". |
| 57 | **Kunywa kwa kutumia vyombo vya dhahabu na fedha** | "Msinywe kwa vyombo vya dhahabu na fedha na msivae Hariri na Dibaji (aina ya hariri), kwani hizo ni (nguo) zao (makafiri) duniani na ni (nguo) zenu (Waislamu) Akhera" |
| 58 | **Kunywa kwa mkono wa kushoto** | "Yeyote katika nyinyi asile kabisa kwa mkono wake wa kushoto na asinywe kwao, kwani shetani anakula kwa mkono wake wa kushoto na anakunywa kwa mkono huo" |
| 59 | **Mkataji udugu** | "Haingii Peponi mkataji". Yaani: Mkataji udugu. |
| 60 | **Kuacha kumsalia Mtume** | "Imegusa mchanga pua ya mtu (amepata unyonge na udhalili) ambaye nimetajwa mbele yake na asinisalie". "Bahili ni yule ambaye nimetajwa mbele yake na asinisalie". |
| 61 | **Kuropoka** | "Na, kwa yakini, ninaowachukia zaidi katika nyinyi na watakaokaa mbali zaidi na mimi Siku ya Kiyama ni wanaoropoka na wanaokejeli na wanaozungumza kwa kiburi". |
| 62 | **Kufuga mbwa** | "Yeyote mwenye kufuga mbwa, isipokuwa mbwa wa kuwindia na wa kulinda mifugo, zitapungua Kirati mbili kila siku katika thawabu zake". |
| 63 | **Kutesa wanyama** | "Ameadhibiwa mwanamke kwa sababu ya paka aliyemfungia mpaka akafa, na kwa sababu hiyo, ataingia motoni". "Msifanye dango (kujifunzia kulenga shabaha) kitu ambacho kina roho" |
| 64 | **Riba** | "Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amemlaani mlaji Riba na mlishaji wake". "Dirhamu ya Riba anayoila mtu na ilhali anajua, ni jambo baya zaidi kuliko Zinaa thalathini na sita" |
| 65 | **Mnywaji pombe** | "Haingii Peponi mnywaji pombe na anayeamini uchawi na mkataji udugu". |
| 66 | **Kuwafanyia uadui Mawalii (Wapenzi) wa Mwenyezi Mungu** | "Kwa yakini, Mwenyezi Mungu amesema: Yeyote aliyemfanyia uadui Walii wangu, hakika nimemtangazia vita". |
| 67 | **Kumuua aliyepewa hifadhi ya amani katika nchi za Kiislamu** | "Yeyote aliyeua nafsi iliyo katika mkataba (wa usalama) bila ya haki yake, hatanusa harufu ya Pepo, na kwa yakini, harufu yake inanusika kutoka masafa ya mwendo wa miaka mia". |
| 68 | **Kumnyima mrithi mirathi yake** | "Yeyote aliyekata mirathi ya mrithi wake, Mwenyezi Mungu ataikata mirathi yake ya Peponi Siku ya Kiyama". |
| 69 | **Kuiweka mbele dunia** | "Na yeyote ambaye dunia ndio kusudio lake, Mwenyezi Mungu atauweka ufukara mbele ya macho yake na atamvurugia mambo yake na hayatamjia katika dunia isipokuwa tu yale aliyokwisha pangiwa". |

# SAFARI YA MILELE

## NJIA YAKO YA KWENDA PEPONI AU MOTONI

**KABURI** Ni kituo cha kwanza cha Akhera. Ni shimo la moto kwa kafiri na mnafiki na ni bustani kwa Muumini. Kaburini kuna kuadhibiwa kutokana na maasi mengi. Miongoni mwa maasi hayo ni: Kutojisafisha (Najisi ya) mkojo, fitina, kutokuwa na uaminifu katika ngawira, kusema uongo, kuacha kusali kwa ajili ya kulala, kuisusa Qur'ani, zinaa, ulawiti, riba kutolipa deni na mengine yasiyokuwa hayo. Yanaokoa adhabu hiyo: Matendo mema yaliyo halisi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kuomba kinga ya adhabu hiyo, kusoma Sura Al-mulk (67) n.k. Anakingwa na adhabu ya kaburi: Shahidi (aliyekufa katika vita vya kidini), Mlinzi wa ngome, aliyekufa siku ya Ijumaa, aliyekufa kwa ugonjwa wa kuumwa na tumbo n.k.

**KUPULIZWA KWA PARAPANDA** Parapanda ni pembe kubwa ambayo (Malaika) Israfiil ameiweka mdomoni akingojea wakati wa kuamrishwa kuipuliza. Kuna mpulizo wa fazaa. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: "***Na ikapulizwa parapanda na, kwa hiyo, wakafazaika walioko mbinguni na walioko ardhini isipokuwa wale aliotaka Mwenyezi Mungu".*** Suratuz-Zumar 39, aya 68. Kwa sababu hiyo, ulimwengu wote utasambaratika. Baada ya arobaini, utapulizwa mpulizo wa kufufuliwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: "***Halafu utapulizwa (mpulizo) mwingine. Mara, wao watakuwa wamesimama wakingojea".*** Suratuz- Zumar 39, aya 68.

**KUFUFULIWA** Halafu Mwenyezi Mungu ataleta mvua na hivyo miili itaota (kutokana na kifupa cha tindi ya uti wa mgongo) na kuwa viumbe wapya, wasiokufa, wasiokuwa na viatu na wasiokuwa na nguo. Watawaona Majini na Malaika. Watafufuliwa wao na matendo yao.

**KUKUSANYWA** Katika siku kubwa ambayo kipimo chake ni miaka elfu 50, Mwenyezi Mungu atawakusanya viumbe kwa kuhesabiwa huku wakiwa wamefazaika kama walevi, kama vile dunia yao ni saa moja. Jua litasogea karibu kiasi cha maili moja. Watu watazama katika jasho lao kwa kadiri ya matendo yao. Siku hiyo wanyonge na wenye kiburi watagombana. Kafiri atagombana na mwenzie na shetani wake na swahiba zake. Watalaaniana wenyewe kwa wenyewe. Dhalimu atauma vidole vyake (akijuta). Jahanamu itaburutwa kwa hatamu (kamba) elfu 70. Kila hatamu moja itaburutwa na malaika elfu 70. Kafiri akiiona Jahanamu, atapenda kuikomboa nafsi yake au awe mchanga. Ama wenye dhambi: Asiyetoa zaka, mali zake zitageuzwa kuwa moto na kuchomwa kwao. Wenye kiburi watafufuliwa kama sisimizi. Laghai, Mporaji na Haini (Mwenye kufanya hiyana) watafedheheshwa. Mwizi atakuja na alichoiba. Yaliyojificha yatadhihirika. Ama wachamungu haitawafazaisha siku hiyo, bali itapita kama sala ya Adhuhuri.

**UOMBEZI (SHUFAA)** Kuna Uombezi Mkubwa unaomhusu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wetu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, atakapowaombea viumbe Siku ya kukusanywa ili waondolewe mateso yao na ili wahesabiwe. Kuna Uombezi wa Wote kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na kwa watu wengine, kama kuomba kutolewa kwa waumini katika moto na kupandishwa daraja zao.

**HESABU** Watu watahudhurishwa kwa Mola wao wakiwa katika mistari. Atawaonesha matendo yao na kuwahoji,kuhusu matendo hayo, umri, ujana, mali, elimu, ahadi, neema, masikio, macho na moyo. Kafiri na mnafiki watahojiwa mbele ya halaiki ili kuwatahayarisha, kuwasimamishia hoja na ili watu, ardhi, usiku, mchana, malaika na viumbe wawe mashahidi kwao mpaka hoja hiyo isimame na waikubali. Ama Muumini, Mwenyezi Mungu atakaa naye faragha na kumtaka akiri makosa yake. Akiona kuwa ameungama, atamwambia: *"Nimekusitiri makosa yako duniani na mimi leo ninakusamehe"*. Watakaohojiwa mwanzo ni umma wa Muhammad. Amali ya kwanza kuhojiwa ni sala, na hukumu ya mwanzo kuhukumiwa ni damu (za watu waliouawa).

**KUPEPERUSHWA NYARAKA** Halafu nyaraka zitapeperuka na ,kwa hiyo, watu Watachukua kitabu ambacho "***Hakiachi dogo wala kubwa isipokuwa kwamba kinalidhibiti tu".*** Suratul-Qahf 18, aya 49. Muumini atachukua kwa mkono wake wa kulia na kafiri na mnafiki kwa mkono wake wa kushoto nyuma ya mgongo wake.

**MIZANI** Halafu matendo ya viumbe yatapimwa ili Mwenyezi Mungu awalipe kwayo. Yatapimwa kwa mizani ya kweli yenye vitanga viwili. Yataielemea mizani hiyo matendo yanawiana na sheria na yaliyo safi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Miongoni mwa yatayoielemea mizani ni: Laa ilaaha illallaa لا إله إلا الله, tabia njema, dhikiri (kama vile kumsifu Mwenyezi Mungu), kumtakasa Mwenyezi Mungu "***Subuhaanallaahi wabihamdihii, subuhaanallahil-adhwiimu***".Watu watabadilishana hukumu kwa mazuri yao na mabaya yao.

**BIRIKA** Halafu waumini wataiendea Birika (Hodhi). Atakayekunywa katika Birika hiyo, hatopata kiu baada yake asilani. Kila Mtume (*Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam*) ana Birika. Kubwa zaidi ya hizo ni ya Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Maji yake ni meupe zaidi kuliko maziwa, matamu zaidi kuliko asali na yananukia zaidi kuliko Misk. Vyombo vyake ni dhahabu na fedha kama idadi ya nyota. Urefu wake ni wa mbali zaidi kuliko kutoka Aila huko Jordan mpaka Aden (Yemen). Maji yake yanatoka katika mto wa Kauthar.

**MTIHANI WA WAUMINI** Siku ya mwisho kabisa ya kukusanywa, makafiri wataifuata Miungu yao waliyokuwa wakiiabudu. Itawafikisha motoni Huku wakiwa makundi makundi kama makundi ya wanyama. Wataingia kwa miguu yao au kwa nyuso zao. Hawatasalia isipokuwa waumini tu na wanafiki. Mwenyezi Mungu atawaendea na kuwaambia: "Mnangoja nini?". Watasema: "Tunamngoja Mola wetu". Watamjua kwa mguu wake[1] atakapoufunua. Watasujudu isipokuwa wanafiki tu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "***Siku utakapofunuliwa***

---

[1] imethibiti kuwa Mwenyezimungu anao mguu na sifa zinginezo zisizokua hizo,lakini sifa za Mwenyezimungu hazifanani na sifa za wanaadamu,lililo wajibu kwetu ni kuziamini bila ya kuzipigia mfano wala kutaka kujua namna yake.

***mundi (mguu) na wakatakiwa kusujudu na hawataweza".*** Suratul-Qalam 68, aya 42. Halafu watamfuata na ataweka Siraat. Atawapa nuru, na nuru ya wanafiki itazimwa.

**SIRAAT** *Siraat* ni daraja lililotandazwa motoni waumini wapite kupitia daraja hilo kuelekea Peponi. Mtume, (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ametaja wasifu wa Siraat kwa kusema kuwa ni: " *Yenye utelezi, inayodondosha. Ina viopoo na kulabu kama miba ya (mti) Saadanin Ni nyembamba sana kuliko unywele na ina makali sana kuliko upanga".* Ameipokea Hadithi hii Muslim. Kwenye Siraat, waumini watapewa mwanga (nuru) kwa kiasi cha amali zao. Wa juu wao zaidi ni kama milima, na wa chini wao zaidi itakuwa katika ncha ya kidole gumba cha mguu wake. Mwanga huo utawaangazia na hivyo watavuka kwa kadiri ya amali zao. "*Muumini atapita kama kupesa kwa jicho na kama umeme na kama upepo na kama ndege na kama farasi wendao kasi na wanyama wengine wanaopandwa" "Kuna atakayepita salama na atakayepita akiwa majeruhi na atakayetumbukizwa katika Jahanamu".* Hadithi hii imepokewa na Bukhariy na Muslim. Ama wanafiki, wao hawatakuwa na nuru. Watarejeshwa na utawekwa ukuta baina yao na baina ya waumini. Halafu watataka kuvuka na watatumbukia katika moto.

**MOTO** Wataingia humo makafiri, halafu baadhi ya waumini waasi, halafu wanafiki. Katika kila 1,000 watauingia 999. Una milango 7. Ni mkali zaidi kuliko moto wa duniani kwa mara 70. Umbo la kafiri humo litakuwa kubwa ili aonje adhabu, na hivyo sehemu ya kati ya mabega yake itakuwa na umbali wa mwendo wa siku tatu. Jino lake litakuwa kama mlima Uhud. Ngozi yake itakuwa nene na kubadilishwa ili aonje adhabu. Kinywaji chao ni maji ya moto yanayokata utumbo wao. Chakula chao ni Zakum, Ghisliin na usaha. Aliye na nafuu zaidi kati yao ni yule atakayewekewa chini ya miguu yake makaa mawili ya moto ambayo ubongo wake utachemka kutokana na makaa hayo. Humo mna kuivishwa ngozi, kuyayushwa, kubabuliwa, kuburuzwa, minyororo na pingu. Kina chake ni kirefu sana. Lau angetumbukizwa humo mtoto mchanga angefika miaka 70 wakati wa kukifikia. Kuni zake ni makafiri na mawe. Hewa yake ni mvuke wa moto na kivuli chake ni moshi mweusi. Nguo zake ni moto unaokula kila kitu; haubakishi na hauachi. Una hasira na unafoka. Unaunguza na unafika kwenye mifupa na mioyo.

**KICHUGUU** Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema: "*Waaumini watasalimika na moto na watazuiwa na kichuguu kitakacho kuwepo baina yao na baina ya moto na pepo. Baadhi yao watalipana dhuluma zilizokuwepo baina yao duniani. Pale watakaposafishwa (kwa kulipana), wataruhusiwa kuingia peponi. Nina'apa kwa (jina la) ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba mmoja wao atayaelewa zaidi makazi yake peponi kuliko anavyoyaelewa makazi yake yaliyokuwepo duniani".* Ameipokea Hadithi hii Bukhariy.

**PEPO** Ni makazi ya waumini. Jengo lake ni dhahabu na fedha. Udongo wake (wa kujengea) ni Miski. Kokoto zake ni Lulu na Yakuti na mchanga wake ni

Zafarani. Ina milango 8. Upana wa mmoja milango hiyo ni mwendo wa siku Tatu, lakini utakuwa na msongamano. Kuna daraja 100. Baina ya daraja mbili ni kama baina ya mbingu na ardhi. Firdausi ndio pepo ya daraja ya juu zaidi, na humo ndimo inamotoka mito yake. Paa lake ni Arshi ya (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehma. Mito yake ni asali, maziwa, tembo na maji. Inapita chini ya mahandaki. Muumini ataipitisha atakavyo. Vyakula vyake ni vya kudumu, vya karibu na rahisi. Humo mna hema la Lulu lenye vitobo, upana wake ni maili sitini. Katika kila pembe kutakuwa na watu wasiokuwa na nywele, wasiokuwa na ndevu, wenye macho yenye wanja. Ujana wao hautoweki na nguo zao hazichakai. Hakuna kukojoa, kunya wala uchafu wowote. Mashanuo yao ni dhahabu, na jasho lao ni Miski. Wanawake wa peponi ni wazuri, bikira, wenye mapenzi (kwa waume zao) na wenye rika sawa. Wa mwanzo kabisa kuingia peponi ni Muhammad, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, na Mitume. Wa chini yao zaidi humo ni yule atakayetamani (kitu) akapewa mara kumi yake. Watumishi wake ni vijana wa milele kama lulu zilizosambazwa. Miongoni mwa neema zake kubwa zaidi ni kumuona Mwenyezi Mungu, radhi zake na maisha ya milele.

# NAMNA YA KUTAWADHA



Haifai kutawadha isipokuwa tu kwa maji twahara, nayo ni yale yaliyobaki katika asili ya umbile lake,kama vile maji ya bahari na visima na chemchem na mito. au yale ambayo rangi yake au harufu yake au ladha yake imebadilika kwa kitu twahara kama maji yaliyo badilika kwa kukaa muda mrefu.

**n.t.** Maji machache yananajisika kwa kupatwa najisi, ama maji mengi, nayo ni yenye kuzidi lita (210) hayo hayanajisiki mpaka najisi ibadilishe rangi yake ,au ladha yake,au harufu yake.



Udhu unaanza kwa "Bismillaah". Inapendekezwa kuosha vitanga viwili katika kila Udhu. Inasisitizwa kuviosha mara tatu kwa aliyeamka kutoka katika usingizi wa usiku.

**Uzindushi :** Inachukiza kuzidisha zaidi ya mara tatu katika kuosha viungo vyote vya udhu..



Halafu mtu atasukutua mara moja. Ni lazima kuyatikisa na kuyazungusha maji ndani ya mdomo. Inapendekezwa kusukutua kuwe mara tatu.

**n.t. 1.** Haitoshi katika kusukutua kuingiza maji kinywani kisha kuyatoa tu bali ni lazima kuyatikisa maji ndani ya mdomo **2.** inapendeza kupiga mswaki wakati wakusukutua .



Halafu atavuta maji puani mara moja Lazima kuvuta maji kuwe kwa njia ya pumzi mpaka yafike ndani ya mionzi ya pua. Inapendekezwa iwe mara tatu.

**Uzindushi:** Haitoshi katika kupandisha maji puani kuyaingiza maji katika pua kisha kuyatoa tu, bali ni lazima kuyaingiza kwa njia ya kuyavuta ndani ya pua kisha kuyatoa kwa kupumua si kwa mkono .Na wajibu ni mara moja lakini akifanya mara tatu ni bora.



Halafu ataosha uso wake na ambao ni kutoka sikio mpaka sikio kwa upana na kutoka maoto ya nywele za kichwa kwa kawaida mpaka kidevuni kwa urefu.

**Uzindushi:** Inapendeza kuziesua ndevu zitakapokua ni nyingi,na itakuwa ni wajibu pindi zikiwa chache.



Halafu ataosha mikono yake kuanzia ncha za vidole pamoja na kongo (vifundo = viwiko) mara moja. Lakini mara tatu ni bora.

**Uzindushi:** I napendeza kuosha mkno wa kulia kabla ya mkono wa kushoto.



Halafu atapaka maji sehemu yote ya nje ya kichwa chake kuanzia mbele yake mpaka kichogoni. Halafu atairudisha mikono yake kwenda mbele ya kichwa. Hatakiwi kuacha kupaka kitu katika mpaka huo wa kichwa. Halafu ataingiza vidole vyake vya shahada katika matundu ya masikio yake na kupaka maji kwa madole yake gumba migongo ya masikio yake. Vyovyote atakavyopaka itatosha.

**Uzindushi:** Sehemu zilizo wajibu katika kupaka kichwa ni: **1.**kutoka katika mpaka wa uso wambele mpaka kichogoni **2.**Si wajibu kuzipaka nywele ndefu (zilizo lala) **3.**Inapakwa ngozi ya kichwa itakapokuwa hamna nywele.**4.**Lazima kupaka katika **weupe wa masikio nyuma ya masikio** .



Halafu ataosha miguu yake pamoja na nguyu (vifundo viwili)mara moja. lakini mara tatu ni bora.

**Uzindushi: 1.**Viungo vya udhu ni vinne, navyo **(a).** Kusukutua na kupandisha maji puani na kuosha uso **(b).**Kuosha mikono miwili **(c).**Kupaka kichwa na masikio mawili. **(d).**Kuosha miguu miwili pamoja na vifundo viwili, ni wajibu kufuata mpangilio kati ya hivi viungo, na unaharibika udhu kwa kukitanguliza kiungo kabla ya kingine. **2.**Ni waji uwe uoshaji wa viungo ni mfululizo,na udhu utabatilika kwa kuchelewesha kuosha baadhi ya viungo mpaka vikakakauka viungo alivyo viosha kabla yake. **3.**Ni suna kusema baada ya udhu Ashhadu anlaa ilaaha illallah wahdahu laa shariika lahu waash-hadu anna Muhammadan abduhuu warasuuluhu.

**Inashartiwa:** Mpangilio baina ya viungo vya Udhu. Mtu aanze kusukutua, kuvuta maji puani na kuosha uso, kuosha mikono, kupaka maji kichwa halafu kuosha miguu.

**Inashartiwa** pia kufululiza (kufuatishia) kati ya viungo hivyo kwa namna ya kuchelewesha kuosha kiungo mpaka kilicho kabla yake kikawa kimekauka.

# NAMNA YA KUSALI



Mtu asimamapo akitaka kusali, ataanza kwa kusema: "Allahu Akbar. Imamu ataisema kwa sauti ya juu Takbira hiyo na Takbira nyinginezo ili walioko nyuma yake wasikie. Asiyekuwa Imamu ataisema kimya kimya. Atanyanyua mikono yake wakati wa kuanza Takbira huku vidole vikiwa vimeambatanishwa na kuinyanyua mikono hiyo mpaka mkabala wa mabega yake. Maamuma ataleta Takbira baada ya Imamu kukamilisha Takbira yake.

**N.t.:**Ni lazima kudhihirishwa katika nguzo na wajibu ambazo ni za maneno kwa kadiri ambavyo anaisikilizisha mwenye kuswali nafsi yake hata katika swala ya siri, na uchache wa kudhihirisha ni kiiasi cha kusikiwa na mwengine,na uchache wa siri ni kujisikia mwenyewe.



Kwa mkono wake wa kulia, atashika kiganja au kifundo cha mkono wake wa kushoto na kuiweka chini ya kifua chake, na macho yake yakiangalia mahali pa kusujudu kwake. Halafu ataanza kwa baadhi ya dua zilizonukuliwa katika Sunna.Mf.:subhaanaka Allaahuma wabihamdika tabaarakasmuka wataala jadduka walaailaaha ghairuka,Halafu ataomba kinga na kusoma Bismillahi. Yote hayo yaliyopita hatayasema kwa sauti ya juu. Halafu atasoma sura Alfaatiha. Halafu atasoma sehemu chache ya Qur'ani. Imamu atasoma kwa sauti ya juu katika sala ya Asubuhi na katika rakaa mbili za mwanzo za sala za Magharibi na Isha. Katika sala zisizokuwa hizo, atasoma kimya kimya.

Inapendeza kuwa yenye kusomwa kama ilivyo katika msahafu kwampangilio wa sura, na niharamu kusoma kinyume nyume, kutanguliza au kuichelewesha kwampangilio wa maneno au aya katika sura moja.



Halafu ataleta Takbira, atanyanyua mikono yake na kurukuu. Ataweka mikono yake juu ya magoti yake kama vile ameyashika, na atavitenganisha vidole vyake. Ataunyoosha mgongo wake na kukiweka kichwa chake usawa wa mgongo wake. Halafu atasema: Sub-haana Rab-biyal Adhiim,. Ni makuruhu kusema mara moja. Ukamilifu wa chini zaidi ni mara tatu.na kwa nguzo hii ndio hudirikiwa rakaa.

N.T. wakati wa takbira na kauli :(samia Allahu limanhamidah) ni wakati wa kitendo cha kuhama sio kabla au baada ya kitendo, na hiyo ni katika takbira zote za swala na atakapo chelewesha kwa makusudi swala itabatilika .



Halafu atanyanyua kichwa chake huku akisema: Samial-laahu Liman-hamidah na atanyanyua mikono yake. Akishasimama sawa sawa, atasema: Rab-banaa Walakal-hamdu Hamdan Kathiiran Twayyiban Mubaarakan Fiih Mil-assamaawaat Wamil-al-ardhi Wamil-amaa Shiita Min-ahai-in Baadu.

**n.t.** wakati wa kusema :(rabbana walakalhamdu ) inakuwa ni baada ya kukamilisha kisimamo kutoka katika rukuui si katika kunyanyuka kwake.



Halafu atainama kwenda kusujudu huku akileta Takbira. Ataitenganisha sehemu ya juu ya mikono yake (sehemu kati ya kongo na bega) isigusane na mbavu zake, na tumbo lake atalitenganisha lisigusane na mapaja yake, na mapaja yake yasigusane na miguu yake. Mikono yake ataiweka mkabala wa mabega yake. Ataegemea ncha za nyayo za miguu yake huku vidole vya mikono na miguu yake akivielekeza Kiblah. Halafu atasema: Sub-haana Rab-biyal-aalaa Inapendekezwa mara tatu. Anaweza kuongeza au kuomba baadhi ya dua zilizothibiti.

**n.t.** Ni wajibu iwe kusujudu ni juu ya viungo saba: Ncha za vidole vya miguu yake,na magoti yake,na viganja vyake,na paji la uso wake, na pua ,na inabatilika sala kwa kuacha kusujudi ju ya baaadhi ya viungo kwa makusudi ila kwa yule mwenye udhuru.



Halafu atanyanyua kichwa chake huku akileta Takbira na atakaa. Kukaa kati ya sijida mbili kuna namna mbili sahihi: **1)** Kuutandaza mguu wake wa kushoto na kuukalia, kuusimamisha mguu wa kulia na kuvipindisha vidole vyake vielekee Kiblah. **2)** Kuisimamisha miguu yake na vidole vyake akivielekeza Kiblah na kuvikalia visigino vyake.
Atasema: Rab-bigh-fir Lii mara tatu. Anaweza kuongeza: War-hamnii, Wajbur-nii, Wa-afaanii, War-zuq-nii, Wansur-nii, Wah-dinii, Wa-aafinii, Wa'fu An-nii
Halafu atasujudu sijda ya pili kama ya kwanza. Halafu atanyanyua kichwa chake huku akileta Takbira. Atasimama akiegemea sehemu ya juu ya nyayo za miguu yake na kusali rakaa ya pili kama ya kwanza.


**n.t.** kisomo cha suuratil faatiha sehemu yake ni katika kisimamo, na pindi atakapo anza kuisoma kabla kusimama wima, ni wajibu kuirejea baada kukamilika kisimamo kinyume cha hivyo imebatilika sala yake.



Akimaliza rakaa mbili, atakaa kwa ajili ya Tashahudi ya Kwanza huku akikaa kikao cha Iftirashi (Kuutandaza mguu wake wa kushoto na kuukalia, kuusimamisha mguu wa kulia na kuvipindisha vidole vyake vielekee Kiblah). Atauweka mkono wake wa kushoto juu ya paja lake la kushoto. Mkono wake wa kulia atauweka juu ya paja lake la kulia. Katika mkono huo wa kulia, atakunja kidole kidogo, kinachofuatia pamoja na cha kati na kidole gumba. Atatoa ishara kwa kidole cha Shahada. Atasoma Tashahudi: At-tahiy-yaatu Lil-llaah Was-swalawaat Wat-twa-yibaat. Assalaamu Alayka Ay-yuhan-nabiy-yu Warah-matullaahi Wabarakaatuh. Assalaamu Alaynaa Wa'alaa Ibaadillahis-swaalihiin. Ash-hadu Al-laa Ilaaha Il-lallaah Wash-hadu An-na Muhammadan Ab-duhuu Warasuuluh. Halafu atanyanyuka katika sala yenye rakaa tatu na yenye rakaa nne huku akileta Takbira na kunyanyua mikono yake. Atasali kama hivyo rakaa zilizobaki isipokuwa tu hatasoma kwa sauti ya juu. na atasoma sura Alfaatiha tu.




Halafu atakaa kwa ajili ya Tashahudi ya Mwisho huku akiwa amekaa kikao cha Tawaruki. Kikao hicho kina namna tatu sahihi. Mtu hatokaa kikao cha Tawaruki isipokuwa tu katika kikao cha mwisho cha sala ambayo ina Tashahudi mbili. Halafu atasoma Tashahudi. Halafu atamsalia Mtume Allaahumma swal-li A'laa Muhammad Wa'alaa Aali Muhammad Kamaa swal-layta A'laa Ibraahiim Wa'laa Aali Ibraahiim In-naka Hamiidun Majiid. Allaahumma Baarik A'laa Muhammad Wa'laa Aali Muhammad Kamaa Baarakta A'laa Ibraahiim Wa'laa Aali Ibraahiim In-naka Hamiidun Majiid. Halafu ataomba dua atakayo. **1)** Atautandaza mguu wa kushoto na kuutoa kupitia mguu wake wa kulia chini ya muundi (ugoko) wake. Atausimamisha unyayo wa mguu wa kulia, na tako lake likiwa ardhini. **2)** Atautandaza mguu wa kushoto na kuutoa kupitia mguu wake wa kulia chini muundi (ugoko) wake. Ataulaza mguu wa kulia na tako lake likiwa ardhini. **3)** Atautandaza mguu wa kushoto na kuutoa kupitia mguu wake wa kulia kati ya muundi na paja lake, na tako lake likiwa ardhini.
Hatokaa kikao cha Tawarruk isipokuwa tu katika kikao cha mwisho cha sala ambayo ina Tashahudi mbili. Halafu atasoma Tashahudi ya kwanza. Halafu atasoma: Allaahumma swal-li A'laa Muhammad Wa'alaa Aali Muhammad Kamaa swal-layta A'laa Ibraahiim Wa'laa Aali Ibraahiim In-naka Hamiidun Majiid. Allaahumma Baarik A'laa Muhammad Wa'laa Aali Muhammad Kamaa Baarakta A'laa Ibraahiim Wa'laa Aali Ibraahiim In-naka Hamiidun Majiid. Inapendekezwa, baada yake, kuomba baadhi ya dua zilizothibiti. Miongoni mwa dua hizo ni: "Auudhu Billaahi Min-a'dhaabin-naar Wa'dhaabil-qabri Wafit-natilmah-yaa Walmamaat Wafitnatil-masiihid-dajjaal.



Halafu atatoa Salaam mbili. Atageuka upande wake wa kulia akisema: Assalaamu a'laykum Warahmatullaah. Atafanya hivyo upande wake wa kushoto. Akimaliza kutoa Salaam, ataomba dua zilizothibiti na ilhali amekaa katika mahali pake aliposali.

# Kaka na dada yangu Mwislamu,

Elimu bila ya utekelezaji imeshutumiwa na Mwenyezi Mungu, Mtume wake na waumini. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema kuwa: "***Enyi ambao mmeamini kwa nini mnasema msiyoyafanya? Imekuwa dhambi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyafanya***". Abuhuraira, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema: "*Mfano wa elimu isiyofanyiwa kazi ni mfano wa mali isiyotolewa katika njia ya Mwenyezi Mungu*". Fudhail, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema: "*Mjuzi ataendelea kuwa mjinga wa anayoyajua mpaka ayatekeleze*". Malik Bin Dinar, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, amesema: "*Unamkuta mtu na hakosei hata herufi moja na matendo yake yote ni makosa*".

## Kaka na dada yangu Mwislamu,

Mwenyezi Mungu amekurahisishia kukisoma kitabu hiki chenye manufaa, na yamebaki matunda ya kusoma kwako na ambayo ni kuyatekeleza yaliyomo.

■ Umezipitia sehemu za Qur'ani na tafsiri yake. Jibidiishe kuyatekeleza maana ya aya hizi ulizozijua. Swahaba wa Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, walikuwa wakijifunza kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aya kumi na hawaingii katika aya kumi nyingine mpaka wayajue na kuyatekeleza yaliyomo katika aya kumi za mwanzo. Wamesema: "Hivyo, tulijifunza elimu na utekelezaji".

Sheria imelihimiza hilo. Ibn-abbas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi yeye na mzazi wake, katika kufasiri kauli ya Mwenyezi Mungu: "***Wanakisoma ukweli wa kukisoma***"(Albaqara 2, aya 121), amesema kuwa: Wanakifuata ukweli wa kukifuata. **Fudhaili,** Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema kuwa: "*Hakuna vingine isipokuwa kwamba Qur'ani imeteremshwa ili itekelezwe, watu wakafanya kuisoma ni amali*".

■ Pia umezipitia sehemu za Sunna za Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani. Fanya haraka kuziitika na kuzifanyia kazi, kwani watu wema wa umma huu (wa Kiislamu) walikuwa hawajifunzi jambo isipokuwa kwamba walikuwa wakishindana kulitekeleza na kulihubiri, ikiwa ni :

**a)** Kufuata kauli ya Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayyo kuwa: "***Nikikuamrisheni jambo lifanyeni kadiri muwezavyo, na ninalokukatazeni liepukeni***" Muslim. **b)** Kuogopa adhabu kali ya Mwenyezi Mungu iliopo katika kauli yake: "***Wajihadhari wale ambao wanapinga amri yake kuwapata wao fitna (mtihani) au kuwapata wao adhabu chungu***" Suratun-Nuur 24, aya 63. Miongoni mwa mifano ya utekelezaji huu ni kwamba:

**1**/ Mama wa Waumini, **Ummu-habiba**, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, anasimulia Hadithi kwamba: "***Yeyote aliyesali rakaa kumi na mbili katika siku moja, atajengewa, kwa rakaa hizo, jumba (la fahari) peponi***". Muslim.

Ummu-habiba amesema: *Sikuachapo kuzisali rakaa hizo tangu nilipozisikia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani.*

**2**/ **Ibn-omar**, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi yeye na mzazi wake (Omar), anasimulia Hadithi kwamba: "***Si haki ya mtu Mwislamu mwenye jambo la kuusia akalala siku tatu isipokuwa usia wake (unatakiwa uwe) umeandikwa***". Bukhariy. Halafu Ibn-umar akasema: Tangu nilipomsikia

Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema hayo, hainipitii siku moja isipokuwa kwamba ninao usia wangu.

**3/ Imam Ahmad**, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema: "Sikuandika Hadithi ila nimeitekeleza. Hata ilinipitia Hadithi kwamba Mtume aliumikwa (alitibiwa kwa kupiga chuku) na kumpa Dinari Abu-twaiba (mtu aliyemuumika), nikampa muumikaji Dinari wakati nilipoumikwa".

**4/ Imam Bukhariy**, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema: "Katu sikumsengenya yeyote tangu nilipojua kwamba kusengenya ni haramu. Mimi nataraji kukutana na Mwenyezi Mungu na asinihoji kwamba mimi nimemsengenya yeyote".

**5/** Imekuja katika Hadithi kwamba: "*Yeyote **aliyesoma Aya Kursiy baada ya kila sala, hakimzuii kitu kuingia peponi isipokuwa kifo tu***". Sunan Kubraa. **Ibn-qayyim,** Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema: Imenifikia kutoka kwa Sheikh wa Uislamu **(Ibn-taymiya)** kwamba amesema: Sikuiacha aya hiyo baada ya kila sala isipikuwa tu kwa kusahau au mfano wake.

■ Baada ya kujua na kutekeleza, ni lazima kuihubiri neema ambayo Mwenyezi Mungu amekuneemesha. Usijinyime thawabu na pia usimnyime mwenzako kheri. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "***Mwenye kuifahamisha kheri, atapata mfano wa malipo ya aliyeitenda kheri hiyo***". Muslim.

Pia Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "***Mbora wenu ni yule aliyejifunza Qur'ani na akaifundisha***". Bukhariy. Pia Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema: "***Fikisheni kutoka kwangu japo aya (moja)***". Kwa kiasi unavyosamabaza kheri kwa wingi ndivyo utakavyopata malipo mengi na makubwa na mambo yako mazuri yataendelea katika uhai na baada ya kifo. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, amesema kuwa: "***Mwanadamu anapokufa, amali zake hukatika isipokuwa tu (amali)itokanayo na mambo matatu: 1) Sadaka inayoendelea au 2) Elimu yenye manufaa (kwa watu) au 3) Mtoto mwema anayemuombea***". Muslim.

**Mwangaza:** Tunasoma Sura Alfaatiha zaidi ya mara kumi na saba kila siku. Katika sura hiyo, tunaomba kinga ya kutofanana na (Waliokasirikiwa) na (Waliopotea) halafu tunawaiga katika vitendo vyao. Tunaacha kujielimisha ili tufanye mambo kwa ujinga na kwa hiyo tunawaiga Wakristo waliopotea, au tunajifunza na hatutekelezi na kwa hiyo, tunawaiga Wayahudi waliokasirikiwa.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe sisi na wewe elimu yenye manufaa na matendo mema. Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani Bwana wetu na Mpenzi wetu Muhammad, Jamaa na Swahaba wake wote.

SWAHELE

# تفسير العشر الأخير

## من القرآن الكريم